

ZAWADI YA MWAKA MPYA
KWA WASOMA KISWAHILI WOTE

SIRI ZA MAOMBI

Yanayojibiwa....!

*Imenukuliwa kutoka kwenye vitabu
vya RYU.*

2025 SWAHILI Edition -Hazina ya Kujifunza Kusali

Kimetafsiriwa kutoka kwenye Kitabu cha Kingereza cha Prayer by EGW

RohoYaUnabii.Org MaarifaMtandaoni.Com
RevivalPlan.Org RohoYaUnabii.Net
MaarifaMtandaoni.Com
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani Ministry
Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam,
Nchini Kote au Mtandaoni kote!-4T472

YALIYOMO

Mpendwa Msomaji.....	i
UTANGULIZI.....	i
SURA YA 1	
MUNGU ANATUALIKA TUOMBE.....	i
SURA YA 2	
UHITAJI WETU WA MAOMBI.....	i
SURA YA 3	
MUNGU HUSIKIA MAOMBI.....	i
SURA YA 4	
MAOMBI NA USHINDI WA NAFSI.....	i
SURA YA 5	
AHADI ZA MUNGU KUHUSU MAOMBI.....	i
SURA YA 6	
MAOMBI YA IMANI.....	i
SURA YA 7	
MAOMBI NA UTIL.....	i
SURA YA 8	
MAOMBI YALETAYO USHINDI.....	i
SURA YA 9	
NGUVU YA MAOMBI.....	i
SURA YA 10	
SABABU ZA KUOMBA.....	i
SURA YA 11	
MAOMBI YALIYOJIBIWA.....	i
SURA YA 12	
MAOMBI NA UAMSHO.....	i
SURA YA 13	

WANAUME NA WANAWAKE WA MAOMBI.....	ii
SURA YA 14	
SALA YA KILA SIKU.....	ii
SURA YA 15	
MFANO WA YESU KATIKA MAOMBI.....	ii
SURA YA 16	
MAOMBI YA FARAGHA.....	ii
SURA YA 17	
MAOMBI KATIKA MZUNGUKO WA NYUMBANI.....	ii
SURA YA 18	
MAOMBI NA IBADA.....	ii
SURA YA 19	
MTAZAMO KATIKA MAOMBI.....	ii
SURA YA 20	
KUOMBA KATIKA JINA LA YESU.....	ii
SURA YA 21	
MWONGOZO WA BWANA KUPITIA MAOMBI.....	ii
SURA YA 22	
MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA.....	ii
SURA YA 23	
MAOMBI KWA AJILI YA MSAMAHA.....	ii
SURA YA 24	
MAOMBI YA KUOMBEA WENGINE- MAOMBEZI.....	ii
SURA YA 25	
MALAIKA NA MAOMBI.....	ii
SURA YA 26	
MAOMBI BANDIA.....	ii
SURA YA 27	
SHETANI NA MAOMBI.....	ii
SURA YA 28	
MAOMBI KATIKA SIKU ZA MWISHO.....	ii
SURA YA 29	
FURSA YA MAOMBI -UPENDELEO WA MAOMBI.....	ii
SURA YA 30	
SALA YA BWANA.....	ii
SURA YA 31	
KUOMBA ILI KUTOA.....	ii
SURA YA 32	

**Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wataalamu
wa Teknolojia, na wengine wote**

William Filbert Kalokaza-Katavi, Tanzania
Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania
Niwaeli Mburuja-Kilimanjaro, Tanzania
Daniel Masaka-Kisii, Kenya
Innocent Wayoga-Mara, Tanzania
Cindy Tustch-Washington, Marekani
Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
Paul Masaka-New Jersey, Marekani
David Masaka-Pennsylvania, Marekani
Gerard Nyafanga- Shirati, Tanzania
Pendo Makori-Momadi-Kibaha, Tanzania
Geoffrey Herman Herra-Manyara, Tanzania
Women Prayer Warriors of TAUS- WPM-
California
Loyce Chaulo-Arusha, Tanzania

Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
Samwel Kilango- Kilimanjaro, Tanzania
Judi Mmari Mugane-Siha, Kilimanjaro
John Mugane-Nakuru, Kenya
Sandra Barron-Kentucky, Marekani.
Stefano Kasiri na Kwandu Kasiri - Bariadi,
Tanzania
Kikundi cha Mbaki/Ngulus cha Maombi, TAUS-
US

Faustin Momadi Mkama - Dar Es Salaam,
Tanzania
James Ongoso-Mara, Tanzania
Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani

Mpendwa Msomaji

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 4000 kati ya 7000 bado hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri.

Ombi letu, usibadilishe chochote, tuite kama kuna kosa! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini, ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, nasit umekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lische, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu vya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini

sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zile au wawe na mwenendo kama ule, na mfano mdogo sana utakuwa kuhusu chakula, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila matayarisho hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia [Email:](#)

UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1-908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana

Tunawatakieni Nyote Neema Ya MUNGU Wetu Mkuu Idumu Ndani Yenu. MARANATHA Wapendwa Wa BWANA! Amina

Kila mwanadamu anahitaji maombi. Hivyo sambaza kwa wote ili tuweze kujiombea na kuombeana! Masihi anakuja, tuombe tuwe tayari kwa zawadi ipitayo zote! Kiswahili ni Lugha ya kumi duniani, na ya tatu kwa madhehebu mengi makubwa, hivyo ombea tafsiri ya maandiko ya uzima wa milele ya Kiswahili.

Mwisho wa sura za kitabu hiki kuna nukuu toka Runinga Ya Upendo kuhusu Maombi na zaidi ya Mafungu 500 ya Maandiko yamenukuliwa humu.

UTANGULIZI

Maandiko yanatuhimiza "Kuomba bila kukoma." Hii haimaanishi kwamba tunapaswa kutumia muda wetu wote tukiwa tumepiga magoti yetu katika maombi rasmi. Bali Inamaanisha kwamba lazima tuishi na kumtumikia Bwana wetu katika mazingira ya maombi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi (structured and unstructured), rasmi na yasiyo rasmi, yenye mpangilio na yasiyo na mpangilio, mfano ukiwa kwenye basi au safarini, ukiwa kanisani, ukiwa kibaruni, si lazima kufumba macho, ila unaweza kuinua mikono mitakatifu kama Biblia inavyoshauri ikibidi, usifikiri ni mambo ya dini fulani kuinua mikono, (1Tim2:5) hapana! Hutakuwa umekiuka sheria za Biblia kuinua mikono bila hasira wala magomvi, hata hivyo polisi akisema “mikono juu -hands up” si utaiweka? Basi kwanini usimwinulie mikono Mungu na kujisalimisha Kwake! Siku moja Kila goti litapigwa na kila ndimi itakiri Masihi ni Bwana).

Maombi ni njia ya mawasiliano kati ya nafsi zetu na MUNGU. MUNGU huzungumza nasi kupitia Neno Lake; tunamwitikia Neno Lake anapozungumza kupitia maombi

yetu, Naye hutusikiliza daima. Hatuwezi kumchosha au kumlelea kwa mawasiliano yetu ya mara kwa mara ya mioyo yetu kwenda kwa moyo Wake.

Tumefika kwenye nyakati ngumu. Matukio katika ulimwengu wetu yanamuhitaji kila mfuasi wa Kristo kuwa na bidii kabisa ndani ya uhusiano wake na MUNGU. Ili kuimarisha uhusiano huu na kutosheleza mahitaji yetu ya kihisia, kijamii, kimwili, kiuchumu na pia kiroho, ni lazima tujifunze nguvu ya maombi. Ni lazima tumsihi Bwana, kama wanafunzi wa awali, tukisema, “Bwana, tufundishe kuomba.” Lazima tuseme kwa kusisitiza kwamba katika nukuu hizi zote maneno mawili yametumika kupita maneno mengine nayo ni Maombi ya Dhati, na Maombi ya bidii na Usongo/ari (Earnest and Fervent Prayers). Hebu yafanyie utafiti maneno haya yana maana gani maana yamesheheni tunu kubwa, ambayo mpaka leo nasi tunajikanyaga kuyaelewa, tunaomba utuandikie na kutumegea nasi upatapo uelewa wake tafadhali sana! Mara nyingi watu hujiita Prayer Warrior wakimaanisha wapigana vita vya maombi, Sura ya Maombezi au Intercessory Prayer ni muhimu kujua tunapojiita jina Hili.

Kwamba MUNGU yuko radhi na yuko tayari kusikiliza na kujibu maombi yetu yanayotoka moyoni katika hali zote ni jambo lenye kutia moyo sana. Yeye ni Baba Mwenye upendo ambaye huzingatia wakati mambo yanaenda vizuri na wakati mabadiliko ya maisha yanapotuletea mapigo yenye kuhuzunisha, yaliyo magumu, na ya kutisha. Tunapojisikia kulia, “MUNGU, uko wapi?” Ni vizuri kujua kwamba Yeye Yupo karibu kupitia kuomba.

Mwandishi mmoja alisema, “Mambo mengi zaidi hufanywa na maombi kuliko ndoto za ulimwengu huu.” Hili ni kweli pia kwa kanisa. “Uamsho wa Ucha MUNGU wa kweli miongoni mwetu ndilo hitaji kuu na la msingi kuliko mahitaji yetu yote. Kuutafuta huu inapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza” (Selected Messages 1:121). MUNGU atatenda kwa ajili yetu tunapomba kile ambacho hangetenda ikiwa hatukumuomba. (The Great Controversy, 525 Nafikiri hii inahusika sana uchaguzi na pambano kuu linaloendelea). Tunakubali kwamba tunahitaji kumimiwa kwa Roho Mtakatifu. Lakini hili linaweza kutimizwa tunapomba maombi ya binafsi na ya pamoja tu. Watu wa MUNGU wanapomba kwa bidii, kwa unyofu, mmoja mmoja, na

kwa pamoja, MUNGU atajibu. Mambo makubwa yatatokea ndani na miongoni mwa watu wa MUNGU. Na ulimwengu utahisi matokeo wakati Roho Mtakatifu anakuja kuwatayarisha na kuwawezesha watu Wake.

Tunaamini kitabu hiki kitapata mapokezi kwa utayari miongoni mwa watu wa asili zote. Tunaposoma nukuu teuzi kutoka kwa RYU- Runinga ya Upendo au Roho ya Unabii juu ya somo muhimu la maombi, tutaona mioyo yetu ikiwa imechochewa kwa njia ya ajabu na changamfu. Jumbe hizi zitagusa mioyo yetu. Tutasadikishwa kwa mambo mengi yaliyoelezwa nayo yatapata nafasi ndani ya mioyo yetu, na kuibua mwitikio wa kuafiki wito wa MUNGU juu ya maisha ya maombi ya kina na mengi zaidi.

"Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio na ukomo/kifani. Kinachoshangaza ni kwamba tunaomba kidogo sana. MUNGU Yuko radhi na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi Kwa nini wana na binti za MUNGU wanasita kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za mbinguni, pahali ambako zimetunzwa hazina tele za Mweza wa Yote?" (Steps to Christ, 94, 95).

Binafsi tumebarikiwa sana kukisoma kitabu hichi, hebu nawe ubarikiwe na kuviombea vitabu hivi 30 kwenye mlolongo huu vipate mhakiki-Proofreader na wataalamu wanaohusika kuvisambaza

Maranatha!

Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

- Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu."
- Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha neno la Mungu
- Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

- Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa. Basi tuendeleo kuyazingatia mambo 7 Muhimu kwa Kila mwanadamu
- Tumwamini Mungu na Kumkiri, na kuziungama dhambi zetu
- Tusome Maandiko Matakatifu Kila siku
- Tusali kila siku bila kukoma
- Tutafute Ushirika unaoafuata Maandiko
- Mtindo wa Maisha Uendane na Maandiko Matakatifu ambayo tunakiri kuwa ni Pumzi na barua ya Mwenyezi Mungu
- Huduma za Jamii, kusaidia wenye mahitaji, yatima, Wajane, masikini, wapekwe nk
- Tuenende ulimwengu kote na kuwaambia watu ujumbe ili wajitayarisha na Ujio wa Masihi (Share!) na hili ndilo sisi tunafanya hapa, nawe tunaomba usambaze kwa magroup yako!

Maombi yetu makuu yawe manne ni Roho Mtakatifu, kujisalimisha kwa MUNGU, tufundishe mambo ya kuombea na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Mungu Atufungulie milango ya kuenenda ulimwenguni mwetu kwa muktadha wa utamaduni wetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma.

SURA YA 1

MUNGU ANATUALIKA TUOMBE

Kuunganishwa Na MUNGU Kupitia Mnyororo Wa Maombi—Ni jambo la ajabu kwamba tunaweza kuomba kwa ufanisi; kwamba wanadamu tusiostahili, tunaokosea tunayo nguvu ya kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kutamani kuliko hii, - kuunganishwa na kuwasiliana na MUNGU asiye na ukomo? Mtu dhaifu, mwenye dhambi ana nafasi ya kuzungumza na Muumba Wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea

njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume.
[Pr 7.1; Maombi Aya ya 1]

Twaweza kuzungumza na MUNGU mioyoni mwetu; tunaweza kutembea katika ushirika na Kristo. Tunapofanya kazi zetu za kila siku, tunaweza kupumua matamania ya mioyo yetu, shauku isiyoweza kusikiwa na sikio la mwanadamu; lakini neno hilo haliwezi kufa na kunyamaza kimya, wala haliwezi kupotea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Kwani hii huiuka juu ya sauti za mitaani, juu ya kelele za mashine. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na maombi yetu husikilizwa.
[Pr 7.2; Maombi Aya ya 2]

Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri na ongezeko la imani. Kwa kila ombi unalotoa kwa dhati na kusadiki moyoni, jibu litakuja. Linaweza lisije kama vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta jibu hilo; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribu, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kila wakati kwa faida yako. (Gospel Workers, 258) [Pr 7.3; Maombi Aya ya 3]

Yesu hutualika sisi Kuomba—Bwana anatupatia sisi fursa binafsi ya kumtafuta Yeye katika maombi ya bidii, ya kutua mizigo ya roho zetu Kwake, bila kumficha chochote Yeye ambaye ametualika, “Njooi Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Nami nitawapumzisha.” Oh, tunapaswa kushukuru kwa ukubwa wa kiasi gani, kwamba Yesu Yuko tayari na ana uwezo wa kubeba madhaifu yetu yote na kututia nguvu na kuponya magonjwa yetu yote ikiwa itakuwa kwa faida yetu na kwa utukufu Wake. - (Medical Ministry, 16) [Pr 8.1; Maombi Aya ya 4]

“Njooi Kwangu,” ndio mwaliko Wake. Haijalishi wasiwasi na majaribu ya kiasi gani wewe uliyo nayo moyoni, wewe lianike wazi tu shauri lako mbele za Bwana. — (The Desire of Ages, 329) [Pr 8.2; Maombi Aya ya 5]

Mwambie Yesu Mahitaji Yako Yote—Kuna watu wachache wanaothamini au kuboresha fursa/upendeleo wa thamani wa maombi tuliopewa na Mungu. Tunapaswa kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu yote.

Tunaweza kumpelekea wasiwasi, masumbufu au fadhaa zetu ndogo na mashaka pamoja na shida zetu kubwa. Chochote kinachojitokeza kutusumbua au kutufadhaisha, tunapaswa kukipeleka kwa Bwana katika maombi. Tutakapohisi kuwa tunahitaji uwepo wa Kristo katika kila hatua, Shetani atakuwa na nafasi ndogo ya kupenyeza majaribu yake. Ni juhudi yake ya makusudi kutuweka mbali na rafiki Yetu bora na mwenye huruma. Hatupaswi kumfanya mtu yeyote kuwa msiri wetu ila Yesu. Tunaweza kuzungumza Naye kwa usalama, yale yote yaliyomo ndani ya mioyo yetu. –(Testimonies for the Church 5:200, 201) [Pr 8.3; Maombi Aya ya 6]

Kufungua Moyo kwa Rafiki—Sala ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Sio kwamba tunamjulisha MUNGU jinsi tulivyo, lakini ili kutuwezesha kumpokea. Maombi hayamshushi MUNGU kwetu, bali hutupeleka Kwake juu. [Pr 8.4; Maombi Aya ya 7]

Wakati Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kudondosha mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho pia kwetu. - (Steps to Christ, 93) [Pr 8.5; Maombi Aya ya 8]

MUNGU hutukaribisha Kwenye Chumba Chake cha kuonana Naye (mtu mmoja Pamoja na Mungu au wengi)—Tunamwendea MUNGU kwa mwaliko maalum, na Yeye anasubiri kutukaribisha kwenye chumba Chake cha kuonana Naye (chumba cha Enzi!). Wanafunzi wa kwanza waliomfuata Yesu hawakuridhika na mazungumzo ya haraka-haraka pamoja Naye njiani; wakasema, "Rabi,... Wewe unakaa wapi? ... Walikuja na kuona mahali alipokuwa akiishi, wakakaa pamoja Naye siku hiyo." Yohana 1:38, 39. Kwa hivyo hata nasi tunaweza kuingizwa katika mahusiano ya karibu sana, na kuwasiliana na Mungu na kuwa na ushirika pamoja na Yeye. "Yeye aketiye mahali pa siri pa Aliye Juu atakaa chini ya uvuli wa Mwenyezi." Zaburi 91: 1. Hebu wale wanaotamani baraka za MUNGU wabishe hodi na kungojea hapo kwenye mlango wa rehema na uhakikisho thabiti, wakisema, Kwa maana Wewe, Bwana, umesema, "Kila mtu aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye

atafunguliwa.”(Thoughts from the Mount of Blessings, 131)
[Pr 9.1; Maombi Aya ya 9]

Upendeleo uliotukuka—Wanapopatwa na matatizo, wanaposhambuliwa na vishawishi vikali, wao [watoto wa MUNGU] wana upendeleo wa maombi. Je, ni fursa iliyotukuka kwa kiasi gani! Viumbe vyenye ukomo, ambavyo ni vumbi na majivu tu, kwamba wamekubaliwa kupitia upatanishi wa Kristo, kwenye chumba Chake cha faragha ili kuonana na Yeye Aliye Juu. Katika mazoezi kama hayo roho, huletwa katika ukaribu mtakatifu na MUNGU, na hufanywa upya katika maarifa, na utakatifu wa Kweli, na kisha kulindwa na kuimarishwa dhidi ya mashambulio ya adui. - (An Appeal to Mothers, 24) [Pr 9.2; Maombi Aya ya 10]

Ombi ni hitaji la Kiroho na ni Upendeleo—Wale ambao wanakiri kwamba wanampenda Kristo, hawafahamu au hata kupata fununu ya uhusiano uliopo kati yao na MUNGU, ... Hawajatambua upendeleo wa hali ya juu na umuhimu mkubwa wa maombi, toba, na utendaji wenye nguvu wa Maneno ya Kristo.-(Selected Messages 1:134) [Pr 9.3; Maombi Aya ya 11]

Maombi Yanatuwezesha Kuishi Katika Mwanga jua wa Uwepo Wake—Ni fursa yetu kuifungua mioyo yetu, na kuruhusu mwangaza wa jua wa uwepo wa Kristo ndani. Kaka yangu, dada yangu, geuka na utazame nuru. Ingia katika mawasiliano halisi, na ya kibinafsi na Kristo, ili uweze kuwa na ushawishi unaoinua na kuleta uamsho. Hebu imani yenu iwe imara, yenye usafi wa moyo na thabiti. Hebu shukrani kwa MUNGU ijaze mioyo yenu. Unapoamka tu asubuhi, piga magoti kando ya kitanda chako, na umwombe MUNGU akupe nguvu ya kutimiza majukumu ya siku hiyo, na kukabiliana na majaribu yake. Mwambie akusaidie kuleta katika kazi zako za siku uzuri wa tabia ya Kristo. Mwambie akusaidie kusema maneno ambayo yatawapatia wale wanaokuzunguka matumaini na ujasiri, na kukuvuta/kukusogeza wewe karibu na Mwokozi. (Sons and Daughters of God, 199)- [Pr 9.4; Maombi Aya ya 12]

Maombi yetu siyo mzigo kwa Mungu na Yeye hachoshwi nayo kamwe— Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa sala/maombi kwa MUNGU. Hakuna

kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya biashara au pilikapilika, tunaweza kutuma maombi yetu kwa MUNGU na kuomba mwongozo Kwake, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kufungua mlango wa moyo kila wakati na kutoa mwaliko wetu kwenda juu ili kumwalika Yesu aje kukaa kama mgeni wa mbinguni katika mioyo yetu. [Pr 10.2; Maombi Aya ya 13]

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira yenye mawaa ya ufisadi na yaliyoharibiwa karibu nasi, sisi hatuhitaji kuivuta hewa hiyo mbaya yenye uvundo, kwenye mapafu yetu na kupata harufu hiyo mbaya na sumu, inayoharibu afya zetu, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango dhidi ya mawazo yasiyo safi na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele ya MUNGU kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea msaada na baraka za MUNGU watatembea katika hali takatifu kuliko ile ya dunia na watakuwa na mawasiliano/ushirika wa mara kwa mara na mbingu. [Pr 10.2; Maombi Aya ya 14]

Tunahitaji kuwa na maoni yakinifu zaidi juu ya Yesu na ufahamu kamili wa thamani ya Ukweli wa milele. Uzuri wa utakatifu utajaza mioyo ya watoto wa MUNGU; na ili kwamba hili liweze kutimizwa, tunapaswa kutafuta mafunuo ya Bwana/mbingu kuhusiana na vitu vya mbinguni. [Pr 10.3; Maombi Aya ya 15]

Hebu roho ivutwe na kwenda juu, ili MUNGU atupe pumzi ya anga la mbinguni. Tunaweza kukaa karibu na MUNGU ili kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili ya ua ligeukiavyo jua (automatiki!). [Pr 10.4; Maombi Aya ya 16]

Yaweke mahitaji yako, furaha yako, huzuni yako, wasiwasi wako, na hofu yako mbele za MUNGU. Hauwezi kumlelea Yeye; huwezi Kumchosha Mwenyezi Mungu. Yeye anayehesabu nywele za kichwa chako, hapuuzii yale yalusuyo mahitaji ya watoto Wake. "Bwana amejaa huruma na rehema" (Yakobo 5:11). Moyo Wake wa upendo unaguswa na huzuni zetu na hata tunapozitaja na kupeleka Kwake kila kitu kinachotatanisha akili. Hakuna kitu

kikubwa mno kwake kitakachomshinda kubeba, kwani Yeye anaushikilia ulimwengu. Yeye Anatawala juu ya mambo yote ya ulimwengu. [Pr 11.1; Maombi Aya ya 17]

Hakuna jambo lolote lile linalohusu mvurugiko wa amani mioyoni mwetu ambalo ni dogo sana Kwake Yeye kutambua. Hakuna sura katika uzoefu wa maisha yetu iliyo yenye giza mno Kwake Yeye kuisoma; hakuna mifadhaiko migumu sana Kwake kuweza kuiondoa Uhusiano kati ya MUNGU na kila nafsi umetofautiana na umesheheni sana, kana kwamba hakuna mwanadamu mwingine duniani ambaye amewahi kushiriki utunzaji Wake, ni kama vile hakuna mtu mwingine duniani ambaye kwaye alimtoa Mwanaye mpendwa isipokuwa mtu huyu mmoja tu. - (Steps to Christ, 99, 100) [Pr 11.2; Maombi Aya ya 18]

Ladha ya Mbinguni—Jipumzishe kabisa mikononi mwa Yesu. Tafakari kwa kina kuhusu upendo Wake mkuu, na wakati unatafakari juu ya kujikana Kwake, kafara Yake isiyo na kikomo iliyotolewa kwa niaba yetu ili uweze kumwamini Yeye, moyo wako utajazwa na furaha takatifu, amani tulivu, na upendo usioweza kuelezeka. Tunapozungumza juu ya Yesu, tunapomwita kupitia maombi, imani na ujasiri wetu kwamba Yeye ni Mwokozi wetu sisi Mwenye upendo, utaimarika na tabia Yake itaonekana kupendeza na kuvutia zaidi.... Tunaweza kufurahia karamu nyingi za upendo, na tunapoamini kabisa kuwa sisi ni Wake kwa kuasiliwa, tunaweza kuwa na muonjo/ladha ya mbinguni. Msubiri Bwana kwa imani. Bwana huuvuta moyo katika maombi, na hutupatia sisi kuhisi upendo Wake wa thamani. Tunao ukaribu Naye, na tunaweza kufanya ushirika mtamu/mzuri sana na Yeye. Tunapata maoni dhahiri juu ya ukarimu na huruma Yake, na mioyo yetu inavunjika na kuyeyuka na kutafakari upendo ambao tumepewa moyoni. Hakika tunapata hisia ya Kristo anayekaa na kudumu ndani ya nafsi. Hakika tunahisi Kristo anayekaa ndani ya mioyo yetu, na tunajisikia kuwa nyumbani na Yesu. Ahadi hutiririka rohoni. Amani yetu ni kama mto, wimbi baada ya wimbi la utukufu linapita ndani ya moyo, na hakika tunakula mlo wa usiku pamoja na Yesu na Yeye pamoja nasi. Tunayo hisia ya kutambua upendo wa MUNGU, na tunatulua katika upendo Wake. [Pr 11.3; Maombi Aya ya 19]

Hakuna lugha inayoweza kuielezea, ni zaidi ya maarifa. Sisi ni wamoja na Kristo, maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika MUNGU. Tumehakikishiwa kwamba wakati Yeye ambaye ni maisha yetu atakapotokea, ndipo pia nasi tutatokea pamoja Naye katika utukufu. Kwa ujasiri mkubwa, tunaweza kumwita MUNGU Baba yetu. - (The SDA Bible Commentary 3: 1147, 1148) [Pr 12.1; Maombi Aya ya 20]

Maombi Huleta kufanywa upya kwenye Maisha ya Kiroho – Maisha yetu yanapaswa kuunganishwa na maisha ya Kristo; tunapaswa kuchota kila wakati kutoka Kwake, tukila mwili Wake (uhai wake), Mkate ulio hai ulioshuka kutoka mbinguni, tukichota kutoka kwenye chemchemi iliyo safi/freshi kila wakati, ikitoa hazina zake tele. Ikiwa tunamuweka Bwana mbele ya macho yetu daima, tukiruhusu mioyo yetu kumshukuru na kumsifu, tutakuwa na hali mpya katika maisha yetu ya kidini. Maombi yetu yatachukua mfumo wa mazungumzo na MUNGU kama ambavyo tungezungumza na rafiki. Yeye Atazungumza na sisi kuhusu mafumbo na siri Zake. Mara nyingi zitatuja hisia tamu za kufurahisha za uwepo wa Yesu. Mara nyingi tutahisi mioyo yetu ikiwaka ndani yetu, Bwana anapokaribia kuzungumza nasi kama alivyofanya na Henoko. Pale ambapo uzoefu huu utakuwa halisia kwenye uzoefu wa maisha ya Mkristo, maisha yake yataonyesha unyenyekevu, utulivu, upole, na moyo wa kujishusha chini, kisha ataonekana kwa wale wenzake waliomzunguka kwamba amekuwa na Yesu na kujifunza kutoka Kwake (Christ's Object Lessons, 129, 130) [Pr 12.2; Maombi Aya ya 21]

Mahali pa Kukimbilia Ambapo pako wazi daima – Njia ya kuendea kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kuendelea kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya kuwezesha na kuongozwa. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono yake ya milele itakuwa chini yako. - (In Heavenly Places, 86) [Pr 12.3; Maombi Aya ya 22]

Siri ya Nguvu za Kiroho—Maombi ni pumzi ya roho. Ni siri ya nguvu za kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na halafu afya ya roho ikawa

salama na hata kuhifadhiwa. Ombi huupatia moyo mawasiliano ya haraka na Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini. Puuzia zoezi la sala, au jihusishe na maombi bila mpangilio, yenye kushtukizwa, mara hapa, au pale kama unavyoona inafaa kwako, nawe utafanya mkono wako upoteze kumshikilia MUNGU. Nguvu za kiroho hupoteza ukali wake, na uzoefu wa kidini hukosa afya na nguvu . [Pr 12.4; Maombi Aya ya 23]

Ni jambo la kushangaza na kupendeza sana, kwamba sisi wanadamu tusiostahili tunaweza kuomba kwa ufanisi, kwamba sisi wakosefu tunao uwezo wa kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kutamani kuliko hii,- kuunganishwa katika ushirika na MUNGU asiye na kikomo (wa milele)? Mtu dhaifu, na mwenye dhambi ana upendeleo wa kuzungumza na Muumba wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanafikia kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa malimwengu yote. Tunaweza kuzungumza na Yesu tunapotembea njiani, na Yeye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume. (Messages to Young People, 249. [Pr 13.1; Maombi Aya ya 24]

Maombi ya Siri, moyo wa Dini (moyo wa mionjo ya kiroho)— Usipuuizie maombi ya siri, kwa maana ni moyo wa mambo ya kiroho. Kwa maombi ya dhati, ya bidii omba usafi wa roho. Omba kwa bidii, kwa shauku, na kwa dhati, kama ambavyo ungelionba endapo maisha yako yangekuwa hatarini. Endelea kubakia hapo kwenye uwepo Wake, ukimtumainia MUNGU mpaka matamania ambayo hayawezi kutamkika, yatakapozaliwa ndani yako kwa ajili ya wokovu, na ushahidi mzuri wa dhambi zilizosomehewa umepatikana. —(Spiritual Gifts 2:264) [Pr 13.2; Maombi Aya ya 25]

Kila Ombi la Dhati na bidii husikiwa— Bado wanafunzi walikuwa hawajajua rasilimali za Mwokozi ambazo hazina ukomo. Yeye Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Yeye Atakuwepo mbele za Baba kuwaombea. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu

huwasilishwa Naye kama matamano Yake Mwenyewe binafsi kwa niaba ya roho hiyo. Kila ombi la dhati na usadikisho husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni kwa dhati, basi litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, Naye ataliwasilisha kwa Baba bila hata neno moja la kuudhi, lenye utata, na lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. [Pr 13.3; Maombi Aya ya 26]

Njia ya unyofu na uadilifu sio njia isiyo na kizuizi, lakini katika kila shida tunapaswa kuona mwito kwaajili ya kutoa maombi. Hakuna mtu aliye hai ambaye anayo nguvu yoyote ile ambayo hajaipokea kutoka kwa MUNGU, na chanzo zinapotoka nguvu hizo iko wazi na huru hata kwa yule mwanadamu aliye dhaifu zaidi. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, nitafanya." [Pr 13.4; Maombi Aya ya 27]

"Kwa Jina Langu," Kristo aliwaamuru wanafunzi Wake waombe katika Jina Lake Kristo. Ni katika Jina la Kristo, ndiyo wafuasi Wake wanapaswa kusimama mbele za MUNGU. Kupitia thamani ya kafara iliyotolewa kwa ajili yao, wao wana thamani machoni pa Bwana. Kwa sababu ya haki kupitia Kristo, wanahesabiwa kuwa wa thamani. Kwa ajili ya Kristo, Bwana huwasamehe wale wamchao. Yeye haoni ubaya/uovu wa mwenye dhambi ndani yao. Yeye Anatambua mfano wa Mwanawe, ambaye wanamuamini, ndani yao. - (The Desire of Ages, 667) [Pr 14.1; Maombi Aya ya 28]

Malaika hunakili Maombi yetu na kutushawishi kuelekea yale yaliyo mema—Unapoamka asubuhi, Je! Unahisi kukosa kwako msaada na kutojiweza, na hitaji lako la kuwezesha kutoka kwa MUNGU? Na je, kwa unyenyekevu, kwa moyo wote unamjulisha Baba yako wa mbinguni matakwa yako? Ikiwa ndivyo, malaika hunakili maombi yako, na ikiwa maombi haya hayajatoka nje ya midomo ya unafiki/feki, basi, wakati umo katika hatari ya kutenda mabaya bila kujua na kutoa ushawishi ambao utasababisha wengine kutenda mabaya, malaika wako mlezi/mlinzi atakuwa kando yako, kukufundisha kilicho bora, akikuchagulia maneno, na kuathiri matendo yako. [Pr 14.2; Maombi Aya ya 29]

Ikiwa hauhisi hatari yoyote, na ikiwa hautoi maombi ya kusihhi msaada na nguvu za kupinga vishawishi, hakika utapoteza dira, kwani utaenda kwenye njia zisizo sahihi; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile ya hukumu. - (Testimonies for the Church 3: 363, 364) [Pr 14.3; Maombi Aya ya 30]

Kama Musa, Sisi Tunaweza Kufurahia Ushirika wa Karibu Na MUNGU— Mkono huo uliomba malimwengu yote (universe), Mkono huo ambao unaishikilia milima ikae katika nafasi zake, unamchukua mtu huyu aliyeumbwa kutoka kwenye mavumbi, - mtu huyu mwenye imani yenye nguvu, - na kwa rehema inamfunika katika pango la mwamba, wakati utukufu wa MUNGU na wema Wake wote ukipita na kujidhihirisha mbele zake. Je! Kweli sisi Tunaweza kushangaa kwamba "utukufu unaopita ubora wote" ulioakisiwa kutoka kwa Yeye Aliye na Nguvu zote uliangaza usoni mwa Musa na mwangaza uliosheheni, kiasi kwamba watu hawakuweza kuutazama kwa macho. Alama hii ya MUNGU iliyokuwa juu yake, ilimfanya aonekane kama mmoja wa malaika wanaoang'aa kutoka kwenye kiti cha enzi. [Pr 14.4; Maombi Aya ya 31]

Uzoefu huu, tofauti na uzoefu wa hapo awali ulionyesha kwamba MUNGU atasikia maombi yake, na kwamba uwepo Wake MUNGU utamhudumia kikamilifu, na jambo hilo likawa la thamani zaidi kwa Musa kama kiongozi kuliko elimu na mafunzo yote aliyopata kwa Wamisri, au mafanikio yake yote katika sayansi ya kijeshi ya Misri. Hakuna nguvu ya kidunia au ustadi au kisomo/elimu, inayoweza kuchukua nafasi ya uwepo wa MUNGU. Katika historia ya Musa tunaweza kuona ushirika wa karibu sana na MUNGU ambao ni fursa ya kila mwanadamu kuufurahia. Kwa mkosaji ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai. Lakini Musa hakuogopa kuwa peke yake na Mwandishi wa sheria hiyo ambayo ilikuwa imenenwa utukufu na ukuu wa kutisha namna ile, kutoka Mlima Sinai; kwani roho yake ilikuwa katika upatanifu wa mapenzi ya Muumba wake. [Pr 15.1; Maombi Aya ya 32]

Maombi ni kuufungua moyo kwa MUNGU kama tuufunguavyo kwa rafiki. Jicho la imani litamtambua MUNGU aliye karibu sana, na mwombaji anaweza kupata

ushahidi wa thamani wa upendo wa Mungu na kujali Kwake. - (Gospel Workers, 34, 35) [Pr 15.2; Maombi Aya ya 33]

Omba kwa ujasiri mtakatifu—Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. "Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni fursa ya upendeleo kwetu kumwendea Yeye tukiwa na ujasiri mtakatifu. Tukiwa dhati na wanyofu, tunamwomba Yeye aache nuru Yake iangaze juu yetu, Yeye Atatusikia na kutujibu. - (Child Guidance, 499) [Pr 15.3; Maombi Aya ya 34]

Mbingu iko wazi kwa ajili ya maombi yetu, na tunaalikwa kwenda "kwa ujasiri kwenye Kiti cha Neema, ili tupate rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa shida." Tunapaswa kwenda kwa imani, tukiamini kwamba tutapata vile vitu tunavyoomba Kwake. - [Pr 15.4; Maombi Aya ya 35]

Ombea Mahitaji Yetu — Kila ahadi katika Neno la MUNGU huja pamoja na jambo/mada ya kuombea, ikileta Neno la Yehova lililoahidiwa kama uthibitisho kwetu. Baraka yoyote ya kiroho tunayohitaji, tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, tukiwa na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda, tukimwomba mkate, mavazi na Mkate wa Uzima na vazi la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, nawe umealikwa kumuomba kuhusu hivi vyote. Ni kwa kupitia Jina la Yesu tu, ndiyo tunapokea kila neema, baraka na kibali (favor). MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake. —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 15.5; Maombi Aya ya 36]

Omba na Amini — Unapomwomba Bwana akusaidie, Mtukuze Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea baraka Yake. Nguvu zote, hekima zote, ziko chini ya maamuzi/uwezo wetu kuziagiza zije * (ziko chini ya amri yetu!). Wajibu wetu sisi ni kuomba tu. [Pr 16.1; Maombi Aya ya 37]

Tembea daima katika nuru ya MUNGU. Tafakari mchana na usiku juu ya tabia Yake. Ndipo utaona uzuri Wake na kufurahi kwa wema Wake. Moyo wako utaangaziwa na

kung'aa na hisia ya upendo Wake. Utainuliwa kana kwamba umebebwa na mikono ya milele. Ukiwa na nguvu na nuru ambayo MUNGU hutoa, unaweza kuelewa zaidi na kutimiza mengi zaidi ya ulivyoona kuwa inawezekana hapo awali. - (The Ministry of Healing, 514) [Pr 16.2; Maombi Aya ya 38]

Songa mbele, ukimtumaini MUNGU— Tunapaswa kuhamasishana katika imani iliyo hai ambayo Kristo amemwezesha kila muumini kuwa nayo. Kazi inapaswa kusonga mbele wakati Bwana akiandaa njia. Yeye Anapowapitisha watu Wake katika maeneo yenye dhiki, basi ni fursa yenye upendeleo kwao kukusanyika pamoja kwa ajili ya maombi, wakikumbuka kuwa vitu vyote vinatoka kwa MUNGU. Wale ambao bado hawajapitia nyakati ngumu, ambazo zinahusu kazi katika siku hizi za mwisho, hivi karibuni watalazimika kupita kwenye matukio ambayo yatajaribu sana imani na ujasiri wao kwa MUNGU. Ni wakati ambapo watu Wake hawaoni njia ya kusonga mbele, wakati Bahari ya Shamu iko mbele yao na jeshi likiwafuata nyuma yao, hapo ndipo MUNGU anawaamuru: "Songeni mbele." kwa kufanya hivi, Yeye anazijaribu imani zao. Wakati uzoefu kama huo unakujia, wewe songa mbele, ukimtumainia Kristo. Tembea hatua kwa hatua katika njia Anayoionyesha kwa kuiwekea alama. Majaribu yatakuja, lakini songa mbele. Hii itakupa uzoefu ambao utaimarisha imani yako kwa MUNGU na kujipatia stahiki kwa huduma ya Kweli. —(Testimonies for the Church 9:273) [Pr 16.3; Maombi Aya ya 39]

SURA YA 2

UHITAJI WETU WA MAOMBI (Hitaji Letu la Sala)

Sala ni ya Muhimu Maishani kama Chakula cha Kila Siku - Maombi ya kila siku ni muhimu sana katika ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha kidunia kilivyo, kwa ustawi wa mwili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika

sala. Ikiwa akili itamangamanga, lazima tuirudishe kwa bidii isiyokoma, hatimaye mazoea haya, yatafanya mambo kuwa rahisi. Hatuwezi hata kidogo kujitenga mbali na Kristo hata kwa nukta moja na kisha tukawa salama. Tunaweza kuwa na uwepo Wake pamoja nasi katika kila hatua tunayopiga, lakini ni kwa kuzingatia tu masharti ambayo Yeye Mwenyewe ameyaweka. – (Messages to Young People, 115) [Pr 17.2; Maombi Aya ya 40]

Maombi ni muhimu Kiroho – Ingawa Kristo alikuwa amewapa wanafunzi Wake ahadi kwamba wangepokea Roho Mtakatifu, hii haikuondoa umuhimu wa sala. Waliomba kwa bidii zaidi; waliendelea kusali kwa moyo mmoja. Wale ambao sasa wanahusika na kazi kuu ya kuandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Bwana, wanapaswa pia kuendelea katika maombi. (Gospel workers, 371) [Pr 17.2; Maombi Aya ya 41]

Wanafunzi wa Yesu hawakutii onyo lililorudiwa "Kesheni na mkaombe." Mwanzoni walipata tabu sana kumwona Bwana na Mwalimu wao, aliyekuwa na tabia tulivu, mwungwana na mwenye kujistahi au hadhi ya kifalme, sasa akipambana mieleka na huzuni ambayo ilikuwa zaidi ya ufahamu wa kawaida. Walikuwa wameomba waliposikia kilio kikuu cha Yule Anayetaabika. Hawakuwa na nia ya kumtelekeza Mola wao, lakini walionekana kupooza kwa usingizi ambao wangeweza kuutupilia mbali ikiwa wangeendelea kumwomba MUNGU. Hawakutambua umuhimu wa kukesha na kuomba kwa bidii ili kuhimili majaribu. - (The Desire of Ages, 688) [Pr 17.3; Maombi Aya ya 42]

Uzoefu wa wanafunzi katika Bustani ya Gethsemane una somo kwa watu wa Bwana leo....Hawakutambua umuhimu wa kukesha na kuomba kwa bidii ili kuyapinga majaribu. Wengi leo wamelala usingizi mzito, kama walivyokuwa wanafunzi. Hawakeshi na kuomba ili wasiingie katika majaribu. Hebu nasi tusome na kuchunguza mara kwa mara kwa uangalifu sehemu hizo za Maneno ya MUNGU ambazo zinarejelea siku hizi za mwisho, yakionyesha hatari ambazo zitakuwa tishio kwa watu wa MUNGU. - (In Heavenly Places, 97) [Pr 18.1; Maombi Aya ya 43]

Maombi ni uhai wa roho – Maombi ni muhimu; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, haya

yana nafasi yake; lakini ni ushirika wetu binafsi wa siri na MUNGU ndio unaodumisha maisha ya roho. (Education, 258) [Pr 18.2; Maombi Aya ya 44]

Sala ni muhimu kwa Afya ya Kiroho - Mara kadhaa, kila siku, nyakati bora zenye thamani, zinatakiwa kuwekwa wakfu kwa njia ya maombi na kusoma Maandiko, hata ikiwa ni kwa kuweka maandishi kwenye kumbukumbu kwa kukariri, ili maisha ya Kidini/kiroho yaweze kuwepo ndani ya roho. Maslahi anuwai ya msingi ya kazi ya Mungu huja/hutupatia chakula cha kutafakari na nguvu kwa sala zetu. Ushirika na MUNGU ni muhimu sana kwa afya ya kiroho, na hapa tu ndipo inaweza kupatikana ile hekima na maamuzi sahihi ambayo ni muhimu sana katika kutekeleza majukumu ya kila siku. –(Testimonies for the Church 4:459) [Pr 18.3; Maombi Aya ya 45]

Kielelezo cha Yesu Huonyesha Umuhimu wa Maombi—Laiti wale wapazao sauti kuu za maonyo kwa ajili ya wakati huu wangelitambua wajibu wao kwa Mungu, wangeliona umuhimu wa maombi yenye bidii/ari. Pale miji iliponyamazishwa tuli katika usingizi wa usiku wa manane, wakati kila mtu alikuwa ameenda nyumbani kwake, Kristo, Mfano wetu, Alienda Mlima wa Mizeituni, na huko katikati ya miti yenye giza nene, alikuwa akikesha usiku mzima katika maombi. Yeye, Yule ambaye hakuwa hata na doa la dhambi,- nyumba ya hazina ya baraka; ambaye sauti Yake ilisikika katika mkesho wa usiku na kisha wanafunzi wakaogopa katika ile bahari yenye dhoruba, katika baraka ya ombi la kimbangu; na ambaye Neno Lake linaweza kuwaita wafu kutoka makaburini mwao, Yeye Ndiye Yule aliyeomba dua kwa kilio kizito na machozi. Yeye hakuomba kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa wale ambao alikuja kuwaokoa. Alipokuwa mwombezi, Akitafuta kwenye Mkono wa Baba Yake nguvu mpya, na akatoka akiwa amepewa nguvu mpya na kama mbadala wa mwanadamu, Alijitambulisha na mateso ya ubinadamu, na akawapa mfano wa umuhimu wa maombi. [Pr 18.4; Maombi Aya ya 46]

Asili Yake haikuwa na doa au uchafu wa dhambi. Kama Mwana wa Adamu, Aliomba kwa Baba, kuonyesha kwamba asili ya ubinadamu inahitaji msaada wote utokao kwa Bwana, ambao mwanadamu anaweza kupata ili aweze kujiandaa kwa majukumu na kutayarishwa kwa majaribu na

mitihani ya maisha. Kama Mfalme wa Uzima, alikuwa na nguvu na MUNGU, na Aliwashindia watu Wake. Mwokozi huyu, ambaye aliwaombea wale ambao waliona hawakuwa na haja ya maombi, na kulia kwa ajili ya wale ambao hawakuona haja ya kutoa machozi, sasa Yuko mbele ya kiti cha enzi, kupokea na kuwasilisha kwa Baba Yake maombi ya wale Aliowaombea duniani (soma kitabu cha Waebrania nane na tisa, kuhusu huduma Yake sasa). Mfano wa Kristo umewekwa kwetu ili tuufuate. Maombi ni muhimu katika utendaji kazi wetu kwa wokovu wa roho za watu. MUNGU peke Yake Ndiye anayeweza kutoa ongezeko la mbegu tunazopanda.–(Gospel Workers, 28, 29) [Pr 19.1; Maombi Aya ya 47]

Yesu alihimiza Umuhimu wa Maombi – Yeye [Yesu] aliwahimiza watu umuhimu wa sala, toba, kukiri, na kuitelekeza dhambi. Aliwafundisha uaminifu, uvumilivu, rehema, na huruma, akiwaamuru wapende sio tu wale wanaowapenda, bali hata wale wanaowachukia, ambao wanawaudhi. Kwa hili alikuwa akiwafunulia tabia ya Baba, ambaye ni mvumilivu, Mwenye huruma, na Mwenye neema, si mwepesi wa hasira, na amejaa wema na Ukweli. - (Christian Education, 74) [Pr 19.2; Maombi Aya ya 48]

Maombi yalikuwa Muhimu kwa Danieli – Danieli alikabiliwa na vishawishi vikali ambavyo vinaweza kuwashambulia vijana wa leo; na bado alikuwa imara kwa mafundisho ya kidini aliyoyapokea hapo awali katika maisha. Alikuwa amezungukwa na vishawishi vilivyokorokotolewa kupotosha wale ambao wangelegalega kutoka katika kanuni na mwelekeo; ila Neno la MUNGU linamwonyesha kama mtu asiye na makosa. Daniel hakuthubutu kutumainia nguvu zake mwenyewe za kiadili. Maombi yalikuwa ni ya lazima kwake. Alimfanya MUNGU kuwa nguvu yake, na hofu ya Mungu ilikuwa mbele yake kila wakati katika shughuli zote, za maisha yake.- (Fundamentals of Christian Education, 78) [Pr 19.3; Maombi Aya ya 49]

Kukua kiroho kunategemea Maombi - Ikiwa kungekuwa na kusali zaidi kati yetu, mazoezi zaidi ya imani hai, na kutegemea kwa udogo sana maombi ya mtu mwingine kuwa kama mbadala wa uzoefu wetu, basi tungekuwa mbali zaidi na mahali tulipo leo katika akili ya kiroho. Tunachohitaji ni uzoefu wa kina, wa moyo na roho wa mtu binafsi. Ndipo

tutaweza kusema ni nini MUNGU anafanya na jinsi anavyofanya kazi. Tunahitaji kuwa na uzoefu hai katika mambo ya MUNGU; na sisi hatuko salama mpaka tutakapokuwa na uzoefu huo. Kuna wengine ambao wana uzoefu mzuri, na wanaweza wakuambie juu yake; lakini unapokuja kuupima, unaona kuwa huo sio uzoefu sahihi, kwani hauedani na Ukweli wa “Bwana asema hivi.” Ikiwa kuna wakati katika historia yetu tuliohitaji kujinyenyekeza roho zetu binafsi mbele za MUNGU, basi ni leo. Tunahitaji kumwendea MUNGU kwa imani katika yote yaliyoahidiwa katika Neno, na kisha tutembeee katika nuru na nguvu zote ambazo MUNGU anatoa. - (The Review and Herald, Julai 1, 1909) [Pr 20.1; Maombi Aya ya 50]

Maombi Yanahitajika Kila Siku – Dini lazima ianze kwa kuumimina, kuusafisha na kuutakasa moyo, na inapaswa kurutubishwa, nakulishwa kwa sala ya kila siku. – (Testimonies for the Church 4:535) [Pr 20.2; Maombi Aya ya 51]

Inafaa, na inawezekana kabisa, na pia ni muhimu sana kwetu, kuomba mara tatu kwa siku kama ilivyokuwa kwa Danieli. Maombi ni pumzi ya roho, msingi wa ukuaji wa kiroho. Nyumbani kwako, mbele ya familia yako, na mbele ya watendakazi wako, unapaswa kushuhudia Ukweli huu. Na unapobahatika na fursa ya kukutana na ndugu zako kanisani, waambie juu ya umuhimu wa kuweka wazi njia ya mawasiliano kati ya MUNGU na moyo wako. Waambie kwamba ikiwa watapata moyo na sauti ya kuomba, basi MUNGU Naye atakuwa na majibu ya maombi yao. Waambie wasipuuze majukumu yao ya kidini. Wahimize ndugu kuomba. Lazima tutafute ikiwa tutapata, lazima tuombe ikiwa tutapokea, lazima tubishe hodi ikiwa tutafunguliwa mlango. - (The Signs of the Times, Februari 10, 1890) [Pr 20.3; Maombi Aya ya 52]

Katika huduma ya ukuhani wa Kiyahudi tunakumbushwa kila wakati juu ya dhabihu na maombezi ya Kristo. Wote wanaokuja kwa Kristo leo wanapaswa kukumbuka kuwa neema Yake ni uvumba unaochanganyika na maombi ya wale wanaotubu dhambi zao na kupokea msamaha na rehema na neema. Hitaji letu la maombezi ya Kristo ni endelevu. Siku kwa siku, asubuhi na jioni, moyo mnyenyekevu unahitaji kutoa maombi ambayo yatarudishiwa majibu ya neema na amani na furaha. “Basi,

kwa njia ya Yesu, tumtolee MUNGU dhabihu ya sifa daima, hayo ni matunda ya midomo yetu, ikitoa shukrani kwa Jina Lake. Msisahau kutenda mema na kusaidiana, maana hizi ndizo dhabihu zinazompendeza Mungu. SDA Bible Commentary 6:1078) [Pr 21.1; Maombi Aya ya 53]

Kama wazee wa zamani, wale wanaodai kumpenda MUNGU tunapaswa kumjengea Bwana madhabahu popote pale wanapopiga hema zao. Ikiwa kuna muda ambapo kila nyumba ilipaswa kuwa nyumba ya sala, basi ni sasa. Akina baba na mama wanapaswa kuinua mioyo yao kwa MUNGU kwa dua ya unyenyekevu kwao na kwa watoto wao. Hebu baba kama kuhani wa nyumba, aweke juu ya madhabahu ya Mungu dhabihu ya asubuhi na jioni, wakati mke na watoto wanaungana katika maombi na sifa. Katika nyumba kama hiyo Yesu atapenda kukaa hapo na atakawia-kawia kutoka hapo. [Pr 21.2; Maombi Aya ya 54]

Nuru takatifu inapaswa kuangaza kutoka katika kila nyumba ya Kikristo. Upendo unapaswa kufunuliwa kwa vitendo. Nao unapaswa kutiririka katika mahusiano yote ya nyumbani, ukijionyesha katika ukarimu, upole, na adabu iliyo na uungwana usio na ubinafsi. Kuna nyumba ambazo kanuni hii hufanywa, nyumba zile ambazo MUNGU huabudiwa, na upendo wa Kweli hutawala. Kutoka kwa nyumba hizi sala ya asubuhi na jioni hupanda juu kwa MUNGU kama uvumba mtamu, na rehema Zake na baraka hushuka juu ya waombaji kama umande wa asubuhi. - (Patriarchs and Prophets, 144) [Pr 21.3; Maombi Aya ya 55]

Katika kumfuata Kristo, kumtazama Yeye Mwenye kuanzisha Na kuitimiza imani yetu, utahisi kuwa unafanya kazi chini ya jicho Lake, kwamba unaathiriwa na uwepo Wake, na kwamba Yeye Anajua nia zako. Katika kila hatua utauliza kwa unyenyekevu: Je! Hili litampendeza Yesu? Je! hii itamtukuza MUNGU? Asubuhi na jioni sala zako za dhati zinapaswa kupaa kwa MUNGU kwa baraka na mwongozo Wake. Maombi ya Kweli humshika Mweza yote na hutupatia ushindi. Kwa magoti yake, Mkristo anapata nguvu ya kuyapinga majaribu. - (Testimonies for the Church 4:615, [Pr 21.4; Maombi Aya ya 56]

Kadiri makuhani walivyoingia asubuhi na jioni mahali Patakatifu wakati wa uvumba, dhabihu ya kila siku ilikuwa tayari kutolewa juu ya madhabahu mahali pa wazi. Huu

ulikuwa wakati wa kuvutia/kupendeza sana kwa washiriki waliokusanyika katika mahali pa kuabudia. Kabla ya kuingia katika uwepo wa MUNGU kupitia huduma ya kuhani, walipaswa kushiriki kwa unyofu na bidii katika kuuchunguza moyo na kukiri dhambi. Waliungana katika sala ya kimya, nyuso zao zikielekea pahali Patakatifu. Kwa hivyo maombi yao yalipaa pamoja na wingu la ubani, huku imani ikiwa juu ya stahiki na sifa za Mwokozi aliyeahidiwa, na zikiwakilisha dhabihu ya upatanisho. Saa zilizowekwa kwa ajili ya dhabihu ya asubuhi na ya jioni zilizingatiwa kuwa takatifu, na zikatumika kama wakati uliowekwa kwa ibada katika taifa lote la Kiyahudi. Na wakati wa baadaye Wayahudi walipotawanyika/walipotawanywa kama mateka katika nchi za mbali, bado waliendelea katika saa ile ile iliyowekwa kuelekeza nyuso zao kuelekea Yerusalemu na kutoa maombi yao kwa MUNGU wa Israeli. Katika desturi hii Wakristo wana mfano kuhusiana na sala ya asubuhi na jioni. Wakati MUNGU analaani milolongo ya kaida na sherehe tu, bila roho ya ibada, Yeye huwaangalia kwa furaha wale wanaompenda, wainamao asubuhi na jioni ili kutafuta msamaha wa dhambi walizotenda na kuwasilisha maombi yao kwa baraka zinazohitajika.—(Patriarchs and Prophets, 353, 354) [Pr 22.1; Maombi Aya ya 57]

Maombi Hutuunganisha na Mbingu — Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko, wataunganishwa na mbingu, kisha watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo mazuri, matamania bora, ufahamu dhahiri kuhusu Ukweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watamiliki shauku ya kuwa usafi wa moyo, nuru, na upendo, na neema zote zinazozaliwa Mbinguni. Maombi yao ya dhati na bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia. Watu hawa watakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na Kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni vipo kwa ajili yao, nao watasafishwa, watainuliwa, na kuboreshwa na uhusiano huu wa karibu na MUNGU. Huo ndio upendeleo walio nao Wakristo wa Kweli. (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 22.2; Maombi Aya ya 58]

Maombi Yanapaswa kuwa Shughuli ya Kwanza ya Siku (mkakati wa kwanza wa siku) — Jiweke wakfu kwa MUNGU

wakati wa asubuhi; fanya hili kuwa kazi yako ya kwanza kabisa. Hebu Ombi lako liwe, “Nichukue, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako.” Hili ni suala la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa MUNGU kwa ajili ya siku hiyo. Salimisha mipango yako yote, ili itekelezwe au isitelekezwe kulingana na hekima/majaliwa Yake Mungu yatakavyoongoza. Kwa namna hiyo unakuwa umeyatoa maisha yako mikononi Mwake MUNGU, na kwa njia hiyo utaumbwa/utafinywanga na kufanana zaidi na zaidi na maisha ya Kristo. - (Steps to Christ, 70) [Pr 23.1; Maombi Aya ya 59]

Shauku ya kwanza kabisa ya roho wakati wa asubuhi inapaswa kuwa kwa ajili ya uwepo wa Yesu. "Pasipo Mimi," Anasema, " wewe huwezi kufanya lolote." Yesu Ndiye tunayemhitaji; Nuru Yake, Maisha Yake, na Roho Yake, vinapaswa kuwa vyetu daima. Tunamuhitaji Yeye kila saa. Na tunapaswa kuomba wakati wa asubuhi kwamba kama jua linavyoangazia nchi, na kuweka nuru katika ulimwengu, basi vivyo hivyo Jua la Haki liangaze katika vyumba vya ubongo na moyo, na kutufanya sisi sote kuwa nuru katika Bwana. Hatuwezi kufanya jambo lolote bila uwepo Wake hata nukta moja. Adui anajua pale tunapoamua kufanya mambo bila Bwana wetu, naye yupo karibu, tayari kuzijaza akili zetu na mapendekezo yake ya uovu ili tushindwe kuwa thabiti; lakini ni shauku ya Bwana kwamba kila wakati tuwe ndani Yake, na kwamba tuwe wakamilifu ndani Yake. - (My Life Today, 15) [Pr 23.2; Maombi Aya ya 60]

Maombi ni Wajibu—Hakuna kitu chenye kukuza afya ya mwili na roho zaidi kuliko roho ya shukrani na sifa. Ni jukumu letu chanya, la uhakika na muhimu sana, kuipinga roho ya huzuni, na pia mawazo na hisia za kutoridhika kama ambavyo ilivyo muhimu kuomba. - (The Ministry of Healing, 251) [Pr 23.3; Maombi Aya ya 61]

Pale Ambapo Hatujisikii Kuomba ndio Maombi yahitajika zaidi — Pale ambapo hatujisikii kuwasiliana na Yesu, hebu tuombe zaidi, kwani ndipo tunapopaswa kuomba zaidi. Kwa kufanya hivyo tutavunja mtego wa Shetani uliojificha, kisha mawingu ya giza yatatoweka, na

tutahisi uwepo wa Yesu. - (Lift Him Up, 372) [Pr 24.1; Maombi Aya ya 62]

Giza Huwafunga Wale Wanaopuuza Maombi – Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa Mungu, alihisi hitaji la maombi/kusali, Je basi hitaji la maombi ya dhati na ya bila kukoma halitakuwa zaidi kwa wanadamu dhaifu, wanyonge, wenye dhambi na wanaokufa? [Pr 24.2; Maombi Aya ya 63]

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu na wingi wa baraka Zake. Tumependelewa kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo Wake usio na mipaka. Inastaajabisha kwa kiasi gani kwamba tunaomba kidogo sana! MUNGU Yupo tayari kusikia maombi ya dhati na ari ya watoto Wake wanyenyekevu na walio na hali duni sana, na bado kuna kusitasita kwingi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU matakwa yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini jamani, kuhusu wanadamu hawa maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa MUNGU wenye upendo usio na kikomo unawainamia wao kwa matamano, Naye akiwa tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kuwazia, lakini bado wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika wanapenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona kuwa karibu na MUNGU ndiyo furaha yao kuu; lakini wanadamu waishio chini duniani, ambao wanahitaji msaada mkubwa ambao unaweza kutolewa na MUNGU tu, wanaonekana kuridhika kutembea bila nuru ya Roho Wake, bila ushirika wa uwepo Wake. [Pr 24.3; Maombi Aya ya 64]

Giza la yule mwovu linawafunga wale wanaopuuza kuomba. Minong'ono ambayo adui anawanong'onezea huwashawishi kutenda dhambi; na hii yote ni kwa sababu hawatumii fursa ambazo MUNGU amewapa katika wasaa mzuri wa miadi Naye kwa maombi. Kwa nini wana na binti za MUNGU wanasita-sita kuomba, wakati maombi ni ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za hazina za mbinguni, ambako zimetunzwa tunu tele, zisizo na kikomo za Mweza wa Yote? - (Steps to Christ, 94) [Pr 24.4; Maombi Aya ya 65]

Epuka Kupuuzia Maombi-Kesha na chungu ndugu, wakati nuru yako ya kwanza inaanza kufifia, wakati

unapuuzia sala kwa mara ya kwanza, wakati unaona dalili za kwanza ya usingizi wa kiroho. –(Testimonies for the Church 4:124) [Pr 24.5; Maombi Aya ya 66]

Unapaswa kukesha, ili pilikapilika nyingi za maisha haya zisisababishe upuuzie maombi wakati unapohitaji zaidi nguvu ambayo maombi yanaweza kutoa. Hali ya utauwa, yaani kumpenda Mungu, ipo hatarini kwa roho kuzongwa/kuminywa zaidi na shughuli za maisha haya. Ni uovu mkubwa kuinyima roho nguvu na hekima ya mbinguni inayokusubiri, na unayoihitaji mno na ambayo ipo tayari kwa ajili yako unapoiomba. Unahitaji nuru ile ambayo MUNGU pekee Ndiye anayeweza kutoa. Hakuna mtu anayeweza kuwa na stahiki ya kuanza kufanya kazi Yake, isipokuwa awe na hekima hii.- (Testimonies for the Church 5:560) [Pr 25.1; Maombi Aya ya 67]

Shetani Huwadanganya Wale Wasiofanya Maombi—
(Wale ambao hawayachunguzi maandiko kwa bidii na kusalimisha kila shauku na kusudi la maisha Kwake Yule Asiyekosea, wote ambao hawamtafuti MUNGU katika maombi kwa ajili ya kuyajua mapenzi Yake, hakika watatangatanga mbali na njia sahihi na kuangukia kwenye hila/udanganyifu wa Shetani—((Testimonies for the Church 5: 192) [Pr 25.2; Maombi Aya ya 68]

Majaribu Hufanya Maombi Kuwa ya Lazima – Nguvu inayopatikana katika kupeleka maombi kwa MUNGU, ikiunganishwa na juhudi za mtu binafsi katika kuifundisha na kuizoeza akili kufikiri kwa kina na kuwa mwangalifu, humwandaa mtu huyo kwa ajili ya majukumu ya kila siku na hufanya roho iwe na amani katika mazingira yote, haijalishi hali ni ngumu kiasi gani. Majaribu ambayo tunaanikwa katika mazingira yake kila siku, hufanya maombi kuwa jambo la lazima. Ili tuweze kulindwa na uweza wa MUNGU kwa njia ya imani, shauku ya nia, inapaswa kuelekezwa daima mbinguni katika maombi ya kimya ili kupata msaada, kupata nuru, kupata nguvu, kupata maarifa. Lakini fikra na maombi hayawezi kuchukua nafasi ya kuwa dhati na juhudi katika kuboresha utumiaji wa muda vizuri na kwa uaminifu. Kazi na sala vyote vinahitajika katika kukamilisha tabia ya Kikristo. [Pr 25.3; Maombi Aya ya 69]

Lazima tuishi maisha ya pande mbili, maisha ya kufikiri na kutenda, maisha ya maombi ya kimya na kufanya kazi kwa juhudi.... Mungu anatutaka tuwe barua hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Roho inayomgeukia Mungu kwa ajili ya kupata nguvu, sapoti/msaada, uwezo, kwa maombi ya bidii ya kila siku, itakuwa na mawazo yaliyoboreshwa, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, malengo ya juu kwenye utendaji, na kuendelea kuwa na njaa na kiu ya haki.—(God’s Amazing Grace, 317) [Pr 25.4; Maombi Aya ya 70]

Sala Inahitajika Sasa Zaidi Kuliko Siku Za Awali – Lazima tuwe katika maombi sana ikiwa tutaendelea mbele katika maisha ya ucha Mungu (Kiungu/kimbingu). Wakati ujumbe wa ile Kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, Lo! ni kwa bidii kiasi gani tuliomba. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika chumbani, ghalani, kwenye bustani ya miti ya matunda, au kwenye vijisitu. Mara kwa mara tulitumia masaa kadhaa kwa maombi ya dhati, watu wawili au watatu wakiwa pamoja walidai ahadi; mara nyingi sauti ya kulia ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa. Sasa siku ya MUNGU (yaani hukumu ya mwisho) iko karibu kuliko wakati tulipoanza kuamini, na tunapaswa kuwa na bidii, kudumu kuwa na usongo/ari, na shauku nzito zaidi kuliko siku zile za mwanzo. Hatari zetu ni kubwa sasa kuliko hapo awali. Mioyo imefanywa kuwa migumu zaidi. Tunahitaji sasa kujazwa na roho ya Kristo, na hatupaswi kupumzika mpaka tuipokee. —(Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 26.1; Maombi Aya ya 71]

Mtafute Bwana kwa Moyo Wote – Maombi yetu yanapaswa kujazwa na upole, huruma na upendo. Tunapotamani ufahamu wa kina na mpana zaidi wa upendo wa Mwokozi, tutamlilia MUNGU atupatie hekima zaidi. Ikiwa kulikuwa na haja ya sala na mahubiri yanayochochea roho, ni sasa. Mwisho wa vitu vyote umekaribia. Laiti tungeweza kuona kama tunavyotakiwa, kuhusiana na umuhimu wa kumtafuta Bwana kwa moyo wote! Basi Tungelimpata. Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba. —(God’s Amazing Grace, 92) [Pr 26.2; Maombi Aya ya 72]

Maombi Sio upotezaji wa muda - Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi yako na sala. Usifikirie kuwa kufanya hivi

ni kupoteza mida tu; huu ni wakati ambao utaishi zama za umilele wote (enzi zote). Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho vitaletwa. Mwili wako utaitikia mguso wa Mkono wa Mwalimu na Bwana. Hakika baraka za MUNGU zinastahili kuombwa, na kazi haiwezi kufanywa vyema au inavyopaswa, isipokuwa ina mwanzo ulio sahihi. Mikono ya kila mfanyakazi lazima iimarishwe, moyo wake lazima utakaswe, kabla Bwana hajamtumia mtu huyo kwa ufanisi zaidi.—(Testimonies for the Church 7:194) [Pr 26.3; Maombi Aya ya 73]

Wachache Wanathamini Fursa ya Maombi – Tunapaswa kukesha na kufanya kazi na kuomba kana kwamba hii ndiyo siku yetu ya mwisho ambayo tumepewa/tutapewa. Je, maisha yetu yangukuwa na bidii nzito na ya dhati kiasi gani. Na ni kwa ukaribu wa jinsi gani tungemfuata Yesu katika maneno na matendo yetu yote. [Pr 26.4; Maombi Aya ya 74]

Kuna wachache tu wanaothamini au kuboresha upendeleo wa thamani wa maombi. Tunapaswa kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu yote. Tunaweza kumpelekea masumbufu na wasiwasi wetu mdogo, dhiki zetu ndogo na hata shida zetu kubwa. Chochote kinachojitokeza kutusumbua au kutufadhaisha, tunapaswa kukipeleka kwa Bwana katika maombi. Tutakapohisi kuwa tunahitaji uwepo wa Kristo kwa kila hatua, Shetani atakuwa na nafasi ndogo ya kupenyeza majaribu yake bila ya kukaribishwa. Ni juhudi yake ya makusudi/anayokusuidia, na anayoifanyia utafiti, kutuweka mbali na rafiki Yetu bora na Mwenye huruma. Hatupaswi kumfanya mtu yeyote kuwa msiri wetu, na kumtumaini, ila Yesu. Tunaweza kuzungumza na kuwasiliana Naye kwa usalama kuhusiana yote yaliyo ndani ya mioyo yetu. – (Testimonies for the Church 5:200, 201) [Pr 27.1; Maombi Aya ya 75]

Maombi Zaidi yanahitajika Mwisho Unapokaribia – Mashirikisho ya vyama yataongezeka kwa idadi na nguvu tunapokaribia mwisho wa wakati (confederacies or unions). Mashirika haya yataunda ushawishi kinzani dhidi ya ile Kweli, na kuunda miungano mipya ya wanaojiita waumini ambao wataziweka kwenye vitendo nadharia zao za udanganyifu. Uasi utaongezeka. "Wengine watajitenga na

imani, wakizingatia roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani" (1 Timotheo 4: 1). Wanaume na wanawake wameungana kumpinga Bwana MUNGU wa mbinguni, na kanisa bado halijaamka kikamilifu ili kuitambua hali hiyo kwa ukamilifu wake. Kuna haja ya kuwa na maombi zaidi, na bidii zaidi, kati ya wale wanaodai kuwa waumini. – (Selected Messages 2:383) [Pr 27.2; Maombi Aya ya 76]

“Kama kulikuwa na wakati ambapo tunapaswa kukesha na kuomba kwa dhati na bidii, ni sasa. Kunaweza kuwa na vitu vinavyodhaniwa kwa mwonekano wake kama ni vitu vizuri, ila bado vinahitaji kuchujwa kwa uangalifu na maombi mengi, kwani ni nyenzo maalum za adui zinazomereta ili kupotosha roho za wanadamu kwenda katika njia inayokaribiana sana na njia ya Kweli na hata kuleta utata katika kutofautisha na ile njia inayoongoza kwenye utakatifu na mbinguni. Lakini jicho la imani linaweza kugundua kwamba njia hii, imechepuka kutoka kwenye njia sahihi, ingawa hila hizo sio rahisi kugundulika. Mwanzoni inaweza kudhaniwa kuwa ni njia chanya na sahihi, lakini baada ya muda itaonekana kuwa imetofautiana sana na njia yenye usalama, mbali sana na njia inayoongoza kwenye utakatifu na mbinguni. - (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 229) [Pr 27.3; Maombi Aya ya 77]

Ushindi Kupitia Maombi ya Kila Siku – Kupitia maombi ya kila siku kwa MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake ili kumudu mizozo, mitafaruku na hali halisi ngumu na kali za maisha, na kisha watatokeza kama washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kuhifadhiwa kwa kukesha na kuomba tu. (Messages to Young People, 80) [Pr 28.1; Maombi Aya ya 78]

Ushindi Unahitaji Maombi ya Dhati – Ushindi haupatikani bila maombi mengi ya bidii, bila kujishusha nafsi kwa kujinyenyekeza katika kila hatua. Nia au mapenzi yetu hayatakiwi kulazimishwa kushirikiana na wakala wa MUNGU/Mbingu, lakini ni lazima yatolewe kwa Bwana kwa hiari yetu wenyewe.-(Thoughts from the Mount of Blessing, 142) [Pr 28.2; Maombi Aya ya 79]

Lazima tutenge muda wa Kuomba – Tunapaswa sasa kujifunza na kujizoeza katika kumfahamu MUNGU kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika wanatunza kumbukumbu ya kila sala ambayo ni ya dhati, yenye usadikisho na yenye unyofu (Malaika wanarekodi kila ombi). Ni bora kujitenga au kutupilia mbali tamaa zetu zenye ubinafsi kuliko kupuuzia ushirika na MUNGU. Umasikini wa kilindi kirefu, kujikana nafsi kwa hali ya juu, vikiwa na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, maisha rahisi, na urafiki bila kibali Chake. Ni Lazima tuchukue muda na kuutenga kwa kwaajili ya sala - (The Great Controversy, 622) [Pr 28.3; Maombi Aya ya 80]

We Must Take Time to Pray—We should now acquaint ourselves

Tumia muda mwingi katika Maombi – Hebu muda mwingi utumike katika maombi na kutafuta kwa ukaribu Neno. Hebu wote wapate Ukweli halisi wa imani katika mioyo yao kwa kuamini kwamba Roho Mtakatifu atamwagwa kwao kwa sababu wana njaa halisi na kiu ya haki.....Hebu kuwe na maombi zaidi, kuamini, na kupokea, na kufanya kazi zaidi pamoja na MUNGU. —(Testimonies for the Church 6:65, 66) [Pr 28.4; Maombi Aya ya 81]

Omba kuliko ulivyowahi kuomba maishani Mwako – Mtazame Yesu kwa usahili na imani. Mkodolee macho Yesu mpaka roho izimie chini ya nuru iliyosheheni. Hatusali hata nusu ya tunavyopaswa kusali. Hatuamini hata nusu ya tunavyopaswa kuamini, tunaambiwa. "Ombeni, nanyi mtapewa." Luka 11:9 Ombeni, aminini, na imarishaneni. Ombeni kuliko mlivyowahi kuomba maishani mwenu, kwamba Bwana atawawekea mkono Wake, ili muweze kufahamu marefu na mapana na kina na kimo, na kujua upendo wa Kristo, upitao ujuzi wote, ili mjazwe utimilifu wote wa MUNGU. —(Testimonies for the Church 7:214) [Pr 28.5; Maombi Aya ya 82]

Omba, ndiyo, omba kuliko ulivyowahi kuomba maishani mwako, ili usidanganywe na hila za Shetani, ili usipate kuangukia ugonjwa wa kutokuwa na usikivu, uzembe, moyo usiojali, na wenye ubatili, na kisha ujihudhurisha kwenye majukumu na shuguli za kidini kwaajili tu ya kutuliza dhamiri yako mwenyewe. — (Testimonies for the Church 2:144) [Pr 29.1; Maombi Aya ya 83]

Ombeni Daima - "Ombeni daima-ombeni bila kukoma;" hiyo ni kwamba, Daima uwe katika roho ya maombi, na hapo ndipo utakapokuwa tayari kwa Ujio wa Bwana wako. – (Testimonies for the Church 5:235) [Pr 29.2; Maombi Aya ya 84]

Hitaji la Maombi mengi – Sasa kuna hitaji la maombi mengi. Kristo anaamuru, "Ombeni bila kukoma;" yaani, ielekeze akili yako juu kwa MUNGU, Chanzo cha nguvu zote na ufanisi. – (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 510) [Pr 29.3; Maombi Aya ya 85]

Shughuli sio mbadala wa Maombi (Pilikapilika nyingi hazichukui nafasi ya Sala)– kadiri shughuli zinavyoongezeka na watu kufanikiwa katika kufanya kazi yoyote kwa MUNGU, kuna hatari ya kutegemea mikakati na njia za kianadamu. Kuna tabia ya kuomba kwa udogo na kuwa na imani kidogo. Kama wanafunzi, tuko katika hatari ya kupoteza machoni mwetu utegemezi wetu kwa MUNGU wetu, na kutamani kufanya shughuli zetu kuwa ndiyo mkombozi. Tunahitaji kumtazama Yesu daima, huku tukitambua kuwa ni nguvu Yake ndiyo ambayo hutenda kazi. Wakati tukiendelea kufanya kazi kwa dhati na bidii kwa ajili ya wokovu wa wapotevu, lazima pia tutenge wakati wa kutafakari, kwa maombi, na kujifunza Neno la MUNGU. Ni ile kazi pekee iliyotekelezwa kwa maombi mengi, na kutakaswa kwa uwezo, stahiki na sifa ya Kristo ndiyo mwishowe itathibitisha kuwa imefaulu kwa ufanisi kwa mema. - (The Desire of Ages, 362) [Pr 29.4; Maombi Aya ya 86]

Maombi yanahitajika ili kuchukua misimamo isiyopendwa au isiyo maarufu -Inahitaji ujasiri wa kiadili, uthabiti, kuazimia, uvumilivu, na maombi mengi kukaa katika upande ule tofauti usio mashuhuri au usiopendwa na wengi. Tunashukuru kwamba tunaweza kuja kwa Kristo kama wale watu maskini waliokuwa wanateseka, walivyomjia Kristo hekaluni.- (Evangelism, 240). [Pr 29.5; Maombi Aya ya 87]

Maombi yanahitajika ili Kufanya Kazi ya MUNGU- Maombi mengi na mazoezi ya nguvu ya akili ni muhimu

ikiwa tungependa tuwe na utayari wa kuifanya kazi ambayo MUNGU atatukabidhi na atatuamini tuifanye. Wengi hawafikii nafasi ambayo wanaweza kuimiliki, kwa sababu wanangojea MUNGU awafanyie yale ambayo Yeye amewapa uwezo wa kuyafanya wao wenyewe. Wote ambao wamechaguliwa kufaa kwa utumishi katika maisha haya lazima wafundishwe kwa nidhamu kali ya kiakili na kimaadili, na kisha MUNGU atawasaidia kwa kuchanganya nguvu Zake za Kiungu/Uungu na juhudi za kianadamu. - (Testimonies for the Church 4: 611) [Pr 30.1; Maombi Aya ya 88]

Maombi Yanahitajika ili Kuielewa ile Kweli -Mada za ukombozi ni mada muhimu na nzito mno leo na siku za usoni, na ni wale tu ambao wana nia ya kiroho, ndiyo wanaweza kutambua kina na umuhimu wake. Ni usalama kwetu, maisha yetu, na furaha yetu, kuishi ndani ya zile Kweli za mpango wa wokovu. Imani na maombi ni muhimu ili tuweze kuyaona mambo ya kina ya MUNGU. Fikra zetu zimefungwa sana na maoni finyu na hafifu, kiasi kwamba tunapata maoni na mitazamo michache tu ya uzoefu ambao ni upendeleo wetu kuwa nayo. Sisi tunaelewa kwa udogo kiasi gani, lile ombi la mtume, aliposema, "kwamba atawapatia, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, Muimarishwe kwa nguvu na roho Yake katika utu wa ndani; ili Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani; ili ninyi, mkiwa na shina, na msingi wa upendo, mpate kuweza kujua pamoja na watakatifu wote jinsi ya mapana, na marefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo wa Kristo, upitao ujuzi, ili mjazwe utimilifu wote wa Mungu. Sasa Kwake Yeye awezaye kufanya mengi kupita yote tunayoomba au kufikiria, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu, utukufu umrudie Yeye kanisani kupitia Kristo Yesu katika vizazi vyote, milele na milele. Amina (na amina, ombi zito sana kupita yote!). The Review and Herald, Novemba 17, 1891) [Pr 30.2; Maombi Aya ya 89]

Maombi Yanahitajika Nyumbani — Mapenzi hayawezi kudumu, hata katika mzunguko wa nyumbani, isipokuwa kuna upatanifu na mwelekeo kwa mapenzi ya MUNGU. Vitivo na shauku zote vinapaswa kuletwa katika upatanifu na sifa za Yesu Kristo. Ikiwa baba na mama katika upendo na hofu ya MUNGU wataungana katika maslahi/shauku na kuwa na mamlaka nyumbani, wataona umuhimu wa

maombi mengi, na kutafakari kwa umakinizaidi. Na wanapomtafuta MUNGU, macho yao yatafunguliwa kuona wajumbe wa mbinguni waliopo kuwalinda kama jibu la maombi ya imani. Watashinda udhaifu wa tabia zao na kutembea kuelekea kwenye ukamilifu. - (The Adventist Home, 315, 316) [Pr 30.3; Maombi Aya ya 90]

Maombi yanahitajika kudumisha uhusiano/muunganiko na MUNGU— Puuza mazoezi ya maombi, au jihusishe na maombi kwa muda mfupi hapa na pale, kwa kushtukiza, na bila mtiririko wa daima, ukitenda kile kinachokuwa rahisi kwako au jinsi unavyopenda, basi utapoteza uhusiano wako na MUNGU. Maisha Kikristo hugeuka kuwa makavu, na nguvu za kiroho zitakuwa hazina makali. kisha Uzoefu wa kidini unakosa afya na nguvu. - (The Signs of the Times, July 31, 1893) [Pr 31.1; Maombi Aya ya]

Maombi yanahitajika ili kupata Nguvu za Kiroho — Sababu ambayo wengine hawana utulivu, ni kwamba hawaendi kwa Yeye ambaye Ndiye Chanzo pekee cha Kweli cha furaha. Kila mara wanajaribu kutafuta kujifurahisha mbali na ile furaha inayopatikana ndani ya Kristo Yake pekee. Ndani Yake Yeye hakuna matumaini yaliyokatishwa tamaa kamwe. Oh! Ni kwa jinsi gani fursa ya thamani ya maombi imepuuziwa! Usomaji wa Neno la MUNGU huandaa akili kwa ajili ya maombi. Moja kati ya sababu kubwa ya kwa nini wengi wana mkao wa kujitoa kwa udogo katika kumkaribia MUNGU kwa njia ya maombi ni, kwamba wamejitenga wenyewe na kazi hii takatifu kwa kusoma hekaya zinazowavutia, ambazo zimeyasisimua mawazo na kuamsha tamaa mbaya. Neno la Mungu linakuwa lenye ladha isiyopendeza (mionjo yao imebadilika kwa habari wanazokula machapishoni au mtandaoni); saa ya maombi haiwekwi mawazoni. Maombi ni nguvu ya Mkristo. Wakati muumini yuko mwenyewe, yeye hayupo peke yake; anahisi uwepo wa Yule aliyenena, "Tazama, Mimi Niko pamoja nawe siku zote."The Review and Herald, Machi 11, 1880) [Pr 31.1; Maombi Aya ya 91]

Maombi Yanahitajika ili Kuingia Mbinguni — Hakuna kitu kama kuingia kwetu kwenye malango ya mbinguni kupitia kujifurahisha, kujiendekeza na upumbavu, maburudisho, ubinafsi, bali tu ni kwa kukesha na kuomba

bila kukoma. Kukesha kiroho kwa kila mmoja wetu ndiyo gharama/bei ya usalama. Usiegeme upande wa Shetani hata sentimita moja, asije akapata manufaa kwako na kukuteka. - (SDA Bible Commentary 6: 1094) [Pr 31.2; Maombi Aya ya 92]

Maombi hutufanya kudumu kuwa Waaminifu – Bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuongeza uzembe, kutojali na kupotoka mbali na njia sahihi. Adui daima anatafuta kuzuia au kufunga njia ya kukifikia Kiti cha Rehema, ili kwa sala ya dhati na imani tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu. - (The Review and Herald, Desemba 8, 1904) [Pr 31.3; Maombi Aya ya 93]

Omba kwa ajili ya roho- Ikiwa tunataka kujifunza juu ya Kristo, lazima tuombe kama vile ambavyo mitume waliomba Roho Mtakatifu alipomwagwa juu yao. Tunahitaji ubatizo wa Roho wa MUNGU. Hatuko salama hata kwa saa moja tunaposhindwa kutoa utii kwa Neno la MUNGU.– (Fundamentals of Christian Education, 537) [Pr 32.1; Maombi Aya ya 94]

Udhaifu hugeuzwa na kuwa Nguvu Kupitia Maombi – Wao [watu wengi wa MUNGU] hawaoni umuhimu wa kuijua mioyo yao na pia kuzitawala nafsi zao wenyewe. Hawakeshi na kuomba, ili wasije wakaingia majaribuni. Ikiwa wangekesha, wangepeweza wangepielimisha kuzitambua pointi/vipengele vyao dhaifu, ambavyo vina uwezekano mkubwa kuwaingiza hatarini, na kuwashambulia kwa majaribu. Kwa kukesha na kuomba, vipengele/maeneo yao dhaifu yanaweza kulindwa vyema na hata mwishowe yakawa vipengele vyao vyenye kuwafanya wawe imara/nguvu, na wanaweza kukabiliana na majaribu bila kushindwa. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kujichunguza mwenyewe kila siku, ili aweze kuujua kwa ukamilifu mwenendo wake mwenyewe.– (Testimonies for the Church 2:511) [Pr 32.2; Maombi Aya ya 95]

Omba katika Hali Zote – Katika biashara yako, katika nyakati za kuburudika kwa pamoja na wengine, na katika muingiliano wa maisha, acha kila mahusiano unayoingia, yawe katika maombi ya dhati, na ya unyenyekevu. Kwa njia hiyo utaonyesha kwamba unamheshimu MUNGU, na

MUNGU atakuheshimu na kukutunukia. Omba moyo unapokuwa dhaifu na kuzimia. Unapokata tamaa, funga mdomo wako kwa wanadamu (Usinyanyue mdomo wako kuwaelezea watu shida zako); usifuate njia ya wengine na kuwa kivuli chao; bali mwambie Yesu kila kitu. Nyosha mikono yako juu na kuomba msaada. Katika udhaifu wako shikilia nguvu isiyo na kikomo. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani, ili uweze kuona mwanga katika nuru ya MUNGU na ufurahie upendo Wake.- (The Ministry of Healing, 513) [Pr 32.1; Maombi Aya ya 96]

SURA YA 3

MUNGU HUSIKIA MAOMBI

MUNGU husikia Maombi ya Wanyenyekavu – Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ujazo/ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio na ukomo. Inashangaza kwa kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! MUNGU Yuko tayari kusikia maombi ya dhati na imani ya watoto Wake wanyenyekavu, na bado kuna kusitasita kwingi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU yale tunayoyataka. Malaika wa mbinguni wanafikiria nini juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo unawainamia kwa matamania, akiwa tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiri, ila bado wao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana? Malaika wanapenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanauchukulia ushirika wao na MUNGU kuwa ndiyo furaha yao kubwa kupita furaha zote; ila wanadamu, ambao wanahitaji msaada mkubwa ambao ni MUNGU tu anayeweza kuutoa, wanaonekana kuridhika kutembea bila nuru ya Roho Wake, ushirika wa uwepo Wake. –(Steps to Christ, 94) [Pr 33.1; Maombi Aya ya 1]

Wale ambao wana unyenyekevu, wamtegemeao Mungu, na kuwa na moyo uliopondeka, Mungu huwakubali, na husikia maombi yao; na MUNGU anaposaidia, vikwazo vyote vitaondolewa. Ni watu wangapi wenye uwezo mkubwa wa vipaji vya asili, akili nyingi, na elimu ya hali ya juu wameshindwa walipowekwa katika nafasi za uwajibikaji, wakati wale wenye akili dhaifu, na mazingira duni, wamefanikiwa sana. Siri ilikuwa: Wale wa kwanza wenye vipaji na visomo, walijiamini wao wenyewe, wakati wale dhaifu na duni waliungana na Yeye ambaye ni Mshauri wa ajabu na hodari katika kufanya kazi ili kutimiza mapenzi Yake. –(Testimonies for the Church 4:538, 539) [Pr 33.2; Maombi Aya ya 2]

MUNGU husikia na Kujibu Maombi – MUNGU husikia maombi. Kristo amesema “Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, Nitafanya.” Tena anasema, “Mtu yeyote

Akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu." Yohana 14:14; Yohana 12:26. Ikiwa tunaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani aliyoitoa itatimizwa kwetu. Hatustahili rehema Yake, lakini tunapojitoa Kwake, Yeye hutupokea. Yeye atafanya kazi kwa ajili, na kupitia wale wanaomfuata. - (The Ministry of Healing, 226, 227) [Pr 34.1; Maombi Aya ya 3]

Hakika Bwana atasikia na kujibu maombi ya watendakazi Wake ikiwa watamtafuta kwa ajili ya ushauri na mafundisho. - (Evangelism, 399) [Pr 34.2; Maombi Aya ya 4]

MUNGU husikia maombi ya wote wanaomtafuta katika Kweli. Yeye Ana nguvu ambayo sisi sote tunahitaji. Yeye Anajaza moyo kwa upendo, na furaha, na amani, na utakatifu. –(Testimonies for the Church 9:169) [Pr 34.3; Maombi Aya ya 5]

Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwaminifu litasikiwa na MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji zaidi, na mara nyingi majibu atakayopata yatazidi matarajio yake. Hakuna ombi la mtakatifu wa kweli linalopotea ikiwa limetumwa kwa imani kutoka katika moyo mkweli/mnyofu. –(Testimonies for the Church 1:121) [Pr 34.4; Maombi Aya ya 6]

MUNGU husikiliza Kila ombi – MUNGU aliye wa milele, alisema Yesu, hufanya iwe fursa yako kumwendea Yeye kwa Jina la Baba. Hebu elewa kila kinachomaanishwa hapa. Hakuna mzazi yoyote wa duniani aliyewahi kumsihi sana mtoto aliyekosea kama Yeye Aliyekuumba anavyomsihi mkosaji. Hakuna nia ya ya upendo wa kibinadamu iliyowahi kumfuata yule asiyetaka toba kwa miito ya upole kiasi hicho. MUNGU hufanya makazi Yake katika kila makazi; Yeye husikia kila neno linalosemwa, husikiliza kila ombi linalotolewa, anaonja huzuni na kukatishwa tamaa kwa kila mwanadamu, Anazingatia jinsi baba, mama, dada, rafiki, na jirani wanavyotendewa. Yeye hujali mahitaji yetu, na upendo Wake na rehema na neema Zake zinaendelea kububujika ili kukidhi hitaji letu.- (The Signs of the Times, Oktoba 28, 1903) [Pr 34.5; Maombi Aya ya 7]

MUNGU husikia kila Maombi ya Dhati – Biblia inatuonyesha MUNGU katika mahali Pake pa juu na

Patakatifu, sio katika hali ya kutokuwa na shughuli, sio kwa ukimya na upweke, ila akiwa amezungukwa na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya viumbe watakatifu na wenye akili (malaika), wote wakingojea kufanya mapenzi Yake. Kupitia mikondo ambayo hatuwezi kutambua Yeye Yuko katika mawasiliano hai na kila sehemu ya himaya Yake. Lakini ni katika sehemu hii ndogo sana kama punje tu ukilinganisha na himaya Yake, yaani dunia yetu, ndipo zipo roho ambazo Yeye, alimtoa Mwanawe wa pekee ili kuziokoa, ambapo shauku Yake na masilahi ya mbinguni yote yamejikita hapo. MUNGU anainama kutoka kwenye kiti Chake cha enzi kusikia kilio cha wanaoonewa. Kwa kila ombi la dhati na imani, Yeye Anajibu, "Mimi hapa." Yeye huwainua waliofadhaika na waliodhulumiwa kwa kukanyagwa-kanyagwa. Katika taabu zetu zote Yeye pia anataabika. Katika kila jaribu na kila mtihani malaika wa uwepo Wake yuko karibu kuokoa. - (The Desire of Ages, 356) [Pr 35.1; Maombi Aya ya 8]

Yaonekana kana kwamba wanafunzi walikuwa bado kujua rasilimali na nguvu za Mwokozi zisizo na kikomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Angelikuwepo mbele za Baba kuomba kwa niaba yao. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu Yeye huyawasilisha kama matamania Yake mwenyewe kwa niaba ya mtu huyo (roho hiyo). Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, Naye ataliwasilisha kwa Baba bila neno hata moja la kuudhi, lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. [Pr 35.2; Maombi Aya ya 9]

Njia ya uaminifu na uadilifu sio kwamba inakosa kizuizi, ila katika kila shida tunapaswa kuona wito wa kuomba. Hakuna mtu aliye hai ambaye ana nguvu yoyote ambayo hajaipokea kutoka kwa MUNGU, na chanzo kinachotoka nguvu hizo kiko wazi hata kwa mwanadamu dhaifu zaidi. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, nitalifanya." [Pr 35.3; Maombi Aya ya 10]

Kristo aliwaagiza wanafunzi Wake waombe "Kwa Jina Langu,". Katika Jina la Kristo wafuasi Wake wanapaswa kusimama mbele za MUNGU. Kupitia thamani ya kafara iliyotolewa kwa ajili yao, wana thamani machoni pa Bwana. Kwa sababu ya kupewa haki kupitia Kristo, wanahesabiwa kuwa wa thamani. Kwa ajili ya Kristo Bwana huwasamehe wale wamchao. Haoni uovu wa kutisha ndani ya wenye dhambi hao. Anatambua mfano wa Mwanawe ndani yao, ambaye wanamuamini. - (The Desire of Ages, 667) [Pr 36.1; Maombi Aya ya 11]

Hakuna Ombi la dhati na bidii ambalo linalopotea – mjulishe maombi yako Muumba wako. Hakuna aliyewahi kumwendea kwa moyo uliopondeka na akafukuzwa. Hakuna ombi hata moja la dhati na imani lilipotea. Katikati ya nyimbo za kwaya ya mbinguni, MUNGU husikia kilio cha mwanadamu dhaifu. Tunamwaga matamaniao ya mioyo yetu ndani ya vyumba vyetu vya siri, tunapumua maombi tunapotembea njiani, na maneno yetu yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu/malimwengu. Sauti zetu zinaweza zisisikike kwenye sikio lolote la mwanadamu, lakini haziwezi kufa kimyakimya tu, wala haziwezi kupotea kupitia shughuli na kelele zinazoendelea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha matamaniao ya moyo. Haya huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya machafuko ya kadarnasi za watu, na kwenda hadi nyua za mbinguni. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunaongea Naye, na maombi yetu yanasikika. Wewe ambaye unajiona hustahili kabisa, usiogope kabisa kuikabidhi kesi yako inayokukabili kwa MUNGU. - (In Heavenly Places, 82) [Pr 36.2; Maombi Aya ya 12]

MUNGU husikia Maombezi ya Yesu Yaliyochanganyika na Maombi Yetu – Kristo ameahidi Mwenyewe kuwa mbadala na mdhamini wetu, na hampuuzii au kumuacha mtu yeyote. Kuna fungu/mfuko usiopungukiwa wa utii kamili unaotokana na utii Wake nao unatitirika daima. Kule mbinguni sifa Zake, kujikana Kwake Mwenyewe na kujitoa mhanga Mwenyewe, kunathaminiwa kama uvumba unaopaswa kutolewa pamoja na maombi ya watu Wake. Wakati maombi ya dhati na usadikisho, na ya unyenyekevu ya mwenye dhambi yanapopanda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, Kristo anachanganya maombi hayo na sifa za maisha Yake Mwenyewe za utii mkamilifu. Maombi yetu

yafanywa kuwa na harufu nzuri na uvumba huu. Kristo ameahidi kufanya maombezi kwa niaba yetu, na siku zote Baba humsikia Mwanawe.—(Sons and Daughters of God, 22) [Pr 36.3; Maombi Aya ya 13]

MUNGU daima hujibu, ingawa wakati mwingine twaweza tusitambue- Ikiwa tunamwendea MUNGU, tukijisikia kwamba tu wanyonge, tusio na uwezo na tegemezi, kama tulivyo, na kwa imani ya unyenyekevu tukitumaini tunawasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana mwisho, anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anatawala kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Yeye anaweza na atashughulikia kilio chetu, na ataangaza nuru mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati na imani, tunaletwa katika muunganiko wa akili ya Yule Asiyeye wa milele. Labda hatuwezi kuwa na ushahidi unaoonekana na wa kustaajabisha wakati huo ambao uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini huo ndio Ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake unaoonekana, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo na huruma ya upole.- (Steps to Christ, 97) [Pr 37.1; Maombi Aya ya 14]

Majibu ya MUNGU siku zote sio yale tunayotarajia— Omba basi; Omba, nawe utapata. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile tunavyotamani, au kwa wakati tunalitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao litakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa kwa upweke, kwa uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kila wakati kwa faida yako (kwa wema kwako). — (Messages to Young People, 250) [Pr 37.2; Maombi Aya ya 15]

MUNGU husikia Maombi kwa ajili ya kuongoa Roho — Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujikana nafsi yaliyoamriwa katika Neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongolewa kwa roho. Watu wa MUNGU wataacha nuru yao iangaze, na wale wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni. - (Counsels on Stewardship, 302) [Pr 37.3; Maombi Aya ya 16]

Amini kwamba MUNGU husikia maombi yako-Watu wa MUNGU lazima wasonge kwa uelewa. Hawapaswi kuridhika mpaka kila dhambi inayojulikana imetubiwa; kisha ni haki na wajibu wao kuamini kwamba Yesu anawakubali. Hawapaswi kungojea mpaka wengine wapige gwaride kusonga mbele ili kuliacha giza na kupata ushindi kwaajili yao kufurahia. Furaha kama hiyo itadumu hadi mkutano utakapofungwa tu. Lakini MUNGU lazima atumikiwe kutoka kwa kanuni badala ya hisia. Asubuhi na usiku jipatieni ushindi kwaajili yenu wenyewe katika familia yenu. Usiruhusu kazi yako ya kila siku ikuzuie katika hili. Chukua muda kuomba na unapoomba, amini Mungu anasikia maombi yako. Ruhusu imani yako ichanganyike na maombi yako. Unaweza usihisi jibu la haraka wakati wote; lakini basi ni kwamba imani hiyo inakuwa inajaribiwa. Unathibitishwa kuona ikiwa utamtegemea MUNGU, ikiwa una imani hai, na inayodumu. “Yeye analiyewaita ninyi atafanya hivyo kwani ni mwaminifu.” Tembea kwenye boriti nyembamba ya imani. Yaache yote juu ya ahadi za Bwana. Mtumaini MUNGU gizani. Huo ni wakati wa wewe kuwa na imani. Lakini mara nyingi mnaruhusu hisia zikutawale. Mnaangalia kustahili ndani yenu wenyewe wakati hamuhisi kufarajiwa na Roho wa MUNGU, na mnakata tamaa kwa sababu hamuwezi kupata. Hamumtumaini Yesu vya kutosha, Yesu wa thamani. Hamfanyi sifa na stahiki Zake kuwa yote, katika yote. Hata mkifanya kwa ubora mnavyoweza kufanya haitaweza kustahili fadhili za MUNGU. Ni kustahili kwa Yesu ndiyo kutawaokoa, damu Yake ndiyo itakayowatakaswa. Lakini mnayo juhudi ya kufanya. Lazima ufanye kile unachoweza kwa upande wako. Uwe na bidii na kutubu, kisha mwamini.

- (Ushuhuda kwa Kanisa 1: 167) [Pr 38.1; Maombi Aya ya 17]

SURA YA 4

MAOMBI NA KULETA ROHO KWA BWANA

Maombi ni Sehemu Muhimu ya Mafanikio katika kuongoa Roho-Ikiwa washiriki wa makanisa wangezifanyia kazi nguvu za akili walizo nazo, kwa juhudi zinazoelekezwa vizuri, katika mipango iliyokomaa vizuri, basi wangeweza kumfanyia Kristo mara mia zaidi ya wanavyofanya sasa. Endapo wangesonga mbele kwa maombi ya dhati, kwa upole na unyenyekevu wa moyo, huku wao binafsi wakitafuta kuwapa wengine ujuzi wa wokovu, ujumbe huo unaweza kuwafikia wakazi wa dunia. - (The Review and Herald, Aprili 11, 1893). [Pr 39.1; Maombi Aya ya 1]

Tunapaswa kuja kwa MUNGU kwa imani, na kumimina dua zetu mbele Yake, tukiamini kwamba atafanya kazi kwa niaba yetu, na kwa niaba ya wale ambao tunatafuta kuwaokoa. Tunapaswa kutumia wakati mwingi kusali kwa bidii.— (SDA Bible Commentary 3: 146, 1147) [Pr 39.2; Maombi Aya ya 2]

Chagua roho nyingine na nyingine tena na kisha kila siku tafuta mwongozo kutoka kwa MUNGU, ukiweka kila kitu mbele Zake kwa maombi ya dhati na bidii, na ufanye kazi kwa hekima ya Bwana. Unapofanya hivi, utaona kwamba MUNGU atampa Roho Mtakatifu kusadikisha, na nguvu ya Ukweli kuiongoa roho. - (Medical Ministry, 245). [Pr 39.3; Maombi Aya ya 3]

Kumbuka kwamba kufaulu kwa karipio kunategemea kwa ukubwa roho ambayo kupitia kwayo onyo linatolewa. Usipuuze maombi ya dhati ili uwe na roho ya kujishusha, inayonyenyekea, na kwamba malaika wa MUNGU waende

mbele yako na kufanya kazi juu ya mioyo unayojaribu kuifikia, na hivyo wailainishe kwa hisia za mbinguni ili juhudi zako zipate kuwa zenye faida. –(Testimonies for the Church 2:53) [Pr 40.1; Maombi Aya ya 4]

Ikiwa watu kadhaa wangekutana pamoja kwa nia moja, na mioyo iliyolemewa na mzigo kwa ajili ya roho zinazoangamia, na watoe maombi ya dhati, ya bidii, hakika matokeo yangekua mazuri. - (The Review and Herald, Agosti 23, 1892) [Pr 40.2; Maombi Aya ya 5]

Kuziombea roho Kutatuleta Karibu na MUNGU— Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho za watu katika maombi yetu, mioyo yetu itadunda na ushawishi wenye nguvu wa kuhuishwa wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu wenyewe yatang'aa kwa unyofu na bidii zaidi ya Kiungu; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa yenye uhalisia zaidi, dhati, na yenye bidii zaidi, na ya maombi zaidi. - (Christ Object Lessons, 354). [Pr 40.3; Maombi Aya ya 6]

Pale ubinafsi unapokufa, kutakuwa na mwamko mkubwa wa matamano ya kina kuhusiana na wokovu wa wengine, - hamu ambayo itasababisha kufanyika kwa juhudi za kudumu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na sala ya dhati na yenye msukumo na mkazo (king'ang'anizi!), na maombi ya kujitolea, yataingia mbinguni kwa niaba ya roho zinazoangamia. - (Gospel Workers, 470). [Pr 40.4; Maombi Aya ya 7]

Mkutane pamoja kuombea uongoaji wa roho— Ikiwa katika sehemu moja wapo wawili tu au watatu tu ambao wanaujua Ukweli, basi na wajifanyie kikundi cha watenda kazi. Hebu watunze mshikamano/dhamana ya muungano wao usivunjike, wakivuta nyavu pamoja kwa upendo na umoja, wakitiana moyo kusonga mbele, kila mmoja akijipatia ujasiri na nguvu kutoka kwenye msaada wa wengine..... Wanapoendelea kufanya kazi na kuomba kwa Jina la Kristo, idadi yao itaongezeka. –(Testimonies for the Church 7:21) [Pr 40.5; Maombi Aya ya 8]

Hebu kanisa la Los Angeles, California liwe na msimu maalum wa maombi kila siku kwa kazi ambayo inafanywa. Baraka ya Bwana itakuja kwa washiriki wa kanisa ambalo linashiriki katika kazi hiyo, wakikusanyika katika vikundi vidogo kila siku kuombea mafanikio yake. Na hivyo

waumini watapata neema, na kazi ya Bwana itasonga mbele.—(Evangelism, 111, 112) [Pr 40.6; Maombi Aya ya 9]

Tunapaswa kufanya makongamano ya maombi, tukimwomba Bwana afungue njia ili Ukweli upate kuingia katika ngome ambazo Shetani ameweka kiti chake cha enzi, na kuondoa kunuiza kwake au kivuli alichotupa katika njia ya wale ambao anatafuta kuwadanganya na kuwaangamiza. —(Testimonies for the Church 6:80) [Pr 41.1; Maombi Aya ya 10]

Oh, kwamba sala ya dhati ya imani ipande kwenda juu kutokea kila mahali, Nipe roho zilizozikwa sasa kwenye takataka za makosa, la sivyo nife! Walete kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. —(This Day With God, 171). [Pr 41.2; Maombi Aya ya 11]

Kila mtu Anaweza Kuziombea roho — Sio wote walioitwa kufanya kazi binafsi katika maeneo ya nchi za kigeni, lakini wote wanaweza kufanya kitu kwa maombi yao na zawadi zao kusaidia kazi ya umishenari. — (Testimonies for the Church 6:29) [Pr 41.3; Maombi Aya ya 12]

Kaka na dada, mmesahau kwamba sala zenu zinapaswa kutoka na kwenda nje, kama mundu kali, pamoja na watendakazi katika shamba kubwa la mavuno? — (Testimonies for the Church 3:162) [Pr 41.4; Maombi Aya ya 13]

Hebu wale walio wa kiroho wazungumze na roho hizi. Omba pamoja nao na kwa ajili yao. Hebu muda mwingi utumike katika maombi na uchunguzaji wa karibu wa Neno kwa karibu. Hebu wote wapate Ukweli halisi wa imani katika nafsi zao kwa kuamini kwamba Roho Mtakatifu ataingia kwao kwa sababu wana njaa halisi na kiu ya haki. —(Testimonies for the Church 6:65) [Pr 41.5; Maombi Aya ya 14]

Wakati nyavu ya injili inatupwa majini, hebu kuwe na kukesha karibu na nyavu, kwa machozi na maombi ya bidii. Hebu watendakazi wadhamirie kutovunjika moyo; na wasiiachilie nyavu hadi itakapotolewa pwani, na matunda ya kazi yao. - (The Signs of the Times, Machi 16, 1882) [Pr 41.6; Maombi Aya ya 15]

Je! Tunawezaje kumheshimu MUNGU, Je, tunawezaje kulitetea na kulithibitisha Neno Lake, pasipo kusali sana na kumwomba aonyeshe nguvu Zake kwa niaba ya wale wanaoangamia? - (The Review and Herald, Agosti 23, 1892) [Pr 42.1; Maombi Aya ya 16]

Jitihada za binafsi za kuongoa zafanikishwa kwa Maombi – Niliamua kwamba juhudi zangu hazipaswi kukoma kwa hizi roho pendwa, nilizokuwa na matamano makubwa nazo, mpaka zimejisalimisha kwa MUNGU. Baadhi ya siku, katika nyakati za usiku, nilizitumia katika maombi ya dhati na imani, kwa wale ambao nilikuwa nimewatafuta na kuwaleta pamoja kwa kusudi la kuwafanyia kazi na kuomba pamoja nao..... [Pr 42.2; Maombi Aya ya 17]

Katika kila moja ya mikutano yetu midogo niliendelea kuhimiza na kumwomba kila mmoja mmoja, hadi kila mmoja alipojitoa kwa Yesu, nikikiri neema na sifa za upendo Wake unaosamehe. Kila mtu aliongolewa kwa MUNGU.—(Testimonies for the Church 1:33, 34) [Pr 42.3; Maombi Aya ya 18]

Kuombea Roho huitoa akili katika wasiwasi wa mambo madogomadogo-Waombe watu watoe sala kwa ajili ya roho za watu unazofanyia kazi; wawasilishe mbele ya kanisa kama mada za dua au maombezi mazito. Litakuwa ni hitaji ambalo ni muhimu kwa kanisa, kuziweka akili zao kutoka kwenye shida zao ndogo na za kipuuzi, ili kuhisi mzigo mkubwa, kuwa na shauku binafsi, juu ya roho ambayo iko tayari kuangamia. - (Medical Ministry, 244, 245) [Pr 42.4; Maombi Aya ya 19]

Ombea Ufanisi Zaidi katika kuongoa roho-Oh! na ionekane ndugu zangu, kwamba Yesu anaishi moyoni, anatia nguvu, anategemeza, anaimarisha, anafariji. Ni fursa yako kupewa ugavi, siku hadi siku kiwango kikubwa cha Roho Wake Mtakatifu, na kuwa na maoni mapana juu ya umuhimu na upeo wa ujumbe tunaotangaza kwa ulimwengu. Bwana Yu tayari kukufunulia mambo ya ajabu na mema kutoka kwenye sheria Yake. Subiri mbele Zake kwa unyenyekevu wa moyo. Omba kwa dhati na bidii sana

ili upate ufahamu wa nyakati tunazoishi, kwa dhana kamili ya kusudi Lake, na kwa kuongezeka kwa ufanisi katika kuokoa roho. –(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 513, 514) [Pr 42.5; Maombi Aya ya 20]

Kuna roho nyingi zinazotamani nuru kupita maelezo, kupata uhakikisho na nguvu zaidi ya vile wanavyoweza kuelewa. Wanahitaji kutafutwa na kufanyiwa kazi kwa uvumilivu, bila kuchoka. Mwombe Bwana katika maombi ya bidii ili kupata msaada. Mwasilishe Yesu kwa watu kwasababu unamjua Yeye kama Mwokozi wako binafsi. Acha upendo Wake unaoyeyusha moyo na laini, neema Yake nyingi, itiririke kutoka kwenye midomo ya wanadamu. Haupaswi kuwasilishe hoja za Mafundisho makuu ya imani isipokuwa umehojiwa au kuulizwa. Lakini chukua Neno, na kwa upendo mwororo na wenye shauku kwa ajili ya roho, waonyeshe haki ya thamani ya Kristo, ambaye Kwake Yeye, wewe na wao lazima muokolewe. - (Evangelism, 442) [Pr 43.1; Maombi Aya ya 21]

Wanafunzi waliomba kwa bidii nzito kwa ajili ya kufaa na utayari wa kuwaendea watu na katika mahusiano yao wa kila siku kuzungumza maneno ambayo yangewaongoza wenye dhambi kwa Kristo. Waliweka pembeni tofauti zao zote, na hamu yote ya ukuu, wakakutana pamoja katika ushirika wa Kikristo. Wakajisogeza karibu na karibu zaidi na MUNGU, na walipofanya hivi walitambua ni upendeleo wa kiasi gani kwao kuruhusiwa kushirikiana kwa karibu na Kristo. Huzuni ilijaza mioyo yao walipofikiria ni mara ngapi walikuwa wamemhuzunisha Yeye kwa uzito wao katika kuelewa, kushindwa kwao kuelewa masomo ambayo, kwa faida yao wenyewe, alikuwa akijaribu kuwafundisha. [Pr 43.2; Maombi Aya ya 22]

Siku hizi za maandalizi zilikuwa siku za uchunguzi wa moyo kwa kina. Wanafunzi walihisi hitaji lao la kiroho na wakalia kwa Bwana kwa ajili ya upako wa Roho mtakatifu, ambaye angewafaa kwa kazi ya kuokoa roho. Hawakuomba baraka kwao wenyewe tu. Walielemewa na mzigo wa kuongoa roho. Walitambua kwamba injili inapaswa kupelekwa ulimwenguni, nao wakadai nguvu ambayo Kristo alikuwa ameahidi. - (The Acts of the Apostles, 37) [Pr 43.3; Maombi Aya ya 23]

Maombi mengi yanahitajika ili kujua jinsi ya kuwafikishia watu Ukweli – Sio kila mtu anayeweza kufanya kazi kwa busara kwa ajili ya ukombozi wa roho. Panahitajika kuwa na kufikiri na tafakari ya kina. Hatupaswi kuingia katika kazi ya Bwana hovyoyvya bila kupanga mikakati na kutarajia mafanikio. Bwana anahitaji watu wenye akili, watu wenye tafakari. Yesu anatoa wito ili kupata watendakazi wenza, na sio waborongaji. MUNGU anataka watu wenye mafikara sahihi na walio na akili kufanya kazi kubwa inayohitajika kwa ajili ya wokovu wa roho. [Pr 43.4; Maombi Aya ya 24]

Fundi mitambo, wanasheria, watu wa stadi mbalimbali, na taaluma zote, hujielimisha wenyewe ili waweze kuwa magwiji waliobobea katika fani zao. Je! Wafuasi wa Kristo wanapaswa kupungukiwa na ufahamu, na akili mahiri na kisha wale wanaodai kuhusika na utumishi Wake ni wajinga (mbumbumbu) katika njia na mbinu zile wanazozitumia? Shughuli ya kupata uzima wa milele iko juu ya kila zingatiao la kidunia. Ili kuongoza roho kwa Yesu lazima kuwe na maarifa ya asili ya mwanadamu na kuisomea akili ya mwanadamu. Tafakari makini sana na maombi ya dhati yanahitajika kujua jinsi ya kuwafikia wanaume na wanawake juu ya mada kuu ya Ukweli. – (Testimonies for the Church 4:67) [Pr 44.1; Maombi Aya ya 25]

Maombi hutenda zaidi Katika kuongoa roho Kuliko Maneno Peke yake— Shetani anakufuatilia kwenye njia yako. Yeye ni mpinzani mjanja, na roho mbaya yenye sumu ambayo unakutana nayo katika kazi yako vimeangaziwa na yeye. Wale ambao yeye huwaweka chini yake wanarudia mwangwi wa maneno yake. Ikiwa pazia lingeweza kuchanwa kutoka kwenye macho yao, wale waliofanya kazi hiyo wangeona Shetani akitumia sanaa yake yote kuwavuta kutoka kwenye Ukweli. Katika kuziokoa roho kutoka katika hila zake, mafanikio yatapatikana zaidi kupitia sala ya unyenyekevu kama ya Kristo kuliko kwa maneno mengi bila maombi. - (Colporteur Ministry, 81) [Pr 44.2; Maombi Aya ya 26]

MUNGU anataka vijana wenye kiasi, wenye kujistahi, wanyenyekevu, watulivu, wenye akili timamu, na wanaume wenye umri wa kukomaa, ambao wana msawaziko wa kanuni (balansi), ambao wanaweza kuomba na kuongea, ambao watainuka mbele ya wazee wenye mvi,

ili kuonyesha heshima kwao, na kuwatendea waliowazidi kwa kuwaheshimu. [Pr 44.3; Maombi Aya ya 27]

Kazi ya MUNGU inateseka kwa ajili ya upungufu wa watenda kazi wenye ufahamu na nguvu ya akili. Ndugu na dada zangu, Bwana amewabariki na uwezo wa vitivo vya kiakili unaoweza kuboresheka zaidi. Kuza talanta zako kwa unyofu na bidii ya kudumu-endelevu. Fanya mazoezi na ifundishe akili kwa kusoma, kwa uchunguzi, kwa kutafakari na kucheua.

Hauwezi kukutana na akili ya MUNGU isipokuwa umetumia kila nguvu. Uwezo wa akili utaimarika na kukuzwa ikiwa utaenda kufanya kazi kwa hofu ya MUNGU, kwa unyenyekevu, na kwa maombi ya dhati na imani. Kusudi thabiti litatimiza maajabu. Muwe wazi, thabiti, Wakristo walioazimia. Mtukuze Yesu, zungumza juu ya upendo Wake, sema juu ya uweza Wake, na hivyo uache nuru yako iangaze kwa ulimwengu. - (Life Sketches, 275) [Pr 44.4; Maombi Aya ya 28]

Ombea Roho -Anza kuombea roho; mkaribie Kristo, karibu na upande Wake unaovuja damu. Hebu roho ya upole na utulivu ipambe maisha yenu, na ombi lenu la bidii na dhati, lililopondeka, na la unyenyekevu lipande Kwake kwaajili ya kupata hekima ili mpate kufaulu kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na roho za wengine. Omba zaidi ya uimbavyo. Je! Wewe huna hitaji kubwa la maombi zaidi kuliko kuimba? Vijana na wanawake, MUNGU anawaiteni mfanye kazi, mumfanyie kazi. Fanya mabadiliko yote katika mwenendo wako. Unaweza kufanya kazi ambayo wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho hawawezi kufanya. Unaweza kulifikia lile tabaka ambalo ambalo wachungaji hawawezi kulifikia.—(Testimonies for the Church 1:513. [Pr 45.1; Maombi Aya ya 29]

Hebu na tuombe kwa bidii pia kwa niaba ya wale ambao tunatarajia kuwatembelea, kwa imani hai kuwaleta, mmoja baada ya mwingine, katika uwepo wa MUNGU. - (Christian Service, 169) [Pr 45.2; Maombi Aya ya 30]

Fanya kazi miongoni mwa watu wa hali ya chini, masikini, na walioonewa. Tunapaswa kuwaombea na kuomba nao wale wanyonge, watu wasiojiweza, wasio na msaada ambao hawana nguvu ya kutawala hamu ya chakula au tamaa ya mwili imeiharibu. Jitihada za dhati na bidii na

za kudumu lazima zifanyike kwa wokovu wa wale ambao mioyo yao imepata uamsho. –(Testimonies for the Church 6:84) [Pr 45.3; Maombi Aya ya 31]

SURA YA 5

AHADI ZA MUNGU KUHUSU MAOMBI

MUNGU Huahidi Kusikia na Kujibu Maombi – Kristo Ndiye kiunganishi kati ya MUNGU na mwanadamu. Yeye Ameahidi maombezi Yake Mwenyewe binafsi kwa kutumia Jina Lake. Anaweka fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo anamuomba mwanadamu kwa kusihi, naye mwanadamu, aanayehitaji msaada wa Mwenyezi Mungu, anajiombea Mwenyewe mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU kuthamini na ukubali wetu wa haki na sifa ya Kristo, manukato hutolewa kwa maombezi yetu. Oh, ni nani anayeweza kuthamini rehema na upendo huu mkubwa! Tunapomkaribia MUNGU

kupitia sifa ya Kristo, tunavikwa mavazi Yake ya kikuhani. Yeye hutuweka karibu Yake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kibinadamu, wakati huo huo kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye anashika kiti cha enzi cha Yeye Asiye na mwisho. Anaweka haki, uzuri na sifa Zake, kama uvumba mtamu, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi yetu. Anaahidi kusikia na kujibu sala zetu. [Pr 46.2; Maombi Aya ya 1]

Maombi rahisi yanayovuviwa na Roho Mtakatifu yatapanda juu kupitia Lango lililofunguliwa, mlango ule ulio wazi ambao Kristo ametangaza: Nimefungua, na hakuna mtu anayeweza kufunga. Maombi haya, yaliyochanganywa na uvumba wa ukamilifu wa Kristo, yatapanda juu kama manukato kwa Baba, na majibu yatakuja. –(Testimonies for the Church 6:467) [Pr 46.2; Maombi Aya ya 2]

Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwadilifu litasikika juu kwa MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji sana, na kwa kawaida majibu yatazidi matarajio yake. Hakuna ombi la mtakatifu wa kweli linalopotea ikiwa limetumwa kwa imani kutoka katika moyo mwadilifu/mkweli.–(Testimonies for the Church 1:121) [Pr 47.1; Maombi Aya ya 3]

Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya uhitaji ni nyenzo ambayo Mkristo anaimiliki na inamuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zitashindikana. Wale wanaofanya kazi zenye kutoa jasho pahali ambapo maisha yana pilikapilika nyingi (busy), waliosongwa na wako karibu kuzidiwa na mifadhaiko, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya mwongozo Wake Bwana. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi kuwasaidia waaminifu Wake, waaminio kila wanapomwita. Katika kila jambo, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na majaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, na usaidizi katika upendo usiomwangusha mtu na nguvu ya MUNGU

anayeshika agano.— (Prophets and Kings, 631, 632) [Pr 47.2; Maombi Aya ya 4]

Tukimwomba, MUNGU atajibu -Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia, kwa kujibu maombi ya imani, yale ambayo hangetoa ikiwa hatukuomba. - (The Great Controversy, 525) [Pr 47.3; Maombi Aya ya 5]

MUNGU husikia maombi. Kristo amesema, Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, Nitafanya.” Tena anasema, "Mtu yeyote Akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu." Yohana 14:14; Yohana 12:26. Ikiwa tutaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani aliyotoa itatimizwa kwetu. Sisi hatustahili rehema Yake, lakini tunapojitua Kwake, Yeye hutupokea. Yeye Atafanya kazi kwaajili yetu na kupitia wale wanaomfuata. - (The Ministry of Healing, 226, 227) [Pr 47.4; Maombi Aya ya 6]

Unapomwomba Bwana akusaidie, Mtukuze, na kumpa heshima Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea baraka Yake. Nguvu zote, hekima yote, ziko chini ya amri/mamlaka yetu. Sisi tuunachopaswa kufanya, ni kuomba tu. - (The Ministry of Healing, 514) [Pr 48.1; Maombi Aya ya 7]

MUNGU ana mbingu iliyojaa mibaraka ambayo Yeye anataka kuwapa wale ambao wanatafuta kwa bidii msaada ule ambao Bwana peke Yake Ndiye anaweza kutoa.—(Sons and Daughters of God, 123) [Pr 48.2; Maombi Aya ya 8]

Yesu Huwasilisha kwa Baba Maombi Yetu Yenye Maneno Mabovu na duni -Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja la kuudhi, na lenye kigugumizi, bali kwa Maneno mazuri na yenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. [Pr 48.3; Maombi Aya ya 9]

Nguvu ya Kushinda majaribu inatolewa kwa Wale Wanaoomba- Wote wanawajibika kwa matendo yao wakiwa katika ulimwengu huu wakati mlango wa rehema haujafungwa bado. Wote wana uwezo wa kudhibiti matendo yao ikiwa watataka. Wakiwa ni dhaifu katika wema na usafi wa mawazo na matendo, wanaweza kupata msaada kutoka kwa Rafiki wa wanyonge. Yesu anauelewa udhaifu wote wa asili ya kibinadamu, na, ikiwa ataombwa,

atatoa nguvu kushinda majaribu yenye nguvu zaidi. Wote wanaweza kupata nguvu hii ikiwa wataitafuta kwa unyenyekevu. - (Child Guidance, 466, 467) [Pr 48.4; Maombi Aya ya 10]

MUNGU Hujibu Maombi Yetu Wakati na Jinsi Anavyoona inafaa - Kila mtakatifu anayekuja kwa MUNGU kwa moyo wa Kweli, na kutuma kwa imani maombi yake yaliyo na unyofu Kwake, atajibiwa maombi yake. Imani yako haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiogope kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za Kweli: "Ombeni, nanyi mtapewa." MUNGU ni Mwenye busara mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaotembea katika unyoofu kitu chochote kizuri. Mtu hufanya makosa, na ingawa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo mnyofu/mkweli, mara zote huwa haombi vitu ambavyo ni vyema kwake, au ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, basi Baba yetu Mwenye busara na mwema husikia maombi yetu, Naye atajibu, wakati fulani hujibu haraka-; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. MUNGU hutupatia baraka; laiti tungeangalia mpango Wake, tungeliona wazi kwamba Yeye Anajua kile kilicho bora kwaajili yetu na kwamba maombi yetu huwa yamejibiwa. Hatupewi chochote cha kutuumiza, bali baraka tunazohitaji hutolewa badala ya kitu ambacho tuliomba ambacho hakitakuwa kizuri kwetu, ambacho kingetuumiza. [Pr 48.5; Maombi Aya ya 11]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu kwa ujasiri, bila kuruhusu mashaka, kwani hayo yatatutenganisha na MUNGU. Imani yetu ikitetereka, hatutapokea chochote kutoka Kwake. Imani na ujasiri wetu kwa MUNGU vinapaswa kuwa imara; na tunapohitaji sana, baraka itatuangukia kama maji ya mvua inaponyesha. – (Testimonies for the Church 1:120, 121) [Pr 49.1; Maombi Aya ya 12]

MUNGU Hutoa Hekima Kwa Kujibu Maombi – Bwana ametupa ahadi hii, “Ikiwa yeyote kati yenu amepungukiwa na hekima, na aombe kwa MUNGU, ambaye huwapa watu wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.” Ni katika utaratibu wa MUNGU kwamba wale wanaobeba

majukumu mara nyingi wanapaswa kukutana pamoja ili kushauriana wao kwa wao, na kuomba kwa bidii hekima hiyo ambayo Yeye peke Yake Ndiye anaweza kutoa. Kwa pamoja mumjulishe MUNGU shida zenu. Zungumzeni kidogo; muda wa thamani unapotea katika mazungumzo ambayo hayana nuru. Ndugu waungane katika kufunga na kuomba kwa ajili ya hekima ambayo MUNGU ameahidi kutoa kwa ukarimu na uhuru mwingi sana. (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 499) [Pr 49.2; Maombi Aya ya 13]

Neema ya Kristo yapatikana hata kabla ya sisi kuiomba - hata kabla ya maombi kutamkwa, ... neema kutoka kwa Kristo inaenda kukutana na neema inayofanya kazi juu ya roho ya mwanadamu.— (Christ's Object Lessons, 206) [Pr 49.3; Maombi Aya ya 14]

Tunaweza Kudai Ahadi Zake Kwa Ujasiri— “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, mtaomba kila mnachotaka, nanyi mtatendewa.” Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni upendeleo kwetu kumwendea Yeye tukiwa na ujasiri mtakatifu. Tukimwomba kwa dhati nuru Yake iangaze juu yetu, Naye Atatusikia na kutujibu. Lakini lazima tuishi kulingana na maombi yetu. Kwani hayana huwa faida yoyote ikiwa tutatembea kinyume nayo. Nimemuona baba ambaye, baada ya kusoma sehemu ya Maandiko kutoa ombi, alipoinuka tu kutoka magotini baada ya sala, mara nyingi alianza kuwagombeza watoto wake. Je! MUNGU angewezaje kujibu ombi hilo aliloomba? Na ikiwa, baada ya kukemea watoto wake, baba atasali, je, sala hiyo itawanufaisha watoto? Hapana; labda ikiwa ni maombi ya kuungama kwa MUNGU. - (Child Guidance, 499) [Pr 50.1; Maombi Aya ya 15]

Malaika Watatusaidia sisi Katika kujibu Maombi — Unapotaka kuzungumza kwa jazba/hasira, funga mdomo wako. Usitamke neno lolote. Omba kabla ya kuzungumza, na malaika wa mbinguni watakuja kukusaidia na watawarudisha nyuma malaika wabaya, ambao wangukuongoza wewe kumvunjia MUNGU heshima, kuiletea aibu au fedheha kazi Yake Mungu, na kudhoofisha roho yako mwenyewe.—(Testimonies for the Church 2:82) [Pr 50.2; Maombi Aya ya 16]

Malaika Watakuwa upande Wetu katika kujibu Maombi
– Uangalizi/ulinzi wa jeshi la mbinguni umetolewa kwa wote ambao watafanya kazi katika njia za MUNGU na kufuata mipango Yake. Tunaweza, kwa maombi ya dhati na bidii, yenye usadikisho, yenye kupondeka moyo na yenye majuto kuwaita wasaidizi wa mbinguni upande wetu. Vikosi vya nuru na nguvu visivyoonekana vitafanya kazi na wanyenyekevu, wapole na wale waliojishusha. [Pr 50.3; Maombi Aya ya 17]

Injili itasonga mbele haraka ikiwa ni matokeo ya maombi – MUNGU angefanya kazi kwa nguvu za kushangaza kwa watu Wake leo ikiwa wangejiweka chini ya uongozi Wake kikamilifu. Wanahitaji kufungamana na Roho Mtakatifu kila wakati. Ikiwa kungekuwa na maombi zaidi katika mabaraza ya wale waliobeba majukumu, unyenyekezaji wa moyo zaidi mbele za MUNGU, tungeliona ushahidi mwingi wa uongozi wa Bwana, na kazi yetu ingelisonga mbele haraka. - (Testimonies for the Church 8: 238) [Pr 50.4; Maombi Aya ya 18]

Maombi Yataleta Uwezo wa Kushinda- Lazima tuwe na silaha zote za MUNGU na tuwe tayari wakati wowote kwa vita dhidi ya nguvu za giza. Wakati majaribu na mitihani vinatukimbilia kwa kasi, twendeni kwa MUNGU na kuteseka/kuhuzunika Naye katika maombi. Hataturudisha na mikono mitupu, lakini atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui. -(Early Writings, 46) [Pr 51.1; Maombi Aya ya 19]

Baraka Zitaendana na Imani Yetu – Omba kwa imani. Na hakikisha unauleta mtindo wako wa maisha upatane na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Hebu imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopatikana zinalingana na imani inayotumika. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Mchukue kwa Neno Lake. "Yeye ni mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati litakalopotea. Mfereji upo wazi; kijito kinatiririka. Kinabeba pamoja nacho sifa za uponyaji, kinamimina umeme wa uzima, afya na wokovu. –(Testimonies for the Church 7:274) [Pr 51.2; Maombi Aya ya 20]

SURA YA 6

MAOMBI YA IMANI

Maombi ni Njia ya Mafanikio ya Mbingu katika Kuishinda Dhambi – Kuna wengi ambao, ingawa wanajitahidi kutii amri za MUNGU, wana amani kidogo au furaha. Upungufu huu katika uzoefu wao ni matokeo ya kushindwa kuizoesha/kuitumia imani yao. Wanatembea kana kwamba wapo katika ardhi yenye chumvi, nyika iliyokauka na udongo wa kupasukapasuka. Wanaomba

kidogo- wanadai ahadi chache, wakati wangeweza kudai mengi; kwani hakuna kikomo kwa ahadi za MUNGU. Hao hawawakilishi kwa usahihi utakaso unaokuja kwa kuitii ile Kweli. Bwana angependa wana na binti Zake wote wawe na furaha, amani, na utiifu. Kupitia kuizoesha imani, yule anayeamini anamiliki baraka hizi. Kupitia kuizoesha imani, kila upungufu wa tabia unaweza kurekebishwa/kujazwa, kila unajisi unaweza kusafishwa, kila kosa kurekebishwa, kila ubora unapata kuendelezwa-kila maboresho yanaweza bora na bora zaidi. [Pr 52.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ni njia ya mbingu, iliyowekwa ili kupata mafanikio katika vita dhidi ya dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo. Ushawishi wa Mwenyezi Mungu ambao unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa msamaha wa dhambi, kwa Roho Mtakatifu, kwa hulka/haiba kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo Yeye ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea." Matendo ya Mitume, 563, 564) [Pr 52.2; Maombi Aya ya 2]

MUNGU hutamani Kutufanyia Mambo Makubwa – Fungu/kazi yetu ni kuomba na kuamini. Kesheni mkiomba. Keshu, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Iweke akilini mwako kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na tenda kwa kupatana na maombi yako. Itafanya tofauti ya milele kwako endapo jaribu litathibitisha imani yako kuwa ni ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfumo fulani tu. [Pr 53.1; Maombi Aya ya 3]

Wakati fadhaa zinatokea, na magumu yanakukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Muachie, mtumaini na kumtegemea MUNGU kwa yote. Kitendo au mazoea ya kuwaambia wengine shida zetu hutufanya tuwe dhaifu tu, na hakileti nguvu yoyote kwao. Kinaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawawezi kuutua. Tunatafuta nguvu kutoka kwa mwanadamu anayekosea, mtu mwenye mwisho/ukomo, anayekufa, wakati tunaweza kuwa na nguvu ya MUNGU asiyekosea, na asiye na ukomo. [Pr 53.2; Maombi Aya ya 4]

Hauna haja ya kujipelekea au kusafiri huku na kule hadi miisho ya dunia ili kupata hekima, kwa maana MUNGU Yuko

karibu nawe. Sio uwezo ulionao sasa au utakaokuwa nao mbeleni, ndio ambao utakupa mafanikio. Ni kile ambacho Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na ujasiri na imani ndogo sana juu ya kile mwanadamu anachoweza kufanya na ujasiri mkubwa zaidi kwa kile MUNGU anachoweza kufanya kwa kila roho inayoamini. Yeye Anatamani mno wewe umuendee kwa imani. Yeye Anatamani sana utarajie kutoka Kwake mambo makubwa mno. Yeye Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kidunia na pia katika mambo ya kiroho. Yeye Anaweza kuzinoa bongo/akili zako na zikawa bora zaidi. Yeye Anaweza kutoa busara na ustadi. Weka talanta zako katika kazi hiyo, mwombe MUNGU akupe hekima, nawe utapewa. - (Christ's Object Lessons, 146) [Pr 53.3; Maombi Aya ya 5]

Maombi na Imani vitafanya Mambo ya Ajabu – Ninaogopa kwamba hakuna imani hiyo ambayo ni muhimu na nyeti kuwa nayo. Je! Hatutavaa njuga dhidi ya kukatishwa tamaa na vishawishi hata tuvunjike moyo? MUNGU ni Mwenye rehema, na tukifurahi katika Kweli, inayotakasa, na inayoboresha maisha, tunaweza kufanya kazi nzuri na thabiti kwa MUNGU. Maombi na imani vitafanya mambo ya kushangaza (mema). Neno lazima liwe silaha yetu ya vita. Miujiza inaweza kufanywa kupitia Neno; kwa kuwa lina faida/manufaa kwa vitu vyote. - (Evangelism, 489) [Pr 53.4; Maombi Aya ya 6]

Imani Kuchanganywa na maombi Yetu -Watu wa MUNGU lazima wasonge kwa uelewa. Hawapaswi kuridhika mpaka watakapotubu kila dhambi inayojulikana; kisha ni haki na wajibu wao kuamini kwamba Yesu anawakubali. Hawapaswi kungojea wengine washinikize kupitia gizani na kupata ushindi ili wafurahie. Furaha kama hiyo itadumu hadi mkutano utakapofungwa tu. Lakini MUNGU lazima atumikiwe kwa kanuni badala ya hisia. Asubuhi na usiku jipatieni ushindi kwako mwenyewe na katika familia yenu. Usiruhusu kazi yako ya kila siku ikuzuie katika hili. Kuwa na muda wa kuomba, na unapoomba, amini kwamba MUNGU anakusikia. Kuwa na imani iliyochanganywa na maombi yako. Unaweza usipate jibu la haraka wakati wote; lakini basi ni kwamba imani hiyo inakuwa inajaribiwa. Unathibitishwa kuona ikiwa utamtegemea MUNGU, ikiwa una imani hai, na inayodumu. “Yeye ni Mwaminifu ambaye awaita, Naye atafanya hivyo (kwani ni Mwaminifu).

Tembea katika njia nyembamba ya imani. Yaache yote juu ya ahadi za Bwana. Mtumaini MUNGU gizani. Huo ndio wakati wa kuwa na imani. Lakini mara nyingi mnaruhusu hisia ziwatawale. Mnatafuta kustahili ndani yenu wakati hamuhisi kufarajiwa na Roho wa MUNGU, na mnakata tamaa kwa sababu hamuwezi kupata. Hamjamtumaini Yesu vya kutosha, Yesu wa thamani. Hamfanyi kustahili Kwake kuwa yote, katika yote, naam yote kabisa. Namna bora zaidi mnayoweza kuifanya kwa uwezo wenu, bado haitazidi fadhili za MUNGU. Ni thamani ya Yesu ndiyo itakayowaokoa, damu Yake ndiyo itakayowatakasa. Lakini mnayo kazi ya kufanya. Lazima mfanye kile mnachoweza kwa upande wenu. Muwe na bidii na kutubu, kisha muamini. [Pr 54.1; Maombi Aya ya 7]

Usichanganye imani na hisia pamoja. Vipo tofauti. Tunapaswa kuwa na imani. Imani hii lazima tuifanyie mazoezi. Amini, amini. Hebu imani yako ishikilie baraka, nazo zitakuwa zako. Hisia zako hazina uhusiano wowote na imani hii. Imani inapoleta baraka moyoni mwako, na unafurahi katika baraka, hiyo sio imani tena, bali ni hisia. – (Testimonies for the Church 1:167) [Pr 54.2; Maombi Aya ya 8]

Sala na Imani Hushikilia Nguvu za Mungu—Imani ya Kweli na sala ya Kweli—zina kubwa nguvu ilioje! Ni kama mikono miwili ambayo mwombaji wa mwanadamu anashikilia nguvu ya Upendo usio na kikomo. Imani ni kumtegemea Mungu,— kuamini kwamba Yeye anatupenda, na anajua ni nini kilicho bora na cha manufaa kwetu. Hivyo, badala ya njia yetu wenyewe, inatuongoza kuchagua njia Yake. Badala ya ujinga wetu, inakubali hekima Yake; badala ya udhaifu wetu, nguvu Zake; badala ya dhambi zetu, haki Yake. Maisha yetu, sisi wenyewe, tayari ni Yake Yeye; imani inakiri umiliki Wake Mungu, na inakubali baraka Zake. Ukweli, unyoofu, usafi, husondwa kidole kwamba ndiyo siri za mafanikio ya maisha. Ni imani ndiyo inatuweka katika kumiliki na kuyashika haya. Kila msukumo wa jambo jema au matamaniao mema ni zawadi ya kutoka kwa Mungu; imani hupokea kutoka kwa Mungu uhai ambao pekee Yake ndiyo unaweza kutokeza ukuaji na ufanisi wa Kweli.—(Gospel Workers, 259) [Pr 54.3; Maombi Aya ya 9]

Maisha yetu Yanapaswa kuendana na Maombi Yetu – Omba kwa imani. Na hakikisha unayapatanisha maisha yako na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopatikana zinalingana/zinatoshana na imani tuliyo nayo. "na iwe kwako kulingana na imani yako. "Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa, kwa sababu amejibu maombi yenu. Muendee kwa Neno Lake. "Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati litakalopotea. Mfereji upo wazi; nao mkondo unatiririka. Unabeba sifa za uponyaji, ukimimina mkondo/umeme wa uhai unaorejesha upya, afya na wokovu. –(Testimonies for the Church 7:274) (Pr 55.1; Maombi Aya ya 10]

MUNGU hukubali Maombi ya Imani - Ombi lililo na unyenyekevu, akili na imani, ambalo hutoka kwenye midomo isiyo feki/udanganyifu, linakubalika kikamilifu kwa MUNGU. Ni maombi ya kina ya moyo, ndiyo ambayo husikika mbinguni na kutuzwa kwa jibu hapa duniani. "Lakini kwa mtu huyu nitamtazama, hata yeye ambaye ni maskini, na mwenye roho iliyopondeka, na anayetetemeka Neno Langu." "Kwa maana asema huyu Mkuu, aliye juu, akaaye milele, Jina Lake ni Mtakatifu; Ninakaa mahali pa juu na Patakatifu, pamoja na yeye ambaye pia ni mwenye roho iliyopondeka na mnyenyekevu, ili kufufua roho ya wanyenyekevu, na kufufua moyo wa wale waliopondeka. "Roho iliyopondeka ni Dhabihu kwa MUNGU; Moyo uliovunjika na uliopondeka, oh! MUNGU, hutaudharau." (The Signs of the Times, December 3, 1896) (Pr 55.2; Maombi Aya ya 11]

Peleka Maombi yako kwa Imani bila kukoma – MUNGU atakuwa kila kitu kwetu kama tunavyohitaji awe. Maombi yetu dhaifu, ya moyo wa nusu nusu hayatatuletea majibu kutoka mbinguni. Lo, tunahitaji kushinikiza ombi letu bila kuchoka! Omba kwa imani, subiri kwa imani, pokea kwa imani, furahiya kwa tumaini, kwani kila mtu atafutaye hupata. Uwe na bidii katika jambo hilo. Mtafute MUNGU kwa moyo wote. Watu huweka moyo mnyofu na bidii katika kila kitu wanachofanya japo ni mambo ya muda mfupi na ya kupita tu, hukazana hadi hadi jasho lao linavalishwa taji ya mafanikio. Kwa bidii kubwa jifunze stadi ya kutafuta

baraka nyingi ambazo MUNGU ameahidi, na kwa uvumilivu, na juhudi zenye bidii utakuwa na nuru Yake na Ukweli Wake na neema Yake nyingi. (Pr 56.1; Maombi Aya ya 12]

Kwa unyofu wa moyo, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Shindana na mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Wekeza mwili na Roho yako yote mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, na amua kuwa wakala Wake mpendwa aliyejiweka wakfu, akiongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na kujazwa na Roho Wake. (Pr 56.2; Maombi Aya ya 13]

Mwambie Yesu matakwa yako kwa unyofu wa roho yako (kwa dhati). Siyo lazima ufanye mabishano au mjadala mrefu Naye, au kumhubiria MUNGU, lakini kwa moyo wa huzuni kwaajili ya dhambi zako, sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi inayousagasaga moyo, utaburudishwa kwa baraka ya amani ya Kristo. –(Our High Calling, 131) (Pr 56.3; Maombi Aya ya 14]

MUNGU hujibu Maombi ya Imani Kwa Uweza – Wakati watu wanajitoa kama Eliya na wana imani aliyokuwa nayo, MUNGU atajifunua kama alivyofanya wakati huo. Watu watakapokuwa wanamsihi Bwana kama vile Yakobo, majibu/matokeo ambayo yalionekana wakati huo yataonekana tena. Nguvu zitatoka kwa MUNGU kujibu maombi ya imani. - (Gospel Workers, 255) (Pr 56.4; Maombi Aya ya 15]

Elewa Sayansi ya Maombi-Maombi na imani ni marafiki walioshikamana kwa karibu sana, na vyote vinahitaji kufunzwa kwa pamoja. Katika ombi la imani kuna sayansi ya Bwana; ni sayansi ambayo kila mtu ambaye anatamani kufanikisha kazi yake ya maisha lazima aelewe. Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Anaweka wazi kwamba ombi letu lazima liwe kulingana na mapenzi ya MUNGU; lazima tuombe vitu ambavyo ameahidi, na chochote tunachopokea lazima kitumike katika kufanya mapenzi Yake. Masharti yakitimizwa, ahadi haizuiliki. [Pr 57.1; Maombi Aya ya 16]

Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya tabia kama ya Kristo, kwa ajili ya hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa ajili ya zawadi yoyote ambayo Ameiahidi, tunaweza kuomba; basi tunapaswa kuamini kwamba tunapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumepokea.—(Education, 257, 258) [Pr 57.2; Maombi Aya ya 17]

Maombi ya siri hudumisha Maisha ya Roho – Hatuna haja ya kutafuta ushahidi wa nje unaoonyesha baraka. Zawadi iko katika ahadi, na tunaweza kuendelea na kazi yetu tukiwa na hakika kwamba kile ambacho MUNGU amekiahidi Ana uwezo wa kukitekeleza, na kwamba zawadi, ambayo tayari tunayo, itadhihirika wakati tunapoihitaji zaidi. (Pr 57.3; Maombi Aya ya 18]

Kuishi kwa Neno la MUNGU kunamaanisha kusalimisha Kwake maisha yote. Kutakuwa na hisia ya kuendelea kuwa na uhitaji na utegemezi, kuuvuta moyo kumfuata MUNGU. Maombi ni lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndiyo unaodumisha maisha ya roho. (Pr 57.4; Maombi Aya ya 19]

Ilikuwa katika mlima pamoja na MUNGU ndiko ambako Musa aliona mfano wa jengo lile la ajabu ambalo lingekuwa mahali pa kukaa pa utukufu Wake. Ni katika mlima pamoja na MUNGU- mahali pa siri pa ushirika - ambapo tunapaswa kuutafakari mpango Wake wa utukufu kwa wanadamu. Ndipo tutakapowezeshwa, na hivyo kutengeneza/kuumba muundo wa tabia yetu ili ahadi Yake itimizwe kwetu, "Nitakaa ndani yao, na nitatembea kati yao, Nami nitakuwa MUNGU wao, nao watakuwa watu Wangu." 2 Wakorintho 6:16. [Pr 57.5; Maombi Aya ya 20]

Ilikuwa ni katika masaa ya maombi ya faragha ndipo ambapo Yesu alipokea hekima na nguvu katika maisha Yake ya duniani. Hebu vijana wafuate mfano Wake katika kutafuta alfajiri na jioni muda wa utulivu kwaajili ya ushirika na Baba yao aliye mbinguni. Hebu wainue mioyo yao kwa MUNGU siku nzima inapoendelea kusonga mbele. Katika kila hatua ya njia zetu anasema, 'Kwa maana Mimi, Bwana, MUNGU wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; nitakusaidia..... Isaya 41:13. Endapo watoto wetu wangeliweza kujifunza masomo haya katika

miaka yao ya mapema/awali, ni upya gani na nguvu, furaha na utamu ulioje, ambao ungeletwa maishani mwao!— (Education, 258, 259) [Pr 58.1; Maombi Aya ya 21]

Kuomba kwa Imani Huleta Baraka nyingi — Kwa maneno tunayoongea kwa watu na katika maombi tunayotoa, MUNGU anatutaka tutoe ushahidi dhahiri kwamba tuna maisha ya kiroho. Hatufurahii utimilifu wa baraka ambazo Bwana ametuandalia, kwa sababu hatumwombi/hatumwulizi Bwana kwa imani. Laiti tungeitumia imani katika Neno la MUNGU aliye hai tungelikuwa na baraka nyingi. Tunamvunjia MUNGU heshima kwa ukosefu wetu wa imani; na hivyo hatuwezi kuwapa maisha wengine kwa kutoa ushuhuda ulio hai, na wenye kuinua. Hatuwezi kutoa kile ambacho hatumiliki. — (Testimonies for the Church 6:63) [Pr 58.2; Maombi Aya ya 22]

Omba kwa Imani; Kisha Pokea — Kuna nguvu inayopatikana kutoka kwa MUNGU. Yeye Anaweza kusaidia. Yeye Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, utapata; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kisha, omba, fanya kazi, ndiyo inapaswa kuwa kauli mbiu yako. - (Testimonies for the Church 2:427) [Pr 58.3; Maombi Aya ya 23]

Imani hupokea Baraka Kabla haijatambulika wala kuhisiwa — nimeona mara kwa mara kwamba watoto wa Bwana hupuuza maombi, haswa maombi ya siri zaidi; kwamba wengi hawatunii imani hiyo ambayo ni haki yao na wajibu wao kuwa nayo, mara nyingi wakingojea hisia ambayo imani pekee inaweza kuleta. Hisia sio imani; hivi ni vitu viwili tofauti. Imani ni yetu, tumepewa ili kuizoeza, lakini hisia za furaha na baraka ni MUNGU hutoa. Neema ya MUNGU huijia nafsi kupitia mkondo wa imani hai, na imani hiyo iko katika uwezo wetu kuwa kuifanyia mazoezi, na kuwa nayo. [Pr 58.4; Maombi Aya ya 24]

Imani ya Kweli inashikilia na kudai baraka iliyoahidiwa kabla haijatambulika na kuhisiwa. Lazima tupeleke ombi letu kwa imani ndani ya pazia la pili na kuacha imani yetu ichukue baraka iliyoahidiwa na kuidai kama yetu. Kisha tunapaswa kuamini kwamba tunapokea baraka, kwa sababu imani yetu imeishikilia, na ni kulingana na Neno, basi ni yetu. Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini

ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Hapa kuna imani, imani dhahiri, iliyo wazi kabisa, kuamini kwamba tunapokea mibaraka, hata kabla ya kuitambua. Baraka iliyoahidiwa inapogunduliwa, inapoonekana na hata kufurahiwa, basi imani inamezwa. Lakini wengi hudhani wanayo imani kubwa wanapokuwa wana ushirika kwa kiasi kikubwa na Roho Mtakatifu na kwamba hawawezi kuwa na imani isipokuwa wanahisi nguvu ya Roho. Hilo linachanganya imani na baraka ambayo huja kupitia imani. Wakati hasa wa kutumia imani ni pale tunapohisi kukosa msaada wa Roho. Wakati mawingu mazito ya giza yanaonekana kuigubika akili, basi huo ndio wakati wa kuruhusu imani iliyo hai itoboe giza na kutawanya mawingu. Imani ya Kweli inapatikana katika ahadi zilizo katika Neno la MUNGU, na ni wale tu ambao wanaolitii Neno hilo ndio ambao wanaweza kudai ahadi Zake tukufu. "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. (Yohana 15:7). na twaweza kupokea Kwake chochote tunachoomba, maana tunazitii amri Zake na kufanya yale yanayompendeza." 1 Yohana 3:22.—(Early Writings, 72, 73) [Pr 59.1; Maombi Aya ya 25]

Usizimie nguvu ikiwa Hakuna Jibu La Mpapo kwa hapo lililotolewa — Imani yako haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiohofu kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za kweli: "Ombeni, nanyi mtapewa." MUNGU ni mwenye hekima mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaotembea katika unyoofu kitu chochote chema- (Testimonies for the Church 1:120) [Pr 59.2; Maombi Aya ya 26]

Omba; na Kisha Matokeo mwachie MUNGU— Fanya kazi kwa imani, na mwachie MUNGU matokeo. Omba kwa imani, na mafumbo na siri ya majaliwa Yake italeta jibu Lake. Kuna mwingine inaelekea kama hutaweza kufaulu. Lakini fanya kazi na uamini, ukiwekamo katika jitihada yako imani, tumaini, na ujasiri. Baada ya kufanya uwezavyo, umngojee Bwana, ukitangaza uaminifu Wake, Naye atatimiza Neno Lake. Subiri, sio kwa hofu, na wasiwasi lakini kwa imani yenye ujasiri, isiyotishika na uwe na kumtegemea Yeye kusikoyumbayumba.—(Testimonies for the Church 7:245) [Pr 59.3; Maombi Aya ya 27]

Omba kwa Ujasiri – Ni maombi ya kutoka moyoni ya imani ambayo husikika mbinguni na kujibiwa duniani. MUNGU anaelewa mahitaji ya wanadamu. Yeye Anajua kile tunachotamani hata kabla hatujamwomba. Yeye Anaona mgogoro/mzozo wa roho na mashaka na majaribu. Yeye Anaona unyofu wa mwombaji. Naye Atapokea fedheha na mateso ya roho. "Nitamtazama mtu huyu," anatangaza, "hata yeye aliye maskini na mwenye roho iliyopondeka, na anayetetemeka kwa Neno Langu." [Pr 60.1; Maombi Aya ya 28]

Ni fursa yetu kuomba kwa ujasiri, Roho akichochea maombi yetu. Kwa unyenyekevu tunapaswa kuelezea mahitaji yetu kwa Bwana, na kudai ahadi Yake. - (God's Amazing Grace, 92) [Pr 60.2; Maombi Aya ya 29]

Yesu Yu tayari Kusikiliza Maombi Leo Kama Alipokuwa Duniani – Hekima ya Ulimwengu inafundisha kwamba sala sio muhimu. Wanasayansi wanadai kuwa hakuna jibu halisi la ombi; kwamba hii itakuwa ukiukaji wa sheria, muujiza, na kwamba miujiza haipo. Wao husema Ulimwengu unasimamiwa na sheria zisizobadilika, na MUNGU Mwenyewe hawezi kufanya chochote kinyume na sheria hizi. Kwa hivyo wanamwakilisha MUNGU akiwa amefungwa na sheria Zake Mwenyewe-kana kwamba utendaji wa sheria za Mungu unaondoa uhuru wa Bwana, Mwenyezi. Mafundisho hayo yanapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je! Miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Huyu Huyu Mwenye huruma anaishi hivi leo, na Yuko tayari kusikiliza maombi ya imani kama vile alipotembea miongoni mwa wanadamu na kukutana nao uso kwa uso (waziwazi kwa kuonekana au mbashara). - (The Great Controversy, 525) [Pr 60.3; Maombi Aya ya 30]

Maombi ya Imani huonyesha Matakwa Rahisi ya roho— Maombi sio mpatanishi wa dhambi; hayana fadhila au sifa yake yenyewe. Maneno yote tunayoyamiliki na kuyarembesha tunapoyatoa hayalingani hata na shauku moja takatifu. Maombi yaliyopangiliwa vizuri kwa ufasaha zaidi hayana tofauti na maneno ya kubwatikabwatika tu ikiwa hayaonyeshi hisia za Kweli za moyo. Lakini ombi linalotoka kwenye moyo wenye dhati na makini, wakati mahitaji sahili ya roho yanapowasilishwa, kama vile tunavyoweza kumwomba jambo rafiki wa kidunia kupata upendeleo (kuomba feva), tukitarajia tutapata-hili ni ombi

la imani. MUNGU hatamani pongezi zetu za sherehe za ibada ya destruri, bali kilio kisichoneneka cha moyo uliovunjika na kuhuzunishwa na hisia za dhambi na udhaifu mwingi hupata kibali kwa Baba wa rehema zote. - (Thoughts from the Mount of Blessing,86, 87) [Pr 60.4; Maombi Aya ya 31]

Maombi humwamsha MUNGU Kutenda-Kwa maombi yako ya imani yenye bidii unaweza kufanya mkono wenye nguvu zote, unaoendesha na kutawala ulimwengu ujongee. Unaweza kuwafundisha watoto wako kuomba kwa ufanisi wanapopiga magoti kando yako. Hebu maombi yapande juu kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, "Uwasamehe watu Wako, Ee Bwana, wala usiwape urithi Wako wakosaji, ili mataifa wasiwatawale; wasije kusema miongoni mwao, Yuko wapi MUNGU wao?" MUNGU Yuko kazini Akitenda. Yeye hufanya maajabu, na ingawa Yupo juu na ameinuliwa, maombi yanaweza kufikia kiti Chake cha enzi. Yeye anayegeuka na kupindua juu-chini mambo au kuyatangua, Yeye anayeweza kufanya mambo ya ajabu, atazingatia maombi ya toba ya imani kutoka kwa watoto Wake wanyenyekavu. - (The Review and Herald, Aprili 23, 1889) [Pr 61.1; Maombi Aya ya 32]

MUNGU Hawezi Kujibu Maombi Asiyooombwa – Maombi na Imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu yoyote duniani inaweza kutimiza. Ni nadra sana, katika hali zote, tunawekwa katika nafasi ile ile mara mbili. Tunakuwa na matukio mapya na majaribu mapya ya kuyashinda, ambapo uzoefu wetu wa zamani hauwezi kuwa mwongozo wa kutosha. Lazima tuwe na nuru siku zote inayotoka kwa MUNGU. Kristo daima hutuma ujumbe kwa wale wanaosikia sauti Yake. [Pr 61.2; Maombi Aya ya 33]

Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia, katika kujibu maombi ya imani, kile ambacho hangeweza kutupa endapo tusingemwuliza/hatukumuomba. - (My Life Today, 15) [Pr 61.3; Maombi Aya ya 34]

Wachungaji/Watumishi Wasichoke Katika Maombi – Watumishi wanapaswa kufanya maandalizi ya moyo kabla ya kuanza kazi ya kuwasaidia wengine, kwani walei wamewatangulia wachungaji walio wengi. Wanapaswa kupigana mieleka bila kuchoka katika sala hadi Bwana awabariki. Wakati upendo wa MUNGU unawaka juu ya

madhabahu ya mioyo yao, hawatahubiri ili kuonyesha busara au ujanja walio nao, bali watamwasilisha Kristo ambaye huondoa dhambi za ulimwengu. - (Testimonies for the Church 5:166) [Pr 61.4; Maombi Aya ya 35]

Tiba ya Kukata Tamaa au kufa moyo Ni Imani, Maombi, na Kazi – Kwa wale wote waliokata tamaa kuna tiba/dawa moja tu, - imani, sala, na kazi. (Testimonies for the Church 6:438) [Pr 61.1; Maombi Aya ya 36]

Maombi Ndio Silaha Ambayo kwayo Tunampinga Adui – Kristo Ndiye tumaini letu pekee. Njoo kwa MUNGU kwa Jina la Yeye aliyetoa uhai wake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu. Tumainia ufanisi wa dhabihu Yake. Onyesha kwamba upendo Wake, furaha Yake, imo katika roho yako, na kwa sababu ya hili, furaha yako imejaa. Katika MUNGU ndiyo nguvu zetu. Omba sana. Maombi ni maisha ya roho. Ombi la imani ni silaha ambayo tunaweza kufanikiwa kupinga kila shambulio la adui. - (The Signs of the Times, Agosti 24, 1904) [Pr 62.2; Maombi Aya ya 37]

Maombi hayapotei, hata ikiwa hayajajibiwa kama tunavyotarajia – Ombi la imani halipotei kamwe; lakini kudai kuwa litajibiwa kila wakati kwa njia ileile na kwa jambo lile lile ambalo tumetarajia, ni dhana tu. - (Testimonies for the Church 1:231) [Pr 62.3; Maombi Aya ya 38]

Mfariji Huja katika kujibu Maombi ya Imani – Wakati wote na mahali pote, katika huzuni zote na shida zote, wakati hali ya nje inaonekana kuwa ni ya giza na ile ya wakati ujao inaleta mfadhaiko, nasi tunajisikia wanyonge na peke yetu, Mfariji atatumwa katika kujibu maombi ya imani. Mazingira yanaweza kututenganisha na kila rafiki wa kidunia; lakini hakuna hali/mazingira, wala umbali, unaoweza kututenganisha na Mfariji wa mbinguni. Popote tulipo, popote tutakapoenda, Yeye Yuko mkono wetu wa kuume kila wakati kutusaidia, kutudumisha, kutuunza, na kutupa nguvu. - (The Desire of Ages, 669, 670) [Pr 62.4; Maombi Aya ya 39]

Malaika hubeba Maombi yetu kwenda Patakatifu pa Mbinguni – Malaika husikia sadaka za sifa na ombi la imani, na hubeba maombi kwa Yeye anayehudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na wanasihi haki na sifa Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli

hujitegemeza/humshikilia Yeye aliye mkuu na hutupatia ushindi. Akiwa magotini mwake, Mkristo anapata nguvu za kupinga vishawishi. - (The Review and Herald, Februari 1, 1912) [Pr 62.5; Maombi Aya ya 40]

Ombi la dhati litakanganya Jitihada kali za Shetani – Mwanadamu ni mateka wa Shetani na kwa kawaida amejikita katika kufuata maoni yake adui na kutii matakwa na amri zake. Yeye mwenyewe hana uwezo wa kupinga upinzani maridhawa wa uovu. Ni pale tu Kristo anapokaa ndani yake kwa imani hai, akiziongoza shauku zake na kumtia nguvu kwa uwezo utokao juu, ndipo mwanadamu anaweza kujitosa ili kukabiliana na adui mbaya sana. Njia nyingine yoyote ya ulinzi ni kazi bure kabisa. Ni kupitia njia ya Kristo pekee, ndiyo kwamba nguvu ya Shetani inawekewa ukomo. Huu ni Ukweli muhimu ambao wote wanapaswa kuelewa. Shetani yuko ‘bize’ kila wakati, akienda huku na huko, akitembea juu na chini katika dunia, akitafuta mtu ambaye anaweza kumeza. Lakini ombi la dhati la imani litakanganya juhudi zake kali. Kisha chukua "ngao ya imani," ndugu, "ambayo kwayo mtaweza kuzima mishale yote ya moto ya yule mwovu." Testimonies for the Church 5:294) [Pr 63.1; Maombi Aya ya 41]

Ombi la Imani Hushinda Dhidi ya Shetani – Ombi la imani ni nguvu kubwa ya Mkristo na hakika litamshinda Shetani. Hii ndiyo sababu yeye anasisitiza kwamba hatuna haja ya maombi. Jina la Yesu, Wakili wetu, Shetani analichukia; na tunapomwendea Kwake kwa dhati kwa ajili ya msaada, Jeshi la Shetani linaogopa. Kusudi lake linatimia vizuri ikiwa tunapuuza mazoea ya kuomba, kwa kuwa maajabu yake ya uwongo yanapokelewa kwa urahisi zaidi. - (Testimonies for the Church 1:296) [Pr 63.2; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 7

MAOMBI NA UTII

Omba na Fanya Kazi – Hatupaswi kukaa kwa utulivu kama maji ya mtungini eti tunangojea udhalimu na dhiki vitufikie, na kukunja mikono yetu, bila kufanya chochote kuzuia maovu. Hebu vilio vyetu kwa pamoja vitumwe juu mbinguni. Omba na ufanye kazi, na fanya kazi na usali. Lakini usifanye chochote kwa kukurupuka. Jifunze kuliko wakati mwingine wowote ule kuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo, hili ni lazima. -(Selected Messages 2:370, 371) [Pr 64.1; Maombi Aya ya 1]

Lazima tuombe na tufanye kazi na kuamini. Bwana Ndiye ufanisi wetu. (Evangelism, 438) [Pr 64.2; Maombi Aya ya 2]

Utalazimika kupambana mieleka na magumu, kubeba mizigo, kutoa ushauri, kupanga mikakati na kuitekeleza, ukimtazama MUNGU kila wakati kwa ajili ya msaada. Omba na fanya kazi, fanya kazi na omba; kama wanafunzi katika shule ya Kristo, jifunzeni kuhusu Yesu. (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 498, 499) [Pr 64.3; Maombi Aya ya 3]

Maombi ni mkakati wa mbingu wa Mafanikio katika Kuishinda Dhambi – Kuna wengi ambao, japo wanajitahidi kuzitii amri za MUNGU, wana amani kidogo au furaha. Upungufu huu katika uzoefu wao ni matokeo ya kushindwa kupata imani. Wanatembea kana kwamba wapo katika nchi yenye chumvi, iliyo na ardhi iliyokauka na kupasuka-pasukua vipandevipande. Wanaomba au kudai kidogo tu, wakati wanaweza kuomba mengi; kwani ahadi za MUNGU hazina kikomo. Hao hawawakilishi kwa usahihi utakaso unaokuja kwa kuitii ile Kweli. Bwana angependa wana na binti Zake wote wawe na furaha, amani, na utiifu. Kwa kuizoesha Imani, mwamini anafikia mahali pa kuzimiliki

baraka hizi. Kupitia imani, kila upungufu wa tabia unakarabatiwa, kila unajisi unasafishwa, kila kosa linarekebishwa, kila ubora unapata kuendelezwa na kuwa na ufanisi zaidi na zaidi. [Pr 64.4; Maombi Aya ya 4]

Maombi ni njia iliyowekwa na mbingu kwaajili ya mafanikio katika vita na dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo. Ushawishi wa Bwana unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwaajili ya Roho Mtakatifu, kwaajili sifa na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea." (The Acts of the Apostles, 563, 564) [Pr 65.1; Maombi Aya ya 5]

Majaribu ya kila siku Hufanya Maombi Kuwa jambo la Lazima— Nguvu inayopatikana katika maombi na MUNGU, ikiunganishwa na juhudi za mtu binafsi katika kuifundisha akili kufikiri kwa kina na kuwa na uangalifu/usikivu, humwandaa mtu huyo kwa ajili ya majukumu ya kila siku na hufanya roho iwe na amani katika hali zote, haijalishi hali ni ngumu kwa kiasi gani. Majaribu ambayo tunakuwa katika mazingira yake kila siku hufanya maombi kuwa jambo la lazima (majaribu ambayo tunaanikwa kwayo kila siku, hufanya maombi kuwa jambo la lazima). Ili tuweze kulindwa na uweza wa MUNGU kwa njia ya imani, shauku za akili zinapaswa kuelekezwa mbinguni daima katika maombi ya kimya ili kupata msaada, kupata nuru, kupata nguvu, kupata maarifa. Lakini fikra na maombi hayawezi kuchukua nafasi ya kuwa dhati, na kutenda kwa juhudi katika kutumia muda vizuri kwa uaminifu. Kazi na sala zinahitajika katika kukamilisha tabia ya Kikristo. — (Testimonies for the Church 4:459) [Pr 65.2; Maombi Aya ya 6]

Maombi ya Kila siku Hugeuza Makosa Kuwa Ushindi — Ikiwa mtu ambaye kila siku anashirikiana na MUNGU anapotea njia kwa kutenda makosa, ikiwa anageuka kwa nukta chache kutoka kwenye kumwangukia Yesu kwa uthabiti, na sio kwa sababu anatenda dhambi kwa makusudi; kwani anapoliona kosa lake, anarudi tena, na kumtazama Yesu, basi ule uhalisia kwamba amekosea, haumfanyi ashuke thamani mbele ya moyo wa MUNGU.

Anajua kwamba ana ushirika na Mwokozi; na anapokemewa kwa kosa lake katika suala fulani la maamuzi yake, hatembei na jazba moyoni au, au chuki ya kimya kimya na kumlalamikia MUNGU, bali huligeuza lile kosa na kuwa ushindi. Anajifunza somo kutoka kwenye Maneno ya Mwalimu, na anachukua tahadhari ili asidanganyike au kudanganywa tena. - (The Review and Herald, Mei 12, 1896) [Pr 65.3; Maombi Aya ya 7]

Kristo Ndiye Njia Ya Maombi Kati Yetu na MUNGU— Kristo Ndiye kiunganishi kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameahidi maombezi Yake binafsi. Anaweka fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo anamuomba mwanadamu, na mwanadamu, anayehitaji msaada wa Mungu, anajiombea mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU ukubali wetu wa uzuri wa Kristo, na **manukato** hutolewa kwa maombezi yetu. Tunapomkaribia MUNGU kupitia fadhila ya Mkombozi, Kristo hutuweka karibu na upande Wake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kibinadamu, wakati kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye anashikishika kiti cha enzi cha Yule Asiye na mwisho. Yeye anaweka sifa, wema na haki Yake, kama uvumba mtamu, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi yetu. Yeye Anaahidi kusikia na kujibu maombi yetu. [Pr 66.1; Maombi Aya ya 8]

Naam, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na MUNGU. Pia amekuwa njia ya baraka kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Watu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya jitihada za bidii, za kudumu na za dhati ili kuwaokoa wale ambao wako tayari kufa. - (Testimonies for the Church 8:178) [Pr 66.2; Maombi Aya ya 9]

Wakati kuhani mkuu ananyunyiza damu iliyo na joto bado juu ya Kiti cha Rehema wakati wingu la uvumba lenye harufu nzuri likipanda mbele za MUNGU, ndivyo ambavyo wakati tunakiri dhambi zetu na kuomba ufanisi na haki ya damu ya upatanisho ya Kristo, sala zetu zinapaswa kupaa mbinguni, zikiwa na harufu nzuri na sifa za tabia ya Mwokozi wetu. Pamoja na kutostahili kwetu, tunapaswa kukumbuka kwamba Yupo Yule Anayeweza kuchukua dhambi, na Ambaye Yuko tayari kufanya hivyo, Naye

Anahangaika kumwokoia mwenye dhambi. Kwa damu Yake Mwenyewe alilipa (penalty) adhabu kwa wakosaji wa sheria wote. Kila dhambi iliyowasilishwa mbele za MUNGU kwa moyo uliopondeka, ataiondoa. "Ijapokuwa dhambi zako ni nyekundu, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama sufu." The Review and Herald, Septemba 29, 1896) [Pr 66.3; Maombi Aya ya 10]

Maombi hayana maana au faida yoyote ikiwa Kuna Uovu wa Kukusudia Moyoni- "Neema ya MUNGU iletayo wokovu imeonekana kwa watu wote, ikitufundisha kwamba, tukikataa uovu na tamaa za ulimwengu, tunatakiwa kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa." Basi, muwe wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. Je! Maombi yako yana thamani au faida gani mkiwa mnawazia au kuuzingatia uovu uliopo ndani ya mioyo yenu? Msipofanya badiliko la dhati, muda sio mrefu, mtachoka kukemewa au kupewa maonyo, kama walivyofanya wana wa Israeli; na, kama wao, mtamwasi MUNGU. Baadhi yenu manakubali kukemewa kwa maneno, lakini mioyoni mwenu hamkubali. Mnaenenda sawa na hapo awali, mkiguswa kwa udogo zaidi na ushawishi wa Roho wa MUNGU, mnazidi kupofushwa zaidi na zaidi, na **kuwa na hekima** pungufu zaidi, kujitawala au kujizuia nafsi kwa udogo zaidi, mmepungukiwa na nguvu ya maadili zaidi, na bidii kidogo na kufurahiya uzoefu wa kidini/kiroho kwa udogo zaidi; na, msipoongoka, hatimaye mtatanga mbali na kumwacha MUNGU kabisa. Hamkufanya mabadiliko katika maisha yenu wakati karipio lilipowajia, kwa sababu hamjaona na kugundua kasoro zenu za kitabia na tofauti kubwa kati ya maisha yenu na maisha ya Kristo. Imekuwa sera yenu kujiweka katika mazingira ambayo hamtapoteza kabisa ujasiri mlio nao kwa ndugu zenu. -(Testimonies for the Church 4:332) [Pr 67.1; Maombi Aya ya 11]

Maombi hayachukui Nafasi ya Utii – Kuna masharti ya kutimizwa ahadi za MUNGU, na ombi haliwezi kuchukua mahali pa wajibu. "Ikiwa mnanipenda," Kristo anasema, "mtazishika amri Zangu." "Azipokeaye amri Zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye. Naye anipendaye Mimi atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha Kwake." Yohana 14:15, 21. Wale ambao

huleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Zake wakati hawafuati masharti, wanamtukana Yehova (au wanamkosea heshima Mungu). Hao huleta Jina la Kristo kama mamlaka yao kwa ajili ya kutimiziwa ahadi, lakini hawafanyi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake Yeye. [Pr 67.2; Maombi Aya ya 12]

Wengi wanapoteza haki ya masharti ya kukubaliwa na Baba. Twahitaji kuchunguza kwa ukaribu tendo la kumtegemea Yeye wakati tunapokuwa tunamkaribia MUNGU. Ikiwa sisi si watiifu, tunamletea Bwana hundi ya kupewa malipo wakati sisi hatujatimiza masharti ambayo yangeidhinisha malipo yetu. Tunawasilisha kwa MUNGU ahadi Zake, na kumwomba azitimize, wakati kwa kufanya hivyo atalivunja heshima Jina Lake Mwenyewe. [Pr 68.1; Maombi Aya ya 13]

Ahadi ni “Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. (Yohana 15:7). Na Yohana anatangaza: “Katika hili twajua ya kuwa tunamjua Yeye, ikiwa tunazishika amri Zake. Mtu akisema kwamba anamjua, lakini hazitii amri Zake, basi mtu huyo ni mwongo, na Kweli haimo ndani yake. Bali yeye ashikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa MUNGU umekamilika kweli-kweli.” 1 Yohana 2: 3-5.— (Christ's Object Lessons, 143, 144) [Pr 68.2; Maombi Aya ya 14]

Twapaswa Kuamini MUNGU Anasikia na Kisha kuyaishi Maombi Yetu – Watoto na vijana wanaweza kuja kwa Yesu na mizigo yao na mifadhaiko yao, wakifahamu kwamba Ataheshimu maombi yao Kwake, na kuwapa yale wanayohitaji. Kuwa na bidii; kuwa imara. Wasilisha ahadi ya MUNGU, na kisha uamini bila shaka hata moja. Usingoje kupata hisia maalum kabla ya kufikiria Bwana anajibu. Usikariri na kuweka alama kwamba kuna njia fulani ambayo Bwana lazima aitumie au kuifanyia kazi kwako kabla ya wewe kuamini kuwa utapokea vitu ulivyoomba Kwake; lakini amini Neno Lake, na Ukabidhi kila kitu mikononi mwa Bwana, ukiwa na imani kamili kwamba maombi yako yataheshimiwa, na jibu litakuja wakati muafaka na kwa njia ambayo Baba yako wa mbinguni anaona ni kwa faida yako; na kisha ishi maombi yako. Tembea kwa unyenyekevu na endelea kusonga mbele. -(Messages to Young People, 123) [Pr 68.3; Maombi Aya ya 15]

Omba kwa ajili ya Neema ya kuyapinga majaribu- Katika maisha ya kila siku utakutana na mishangao ya ghafla, kukatishwa tamaa, na vishawishi. Neno linasema nini? "Mpingeni shetani," kwa kumtegemea Mungu kabisa, "naye atawakimbia. Mkaribieni MUNGU, Naye atawakaribia ninyi. Na ashikilie nguvu Zangu, ili afanye amani Nami; naye atafanya amani Nami." Mtazame Yesu kila wakati na kila mahali, ukitoa maombi ya kimya kutoka katika moyo mwaminifu ili ujue jinsi ya kufanya mapenzi Yake. Kisha adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Bwana atakuinua kiwango chako dhidi ya adui. Unapokaribia kuanguka au kutekewa na jaribu, kupoteza uvumilivu na kuitawala nafsi, kuwa mgumu na mwenye kulaani, kutafuta makosa na kumchukia mtu, kukosoa, kufanya ujeuri, kufanya ukatili au kulaumu – huu ni wakati wako kutuma ombi mbinguni, "Nisaidie, Ee MUNGU, kupinga jaribu, kuondoa uchungu wote na ghadhabu na kunena mabaya kutoka moyoni mwangu. Nipe upole Wako, unyenyekevu Wako, uvumilivu Wako, na upendo Wako. Usiniache nimuaibishe Mkombozi wangu, nisitafsiri vibaya maneno na nia ya mke wangu, watoto wangu, na kaka na dada zangu katika imani. Nisaidie nipate kuwa mwema, mwenye moyo laini/mwororo, mwenye huruma, mwenye kusamehe. Nisaidie kuwa mfunga-nyumba (mweka nyumba sawa), yaani mlinzi wa kweli nyumbani mwangu na kuwakilisha tabia ya Kristo kwa wengine." *(mume kingereza ni husband-houseband Kamba ya kufunga nyumba yake kwa ulinzi na upendo na yale bora) (The Adventist Home, 214, 215) [Pr 68.4; Maombi Aya ya 16]

Tunajua hatari na vishawishi zinazowazinga vijana wakati huu sio chache au ndogo.....Twaishi katika wakati ambapo kupinga uovu kunahitaji kukesha na kuomba kila wakati. Neno la MUNGU lenye thamani ndiyo kiwango kwa vijana ambao watakuwa waaminifu kwa Mfalme wa mbinguni. Hebu na wasome Maandiko. Hebu na waweke kwenye kumbukumbu kwa kukariri mstari baada ya mstari, na wapate ujuzi wa kile Bwana Alichosema Na katika majaribu hebu vijana watandaze Neno la MUNGU mbele yao, na kwa mioyo iliyo na unyenyekevu, na kwa imani, wamtafute Bwana kwa ajili ya hekima ili kujua njia Yake, na kwa nguvu wakanyage na kutembea ndani Yake [Pr 69.1; Maombi Aya ya 17]

Hebu vijana wetu waanzishe vita dhidi ya kila tabia ambayo ina hatari hata ile ndogo ya kuongoza roho mbali na wajibu na kujitoa wakfu. Na watenge misimu fulani kwa ajili ya maombi, bila kupuuza masaa hayo kamwe, ikiwa inaweza kuepukika. Ikiwa wataenda vitani na tabia zao mbaya walizokuwa nazo kabla ya kukiri ushirika na Kristo, wataangukia kuwa windo la hila za Shetani kwa urahisi. Lakini wakiwa wamejihami na Neno la MUNGU, wakiwa wamelithamini moyoni na akilini, watatoka bila kuumizwa na mashambulio yote ya maadui wa MUNGU au mwanadamu. - (My Life Today, 315) [Pr 69.2; Maombi Aya ya 18]

SURA YA 8

MAOMBI YALETAYO USHINDI

Usiachilie ahadi za MUNGU— Kila mtakatifu ambaye anamuendea MUNGU kwa moyo wa kweli/dhati, na kutuma maombi yake ya uaminifu Kwake kwa imani, atajibiwa maombi yake. Imani yako haipaswi kuziachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka kwa maombi yako. Basi Usipate hofu kumtumaini MUNGU-Usiogope kumtumaini Mungu. Zitegemee ahadi Zake za Kweli: "Ombeni, nanyi mtapewa." MUNGU ni Mwenye busara isiyo na ukomo kiasi kwamba hawezi kukosea kamwe, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaotembea kwa unyoofu mbele Zake kitu chochote kilicho kizuri. Mwanadamu hukosea, na japokuwa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo ulio mkweli, huwa haombi mara zote vitu ambavyo ni vyema kwake, au vile ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, Baba yetu Mwenye busara na mwema husikia maombi yetu, Naye atajibu, wakati mwingine hujibu haraka-; lakini Yeye hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. MUNGU hutupatia baraka; laiti tungeangalia mkakati Wake, tungeona kwa uwazi kwamba, Yeye Anajua kilicho bora kwaajili yetu na kwamba maombi yetu

hujibiwa. Hakuna chochote cha kutuumiza tutakachopewa, ilar tu baraka tunazohitaji, badala ya kile kitu tuliomba ambacho hakitakuwa kizuri kwetu, na ambacho kingetuumiza. [Pr 70.1; Maombi Aya ya 1]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi/hatuoni majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu kwa bidii, bila kuruhusu mashaka kuingia ndani yetu, kwani hayo yatatutenganisha tu na MUNGU. Endapo Imani yetu itatetereka, basi hatutapokea kitu chochote kutoka Kwake. Imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa imara; na tunapokuwa na uhitaji mkubwa zaidi, baraka itatuangukia kama mvua inavyomwagika. –(Testimonies for the Church 1:120, 121) [Pr 70.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya bidii, yasiyochoka na yasiyotikiswa— MUNGU hasemi uombe mara moja tu, na kisha utapokea. Yeye Anatumuru kuomba. Bila kuchoka tusitikisike katika maombi. Kuomba kwa imani imara humleta mwombaji kwenye mkaao wa bidi, na humfanya awe na matamano zaidi, wakati wa kungoja kupokea mambo aliyoyaomba. Kristo alisema kwa Martha kaburini kwa Lazaro, “Mimi sikukwambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?” Yohana 11:40. [Pr 71.1; Maombi Aya ya 3]

Lakini wengi hawana imani iliyo hai. Hii ndio sababu hawaoni zaidi nguvu za MUNGU. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika matendo na kazi zao kuliko utendaji kazi wa MUNGU kwao. Wanajipigania wenyewe-(wanajitunza wenyewe). Wanapanga na kuweka mikakati, lakini husali kidogo, na kumtumaini Mungu, kwa kiasi kidogo tu. Wao hufikiri kwamba wana imani, lakini kumbe ni msukumo tu wa muda mfupi. Wanashindwa kutambua uhitaji wao wenyewe, au utayari wa MUNGU kutoa, nao hawavumilii katika kuweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 71.2; Maombi Aya ya 4]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya dhati na bidii na yasiyotikiswa kama ilivyokuwa ombi la yule rafiki masikini aliyekwenda kuomba mikate usiku wa manane. Kwa kadiri tunavyoomba kwa dhati, bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa wa karibu zaidi. Tutapokea baraka zilizoongezeka kwa sababu tumeongezeka kiimani. [Pr 71.3; Maombi Aya ya 5]

Fungu letu ni kuomba na kisha kuamini. kesheni mkiomba. Kisha, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Kumbuka kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na kutenda kulingana na maombi yako. Na hilo litafanya tofauti kubwa kwako pale jaribu litakapokujia ili kuhakikisha kuwa Imani yako ni ya Kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfano tu au maneno tu. [Pr 71.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi ya dhati na bidii yana manufaa mno – Sala ile inayotoka katika moyo wenye bidii, na mnyofu, na unaoamini ndiyo itakuwa na matokeo mema, maombi yenye bidii ambayo yatakuwa na matokeo makubwa na mema mno. MUNGU huwa hajibu maombi yetu kila wakati kama tunavyotarajia, kwani hatuna uwezo wa kuombea kile ambacho kingekuwa bora zaidi kwetu; lakini kwa upendo na hekima Yake isiyo na kikomo, Yeye atatupatia vile vitu ambavyo hakika tunavihitaji. -(Testimonies for the Church 4:531) [Pr 71.5; Maombi Aya ya 7]

Usiuachilie mkono wa MUNGU haraka- Nilimuuliza malaika kwa nini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, “wanauachilia mkono wa Bwana upesi mno. Peleka maombi yako kwa bidii kwenye kiti cha enzi, na kisha ungojee hapo kwa imani thabiti. Ahadi za Mungu ni za uhakika na Kweli. Amini kwamba unapokea vile ulivyoomba, nawe utapata.” Kisha nikaelekezwa kwa Eliya. Alikuwa na hisia za mwanadamu kama sisi, naye akaomba kwa bidii na unyofu. Imani yake ilivumilia jaribu/mtihani. Aliomba mara saba mbele za Bwana, na mwishowe wingu likaonekana. Niliona kwamba tulikuwa na shaka na ahadi za hakika, na tukamjeruhi Mwokozi kwa ukosefu wetu wa imani. Malaika alisema, “Jifunge silaha, na juu ya yote chukua ngao ya imani; kwa kuwa hiyo italinda moyo, na maisha, dhidi ya mishale ya moto ya muovu.” Ikiwa adui anaweza kusababisha wale waliokata tamaa kuondoa macho yao kutoka kwa Yesu, na wajitazame wenyewe, na kukita kwenye kutostahili kwao, badala ya kukaa juu ya stahiki za Yesu, upendo Wake, sifa Zake, na rehema Zake kuu, ataponyoka na ngao yao ya imani na kulitimiza lengo lake; basi wataanikwa kwenye vishawishi vyake hatarishi. Kwa hiyo wanyonge/dhaifu wanapaswa kumtazama Yesu, na kumwamini Yeye; ndivyo wanavyoizoesha Imani yao na

kuionyesha/kuitumia.—(Early Writings, 73) [Pr 72.1; Maombi Aya ya 8]

Dumu katika maombi bila kuchoka— Wakati mtu anapumua kwa ombi la bidii na dhati kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee chini ya mbingu walilopewa wanadamu ambalo linatupasa kuokolewa kwalo), katika ile nguvu, unyofu, na bidii kuna ahadi kutoka kwa MUNGU kwamba Yeye Yupo karibu kujibu hilo ombi na zaidi ya inavyopotegemewa, Naye atafanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria. Hatupaswi kuomba tu kwa Jina la Yesu, bali kwa uvivio na uwepo na nguvu za Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa ina maana gani tunaposema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua-maumivu mazito yasiyoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhati. Kisha yatakifikia kiti cha rehema. Dumu katika maombi bila kuchoka. MUNGU hasemi, Omba mara moja, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, uwe mwepesi na mwenye utayari katika kuomba, ukiamini umeshavipata vile vitu unavyoomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu. - (Gospel Herald, Mei 28, 1902) [Pr 72.2; Maombi Aya ya 9]

Maombi ya dhati na ya bidii yanahitajika, sio dhaifu, sio Maombi yasiyo na moyo ndani yake — Kuna haja ya maombi, -ya dhati sana, yenye bidii, yenye **uchungu mzito**, - Ombi kama aliloomba Daudi akisema: "Kama paa anayetamani vijito vya maji, ndivyo ninavyo tamani roho yangu ikufuate, ee MUNGU."Nimetamani maagizo Yako; "Nimetamani wokovu Wako."Nafsi yangu inatamani, naam, inazimia kwa ajili ya hekalu la Bwana: moyo wangu na mwili wangu vinamlilia MUNGU aliye hai." Nafsi yangu inavunjika kwa hamu iliyo nayo juu ya hukumu Zako." Hii ni roho ya ombi la kupambana mieleka, Kama aliyokuwa nayo mtunga Zaburi wa kifalme. [Pr 73.1; Maombi Aya ya 10]

Danieli alimwomba MUNGU, hakujiinua mwenyewe wala kudai wema wowote: "Ee Bwana, sikia; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, sikiliza na utende; usichelewe, kwa mapenzi Yako, Ee MUNGU wangu." Hivi ndivyo Yakobo anavyoliita ombi linalofaa, lenye ufanisi, na la bidii. Kuhusu Kristo imeandikwa: "Na akiwa katika uchungu aliomba kwa dhati na bidii zaidi." Kwa kulinganisha na maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni ni maombi ya kusikitisha na dhaifu kiasi

gani, maombi yasiyo na kumimina roho, ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya mdomo au maneno tu, na ni wachache tu, ndio walio na shauku ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. -(Testimonies for the Church 4:534) [Pr 73.2; Maombi Aya ya 11]

Ombi linaloshinda au lenye ufanisi, Si Lazima Litolewe kwa Machozi na Mapambano – Kuna roho nyingi ambazo zinapigana mieleka kwa ajili ya ushindi maalum na baraka maalum ili ziweze kufanya jambo kubwa. Kwenye upande huu wa ulimwengu daima huhisi kwamba lazima wapigane mieleka mikali katika maombi na machozi. Watu hawa wanapochunguza Maandiko na maombi ili kujua mapenzi ya MUNGU yaliyoonyeshwa au kufunuliwa, na kisha kufanya mapenzi Yake kutoka moyoni kwa hali na mali bila kujifurahisha, watapata pumziko. Uchungu na mateso yote, machozi yote na mapambano, hayatawaletea baraka wanayoitamani. Nafsi inatakiwa kujisalimisha kabisa (100%). Lazima wafanye kazi inayojionyesha yenyewe, wakichukua wingi wa neema ya MUNGU ambayo imeahidiwa kwa wote wanaoomba kwa imani. - (Testimonies for the Church 9:165) [Pr 73.3; Maombi Aya ya 12]

Maombi ya bidii na ya daima/kudumu ni ya lazima – Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa MUNGU Mwenyewe, alihisi hitaji la maombi, Je, ni muhimu kwa kiasi gani zaidi basi kwa sisi wanadamu tulio dhaifu na wenye dhambi tunatakiwa kuhisi umuhimu wa maombi ya bidii, na endelevu, yale ya kila wakati? [Pr 73.4; Maombi Aya ya 13]

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa wingi kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio na ukomo. Ni jambo la kushangaza kwa kiasi gani kwamba tunaomba kidogo sana! MUNGU Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake wanyenyekevu, lakini bado kuna kusitasita kwingi kwa upande wetu, kumjulisha MUNGU yale tunayoyataka. Malaika wa mbinguni wanafikiria nini juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wanakabiliwa na majaribu, wakati moyo wa MUNGU Mwenye upendo usio na kikomo unainama kwao, tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiri, lakini bado wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo

sana? Malaika wanapenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona kuwa karibu na MUNGU ndiyo furaha kuu kupita zote; lakini wana wa mwanadamu wanaoishi hapa chini duniani, ambao wanahitaji msaada mkubwa ambao unaweza kutolewa na MUNGU tu, wanaonekana kuridhika kabisa kutembea bila nuru ya Roho Wake, ushirika wa uwepo Wake. [Pr 74.1; Maombi Aya ya 14]

Giza la mwovu huwazunguka na kuwafunga wale wanaopuuzia kuomba. Majaribu yanayonong'onezwa na adui yanawashawishi kutenda dhambi; na hii yote ni kwa sababu hawatumii upendeleo/fursa ambazo MUNGU amewapa katika miadi ya maombi pamoja Naye. Kwa nini wana na binti za MUNGU wasitesite kuomba au wawe na tabia ya kutopenda maombi, wakati maombi ni ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za mbinguni, mle ambako zimetunzwa ghala/hazina zisizo na kikomo za Mweza wa Yote? - (Steps to Christ, 94) Bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuongeza uzembe/kutojali, na kuchepuka kutoka kwenye njia sahihi. Kila wakati adui anatafuta kuzinga/kufunga njia inayoelekea kwenye Kiti cha Rehema, ili kwa sala ya dhati na imani tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu. - (Steps to Christ, 93, 94) [Pr 74.2; Maombi Aya ya 15]

Kama vile Yakobo, wewe pambana mieleka katika Maombi – Kuwa na bidii, kuwa mkweli/mnyofu. Maombi ya bidii yanafaa sana. Kama Yakobo, pambana katika maombi. Omba ukiwa na uchungu moyoni. Yesu, bustanini, alitokwa na matone mengi ya jasho la damu; lazima ufanye juhudi. Usiache chumba chako cha siri mpaka ujisikie kuwa na nguvu ndani ya MUNGU; kisha kesho, na maadamu unakesha na kuomba unaweza kuzikanyaga chini dhambi hizi zinazokuzinga vibaya kwa upesi, na kisha neema ya MUNGU inaweza na itaonekana ndani yako. - (Testimonies for the Church 1:158) [Pr 74.3; Maombi Aya ya 16]

Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na aliazimia. Uzoefu wake unathibitisha nguvu ya ombi la dharura, la kutokata tamaa au kuchoka. Ni wakati huu ndiyo ambapo tunapaswa kujifunza somo hili la maombi yanayoshinda na yenye kutochoka, yenye imani isiyokubali kushindwa. Ushindi mkubwa kwa kanisa la Kristo au Mkristo

mmoja mmoja sio ule unaopatikana kwa talanta, kisomo, elimu, kwa utajiri au kupendelewa na watu. Bali ni ushindi ambao hupatikana katika chumba cha siri pamoja na MUNGU, wakati imani ya dhati na yenye bidii, yenye uchungu mzito, inamshikilia Mkono wenye Mkuu wenye nguvu, [Pr 75.1; Maombi Aya ya 17]

Wale ambao hawataki kuacha kila dhambi na kutafuta kwa bidii baraka ya MUNGU, basi hawataipata. Lakini wote watakaoshika ahadi za MUNGU kama alivyofanya Yakobo, na kuwa dhati na bidii na uvumilivu kama yeye, watafaulu kama alivyofaulu. - (Patriarchs and Prophets, 203) [Pr 75.2; Maombi Aya ya 18]

Pambana mweleka katika Maombi Mpaka Ushindi Uje – MUNGU atakuwa kwetu kila kitu tunachotaka Yeye awe. Maombi yetu dhaifu, yasiyo na bidii, yenye moyo nusu-nusu, hayatatuletea majibu kutoka mbinguni. Oh, tunahitaji bidii katika kuwasilisha maombi yetu! Omba/Uliza kwa imani, subiri kwa imani, pokea kwa imani, furahi katika tumaini, kwani kila mtu atafutaye hupata. Uwe dhati na bidii katika jambo hilo. Mtafute MUNGU kwa moyo wote. Watu huweka roho na bidii katika kila kitu wanachofanya katika vitu vya kupita, hadi juhudi zao zitakapofanikiwa. Kwa unyofu na bidii nzito, jifunze stadi ya kutafuta baraka nyingi ambazo MUNGU ameahidi, na kwa uvumilivu, bidii, na juhudi utakuwa na nuru Yake na Ukweli Wake na neema Yake nyingi. [Pr 75.3; Maombi Aya ya 19]

Kwa unyofu, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Shindana na mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Jiweke kikamilifu mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, kisha uazimie kuwa wakala Wake mpendwa aliyejiweka wakfu, anayeongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na kujazwa na Roho Wake. [Pr 75.4; Maombi Aya ya 20]

Mwambie Yesu haja zako kwa unyofu wa roho yako. Hautakiwi kufanya mazungumzo marefu kwa vita, au kumhubiria MUNGU (au kumtolea hotuba Mungu), lakini kwa moyo wa huzuni juu ya dhambi zako, sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi

unaoponda-ponda roho, wewe utapata baraka ya amani ya Kristo. –(Our High Calling, 131) [Pr 75.5; Maombi Aya ya 21]

Omba bila kukoma- Katika kazi ya utunzaji wa moyo, ni lazima tuwe wepesi katika utayari wa maombi, bila kuchoka katika kuomba kiti cha neema ili kupata msaada. Wale ambao huchukua jina la "Mkristo" wanapaswa kumjia MUNGU kwa bidii, unyofu na unyenyekevu, wakiomba msaada. Mwokozi ametuambia tuombe bila kukoma. Mkristo hawezi kuwa katika nafasi au mkao wa kuomba kila wakati, lakini mawazo na matamaniao yake yanaweza kuwa juu kila wakati. Kujiamini wenyewe kungetoweka, kama tungeongea kidogo na kuomba zaidi. - (Sons and Daughters of God, 99) [Pr 76.1; Maombi Aya ya 22]

Kila Pumzi yapaswa Kuwa ombi-Sababu ya watu wengi kuachwa peke yao katika sehemu za majaribu ni kwamba hawamuweki Bwana mbele yao kila wakati. Tunaporuhusu ushirika wetu na MUNGU uvunjwe, ulinzi wetu unaondolewa kwetu. Madhumuni yako yote mazuri na nia njema havitakuwezesha kuhimili uovu. Lazima muwe wanaume na wanawake wa maombi. Maombi yako hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu kwa kushtukiza, au kutetereka (hapa na pale na siyo ya kudumu), bali yawe na bidii, ya kudumu, na ya mara kwa mara. Si lazima kila wakati upige magoti ili kuomba. Palilia tabia ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, unapotembea, na unapokuwa na shughuli nyingi katika kazi zako za kila siku. Hebu moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la kuomba msaada, kwa ajili nuru, nguvu, na maarifa. Hebu kila pumzi iwe sala. - (The Ministry of Healing, 510, 511) [Pr 76.2; Maombi Aya ya 23]

Omba kwa Imani Isiyotetereka – Omba, ndio, omba ukiwa na imani isiyoyumbayumba na amini. Malaika wa agano, yaani Bwana wetu Yesu Kristo, Ndiye Mpatanishi na Mwombezi anayesimamia kukubaliwa kwa maombi ya waamini Wake. - (Testimonies for the Church 8:179) [Pr 76.3; Maombi Aya ya 24]

Njoo kwa Ujasiri katika Maombi – Kwanini usisali kana kwamba una dhamiri isiyo na kosa (bila hatia), na kwamba unaweza kuja kwenye kiti cha neema kwa unyenyekevu, lakini kwa ujasiri mtakatifu, ukiinua mikono mitakatifu bila

ghadhabu na mashaka? Usisujudu na kufunika uso wako kana kwamba kulikuwa na kitu ambacho ulitamani kuficha; lakini inua macho yako kuelekea Patakatifu pa mbinguni, pale ambapo Kristo Mpatanishi wetu amesimama mbele za Baba kuwasilisha sala zetu, zilizochanganywa na wema na sifa Zake Mwenyewe na haki Yake isiyo na doa, kama ubani wa manukato. [Pr 76.4; Maombi Aya ya 25]

Wewe umealikwa kuja, kuomba, kutafuta, kubisha; na umehakikishiwa kuwa hautatoka mtupu/bure. Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.” Mathayo 7:7, 8.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 241, 242. [Pr 77.1; Maombi Aya ya 26])

Maombi ya bidii hupanda kama manukato yanayovuta usikivu— Wamevumilia kwa shida, ufukara na taabu kwa kudhamiria kwao, na wamekesha na kuomba ili kufanikiwa katika kazi ya Mungu. Zawadi zao na dhabihu zinaonyesha shukrani za dhati na sifa ya mioyo yao kwa Yeye ambaye amewaita kutoka gizani, ili waingie katika nuru Yake ya ajabu. Basi Hakuna manukato ya ushawishi mzuri zaidi yanayoweza kupaa mbinguni. Maombi yao na sadaka zao huja kama ukumbusho mbele za MUNGU. - (Selected Messages 2:212) [Pr 77.2; Maombi Aya ya 27]

Makerubi wawili wa kupendeza, mmoja kila upande wa Sanduku la Agano, walisimama na mabawa yao yakinyoshwa juu yake, na kugusana juu ya kichwa cha Yesu aliposimama mbele ya Kiti cha Rehema. Nyuso zao zilielekeana, na wakatazama chini kwenye sanduku, ikiwakilisha jeshi lote la malaika wakitazama kwa shauku sheria ya MUNGU. Kati ya makerubi kulikuwa na chetezo cha dhahabu, na kadiri maombi ya watakatifu, yalivyotolewa kwa imani, yalipomjia Yesu, Yeye aliyapeleka kwa Baba Yake, wingu la harufu ya manukato likapanda kutoka kwenye uvumba, likionekana kama moshi wa rangi nzuri zaidi. Juu ya mahali ambapo Yesu alisimama, mbele ya Sanduku la Agano, kulikuwa na utukufu wenye mng'ao mkali sana ambao sikuweza kuutazama; ilionekana kama kiti cha enzi cha MUNGU. Wakati uvumba ulipopanda kwenda kwa Baba, utukufu bora

ulimjia Yesu kutoka katika kiti cha enzi, na kutoka Kwake ulimwagwa juu ya wale ambao maombi yao yalikuwa yamekuja kama uvumba mtamu. Nuru ilimiminwa juu ya Yesu kwa wingi sana na kukigubika Kiti cha Rehema, na gari moshi la utukufu likajaza hekalu. Sikuweza kuangalia kwa muda mrefu ule mwangaza unaozidi kipimo. Hakuna lugha inayoweza kuelezea haya. Nilitekewa kwa kuzidiwa, hata kugeuka kutoka kwa Ukuu na utukufu wa tukio lile. - (Writings Early, 252) [Pr 77.3; Maombi Aya ya 28]

Twapaswa Kuiga Mfano wa Kristo wa Maombi yasiyokoma au kuchoka, yanayotegemea ahadi Zake— Nguvu ya Kristo ilikuwa katika maombi. Yeye Alichukua ubinadamu, na kuchukua madhaifu yetu na akawa dhambi kwa ajili yetu. Kristo alitoka kwenda mashambani, misituni au milimani huku akijitenga na ulimwengu na mambo mengine yote. Alikuwa peke yake na Baba Yake. Kwa bidii kubwa na unyofu, Yeye Alimimina maombi Yake, na kuelekeza nguvu Zake zote za roho Yake katika kushikilia mkono wa Yule asiye na mwisho. Wakati Majaribu mapya na makuu yalipokuwa mbele Zake, Yeye alichepuka kwa siri mahali penye utulivu milimani, Naye akiwa peke yake akatumia usiku mzima kwa ajili ya maombi kwa Baba Yake wa Mbinguni. [Pr 78.1; Maombi Aya ya 29]

Kwa kuwa Kristo ni mfano wetu katika mambo yote, nasi ikiwa tutaiga mfano Wake kwa bidii, wa kuwasilisha maombi yasiyochoka, ya dhati na **yenye** bidii kwa Mungu ili tuweze kuwa na nguvu katika Jina Lake, Yeye Ambaye hakujisalimisha kwa majaribu ya Shetani, na akazipinga hila za adui mjanja, vivyo hivyo nasi hatutatekewa naye adui huyu (sisi nasi hatutashindwa na Shetani). - (Mkufunzi wa Vijana, Aprili 1, 1873) [Pr 78.2; Maombi Aya ya 30]

Jitihada za kudumu na Maombi hututayarisha kwa ajili ya Majukumu ya Kila siku — Wale wanaomtafuta MUNGU kwa siri wakimwambia Bwana mahitaji yao na kuomba msaada, maombi yao hayataenda bure. "Baba yako aonaye kwa siri, Mwenyewe atakupa thawabu." Tunapomfanya Kristo kuwa Rafiki yetu wa kila siku, tutahisi kuwa nguvu za ulimwengu usioonekana zinatuzingira; na kwa kumtazama Yesu tutafanana na sura Yake. Kwa kumtazama Yeye, sisi tunabadilishwa. Tabia inalainishwa, inasafishwa, inatakaswa, na kuboreshwa kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Matokeo ya hakika ya muunganiko wetu na

ushirika na Bwana wetu yatakuwa ni kuongeza ucha MUNGU, usafi, utakaso, na shauku. Kutakuwa na kukua katika akili kwenye maombi yetu. Tunapata elimu ya Bwana, na hili linadhahirishwa katika maisha ya bidii, uadilifu, umakini na ari/usongo. [Pr 78.3; Maombi Aya ya 31]

Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada, uwezo, na sapoti kwa maombi ya dhati na bidii kila siku, itakuwa na matamano bora yanayoelekea juu, uelewa dhahiri wa Ukweli na wajibu, malengo ya juu katika utendaji, na kudumu katika njaa na kiu ya haki. Kwa kudumisha muunganiko na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine, nuru, amani, utulivu, utakaotawala mioyoni mwetu, kupitia ushirika wetu nao. Nguvu inayopatikana katika maombi kwa MUNGU, ikiwa pamoja na bidii ya kudumu katika kuifundisha akili na nia kwa makini na kujali, humuandaa mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na huweka roho katika amani kwenye hali zote. - (Thoughts from the Mount of Blessing, 85) [Pr 78.4; Maombi Aya ya 32]

Hakuna kinachopaswa Kutuchepusha sisi kutoka kwenye Mafunzo ya Biblia na Maombi ya bidii – Usiruhusu chochote, hata uwe unakipenda kwa jinsi gani, kunyonya akili yako na mapenzi yako, kukukengeusha ili usisome Neno la MUNGU au kuwa maombi ya dhati na bidii. Kesheni mkiomba. Ishi maombi yako mwenyewe. - (Testimonies for the Church 8:53) [Pr 79.1; Maombi Aya ya 33]

Ombi linaloshinda hujumuisha Imani katika ahadi za Mungu, kutokata tamaa na kutochoka – kipengele kingine cha ombi linaloshinda ni imani. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yupo, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." (Waebrania 11:6). Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24.— (Steps to Christ, 96) [Pr 79.2; Maombi Aya ya 34]

Imani ni kipengele muhimu katika maombi yanayoshinda. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yupo, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba

Yeye hutusikia, lolote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba." Waebrania 11: 6; 1 Yohana 5:14, 15. Tukiwa na imani ya kudumu na yenye uvumilivu kama ya Yakobo, na uvumilivu kwa kutokata tamaa kama Eliya, tunaweza kuwasilisha maombi yetu kwa Baba, tukidai yote ambayo ameahidi. Heshima ya kiti Chake cha enzi iko hatarini kwaajili ya utimilifu wa Neno Lake (Mungu anatimiza Neno Lake pia kulinda Jina Lake). - (Prophets and Kings, 157, 158) [Pr 79.3; Maombi Aya ya 35]

Maombi Yanatoa Ushuhuda wa ujasiri na Kumtumaini Kwetu MUNGU— Bwana anasema, "Niite Siku ya Taabu." Zaburi 50:15. Yeye Anaturalika kumpa shida zetu na mahitaji yetu, na hitaji letu la msaada Wake Bwana. Yeye anatuamuru tuwe tayari kuomba wakati wowote-tuwe na utayari kuomba muda wowote. Mara tu shida zinapotokea, tunapaswa kumpa Yeye maombi yetu ya dhati, na ya bidii. Kwa maombi yetu ya kujitoa tunatoa ushahidi wa ujasiri na imani yetu kubwa kwa MUNGU. Hisia ya hitaji letu inatuongoza kuomba kwa bidii, na Baba yetu wa mbinguni anaguswa na sala zetu.- (Christ Object Lessons, 172) [Pr 79.4; Maombi Aya ya 36]

MUNGU Hujibu Maombi ya Dhati — Ni pale tu tunapoomba kwa maombi ya dhati, kusadiki, ndipo MUNGU atatupatia haja za mioyo yetu. - (Gospel Workers, 255) [Pr 80.1; Maombi Aya ya 37]

Baada ya Kuomba, Endelea Kudai Ahadi -Baada ya maombi kufanywa, ikiwa jibu halitaonekana mara moja, usichoke kungojea na ukatikisika. Usitetereke kwa mashaka. Ng'ang'ania ahadi, "Yeye ni mwaminifu ambaye Awaita, Naye Atatenda" Kama mjane aliyekazana kwa bidii hata kumuudhi yule jaji, wewe pia sisitiza kwa bidii hoja/shauri lako, ukiwa thabiti katika kusudi lako. Je! Kitu hicho unachoomba ni muhimu na chenye matokeo makubwa kwako? Hakika ni hivyo. Basi usitetereke, kwani imani yako inaweza kujaribiwa. Ikiwa kitu unachotamani ni cha thamani, basi kinastahili juhudi nzito, na yenye bidii. Wewe una ahadi; kesho na uombe. Simama imara na sala yako itajibiwa; Je, sio Mungu Ndiye ambaye ameahidi? Ikiwa inakugharimu kukipata basi utakipa thamani zaidi wakati kitakapopatikana. Unaambiwa waziwazi kwamba ikiwa utayumbayumba kwa mashaka, basi haupaswi

kufikiria kwamba utapokea chochote kutoka kwa Bwana. Tahadhari imetolewa hapa kwamba usichoke, bali utulie tuli katika kwenye ahadi. Ukiomba, Naye atakupa kwa ukarimu na wala hakemei. - (Testimonies for the Church 2:131) [Pr 80.2; Maombi Aya ya 38]

MUNGU hatatuambia tuondoke au kutufukuza tukiwa watupu (bila chochote)— Wakati majaribu na mitihani ya maisha inapotuvamia, hebu tumwendee MUNGU na kumlilia katika maombi. Yeye hatatuambia tuondoke mikono mitupu, lakini atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui. -(Early Writings, 46) [Pr 80.3; Maombi Aya ya 39]

Maombi Bila Imani iliyo Hai hayana manufaa yoyote - Imani sio hisia. “imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana” Waebrania 11:1. Imani ya Kweli haina uhusiano wowote na dhana potofu ya imani bandia, au ujasiri wenye kiburi. Ni yeye tu aliye na imani ya Kweli, ndiye aliye salama dhidi ya mawazo potofu ambayo yanachukuliwa kuwa kweli kwa msingi wa uwezekano, na kuwa shupavu, kiasi cha kutozingatia mapenzi ya Mungu, na kuwa na imani bandia (presumption), yaani kujiamini kupita kiasi bila kuzingatia Neno la Mungu, imani bandia, kiburi, kwani dhana hii potofu ni udanganyifu na mbadala wa Shetani wa imani. [Pr 80.4; Maombi Aya ya 40]

Imani hudai ahadi za MUNGU na huzaa matunda ya utii. Dhana potofu, yaani imani bandia pia, hudai ahadi hizo, lakini huzitumia kama Shetani alivyofanya, ili kutetea dhambi/makosa. Imani ingewaongoza wazazi wetu wa kwanza kuamini upendo wa MUNGU na kuzitii amri Zake. Dhana potofu yenye imani bandia, isiyotii mapenzi na Neno la Mungu, iliwaongoza kuvunja sheria Yake, wakiamini kwamba upendo Wake mkuu ungewaokoa kutoka kwenye matokeo ya dhambi zao. Imani haidai upendeleo wa Mbingu bila kufuata masharti ambayo kwayo rehema inapaswa kutolewa. Imani ya kweli ina msingi wake katika ahadi na mpango wa Maandiko. [Pr 80.5; Maombi Aya ya 41]

Kuzungumza juu ya dini kwa namna ya kawaida, kuomba bila njaa ya roho na imani hai, havina faida yoyote. Imani ya Jina tu kwa Kristo, ambayo inampokea Yeye kama Mwokozi wa ulimwengu tu, haiwezi kuleta uponyaji rohani.

Imani inayohusu wokovu sio kukubaliana na ile Kweli kwa akili tu. Yeye ambaye anasubiri maarifa kamili kabla ya kutumia imani, hawezi kupokea baraka kutoka kwa MUNGU. [Pr 81.1; Maombi Aya ya 42]

Haitoshi kuamini kuhusu Kristo; lazima tumwamini Yeye. Imani pekee itakayotunufaisha ni ile inayomkubali Yeye kama Mwokozi wetu binafsi; ambayo inaweka sifa Zake kwetu sisi binafsi. Wengi wanashikilia imani kama maoni. Lakini imani inayookoa ni muamala/dili, ambayo wale wanaompokea Kristo hujiunga katika uhusiano wa agano na MUNGU. Imani ya Kweli ni uzima. Imani hai inamaanisha kuongezeka kwa nguvu, uthabiti wa imani, ambavyo kwa hivyo roho inakuwa uwezo wa ushindi. - (Gospel Workers, 260, 261) [Pr 81.2; Maombi Aya ya 43]

Ombi litashinda Dhidi ya Shetani – Maombi ya imani ni nguvu kubwa ya Mkristo na hakika yatamshinda Shetani. Hii ndiyo sababu yeye anasisitiza kwamba hatuna haja ya maombi/kuomba. Jina la Yesu, Wakili wetu; Ibilisi analichukia na tunapomwendea kwa dhati kwa ajili ya msaada, Jeshi la Shetani linashtushwa kwa hofu. Kusudi lake linatimizwa vizuri pale tunapopuuza mazoea ya kuomba (tabia ya kuomba), kwa kuwa maajabu yake ya uwongo yanapokelewa kwa urahisi zaidi. - (Testimonies for the Church 1:296) [Pr 81.3; Maombi Aya ya 44]

Maombi Huleta Ushindi Mkubwa Zaidi – Ushindi mkubwa uliopatikana kwa sababu ya MUNGU sio matokeo ya uhodari wa kuleta hoja zetu kwa juhudi, au kuwa na vifaa au miundo mbinu ya kutosha, ushawishi mpana, au mali nyingi; bali hupatikana katika chumba cha hadhira na MUNGU, wakati kwa imani ya dhati na bidii, na yenye uchungu, wanadamu wanaushikilia Mkono mkuu wenye nguvu. - (Gospel Workers, 259) [Pr 81.4; Maombi Aya ya 45]

SURA YA 9

NGUVU YA MAOMBI

Maombi huongeza nguvu za Kiroho— Wale wanaomtafuta MUNGU kwa siri wakimwambia Bwana mahitaji yao na kuomba msaada, hawataomba au kutoka bure. "Baba yako aonaye kwa siri Mwenyewe atawapa thawabu." waziwazi. Tunapomfanya Kristo kuwa Mwenzi wetu wa kila siku tutahisi kuwa nguvu za ulimwengu usioonekana zinatuzunguka; na kwa kumtazama Yesu tutafanana na Naye (tutafanana na Sura Yake). Kwa kumtazama tunabadilishwa. Tabia inalainishwa, inasafishwa, na kuboreshwa kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Matokeo ya hakika ya muunganiko wa ushirika na Bwana wetu yatakuwa ni kuongeza ucha MUNGU, usafi wa moyo, na ari/usongo. Kutakuwa na kukua akili kuhusiana na maombi. Tunapata elimu ya Mbingu, na hili linadhihirishwa katika maisha ya uadilifu na ari. [Pr 82.1; Maombi Aya ya 1]

Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada (sapoti), na uwezo kwa maombi ya dhati na bidii ya kila siku, itakuwa na matamanio bora, uelewa dhahiri wa

ile Kweli na wajibu, malengo makuu, yaliyo juu zaidi katika utendaji kazi, na itadumu kuwa na njaa na kiu ya haki. Kwa kudumisha muungano na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine kupitia ushirika wetu nao, nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni mwetu. Nguvu inayopatikana katika maombi kwa MUNGU, ikiunganishwa na bidii ya kudumu katika kuifundisha akili kwa makini na kujali, huandaa mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na huweka roho katika amani chini ya hali zote. -(Thoughts from the Mount of Blessing, 85) [Pr 82.2; Maombi Aya ya 2]

Nguvu na neema zinaweza kupatikana katika maombi. Upendo wa dhati unapaswa kuwa kanuni inayotawala moyo. - (The Adventist Home, 127) [Pr 83.1; Maombi Aya ya 3]

Itoe wakfu akili yako kwa ajili ya mambo ya kiroho-akili ikite kwenye mambo ya kiroho. Epusha akili yako na mazoea ya kujitegemea mwenyewe. Palilia na kukuza roho ya kuridhika, yenye uchangamfu. Unazungumza sana juu ya vitu visivyo vya muhimu. Haupati nguvu ya kiroho kutoka katika hayo. Ikiwa nguvu ulizotumia katika kuongea zingetumika katika maombi, ungepokea nguvu za kiroho na ungemuimbia wimbo MUNGU moyoni mwako. - (Testimonies for the Church 2: 434, 435) [Pr 83.2; Maombi Aya ya 4]

Baraka kuu ambayo MUNGU anaweza kumpa mwanadamu ni roho ya maombi ya dhati. Mbingu zote zimefunguliwa mbele ya mtu wa maombi/ Mabalazi wa Kristo watakuwa na nguvu kwa watu baada ya wao, kwa sala ya dhati, kuja mbele za MUNGU. - (The Review and Herald, Oktoba 20, 1896) [Pr 83.3; Maombi Aya ya 5]

Hatuthamini Nguvu ya Maombi Kama Tunavyopaswa – Hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi kama tunavyopaswa. Maombi na imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu yoyote duniani inaweza kutimiza. Ni kwa nadra sana katika kila kipengele na hali, sisi tunawekwa katika nafasi ile ile mara mbili. Daima tunakutana na matukio mapya, madhari mpya na majaribio mapya ya kuyashinda, ambapo uzoefu wa zamani hauwezi kuwa mwongozo tosha, katika kusaidia. Lazima tuwe na nuru isiyokoma kutoka kwa MUNGU.- (The Ministry of Healing, 509) [Pr 83.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi Hutuweka Katika Nguvu za MUNGU— Nguvu tunayopata katika maombi kwa MUNGU itatutayarisha kwa ajili ya majukumu yetu ya kila siku. Majaribu ambayo tunaanikwa kwayo katika mazingira ya kila siku hufanya maombi kuwa jambo la lazima. Ili tuweze kulindwa na uweza wa MUNGU kwa njia ya imani, shauku za akili yapaswa kuelekezwa mbinguni daima katika maombi ya siri Wakati tunazungukwa na vishawishi vilifanyiwa mahesabu kutupeleka mbali na MUNGU, maombi yetu ili kupata msaada na nguvu yanapaswa yasichoke. Tofauti na hapo, hatutafanikiwa kamwe katika kuvunja kiburi na kushinda nguvu ya majaribu dhidi ya tamaa za dhambi ambazo hutuweka mbali na Mwokozi. Nuru ya ile Kweli, inayotakasa na kusafisha maisha, itagundua kwa mpokeaji tamaa za dhambi za moyo wake, ambazo zinapigana vita kutawala, na ambazo hufanya iwe muhimu kwake huyu mtu, kutumia akili yote kunyumbulisha na kushinikiza kila nguvu ili kumpinga Shetani ili aweze kuwa mshindi kupitia sifa za Kristo. - (Messages to Young People, 248) [Pr 83.5; Maombi Aya ya 7]

Nguvu ya Mungu Huwangojea Wale Wanaoitaka- Unaweza kuwa na hisia ya kina na ya kudumu ya vitu vya milele na ule upendo kwa wanadamu ambao Kristo ameonyesha katika maisha Yake. Muunganiko wa karibu na mbingu utatoa toni sahihi kwa uadilifu wako na utakuwa msingi wa mafanikio yako. Hisia zako kwamba wewe ni mhitaji na tegemezi zitakusukuma kwenye maombi, na akili yako ya kuzaliwa itakuwajibisha kuwa na bidii. Maombi na bidii, bidii na maombi, vitakuwa shughuli ya maisha yako. Lazima uombe kana kwamba ufanisi na sifa zote zinatokana na MUNGU tu, na kisha ufanye kazi kwa juhudi kubwa kana kwamba jukumu lote ni lako mwenyewe. Ukitaka nguvu unaweza kuwa nazo; inasubiri rasimu yako tu ili uwe nazo (nguvu zinangoja wewe ni kuziagiza kuja kwako). Mwamini tu MUNGU, Mchukue kwa Neno Lake- kama Yeye alivyosema, tenda kwa imani, na baraka zitakuja. -(Testimonies for the Church 4:538, 539) [Pr 84.1; Maombi Aya ya 8]

Hata Ombi Fupi laweza Kuleta Nguvu za Kiroho - "Niliomba," alisema [Nehemia], "kwa MUNGU wa mbinguni." Katika sala hiyo fupi Nehemia alisisitiza mbele ya Mfalme wa wafalme na kushinda nguvu inayoweza kugeuza mioyo

kama mito ya maji inavyoweza kugeuzwa. [Pr 84.2; Maombi Aya ya 9]

Kuomba kama vile Nehemia alivyoomba katika saa yake ya uhitaji ni nyenzo iliyo chini ya uwezo na amri ya Mkristo chini ya hali wakati aina nyingine za maombi zinaweza kuwa haziwekani.— (Prophets and Kings, 631) [Pr 84.3; Maombi Aya ya 10]

Ombi ni siri ya nguvu ya kiroho-Maombi ni pumzi ya roho. Ni siri ya nguvu ya kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na kisha afya ya roho ikatunzwa salama. Ombi huupatia moyo mawasiliano ya karibu kabisa na Chemchemi ya uhai/uzima, na kuimarisha mshipa na misuli ya uzoefu wa kidini. Puuzia zoezi la sala, au jihusishe na maombi hapa na pale kwa kushtukiza, yaani pale unapojisikia kwamba itakuwa mtelemko kwako, au jinsi unavyojisikia, nawe utapoteza ukaribu wako kwa MUNGU. Vitivo vya kiroho hupoteza nguvu, uzoefu wa kidini hupungukiwa afya na nguvu. - (Messages to Young People, 249, 250) [Pr 84.4; Maombi Aya ya 11]

Maombi Huleta Nguvu Kutoka kwa MUNGU- Nguvu zitatoka kwa MUNGU kwenda kwa mwanadamu kujibu maombi ya imani. - (Testimonies for the Church 4:402) [Pr 85.1; Maombi Aya ya 12]

Maombi Huleta Mafanikio katika pambano dhidi ya Dhambi - Maombi ni njia ya mafanikio iliyowekwa na mbingu katika vita na dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo. Ushawishi wa Bwana unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwa kupata Roho Mtakatifu, kwa uimara kama wa Kristo, kwa hulka kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo Yeye ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea." (Matendo 1:8). The Acts of the Apostles, 564 au Matendo ya Mitume [Pr 85.2; Maombi Aya ya 13]

Maombi Hushikilia Nguvu isiyo na Ukomo - Imani ya Kweli na ombi la Kweli— Vina nguvu kubwa kwa kiasi gani! Ni kama mikono miwili ambayo mwombaji wa kibinadamu hutegemea na kushikilia nguvu ya Upendo usio na mwisho. - (Gospel Workers, 259) [Pr 85.3; Maombi Aya ya 14]

Maombi Hutuimarisha Dhidi ya Majaribu ya Shetani – Shetani huwasilisha majaribu mengi kwa vijana. Anacheza mchezo wa maisha kwa ajili ya roho zao, na haachi hata njia moja ya kuwavutia waje kwake na kisha awaharibu (hutumia njia zote zilizopo kuwashawishi waje kwake kwa game of life). Lakini MUNGU hawaachi wapambane bila msaada dhidi ya mshawishi. Binadamu wana Msaidizi Mwenye nguvu zinazopita nguvu za adui, Yeye ambaye aliishi katika ulimwengu huu na katika maumbile ya kibinadamu alikutana na Shetani na kumshinda, Yeye anasukumilia mbali na kupinga kila jaribu linalowapata vijana leo. Yeye ni Kaka/Ndugu Yao mkubwa. Ana shauku huruma nyororo na ya kina kwao. Yeye Anaweka juu yao uangalizi wa kila wakati, na anafurahi wanapojaribu kumpendeza. Wanapoomba, Yeye huchanganya maombi yao na uvumba wa haki Yake, na kuyawasilisha kwa MUNGU kama dhabihu yenye manukato mazuri. Kwa nguvu Zake vijana wanaweza kuvumilia ugumu kama askari wazuri wa msalaba. Wakiwa wameimarishwa na nguvu Zake, wamewezeshwa kufikia malengo ya juu yaliyoko mbele yao (wanaweza kabisa kuyafikia). Dhabihu iliyotolewa juu ya Kalvari ni ahadi ya ushindi wao. -(Messages to Young People, 95, 96) [Pr 85.4; Maombi Aya ya 15]

Maombi Yetu Hukifikia Kiti cha Enzi cha MUNGU– Kwa maombi yako ya dhati, ya bidii na imani, unaweza kuusogeza Mkono unaoendesha/unaousogeza ulimwengu. Unaweza kuwafundisha watoto wako kuomba kwa ufanisi wanapopiga magoti kando yako. Acha maombi yako yaende kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, "Uwasamehe watu Wako, Ee Bwana, wala usiwape urithi Wako wakoaji, ili mataifa wasiwatawale; wasije kusema miongoni mwao, Yuko wapi MUNGU wao?" [Pr 86.1; Maombi Aya ya 16]

MUNGU Yuko kazini. Yeye hufanya maajabu, na ingawa Yuko juu na ameinuliwa juu na kutukuka, maombi yanaweza kufikikia kiti Chake cha enzi. Yeye anayegeuza-geuza na kupindua-pindua, Yeye anayeweza kufanya mambo ya ajabu, atasikia na kuzingatia maombi ya toba ya imani kutoka kwa watoto Wake wanyenyekevu. - (The Review and Herald, Aprili 23, 1889) [Pr 86.2; Maombi Aya ya 17]

Sauti Zetu Hulifikia Sikio La MUNGU– Neno ambalo lilisemwa kwa Yesu huko Yordani, "Huyu ni Mwanangu

mpendwa, ambaye nimependezwa Naye," linaukumbatia ubinadamu wote. MUNGU alizungumza na Yesu kama Mwakilishi wetu. Pamoja na dhambi zetu zote na udhaifu, hatutelekezwi kama watu wasio na thamani. "Yeye Ametufanya tukubalike katika "Mpendwa." Waefeso 1: 6. Utukufu ambao ulikaa juu ya Kristo ni ahadi ya Mungu ya upendo kwetu sisi. Unatuambia juu ya nguvu ya maombi, - jinsi sauti ya mwanadamu inavyoweza kufikia sikio la MUNGU, na maombi yetu yanapata kukubalika katika kumbi za mbinguni. Kwaajili ya dhambi, dunia ilikatiliwa mbali kutoka mbinguni, na kutengwa na ushirika wa mbingu; lakini Yesu ameiunganisha dunia tena na duru ya utukufu. Upendo Wake umemzunguka mwanadamu, na umefikia mbingu ya juu zaidi. Nuru ambayo ilianguka kutoka kwenye milango wazi juu ya kichwa cha Mwokozi wetu itatuangukia tunapoomba msaada wa kupinga majaribu. Sauti ambayo ilizungumza na Yesu inamwambia kila mtu anayeamini, Huyu ni mwanangu/mtoto Wangu mpendwa, ambaye nimependezwa Naye. - (The Desire of Ages, 113) [Pr 86.3; Maombi Aya ya 18]

Tunahitaji Kupigana mieleka na MUNGU katika Maombi – Je! Tutaendeleza kazi katika njia ya Bwana? Je! Tuko tayari kufundishwa na MUNGU? Je! Tutapigana mieleka na MUNGU katika maombi? Je! Tutapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hii ndio tunayohitaji na tunaweza kuwa nayo wakati huu. Ndipo tutakapokwenda na ujumbe kutoka kwa Bwana, na nuru ya ile Kweli itang'aa kama taa inayowaka, huku ikifika sehemu zote za ulimwengu. Ikiwa tutatembea kwa unyenyekevu na MUNGU, Mungu atatembea nasi. Hebu na tunyenyekeze roho zetu, na tutaona wokovu Wake. - (The Review and Herald, Julai 1, 1909) [Pr 87.1; Maombi Aya ya 19]

Ushindi Mkubwa Zaidi hupatikana kupitia Maombi ya Dhati na bidii – Ayubu alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na aliyeazimia. Uzoefu wake unathibitisha nguvu ya maombi ya kudiriki na yasiyochoka. Ni wakati huu ndio ambao tunapaswa kujifunza somo hili la maombi yanayoshinda, yasiyochoka, na yenye imani isiyokubali kushindwa, inayongoja matokeo kwa uvumilivu. Ushindi mkubwa kwa kanisa la Kristo au kwa Mkristo mmoja mmoja, sio ule unaopatikana kwa talanta, kisomo, elimu, utajiri, au upendeleo wa watu. Bali ni ushindi ule ambao

hupatikana katika chumba cha hadhira na MUNGU ambaye ni Mfalme, wakati imani yenye unyofu, bidii, na uchungu moyoni, inategemea na kuushika Mkono wa Mungu Mkuu Mwenye nguvu. [Pr 87.2; Maombi Aya ya 20]

Wale ambao hawataki kuacha kila dhambi na kutafuta kwa bidii baraka ya MUNGU, hawataipata. Lakini wote watakaoshika ahadi za MUNGU kama alivyofanya Yakobo, na kuwa na bidii, unyofu, na uvumilivu kama yeye, watafaulu kama alivyofaulu. - (Patriarchs and Prophets, 203) [Pr 87.3; Maombi Aya ya 21]

Sifa na Shukrani huleta Nguvu kwenye Maombi yetu – Je! Mazoezi yetu yote ya ibada yote ni lazima yawe katika kuomba na kupewa au kupokea tu? Je! Daima sisi tufikirie mahitaji yetu tu bila hata ya kufikiria faida/manufaa ambayo tumeyapokea tayari? Je! Tutakuwa wapokeaji wa rehema Zake tu na kamwe tusiwe wenye roho ya shukrani, na kumsifu kwa kile ambacho Yeye Mungu ametutendea? Sisi huwa hatuna maombi mengi (wala hatuombi sana), ila shukurani zetu ni chache mno. Ikiwa upendo wa MUNGU utaleta shukrani zaidi na sifa, tutakuwa na nguvu zaidi katika maombi. Sisi tungefungamana zaidi katika upendo wa MUNGU na kupata kitu kitakatochotusaidia kumtukuza. Wewe ambaye unalalamika kwamba MUNGU hasikii maombi yako, badilisha utaratibu wako wa sasa na uchanganye sifa katika maombi yako. Unapozingatia wema na rehema Zake utagundua kuwa atazingatia matakwa yako. [Pr 87.4; Maombi Aya ya 22]

Omba, omba kwa dhati na bidii na bila kukoma, lakini usisahau kumsifu Mungu (Kusifu). - (Testimonies for the Church 5:317) [Pr 88.1; Maombi Aya ya 23]

Nguvu ya Maombi Huleta Matunda katika Kazi Yetu kwa MUNGU— Wale walio katika giza la makosa ni ununuzi uliopatikana kwa gharama ya damu ya Kristo. Wao ni matunda ya mateso Yake, na wanapaswa kufanyiwa kazi. Hebu wainjilisti wa vitabu wajue kwamba wanafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kuendeleza ufalme wa Kristo. Wanapoendelea na kazi waliyopewa na MUNGU, Yeye atawafundisha kwenda kuuonya ulimwengu juu ya hukumu inayokuja hivi karibuni. Ikiandamana pamoja na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, na nguvu ya upendo wa MUNGU, kazi ya mwinjilisti wala haitakuwa, na haiwezi

kuwa bila matunda. Fikiria ni kiasi gani Baba na Mwana wanaijali na kuionea shauku kazi hii. Kama vile Baba ampendavyo Mwana, vivyo hivyo na Mwana huwapenda walio Wake--wale wanaofanya kazi hii, kama Yeye Alivyofanya kazi ili kuokoa roho zinazoangamia. Hakuna anayehitaji kuhisi kuwa hana nguvu: kwa maana Kristo anatangaza, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." Naye Ameahidi kwamba atawapa nguvu hii watendakazi Wake. Nguvu Zake zitakuwa nguvu zao.- (Colporteur Ministry, 108) [Pr 88.2; Maombi Aya ya 24]

Shetani Hawezi Kumshinda Mtu Wa Maombi (Mtu anayesali) - Adui hawezi kumshinda mwanafunzi mnyenyekevu wa Kristo, yule ambaye anatembea kwa maombi mbele za Bwana. Kristo anaingilia kati Mwenyewe kama mlinzi/kivuli, kimbilio, dhidi ya mashambulio ya yule mwovu. Ahadi imetolewa, "Wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua viwango dhidi yake." ... Hakuna nguvu katika misukumo yote ya kishetani ambazo zinaweza kulemaza roho inayotegemea, kwa ujasiri yakinifu na sahili, katika hekima inayotoka kwa MUNGU. - (My Life Today, 316) [Pr 88.3; Maombi Aya ya 25]

Maombi Huleta Nguvu za kupinga Jaribu -Tusipoomba bila kukoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuzembea zaidi, na kuchepuka kutoka katika njia sahihi. Kila wakati adui anatafuta kuziba njia iendayo kwenye Kiti cha Rehema, ili tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu kwa ombi la dhati na imani. - (Steps to Christ, 93, 94) [Pr 89.1; Maombi Aya ya 26]

Kupuuzia Maombi na Kujifunza Biblia Kunatufanya Tuwe katika hatari ya kuingia majaribuni- Majaribu mara nyingi huonekana kuwa hayazuiliki/hayapingiki kwa sababu, kupitia kupuuzia maombi na kusoma Biblia, mtu anayejaribiwa hawezi kukumbuka ahadi za MUNGU kwa haraka na kumkabili Shetani kwa silaha za Maandiko. Lakini malaika wanawazunguka wale ambao wako tayari kufundishwa au kufundishika katika mambo ya Mbingu/Kiungu; na wakati wa uhitaji mkubwa, watawakumbusha Kweli zile ambazo zinahitajika. - (The Great Controversy, 600) [Pr 89.2; Maombi Aya ya 27]

Shetani anaogopa kwa kutetemeka tukiwa tunaomba - Kuna nguvu kubwa katika maombi. Adui yetu mkuu anatafuta kila mara kuiweka roho inayofadhaika mbali na MUNGU. Ombi la mtakatifu mnyenyekevu, linapoenda Mbinguni, linaogopwa na Shetani (linampa homa au fadhaa), na linampa kutetemeka na hofu, kuliko amri za mabaraza au maagizo ya wafalme. - (In Heavenly Places, 82) [Pr 89.3; Maombi Aya ya 28]

Chanzo cha Nguvu katika nyakati za Matengenezo ya kanisa kilikuwa ni Maombi - Kutoka mahali pa siri pa maombi kulikuja nguvu ambayo ilitikisa ulimwengu katika Matengenezo Makubwa. Hapo, kwa utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana waliweka miguu yao juu ya mwamba wa ahadi Zake. Wakati wa mapambano huko mji wa Augsburg, Luther "hakupitisha siku bila kutenga angalau masaa matatu kwaajili ya maombi, na haya yalikuwa masaa yaliyochaguliwa katika yale masaa bora ya kujisomea/kujifunza." Katika faragha ya chumba chake alisikika akimimina roho yake mbele za MUNGU kwa maneno "yaliyojaa ibada ya sifa, kicho, hofu, na matumaini, kama vile ambavyo mtu anapozungumza na rafiki yake." (The Great Controversy, 210) [Pr 89.4; Maombi Aya ya 29]

SURA YA 10

SABABU ZA KUOMBA

Huangazia Akili ijue Ukweli Ni Nini – Je, ni kwanini hatupokei zaidi kutoka Kwake ambaye Ndiye chanzo cha nuru na nguvu? Ni kwa vile "Tunatarajia kidogo sana." Je! MUNGU amepoteza upendo Wake kwa mwanadamu? Je! Upendo Wake hauendelei tena kububujika hapa chini duniani? Je, Yeye Amepoteza shauku Yake ya kujionyesha Mwenye nguvu kwa niaba ya watu Wake? (2Mambo ya

Nyakati 16;9). Kristo atatupa ushindi katika vita. Ni nani anayeweza kutilia shaka hili wakati tunajua kwamba Yeye aliweka kando vazi Lake na taji Yake ya kifalme, kisha akaja ulimwenguni kwa vazi la ubinadamu, ili asimame kama mbadala na mdhamini wa mwanadamu? [Pr 90.1; Maombi Aya ya 1]

Hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi kama tunavyopaswa. "Roho Naye hutusaidia udhaifu wetu; kwa maana hatujui kuomba kama itupasavyo; lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kwingi, yaani uchungu mkubwa usioelezeka." MUNGU anatutaka tuje Kwake katika maombi, ili aziangazie akili zetu. Yeye peke yake Ndiye anayeweza kutupa dhana wazi za Ukweli. Yeye peke yake Ndiye anayeweza kulainisha na kutiisha moyo. Yeye Anaweza kutuhuisha ili kuharakisha uelewa wa kutambua Ukweli dhidi ya uwongo. Yeye Anaweza kuiweka kwenye msingi mwema akili inayotetereka, na kuipatia maarifa na imani ambayo itavumilia mtihani. Omba basi; omba bila kukoma. Bwana aliyesikia maombi ya Danieli, atasikia yako pia ikiwa utamwendea kama Danieli alivyofanya. - (The Review and Herald, Machi 24, 1904) [Pr 90.2; Maombi Aya ya 2]

Yanatutambulisha kwa Baba – Oh jamani, Je sisi tunamjua MUNGU jinsi tunavyopaswa kumjua? Ni faraja iliyoje, furaha iliyoje, tunayopaswa kuwa nayo ikiwa tungejifunza kila siku masomo ambayo Yeye anataka tujifunze! Lazima tumjue Yeye kwa ujuzi wa vitendo. Itakuwa faida kwetu kutumia muda mwingi katika maombi ya siri, ili tuelekee kwenye safari ya kumjua binafsi, Baba yetu wa mbinguni. - (Medical Ministry, 102) [Pr 91.1; Maombi Aya ya 3]

Hutuunganisha sisi kwa sisi na sisi na MUNGU- Maombi yanatuunganisha sisi kwa sisi na MUNGU. Maombi humleta Yesu upande wetu, na huipa roho iliyozimia, na kufadhaika nguvu mpya ya kuushinda ulimwengu, mwili, na Shetani. Maombi huyaweka kando mashambulio ya Shetani. - (Christ's Object Lessons, 250) [Pr 91.2; Maombi Aya ya 4]

Hutusaidia kupinga majaribu- Hivi ni kwanini wana na binti za MUNGU wanasitasita kuomba, wakati maombi ni ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua hazina/ghala la mbinguni, mahali ambako zimetunzwa hazina tele za

Mweza wa Yote? - (Steps to Christ, 94) Bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa bidii na uadilifu, tuko katika hatari ya kuzembea zaidi, na kupotoka/kuchepuka kutoka kwenye njia sahihi. Daima adui anatafuta kufunga njia ya kuelekea kwenye Kiti cha Rrehema, ili kwa dua ya dhati na imani tusiweze kupata neema na nguvu ya kupinga majaribu. - (Steps to Christ, 93, 94) [Pr 91.3; Maombi Aya ya 5]

Kristo Ndiye tumaini letu pekee. Njoo kwa MUNGU kwa Jina la Yeye Yule aliyetoa uhai Wake kwa ajili ya uhai/uzima wa ulimwengu. Itumainie dhabihu ya ufanisi Wake. Onyesha kwamba upendo Wake, furaha Yake, imo ndani ya roho yako, na kwa sababu ya hili, furaha yako imesheheni na ni kamili. MUNGU Ndiye Nguvu zetu. Omba sana/mno. Maombi ni uhai wa roho. Maombi ya imani ni silaha ambayo kwayo tunaweza kufanikiwa kwa ukamilifu kupinga kila shambulio la adui. - (Selected Messages 1:88) [Pr 91.4; Maombi Aya ya 6]

Hutuandaa kwa ajili ya Ushirika katika Kanisa la Huko juu – Kwa ile roho nyenyekevu, na inayoamini, nyumba ya MUNGU duniani ni lango la mbinguni. Wimbo wa Kumsifu Mungu, Sala, na maneno yaliyonenwa na wawakilishi wa Kristo, ni wakala ulioteuliwa na MUNGU kwaajili ya kuwaandaa watu kwa ajili ya kanisa lililo juu, kwa ajili ibada hiyo iliyotukuka juu zaidi ambako chochote kilicho najisi/kichafu kamwe hakiwezi kuingia. - (Testimonies for the Church 5:491) [Pr 91.5; Maombi Aya ya 7]

Huimarisha Usadikisho wetu- Kila siku Usadikisho wetu unahitaji kuimarishwa kwa ombi la unyenyekevu, ombi la dhati na kusoma Neno. Ingawa kila mmoja ana upekee wake, na ijapokuwa kila mmoja wetu anapaswa kushikilia usadikisho yaani imani yake kwa uthabiti, lazima sote tuishike kama Kweli ya MUNGU na katika nguvu ambayo MUNGU Mwenyewe hutoa, tusipofanya hivyo, zitakamuliwa kwa ujeuri ili zitoke nje ya ufahamu wetu. - (Testimonies for the Church 6:401) nje ya ufahamu wetu. [Pr 92.1; Maombi Aya ya 8]

Hutupa/Hutoa Mahitaji ya Muda – Kila ahadi katika Neno la MUNGU huja kwetu na mada ya kuombea, ikileta Neno la Yehova lililoahidiwa kama dhamana/uhakikisho wetu. haijalishi Baraka yoyote ya kiroho tunayoihitaji, sisi

tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa usahili na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa (tubainishe). Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi, ya hapa duniani, tukimwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na Vazi la haki ya Kristo. Baba yetu wa mbinguni anajua kuwa tunahitaji vitu hivi vyote, na sisi tumealikwa kumuomba juu ya vyote. Ni kupitia kwa Jina la Yesu ndiyo kila neema hupokelewa/hutolewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake. –(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 92.2; Maombi Aya ya 9]

Kila nafsi ina upendeleo/fursa ya kumwambia Bwana mahitaji yake maalum na kuleta shukrani zake binafsi kwa baraka ambazo hupokea kila siku. - (Testimonies for the Church 9:278, 279) [Pr 92.3; Maombi Aya ya 10]

Hayatoi Habari Mpya kwa MUNGU- Maombi au Sala havieleweki kama inavyopaswa kueleweka. Kusali sio kumpasha MUNGU habari ambazo Yeye hazijui. Bwana anazifahamu fika siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti ya juu (kubwa). MUNGU anasoma mawazo yaliyofichika ndani. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona sirini atasikia, na atatupatia thawabu hadharani. - (Messages to Young People, 247) [Pr 92.4; Maombi Aya ya 11]

Uwepo wa Neema ya kila siku Umetolewa— Wale ambao wakati wa Pentekoste walivikwa na uwezo kutoka juu, hawakuepushwa au kuwa huru dhidi ya majaribu na mitihani inayokuja mbeleni. Waliposhuhudia Ukweli na haki, walishambuliwa mara kwa mara na adui wa ile Kweli Yote, ambaye alitaka kuuteka ujuzi na uzoefu wao wa Kikristo. Walilazimika kuweka jitihada kwa nguvu zao zote walizopewa na MUNGU ili kufikia kimo cha mfano wa wanaume na wanawake walio katika Kristo Yesu. Kila siku waliomba msaada wa ugavi mpya wa neema, ili waweze kufika juu zaidi na kwenda juu zaidi tena kuelekea kwenye ukamilifu. Chini ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu, hata yule aliye dhaifu sana, kwa kuizoesha na kuitumia imani kwa MUNGU, alijifunza kuboresha uwezo aliokabidhiwa na kutakaswa, kusafishwa, na kuboreshwa/kuheshimishwa. Kwa unyenyekevu walitii ushawishi wa Roho Mtakatifu, wakapokea utimilifu wa Uungu na

wakaumbwa/wakafinyangwa kwa mfano wa MUNGU. - (The Acts of the Apostles, 49, 50) [Pr 92.5; Maombi Aya ya 12]

Hekima inatolewa - Lazima tutafute hekima kutoka juu ili tuweze kusimama katika siku hii ya leo ya makosa, upotofu na udanganyifu. - (Early Writings, 87, 88) [Pr 93.1; Maombi Aya ya 13]

Omba kwa bidii sana kwa ajili ya ufahamu wa nyakati tunamoishi, kwa ajili ya dhana kamili ya kusudi Lake, na kwa ufanisi zaidi katika kuokoa roho. -(Selected Messages 2:399) [Pr 93.2; Maombi Aya ya 14]

Ubatizo wa Roho Mtakatifu tuliopewa - wajumbe waaminifu wa MUNGU wanapaswa kutafuta kuendelea na kazi ya Bwana kwa njia Yake iliyoteuliwa. Wanapaswa kujiweka karibu na Mwalimu Mkuu, ili waweze kufundishwa kila siku kuhusu MUNGU. Wanapaswa kupigana mieleka na MUNGU katika maombi ya dhati kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ili waweze kukidhi mahitaji ya ulimwengu unaopotea katika dhambi. Nguvu zote zinaahidiwa kwa wale wanaokwenda kwa imani kutangaza injili ya milele. Wakati watumishi wa MUNGU wanapobeba ujumbe hai kwenda kwenye ulimwengu kutoka katika kiti cha enzi cha utukufu, nuru ya Ukweli itang'aa kama taa inayowaka, ikifika sehemu zote za ulimwengu. Kwa hivyo giza la upotovu na kutokuamini vitaondolewa kutoka katika akili za watu waaminifu katika nchi zote, ambao sasa wanamtafuta MUNGU, "Labda watamtafuta, na kumpata." - (Testimonies to Ministers and Gospel Wafanyakazi, 459, 460) [Pr 93.3; Maombi Aya ya 15]

Mahitaji ya leo Yanakidhiwa kwetu- Kweli ya MUNGU iliyopokelewa moyoni ina uwezo wa kukufanya uwe na hekima katika wokovu. Kwa kuamini na kuitii, wewe utapokea neema ya kutosha kwa ajili ya majukumu na majaribu ya leo. Hauhitaji Neema ya kesho. Unapaswa kuhisi kuwa unahusiana na kushugulika na leo tu. Pata ushindi leo; jikane leo; kesho na uombe leo; jipatie ushindi kwa MUNGU leo. - (Testimonies for the Church 3:333) [Pr 93.4; Maombi Aya ya 16]

Mahitaji ya Kazi ya MUNGU yanatolewa kwetu kwetu- (Mungu anatupa mahitaji ya kazi Yake)-Mahitaji/Masilahi anuwai ya msingi hutupatia chakula cha kutafakari na msukumo kwa ajili ya maombi yetu (Yote tunayoyahitaji ili

kufanya kazi ya Mungu huwa tunayafikiria kwa kina, basi hii itupe nguvu ya kuyaombea mahitaji haya, baada ya kuyacheua). - (Testimonies for the Church 4:459) [Pr 94.1; Maombi Aya ya 17]

Maombi Yaliyojibiwa ni Msingi wa Sifa na Shukrani (Sababu tosha ya Kububujika Shukrani) -Katika sura ya pili ya 1Samweli imeandikwa sala ya mwanamke aliyejitoa wakfu na ambaye alimtumikia na kumtukuzwa MUNGU. Huyu Aliomba: "Moyo wangu wamshangilia BWANA, Pembe yangu imetukuka katika BWANA, Kinywa changu kimepanuka juu ya adui zangu; Kwa kuwa naufurahia wokovu Wako". Hakuna mtakatifu kama Bwana, kwa kuwa hakuna mwingine isipokuwa Yeye, wala hakuna mwamba kama MUNGU wetu." Kutoa shukrani kwa Hana kwa ajili ya jibu la maombi yake ni somo kwa wale ambao leo wanapokea majibu ya maombi yao. Je! Sisi hatupuzii/tunapuuzia kurudisha sifa na shukrani kwa Mungu kwa fadhili Zake? [Pr 94.2; Maombi Aya ya 18]

Daudi anatangaza, "Nampenda Bwana, kwa sababu amesikia sauti yangu na dua zangu. Kwa sababu amenitegea sikio Lake, kwa hivyo nitamwita siku zote za maisha yangu." Wema wa MUNGU katika kusikia na kujibu maombi hutuweka chini ya jukumu zito la kutoa shukrani zetu kwa upendeleo na neema tulizopewa. Tunapaswa kumsifu MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya sasa. Baraka zilizopokelewa katika jibu la maombi zinapaswa kutambuliwa mara moja. Kumbukumbu zake zinapaswa kuwekwa katika shajara yetu (diary), ili tunapokishika kitabu mkononi, tuweze kukumbuka wema wa Bwana, na kulisifu Jina Lake takatifu. - (The Review and Herald, Mei 7, 1908) [Pr 95.3; Maombi Aya ya 19]

Tabia zetu zinaweza Kubadilishwa — Mabadiliko tunayohitaji ni mabadiliko ya moyo, na yanaweza kupatikana tu kwa kumtafuta MUNGU, na ili kupata badiliko lolote, mtu binafsi, anapaswa kumtafuta Mungu yeye mwenyewe, kwa ajili ya baraka Zake, kwa kumwomba Yeye kwa ajili ya nguvu Zake, kwa kuomba kwa bidii ili neema Yake itujie, na kwamba tabia zetu zinaweza kubadilishwa. Haya ndiyo mabadiliko tunayohitaji leo, na ili kupata uzoefu huu tunapaswa kutumia nguvu ya kudumu na kuonyesha bidii ya dhati moyoni. Tunapaswa kuuliza kwa dhati, kwa unyofu wa moyo- tukiwa wakweli, "Nifanye

nini ili niokolewe?" Lazima tujue ni hatua zipi tunazichukua ili kuelekea mbinguni ITunapaswa kujua ni yapi ya kufanya ili tueleke mbinguni. - (Selected Messages 1:187) [Pr 94.4; Maombi Aya ya 20]

Uelewa wetu wa Neno la MUNGU utapanuliwa— Hakuna mtu aliye salama hata kwa siku moja au saa bila maombi. Hakika tunapaswa kumwomba Bwana kwa ajili ya hekima ya kulielewa Neno Lake. Hapa Unafunuliwa ujanja na hila zake mshawishi na zile mbinu ambazo anaweza kupingwa kwa mafanikio. Shetani ni mtaalam aliyebobea katika kunukuu Maandiko, akiweka tafsiri yake mwenyewe juu ya Aya ambazo anatarajia kutufanya sisi tujikwae. Tunapaswa kujifunza Biblia kwa unyenyekevu wa moyo, bila kupoteza mtazamo wetu juu ya utegemezi wetu kwa MUNGU. Ingawa inabidi tujilinde kila wakati dhidi ya hila mahiri za Shetani, tunapaswa kuomba kwa imani daima: "Usitutie kwenye majaribu." The Great Controversy, 530) [Pr 95.1; Maombi Aya ya 21]

Biblia haifai kusomwa bila maombi. Roho Mtakatifu Ndiye peke yake anaweza kutufanya tuhisi umuhimu wa vile tunavyovisoma kueleweka, au kutuepusha kuunyagua ule Ukweli mgumu katika ufahamu ili uendane na matakwa yetu. Ni kazi ya ofisi ya malaika wa mbinguni kuandaa mioyo ili kulielewa Neno la MUNGU ili tuweze tuvutiwe na uzuri Wake kama sumaku inavyovuta, tukishauriwa na maonyo Yake, au kuhuishwa, kuchangamshwa na kuimarishwa na ahadi Zake. Tunapaswa kufanya ombi la mwandishi wa-Zaburi kuwa letu wenyewe: "Fungua macho yangu, ili nipate kuona maajabu ya sheria Yako." Zaburi 119:18. Majaribu mara nyingi huonekana kuwa hayapingiki kwa sababu, kupitia kupuuza maombi na kusoma Biblia, mtu aliyejaribiwa hawezi kukumbuka ahadi za MUNGU kwa urahisi na kukutana na Shetani akiwa na silaha za Maandiko. Lakini malaika wanawazunguka wale ambao wako tayari kufundishwa katika mambo ya Bwana/mbingu; na wakati wa ulazima mkubwa au muafaka, watawakumbusha Kweli zile ambazo zinahitajika. Kwa hivyo "wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua kiwango dhidi yake." Isaya 59: 19— (The Great Controversy, 599, 600) [Pr 95.2; Maombi Aya ya 22]

SURA YA 11

MAOMBI YALIYOJIBIWA

MUNGU Atajibu, ikiwa tutaomba- Hekima ya ulimwengu inafundisha kwamba maombi sio jambo la lazima. Wanasayansi wanadai kuwa hakuna jibu halisi kwa sala; kwamba hii itakuwa ukiukaji wa sheria, yaani muujiza, na kwamba miujiza haipo. Wao husema kwamba Ulimwengu wote (Sayari zote au universe), unasimamiwa na sheria zisizobadilika, na hata MUNGU Mwenyewe hafanyi chochote kinyume na sheria hizi. Kwa hivyo wanamwakilisha MUNGU akiwa amefungwa na sheria Zake mwenyewe-kana kwamba kuendelea kwa utendaji wa sheria za Bwana kunamwondolea Yeye uhuru Wake kama Mungu (Uungu unakosa uhuru na uwezo kufanya unavyotaka). Mafundisho hayo yanapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je! Miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Huyu Huyu Mwenye huruma anaishi leo, na Yeye Yuko tayari kusikiliza maombi ya imani kama vile alipotembea waziwazi na akaonekana kwa macho miongoni mwa wanadamu. Maumbile ya asilia hushirikiana na nguvu za Mungu zipitizao nguvu zote, kutenda miujiza. Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia sisi kwa kuyajibu maombi ya imani, yale ambayo Yeye asingetupatia kama tusingemwuliza/tusingemwomba {Leo kuna utafiti mwingi sana wa kisayansi unaopitia hatua 5 za sayansi, kuhusu ufanisi wa maombi, mfano, wagonjwa wa moyo katika hospitali moja wamechukuliwa kwa utafiti, na wakagawa makundi mawili, wagonjwa wa kundi la kwanza hawakuombea na kundi la pili, la wagonjwa likaombewa, majibu ya utafiti yaliyonyesha matokeo tofauti, na walipojaribu tena wakaona hivyo hivyo, kwamba kundi lililombewa watu walipona haraka, walikaa hospitalini

muda mfupi, na hata wengine hawakuhitaji upasuaji! Haya yameandikwa kwenye magazeti maarufu kama vile Times, New York Times, Newsweek, British Medical Journal nk Japokuwa hii si sababu yetu Wakristo kuamini kwamba maombi yanafanya kazi, kwani tunaamini kile Neno la Mungu limesema, Biblia imesema na hiyo inasawazisha yote! Njia za Mungu hazichunguziki, nami siyo lazima nizijue kwa kinagaubaga! Baada ya dhambi Mungu hakuzungumza na mwanadamu uso kwa uso, ila anazungumza nasi kwa maombi. Hata hivyo mimi nisingependa kuwa mgonjwa nisiyeombewa kwaajili ya majaribio au utafiti wa watu fulani wakana-Mungu, je, wewe ungependa iwe hivyo kwako?} (The Great Controversy, 525) [Pr 96.1; Maombi Aya ya 1]

Unapopata fursa ya kukutana na ndugu zako kanisani, waambie juu ya umuhimu wa kuweka wazi mfereji wa mawasiliano kati ya MUNGU na roho/moyo. Waambie kwamba ikiwa watakuwa/watapata moyo na sauti ya kuomba, basi MUNGU pia atapata/atakuwa na majibu kwa maombi yao. Waambie wasipuuze majukumu yao ya kidini/kiroho. Wahimize na kuwatia moyo ndugu zako kusali. Lazima tutafute ikiwa tutapata, lazima tuombe ikiwa tutapokea, lazima tubishe hodi ikiwa tutafunguliwa mlango. - (The Signs of the Times, Februari 10, 1890) [Pr 96.2; Maombi Aya ya 2]

Yesu hatuiti tumfuate, na kisha atutelekeze. Ikiwa tusalimisha maisha yetu kwa ajili ya huduma Yake, basi hatuwezi kamwe kuwekwa katika nafasi ambayo MUNGU hajaandaa majaliwa/mipango Yake. Katika hali yetu yoyote, tuna Mwongozo wa kuongoza njia yetu; katika shida zetu zozote, sisi tunaye Mshauri wa kweli; katika huzuni yetu yote, kufiwa, au upweke, tunaye Rafiki anayetuhurumia. Hata pale tunapofanya makosa pasipo kujua, kwasababu ya ujinga wetu, Kristo hatuachi [Pr 97.1; Maombi Aya ya 3]

Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." [Mathayo 21:22.] - (Gospel Workers, 263) [Pr 97.2; Maombi Aya ya 4]

Baraka za MUNGU zitakuja kama matokeo ya Imani ya Unyenyekevu -Uhusiano wa karibu na mbingu utatoa toni/mwitikio sahihi kwa uadilifu wako na utakuwa msingi

wa mafanikio yako. Hisia zako za utegemezi zitakusukuma kwenye sala, na kuhisi kwako kuwajibika kutakupelekea kufanya jitihada za dharura. Maombi na bidii, bidii na maombi, vitakuwa biashara/shughuli ya maisha yako. Lazima uombe kana kwamba ufanisi na sifa zote zinategemea na utendaji wa MUNGU tu, na kufanya kazi kana kwamba jukumu ni lako wewe mwenyewe tu. Ukitaka nguvu unaweza kuwa nayo; inasubiri rasimu/amri yako tu. Mwamini MUNGU tu, muendee kwa Neno Lake, tenda kwa imani, na baraka zitakuja. [Pr 97.3; Maombi Aya ya 5]

Katika suala hili, uwezo wa akili mahiri za asili kwenye ubongo (genius), mantiki, na ufasaha/umbuji havitafaulu. Wale ambao wana unyenyekevu, wanamtegemea Mungu, na wenye moyo uliopondeka, MUNGU huwakubali, na husikia maombi yao; na MUNGU anaposaidia, vikwazo vyote vitaondolewa. Ni watu wangapi wenye uwezo mkubwa wa asili, talaluma/elimu ya hali ya juu wameshindwa walipowekwa katika nafasi za uwajibikaji, wakati wale wa akili dhaifu, na mazingira duni zaidi, wamefanikiwa kupindukia. Siri ni: Wale wenye uwezo wa asili na elimu, walijiamini wao wenyewe, wakati wale dhaifu waliungana na Yeye ambaye ni Mshauri wa Ajabu na Jemedari hodari katika kufanya kazi kutimiza Yale ambayo amepanga kutokana na mapenzi Yake. – (Testimonies for the Church 4:538, 539) [Pr 97.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi rahisi ambayo yamesukumwa na Roho Mtakatifu, yatapanda kupitia malango wazi, mlango ulio wazi ambao Kristo ametangaza: Nimefungua malango, na hakuna mtu anayeweza kuyafunga. Maombi haya, yaliyochanganywa na uvumba wa ukamilifu wa Kristo, yatapanda kama manukato kwa Baba, na majibu yatakuja. –(Testimonies for the Church 6:467) [Pr 97.5; Maombi Aya ya 7]

Maombi ya Unyenyekevu na Imani kama ya Mtoto Yatajibiwa - "Ikiwa mtu yeyote ana kiu, na aje Kwangu anywe." Lakini atakayekunywa maji nitakayompa Mimi, hataona kiu milele. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji ya uzima na kumpatia uzima wa milele." Yohana 7:37; Yohana 4:14. [Pr 98.1; Maombi Aya ya 8]

Ikiwa, pamoja na ahadi hizi mbele yetu, sisi tunachagua kubaki wakavu-wakavu na kuwa na kiu kwa kukosa maji ya uzima, ni kosa letu wenyewe. Ikiwa tungekuja kwa Kristo tukiwa na unyenyekevu kama wa mtoto anavyokwenda kwa wazazi wake wa kidunia, na kuomba vitu ambavyo ameahidi, tukiamini kwamba tunavipokea, hakika tutakuwa navyo. - (Testimonies for the Church 9:179) [Pr 98.2; Maombi Aya ya 9]

Omba na Amini – MUNGU hasemi, Omba mara moja, nawe utapata. Yeye anatusihi sisi tuombe. Tuendeleo kuomba bila kupata uchovu au kukosa uvumilivu. Kudumu katika maombi kunamleta mwombaji katika kujibidisha zaidi, na kumpa shauku ya dhati zaidi, na kuongeza matamano ya kupokea vitu anavyoomba. Kristo alimwambia Martha kwenye kaburi la Lazaro, "Ikiwa utaamini, utaona utukufu wa MUNGU." Yohana 11:40. [Pr 98.3; Maombi Aya ya 10]

Lakini wengi hawana imani hai. Hii ndio sababu hawaoni uwezo wa MUNGU zaidi. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika matendo yao kuliko utendaji kazi wa MUNGU kwao. Wanajipigania na kujitunza wao wenyewe.

Wanapanga na kuweka mikakati makini, na ya kinagaubaga, ila wanasali kidogo, wanamtumiani Mungu kwa udogo tu, na wanatarajia kidogo tu kutoka kwa MUNGU. Wao hufikiri kwamba wana imani, lakini ni mihemko au msukumo tu wa kitambo kidogo tu. Wanashindwa kutambua hitaji lao wenyewe, au utayari wa MUNGU kutoa, hawana uvumilivu katika kuyaweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 98.4; Maombi Aya ya 11]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya dhati, bidii na ya kudumu hata katika wakati mgumu kama ilivyokuwa ombi la rafiki masikini aliyeomba mikate usiku wa manane. Kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa karibu zaidi. Tutapokea baraka zilizoongezeka kwa sababu tumeongezeka kiimani. [Pr 98.5; Maombi Aya ya 12]

Fungu letu ni kuomba na kuamini. kesheni mkiomba. Keshu, na ushirikiane na MUNGU asikiaye maombi. Kumbuka kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na tenda kulingana na maombi

yako. Itafanya tofauti kubwa kwako hata utakapojaribiwa imani yako kuhakikisha kuwa ni ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni desturi au kutekeleza wajibu tu.— (Christ's Object Lessons, 145, 146) [Pr 99.1; Maombi Aya ya 13]

Omba kwa Imani na Majibu Yatakuja — Masomo ambayo MUNGU hutuma kila wakati, ikiwa yataeleweka vizuri, yataleta msaada kwa wakati unaofaa. Weka tegemeo lako kwa MUNGU Omba sana, na uamini. Kwa Kuamini, kutumaini, kutegemea, mkishikilia kwa nguvu Mkono wenye Nguvu isiyo na kipimo, mtakuwa zaidi ya washindi. [Pr 99.2; Maombi Aya ya 14]

Wafanyakazi wa kweli hutembea na kufanya kazi kwa imani. Wakati mwingine wanachoka kwa kutazama maendeleo ya kazi yanavyozorota wakati vita vinapopamba moto kati ya nguvu za mema na mabaya. Lakini wakikataa kushindwa au kuvunjika moyo wataona mawingu yakitawanyika na ahadi ya ukombozi ikitimizwa. Kupitia ukungu ambao Shetani amewazunguka nao, wataona mwangaza wa miale inayong'aa ya Jua la Haki. [Pr 99.3; Maombi Aya ya 15]

Fanya kazi kwa imani, na mwachie MUNGU matokeo-yakabidhi matokeo Kwake. Omba kwa imani, na mafumbo/siri ya majaliwa Yake, italeta jibu Lake. Wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa huwezi kufaulu. Lakini fanya kazi na uamini, ukiweka juhudi zako katika imani, tumaini, na ujasiri. Baada ya kufanya kile uwezacho, wewe mngojee Bwana, ukitangaza uaminifu Wake, Naye atalitimiza Neno Lake. Subiri, sio kwa wasiwasi au kwa kukosa utulivu, lakini kwa imani imara na uaminifu usiotetereka.—(Testimonies for the Church 7:245) [Pr 99.4; Maombi Aya ya 16]

Kuna nguvu inayotakiwa kupatikana kutoka kwa MUNGU. Yeye ana uwezo wa kusaidia. Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, wewe utapokea; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kesho, omba, fanya kazi, inapaswa kuwa kauli mbiu yako . - (Testimonies for the Church 2:427) [Pr 99.5; Maombi Aya ya 17]

MUNGU ametutuma tufanye kazi katika shamba Lake la mizabibu. Ni wajibu wetu kufanya yote tuwezayo. "Panda

mbegu yako asubuhi, wala usizuie mkono wako jioni; kwa maana haujui ni nini kitafanikiwa, ama hiki au kile." Tuna imani ndogo sana. Tunamwekea mipaka Mtakatifu wa Israeli. Tunapaswa kushukuru kwamba Yeye anashuka chini kabisa na kumtumia yeyote miongoni mwetu kama vyombo Vyake. Kwa kila ombi la dhati na bidii lililowekwa kwa imani, jibu litarudishwa. Linaweza lisije vile vile tulivyotarajia; lakini jibu huja wakati ambao tunalihitaji zaidi (muafaka). Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho, nanyi mtapewa. The Review and Herald, Machi 23, 1897) [Pr 99.6; Maombi Aya ya 18]

Ikiwa tupata muda wa Kuomba, MUNGU Atapata muda wa Kujibu- Kila ombi la dhati kwa ajili ya kupata neema na nguvu litajibiwa. Mwombe MUNGU akufanyie mambo yale ambayo wewe mwenyewe huwezi kujifanyia. Mwambie Yesu kila kitu. Zianike siri za moyo wako waziwazi mbele Zake; kwani jicho Lake huchunguza vichocho vya ndani kabisa ya moyo, Naye husoma mawazo yako kama kitabu kilicho wazi. Wakati umeomba vitu ambavyo ni muhimu kwa faida ya roho yako, amini kwamba unavipokea, na utakuwa navyo. Kubali zawadi Zake kwa moyo wako wote; kwani Yesu amekufa ili vitu vya thamani vya mbinguni vipate kuwa vyako, na mwishowe upate makao na malaika wa mbinguni katika ufalme wa MUNGU. [Pr 100.1; Maombi Aya ya 19]

Ikiwa utapata sauti na wakati wa kuomba, MUNGU Naye atapata wakati na sauti ya kujibu. - (My Life Today, 16) [Pr 100.2; Maombi Aya ya 20]

Shangilia kabisa Kwamba MUNGU Ameyajibu Maombi Yako – Omba kwa imani. Na hakikisha unayaleta maisha yako kupatana na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Usiache imani yako idhoofike, kwani baraka utakazopokea huliangana/zinatoshana na imani uliyonayo. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Mwendeeni/mchukue kwa Neno Lake. "Yeye ni mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna hata ombi moja la dhati linalopotea. Njia iko wazi; mkondo unabubujika.

Unabeba sifa Zake za uponyaji, ukimimina mkondo unaorejesha uzima/uhai mpya, afya na wokovu. – (Testimonies for the Church 7:274) [Pr 100.3; Maombi Aya ya 21]

Uzito wa Maombi yetu ni Ahadi kwamba MUNGU Atajibu— Wakati mtu anatoa ombi dhati, ari na bidii kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee tulilopewa chini ya mbingu ambalo Kwalo tunaweza kuokolewa), kuna ahadi katika nguvu na bidii hiyo ya dhati kutoka kwa MUNGU kwamba Yuko njiani kujibu hilo ombi zaidi, na juu ya yote ambayo tunaweza kuomba au kufikiria (kupiga picha kichwani). Hatupaswi kuomba kwa Jina la Yesu tu, bali kwa uvuvio na moto* wa nguvu za Roho Mtakatifu. Hii inaelezea na kumaanisha nini? Ni kusema, "Roho Mwenyewe hutuomba kwa kuugua maumivu makali yasiyoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhati. Kisha yatafikia kiti cha rehema. Endelea kuomba bila kusita. MUNGU hasemi, Omba mara moja tu, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, na kuwa mwepesi, na mwenye utayari kuomba saa yoyote, ukiamini unavyo tayari vile vitu unavyoomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu wewe. - (Gospel Herald, Mei 28, 1902. [Pr 101.1; Maombi Aya ya 22]

("kindling" ni inaweza kuwaka kwa urahisi - kwa maneno mengine, ni kitu kidogo kama vijiti ambavyo vinaweza kutumika kuwasha moto. Kwa kupendeza, Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentekoste katika ndimi za moto. Kwa hivyo naona kwa hapa Roho Mtakatifu ni kama dutu inayoweza kuwaka ambayo huipa maombi yetu nguvu na hutumika kama mbebaji wa maombi yetu kwenye kiti cha enzi cha Mungu)

Masharti ya Kujibiwa kwa Maombi — Kuna mazingira fulani ambayo tunaweza kutarajia kwamba MUNGU atasikia na kuyajibu maombi yetu. La kwanza kati ya sababu hizi ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Yeye Ameahidi, "Nitamwaga maji juu yake yeye aliye na kiu, na mafuriko juu ya nchi kavu." Isaya 44: 3. Wale walio na njaa na kiu ya haki, ambao wanamfuata MUNGU, wanaweza kuwa na uhakika kwamba watajazwa. Moyo lazima uwe wazi kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu, la sivyo baraka ya MUNGU haiwezi kupokelewa. [Pr 101.2; Maombi Aya ya 23]

Uhitaji wetu wenyewe ni hoja kubwa tosha na inasihhi kwa umbuji zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa

kutafutwa ili atufanyie mambo haya. Yeye anasema "Ombeni, nanyi mtapewa." Yeye ambaye hakumhurumia hata Mwanae wa pekee, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. Ikiwa amefanya hivyo, je, atakosaje kutukirimia mema yote pia? Mathayo 7:7; Warumi 8:32. [Pr 101.3; Maombi Aya ya 24]

Ikiwa tunazingatia uovu mioyoni mwetu, ikiwa tunaing'ang'ania dhambi yoyote inayojulikana, basi Bwana hatatusikia; lakini ombi la mtu mwenye majuto, kupondeka moyo na toba, daima linakubaliwa. Wakati makosa yote yanayojulikana yanasahihishwa, tunaweza kuamini kwamba MUNGU atajibu maombi yetu. Uzuri au sifa yetu wenyewe haitatufanya tufae kupata upendeleo au neema ya MUNGU; ni sifa na stahiki za Yesu ndizo ambazo zinatuokoa, Ni damu Yake ndiyo ambayo itatutakasa/inatusafisha; lakini tuna kazi ya kufanya ili kutimiza masharti ya kukubaliwa. [Pr 101.4; Maombi Aya ya 25]

Kipengele kingine cha ombi linaloshinda, lenye ustahimilivu na lenye ushawishi ni imani. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yupu, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." (Waebrania 11:6). Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Je! Tunamwendea na kumchukua kutokana na Neno Lake? [Pr 101.1; Maombi Aya ya 26]

Hakikisho letu ni pana na halina kikomo, na Yeye ni waminifu ambaye ameahidi. Wakati hatupokei yale tuliyoomba, wakati tunaomba, bado tunapaswa kuamini kwamba Bwana anasikia na kwamba Yeye atajibu maombi yetu. Sisi ni wakosefu sana na tumepungukiwa na uoni (macho yenye mapungufu), na uelewa wetu ni finyu kiasi kwamba wakati mwingine tunaomba vitu ambavyo havingekuwa baraka kwetu, na Baba yetu wa mbinguni kwa upendo hujibu maombi yetu kwa kutupatia kile kitakachokuwa kwa faida yetu ya juu zaidi - kile ambacho sisi wenyewe tungetamani tukiwa na maono/utashi yaliyoangaziwa na MUNGU tunaweza kuona vitu vyote kama vilivyo. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia ahadi; kwani wakati wa majibu hakika utakuja, na tutapokea baraka wakati ule ambapo tunaihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi yatajibiwa

kila wakati kwa njia ile ile tuliyoomba na kwa kile kile ambacho tunatamani, ni dhana potofu, isiyoendana na mapenzi ya Mungu (au kiburi wakati mwingine). MUNGU ni Mwenye busara mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanaoenenda kwa unyoofu kitu chochote kizuri. Basi usiwe na woga au hofu kumtumainia, ingawa huoni jibu la maombi yako papo hapo. Tegemea ahadi Yake ya hakika, "Ombeni, nanyi mtapewa." [Pr 101.2; Maombi Aya ya 27]

Ikiwa tutachukua ushauri na mashaka na hofu mioyoni mwetu, au kujaribu kutatua kila kitu ambacho hatuwezi kuona wazi, kabla ya kuwa na imani, mashaka yatazidi kuongezeka tu, na kuwa na kina kirefu. Ila pale tunapomwendea MUNGU, tukijisikia tu hoi bin taabani na tegemezi, kama tulivyo kihalisia, na kwa imani ya kumtegemea Yeye na tukiwasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana mwisho, Yule anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anasimamia na kuongoza kila kitu kwa mapenzi Yake na Neno Lake, Yeye Anaweza na atashughulikia kilio chetu, na atatuangazia nuru mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika ushirika na Nia na akili ya Yule Asiye na mwisho/kikomo. Labda hatuwezi kuwa na ushahidi wa wazi, wa kushangaza, usio wa kawaida au unaoonekana wakati huo kwamba uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini hii ndiyo ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake unaoonekana, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo, rehema na huruma kubwa. [Pr 102.3; Maombi Aya ya 28]

Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha mioyoni mwetu. Je! Tunawezaje kuomba, "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu," na bado tukaendekeza roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatarajia maombi yetu wenyewe yasikilizwe lazima tusamehe wengine kwa njia ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotarajia kusamehewa. [Pr 103.1; Maombi Aya ya 29]

Kutochoka yaani uvumilivu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea. Lazima tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu. Tunapaswa kuwa "na utayari saa yote katika maombi," "Tunapaswa kudumu katika sala, na kukesha, haya mawili yatoshane na

kushukuru kwetu." Warumi 12:12; Wakolosai 4: 2. Petro anawahimiza waumini kuwa "wenye kiasi, na wakeshe katika maombi." 1 Petro 4: 7. Paulo anaelekeza, "Katika kila jambo kwa maombi na dua pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na MUNGU." (Wafilipi 4:6). "Lakini ninyi, wapenzi," anasema Yuda, "mkiomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa MUNGU." Yuda 20, 21 .— (Steps to Christ, 95-97) [Pr 103.2; Maombi Aya ya 30]

Ikiwa tutampa Yeye utii nusu-nusu tu, ahadi Zake hazitatimizwa kwetu. - (The Ministry of Healing, 227) [Pr 103.3; Maombi Aya ya 31]

Lazima tuishi Maombi yetu ikiwa yataenda kujibiwa – Tunapaswa kuomba na kukesha katika maombi, ili kusiwe na mapishano katika maisha yetu-(twapaswa kuwa na uthabiti, uendelevu). Hatupaswi kukosa kuwaonyesha wengine kwamba tunaelewa kuwa kukesha katika maombi kunamaanisha kuishi maombi yetu mbele za MUNGU, ili kwamba Yeye ayajibu. – (Selected Messages 1:116, 117) [Pr 103.4; Maombi Aya ya 32]

Maombi ni kazi bure ikiwa Maisha hayashabihiani na Maombi - "Mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa." Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni upendeleo kwetu kumwendea tukiwa na ujasiri mtakatifu. Kwa unyofu tukimwomba nuru Yake iangaze juu yetu, Yeye Atatusikia na kutujibu. Lakini lazima tuishi kulingana na maombi yetu. Maombi ni kazi bure, yaani hayana faida yoyote ikiwa tunatembea kinyume nayo. Nimemwona baba ambaye, baada ya kusoma sehemu ya Maandiko na kuomba, mara nyingi kabla ya kuinuka baada tu ya kupiga magoti ili aombe, alianza kuwagombeza/kuwafokea watoto wake. MUNGU angewezaje kweli kujibu ombi lile aliloomba? Na ikiwa, baada ya kuwagombeza watoto wake, baba anasali, je, sala hiyo inawanufaisha watoto kweli? Hapana; labda ikiwa anatoa maombi ya kuungama kwa MUNGU. - (Child Guidance, 499) [Pr 103.5; Maombi Aya ya 33]

Tunapaswa kuambatanisha sifa ikiwa tunahitaji maombi yetu yajibiwe – Je! Shughuli na uzoefu wetu wote wa ibada unapaswa kujumuisha kuomba na kupata peke yake tu? Je! Tunapaswa kufikiria kila wakati matakwa/mahitaji yetu na sio ile faida tunayopokea? Je!

Sisi Tutakuwa wapokeaji wa rehema Zake na kamwe tusitoe shukrani zetu kwa MUNGU, na wala tusimsifu kwa yale aliyotutendea? Sisi wala Hatuombi sana, ila tuna ubahili wa kutoa shukrani. Ikiwa upendo mkarimu wa MUNGU ungeleta shukrani zaidi na kumsifu Yeye, basi tungelikuwa na nguvu zaidi katika maombi. Tungependana zaidi katika upendo wa MUNGU na kuzidi kumtukuza. Wewe ambaye unalalamika kwamba MUNGU hasikii maombi yako, badilisha zoezi la utaratibu wako wa sasa na uchanganye sifa na maombi yako. Unapozingatia wema na rehema Zake utagundua kuwa Yeye atazingatia matakwa yako. [Pr 104.1; Maombi Aya ya 34]

Omba, omba kwa bidii na bila kukoma, lakini usisahau kusifu. - (Testimonies for the Church 5:317) [Pr 104.2; Maombi Aya ya 35]

Kukosa uaminifu katika Uwakili Kunaweza Kuwa Sababu ya Maombi Kutojibiwa – Kama Mtoaji wa kila baraka, MUNGU anadai sehemu fulani ya vitu vyote tulivyo navyo. Huu ni mpango Wake wa kuendeleza kuhubiri kwa injili. Na kwa kumrudishia MUNGU, tunakuwa tumeonyesha kuthamini kwetu na shukrani zetu kwa zawadi Zake. Lakini ikiwa tunamzuilia Yeye kilicho Chake Mwenyewe, tunawezaje basi kumtarajia Yeye atuamini na kutukabidhi vitu vya mbinguni? Je, inawezekana kuwa hii ndiyo siri ya sala isiyojibiwa. – (Christ’s Object Lessons, 144) [Pr 104.3; Maombi Aya ya 36]

Twamtukana Mungu na kumdhalilisha kwa kuzidai Ahadi Zake bila Kukidhi Masharti – Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi hayawezi kuchukua mahali na nafasi ya wajibu (maombi si mbadala wa wajibu). "Ikiwa mnanipenda," Kristo anasema, "mtazishika amri Zangu." Yeye Azipokeaye amri Zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye. Naye anipendaye Mimi atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake." Yohana 14:15, 21. Wale ambao huleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Yake wakati hawafuati masharti yake, wanamtukana na kumdhalilisha Yehova. Wao huleta Jina la Kristo kama mamlaka yao ya kutimiziwa ahadi, lakini hawafanyi mambo ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo wao Kwake. - (Christ Object Lessons, 143) [Pr 104.4; Maombi Aya ya 37]

Ikiwa Masharti yametimizwa, Ahadi ya Maombi yanayojibiwa haizuiliki (haina mashaka) – Maombi na imani vimeunganishwa kwa karibu (ni pacha), na vinahitaji kuchunguzwa/kufunzwa kwa pamoja. Katika ombi la imani kuna sayansi ya Bwana/mbingu; ni sayansi ambayo kila mtu ambaye anatamani kufanikisha kazi yake ya maisha lazima aelewe. Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Yeye Anaweka wazi kwamba ombi letu lazima liwe kulingana na mapenzi ya MUNGU; lazima tuombe vitu ambavyo ameahidi, na chochote tunachopokea lazima kitumike katika kufanya mapenzi Yake. Masharti yakitimizwa, ahadi haizuiliki (hakuna maswali yanabakia). [Pr 105.1; Maombi Aya ya 38]

Kwa msamaha wa dhambi, kwa Roho Mtakatifu, kwa hulka na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo Yeye ameahidi, sisi tunaweza kuomba; kisha tunapaswa kuamini kwamba tunapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumekwishapokea. [Pr 105.2; Maombi Aya ya 39]

Hatuhitaji kutafuta ushahidi wa nje wa baraka. Zawadi iko katika ahadi, na tunaweza kwenda kuendelea na kazi yetu tukiwa na uhakikisho kwamba kile ambacho MUNGU amekiahidi, Yeye Ana uwezo wa kukitekeleza, na kwamba zawadi, ambayo tayari tunayo, itadhihirika haswa wakati tutakapokuwa tunaihitaji zaidi. – (Education, 257, 258) [Pr 105.3; Maombi Aya ya 40]

Maombi yetu Sio Amri za kumwamrisha MUNGU— Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake. Maombi yetu hayapaswi kuchukua mfumo wa amri, bali umbo la maombezi Kwake Yeye, ili afanye mambo tunayotamani kutoka Kwake. (Testimonies for the Church 2:149) [Pr 105.4; Maombi Aya ya 41]

Maombi hayajibiwi Papo hapo mara zote – MUNGU ana mbingu iliyojaa baraka kwa wale watakaoshirikiana Naye. Wote wanaomtii wanaweza kudai kwa ujasiri utimizo wa ahadi Zake. Lakini lazima tuonyeshe kumtegemea Yeye kikamilifu na uaminifu thabiti usiokengeuka kwa MUNGU. Mara nyingi Yeye hucheleweshwa kutujibu ili kuitahini imani yetu au kujaribu unyofu wa matamano yetu. Baada ya kuomba kulingana na Neno Lake, sisi tunapaswa kuamini

ahadi Yake na kukazana bila kuchoka katika maombi yetu kwa kunuia ambako hakutakataliwa. – (Christ’s Object Lessons, 145) [Pr 105.5; Maombi Aya ya 42]

Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujinyima yaliyoamriwa katika Neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongoa roho. Watu wa MUNGU wataruhusu nuru yao iangaze, na kisha wale wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni. - (Messages to Young People, 315) [Pr 106.1; Maombi Aya ya 43]

Kuchelewa kwa Kristo kwa siku mbili baada ya kusikia kwamba Lazaro alikuwa mgonjwa haukuwa upuuziaji au kukataa kwa upande Wake. Lilikuwa ni kusudi Lake kubaki pale alipokuwa mpaka kifo cha Lazaro kitokee, ili aweze kuwapa watu ushahidi wa Uungu Wake, sio kwa kumponya mtu anayekaribia kufa, bali kwa kumfufua mtu aliyezikwa tayari. [Pr 106.2; Maombi Aya ya 44]

Jambo hili linapaswa kuwa faraja kwetu. Wakati mwingine tunajaribiwa kufikiri kwamba ahadi, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa,” haitimizwi mpaka pale ambapo jibu linatolewa mara tu ombi linapowasilishwa. Ni upendeleo kwetu kuomba baraka maalum, na kuamini kwamba tutapewa. Lakini ikiwa baraka zilizoombwa hazitolewi mara moja, hatupaswi kufikiria kwamba maombi yetu hayasikilizwi. Hakika tutapokea, hata kama jibu litacheleweshwa kwa muda. Katika kutekeleza mpango wa ukombozi, Kristo anaona mengi katika ubinadamu ya kumvunja moyo. Lakini Yeye havunjiki moyo au kukata tamaa. Kwa rehema na upendo, Yeye Anaendelea kutupatia fursa na upendeleo. Kwa hivyo tunapaswa kupumzika katika Bwana, na kumngojea Yeye kwa uvumilivu. Jibu la maombi yetu linaweza lisije haraka kama tunavyotamani, na inaweza kuwa sio kile kitu ambacho tuliomba rasmi; lakini Yeye ambaye anajua ni kipi bora kupita vyote kwa ajili ya watoto Wake atatoa mema zaidi kuliko tulivyoomba, tusipopoteza imani (au kuwa makafiri) na kuvunjika moyo. –(The Youth’s Instructor, April 6, 1899) [Pr 106.3; Maombi Aya ya 45]

Sisi sote tunatamani majibu ya haraka na ya moja kwa moja kwa maombi yetu, na tunajaribiwa kuvunjika moyo

wakati jibu linapocheleweshwa au likiwa katika fumbo ambalo hatukulitazamia. Lakini MUNGU ni Mwenye busara sana na mwema kujibu maombi yetu wakati ule ule na namna ile ile tunayotamani mara zote. Yeye Atatutendea zaidi na bora kwetu, kuliko kutimiza matamano yetu yote. Na kwa sababu tunaweza kuamini hekima na upendo Wake, sisihatupaswi kumuomba aridhie mapenzi yetu, lakini tunapaswa kutafuta kuingia safari ya kutimiza kusudi Lake. Matamano na shauku zetu zinapaswa kuzama katika mapenzi Yake. Uzoefu huu unaojaribu imani ni kwa faida yetu. Kwa huo inadhihirishwa kama imani yetu ni ya Kweli na ya dhati, na inayotegemea Neno la MUNGU peke yake, au inatokana na mazingira tu, na inakuwa sio ya kutegemewa na hubadilika-badilika tu. Imani huimarishwa kwa mazoezi/kuizoeza. Lazima tuache uvumilivu utende kazi yake kamilifu, tukikumbuka kwamba kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wanaomsabiri Bwana. - (The Ministry of Healing, 230, 231) [Pr 107.1; Maombi Aya ya 46]

Niliona kwamba watumishi wa MUNGU na kanisa walikuwa wanavunjika moyo kwa urahisi sana. Walipomuomba Baba yao wa mbinguni vitu ambavyo walidhani kuwa wanavihitaji, na hivi havikuja mara moja, imani yao iliyumba, ujasiri wao ukatoweka, na hisia za kunung'unika zikawajaa. Niliona, hili halikumpendeza MUNGU. [Pr 107.2; Maombi Aya ya 47]

Kila mtakatifu anayemwendea MUNGU kwa moyo wa kweli, kwa imani, na kutuma maombi yao ya kweli Kwake, atajibiwa maombi yake. Imani yao haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU ikiwa hawaoni au hawasikii majibu ya mara moja ya maombi yao. Usiogope kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi zake za kweli: Ombeni, nanyi mtapokea.' MUNGU ni mwenye busara mno na hivyo Yeye hakosei kamwe, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake kitu chochote kizuri wanao tembea katika unyoofu. Mtu hukosea, huwa anatoka katika njia nyofu, na ingawa maombi yake yanatumwa kutoka katika moyo mkweli, mara zote huwa haombi vitu ambavyo ni vyema kwake, au ambavyo vitamtukuza MUNGU. Wakati hili likiwa hivyo, Baba yetu Mwenye busara na mwema anasikia maombi yetu, na atajibu, wakati fulani hujibu haraka-; lakini Yeye

hutupatia vitu ambavyo ni kwa faida yetu na utukufu Wake Mwenyewe. [Pr 107.3; Maombi Aya ya 48]

Ikiwa watoto wa MUNGU wangeweza kuona mpango Wake, wangejua kuwa Yeye huwapa kile ambacho ni kwa faida yao. Ingawa hawawezi kupokea yale mambo waliyotarajia tu, au waliyoomba, bado maombi yao yalijibiwa Hakuna chochote cha kuumiza walichopewa, bali baraka waliyohitaji zaidi, badala ya kitu ambacho walikuwa wameomba, ambacho kisingekuwa kizuri kwao, bali kingewaumiza. [Pr 107.4; Maombi Aya ya 49]

Niliona kwamba ikiwa hatuhisi majibu ya haraka ya maombi yetu, tunapaswa kushikilia imani yetu, bila kuruhusu mashaka na fadhaa, kwani hayo yatatutenganisha na MUNGU. Imani yetu ikitetereka, hatutapokea chochote kutoka kwake. Imani yetu kwa MUNGU inapaswa kuwa imara; na wakati tunapoihitaji sana, baraka itatuangukia kama maji ya mvua. [Pr 108.1; Maombi Aya ya 50]

Wakati watumishi wa MUNGU wanapoomba kwaajili ya Roho Wake na baraka, wakati mwingine hivi huja papo hapo; lakini sio kila wakati basi huwa hivyo. Katika nyakati kama hizo, usizimie roho. Hebu imani yako ishikilie ahadi kwamba, itakuja. Acha tumaini lako liwe kamili kwa MUNGU, na mara nyingi baraka hiyo itakuja wakati unapoihitaji zaidi, na bila kutarajia utapokea msaada kutoka kwa MUNGU, wakati unazungumza ile Kweli kwa wale wasioamini, utazungumza kwa uwazi Neno, na kwa nguvu. [Pr 108.2; Maombi Aya ya 51]

Ilionyeshwa kwangu kama watoto wakiomba baraka ya wazazi wao wa kidunia wanaowapenda. Wanaomba kitu ambacho mzazi anajua kitawaumiza; ila mzazi huwapa vitu ambavyo vitakuwa vyema na vyenye afya kwao, mahali pa kile ambacho mtoto alitaka/alitamani. Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwadilifu litasikika juu kwa MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji sana/zaidi, na mara nyingi majibu yatazidi matarajio yake. Hakuna sala ya mtakatifu wa kweli inayopotea ikiwa imetumwa kutoka katika moyo wa mnyofu kwa imani. - (Spiritual Gifts 4b, 7-9) [Pr 108.3; Maombi Aya ya 52]

Baada kutoa ombi, ikiwa jibu halitakuja mara moja, wewe usichoke kusubiri na kuwa kuanza kuyumbayumba.

Mawazo yako yasimangemange kama wimbi la bahari. Ing'ang'anie ahadi, "Yeye ni mwaminifu ambaye Awaita, Naye Atatenda" Kama mjane aliyekuwa na bidii isiyokatishwa tamaa, peleka kesi yako kwa Mungu, ukiwa thabiti katika kusudi lako. Je! Kitu hicho ni cha muhimu na chenye matokeo makubwa kwako? Hakika ni hivyo. Basi usitetereke, kwani imani yako inaweza kujaribiwa. Ikiwa kitu unachotamani ni cha thamani kubwa, basi kinastahili juhudi imara, na yenye bidii. Unayo ahadi; basi kesho na uombe. Uwe imara na maombi yako yatajibiwa; kwa maana si ni Mungu Ndiye ameahidi? kama itakugharimu kukipata basi utakipa thamani zaidi wakati kitakapopatikana. Unaambiwa waziwazi kwamba ikiwa utakuwa na shaka haupaswi kufikiria kwamba utapokea chochote kutoka kwa Bwana. Tahadhari imetolewa hapa ili usichoke, bali utulie kwa uthabiti kwenye ahadi za Bwana. Unapoomba, Yeye atakupa kwa kwa moyo mkujunfu na ukarimu na wala hutakemewa.-(Testimonies for the Church 2:131) [Pr 108.4; Maombi Aya ya 53]

“Ombeni, nanyi mtapewa.” Uhakikisho ni mpana na hauna kikomo, na Yeye ni Mwaminifu ambaye ameahidi. Wakati mwingine tunashindwa katika imani kwa sababu Hekima isiyo na kikomo haiji kwa kufuata sera au mkataba wetu. Wakati kwa sababu yoyote ile hatupokei yale tunayoomba kwa wakati tunaoomba, bado tunapaswa kuamini kwamba Bwana anasikia, na kwamba atatupatia vitu ambavyo ni bora kwetu. Utukufu Wake Mwenyewe ni sababu tosha ya wakati mwingine kuzuia kile tunachoomba, na kisha kujibu maombi yetu kwa njia ambayo hatukutarajia. Lakini tunapaswa kuikumbatia ahadi; kwani wakati wa majibu utafika, na tutapokea baraka tunazohitaji zaidi. - (The Signs of the Times, Agosti 21, 1884) [Pr 109.1; Maombi Aya ya 54]

MUNGU Hatujibu Kama Tunavyotarajia mara zote, Bali Daima Kwa Manufaa Yetu – omba, basi; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati (nyofu) jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unalitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke, ukiwa umechoka, katika mitihani ya maisha, MUNGU huyajibu, sio kila wakati kulingana na

matarajio yako, lakini mara zote kwa faida yako. – (Messages to Young People, 250) [Pr 109.2; Maombi Aya ya 55]

Wakati ulipoomba katika shida au mateso yako kwaajili ya amani katika Kristo, wingu la giza lilionekana kutia weusi kwenye akili yako. Pumziko na amani havikuja kama ulivyotarajia. Wakati mwingine imani yako ilionekana kujaribiwa kupita kiasi. Ulipotazama nyuma katika maisha yako ya zamani, uliona huzuni na kukatishwa tamaa; ulipoangalia siku zijazo, yote yakawa yasiyo na uhakika kwako. Mkono wa Bwana ulikuongoza kwa namna ya kushangaza kwa kukuleta wewe msalabani na kukufundisha kwamba hakika MUNGU Ndiye mtoa thawabu kwa wale wanaomtafuta kwa uadilifu. Wale wanaoomba kwa usahihi watapokea. Yule Anayetafuta kwa imani atapata. Uzoefu unaopatikana katika tanuru la majaribu na mateso ni wa thamani zaidi kuliko usumbufu wake wote na gharama ya maumivu yake. [Pr 109.3; Maombi Aya ya 56]

Maombi ambayo ulitoa katika upweke wako, katika kuchoka kwako na majaribu, MUNGU alijibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kwa faida yako. Haukuwa na maoni wazi na sahihi kuhusiana na ndugu zako, wala haukujiona katika nuru sahihi. Lakini, kwa majaliwa/mipango/mwongozo wa MUNGU, Yeye Amekuwa kazini kujibu maombi uliyotoa katika taabu yako, kwa namna ya kukuokoa na kulitukuza Jina Lake Mwenyewe. Kwa kutotambua au ujinga wako, wewe uliomba vitu ambavyo havikuwa bora kwako. MUNGU alisikia maombi yako yenye unyoofu, lakini baraka uliyopewa ilikuwa kitu tofauti sana na matarajio yako. MUNGU amekusudia, katika mipango/uongozi Wake, kukuweka moja kwa moja katika uhusiano na kanisa Lake, ili ujasiri wako uwe kwa kiasi kidogo juu yako mwenyewe na uwe mkubwa zaidi katika wengine ambao Anawaongoza kuendeleza kazi Yake mbele. [Pr 110.1; Maombi Aya ya 57]

MUNGU husikia kila ombi la dhati-lenye unyofu wa moyo. - (Testimonies for the Church 3:415, 416) [Pr 110.2; Maombi Aya ya 58]

MUNGU Hujibu Maombi kwa Wakati Wake Aliouchagua- Katika maisha yake yote ya ndoa, Zakaria alikuwa ameomba apate mtoto wa kiume. Yeye na mkewe

walikuwa wamezeeka sasa, na bado maombi yao yalikuwa hayajajibiwa; lakini hakunung'unika. MUNGU hakuwa amesahau. Alikuwa na wakati Wake uliowekwa wa kujibu ombi hili, na suala hilo lilipoonekana kutokuwa na matumaini, Zakaria alipokea jibu lake. - (SDA Bible Commentary, juz. 5, 1114) [Pr 110.3; Maombi Aya ya 59]

Kwa nini majibu kwa maombi yanaweza kuchelewa- MUNGU huwa hajibu mara zote maombi yetu pale tunapomwomba kwa mara ile ya kwanza; kwani akifanya hivi, tunaweza kuichukulia kirahisi kwamba tulikuwa na haki ya mibaraka na neema zote Alizotupatia. Badala ya kuchukua muda katika tukipekua mioyo yetu ili kuona ikiwa tumeendekeza uovu wowote, au dhambi yoyote tunayoifurahia, au kufanya mambo kizembe na kisha tukashindwa kutambua utegemezi wetu Kwake, na hitaji letu la msaada Wake. - (The Review and Herald, Juni 9, 1891) [Pr 110.4; Maombi Aya ya 60]

Kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wanaomsubiri Bwana. Sisi sote tunatamani jibu la haraka kwa maombi yetu na tunajaribiwa kuvunjika moyo ikiwa ombi letu halijajibiwa mara moja. Sasa, uzoefu wangu umenifundisha kuwa hili ni kosa kubwa. Uchelewesho ni kwa faida yetu maalum. Tuna nafasi ya kuona ikiwa imani yetu ni ya Kweli na ya dhati au inaweza kuyumbayumba kama mawimbi ya bahari. Lazima tujifunge juu ya madhabahu kwa kamba kali za imani na upendo, na kuacha uvumilivu uwe na kazi yake kamilifu. Imani inaimarika kupitia mazoezi ya kila wakati. Kusubiri huku hakumaanishi kwamba kwa sababu tumeshamwomba Bwana uponyaji, basi sasa hakuna chochote tunachopaswa kukifanya. Badala yake (kinyume chake), sisi tunapaswa kutumia mbinu bora kabisa ambazo Bwana kwa wema Wake ametupatia katika mahitaji yetu. - (Counsils on Health, 380, 381) [Pr 110.5; Maombi Aya ya 61]

Dumu kuomba, Hata ikiwa Jibu haliji— Wakati mwingine majibu ya maombi yetu huja mara moja; na wakati mwingine tunalazimika kungojea kwa uvumilivu na kuendelea kuomba kwa dhati na bidii vitu tunavyohitaji, kesi zetu zikiwakilishwa kwa mfano wa mwombezi wa mkate mwenye bidii isiyochoka, aliyeingia kwa ghafla nyumbani mwa mtu usiku. "Ni yupi kati yenu ambaye atakuwa na rafiki, na atamwendea usiku wa manane," nk.

Somo hili lina maana zaidi ya vile tunavyoweza kufikiria. Tunapaswa kuendelea kuomba, hata ikiwa hatuyaoni majibu ya haraka kwa maombi yetu. Kwa hiyo, Mimi nawaambieni, ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa. Maana yeyote aombaye hupewa, atafutaye hupata na abishaye hufunguliwa. Luka 11: 9, 10. [Pr 111.1; Maombi Aya ya 62]

Tunahitaji neema, tunahitaji kuangaziwa na Bwana, ili kupitia kwa Roho Wake tuweze kujua jinsi ya kuomba yale mambo ambayo tunayahitaji. Hebu Bwana na ayaandike maombi yetu kwa ufanisi na kwa ukubali Wake, na kisha ayajibu.— (Counsels on Health, 380) [Pr 111.2; Maombi Aya ya 63]

Majibu Yanacheleweshwa ili kufunua Ubinafsi Wetu — Yeye aliyembariki mtu mwenye cheo wa Kapernaumu anataka kutubariki sisi pia. Lakini kama baba aliyeteseka, mara nyingi tunaongozwa kumtafuta Yesu kwa shauku ya kujipatia mema ya kidunia; na katika kutoa ombi letu, tunaweka imani yetu katika upendo Wake. Mwokozi anatamani kutupa baraka kubwa kuliko tunavyoomba; Naye huchelewesha jibu la ombi letu ili atuonyeshe uovu ulio mioyoni mwetu wenyewe, na hitaji letu kubwa la neema Yake. Yeye Anatamani tuukane ubinafsi, na hii itatuongoza kumtafuta Yeye. Tukiri kutojiweza kwetu na hitaji letu chungu, tunapaswa kujidondosha kikamilifu kabisa katika upendo Wake, tukimtegemea na kumwamini Yeye. [Pr 111.3; Maombi Aya ya 64]

Mtu huyu mwenye cheo alitaka kuona utimilifu wa maombi yake kabla ya kuamini; lakini ilimbidi akubali Neno la Yesu kwamba ombi lake lilisikilizwa na baraka zikatolewa. Sisi nasi tunapaswa kujifunza somo hili pia. Sio kwa sababu tunaona au kuhisi kwamba MUNGU anatusikia ndio tunapaswa kuamini. Tunapaswa kuziamini ahadi Zake. Tunapomjia kwa imani, kila ombi huingia moyoni mwa MUNGU. Tunapokuwa tumeomba baraka Yake, tunapaswa kuamini kwamba tumeipokea, na kumshukuru kwamba tumeipokea. Halafu tunapaswa kuendelea na majukumu yetu, tukiwa na hakika kwamba baraka itapatikana wakati tutapokuwa na uhitaji zaidi. Tutakapokuwa tumejifunza kufanya hivi, tutajua kwamba maombi yetu yanajibiwa. MUNGU atatutendea kwa kupita kipimo na ukarimu "sana",

"kulingana na utajiri wa utukufu Wake," na "utendaji wa nguvu Zake kuu." Waefeso 3:20, 16; Waefeso 1:19 .– (The Desire of Ages, 200) [Pr 112.1; Maombi Aya ya 65]

Maombi yanayoonekana kutojibiwa Yanaweza Kuwa Kati ya Baraka Zetu Kubwa Zaidi – Katika kujali Kwake kwa upendo na masilahi mema kwetu, mara nyingi Yeye ambaye anatuelewa sisi vizuri zaidi ya sisi tunavyojielewa wenyewe hukataa kuturuhusu kujiridhisha wenyewe na ubinafsi na matamania ya ukuu. Yeye hatupi leseni kuyapita majukumu matakatifu ya nyumbani ambayo yanayoonekana kuwa hayavutii ila yapo karibu nasi. Mara nyingi majukumu haya yanatoa mafunzo muhimu sana katika kututayarisha kwa kazi ya juu zaidi. Mara nyingi mipango yetu inashindwa/inafeli ili mipango ya MUNGU kwetu ifanikiwe. [Pr 112.2; Maombi Aya ya 66]

Kamwe hatujaitwa kutoa kafara halisi kwa MUNGU. Kuna vitu vingi ambavyo Yeye anavyotuomba tuvisalimisha Kwakei, lakini kwa kufanya hivyo tunatoa kile kinachotuzuia katika njia ya kwenda mbinguni. Hata tunapoombwa kusalimisha vitu ambavyo kwa vyenyewe ni vyema, tunaweza kuwa na uhakika kwamba MUNGU anafanya kazi kwa mema mengine za juu zaidi kwetu. Mara nyingi mipango yetu hufeli ili mipango ya Mungu ifanikiwe. [Pr 112.3; Maombi Aya ya 67]

Katika maisha ya baadaye mafumbo na siri ambazo hapa zimetukasirisha au kutupa usumbufu na kutukatisha tamaa zitawekwa wazi. Tutagundua kwamba maombi yetu yaliyoonekana kutokuwa na majibu na matumaini au matarajio yetu yaliyokatishwa tamaa, hayo yamekuwa miongoni mwa baraka zetu kubwa. [Pr 112.4; Maombi Aya ya 68]

Tunapaswa kuzingatia kila wajibu kama ni mtakatifu, hata uwe ni wa unyenyekevu au umasikini wa kiasi gani, kwa sababu ni sehemu ya huduma ya MUNGU. Maombi yetu ya kila siku yanapaswa kuwa, “Bwana, nisaidie kufanya bidii kwa kadiri navyoweza. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo wa Mwokozi.” (The Ministry of Healing, 473, 474) [Pr 112.5; Maombi Aya ya 69]

Wakati mwingine MUNGU Hatupi Tunachoombea Kwa sababu Ana Kitu Bora zaidi Kwetu – Tunapokuja Kwake tunapaswa kuomba ili tuweze kuingia na kutimiza kusudi Lake, na kwamba matamano yetu na masilahi yetu yazame/yapotee ndani Yake. Tunapaswa kutambua ukubali wetu kwa mapenzi Yake, sio kumuomba akubaliane na mapenzi yetu. Ni afadhali kwetu kwamba MUNGU huwa hajibu maombi yetu kila wakati pale ambapo tunaanza kutaka kitu, na kwa namna tunayotaka. Yeye Atatufanyia zaidi, na mazuri kuliko kutimiza matakwa yetu yote, kwani hekima yetu ni upumbavu. - (Testimonies for the Church 2:148) [Pr 113.1; Maombi Aya ya 70]

Lile Ombi la dhati litokalo moyoni kwa bidii na Imani lina ufanisi, usiochoka, wenye manufaa, na msaada wa hali ya juu. MUNGU hajibu maombi yetu kila mara kama sisi tunavyotarajia, kwani tunaweza tusiombe kile kilicho bora zaidi kwetu; bali kwa upendo na hekima Yake isiyopimika, Yeye atatupatia vile vitu ambavyo ndivyo tunavyovihitaji sana. - (Testimonies for the Church 4:531) [Pr 113.2; Maombi Aya ya 71]

Tunapaswa Kushirikiana na MUNGU Katika Kujibu Maombi Yetu – Katika Neno la MUNGU zimewasilishwa pande mbili zinazoshindana ambazo zinaathiri na kudhibiti mashirika ya kibinadamu katika ulimwengu wetu. Mara kwa mara vyama hivi vinafanya kazi na kila mwanadamu. Wale ambao wako chini ya udhibiti wa MUNGU na ambao wanaongozwa na malaika wa mbinguni, wataweza kutambua hila za nguvu zisizoonekana za giza. Wale ambao wanataka kuwa sawa na wakala wa mbinguni wanapaswa kuwa wenye bidii sana kufanya mapenzi ya MUNGU. Yabidi wasimpe nafasi yoyote Shetani na malaika zake. [Pr 113.3; Maombi Aya ya 72]

Lakini tusipokuwa macho kila wakati, tutatwezwa na adui. Ingawa ufunuo makini wa mapenzi ya MUNGU juu yetu umefunuliwa kwa wote, lakini ujuzi wa mapenzi Yake hauweki kando ulazima wa kutoa maombi ya dhati Kwake kwaajili ya msaada, na kwa bidii kutafuta kushirikiana Naye katika kujibu maombi yaliyotolewa. Yeye hutimiza makusudi Yake kupitia vyombo vya kibinadamu. - (SDA Bible Commentary 6: 1119) [Pr 113.4; Maombi Aya ya 73]

Sala bila kuutoa moyo kikamilifu haitaleta Majibu (maombi ya moyo nusu- nusu)-MUNGU Atakuwa kila kitu kwetu kwa kadiri tunavyomruhusu Awe. Maombi yetu yenye unyonge, yasiyoutoa moyo kikamilifu hayatatuletea majibu kutoka mbinguni. Oh, tunahitaji kuweka usongo/bidii katika kuwasilisha ombi letu! Omba kwa imani, subiri kwa imani, pokea kwa imani, shangilia kwa matumaini, kwani kila mtu atafutaye hupata. Kuwa na bidii na unyofu katika jambo hilo. Mtafute MUNGU kwa moyo wote. Watu huweka moyo wote na bidii katika kila kitu wanachofanya kwenye vitu vya muda mfupi vipitavyo, hadi juhudi zao zitakapofanikiwa. Kwa bidii nzito jifunze stadi na shuguli ya kutafuta baraka nyingi ambazo MUNGU ameahidi, na kwa uvumilivu, kwa juhudi zenye bidii na kuazimia, wewe utakuwa na nuru Yake na Ukweli Wake na neema Yake nyingi. [Pr 114.1; Maombi Aya ya 74]

Kwa unyofu wa moyo, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Pigana mieleka na mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Weka moyo na utu wako wote mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, na amua kwa kuvalia njuga kwa kuwa wakala mpendwa aliyejiweka wakfu, akiongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na aliyejazwa na Roho Wake (akichajiwa na Roho Mtakatifu). [Pr 114.2; Maombi Aya ya 75]

Mwambie Yesu matakwa yako kwa unyofu wa roho yako. Hautakiwi kutoa hoja ndefu au mabishano, au kutoa hubiri kwa MUNGU (usimhubiri Mungu), lakini kwa moyo wa huzuni juu ya dhambi zako, wewe sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi unaosagasaga roho, utapata baraka ya amani ya Kristo. –(Our High Calling, 131) [Pr 114.3; Maombi Aya ya 76]

Ombi la Msamaha Daima Hujibiwa Papo hapo – Katika visa vingine vya uponyaji, Yesu hakutoa baraka iliyotafutwa pale pale. Lakini katika kisa cha ukoma, ombi lilijibiwa punde mara tu baada ya wito wa kusihhi uponyaji ulipotolewa. Tunapomba baraka za kidunia, jibu la maombi yetu linaweza kucheleweshwa, au MUNGU anaweza kutupa kitu kingine zaidi ya kile tunachoomba, lakini si hivyo pale tunapomba ukombozi kutoka dhambini. Ni mapenzi Yake kututakasa dhidi ya dhambi, na

kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. “Kristo alijitoa Mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu ili apate kutuokoa katika ulimwengu huu wenye uovu kwa sasa, kulingana na mapenzi ya MUNGU na Baba yetu. Wagalatia 1: 4. "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Atusikia; na kama tukijua kwamba asikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15. "Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi MUNGU ni Mwaminifu na wa Kweli, Naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote." 1 Yohana 1: 9— (The Desire of Ages, 266) [Pr 114.4; Maombi Aya ya 77]

Kristo Huwasilisha Maombi Yetu Mbele ya Baba kama Ombi Lake Mwenyewe— Mara tu mtoto wa MUNGU anapokaribia kuingia kwenye Kiti cha Rehema, yeye anakuwa mteja wa Wakili mkuu. Katika kutamka kwake kwa mara ya kwanza toba na kuomba msamaha Kristo, anaikaribisha kesi yake kwa kuikubali na kuifanya iwe Yake Mwenyewe, akiwasilisha ombi mbele ya Baba Yake kama ombi Lake Mwenyewe. - (Testimonies for the Church 6:364) [Pr 115.1; Maombi Aya ya 78]

Omba Kumshukuru na Kumsifu MUNGU kwa ajili ya Maombi Yaliyojibiwa- Katika sura ya pili ya 1 Samweli imeandikwa sala ya mwanamke aliyejitoa bila kuchoka, na ambaye alimtumikia na kumtukiza MUNGU. Aliomba: "Moyo wangu wamshangilia BWANA, Pembe yangu imetukuka katika BWANA, Kinywa changu kimepanuka juu ya adui zangu; Kwa kuwa naufurahia wokovu Wako". Hakuna mtakatifu kama Bwana, kwa kuwa hakuna mwingine isipokuwa Yeye, wala hakuna mwamba kama MUNGU wetu." Sadaka ya Shukrani ya Hana kwa ajili ya jibu la maombi yake ni somo kwa wale ambao leo wanapokea majibu ya maombi yao. Je! Sisi tunapuuzia kurudisha sifa na shukrani kwa MUNGU kwa fadhili Zake za upendo? [Pr 115.2; Maombi Aya ya 79]

Daudi anatangaza, “Nampenda Bwana, kwa sababu amesikia sauti yangu na dua zangu. Kwa sababu amenitegea sikio Lake, kwa hivyo nitamwita maadamu ninaishi.” Wema wa MUNGU katika kusikia na kujibu maombi, hutuweka chini ya jukumu zito la kuonyesha shukrani zetu kwa neema tulizopewa (kwa mdomo na matendo). Tunapaswa kumsifu MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya sasa. Baraka zilizopokelewa katika jibu la

maombi zinapaswa kutambuliwa mara moja kwa ushuhuda wa mdomo na katika maisha. Kumbukumbu zake zinapaswa kuwekwa katika shajara yetu, ili tunapokishika kitabu hicho cha kumbukumbu mkononi, tuweze kukumbuka wema wa Bwana, na kulisifu Jina Lake takatifu. - (The Review and Herald, Mei 7, 1908) [Pr 115.3; Maombi Aya ya 80]

SURA YA 12

MAOMBI NA UAMSHO

Uamsho Utakuja Tu Kama Jibu La Maombi – Uamsho wa utauwa wa Kweli miongoni mwetu ndio hitaji kubwa na la dharura kuliko mahitaji yetu yote. Kuutafuta uamsho huu inapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza. Lazima ziwepo juhudi za dhati kujitwalia baraka ya Bwana kwetu, sio kwa sababu MUNGU Hayuko tayari kutumwagia baraka Yake, lakini kwa sababu sisi hatujajiandaa kuipokea. Baba yetu wa Mbinguni Yuko tayari kuwapatia Roho Wake Mtakatifu wale wanaomwomba, kuliko ambavyo wazazi wa hapa duniani walivyo tayari kutoa zawadi nzuri kwa watoto wao. Lakini ni kazi yetu, kwa kukiri, kujidhili/kujinyenyekeza, kutubu, na kutoa maombi ya dhati na bidii, kutimiza masharti ambayo kwayo MUNGU ameahidi kutupa baraka Yake. Uamsho unapaswa kutarajiwa tu katika jibu la

maombi.—(Selected Messages 1:121) [Pr 116.1; Maombi Aya ya 1]

Leo kuna haja ya uamsho wa dini ya Kweli ya moyoni kama ilivyokuwa kwa Israeli ya zamani. Kama wao, tunahitaji kuzaa matunda yanayofaa kwa toba, - kuweka mbali dhambi zetu, kuziondoa kabisa, kusafisha hekalu lililochafuliwa la moyo ili Yesu aweze kutawala ndani. Kuna haja ya maombi - maombi ya dhati, ya bidii, yasiyochoka, na ya kudumu. Mwokozi wetu ameacha ahadi za thamani kwa mwombaji atubuye kweli. Huyo hatautafuta uso Wake bure. Yeye pia kwa mfano Wake Mwenyewe ametufundisha umuhimu wa maombi. Yeye Mwenyewe, Mfalme wa Mbingu, Mara nyingi alitumia usiku kucha katika ushirika na Baba Yake. Ikiwa Mkombozi wa ulimwengu hakujiona kuwa Yeye ni safi sana, Mwenye busara sana, au mtakatifu sana kutafuta msaada kutoka kwa MUNGU, hakika sisi wanadamu dhaifu, wenye makosa tuna kila hitaji la msaada huo wa Bwana. Kwa toba na imani, kila Mkristo wa kweli atakuwa akitaafuta daima “Kiti cha Neema, ili apate rehema, na kupata neema ya kusaidia wakati wa shida” (The Signs of the Times, January 26, 1882) [Pr 116.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi Hutuleta katika ushirika na MUNGU - Ikiwa tunamwendea MUNGU, tukijisikia hoi, wasiojiweza na tegemezi, kama vile tulivyo kihalisia, na kwa imani ya unyenyekevu na tumaini tukiwasilisha matakwa yetu Kwake Yeye ambaye maarifa Yake hayana kikomo, Yule anayeona kila kitu katika uumbaji, na ambaye anatawala na kuongoza kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, Anaweza na atashughulikia kilio chetu, na ataangazia nuru mioyoni mwetu. Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika mwuunganiko wa ile akili ya Yule Asiye na mwisho. Pengine tunaweza tusiwe na ushahidi unaoonekana kwa namna ya ajabu na wazi wakati ule ambao uso wa Mkombozi wetu umeinama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini huo ndio ukweli wenyewe. Tunaweza tusihisi mguso Wake kwa kuonekana uso kwa uso, yaani dhahiri lakini mkono Wake u juu yetu kwa upendo na huruma yenye sikitiko.—(Steps to Christ, 97) [Pr 117.1; Maombi Aya ya 3]

Maombi yetu hupanda mbinguni kama umande wenye unyevunyevu wa damu ya Kristo itakasayo—Huduma za kidini, kiroho, sala, sifa, kukiri dhambi kwa toba, hupanda juu kutoka kwa waumini wa kweli kama uvumba kwenda

Patakatifu pa mbinguni, lakini kwa kupita katika njia oву na fisadi za ubinadamu, hunajisiwa sana kiasi kwamba visipotakaswa kwa damu, kamwe haviwezi kuwa vya thamani kwa Mungu. Hukwea juu vikiwa na waa na madoa hivyo pasipo Mwombezi, aliye Mkono wa Kuume wa Mungu ili kuwasilisha na kutakasa vyote kwa Haki Yake, hayakubaliki kwa Mungu. Uvumba wote kutoka madhabahu za kidunia, lazima uwe na umande wa matone ya utakaso wa damu ya Kristo. Mbele Zake Baba. Yeye Anashikilia chetezo cha haki na sifa Zake Mwenyewe, ambamo ndani yake hakuna uchafu wa rushwa au uфisadi wa kidunia. Yeye Hukusanya maombi sifa na maungamo ya watu Wake ndani ya chetezo hiki na pamoja nayo huweka Haki Yake isiyo na doa. Ukiwa na harufu ya manukato ya sifa za upatanishi wa Kristo, uvumba huu huja na mbele za Mungu moja kwa moja na kwa ukamilifu tayari kwa kukubalika kabisa. Kisha, majibu yenye Neema hurudishwa. - (Selected Messages 1:344) [Pr 117.2; Maombi Aya ya 4]

Katika Maombi Twahisi Uwepo wa Yesu – Iwapo tutamweka Bwana mbele yetu daima, tukaruhusu mioyo yetu kwenda kumshukuru na kumsifu, tutafanywa upya katika maisha yetu ya kiroho/kidini. Maombi yetu yachukua mfumo wa mazungumzo na MUNGU kama ambavyo tungezungumza na rafiki. Atazungumza nasi kuhusu mafumbo na siri Zake. Hisia nzuri za shangwe ya uwepo wa Yesu zitatumia mara kwa mara.—(Christ's Object Lessons, 129) [Pr 118.1; Maombi Aya ya 5]

Roho Mtakatifu alikuja wakati wa Pentekoste Kama Jibu La Maombi – Roho alikuja juu ya wanafunzi wanaosubiri, wanaosali kwa utimilifu uliofikia kila moyo. Yule asiye na mwisho alijifunua katika uongozi kwa kanisa Lake. Ilikuwa kana kwamba kwa miaka mingi ushawishi huu ulikuwa umezuiliwa, na sasa mbingu ilifurahi kumwaga juu ya kanisa utajiri wa neema ya Roho. Na, chini ya ushawishi wa Roho, maneno ya toba na kukiri yalichanganywa na nyimbo za kumsifu Mungu kwa ajili ya dhambi zilizosamehewa. Maneno ya shukrani na ya unabii yalisikika. Mbingu zote ziliinama chini kutazama na kuabudu hekima ya Upendo usiolinganishwa, usioelezeka/usioeleweka na binadamu. Wakiwa wamepotelea katika mshangao, wakiwa wametekewa, mitume wakasema, "Hapa pana upendo." Walishika na

kuilewa zawadi waliyopewa. Na nini kilifuata basi? Upanga wa Roho, ukiwa umenolewa na nguvu na kusafishwa na umeme wa mbinguni, nao ulikatakata hali ya kutokuamini. Maelfu wakaongolewa siku ile.—(The Acts of the Apostles, 38) [Pr 118.2; Maombi Aya ya 6]

Tunapaswa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kama walivyofanya Wanafunzi katika Pentekoste — Moyo lazima ukungutwe kila punje ya unajisi na kusafishwa kwa ajili ya kukaa kwa Roho. Ilikuwa kwa kuungama na kuacha dhambi, kwa kuomba kwa dhathi na bidii na kujitoa wakfu kikamilifu wenyewe kwa MUNGU, ndivyo wanafunzi wa awali walivyojiandaa kwa ajili ya kumwagiwa kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste. Kazi hiyo hiyo, lakini kwa kiwango kikubwa zaidi, lazima ifanyike sasa.... [Pr 118.3; Maombi Aya ya 7]

Pasipo kusonga mbele katika kielelezo cha fadhila za Kikristo kila siku, hatutaweza kutambua udhihirisho wa Roho Mtakatifu katika mvua ya masika. Inaweza kuwa ikianguka kwenye mioyo ya wengine kila mahali kutuzunguka, lakini sisi hatutatambua au kupokea.... [Pr 119.1; Maombi Aya ya 8]

Neema ya Mungu inahitajika mwanzoni, neema ya Bwana inahitajika katika kila hatua ya mafanikio, na neema ya Mungu pekee ndiyo inaweza kumaliza kazi hiyo. Hakuna nafasi kwetu sisi kubweteka na mielekeo ya kizembezembe. Kamwe tuisahau maonyo ya Kristo, "Kesha katika maombi," "daima.....kesha na uombe" Kuungana na wakala wa kimbingu kila nukta ni muhimu kwa maendeleo yetu. Yawezekana tuliwahi kupata kipimo fulani cha Roho wa MUNGU huko nyuma, lakini kwa maombi na imani tunapaswa kuendelea kuomba ili tuwe na Roho zaidi. — (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 507, 508) [Pr 119.2; Maombi Aya ya 9]

Tunapaswa kuomba kwa bidii kwa ajili ya kushuka kwa Roho Mtakatifu kama wanafunzi walivyoomba siku ya Pentekoste. Ikiwa walimhitaji Roho wakati huo, basi sisi tunamhitaji zaidi leo. [Pr 119.3; Maombi Aya ya 10]

Bila Roho na nguvu ya MUNGU, kujitahidi kwetu kuwasilisha Ukweli itakuwa ni kazi bure tu.—((Australasian) Union Conference Record, April 1, 1898) [Pr 119.4; Maombi Aya ya 11]

Dai Ahadi ya Roho kwa Imani – Ni kwa wale tu ambao humngojea MUNGU kwa unyenyekevu, wale ambao hutazama Uongozi na neema Yake, ndio hupewa huyo Roho. Nguvu ya MUNGU inasubiri takwa lao na mapokezi. Baraka hii ya Roho Mtakatifu iliyoahidiwa, na kudaiwa kwa imani, huleta baraka zingine zote kwenye mlolongo wa mabehewa yake, kama ilivyo treni inaposafiri. Inatolewa kulingana na utajiri wa rehema za Kristo, na Yeye Yuko tayari kuipatia kila nafsi kulingana na uwezo wa kupokea kwake mtu. –(The Desire of Ages, 672) [Pr 119.5; Maombi Aya ya 12]

Ombea Mvua ya masika-Lazima tuombe ili MUNGU afungue chemchemi ya maji ya uzima. Na lazima sisi wenyewe tupokee maji ya uzima. Hebu sisi, kwa mioyo mikunjufu na uliopondeka, tuombe kwa dhati na bidii ili sasa, wakati wa mvua ya masika, mvua za neema ziweze kutuangukia. Katika kila mkutano tunaohudhuria, sala zetu zinapaswa kupanda juu, ili wakati kama huu MUNGU atoe joto na unyevunyevu kwenye roho zetu. Tunapomtafuta MUNGU kwa ajili ya Roho Mtakatifu, atafanya kazi ndani yetu kuwa wapole, unyenyekevu wa nia n aakili, kumtegemea MUNGU kwa ajili ya kupata mvua ya masika. Ikiwa tunaomba baraka kwa imani, tutapokea kama vile MUNGU alivyoahidi. –(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 508) [Pr 119.6; Maombi Aya ya 13]

Uwe na ari katika Maombi na katika Uwezo wa Roho Mtakatifu – Tunachohitaji ni ushawishi wa Roho Mtakatifu wa MUNGU uhuishao. "Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi." Omba bila kukoma, na kesha ukifanya kazi kulingana na maombi yako. Unapomba, amini, mtumaini MUNGU. Ni wakati wa mvua ya masika, wakati ambao Bwana atatoa kwa kiasi kikubwa Roho Wake. Dumu katika maombi kwa shauku kubwa, na kesha katika Roho- (Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 512) [Pr 120.1; Maombi Aya ya 14]

Shetani Huogopa watu wa MUNGU wanaomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu- Hakuna kitu ambacho humogofya Shetani kama habari kuwa watu wa MUNGU watafungua njia kwa kuondoa kila kikwazo, ili Bwana aweze kumwaga Roho Wake juu ya kanisa lenye uchovu na kutaniko ambalo halijafanya toba. Ikiwa Shetani angelikuwa na njia yake, hakungekuwa na uamsho mwingine, mkubwa au mdogo,

hadi mwisho wa wakati. Lakini sisi si wajinga katika kutambua hila zake. Inawezekana kuzipinga nguvu zake. Pale njia ipoandaliwa kwa ajili ya Roho wa MUNGU, baraka itakuja. Shetani hawezi kuzuia mvua ya baraka zisishuke juu ya watu wa MUNGU kama vile asivyoweza kufunga madirisha ya mbinguni ili mvua isiweze kufikia watu duniani. Watu waovu na mapepo/mashetani hawawezi kuzuia kazi ya MUNGU, au kufungia uwepo Wake kwenye mikusanyiko ya Watu Wake, Ikiwa kwa mioyo iliyotiishwa, yenye toba na kupondeka, watakiri na kuachana na dhambi zao, na kudai ahadi Zake kwa Imani. —(Selected Messages 1:124) [Pr 120.2; Maombi Aya ya 15]

Roho Huandamana na Kila Ombi la Dhati — Dini inayotoka kwa MUNGU ndiyo dini pekee itakayoongoza kumuelekea MUNGU. Ili kumtumikia Yeye sawasawa, lazima tuzaliwe na Roho Mtakatifu. Hii itasafisha moyo na kufanya upya akili, ikitupatia uwezo mpya wa kumjua na kumpenda MUNGU. Itatupa utii wa hiari kwa matakwa Yake yote. Hii ndio ibada ya Kweli. Ni tunda la utendaji wa Roho Mtakatifu. Kwa Roho kila sala ya dhati inaandikwa na kupewa ukubali Wake, na sala kama hiyo inakubalika kwa MUNGU. Mahali popote ambapo roho inamfuata MUNGU, hapo utendaji wa Roho unadhihirika, na MUNGU atajifunua kwa nafsi hiyo. Kwa maana Yeye Bwana anawatafuta wale wamwabuduo namna hii. Yeye anangojea kuwapokea, na kuwafanya wana na binti Zake. —(The Desire of Ages, 189) [Pr 120.3; Maombi Aya ya 16]

Maombi bila Shughuli iliyo dhati na ya Bidii kwa ajili ya watu Wengine husababisha kutumbukia katika mapokeo ya urasmi— MUNGU hamaainishi kwamba yeyote miongoni mwetu lazima awe mtawa aliyejitenga na watu au anayetoroka watu na kukaa mbali kusiko na watu kabisa (monk or hermit) na kwamba sasa tuukimbie ulimwengu na kujitoa masaa yote kwa vitendo vya ibada tu. Maisha lazima yawe kama maisha ya Kristo, katikati ya mlima na umati (akisali mlimani peke yake na akihudumu kwenye umati). Yule ambaye hafanyi chochote isipokuwa kuomba tu, ataacha kuomba hivi karibuni, au sala zake zitakuwa ni taratibu za mapokeo ya kila siku, kufuata ratiba kavukavu tu, bila moyo kuhusika, na destruri ngumu (rigid rules). Wakati watu wanapojiondoa katika maisha yao na jamii, mbali na uwanja wao wa wajibu wa Kikristo, pamoja na kubeba msalaba; wanapoacha kufanya kazi kwa unyofu na

bidii kwa Bwana, ambaye alifanya kazi kwa dhati na bidii kwa ajili yao, wanapoteza mwelekeo na msingi wa maombi, na wanakosa motisha wa kujitoa wakfu kwaajili ya ibada. Maombi yao huwa yanahusu wao wenyewe na hivyo ya ubinafsi. Hawawezi kuomba kwa kuzingatia matakwa ya wanadamu au kuhusiana na kujengwa kwa ufalme wa Kristo, wakiugua kwaajili ya kupewa nguvu ya kufanya kazi.—(Steps to Christ, 101) [Pr 121.1; Maombi Aya ya 17]

Maendeleo ya Kiroho Hutegemea Maombi — Lazima tudumu katika maombi ikiwa tunahitaji kupiga hatua katika maisha ya Kiungu/mbingu. Wakati ujumbe wa ile Kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, ni kwa kiasi gani tuliomba. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika chumbani, ghalani, kwenye shamba la matunda, au vijisitu. Mara kwa mara tulitumia masaa kwa maombi ya dhati, wawili au watatu pamoja wakadai ahadi; mara nyingi sauti ya kulia ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa. Sasa siku ile ya MUNGU iko karibu kuliko wakati tulipoanza kuamini, na tunapaswa kuwa na unyofu, shauku, ari, na bidii ya kudumu zaidi kuliko siku zile za mwanzo. Hatari tulizo nazo sasa ni kubwa kuliko hapo awali.— (Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 121.2; Maombi Aya ya 18]

SURA YA 13

WANAUME NA WANAWAKE WA MAOMBI

Henoko

Maombi yalikuwa Pumzi ya Nafsi Yake – kwa kuwasiliana na MUNGU, Henoka alizidi kuakisi sura ya Mungu. Uso wake ulikuwa uking'aa na nuru takatifu, hata ile nuru inayoangaza usoni mwa Yesu. Alipokuwa akitoka kwenye mawasiliano/mazungumzo haya na Bwana, hata wale wasiompanda Mungu (makafiri) walitazama kwa mshangao mkubwa mvuto (muhuri) wa mbinguni juu ya uso wake. [Pr 122.1; Maombi Aya ya 1]

Imani yake ilizidi kuimarika, upendo wake ukawa wenye shauku kali zaidi (enthusiasm), ukidumu kwa karne nyingi. Kwake maombi yalikuwa kama pumzi ya roho. Aliishi katika angahewa la mbinguni. - (Gospel Workers, 52) [Pr 122.2; Maombi Aya ya 2]

Akifadhaishwa na uovu uliokithiri wa wale wasiomcha MUNGU, na akiogopa kwamba kukosa uadilifu kwao kungeweza kupunguza kicho chake kwa MUNGU, Henoka aliepuka kushirikiana nao mara kwa mara, na alitumia muda mwingi akiwa amejitenga peke yake, akajitoa wakfu kwa tafakari na sala. Hivyo ndivyo alivyojihudhurisha mbele za Bwana, akitafuta maarifa wazi ya mapenzi Yake, kwa makusudi ya kuyatimiza. Kwake maombi yalikuwa kama pumzi ya roho; aliishi katika angahewa ya mbinguni. - (Patriarchs and Prophets, 85) [Pr 122.3; Maombi Aya ya 3]

Henoka Alitembea Na MUNGU Kupitia Maombi – Natamani ningeweza kumhimiza/kumhamasisha kila mtendakazi katika kazi ya MUNGU, hitaji kuu la sala ya kudumu na ya bidii. Hawawezi kupiga magoti daima, lakini wanaweza kuendelea kuinua mioyo yao kwa MUNGU. Hii ndio njia ambayo Henoka alitembea na MUNGU. - (The Review and Herald, Novemba 10, 1885) [Pr 123.1; Maombi Aya ya 4]

Wakati tunafanya kazi zetu za kila siku, tunapaswa kuinua mioyo yetu mbinguni kwa ajili ya maombi. Maombi haya ya kimyakimya, hupanda kama uvumba mbele ya kiti cha neema; na adui hupatwa na mshtuko wa fadhaa. Mkristo ambaye moyo wake umekaa kwa MUNGU hawezi kutindikiwa. Hakuna sanaa za uovu au giza ambazo zinaweza kuharibu amani yake. Ahadi zote za Neno la MUNGU, nguvu zote za neema ya Bwana, rasilimali zote za Yehova, zimeahidiwa kama uhakikisho wa ukombozi Wake. Ilikuwa kwa jinsi hiyo ndiyo Henoka alivyotembea na

MUNGU. Na MUNGU alikuwa pamoja naye, msaada ulio tele wakati wa mateso au mahitaji. - (Messages to Young People, 249) [Pr 123.2; Maombi Aya ya 5]

Watu Walimtafuta Henoka kwa ajili ya Maombi – Henoka alikua mhubiri wa haki, akiwajulisha watu kile ambacho MUNGU alikuwa amemfunulia. Wale waliomcha Bwana walimtafuta mtu huyu mtakatifu, ili ashiriki nao maagizo yake na sala zake. - (Patriarchs and Prophets, 86) [Pr 123.3; Maombi Aya ya 6]

Kadiri kazi ya Henoka ilivyozidi kuwa kubwa, ndivyo Maombi yake yalivyokuwaya dhati na bidii zaidi – Katika maisha ya kazi ya bidii, Henoka alidumisha uhusiano wake na MUNGU. Kadiri kazi yake ilivyokuwa kubwa na kupata msukumo zaidi, ndivyo maombi yake yalikuwa ya kudumu na ya dhati, usadikisho na bidii zaidi. Aliendelea kujitenga mwenyewe, katika vipindi fulani, mbali na jamii yote. Baada ya kukaa kwa muda kati ya watu, akitenda kazi ili kuwanufaisha kwa kuwafundisha na kutoa mfano, alijitenga, kutumia msimu katika upweke, akiwa na njaa na kiu ya maarifa ya Bwana ambayo MUNGU peke yake Ndiye anayeweza kuyatoa. - (Patriarchs and Prophets, 86, 87) [Pr 123.4; Maombi Aya ya 7]

Abrahamu

Maombi ya kila siku yanapaswa kupaa kwa MUNGU kama ubani unaonukia— Maisha ya Ibrahimu, rafiki wa MUNGU, yalikuwa maisha ya maombi. Kila mahali alipopiga hema lake, karibu naye ilijengwa madhabahu, ambayo juu yake ilitolewa dhabihu ya asubuhi na ya jioni. Wakati hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Na Mkanaani aliyekuwa akirandaranda au akihamahama huko na kule, alipofika kwenye madhabahu hiyo, alijua ni nani aliyekuwepo hapo. Naye huyu mkanani alipopiga hema lake aliikarabati ile madhabahu na kumwabudu MUNGU Aliye hai. [Pr 123.5; Maombi Aya ya 8]

Hivyo ndivyo nyumba za Wakristo zinapaswa kuwa taa ulimwenguni leo. Kutoka humo, asubuhi na jioni, sala inapaswa kupanda juu kwa MUNGU kama uvumba unaonukia. Na kama umande wa asubuhi, rehema Zake na

baraka zitashuka juu ya waombaji. [Pr 124.1; Maombi Aya ya 9]

Akina baba na akina mama, kila asubuhi na jioni wakusanye watoto wako karibu na wewe, na kwa dua ya unyenyekevu inua moyo kwa MUNGU kwa ajili ya msaada. Wapendwa wako wanaanikwa kwenye majaribu. Kero za kila siku zinasonga njia ya vijana na wazee. Wale ambao wataishi maisha ya uvumilivu, ya upendo, na uchangamfu lazima waombe. Ni kwa kupokea msaada wa kila wakati kutoka kwa MUNGU ndipo tunaweza kupata ushindi juu ya nafsi yetu. [Pr 124.2; Maombi Aya ya 10]

Kila asubuhi jiwekeni wakfu kwa MUNGU na watoto wenu kwa ajili ya siku hiyo. Msifanye mahesabu ya miezi au miaka; hiyo sio yenu. Wewe umepewa siku moja fupi, kama vile ndio siku yako ya mwisho duniani, fanya kazi kwa Bwana katika masaa hayo. Weka mipango yako yote mbele za MUNGU, ili itekelezwe au ihahirishwe, kama vile maagizo Yake Mungu yatakavyoelekeza. Kubali mipango Yake badala mipango yako mwenyewe, hata kama kuikubali mipango Yake, kutakuhitaji wewe kuiacha miradi unayoipenda. Ndipo maisha yako yatatengenezwa/yatafinyangwa zaidi na zaidi katika mfano wa Kiungu/mbingu; "Na amani ya MUNGU, ipitayo akili zote, italinda mioyo yenu na akili zenu kupitia Kristo Yesu." Wafilipi 4: 7 .— Testimonies for the Church (7:44) [Pr 124.3; Maombi Aya ya 11]

Ibrahimu aliomba kwa Imani licha ya mazingira yenye changamoto – Ibrahimu hakuweza kuelezea mwongozo au majaliwa ya Mungu; alikuwa hajajua matokeo yatakuwaje; lakini alishikilia ile ahadi, “nitakubariki, na kulitukuza Jina Lako; nawe utakuwa baraka.” Kwa maombi ya dhati alifikiria jinsi ya kuhifadhi maisha ya watu wake na mifugo yake, lakini hakuruhusu mazingira yale yatikise imani yake katika Neno la MUNGU. - (Conflict and Courage, 45) [Pr 124.4; Maombi Aya ya 12]

Ibrahimu alimwomba MUNGU kwa Ujasiri wa Mtoto, Akamsihi Baba Yake -Wajumbe wawili wa mbinguni waliondoka, wakimwacha Ibrahimu peke yake na Yeye ambaye sasa alijua kuwa ni Mwana wa MUNGU. Na yule mtu wa imani alisihi, yaani alifanya maombezi kwa wakaaji wa Sodom. Siku za awali alikuwa amewaokoa kwa upanga

wake, na sasa alijitahidi kuwaokoa kwa sala. Lutu na nyumba yake walikuwa bado wakazi huko; na upendo usio na ubinafsi ndio uliomsukuma Ibrahimu kuwaokoa kutoka kwa Waelamu, sasa ulitafuta kuwaokoa kutoka kwenye dhoruba ya hukumu ya Bwana, ikiwa ni kwa mapenzi ya MUNGU (Mwanzo 14). [Pr 124.5; Maombi Aya ya 13]

Kwa heshima kubwa na unyenyekevu alitoa ombi lake: "Nimejitolea kusema na Bwana, mimi ambaye ni mavumbi na majivu tu." Hakukuwa na kujiamini mwenyewe, wala kujisifu kwa haki yake mwenyewe. Yeye hakudai upendeleo kwa sababu ya utii wake, au dhabihu alizotoa kwa kufanya mapenzi ya MUNGU. Mzee huyu, ambaye mwenyewe akiwa mwenye dhambi, aliomba rehema kwa niaba ya mdhambi. Roho kama hiyo tunapaswa kumiliki wote tunaomkaribia MUNGU. Walakini Ibrahimu alionyesha ujasiri wa mtoto anayemwomba baba yake mpendwa. Alimkaribia Mjumbe wa mbinguni, na akahimiza ombi lake kwa bidii.... Pr 125.1; Maombi Aya ya 14]

Upendo kwa roho zinazoangamia ulimsukuma/ulimbidisha Ibrahimu kusihhi. Wakati alikuwa anachukia dhambi za mji huo wenye ufiadini, matamano yake yalikuwa kwamba wenye dhambi waweze kukolewa. Kuijali kwake Sodoma kwa kina kunaonyesha tashwishwi ambayo tunapaswa kuhisi kwa wale wasiotubia dhambi zao. Tunapaswa kuichukia dhambi mioyoni mwetu, lakini kumwonea huruma na kumpenda mwenye dhambi. - (Patriarchs and Prophets, 139, 140) [Pr 125.2; Maombi Aya ya 15]

Yakobo

Uzoefu wa Yakobo Unafundisha Umuhimu wa ombi linaloshinda, lisilochoka. lenye bidii na linaloleta ushawishi kwa wengine (prevailing prayer) – Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa mvumilivu na mwenye kuazimia. Uzoefu wake unathibitisha nguvu ya sala ya ustahimilivu, na ya dharura, yenye kusihhi kwa imani bila kuchoka, mpaka majibu yapatikane (importunate prayer). Wakati huu ndio wa kujifunza somo hili la ombi linaloshinda, lenye bidii, lisilochoka, na lisilokata tamaa mpaka majibu yapatikane. Ushindi mkubwa kwa kanisa la Kristo au kwa Mkristo mmoja mmoja sio ule unaopatikana kwa talanta au elimu, kwa

utajiri au upendeleo wa watu. Bali ni ushindi ambao hupatikana katika chumba cha hadhira na MUNGU, wakati imani yenye dhati na yenye bidii, yenye uchungu inashikilia mkono wa Yule aliye mkuu na Mwenye nguvu zote. [Pr 125.3; Maombi Aya ya 16]

Wale ambao hawataki kutelekeza au kutupilia mbali kila dhambi na kutafuta kwa bidii baraka za MUNGU, basi hawatazipata. Lakini wote watakaoshika ahadi za MUNGU kama alivyofanya Yakobo, na kuwa na bidii na uvumilivu kama yeye, watafaulu kama yeye alivyofaulu. - (Patriarchs and Prophets, 203) [Pr 125.4; Maombi Aya ya 17]

Musa

Fuata Mfano wa Musa katika kuomba— Ongea kidogo (fanya magumzo kwa uchache sana); wakati wa thamani unapotea katika mazungumzo ambayo hayana nuru. Hebu ndugu waungane katika kufunga na kuombea hekima ambayo MUNGU ameahidi kuitoa kwa kila mtu na kwa ukarimu. Mjulishe MUNGU shida zako. Mwambie, kama alivyofanya Musa, "Siwezi kuwaongoza watu hawa mpaka uwepo Wako utakapoenda nami." Na kisha omba zaidi; omba na Musa, "Nionyeshe utukufu Wako." [Kutoka 33:18.] Utukufu huu ni nini? —Ni Tabia na sifa ya MUNGU. Hivi ndivyo alimtangazia Musa. - (Gospel Workers, 417) [Pr 126.1; Maombi Aya ya 18]

Musa alifanya maombezi yenye Mafanikio kwa ajili ya Israeli - Agano la MUNGU na watu Wake lilikuwa limefutwa, na alimwambia Musa, "Niache, ili hasira Yangu iwake juu yao, na niwaangamize; Nami nitakufanya wewe uwe taifa kubwa." Watu wa Israeli, haswa umati uliokuwa mseto (uliochangamana waisraeli na wamisri), walikuwa wana mwelekeo wa kumuasi MUNGU daima. Pia walilalamika dhidi ya kiongozi wao, na walimuhuzunisha kwa kutokuamini na ukaidi wao, na hivyo ingekuwa kazi ya kutoa jasho na ya kujaribu roho, kuwaongoza mpaka Nchi ya Ahadi. Dhambi zao tayari zilikuwa zimepoteza neema ya MUNGU, na haki ilidai waangamizwe. Kwa hiyo Bwana alipendekeza kuwaangamiza, na kumfanya Musa kuwa taifa lenye nguvu. [Pr 126.2; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 19]

"Niachie Mimi,... ili niwaangamize," yalikuwa Maneno ya MUNGU kwa Musa. Ikiwa MUNGU alikuwa amekusudia kuangamiza Israeli, ni nani angetaka kufanya maombezi kwa niaba yao? Ni wangapi kama si wachache tu ambao wangewaachia wenye dhambi kuikabili hatima yao! Ni wangapi kama si wachache wangepurahi kubadilishana na taabu nyingi na mzigo mzito na kujitoa kafara, kulipwa kwa 'shukurani ya punda mateke' na manung'uniko, kupewa nafasi ya raha na heshima, wakati ni MUNGU Mwenyewe Ndiye aliyekuwa anatoa afueni kwa Musa (Mungu alimruhusu Musa awe huru na uzao wake uendelee! Naye akakataa na kuwaombea watu wake Israeli). [Pr 126.3; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 20]

Lakini Musa alitambua msingi wa tumaini pale ambapo palionekana panavunja moyo na ghadhabu tu. Maneno ya MUNGU, "Niache Mimi," aliyaelewa kama kutomaanisha kumkataza yeye (Musa) bali kumhamasisha afanye maombezi, Akimaanisha kuwa hakuna chochote isipokuwa maombi ya Musa yangeweza kuokoa Israeli, yaani yabidi aombe kwa niaba yao na kwa kufanya hilo, MUNGU angewasamehe watu Wake [Pr 126.4; Maombi Aya ya ; Maombi Aya ya 21]

Kadiri Musa alivyofanya maombezi kwa ajili ya Israeli, unyonge na woga wake ulipotokomea katika shauku yake ya kina na upendo kwa wale ambao aliwaweka mikononi mwa MUNGU, ambaye Ndiye njia ya kufanya mengi. Bwana alisikiza maombi yake, na akajibu maombi yake yasiyo ya ubinafsi. MUNGU alikuwa amemthibitisha mtumishi Wake; Alikuwa amejaribu uaminifu wake na upendo wake kwa watu hao wakosaji, wasio na moyo wa shukurani, na kwa ubora na busara, Musa alivumilia jaribu. Masilahi yake kwa Israeli hayakutokana na nia ya ubinafsi. Ustawi wa watu waliochaguliwa/walioteuliwa na MUNGU ulikuwa wa kupendeza kwake kuliko heshima ya binafsi, wenye kupendeza kuliko fursa ya yeye kuwa baba wa taifa lenye nguvu. MUNGU alifurahishwa na uaminifu wake, unyenyekevu wa moyo, usahili wa moyo, na uadilifu wake, na akamkabidhi yeye, kama mchungaji mwaminifu, jukumu kubwa la kuongoza Israeli kwenda Nchi ya Ahadi. - (Patriarchs and Prophets, 318, 319) [Pr 127.1; Maombi Aya ya 22]

Musa Aliendelea kuwasilisha Maombi yake kwa MUNGU—Musa alijua upotovu na upofu wa wale ambao waliwekwa chini ya uangalizi wake; alijua shida na changamoto anazopaswa kushindana nazo. Lakini alikuwa amejifunza kwamba ili kufanikiwa kuongoza watu hao, lazima awe na msaada kutoka kwa MUNGU. Aliomba ufunuo wazi wa mapenzi ya MUNGU na uhakikisho wa uwepo Wake: “Tazama, unaniambia, Walete watu hawa: na hukunijulisha ni nani utakayemtuma pamoja nami. Lakini umesema, nakujua kwa Jina Lako, nawe umepata neema mbele Zangu. Basi sasa, nakuomba, ikiwa nimepata neema machoni pako, nionyeshe njia Yako, ili nipate kukujua, ili nipate kibali machoni Pako; na zingatia kuwa taifa hili ni watu Wako.” [Pr 127.2; Maombi Aya ya 23]

Jibu lilikuwa, "Uwepo Wangu utaenda nawe, Nami nitakupa raha." Lakini Musa alikuwa bado hajaridhika. kulikuwa na shinikizo la kuogofya juu ya nafsi yake juu ya hisia ya matokeo mabaya ikiwa MUNGU angewaacha Israeli wakutane na maisha magumu na kutojutia dhambi zao. Hakuweza kuvumilia kwamba masilahi yake yatenganishwe na yale ya ndugu zake, na aliomba kwamba neema ya MUNGU irejeshwe kwa watu Wake, na kwamba ishara ya uwepo Wake iendeleo kuongoza safari zao: " Uwepo Wako usipoenda nami, usituchukue kutoka hapa. Kwa maana itajulikanaje hapa kuwa mimi na watu Wako tumepata neema mbele Zako? Je! Si kwa sababu Wewe unaenda pamoja nasi? Basi tutatenganishwa, mimi na watu Wako, dhidi ya watu wote walio juu ya uso wa dunia." [Pr 127.3; Maombi Aya ya 24]

Bwana akasema, "Nitafanya jambo hili pia ulilolinena; kwa kuwa umepata neema mbele Zangu, na nakujua kwa jina." Bado nabii hakuacha kuomba/kusihi. Kila sala ilikuwa imejibiwa, lakini alikuwa na kiu ya ishara kubwa za upendeleo wa MUNGU. Sasa alifanya ombi ambalo hakuna mwanadamu aliyewahi kufanya hapo awali: "Ninakuomba, nionyeshe utukufu Wako." [Pr 128.1; Maombi Aya ya 25]

MUNGU hakulikemea ombi lake kama la kujiamini kwa kupitiliza, au ujasiri potofu na imani bandia isiyofuata mapenzi ya Mungu (au kuonyesha ukaidi au kiburi); lakini maneno ya neema yalisemwa, "Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako." Utukufu uliofunuliwa wa MUNGU, hakuna mtu katika hali hii ya kufa anayeweza kutazama na

kuishi; lakini Musa alihakikishiwa kwamba angeliangalia utukufu wa Mungu kwa kadiri atakavyoweza kuvumilia. Kisha akaitwa tena kwenye kilele cha mlima; halafu Mkono ule ulioumba ulimwengu, ule Mkono "unaoondoa milima, nao watu hawajui" (Ayubu 9: 5), ukambeba kiumbe huyu aliyeumbwa kwa mavumbi tu, mtu huyu hodari wa imani, na kumweka katika pango la mwamba, wakati utukufu wa MUNGU na wema Wake wote ukapita mbele yake. [Pr 128.2; Maombi Aya ya 26]

Uzoefu huu - Zaidi ya yote, ahadi ya kwamba Uwepo wa MUNGU ungemhudumia - kwake Musa ulikuwa ni uhakikisho wa kufanikiwa katika kazi iliyokuwa mbele yake; na aliihesabu hili kuwa lenye thamani isiyopimika kuliko elimu yote ya Misri au mafanikio yake yote kama kiongozi wa serikali au kiongozi wa jeshi. Hakuna nguvu ya kidunia au ujuzi au ujifunzaji unaoweza kuwa mbadala wa uwepo wa MUNGU unaodumu (alikuwa amesoma shahada tano mbalimbali). - (Patriarchs and Prophets, 327, 328) [Pr 128.3; Maombi Aya ya 27]

Chini ya Msongo, Maombi ya Musa yakafanana kama Malalamiko kwa kiasi fulani-Moyo wa Musa ukazama. Alikuwa ameomba kwamba Israeli wasiangamizwe, hata kama kizazi chake kingeweza kuwa taifa kubwa wakati huo. Katika upendo wake kwao alikuwa ameomba kwamba jina lake lifutwe kutoka kitabu cha uzima kuliko waisraeli waachwe na kuangamia. Alikuwa amehatarisha yote kwa ajili yao Wana Israeli, na haya ndiyo yalikuwa majibu yao. Shida zao zote, na hata mateso yao ya kufikirika, watu hao wa Israeli walimtuhumu yeye; na manung'uniko yao mabaya ukawa mzigo uliomlelea mara mbili kwa utunzaji, masumbufu na uwajibikaji ambao aliubeba. Katika dhiki yake alijaribiwa hata kutomwamini MUNGU. Maombi yake yalikuwa kama malalamiko. "Kwa nini umemtesa mtumishi Wako? Kwa nini sikupata kibali machoni Pako, hata ukaniwekea mzigo wa watu hawa wote juu yangu? ni wapi nitapata nyama kuwapa watu hawa wote? maana wanaililia wakisema, Tupe nyama, tule. Siwezi kubeba watu hawa wote peke yangu, kwa sababu ni mzigo mzito kwangu. [Pr 128.4; Maombi Aya ya 28]

Bwana alisikiza sala yake, na akamwongoza aite wanaume sabini miongoni mwa wazee wa Israeli-wanaume sio tu walio na umri mkubwa, lakini waliokuwa na hadhi,

maamuzi mazuri, hekima na uzoefu. "Na uwalete kwenye hema ya kukutania," alisema, "ili wasimame hapo pamoja nawe. Nami nitashuka na kuzungumza nawe huko; Nami nitachukua baadhi ya roho iliyo juu yako, na kuiweka juu yao; nao watabeba mzigo wa watu pamoja nawe, ili usibebe wewe peke yako." (Patriarchs and Prophets, 379, 380) [Pr 129.1; Maombi Aya ya 29]

Musa aliomba Rehema kwa ajili ya Israeli – Musa sasa akainuka na kuingia katika madhabahu ya kukutania. Bwana akamtangazia hivi, "Nitawapiga kwa tauni, na kuwazuia, na nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa zaidi." Lakini tena Musa alisihi kwa maombezi kwa ajili ya watu wake. Hangekubali waangamizwe, na yeye mwenyewe afanywe kuwa taifa lenye nguvu. Akiomba huruma ya MUNGU, alisema: "Ninakuomba, nguvu za Bwana wangu ziwe kubwa kama ulivyozungumza, ukisema, Bwana ni mvumilivu, na mwingi wa rehema wasamehe, ninakuomba Wewe, uovu wa watu hawa kulingana na ukuu wa rehema Zako, na jinsi ulivyowasamehe watu hawa, kutoka Misri hata sasa." [Pr 129.2; Maombi Aya ya 30]

Bwana aliahidi kuwaepusha Israeli na uangamivu/uharibifu wa papo hapo; lakini kwa sababu ya kutokuamini kwao na woga hakuweza kudhihirisha nguvu Zake katika kuwashinda adui zao. Kwa hiyo kwa rehema Yake aliwaamuru, kama njia pekee salama, warudi nyuma kuelekea Bahari ya Shamu. - (Patriarchs and Prophets, 390, 391) [Pr 129.3; Maombi Aya ya 31]

Maombi ya Musa yaliwaokoa Waisraeli dhidi ya Hukumu za MUNGU— watu walipomwangalia mzee huyu mwenye umri mkubwa, aliyekuwa anakaribia kuchukuliwa kutoka kwao, walikumbuka, kwa shukrani mpya na ya kina, huruma yake ya 'mzazi', mashauri yake ya busara, na kazi yake isiyochoka. Ni mara ngapi, ambapo dhambi zao zilikuwa zimealika hukumu za haki za MUNGU, na sala za Musa zikaendelea bila kuchoka na kushinda pamoja Naye Mungu na kisha Yeye hawakuwaangamiza! Huzuni yao iliongezeka kwa majuto. Walikumbuka kwa uchungu kwamba upotovu wao wenyewe ulikuwa umempelekea Musa kwenye dhambi ambayo kwayo anapaswa kufa.- (Patriarchs and Prophets, 470) [Pr 129.4; Maombi Aya ya 32]

Ombi la Mwisho la Musa lililotimizwa katika Mlima wa kugeuka sura kwa Yesu kwa mng'ao usoni— hakuna muda hapo awali, mpaka ilipodhihirika katika mfano wa dhabihu ya Kristo, ambapo haki na upendo wa MUNGU vilionyeshwa kwa kushangaza zaidi kuliko wakati wowote, katika kushugulika Kwake na Musa. MUNGU alimfungia Musa nje ya Kanaani, ili kufundisha somo ambalo halipaswi kusahaulika kamwe— kwamba Anahitaji utii kamili, na kwamba watu wanapaswa kuwa waangalifu dhidi ya kujichukulia utukufu ambao ni wa Muumba wao tu. Bwana hakuweza kulitimiza ombi la Musa kwamba apate kushiriki urithi wa Israeli, hata hivyo hakumsahau au kumwacha mtumishi Wake. MUNGU wa mbinguni alielewa mateso ambayo Musa alikuwa amevumilia; Alikuwa ameona kila tendo la huduma ya uaminifu kwa miaka hiyo mingi ya mizozo na majaribio/mitihani. Juu ya Pisga, MUNGU alimwita Musa kwenye urithi mtukufu zaidi kuliko Kanaani ya kidunia. [Pr 130.1; Maombi Aya ya 33]

Juu ya mlima wa mng'ao wa uso wa Yesu (transfiguration), Musa alikuwepo na Eliya, ambaye alikuwa ametwaliwa kwenda mbinguni. Walitumwa kama wabebaji wa nuru na utukufu kutoka kwa Baba kwenda kwa Mwanawe. Na hivyo ombi la Musa, alilolitoa karne nyingi zilizopita, mwishowe lilitimizwa. Alisimama juu ya "mlima mzuri", ndani ya nchi ya urithi wa watu wake Israeli, akishuhudia kwake Yeye Yule ambaye ahadi zote kwa Israeli zimejikita Kwake. Hili ndilo lilikuwa tukio la mwisho alilofunuliwa Musa katika maono wakati bado akiwa na mwili unaokufa, katika historia ya mtu huyo aliyeheshimiwa sana na Mbingu. - (Patriarchs and Prophets, 479) [Pr 130.2; Maombi Aya ya 34]

Hana

Mfano wa Hana unamtia moyo Kila Mama — Kutoka Shilo, Hana alirudi kimya nyumbani kwake huko Rama, akimwacha mtoto Samweli afundishwe utumishi katika nyumba ya MUNGU, chini ya maagizo ya kuhani mkuu. Kuanzia mafunzo ya awali ya akili yake alikuwa amemfundisha mtoto wake kumpenda na kumcha MUNGU na kujiona kama yeye ni wa Bwana. Kwa kila kilichomzunguka alichokifahamu, alikuwa anatarajia kuwa atapeleka mawazo yake kwa Muumba. Walipotengana na

mtoto wake, upweke wa mama mwaminifu haukukoma. Kila siku Samweli alikuwa mlengwa wa maombi yake. Kila mwaka alimtenezea kwa mikono yake mwenyewe, joho la utumishi wake; na alipokwenda pamoja na mumewe kuabudu huko Shilo, alimpa mtoto ukumbusho huu wa upendo wake. Kila nyuzi ya vazi dogo ilikuwa imesokotwa na maombi ili awe safi, adhimu, bora na mkweli. Hakuomba ukuu wa ulimwengu kwa mtoto wake, lakini aliomba kwa bidii ili apate ukuu ambao Mbingu inathamini ili amheshimu/amche MUNGU na kubariki wanadamu wenzake. [Pr 130.3; Maombi Aya ya 35]

Hana alikuwa na thawabu kubwa iliyoje! Naye ni mfano wa faraja ya kutia moyo kwa namna bora kiasi gani, juu ya uaminifu wake! Kuna fursa za thamani isiyo na kifani, masilahi yenye thamani kubwa, yaliyowekwa kwa kila mama. Duru za unyenyekevu ambazo wanawake wameziona kama kazi ya kuchosha zinapaswa kuangaliwa kama kazi kuu na bora. Ni fursa ya mama kuubariki ulimwengu kwa ushawishi wake, na kwa kufanya hivyo ataleta furaha moyoni mwake. Anaweza kutengeneza njia zilizonyooka kwa ajili ya miguu ya watoto wake kupitia katika mwangaza wa jua na kivuli, hadi utukufu wa juu kabisa. Lakini ni wakati tu anapotafuta katika maisha yake mwenyewe kufuata mafundisho ya Kristo, ndipo ambapo mama anaweza kutumaini kuunda tabia ya watoto wake kulingana na mfano wa Mungu/mbingu. Ulimwengu unafurika na ushawishi mbaya. Mitindo na desturi zina nguvu kubwa juu ya vijana. Ikiwa mama atashindwa katika jukumu lake la kufundisha, kuongoza, na kuzuia, watoto wake, kwa asilia/kawaida watakubali uovu, na kuachana na wema. Hebu kila mama aende mara kwa mara kwa Mwokozi wake na sala, "Tufundishe, tutamwamuru vipi mtoto, na tufanye nini kwake?" Hebu azingatie mafundisho ambayo MUNGU ametoa katika Neno Lake, naye atapewa hekima kadiri atakavyohitaji. - (Patriarchs and Prophets, 572, 573) [Pr 131.1; Maombi Aya ya 36]

Hana alikuwa Mwanamke wa Maombi — Hana hakutoa lawama kwa mumewe kuhusiana na ndoa yake isiyo na busara. Huzuni ambayo hakuweza kushiriki na rafiki wa kidunia, aliipeleka kwa Baba yake wa Mbinguni, na kutafuta faraja kutoka kwa Yeye peke yake ambaye alisema, "Niite siku ya shida, Nami nitakuokoa." Kuna nguvu

kubwa katika maombi. Adui yetu mkuu anatafuta kila mara kuweka roho iliyofadhaika mbali na MUNGU. Ombi kuelekea Mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi, hutazamwa kwa 'kuwaka moto tumbo' na Shetani kuliko sheria za mabaraza ya nchi au maagizo ya wafalme. [Pr 131.2; Maombi Aya ya 37]

Sala ya Hana haikusikiwa na sikio la mwandamu anayekufa, lakini iliingia kwenye sikio la Bwana wa majeshi. Aliomba kwa dhati na bidii kwamba MUNGU aiondoe aibu yake, na ampe kibali cha kuthaminiwa zaidi na wanawake wa umri huo, - baraka ya kuwa mama. Alipokuwa akishindana mieleka katika maombi, sauti yake haikutoa mlio (haikusikika), lakini midomo yake ilisogea na uso wake ulitoa ushahidi wa hisia za ndani za kina. Na sasa mtihani mwingine ulimngojea mwombaji huyu mnyenyekevu. Jicho la Eli kuhani mkuu lilipotua kwake, aliamua kwa haraka kwamba alikuwa amelewa. Sherehe za karamu zisizo na adabu zilizohusisha ulevi na uzinzi zilikuwa zimeukanyaga utauwa wa kweli miongoni mwa watu wa Israeli. Matukio ya kukosekana kwa adabu na kutotawala nafsi kwa vileo, hata kati ya wanawake, yalitokea mara kwa mara, na sasa Eli aliazimia kusimamia kile alichokiona kuwa kinastahili kukemewa. "Utalewa mpaka lini? Ondoa divai yako." [Pr 132.1; Maombi Aya ya 38]

Hana alikuwa akiongea na MUNGU. Aliamini kwamba sala yake imesikilizwa, na amani ya Kristo iliujaza moyo wake. Haiba yake ilikuwa ya woga, upole, unyenyekevu na nyeti, na bado hakutumbukia katika sikitiko wala hasira kwa kutuhimiwa pasipo haki na kwa hasira kwamba amelewa katika nyumba ya MUNGU. Akiwa na heshima kubwa kwa watiwa-mafuta wa Bwana, alituliza mashtaka hayo kwa utulivu na kusema sababu ya hisia zake. "Hapana Bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye roho ya huzuni. Sikunywa divai wala kileo, lakini nimemwaga roho yangu mbele za Bwana. Usimhesabie mjakazi wako kuwa binti wa Beliali, kwa kuwa kwa sasa niliongea kwa malalamiko yangu na huzuni yangu." Akishawishika kwamba maonyo yake hayakuwa ya haki, Eli alijibu, "Nenda kwa amani, na MUNGU wa Israeli akutunukie ombi lako ulilomwomba." [Pr 132.2; Maombi Aya ya 39]

Katika sala yake, Hana alikuwa ameweka nadhiri kwamba ikiwa ombi lake litakubaliwa, atamtoa mtoto wake kwa ajili ya huduma kwa MUNGU. Kiapo hiki alimjulisha mumewe, na alithibitisha katika hafla adhimu ya ibada, kabla ya kuondoka Shilo. [Pr 132.3; Maombi Aya ya 40]

Sala ya Hana ilijibiwa, na akapokea zawadi ambayo alikuwa ameiomba kwa unyofu na bidii. Alipotazama ahadi ya upendeleo wa Bwana alimwita mtoto Samweli – Nilimwombwa kwa MUNGU. - (The Signs of the Times, Oktoba 27, 1881) [Pr 133.1; Maombi Aya ya 41]

Eliya

Eliya aliomba kwa ajili ya kutubu kwa Israeli – Kati ya milima ya Gileadi, mashariki mwa Yordani, katika siku za Ahabu kulikuwa na mtu wa imani na maombi ambaye huduma yake isiyo na woga ilikusudiwa kusitisha kuenea kwa uasi haraka katika Israeli. Akiwa mbali sana na mji wowote mashuhuri, na bila ya kuwa na nafasi ya juu maishani, hata hivyo Eliya mtishibi aliingia katika utume wake akiwa na ujasiri katika kusudi la MUNGU la kuandaa njia mbele yake na kumpa mafanikio tele. Neno la imani na nguvu lilikuwa juu ya midomo yake, na maisha yake yote yalikuwa ya kujitolea kwa kazi ya matengenezo. Sauti yake ilikuwa ya mtu anayelia nyikani kukemea dhambi na kuzuia wimbi la uovu lirudi nyuma. Na wakati alipoenda kwa watu kama mkemeaji wa dhambi, ujumbe wake ulitoa zeri ya Gileadi kwa roho za wagonjwa na wadhambi wote ambao walitaka kuponywa. [Pr 133.2; Maombi Aya ya 42]

Kadiri Eliya alivyoona Israeli inazidi kudumbukia chini zaidi katika ibada ya sanamu, ndivyo roho yake ilifadhaika na hasira yake ikaamka. MUNGU alikuwa amefanya mambo makubwa kwa watu Wake. Alikuwa amewaokoa kutoka utumwani na kuwapa "nchi za mataifa (pagani),.... ili wazishike amri Zake, na kuzishika sheria Zake." Zaburi 105: 44, 45. Lakini mipango ya neema ya Yehova ilikuwa imesahaulika. Kutoamini kulikuwa kunalitenganisha haraka taifa lililochaguliwa kutoka kwenye Chanzo cha nguvu zake. Akiuona uasi huu kutoka katika mfungo/kujitenga kwake mlimani, Eliya aligubikwa na huzuni. Kwa uchungu wa roho alimsihi MUNGU awakamate watu waliowahi kupendelewa katika mwenendo wao mbaya, awatembelee

na hukumu, ikiwa ni lazima, ili waongozwe kuona katika nuru ya kweli na kuchepuka kwao kutoka kwenye mpango wa mbingu. Alitamani kuwaona wakitubu kabla hawajazama katika maovu kiasi cha kumfanya Bwana awaangamize kabisa. [Pr 133.3; Maombi Aya ya 43]

Ombi la Eliya lilijibiwa. Wito uliorudiwa mara kwa mara, majibizano, na maonyo vilishindwa kuileta Israeli kwenye toba. Wakati ulikuwa umefika ambapo lazima MUNGU azungumze nao kwa njia ya hukumu. Japokuwa waabudu Baali walidai kwamba hazina za mbinguni, umande na mvua, havikutoka kwa Yehova, bali kutoka kwenye nguvu asilia za maumbile, na kwamba ilikuwa kupitia nishati ya uumbaji wa jua kwamba dunia ilitajirika na kufanywa kuleta mazao kwa wingi, laana ya MUNGU ilikuwa inaenda kukaa juu ya ardhi iliyonajisiwa. Makabila ya waasi wa Israeli yalipaswa kuonyeshwa upumbavu wa kuamini nguvu ya Baali kwa kutoa mibaraka ya muda (kama mvua). Mpaka watakapomgeukia MUNGU wakiwa na toba, na kumkubali kuwa Ndiye chanzo cha baraka zote, mvua wala umande havitaanguka juu ya nchi. - (Prophets and Kings, 119, 120) [Pr 134.1; Maombi Aya ya 44]

Hofu ya MUNGU ilikuwa ikipungua kila siku katika Israeli. Ishara za kukufuru za upofu wao wa kuabudu sanamu zao zilikuwa zikionekana kati ya Israeli wa MUNGU. Hakukuwa na mtu aliyethubutu kufichua maisha yao kwa kusimama waziwazi kinyume na ibada ya sanamu yenye kukufuru iliyokuwepo. Madhabahu za Baali, na makuhani wa Baali ambao walitoa dhabihu kwa jua, mwezi, na nyota, zilikuwa maarufu kila mahali. Walikuwa wameweka wakfu mahekalu na miti, ambapo ndani yake kuliwekwa kazi ya mikono ya watu kwa ajili ya kuabudu. Manufaa ambayo MUNGU aliwapa watu hawa hayakuleta shukrani kwa Mpaji. Kwa neema zote za Mbingu, vijito vya maji, na mikondo ya maji yaliyo hai, umande mwororo, na manyunyu ya mvua ili kuiburudisha dunia, na kusababisha mashamba yao yatoe mazao kwa wingi, walidai ni neema ya miungu yao. [Pr 134.2; Maombi Aya ya 45]

Nafsi ya uaminifu ya Eliya ilihuzunika. Hasira yake iliwashwa, na alikuwa na wivu kwa utukufu wa MUNGU. Aliona kwamba Israeli ilikuwa imetumbukia katika uasi wa imani unaotisha. Alitindikiwa na mshangao na huzuni kwa

uasi wa watu, wakati alipokumbuka mambo makubwa ambayo MUNGU alikuwa amewafanyia. Lakini hii yote ilisahaulika na watu wengi. Alikwenda mbele za MUNGU, na roho yake ikiwa imebanwa kwa uchungu, akamsihi Yeye awaokoe watu Wake ikiwa ni lazima awahukumu. Akamsihi MUNGU azuie umande, hazina za mbinguni na mvua kwa watu Wake wasio na shukrani, ili waasi wa Israeli waweze kutazama na kuona kwamba sanamu zao ni kazi bure, sanamu zao za dhahabu, mbaao, na jiwe, jua, mwezi, na nyota, miungu yao, haziwezi kumwagilia ardhi na kuipatia utajiri, na kuifanya itoe mazao kwa wingi sana. MUNGU alimwambia Eliya alikuwa amesikia maombi yake. Naye angewazuilia watu Wake umande na mvua, mpaka wamgeukie Yeye kwa toba. - (The Review and Herald, September 16, 1873) [Pr 134.3; Maombi Aya ya 46]

Katika miaka mingi ya ukame na njaa, Eliya aliomba kwa bidii ili mioyo ya Israeli igeuzwe kutokakwenye ibada ya sanamu na kuwa watiifu kwa MUNGU. Kwa subira nabii huyo akangojea, wakati mkono wa Bwana ulikaa kwa uzito wa adhabu katika nchi iliyopigwa na ukame. Alipoona dalili za mateso na umasikini unazidi kila upande, moyo wake ulikuwa umefunikwa na huzuni, na alitamani nguvu ya kuleta matengenezo haraka. Lakini MUNGU Mwenyewe alikuwa akiweka mkakati Wake, na yote ambayo mtumishi Wake angefanya ni kusali kwa imani na kungojea wakati wa kuchukua hatua bainishi. - (Prophets and Kings, 133) [Pr 135.1; Maombi Aya ya 47]

Eliya Mfano wa Mtu Ambaye Alishinda Kupitia Maombi ya Dhati – Tunapaswa kuwa katika maombi ya siri daima. Kristo Ndiye mzabibu, ninyi ni matawi. Ili tuweze kushamiri, lazima tuendeleo kupata maji na lishe ya utomvu kutoka kwenye Mzabibu ulio Hai; kwa kuwa tukitengwa kutoka kwa Mzabibu tutakuwa hatuna nguvu (Xylem hupitisha maji, Phloem hupitisha chakula kwenye shina la mmea). [Pr 135.2; Maombi Aya ya 48]

Nilimuuliza malaika kwanini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, “Ninyi mnaachilia mkono wa Bwana mapema sana. Wasilisha maombi yako kwenye kiti cha enzi kwa ari/usongo, na ushikilie kwa imani thabiti. Ahadi ni za Kweli. Amini kwamba mnapokea mnayoomba, nanyi mtayapata.” Kisha nikaelekezwa kwa Eliya. Alikuwa na haiba ya wanadamu kama sisi, na aliomba

kwa dhati na bidii. Imani yake ilivumilia jaribu. Aliomba mara saba mbele za Bwana, na mwishowe wingu likaonekana. Niliona kwamba tulikuwa tumetilia mashaka ahadi za hakika, na tukamjeruhi Mwokozi kwa ukosefu wetu wa imani. Malaika alisema, “Jifunge silaha, na juu ya yote chukua ngao ya imani; kwa kuwa hiyo italinda moyo, na uzima, na mishale ya moto ya waovu.” Ikiwa adui anaweza kusababisha wale waliokata tamaa kuondoa macho yao kutoka kwa Yesu, na kujitazama wenyewe, na kukita kwenye kutostahili kwao, badala ya kukaa juu ya sifa na stahiki za Yesu, upendo Wake, sifa Zake, na rehema Zake kuu, adui ataondoa ngao yao ya imani na kupata lengo lake; watakuwa katika hatari ya vishawishi vyake vya moto mkali. Kwa hiyo wanyonge wanapaswa kumtazama Yesu, na kumwamini; hivyo huonyesha na kuizoesha imani yao. - (Early Writing, 73) [Pr 135.3; Maombi Aya ya 49]

Wajumbe wa MUNGU wasifanye haraka kuondoka mbele za Mungu bali wakae Naye kwa muda mrefu (wachelewe miguuni pake), ikiwa wangetaka kufanikiwa katika kazi yao. Kisa hiki kimesimuliwa ya mwanamke mzee wa Lancashire ambaye alikuwa akisikiliza sababu ambazo majirani zake walitoa kwa kufanikiwa kwa mchungaji wao. Walizungumza juu ya vipawa vyake, namna anavyojieleza, mtindo wake wa mahubiri, juu ya adabu zake au hulka. “La,” alisema kikongwe, “nitakuambia ni nini. Mtu wako amejazwa sana na Mwenyezi.” [Pr 136.1; Maombi Aya ya 50]

Watu watakapojitoa wakfu kama Eliya na watakapokuwa na imani aliyokuwa nayo, MUNGU atajifunua kama alivyofanya wakati ule. Wakati watu watakapomsihi Bwana kama vile Yakobo, matokeo ambayo yalionekana wakati huo yataonekana tena. Nguvu zitatoka kwa MUNGU katika kujibu maombi ya imani. - (Gospel Workers, 255) [Pr 136.2; Maombi Aya ya 51]

Maombi ya Eliya juu ya Mlima Karmeli Yalijibiwa kwa mshindo na ajabu – Akiwakumbusha watu juu ya uasi ulioendelea ambao umeamsha ghadhabu ya Yehova, Eliya aliwatolea wito wanyenyekeze mioyo yao na kumrudia MUNGU wa baba zao, Ili laana juu ya nchi ya Israeli iweze kuondolewa. Halafu, akiinama na kusujudu kwa heshima mbele ya MUNGU asiyeonekana, akainua mikono yake kuelekea mbinguni na kutoa sala rahisi. Makuhani wa Baali

walikuwa wamepiga kelele, wametoa povu mdomoni, na wamepata jazba na kuruka-ruka, kutoka asubuhi hadi jioni; lakini Eliya anapoomba, hakuna kelele za kugumia na mayowe yenye sauti ya juu, yasiyo na maana yanayosikika kwenye kilele huko Karmeli. Anaomba kana kwamba anajua kuwa Yehova Yuko hapo, shahidi wa tukio hilo, msikilizaji wa ombi lake. Manabii wa Baali wameomba vikali kwa kuchanganyikiwa na mihemko mingi (wildly), wakiwa wamekanganyikiwa hivyo hawakuweza kueleweka kwamba wanazungumza nini. Eliya anasali kwa urahisi na kwa bidii, akimwomba MUNGU aonyeshe ukuu Wake juu ya Baali, ili Israeli iongozwe kumrudia Yeye. [Pr 136.3; Maombi Aya ya 52]

"Bwana MUNGU wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli," nabii anaomba, "na ijulikane leo kuwa Wewe Ndiwe MUNGU katika Israeli, na kwamba mimi ni mtumishi Wako, na kwamba nimefanya haya yote kwa Neno Lako. Nisikilize, Bwana, unisikilize, ili watu hawa wapate kujua ya kuwa Wewe Ndiwe Bwana MUNGU, na ya kuwa umeirudisha mioyo yao tena. [Pr 136.4; Maombi Aya ya 53]

Ukimya, mzito unaotesa katika ukuu wake unakaa juu ya wote. Makuhani wa Baali wanatetemeka kwa hofu. Kwa ufahamu wa hatia yao, wanatafuta kisasi cha haraka. [Pr 137.1; Maombi Aya ya 54]

Mara tu maombi ya Eliya yalipotamkwa, kukashuka miali ya moto kama umeme angavu wa radi kutoka mbinguni juu ya madhabahu iliyo inuliwa, ukiteketeza dhabihu, ukilamba maji ya mtaro, na kuteketeza hata mawe ya madhabahu. Mwangaza wa moto unaangaza mlima na kuangaza macho ya umati. Katika mabonde chini, ambapo wengi wanaangalia katika hali ya kutojua la kufanya kwa mashaka kuhusu harakati za wale walio juu, kushuka kwa moto kunaonekana wazi, na wote wanashangaa kuona. Unafanana na nguzo ya moto ambayo kwenye Bahari ya Shamu ilitenganisha watoto wa Israeli na jeshi la Wamisri. - (Prophets and Kings, 152, 153) [Pr 137.2; Maombi Aya ya 55]

Maombi ya Eliya Yalitoka kwa Imani katika Kudai Ahadi za MUNGU— Pamoja na kuuawa kwa manabii wa Baali, njia ilifunguliwa ya kuendelea na matengenezo makubwa ya kiroho kati ya makabila kumi ya ufalme wa kaskazini. Eliya

alikuwa amewaonyesha watu uasi wao; alikuwa amewataka wanyenyekeze mioyo yao na kumrudia Bwana. Hukumu za Mbinguni zilikuwa zimetetelezwa; watu walikiri dhambi zao, na walimkubali MUNGU wa baba zao kama MUNGU aliye hai; na sasa laana ya Mbingu ilikuwa inaenda kuondolewa, na baraka za muda za maisha zikafanywa upya. Ardhi ilipaswa kuburudishwa na mvua. “Ondoka, ule, unywe,” Eliya akamwambia Ahabu; “Kwa maana kuna sauti ya mvua nyingi.” Kisha nabii akaenda juu ya mlima ili kuomba. [Pr 137.3; Maombi Aya ya 56]

Haikuwa kwaajili ya uthibitisho wowote wa nje kwamba mvua ilikuwa karibu kunyesha, ndiyo kwamba Eliya aliweza kumwambia Ahabu kwa uhakika kwamba ajitayarisha kwa ajili ya mvua inayokuja. Nabii hakuona mawingu mbinguni; hakisikia ngurumo. Alizungumza tu Neno ambalo Roho wa Bwana alikuwa amemsukuma kunena katika kuitikia imani yake yenye nguvu. Siku nzima alikuwa ametenda mapenzi ya MUNGU bila kuyumbayumba na alikuwa amedhirisha imani yake kamili katika unabii wa Neno la MUNGU; na sasa, akiwa amefanya yote ambayo yalikuwa katika uwezo wake kufanya, alijua kwamba Mbingu ingetoa kwa uhuru na ukarimu baraka zilizotabiriwa. MUNGU Yule Yule ambaye aliyekuwa ametuma ukame alikuwa ameahidi mvua tele kama thawabu ya kutenda sahihi; na sasa Eliya alisubiri kumwagwa kwa ahadi. Katika mtazamo wa unyenyekevu, “uso wake katikati ya magoti yake,” alifanya maombezi kwa MUNGU kwa ajili ya Israeli iliyotubu. [Pr 137.4; Maombi Aya ya 57]

Tena na tena, Eliya alimtuma mtumishi wake aende kwenye eneo lililo karibu ambalo angeweza kutazama bahari ya Mediterania, ili ajue ikiwa kulikuwa na ishara yoyote inayoonekana kuonyesha kwamba MUNGU alikuwa amesikia sala yake. Kila wakati mtumishi alirudi na neno, “Hakuna kitu.” Nabii hakukosa subira au kupoteza imani, lakini aliendelea kuomba kwa dhati na bidii. Mara sita mtumishi alirudi na neno kwamba hakuna dalili ya mvua katika mawingu ya mbingu yaliyokuwa na rangi ya kahawia. Bila woga, Eliya akamtuma mara moja tena; na wakati huu mtumishi akarudi na neno, “Tazama, wingu dogo linatoka katika bahari ukubwa wa kiganja cha mkono wa mwanadamu.” [Pr 138.1; Maombi Aya ya 58]

Hii ilitosha. Eliya hakungojea mbingu ziweze kukusanya weusi zaidi. Katika wingu hilo dogo aliona kwa imani mvua tele; naye akatenda kupatana na imani yake, akimtuma mtumishi wake haraka kwa Ahabu na ujumbe huu, "Tengeneza gari lako, ukashuke, ili mvua isikuzuie." [Pr 138.2; Maombi Aya ya 59]

Ilikuwa ni kwa sababu Eliya alikuwa mtu wa imani kubwa kwamba MUNGU angeweza kumtumia katika dharura na mgogoro huu mbaya katika historia ya Israeli. Alipokuwa akiomba, imani yake ilifikia na kuzishikilia kwa nguvu ahadi za Mbingu, na alidumu katika maombi hadi maombi yake yakajibiwa. Hakungoja uthibitisho kamili kwamba MUNGU alikuwa amemsikia, bali alikuwa tayari kujitosa kwa ishara hata ndogo, ya upendeleo wa Bwana. Ila, kile alichowezesha kukifanya chini ya uwezo wa Mungu, wote tunaweza kukifanya katika nyanja yetu ya utendaji katika huduma/utumishi kwa MUNGU; Kwa maana imeandikwa hivi kuhusu nabii kutoka milima ya Gileadi: "Eliya alikuwa mtu wa tabia kama sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe; na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu, miezi sita." Yakobo 1: 5, 17, [Pr 138.3; Maombi Aya ya 60]

Imani ya namna hii inahitajika ulimwenguni leo-imani ambayo itazishika ahadi za Neno la MUNGU na kukataa kuziacha hadi Mbingu itakaposikia. Imani kama hii hutuunganisha kwa karibu na Mbingu, na hutuletea uwezo wa kukabiliana na nguvu za giza. Kwa imani watoto wa MUNGU "wamezitiisha falme, wametenda haki; walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, walizima udhalimu wa moto, waliokoka katika makali ya upanga, kutoka katika udhaifu walifanywa kuwa hodari, wakawa hodari katika vita, wakafukuza majeshi ya wageni. Waebrania 11:33, 34. Na kwa njia ya imani sisi leo tunapaswa kufikia kilele cha kusudi la MUNGU kwetu. "Ukiweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwake yeye aaminiye." Marko 9:23. [Pr 138.4; Maombi Aya ya 61]

Imani ni jambo muhimu katika maombi yanayoshinda na yasiyochoka. "Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao." "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba Yeye hutusikia, lolote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba." Waebrania 11: 6; 1 Yohana

5:14, 15. Tukiwa na imani ya kudumu ya Yakobo, na uvumilivu wa Eliya, tunaweza kuwasilisha maombi yetu kwa Baba, tukidai yote ambayo Yeye ameahidi. Heshima ya kiti Chake cha enzi imo hatarini kwa utimilifu wa Neno Lake. (heshima ya Ukuu Wake imo hatarini endapo Neno Lake halitatimizwa kama vile ALIVYONENA YEYE) - (Prophets and Kings, 157, 158) [Pr 139.1; Maombi Aya ya 62]

Eliya Alidumu kwa uvumilivu Katika Maombi Hadi Jibu lilipokuja— Masomo muhimu huwasilishwa kwetu katika uzoefu wa Eliya. Akiwa juu ya mlima Karmeli aliomba maombi kwaajili ya mvua, imani yake ilijaribiwa, lakini aliendelea kwa subira kumjulisha ombi lake MUNGU. Aliomba kwa bidii mara sita kwa dhati na bidii, na bado hakukuwa na ishara kwamba ombi lake lingejibiwa, lakini kwa imani thabiti alihimiza ombi lake katika kiti cha neema. Kama angekata tamaa ile mara ya sita, maombi yake yasingejibiwa, lakini alivumilia hadi jibu lilipokuja. Tunaye MUNGU ambaye sikio Lake halijazibwa/hajaliziba kwaajili ya kupokea maombi yetu; na ikiwa tutalithibitisha Neno Lake (tutalipima na kuliona ndiyo kama anavyosema), Yeye ataheshimu imani yetu. Yeye anataka matamano yetu yote yafumwe pamoja na matamano yake, ndipo anaweza kutubariki sana; kwani hatutajivunia wakati baraka zinapokuwa zetu, lakini tutampa/tumtarudishia MUNGU sifa zote. MUNGU huwa hajibu maombi yetu mara ya kwanza tunapomuomba; kwani akifanya hivi, tunaweza kuichukulia hiyo kirahisi kwamba sisi tuna haki ya baraka na neema zote alizotupatia. Badala ya kujitazama mioyo yetu kuona ikiwa kuna uovu wowote tunaouendekeza, au dhambi yoyote iliyoendekezwa, tunakuwa wazembe, na tunashindwa kutambua utegemezi wetu Kwake, na hitaji letu la msaada Wake. [Pr 139.2; Maombi Aya ya 63]

Eliya alijinyenyekeza mpaka alipokuwa katika hali ambayo asingejichukulia utukufu mwenyewe. Hili ndilo sharti ambalo kwalo Bwana husikia maombi, kwa kuwa tutampa sifa Yeye. Desturi ya kuwapa sifa wanadamu ndiyo inayosababisha uovu mkubwa. Mtu humsifu mwingine, na kwa hivyo mtu huyo huongozwa kuhisi kuwa utukufu na heshima ni mali yao, kwamba wao ndiyo wamiliki. Unapomwinua mwanadamu, unamwekea mtego katika nafsi yake, na kufanya kama Shetani anavyotaka ufanye.

Unapaswa kumsifu MUNGU kwa moyo wako wote, roho, uwezo, akili na nguvu zote; kwa maana MUNGU peke yake Ndiye anayestahili kutukuzwa. - (SDA Bible Commentary 2: 1034, 1035) [Pr 140.1; Maombi Aya ya 64]

Mtumishi alitazama wakati Eliya akiomba. Alirudi mara sita kutoka kwenye lindo, akisema, Hakuna kitu, hakuna wingu, wala ishara ya mvua. Lakini nabii huyo hakukata tamaa kwa kuvunjwa moyo. Aliendelea kupitia maisha yake, kuona ni wapi alikuwa ameshindwa kumheshimu MUNGU, kisha alikiri dhambi zake, na hivyo akaendelea kuitesa nafsi yake mbele za MUNGU, wakati akitafuta ishara kuona kwamba sala yake imeshajibiwa. Alipoendelea kuchunguza moyo wake, alionekana kuwa mdogo na amepungua, kwa makadirio yake mwenyewe na pia mbele ya MUNGU. Ilionekana kwake kuwa yeye si kitu, na kwamba MUNGU Ndiye kila kitu; na alipofikia hatua ya kujikana nafsi yake mwenyewe, huku akimshikilia kwa nguvu Mwokozi kama nguvu na haki yake pekee, basi jibu lilikuja. - (The Review and Herald, Mei 26, 1891) Herald, Mei 26, 1891) [Pr 140.2; Maombi Aya ya 65]

Daudi

Anguko la Daudi ni Onyo kwetu la Kutopuuza Maombi - MUNGU alikusudia historia ya anguko la Daudi iwe kama onyo kwamba hata wale ambao Yeye Amewabariki sana na kuwapendelea hawapaswi kujisikia salama na kupuuza kukesha na maombi. Na hivyo ndivyo imedhihiriswa kwa wale ambao kwa unyenyekevu wametafuta kujifunza somo ambalo MUNGU amekusudia kufundisha. Kutoka kizazi hadi kizazi maelfu wameongozwa hivyo kutambua hatari yao wenyewe dhidi ya nguvu ya mshawishi. Kuanguka kwa Daudi, aliyeheshimiwa sana na Bwana hapo mwanzo, kumeamsha kwao, kutokujiamini. Wamehisi kwamba MUNGU pekee, Ndiye awezaye kuwatunza wao kwa uwezo Wake kupitia imani. Wakajua kwamba ndani Yake kulikuwa na nguvu na usalama wao, wamekuwa na hofu ya kukanyaga mguu wao kwenye ile hatua ya kwanza kuelekea uwanja wa Shetani.—(Patriarchs and Prophets, 724) [Pr 140.3; Maombi Aya ya 66]

MUNGU alijibu Maombi ya Daudi ya Msamaha - Moja ya maombi ya dhati kabisa yaliyoandikwa katika Neno la MUNGU ni lile la Daudi wakati alipoomba, "Uniumbie au

unda ndani yangu moyo safi, Ee MUNGU." Jibu la MUNGU kwa maombi kama haya ni, nitakupa moyo mpya. Hii ni kazi ambayo hakuna mwanadamu mwenye kufa anayeweza kuifanya. Wanaume na wanawake wanapaswa kuanza toka mwanzoni, kumtafuta MUNGU kwa bidii zaidi kwa uzoefu wa kweli wa Kikristo. Wanapaswa kuhisi uwezo wa uumbaji wa Roho Mtakatifu. Wanapaswa kupokea moyo mpya, ambao huwekwa laini na huruma na mkunjufu kwa neema ya mbinguni. Nafsi yenye ubinafsi inapaswa kusafishwa kutokea kwenye roho. Tunapaswa kufanya kazi kwa dhati, bidii na kwa unyenyekevu wa moyo, kila mmoja akimwangalia Yesu kwa ajili ya mwongozo na kutiwa moyo. Kisha jengo hilo, ambalo limeundwa/limejengwa kwa pamoja, litakuwa hekalu takatifu katika Bwana. ((SDA Bible Commentary 4: 1165) [Pr 141.1; Maombi Aya ya 67]

Sulemani

Tunahitaji Kujifunza Somo Katika Maombi ya Unyenyekevu ya Sulemani – Mwanzoni mwa utawala wake, Sulemani aliomba: "Ee Bwana MUNGU wangu, Umemfanya mtumwa Wako awe mfalme badala ya Daudi baba yangu: nami ni mtoto mdogo. Nami sijui namna ya kutoka au kuingia." 1 Wafalme 3: 7. [Pr 141.2; Maombi Aya ya 68]

Sulemani alikuwa amemrithi baba yake Daudi katika kiti cha enzi cha Israeli. MUNGU alimheshimu sana, na, kama tunavyojua, alikuja kuwa mfalme mkuu, tajiri, na mwenye hekima aliyewahi kukalia kiti cha enzi duniani, katika miaka ya baadaye. Mwanzoni mwa utawala wake Sulemani alivutiwa/alipendezwa na Roho Mtakatifu na uzito wa majukumu yake, na, ingawa alikuwa na talanta nyingi na uwezo, aligundua kuwa bila msaada wa Bwana alikuwa mnyonge kama mtoto mdogo kutenda lolote. Sulemani hakuwahi kuwa tajiri sana au mwenye busara sana au mkuu sana kama ule wakati alipomkiri Bwana kwa kusema: "Mimi ni mtoto mdogo: sijui kutoka au kuingia..... [Pr 141.3; Maombi Aya ya 69]

Na tamko hili lilimpendeza Bwana, ya kwamba Sulemani alikuwa ameomba hili jambo. MUNGU akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha marefu; wala hujaomba utajiri kwa ajili yako mwenyewe, wala hukutaka uhai wa adui zako; bali umejitakia ufahamu wa kupambanua hukumu; tazama, nimetenda sawasawa na

maneno yako; tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. Na pia nimekupa yale ambayo haujaomba, utajiri na heshima: hivi kwamba hakutakuwa na yeyote kati ya wafalme kama wewe siku zako zote.” Sasa masharti yalikuwa haya: "Na ikiwa utakwenda katika njia Zangu, ukazishika sheria Zangu na amri Zangu, kama vile baba yako Daudi alivyotembea, ndipo nitakurefushia siku zako." [Pr 141.4; Maombi Aya ya 70]

Wote wanaoshika nafasi za uwajibikaji, wanahitaji kujifunza somo ambalo linafundishwa katika sala ya unyenyekevu ya Sulemani. Wanapaswa kukumbuka daima kwamba cheo hakitabadilisha tabia kamwe au kumzuia/kumwezesha mtu asitende dhambi tena kamwe. Kadiri mtu anavyochukua nafasi ya juu, ndivyo jukumu analobeba linavyozidi kuwa kubwa zaidi, na ndivyo ushawishi anaoshinikiza unavyokuwa mpana zaidi na ndivyo hitaji lake la kuhisi utegemezi wake juu ya hekima na nguvu za MUNGU na kustawisha tabia bora na takatifu zaidi huongezeka.— (Testimonies for the Church 9:281, 282). [Pr 142.1; Maombi Aya ya 71]

Mfano wa Sulemani - funzo La kukesha katika Maombi
— ilikuwaje-kuwaje, katika kisa chake Sulemani mpaka akawa mtu dhaifu, mwenye tabia ya kusuasua— Jinsi mtu aliye jasiri kwa kawaida, thabiti, na mwenye kuazimia — alivyotikiswa kama mwanzi katika upepo chini ya nguvu ya mshawishi! Je! ilikuwaje Mwerezi wa Lebanoni mzee na uliokunjwa, mwaloni imara wa Bashani, ukainama mbele ya mlipuko wa majaribu! Ni somo lililoje kwa wote wanaotaka kuokoa roho zao wakeshe katika maombi daima. Ni onyo lililoje la kuweka neema ya Kristo mioyoni mwao, kupigana na ufisadi na uharibifu wa ndani ya moyo na majaribu ya nje.— (Manuscript Relees 21:383) [Pr 142.2; Maombi Aya ya 72]

Mfalme Hezekia

Hezekia aliwaombea masalia wa Israeli- "Siku hii ni siku ya taabu, na ya kukemea, na ya kukufuru," ndilo neno mfalme alilotuma. Huenda Bwana, MUNGU wako, atayasikia maneno yote ya amiri, ambaye mfalme wa Ashuru, bwana wake, amemtuma ili amtukane MUNGU

aliye hai; naye atayakemea maneno aliyoyasikia Bwana, MUNGU wako; kwa hivyo inua maombi yako kwa masalia waliobaki." Mstari wa 3, 4. [Pr 142.3; Maombi Aya ya 73]

"Kwa sababu hii, mfalme Hezekia, na nabii Isaya mwana wa Amози, waliomba, wakalia Mbinguni." 2 Mambo ya Nyakati 32:20. [Pr 143.1; Maombi Aya ya 74]

MUNGU alijibu maombi ya waja Wake. Isaya alipewa ujumbe huu kwa ajili ya Hezekia: "BWANA asema hivi, Usiogope maneno uliyoyasikia, ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru wamenitukana Mimi. Tazama, nitapeleka mlipuko juu yake, naye atasikia fununu, na kuirudia nchi yake mwenyewe; na Nitamwangusha kwa upanga katika nchi yake mwenyewe." 2 Wafalme 19: 6, 7— (Prophets and Kings, 354) [Pr 143.2; Maombi Aya ya 75]

Ombi la Hezekia Lilipatana na mapenzi ya MUNGU- Wakati mfalme wa Yuda alipopokea barua ya kumtukana, kumdhihaki, na kumtishia na kumchokoza, aliipeleka hekaluni na "kuifungua mbele za Bwana" na kuomba kwa imani thabiti msaada kutoka mbinguni, ili mataifa ya dunia yapate kujua kwamba MUNGU wa Waebrania bado Yuko hai na anatawala. Mstari wa 14. Heshima ya Yehova ilikuwa hatarini; Yeye peke yake Ndiye angeweza kuleta ukombozi. [Pr 143.3; Maombi Aya ya 76]

"Ee Bwana, MUNGU wa Israeli, ukaaye kati ya makerubi," Hezekia aliomba, "Wewe Ndiwe MUNGU, Wewe peke Yako, wa falme zote za dunia; Wewe Ndiwe uliyefanya mbingu na nchi. Bwana, inamisha sikio Lako, usikie; fungua, Bwana, macho Yako, uone; na usikie maneno ya Senakeribu, aliyomtuma kumtukana MUNGU aliye hai. Kwa kweli, Bwana, wafalme wa Ashuru wameharibu mataifa na nchi zao, na wametupa miungu yao motoni; kwa kuwa hawakuwa miungu, bali kazi ya mikono ya wanadamu, miti na mawe; kwa hivyo wameiangamiza. Basi sasa, Ee Bwana, MUNGU wetu, nakuomba utuokoe na mkono wake, ili falme zote za dunia zijue ya kuwa Wewe Ndiwe Bwana MUNGU, Wewe peke yako. " 2 Wafalme 19: 15-19 [Pr 143.4; Maombi Aya ya 77]

Maombi ya Hezekia ya kusihi kwa niaba ya Yuda na heshima ya Mtawala wao Mkuu yalikuwa katika umoja/upatanifu na mapenzi ya MUNGU. Sulemani, katika baraka zake wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu,

alikuwa amemwomba Bwana asimamie "hoja ya watu Wake Israeli wakati wote, kama itakavyohitajika: ili watu wote wa dunia wapate kujua kwamba Bwana Ndiye MUNGU, na kwamba hakuna mwingine." 1 Wafalme 8:59, 60. Bwana alikusudia kuonyesha upendeleo haswa wakati wa vita au ukandamizaji wa kijeshi, wakuu wa Israeli walipaswa kuingia katika nyumba ya sala na kuomba ukombozi. Mstari wa 33, 34. [Pr 143.5; Maombi Aya ya 78]

Hezekia hakuachwa bila tumaini. Isaya akatumwa kwake, akisema, "Bwana, MUNGU wa Israeli, asema hivi, Hilo uliloliomba dhidi ya Senakeribu mfalme wa Ashuru nimelisikia."—(Prophets and Kings, 355, 356, 359) [Pr 144.1; Maombi Aya ya 79]

Hezekia Aliponywa katika Jibu la Maombi — Tangu siku za Daudi, hakukuwa na mfalme aliyetawala ambaye alifanya kazi kubwa sana kwa ajili ya ujenzi wa ufalme wa MUNGU wakati wa kipindi cha uasi na kukata tamaa kama alivyofanya Hezekia. Mtawala aliyekaribia kufa alikuwa amemtumikia MUNGU wake kwa uaminifu, na alikuwa amefanya mengi kuimarisha imani ya watu kwa Yehova kama Mtawala wao Mkuu. Na, kama Daudi, sasa aliweza kusihi: "Maombi yangu na yaje mbele Zako; tega sikio Lako usikie kilio changu; kwa maana nafsi yangu imejaa taabu, na maisha yangu yanakaribia kaburi." "Wewe Ndiye tumaini langu, Ee Bwana MUNGU: Ndiwe tegemeo langu tangu ujana wangu. Nimeshikiliwa na Wewe.... Usiniache nguvu zangu zipungukapo. Ee MUNGU, usiwe mbali nami: Ee MUNGU wangu, ufanye haraka kunisaidia. Ee MUNGU, usiniache; hata nitakaponyesha nguvu Yako kwa kizazi hiki, na uweza Wako kwa kila mtu atakayekuja." Zaburi 88: 2, 3; Zaburi 71: 5-18. [Pr 144.2; Maombi Aya ya 80]

Yeye ambaye "huruma Zake hazikomi" (Maombolezo 3:22) alisikia maombi ya mtumishi Wake. "Ikawa, kabla Isaya hajaenda katika ua wa katikati, Neno la Bwana likamjia, kusema, Rudi, ukamwambie Hezekia, mkuu wa watu Wangu, Hivi ndivyo asemavyo Bwana, Mungu wa baba yako Daudi nimesikia ombi lako na nimeona machozi yako. Nitakuponya na baada ya siku tatu utakwenda katika nyumba ya Bwana. Nami nitakuongezea siku zako miaka kumi na tano; Nami nitakuokoa wewe na mji huu kutoka mkononi mwa mfalme wa Ashuru; Nami nitaulinda mji huu

kwa ajili Yangu Mwenyewe, na kwa ajili ya mtumishi Wangu Daudi. 2 Wafalme 20: 4-6.— (The Review and Herald, Mei 6, 1915) [Pr 144.3; Maombi Aya ya 81]

Danieli

Sala ya Danieli Yenye Ufanisi, matokeo na unyofu na Nguvu—Danieli alimwomba MUNGU, hakujiinua mwenyewe au kudai wema wowote: “Ee Bwana, sikia; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, sikiliza na utende; usichelewe, kwa mapenzi Yako, Ee MUNGU wangu.” Hivi ndivyo Yakobo anavyoliita ombi la bidii, lenye ufanisi, linalofaa, la dhati. Kuhusu Kristo imeandikwa: “Na akiwa katika uchungu aliomba kwa bidii zaidi.” Kwa kulinganisha na maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni ni maombi dhaifu, yasiyo na moyo ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya midomo, na ni wachache walio na shauku ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. -(Testimonies for the Church 4:534) [Pr 145.1; Maombi Aya ya 82]

Danieli Alidumu kuwa mwaminifu Katika Maombi Licha ya Mateso — Je! Danieli aliacha kuomba kwa sababu agizo hilo lingeanza kutekelezwa! —Hapana, huo ndio wakati hasa aliohitaji kuomba. “Danieli alipojua ya kuwa maandishi yamesainiwa, aliingia nyumbani kwake; na, kwa kuwa dirisha lake lilikuwa wazi katika chumba chake kuelekea Yerusalemu, alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, akashukuru mbele za MUNGU wake, kama vile alivyofanya zamani. ” Danieli hakutafuta kuficha uaminifu wake kwa MUNGU. Yeye hakuomba kimya moyoni mwake, lakini kwa sauti yake, ya juu, dirisha lake likiwa wazi kuelekea Yerusalemu, alituma ombi lake mbinguni. Ndipo maadui zake wakalalamika kwa mfalme, na Danieli akatupwa ndani ya shimo la simba. Lakini Mwana wa MUNGU alikuwepo. Malaika wa Bwana alipiga kambi karibu na mtumishi wa Bwana, na mfalme alipokuja asubuhi, na kuita, “Ee Danieli, mtumishi wa MUNGU aliye hai, ni MUNGU wako, ambaye unamtumikia daima, ameweza kukuokoa simba? Ndipo Danieli akamwambia mfalme, Ee mfalme, uishi milele. MUNGU wangu amemtuma malaika Wake, na kuziba vinywa vya simba, wasinidhuru.” Hakuna madhara yaliyompata, na alimtukuza Bwana MUNGU wa

mbinguni. - (The Review and Herald, Mei 3, 1892) [Pr 145.2; Maombi Aya ya 83]

Sala ya Danieli yenye Bidii na Shauku—Wakati ulipokaribia mwisho wa miaka sabini ya utumwa wao (walikuwa mateka miaka 70), Akili ya Danieli ilifikiria na kuchunguza sana unabii wa Yeremia (Yer 25). Aliona kwamba wakati ulikuwa umefika ambapo Mungu angewapa watu Wake wateule jaribu lingine; na kwa kufunga, kujifedhehesha, na sala, alimsihi Mungu wa mbinguni kwa ajili ya Israeli, kwa maneno haya: “Ee Bwana, Wewe ni Mungu mkuu na wa kuogofya. Wewe ni Mwaminifu kwa agano lako na unawafadhili wakupendao na kuzitii amri Zako. Sisi Tumetenda dhambi, tumekosa, tumetenda maovu na kukuasi. Tumezikiuka amri Zako na kanuni Zako. Hatukuwasikiliza watumishi Wako manabii, ambao kwa Jina Lako waliongea na wafalme wetu, wakuu wetu, wazee wetu na taifa letu lote.” (Danieli 9:4-6)[Pr 145.3; Maombi Aya ya 84]

Danieli hatangazi uadilifu wake mwenyewe mbele za Bwana. Badala ya kudai kuwa safi na mtakatifu, nabii huyu aliyeheshimiwa anajitambulisha kwa unyenyekevu na yule mwenye dhambi tele wa Israeli. Hekima ambayo MUNGU alikuwa amempa ilikuwa bora zaidi kuliko hekima ya watu wakuu wa ulimwengu, kama vile nuru ya jua inayoangaza mbinguni wakati wa aduhuri inavyong'aa kuliko nyota dhaifu zaidi. Walakini tafakari ya maombi kutoka kwenye midomo ya mtu huyu aliyependelewa sana na Mbingu. Kwa unyonge na unyenyekevu/kujidhili kukubwa, kwa machozi na kupondeka kwa moyo, anasihi kwaajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wake. Anaiweka nafsi yake wazi mbele za MUNGU, akikiri kutostahili kwake na kukiri ukuu, utukufu na utawala wa Bwana. [Pr 146.1; Maombi Aya ya 85]

Ni unyoofu na ari iliyoje vilivyotawala dua zake! Mkono wa imani unainuliwa juu ili kushika ahadi zisizoshindwa kamwe za Yule Aliye Juu Zaidi. Nafsi yake inapigana mweleka kwa uchungu. Na ana ushahidi kuwa maombi yake yamesikika. Anajua kuwa ushindi ni wake. Ikiwa sisi kama watu tungeomba kama Danieli alivyoomba, na kupambana mieleka kama alivyopambana, tukizinyenyekeza nafsi zetu mbele za MUNGU, tunapaswa kutambua majibu ya maombi yetu kama yalivyotolewa kwa Danieli. Sikia jinsi

anavyosisitiza kesi yake katika nyua za mbinguni: [Pr 146.2; Maombi Aya ya 86]

“Ee MUNGU wangu, tega sikio Lako, usikie; fungua macho Yako, utazame ukiwa wetu, na mji ulioitwa kwa Jina Lako; kwa maana hatutoi maombi yetu mbele Zako kwa ajili ya haki yetu, bali kwa ajili ya rehema Zako nyingi. Ee Bwana, usikie; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, usikie ukafanye; usicheleweshe; kwa ajili Yako, Ee MUNGU wangu, kwa maana mji Wako na watu Wako wanaitwa kwa Jina Lako” (mistari 18, 19). [Pr 146.3; Maombi Aya ya 87]

Mtu wa MUNGU alikuwa akiomba baraka za Mbinguni juu ya watu Wake na ujuzi ulio wazi zaidi wa mapenzi ya MUNGU. Mzigo wa moyo wake ulikuwa kwa ajili ya Israeli, ambao hawakuishika sheria ya MUNGU kwa uthabiti kabisa. Alikubali kuwa misiba yao yote imewajia kama matokeo ya ukiukaji wao wa sheria hiyo takatifu. Anasema, “Tumetenda dhambi, tumetenda maovu Kwa sababu kwa ajili ya dhambi zetu, na maovu ya baba zetu, Yerusalemu na watu wako wamekuwa aibu kwa wote wanaotuzunguka” (mistari 15, 16). Wayahudi walikuwa wamepoteza tabia yao ya kipekee, takatifu kama watu waliochaguliwa na MUNGU. “Basi sasa, Ee MUNGU wetu, uyasikie maombi ya mtumishi wako, na dua zake, ukaangazie uso wako juu ya Patakatifu Pako palipojitenga” (mistari 17). Moyo wa Danieli unageukia kwa shauku kuu kuelekea Patakatifu pa Mungu palipojitenga, yaani kwenye upwek na mahame. Anajua kwamba usitawi wake unaweza kurejeshwa pale tu Israeli watakapotubu makosa yao ya kuasi sheria ya MUNGU, na kuwa wanyenyekevu, waaminifu na watiifu. [Pr 147.1; Maombi Aya ya 88]

Wakati maombi ya Danieli yanaendelea, malaika Gabrieli anakuja akishuka kutoka nyua za mbinguni kumwambia kwamba maombi yake yamesikilizwa na kujibiwa. Malaika huyu mwenye nguvu ameagizwa kumpa ujuzi na ufahamu—kufungua mbele yake siri na mafumbo ya enzi zijazo (vizazi vijavyo). Kwa hiyo, huku akitafuta kwa bidii kujua na kuelewa Ukweli, Danieli aliletwa katika ushirika na mjumbe aliyetumwa wa Mbinguni. [Pr 147.2; Maombi Aya ya 89]

Katika kujibu ombi lake, Danieli alipokea si tu nuru na Ukweli ambao yeye na watu wake walihitaji zaidi, bali mtazamo wa matukio makuu ya wakati ujao, hata ule ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Wale wanaodai kuwa wametakaswa, wakati hawana matamano/hamu ya kuchunguza Maandiko au kupigana mieleka na Mungu katika maombi ili kupata uelewa wa wazi wa ile Kweli ya Biblia, hawajui utakaso wa Kweli ni nini. (The Sanctified Life, 46-49) [Pr 147.3; Maombi Aya ya 90]

Nehemia

Ombi la Nehemia Ni Mfano kwa Watu wa MUNGU Leo—Mioyo ya wale wanaotetea jambo hili lazima ijazwe na Roho wa Yesu. Tabibu Mkuu peke yake Ndiye anayeweza kupaka zeri ya Gileadi (tiba/dawa). Hebu watu hawa wasome kitabu cha Nehemia kwa mioyo minyenyekevu iliyoguswa na Roho Mtakatifu, na mawazo yao ya uongo yatarekebishwa, na kanuni sahihi zitaonekana, na utaratibu uliopo sasa wa mambo utabadilishwa. Nehemia alimwomba MUNGU amsaidie, na MUNGU akasikia maombi yake. Bwana alifanya kazi kwenye mioyo ya wafalme wa mataifa wasiomjua Mungu wa mbinguni, waje kumsaidia. Wakati maadui zake walipofanya kazi kwa bidii dhidi yake, Bwana alifanya kazi kupitia wafalme kutekeleza kusudi Lake, na kujibu maombi mengi ambayo yalikuwa yakipanda kwenda Kwake kwa ajili ya msaada ambao waliuhitaji sana. - (The Review and Herald, Machi 23, 1911) [Pr 147.4; Maombi Aya ya 91]

Maombi yaliimarisha Imani na Ujasiri wa Nehemia—Kupitia wajumbe kutoka Yuda, yule mzalendo Mwebrania alijua kwamba siku za majaribu zilikuwa zimefika Yerusalemu, jiji lililochaguliwa. Mateka waliorudi walikuwa wakipitia mateso na aibu. Hekalu na sehemu za mji zilikuwa zimejengwa upya; lakini kazi ya kurejesha hali ya mji na ukarabati ilikuwa inazuiliwa, huduma za hekalu zilivurugwa, na watu wakaendelea kupata mshtuko wa kuogofya kwa sababu kuta za jiji bado zilikuwa magofu kwa sehemu kubwa. [Pr 148.1; Maombi Aya ya 92]

Akiwa amelemewa na huzuni, Nehemia hakuweza kula wala kunywa; "alilia, na kuomboleza siku kadha wa kadha, na kufunga." Katika huzuni yake alimgeukia Msaidizi wake ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe. "Niliomba," alisema,

"mbele za MUNGU wa mbinguni." Kwa uaminifu aliungama dhambi zake na dhambi za watu wake. Alisihi kwamba Mungu asimamie mambo ya Israeli, awarudishie ujasiri na nguvu, na awasaidie kujenga maeneo yaliyoharibiwa ya Yuda. [Pr 148.2; Maombi Aya ya 93]

Kadiri Nehemia alivyoomba, imani yake na ujasiri viliimarika. Kinywa chake kilijaa hoja takatifu. Alisonda kidole zile fedheha ambazo zingetupwa kwa Mungu, ikiwa watu Wake, ambao sasa wamerudi Kwake, wangeachwa katika udhaifu na mateso; naye akamsihi Bwana kutimiza ahadi Yake: "Mkinigeukia Mimi, na kuzishika Amri Zangu, na kuzifanya; ijapokuwa baadhi yenu walitupwa hata mwisho wa mbingu, lakini nitawakusanya kutoka huko, na kuwaleta mpaka mahali pale nilipochagua kuliweka Jina Langu huko." Tazama Kumbukumbu la Torati 4:29-31. Ahadi hii ilikuwa imetolewa kwa Israeli kupitia Musa kabla hawajaingia Kanaani, na kwa karne nyingi ilikuwa imesisima/imesalia hivyo bila kubadilika. Watu wa MUNGU sasa walikuwa wamemrudia Yeye kwa toba na imani, na ahadi Yake haikushindwa. Mara nyingi Nehemia alikuwa amemwaga roho yake kwa niaba ya watu wake. Lakini sasa alipokuwa akiomba kusudi takatifu lilijengwa akilini mwake. Aliazimia kwamba ikiwa angeweza kupata kibali cha mfalme, na usaidizi unaohitajika katika kupata zana na nyenzo, yeye mwenyewe angefanya kazi ya kujenga upya kuta za Yerusalemu na kurejesha nguvu za taifa la Israeli. Naye akamwomba Bwana amjalie kibali machoni pa mfalme, ili mpango huu utimie. "kufanikiwa, nakuomba, mtumishi wako leo," akasihi, "na umpe rehema machoni pa mtu huyu." [Pr 149.1; Maombi Aya ya 94]

Kwa miezi minne Nehemia alingoja nafasi nzuri ya kuwasilisha ombi lake kwa mfalme. Wakati huo, ingawa moyo wake ulikuwa mzito na wenye huzuni, alijitahidi kujistahi kwa uchangamfu mbele ya mfalme. Katika kumbi hizo za anasa (luxury) na fahari, lazima wote waonekane wenye moyo mwepesi na wenye furaha. Mifadhaiko isiweke kivuli chake juu ya uso wa mtumishi yeyote wa kifalme. Lakini katika nyakati za Nehemia za kupumzika kutoka kibaruni, wakati ambapo alikuwa haonekani machoni pa wanadamu, sala nyingi, maungamo, machozi, yalisikiwa na kushuhudiwa na MUNGU na malaika.— (Prophets and Kings, 628- 630) [Pr 149.2; Maombi Aya ya 95]

Nehemia Alikubali Dhambi Yake Binafsi Katika Maombi Yake— Sio tu kwamba Nehemia alisema kwamba Israeli walikuwa wametenda dhambi. Ila pia alikubali kwa toba kwamba yeye na nyumba ya baba yake walikuwa wamefanya dhambi. “Tumetenda kwa ufisadi dhidi Yako,” alisema, akijiweka mwenyewe miongoni mwa wale ambao walikuwa wamemvunjia MUNGU heshima kwa kutosimama kwa imara kwa ajili ya ile Kweli.... [Pr 149.3; Maombi Aya ya 96]

Nehemia alijinyenyekeza mbele za MUNGU, akimpa Yeye utukufu unaostahili Jina Lake. Ndivyo pia alivyofanya Danieli huko Babeli. Hebu tujifunze maombi ya watu hawa. Yanatufundisha kwamba tunapaswa kujinyenyekeza, lakini kwamba hatupaswi kamwe kufuta mpaka au mstari kati ya watu wa MUNGU wanaoshika amri na wale ambao hawaheshimu sheria Yake.—(SDA Bible Commentary 3:1136) [Pr 149.4; Maombi Aya ya 97]

Nehemia Aliomba, Akiwa na Uhakika Kwamba MUNGU Angetimiza Ahadi Zake—Imani yake ikishikilia sana ahadi za Bwana, Nehemia aliwasilisha kwenye Kiti cha Rehema cha mbinguni ombi lake kwamba MUNGU angedumisha kazi ya watu Wake wenye kutubu, na kurejesha nguvu zao; na kujenga mahali pao palipokuwa mahame. MUNGU alikuwa mwaminifu kwa vitisho Vyake wakati watu Wake walipojitenga Naye; Alikuwa amewatapanya kote kati ya mataifa, kulingana na Neno Lake. Naye Nehemia alipata katika Ukweli huu uhakikisho kwamba Bwana Angekuwa Mwaminifu vile vile katika kutimiza ahadi Zake (kuwarudisha).—(SDA Bible Commentary 3:1136) [Pr 150.1; Maombi Aya ya 98]

Nehemia Alifanya Sala Zake Kuendana na Mahitaji ya Wakati Huo—kumbukumbu ya hali ya Yerusalemu iliamsha huruma ya mfalme bila kuamsha chuki zake. Swali lingine lilitoa fursa ambayo Nehemia alikuwa ameingoja kwa muda mrefu: “Unataka nini? Lakini mtu wa MUNGU hakuthubutu kujibu mpaka alipotaka mwongozo kutoka kwa Yule Aliye juu kuliko Artashasta. Alikuwa na muamala/dhamana takatifu ya kutimiza, ambao ulihitaji msaada kutoka kwa mfalme; na alitambua kwamba mengi yalitegemea juu ya kuwasilisha kwake jambo hilo kwa njia ya kupata kibali chake mfalme na kuomba msaada wake. “Nikaomba,” alisema, “kwa MUNGU wa mbinguni.” Katika sala hiyo fupi

Nehemia alisisitiza katika uwepo wa Mfalme wa wafalme na kushinda nguvu inayoweza kugeuza mioyo kama mito ya maji inavyogeuzwa. [Pr 150.2; Maombi Aya ya 99]

Maombi ya Nehemia yaliimarishwa na Kusudi Imara—Kuna hitaji la kuwa na akina Nehemia katika kanisa leo,—sio watu wanaoweza kuomba na kuhubiri tu, bali watu ambao maombi na mahubiri yao yameimarishwa kwa kusudi thabiti na yenye maazimio yenye shauku.—(The Signs of the Times, Desemba 6, 1883) [Pr 150.3; Maombi Aya ya 100]

Kama Nehemia, sisi tunaweza kuomba Wakati Wowote au Mahali Popote—Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya hitaji ni nyenzo ya kumuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zitashindikana. Watenda kazi wanaohenyekakwa bidii katika safari ya maisha, waliokuwa katika msongamano na kutindikiwa na wasiwasi au fedheha, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya mwongozo Wake wa Kiungu/mbingu. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi kuwasaidia waaminifu Wake, wale wanaoamini, kila wanapomwita. Katika kila jambo, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na jaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, na sapoti/utegemezi katika upendo usiokoma na nguvu ya MUNGU anayeshika agano. [Pr 151.1; Maombi Aya ya 101]

Katika wakati huo mfupi wa maombi kwa Mfalme wa wafalme, Nehemia alikusanya ujasiri kumwambia Artashasta kuhusu matamano yake ya kupewa muda kutoka katika majukumu yake katika nyua za kifalme, naye akaomba mamlaka ya kujenga mahali palipokuwa ukiwa Yerusalemu na kupafanya tena kuwa jiji lenye nguvu na ulinzi. Matokeo muhimu kwa taifa la Kiyahudi yalikita kwenye ombi hili. “Na,” Nehemia atangaza, “mfalme alinipa kibali, kulingana na mkono mwema wa MUNGU wangu ulio juu yangu.” (Prophets and Kings, 631-633) [Pr 151.2; Maombi Aya ya 102]

MUNGU katika majaliwa Yake haturuhusu kuujuu mwisho tangu mwanzo; bali anatupa nuru ya Neno Lake ili kutuongoza tunapopita, na anatuagiza kuweka mawazo yetu kukita kwa Yesu. Popote tulipo, haijalishi kazi tuliyo nayo, mioyo yetu inapaswa kuinuliwa kwa MUNGU katika maombi. Hii ni kuwa na utayari kuomba wakati wowote. Hatuhitaji kusubiri hadi tuweze kupiga magoti kabla ya kuomba. Wakati fulani, Nehemia alipofika mbele ya mfalme, mfalme aliuliza ni kwanini alionekana mwenye huzuni, na ni ombi gani aliazimia kumwambia mfalme. Lakini Nehemia hakuthubutu kujibu papo hapo. Masilahi muhimu yalikuwa hatarini. Hatima ya taifa ilining'inia juu ya mtazamo ambao unapaswa kutengenezwa juu ya akili ya mkuu wa himaya; naye Nehemia akatuma maombi kwa MUNGU wa Mbinguni, kabla hajathubutu kumjibu mfalme. Matokeo yake ni kwamba alipata yote aliyoomba au hata yale aliyotamani. - (The Signs of the Times, October 20, 1887) [Pr 151.3; Maombi Aya ya 103]

Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutuma ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika moyo wa maombi ya dhati na bidii. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama alivyofanya Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kufungua mlango wa moyo kila wakati na mwaliko wetu kwa Yesu kwenda juu ili aje kukaa kama mgeni wa mbinguni katika nafsi zetu (mioyo yetu). [Pr 151.4; Maombi Aya ya 104]

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira yenye uchafuzi, ufisadi, na uharibifu karibu nasi, hatuhitaji kuvuta pumzi ya harufu ya uvundo wake, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango kwa mawazo yasiyofaa na mawazo yasiyo matakatifu kwa kuinua roho mbele ya MUNGU kupitia maombi ya dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea msaada na baraka za MUNGU watatembea katika angahewa takatifu kuliko ile ya dunia na watakuwa na ushirika wa mara kwa mara na mbingu. —(Steps to Christ, 99). [Pr 152.2; Maombi Aya ya 105]

Nehemia Aliomba kwa Bidii Usiku Wote—Kwa siri na kimya, Nehemia alikamilisha mzunguko wake wa zile kuta.

Anatupa habari kuwa “Watawala hawakujua nilikokwenda, wala nilichokofanya; wala nilikuwa sijawaambia Wayahudi, wala makuhani, wala wakuu, wala viongozi, wala wengine waliofanya kazi hiyo.” Katika uchunguzi huu mchungu hakutaka kuvutia umakini wa marafiki au maadui, taharuki isije ikazuka, na ripoti kuletwa na kusambaa, jambo ambalo Ingeweza kufanya misheni kufeli au hata kuzuia, kazi yake. Nehemia alitumia muda uliosalia wa usiku kwa maombi; asubuhi lazima kuwe na jitihada ya bidii ya kuwaamsha na kuwaunganisha watu wa nchi yake waliokata tamaa na waliogawanyika.— (Christian Service, 174) [Pr 152.3; Maombi Aya ya 106]

Mafanikio ya Nehemia Yanaonyesha Nguvu ya Maombi— Katika kazi yao, Ezra na Nehemia walijinyenyekeza mbele ya MUNGU, wakiungama dhambi zao na dhambi za watu wao, na kuomba msamaha kana kwamba wao wenyewe ndio wakosaji. Kwa subira walijitaabisha kufanya kazi, wakisali na kuteseka. Jambo ambalo lilifanya kazi yao kuwa ngumu zaidi lilikuwa sio uadui wa wazi wa watu wa mataifa (wapagani), bali upinzani wa siri wa marafiki wa kujifanya, ambao, kwa kutoa ushawishi wao kwa ajili ya huduma za uovu, waliongeza mzigo mara kumi zaidi, kwa watumishi wa MUNGU. Wasaliti hawa waliwapa adui za Bwana nyenzo za kutumia katika vita vyao juu ya watu Wake. Tamaa zao mbaya na nia yao ya uasi vilikuwa vikipigana vita daima na matakwa ya MUNGU yaliyo wazi. [Pr 152.4; Maombi Aya ya 107]

Mafanikio yanayoambatana na jitihada za Nehemia yanaonyesha kile ambacho sala, imani, hekima na utendaji wenye msukumo wa bidii unavyoweza kutimiza. Nehemia hakuwa kuhani; hakuwa nabii; hakuajifanya kuwa na cheo cha juu. Mtu huyu alikuwa mwanamatengenezo aliyeinuliwa kwa wakati muhimu. Lilikuwa lengo lake kuwaweka watu wake kuwa waadilifu kwa MUNGU (waweke mambo yao sawa na Mungu). Akisukumwa na kusudi kuu, alipinda/aliweka kila nguvu ya uhai wake ili kutimiza lengo hilo. Uadilifu wa hali ya juu, usiobadilika uliashiria juhudi zake. Alipokutana na uovu na upinzani katika kutenda kile kilicho haki, alichukua msimamo mkali sana kiasi kwamba watu waliamshwa kufanya kazi kwa bidii na ujasiri mpya. Hawakuwa na jinsi isipokuwa kutambua uaminifu wake, uzalendo wake, na upendo wake wa kina kwa MUNGU; na,

walipoona hivyo, walikuwa tayari kufuata alikowaongoza.—
(Prophets and Kings, 675, 676) [Pr 153.1; Maombi Aya ya
108]

Yohana Mbatizaji

Yohana Alitumia Muda Katika Kutafakari na Kuomba Kujua mapenzi ya MUNGU kwa ajili ya maisha yake—Maisha ya Yohana hayakutumika katika uvivu, uzembe, utawa, au kujitenga kwa ubinafsi. Mara kwa mara alienda kuchangamana na watu; na alikuwa mtazamaji makini mwenye nia ya kujua kile kilichokuwa kinaendelea duniani. Akiwa kwenye pumziko lake tulivu nyikani alitazama matukio yalivyokuwa. Akiwa na maono yaliyoangaziwa na Roho wa MUNGU alisoma tabia za wanadamu, ili apate kuelewa jinsi ya kuifikia mioyo yao kwa ujumbe wa mbinguni. Mzigo wa utume wake ulikuwa juu yake. Akiwa peke yake, kwa kutafakari na kusali, alitafuta kujifunga mshipi wa uimara kwenye nafsi yake kwa ajili ya kazi ya maisha iliyokuwa mbele yake.—(The Desire of Ages, 102) [Pr 153.2; Maombi Aya ya 109]

Maombi Yalimwezesha Yohana Kuwakabili Wafalme wa Dunia—Yohana Mbatizaji katika maisha yake ya jangwani alifundishwa na MUNGU. Alisoma mafunuo ya MUNGU katika asili/uumbaji. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, alisoma hati-kunjo za manabii. Mchana na usiku, Kristo alikuwa somo lake, na tafakari yake, mpaka akili na moyo na roho vilijaa maono yenye utukufu. [Pr 153.3; Maombi Aya ya 110]

Alimtazama Mfalme katika uzuri Wake, na nafsi yake ikapotea (ubinafsi wake ukaisha). Aliona ukuu wa utakatifu na akajua kwamba anapokuwa peke yake, basi, hana ufanisi na stahiki. Ulikuwa ni ujumbe wa MUNGU ambao alipaswa kuutangaza. Ilikuwa katika uwezo wa MUNGU na haki Yake kwamba alipaswa kusimama. Alikuwa tayari kwenda kama mjumbe wa Mbinguni, bila kukatishwa tamaa na mwanadamu, kwa maana alikuwa amemtazama MUNGU. Angeweza kusimama bila woga mbele ya wafalme wa kidunia kwa sababu kwa kutetemeka alikuwa ameinama na kusujudu mbele ya Mfalme wa wafalme.— (Testimonies for the Church 8:331, 332) [Pr 154.1; Maombi Aya ya 111]

Petro

MUNGU Alijibu Sala ya Petro ya Kumfufua Dorkasi—Moyo wa mtume huyo uliguswa na huruma alipoona huzuni yao. Kisha, akielekeza kwamba marafiki waliokuwa wakilia watolewe chumbani, alipiga magoti na kusali kwa dhati na bidii kwa MUNGU ili amrudishie Dorkasi uhai na afya. Akiugeukia ule mwili, akasema, Tabitha, inuka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro, akaketi.” Dorkasi alikuwa amefanya utumishi mkubwa kwa kanisa, na MUNGU aliona inafaa kumrudisha kutoka nchi ya adui, ili ustadi wake na nguvu zake zipate kuwa baraka kwa wengine, na pia kwamba kwa udhihirisho huu wa uweza Wake kusudi la Kristo lipate kuimarishwa.— (Matendo ya Mitume, 132) [Pr 154.2; Maombi Aya ya 112]

SURA YA 14

SALA YA KILA SIKU

Sala ni Muhimu Kama Chakula Chetu cha Kila Siku—Ikiwa tutakuza tabia ambayo MUNGU anaweza kukubali (kuipa kibali), ni lazima tutengeneze mazoea sahihi katika maisha yetu ya kidini. Maombi ya kila siku ni muhimu kwa ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha muda kwa ustawi wa kimwili na kiakili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika sala. Akili ikimangamanga, lazima tuirudishe; kwa bidii ya kudumu, na isiyochoka, mazoea haya hatimaye yatafanya iwe rahisi. Hatuwezi kujitenga mbali na Kristo hata wakati mmoja tukawa salama. Tunaweza kuwa na uwepo Wake pamoja nasi katika kila hatua, lakini kwa kuzingatia tu masharti ambayo Yeye Mwenyewe ameweka. —(Messages to Young People, 115.114, 115) [Pr 155.1; Maombi Aya ya 1]

Hitaji letu la sala ya kila siku- Wote wanaokuja kwa Kristo leo wanapaswa kukumbuka kuwa haki na sifa Yake ni uvumba unaochanganywa na maombi ya wale wanaotubu

dhambi zao na kupokea msamaha na rehema na neema. Hitaji letu la maombezi ya Kristo ni la daima, endelevu. Siku baada ya siku, asubuhi na jioni, moyo mnyenyekevu unahitaji kutoa maombi ambayo yatarudishiwa majibu ya neema na amani na furaha. “Basi kupitia Yeye na tutoe dhabihu ya sifa kwa MUNGU mara kwa mara, yaani, tunda la midomo yetu itoe shukrani kwa Jina Lake. Lakini msisahau kutenda mema na kuwasiliana; kwa maana dhabihu za namna hii MUNGU hupendezwa nazo” (SDA Bible Commentary 6:1078) [Pr 155.2; Maombi Aya ya 2]

Anza Siku Yako Kwa Maombi—Ni upendeleo kwetu kufungua mioyo yetu, na kuruhusu mwanga wa jua wa uwepo wa Kristo uingie. Kaka yangu, dada yangu, hebu uso wako uitazame nuru (ikabili nuru). Njoo katika mawasiliano halisi ya na ya binafsi na Kristo, ili uweze kuwa na ushawishi wa kuinua na kuleta uamsho. Acha imani yako iwe imara na safi na thabiti. Hebu shukrani kwa MUNGU ijaze mioyo yenu. Unapoamka asubuhi, piga magoti kando ya kitanda chako, na kisha umwombe MUNGU akupe nguvu ya kutimiza majukumu ya siku, na kukabiliana na majaribu yake. Mwambie Yeye akusaidie kuleta katika kazi yako utamu na uzuri wa tabia ya Kristo. Muombe akusaidie wewe kusema maneno ambayo yatawapatia wale wanaokuzunguka tumaini na ujasiri, na kukusogeza karibu na Mwokozi. (Sons and Daughters of God, 199)- [Pr156.1; Maombi Aya ya 3]

Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi zako kwa ombi. Usifikirie kuwa huku ni kupoteza muda, au muda uliopotea tu; kwani ni muda ambao utaishi kwa nyakati za milele. Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho utaletwa. Mwili wako utajibu mguso wa mkono wa Mwalimu Mkuu (maschine ya mwili itajibu Mguso wa Bwana). Hakika kuomba baraka ya MUNGU kunastahili wakati wetu, na kazi haiwezi kufanywa kwa usahihi isipokuwa ina mwanzo sahihi.— (Testimonies for the Church 7:194) [Pr 156.2; Maombi Aya ya 4]

Ndugu na dada zangu, wazee na vijana, mnapokuwa na saa moja ya kupumzika na burudani (mnapokuwa hamna la kufanya), fungueni Biblia na mhifadhi akilini mwenu na Kweli zake wa thamani. Unapojishughulisha na kazi, linda akili, uwe thabiti katika kuiachilia akili iendeleo kukaa kwa

MUNGU, ongea kidogo, na tafakari zaidi. Kumbuka: "Kila neno lisilofaa ambalo watu watazungumza, watatoa hesabu yake siku ya hukumu." Chunga maneno yako kwa kuyachagua kwa uangalifu kabla ya kuyatamka; hii itafunga mlango dhidi ya adui wa roho. Hebu uingie katika siku yako mpya kwa kuanza na maombi; fanya kazi kama upo machoni pa MUNGU. Malaika Wake huwa karibu nawe kila wakati, wakirekodi maneno yako, hulka na mwenendo wako, na namna ya utendaji kazi wako. Unapoacha ushauri mzuri na kuchagua kushirikiana na wale ambao una sababu ya kuwashuku kwamba hawana mwelekeo wa mambo ya kidini/kiroho, ingawa wanadai kuwa Wakristo, hivi karibuni utakuwa kama wao. Unajiweka mwenyewe katika barabara ya majaribu, kwenye uwanja wa vita wa Shetani, na, pasipo ulinzi endelevu, wewe utashindwa na hila zake mwovu.—(Testimonies for the Church 4:588, 589) [Pr 156.3; Maombi Aya ya 5]

Mwendee Bwana kila siku kwa ajili ya mafundisho na mwongozo; Mtegemee MUNGU kwa nuru na maarifa. Omba kwa ajili ya mafundisho haya na mwanga huu, hadi upate. Haitakufaa wewe kuomba, kisha ukasahau jambo uliloliombea. Weka akili yako juu ya maombi yako. Unaweza kufanya hivyo wakati unafanya kazi kwa mikono yako. Unaweza kusema, Bwana, naamini; kwa moyo wangu wote naamini Acha nguvu za Roho Mtakatifu zije juu yangu. — (Fundamentals of Christian Education, 531) [Pr 157.1; Maombi Aya ya 6]

Katika kumfuata Kristo, ukimtazama Yeye ambaye Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yako, utahisi kuwa unafanya kazi chini ya jicho Lake, kwamba unashawishiwa na uwepo Wake, na kwamba Yeye Anajua nia zako. Katika kila hatua utauliza kwa unyenyekevu: Je! Hii itampendeza Yesu? Je! Itamtukuza MUNGU? Asubuhi na jioni sala zako za dhati zinapaswa kupaa kwa MUNGU kwa ajili ya baraka na mwongozo Wake. Maombi ya Kweli hujitegemeza kwa Mweza na hutupatia ushindi. Akiwa amepiga magoti yake Mkristo hupata nguvu za kushinda vishawishi.— Yoh. (Testimonies for the Church 4:615) [Pr 157.2; Maombi Aya ya 7]

Tenga muda kila siku kwa ajili ya maombi — Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma

Maandiko, wataunganishwa na mbingu na watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo makuu, matamano bora, ufahamu dhahiri kuhusu ile Kweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa wana matamano ya kuwa na usafi wa moyo, utakaso wa moyo, kuwa na nuru, kuwa na upendo, na kuwa na neema zote zitokazo mbinguni. Maombi yao ya dhati na bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia (Waebrania 8 na 9 na Walawi 16). Kundi hili litakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yule Asiye na kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni upo kwa ajili yao, na watasafishwa, watatakaswa, watainuliwa, wataboreshana kuadilishwa na uhusiano huu wa karibu na MUNGU. Huo ndio upendeleo walionao Wakristo wa kweli. [Pr 157.3; Maombi Aya ya 8]

Kutafakari nadharia tu bila vitendo halisi haitoshi (abstract meditation); shughuli au utendaji mwingi pia hautoshi; vyote viwili ni muhimu kwa uundaji wa tabia ya Kikristo. Nguvu inayopatikana katika maombi ya dhati, na ya siri, hututayarisha kustahimili vivutio/vishawishi vibaya kwenye jumuiya. Na bado hatupaswi kujitenga na ulimwengu, kwani uzoefu wetu wa Kikristo unapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. Jamii ya wasioamini haitatudhuru ikiwa tutachangamana nao kwa kusudi la kuwaunganisha na Mungu na kuwa na nguvu za kutosha kiroho kuhimili ushawishi wao. - (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 158.1; Maombi Aya ya 9]

Matokeo ya Maombi ya kila siku -Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada, uwezo, kwa maombi ya dhati na bidii kila siku, itakuwa na matamano bora, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, malengo yaliyo ya juu katika utendaji wa kazi, na taendelea daima kuwa na njaa na kiu ya haki.—(God's Amazing Grace 317) [Pr 25.4; Maombi Aya ya 10]

Kwa kudumisha uhusiano na MUNGU, na kisha kupitia ushirika wetu na watu wengine, tutawezeshwa kusambaza kwa wanadamu wenzetu nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni mwetu. Nguvu inayopatikana katika sala kwa MUNGU, ikiunganishwa na jitihada ya kudumu katika kuzoeza akili katika kufikiria, umakini na kutenda, hutayarisha mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na

kuiweka roho katika amani chini ya hali zote. [Pr 158.2; Maombi Aya ya 11]

Tukimkaribia Mungu, Yeye ataweka neno kinywani mwetu kuzungumza kwa niaba Yake, hata sifa kwa Jina Lake. Yeye Atatufundisha mkazo kutoka katika wimbo wa malaika, hata shukrani kwa Baba yetu wa mbinguni. Katika kila tendo la maisha, nuru na upendo wa Mwokozi anayeishi ndani vitafunuliwa mbele za watu. Shida za nje haziwezi kuyafikia maisha ya mtu ambaye anaishi kwa imani katika Mwana wa MUNGU.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 85) [Pr 158.3; Maombi Aya ya 12]

Maombi yanahitajika Kila Siku Ili Kumpinga (kumsukuma) Shetani – Utakaso sio kazi ya wakati mmoja, nukta moja, saa moja, siku moja au wakati mmoja. Ni ukuaji endelevu katika neema. Hatujui hata siku moja changamoto au mzozo wetu vitakuwa na nguvu kiasi gani siku inayofuata. Shetani anaishi, na anafanya kazi kwa bidii, na kila siku tunahitaji kumlilia MUNGU kwa dhati ili kupata msaada na nguvu za kumpinga. Maadamu Shetani anatawala (na hajaongoka) tutapaswa kutiisha ubinafsi daima, tutakuwa na usumbufu na mashambulizi ya kukabili, na hakuna mahali ambapo tutasimama (na kujishangilia tumefika), hakuna hatua ambayo tunaweza kuichukua na kusema tumeiwezea kikamilifu. – (Testimonies for the Church 1:340) [Pr 158.4; Maombi Aya ya 13]

Maombi ya Kila Siku yajumuishe Mahitaji ya Kimwili na Kiroho— Maombi ya mkate wa kila siku yanajumuisha sio tu chakula cha kutegemeza mwili, lakini mkate wa kiroho ambao utarutubisha na kulisha roho hata kwenye uzima wa milele. Yesu anatuagiza, “Msikifanyie kazi chakula chenye kuharibika, bali kile kidumucho hata uzima wa milele.” Yohana 6:27. Anasema, "Mimi Ndimi mkate hai uliyoshuka kutoka mbinguni. Mtu yeyote akila mkate Huu, ataishi milele." Mstari wa 51. Mwokozi wetu ni mkate wa uzima, na ni kwa kutazama upendo Wake, kwa kuupokea rohoni, ndio tunakula mkate ulioshuka kutoka mbinguni. [Pr 159.1; Maombi Aya ya 14]

Tunampokea Kristo kupitia Neno Lake, na Roho Mtakatifu anatolewa ili kulifungua Neno la MUNGU katika ufahamu wetu, na kuleta Kweli Zake mioyoni mwetu. Tunapaswa kuomba siku baada ya siku kwamba tunaposoma

Neno lake, ili MUNGU atume Roho Wake ili kutufunulia Ukweli ambao utaimarisha roho zetu kwa hitaji la siku. [Pr 159.2; Maombi Aya ya 15]

Katika kutufundisha kuomba kila siku kile tunachohitaji – baraka za kimwili na za kiroho—MUNGU ana kusudi la kutimiza kwa manufaa yetu. Yeye angependa tutambue utegemezi wetu juu ya utunzaji Wake wa daima/endelevu, kwa kuwa anatafuta kutuvuta katika ushirika na Yeye Mwenyewe. Katika mawasiliano na ushirika huu na Kristo, kwa njia ya maombi na kujifunza zile Kweli kuu na za thamani za Neno Lake, kama roho zenye njaa tutalishwa; kama wale walio na kiu, tutaburudishwa kwenye chemchemi ya uzima.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 112, 113) [Pr 159.3; Maombi Aya ya 16]

Kama Wakristo wa awali, Tunahitaji Kuomba Kila Siku kwa Ajili ya Roho Mtakatifu—Wale ambao katika Pentekoste walivishwa nguvu kutoka juu, hawakuwekwa huru dhidi ya mitihani na majaribu siku za mbeleni. Waliposhuhudia Ukweli na haki, walishambuliwa mara kwa mara na adui wa Kweli zote, ambaye alitaka kuwaibia uzoefu wao wa Kikristo. Walilazimika kujitahidi kwa nguvu zao zote walizopewa na MUNGU kufikia kiwango cha mfano wa wanaume na wanawake walio katika Kristo Yesu. Kila siku waliomba msaada mpya wa neema, ili waweze kufikia juu na juu zaidi kuelekea ukamilifu. Chini ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu hata wale walio dhaifu, kwa kuizoeza imani yao kwa MUNGU, walijifunza kuboresha nguvu walizokabidhiwa na kutakaswa, kusafishwa, na kuboreshwa. Kwa unyenyekevu walijitiisha chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, wakapokea utimilifu wa Uungu, nao wakaandaliwa kuwa mfano wa MUNGU. - (The Acts of the Apostles, 49, 50) [Pr 159.4; Maombi Aya ya 17]

Kupita kwa wakati hakujaleta mabadiliko katika ahadi ya Kristo alipokuwa akiondoka ya kumtuma Roho Mtakatifu kama mwakilishi Wake. Si kwa sababu ya kizuizi chochote kwa upande wa MUNGU kwamba utajiri wa neema Yake hautiririki duniani kwa wanadamu. Ikiwa utimilifu wa ahadi hauonekani jinsi unavyoweza kuonekana, ni kwa sababu ahadi haithaminiwi kama inavyopaswa kuthaminiwa. Kama wote wangekubali, wote wangejazwa na Roho Mtakatifu. Popote pale ambapo hitaji la Roho Mtakatifu ni jambo linalofikiriwa kwa udogo sana, panaonekana kuwa na

ukame wa kiroho, giza la kiroho, mporomoko wa kiroho na kifo. Wakati mambo madogo yanachukua umakini, na nguvu ya Kiungu/Bwana ambayo ni muhimu kwa ukuaji na ustawi wa kanisa, na ambayo italeta baraka zingine zote kwenye mlolongo wake, kama mabehewa ya treni, inakosekana, ingawa hutolewa kwa wingi Wake usio na kipimo. [Pr 160.1; Maombi Aya ya 18]

Kwa kuwa hii ndiyo njia ambayo kwayo tunapaswa kupokea nguvu, Je, kwa nini hatuna njaa na kiu ya karama ya Roho? Kwa nini hatuizungumzii, hatuiombei, na kuhubiri kuhusu hiyo? Bwana Yupo tayari sana kumtoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomtumikia zaidi ya wazazi wanavyokuwa na shauku ya kutoa zawadi bora kwa watoto wao. Kila mfanyakazi anapaswa kutoa ombi lake kwa MUNGU kwa ubatizo wa kila siku wa Roho. Vikundi vya watendakazi Wakristo vinapaswa kukusanyika ili kuomba msaada wa kipekee, kwa ajili ya hekima ya mbinguni, ili wajue jinsi ya kupanga na kutekeleza mikakati kwa hekima. Hasa, wanapaswa kuomba ili MUNGU awabatize mabalozi Wake waliochaguliwa kufanya kazi kwenye maeneo ya misheni, kwa kipimo kikubwa cha Roho Wake. Uwepo wa Roho pamoja na watenda kazi wa MUNGU utatoa nguvu juu ya utangazaji wa Ukweli ambao hakuna heshima au utukufu wote wa ulimwengu ungeweza kutoa.—(The Acts of the Apostles , 49-51) [Pr 160.2; Maombi Aya ya 19]

Ombea Neema kwa Mahitaji ya Kila Siku—Ukweli wa MUNGU uliopokelewa moyoni unaweza kukufanya uwe na hekima hata kufikia wokovu. Kwa kuiamini na kuitii ile Kweli, utapokea neema ya kutosha kwa ajili ya majukumu, mitihani na majaribu ya leo. Hautitaji Neema ya kesho. Unapaswa kuhisi kuwa unahusika na leo tu (siyo changamoto za kesho). Kushinda kwa leo; kujikana kwa leo; kuomba na kukesha kwa leo; kupata ushindi katika MUNGU leo. Hali zetu na mazingira yetu, mabadiliko ya kila siku yanayotuzunguka, na Neno lililoandikwa na MUNGU ambalo hutambua na kuthibitisha mambo yote hayo, hivi vinatosha kutufundisha wajibu wetu na kile ambacho tunapaswa kufanya, siku baada ya siku. Badala ya kuitesa akili yako kukimbia katika njia ya mawazo ambayo hutapata faida yoyote nayo, wewe unapaswa kuwa unachunguza Maandiko kila siku na kufanya kazi zile za maisha ya kila siku ambazo sasa zinaweza kuonekana ni

usumbufu tupu, lakini ni zile ambazo lazima zifanywe na mtu fulani.—(Testimonies for the Church 3:333) [Pr 160.3; Maombi Aya ya 20]

Omba kila siku kwa ajili ya Uelewa wa Biblia – Wale wanaodai kumwamini Yesu, daima wanapaswa kusonga mbele kwenye nuru kwa bidii. Wanapaswa kuomba kila siku, ili nuru ya Roho Mtakatifu iangaze kwenye kurasa za Kitabu Kitakatifu (Biblia), ili waweze kuwezesha kuelewa mambo ya Roho wa MUNGU. - (Fundamentals of Christian Education, 188, 189) [Pr 161.1; Maombi Aya ya 21]

Omba Kila Siku kwa ajili ya Baraka Inayoletwa na Sabato – Wote wanaoichukulia Sabato kama ishara kati yao na MUNGU, wakionyesha kwamba Yeye Ndiye MUNGU anayewatakasa, watawakilisha kanuni za serikali Yake. Wataleta katika utendaji wao wa kila siku sheria za ufalme Wake. Itakuwa ombi lao la kila siku kwamba utakaso wa Sabato uwe juu yao. Kila siku watakuwa na ushirika wa Kristo na wataonyesha ukamilifu wa tabia Yake. Kila siku nuru yao itawaangazia wengine kupitia matendo mema.— (Testimonies for the Church 6:353) [Pr 161.2; Maombi Aya ya 22]

Ombi la kila siku la Mzazi—Fanya kazi yako iwe ya kupendeza kwa nyimbo za sifa. Ikiwa ungependa kuwa na rekodi safi katika vitabu vya mbinguni, usiudhike, usikerwe, wala kukemea. Acha sala yako ya kila siku iwe, "Bwana, nifundishe kutenda vyema. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu." Mlete Kristo katika yote unayoyafanya. Ndipo maisha yenu yatajazwa na mwangaza na shukrani. Hebu na tujitahidi, tukiendelea kusonga mbele kwa uchangamfu katika utumishi wa Bwana, mioyo yetu ikiwa imesheheni furaha Yake.—(Child Guidance, 148) [Pr 161.3; Maombi Aya ya 23]

Vijana waombe Kila Siku kwa ajili ya Hekima na Neema – Majaribu na ufukara ambao vijana wengi wanalalamikia, Kristo alivumilia bila kunung'unika. Na nidhamu hii ndiyo ule uzoefu ambao vijana wanauhitaji, na ambao utawapa uthabiti katika tabia zao, na kuwafanya wawe kama Kristo, wenye nguvu katika roho ya kupinga majaribu. Hawataweza kushindwa na hila za Shetani, ikiwa watajitenga na ushawishi wa wale ambao watawapotosha na kuharibu maadili yao. Kupitia maombi ya kila siku kwa

MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake, ya kubeba migogoro na uhalisia mkali wa maisha, na kuwa washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kutunzwa tu kwa kukesha na kuomba. Maisha ya Kristo yalikuwa kielelezo cha nguvu ya kudumu, ambacho hakikuruhusiwa kudhoofishwa na lawama, dhihaka, ufukara au shida. [Pr 162.1; Maombi Aya ya 24]

Ndivyo inavyopaswa kuwa kwa vijana. Ikiwa Majaribu yataongezeka juu yao, wanaweza kujua kwamba MUNGU anajaribu na kudhihirisha uaminifu wao. Na ni katika kiwango hicho tu ambacho wanadumisha uadilifu wao wa tabia katika mazingira ya kukatishwa tamaa, ndipo uimara, ujasiri, uthabiti, na uwezo wao wa kustahimili utakapongezeka, nao watakuwa na nguvu katika roho.— (Messages to Young People, 80) [Pr 162.2; Maombi Aya ya 25]

Haja ya Mwalimu Kusali Kila Siku—Kila mwalimu anapaswa kupokea kila siku mafundisho kutoka kwa Kristo, na anapaswa kufanya kazi daima chini ya uongozi Wake. Haiwezekani kwake kuelewa vizuri au kufanya kazi yake ipasavyo isipokuwa anakuwa na Mungu katika maombi mengi. Ni kwa msaada wa Bwana tu, pamoja na unyofu wa moyo, na juhudi katika kujikana, ndipo anaweza kutumaini kufanya kazi yake kwa busara na vizuri zaidi. [Pr 162.3; Maombi Aya ya 26]

Pasipo Mwalimu kutambua hitaji la maombi na kuunyenyekeza moyo wake mbele za MUNGU, atapoteza moyo/kiini hasa cha elimu. Anapaswa kujua jinsi ya kuomba na ni lugha gani aitumie katika maombi. “Mimi ni Mzabibu,” Yesu alisema, “ninyi ni matawi; yule akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo atazaa matunda mengi; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.” Yohana 15: 5 Mwalimu anapaswa kuacha matunda ya imani yaonekane katika maombi yake. Anapaswa kujifunza jinsi ya kuja mbele za Bwana na kumsihi Yeye kwa sala mpaka apate uhakikisho kwamba maombi yake yamesikiwa.—(Counsels to Parents, Teachers, and Students, 231) [Pr 162.4; Maombi Aya ya 27]

Katika Nyakati za Agano la Kale, Waisraeli Waliomba Kila Siku— Pale makuhani walipoingia asubuhi na jioni katika Patakatifu wakati wa uvumba, dhabihu ya kila siku

ilikuwa tayari kutolewa juu ya madhabahu katika ua wa nje. Huu ulikuwa wakati wa kupendeza sana kwa washiriki waliokusanyika mahali pa kuabudia. Kabla ya kuingia katika uwepo wa MUNGU kupitia huduma ya kuhani, walipaswa kuichunguza mioyo yao kwa dhati na kukiri dhambi zao. Waliungana katika sala ya kimya, na nyuso zao zikielekea mahali Patakatifu. Hivyo maombi yao yalipanda juu pamoja na wingu la uvumba, imani yao ikiwa imeshikilia sifa/stahiki za Mwokozi aliyeahidiwa ambaye aliwakilishwa na dhabihu ya upatanisho. Saa zilizowekwa kwa ajili ya dhabihu ya asubuhi na ya jioni zilizingatiwa kuwa takatifu, na zikaadhimishwa kama muda wa ibada katika taifa lote la Kiyahudi. Na katika nyakati za baadaye Wayahudi walipotawanywa kama mateka katika nchi za mbali, bado katika saa hiyo iliyoamriwa walielekeza nyuso zao kuelekea Yerusalemu na kutoa maombi yao kwa MUNGU wa Israeli. Katika desturi hii Wakristo wana mfano kwa ajili ya sala ya asubuhi na jioni. Ingawa MUNGU hushutumu mzunguko tu wa mapokeo ya sherehe au kaida kavukavu, bila roho ya ibada, Yeye huwatazama kwa kupendezwa/furaha sana wale wanaompenda, wakisujudu asubuhi na jioni ili kuomba msamaha wa dhambi zilizotendwa na kuwasilisha maombi yao kwa baraka zinazohitajiwa.—(Patriarchs and Prophets, 353, 354) [Pr 163.1; Maombi Aya ya 28]

Maombi ya Kila Siku Hustawisha na kuboresha Uzoefu Wetu wa Kidini/kiroho—Dini lazima ianze kwa kusafisha na kutakasa moyo, na lazima ipewe lishe kwa maombi ya kila siku.— (Testimonies for the Church 4:535) [Pr 163.2; Maombi Aya ya 29]

Maisha ya Maombi ya Kila Siku Yanahitaji Jitihada dhati — Maisha ya sala na sifa kila siku, maisha ambayo yataangazia njia ya wengine, hayawezi kudumishwa bila juhudi za dhati. Lakini bidii kama hiyo itazaa matunda ya thamani, yatakayobariki sio tu mpokeaji, bali mtoaji pia. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine inatoa kina, uthabiti, na uzuri wa tabia kama wa Kristo kwa mhusika na huleta amani na furaha kwa yule aliye nayo. Matarajio yanakuwa yameinuliwa. Hakuna nafasi ya ugoigoi au ubinafsi. Wale walioonyesha neema za Kikristo watakuwa na mishipa na misuli ya kiroho, na watakuwa na nguvu ya kufanya kazi kwa MUNGU. Watakuwa na mitazamo wazi ya kiroho, imani thabiti inayoongezeka, na

nguvu za kudumu na zinazoshinda katika maombi. Wale ambao wanakesha kwaajili ya kuzilinda roho, ambao hujitolea kikamilifu kwa wokovu wa wakosaji, hakika wanafanya kazi ya wokovu wao wenyewe pia. – (Testimonies for the Church 5:607) Pr 163.3; Maombi Aya ya 30]

Malaika Hurekodi Sala ya Asubuhi–Nyinyi nyote mna ushawishi kwa wema au uovu katika akili na tabia za wengine. Na ushawishi unaoutoa au kushinikiza umeandikwa katika kitabu cha kumbukumbu mbinguni. Malaika anakutembelea na anachukua rekodi ya maneno na matendo yako. Unapoamka asubuhi, Je! Unahisi kutojiwezea kwako na hitaji lako la nguvu kutoka kwa MUNGU? na Je, kwa unyenyekevu, na kwa moyo wako wote unamjulisha Baba yako wa mbinguni matakwa yako? Ikiwa ndivyo, malaika hunakili maombi yako, na ikiwa maombi haya hayajatoka nje ya midomo ya uwongo au hila, basi wakati uko katika hatari ya kufanya makosa bila kujua na kutoa ushawishi ambao utasababisha wengine kutenda uovu, malaika wako mlezi atakuwa kando yako, kukufundisha kile kilicho bora, kukuchagulia maneno ili uyatumie, na kuathiri matendo yako. [Pr 164.1; Maombi Aya ya 31]

Ikiwa huhisi kwamba uko katika hatari yoyote, na ikiwa hautoi sala yoyote ya kuomba msaada wa nguvu za kupinga majaribu, utakuwa na uhakika wa kupotoka; Kupuuzia kwako wajibu kutarekodiwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, nawe utaonekana kuwa umepungua katika siku ile ya hukumu.–(Testimonies for the Church 3:363, 364) [Pr 164.2; Maombi Aya ya 32]

Mazoea ya Maombi ya Kila Siku hayapaswi Kufuatwa Kiholela (bila mpangilio au kanuni) - Ibada ya Familia haipaswi kuongozwa na matukio au hali ya hewa. Haupaswi kuomba hapa na pale, au kwa nadra, kulingana na matukio fulani, au kwa kushtukiza na kisha unapojikuta, una kazi kubwa ya kufanya siku hiyo, unaacha kuomba kabisa. Kwa kufanya hivi unawaongoza watoto wako kuona kama maombi hayana matokeo yoyote maalum. Maombi yana maana kubwa sana kwa watoto wa MUNGU, na utoaji wa shukrani unapaswa kuja mbele za MUNGU asubuhi na jioni. Mwandishi wa kitabu cha Zaburi anasema "Njoni,

tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Hebu na tuje mbele Zake kwa shukrani, na tumfanyie shangwe kwa Zaburi. [Pr 164.3; Maombi Aya ya 33]

Akina baba na akina mama, haijalishi kama unabanwa na shuguli zako kwa kiasi gani, usishindwe kukusanya familia yako karibu na madhabahu ya MUNGU. Omba ulinzi wa malaika watakatifu nyumbani mwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanakabiliwa na vishawishi. [Pr 165.1; Maombi Aya ya 34]

Katika jitihada zetu za kuwafariji na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mjichoshe na kuwa hoi kabisa kiasi cha kutofurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Katika Saa ya mapema ya jioni, tunapoweza kusali bila haraka na kwa uwazi wa kuelewa mambo ubongoni mwetu vyema, tunapaswa kutoa dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha na sifa ya shukrani. [Pr 165.2; Maombi Aya ya 35]

Hebu wale wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huongeza ushawishi ulio bora, safi, na wenye kuyaelekeza mawazo juu mbinguni kwa wale wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho pia .— (Child Guidance, 520, 521) [Pr 165.3; Maombi Aya ya 36]

Maombi ya Kila Siku hupaa juu kwa MUNGU kama Uvumba Mtamu—Maisha ya Abrahamu, rafiki ya MUNGU, yalikuwa maisha ya maombi. Kila mahali alipopiga hema lake, karibu nalo ilijengwa madhabahu, ambayo juu yake ilitolewa sadaka ya asubuhi na ya jioni. Wakati hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Na Mkanaani aliyekuwa anarandaranda huko, alipofika kwenye madhabahu hiyo, alijua ni nani aliyekuwepo hapo. Naye huyu Mkaanani alipopiga hema lake, alitengeneza madhabahu na kumwabudu MUNGU aliye hai. [Pr 165.4; Maombi Aya ya 37]

Kwa hivyo nyumba za Wakristo zinapaswa kuwa taa/nuru ulimwenguni. Kutoka kwazo, asubuhi na jioni,

sala inapaswa kupaa kwa MUNGU kama uvumba mtamu. Na kama umande wa asubuhi, rehema Zake na baraka zitashuka juu ya waombaji. [Pr 165.5; Maombi Aya ya 38]

Enyi akina baba na akina mama, kila asubuhi na jioni wakusanyeni watoto wenu karibu nanyi, na kwa dua ya unyenyekevu inueni moyo kwa MUNGU kwa ajili ya msaada. Wapendwa wenu wanakabiliwa na majaribu. Kero na masumbufu ya kila siku hushambulia, hutishia na kuleta matatizo katika njia za vijana na wazee. Wale ambao wanahitaji kuishi maisha ya uvumilivu, ya upendo, na uchangamfu lazima waombe. Ni kwa kupokea msaada wa kila wakati kutoka kwa MUNGU, ndiyo tunaweza kupata ushindi juu ya nafsi yetu (kushinda ubinafsi). [Pr 166.1; Maombi Aya ya 39]

Kila asubuhi jiweke wakfu kwa MUNGU na watoto wako kwa siku hiyo. Usifanye hesabu kwa miezi au miaka; hiyo sio yako. Umepewa siku moja fupi. Kana kwamba ndiyo mwisho wa maisha yako duniani, fanya kazi kwa Mwalimu wakati wa saa zake. Weka mipango yako yote mbele za MUNGU, itekelezwe au iharishwe, kama vile uelekezaji/uongozi Wake Bwana utakavyoonyesha. Kubaliana na mipango Yake badala ya mipango yako mwenyewe, ingawa kuafikiana na jambo hili, kunatulazimisha kuacha miradi iliyo vipenzi kwetu. Hivyo maisha yatafinyangwa zaidi na zaidi na kushabihiana na mfano wa Bwana/Kiungu; "Na amani ya MUNGU, ipitayo akili zote, itahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." Wafilipi 4:7 .—(Testimonies for the Church 7:44) [Pr 166.2; Maombi Aya ya 40]

Mambo ya Kuombea Kila Siku—Tunapaswa kulitazama kila jukumu kuwa takatifu, hata liwe la unyenyekevu wa kiasi gani, kwasababu ni sehemu ya utumishi wa Mungu. Ombi letu la kila siku linapaswa kuwa , “Bwana, nisaidie kufanya vizuri kwa uwezo wangu wote. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo ya Mwokozi.” (The Ministry of Healing, 474) [Pr 166.3; Maombi Aya ya 41]

Jiweke wakfu kwa MUNGU asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, “Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote

miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako.” Hii ni mada/suala la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au isitelekezwe kulingana na atakavyoongoza. Kwa hivyo siku baada ya siku unakuwa unayakabidhi maisha yako mikononi Mwake Mungu, na ndivyo maisha yako yataundwa/yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.—(Steps to Christ, 70) [Pr 166.4; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 15

MFANO WA YESU KATIKA MAOMBI

Fuata Kielelezo cha Yesu kwa Kuanza Siku kwa Sala— Ilikuwa katika saa za sala ya peke Yake ndipo Yesu katika maisha Yake duniani alipata hekima na nguvu. Hebu vijana wafuate mfano Wake katika kutafuta alfajiri na jua lizamapo magharibi, muda wa utulivu kwaajili ya ushirika na Baba yao aliye mbinguni. Na pia wainue mioyo yao kwa MUNGU siku nzima. Katika kila hatua ya njia zetu, Yeye anasema, 'Kwa maana Mimi, Bwana, MUNGU wako, nitakushika mkono wako wa kuume, Usiogope; nitakusaidia.” Isaya 41:13. Laiti watoto wetu wangeweza kujifunza masomo haya katika miaka yao ya awali, wakati jua la maisha yao linaanza kupambazuka, Je, ni upya na nguvu, furaha na utamu wa jinsi gani, ambao ungeletwa maishani mwao!—(Education, 258, 259) [Pr 167.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya dhati na yenye bidii ya Yesu yanatofautiana na maombi yetu dhaifu—Kuhusu Kristo inasemwa: “Na akiwa katika uchungu mkubwa aliomba kwa bidii zaidi.” Je ni tofauti iliyoje tukilinganisha maombezi

haya ya Mkuu wa mbinguni na maombi yetu dhaifu, yanayozimia, yasiyojumuisha moyo, ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya mdomo tu, na ni wachache walio na shauku ya dhati, ya bidii, na yenye mapenzi kwa MUNGU. -(Testimonies for the Church 4:534) [Pr 167.2; Maombi Aya ya 2]

Ikiwa Yesu Alihitaji Kuomba Akiwa Duniani, sisi tunapaswa kusali zaidi kwa kiasi gani basi—Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kumtupia/kuitwika mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho kwetu pia. [Pr 168.1; Maombi Aya ya 3]

Yesu Mwenyewe, alipokuwa akiishi miongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi. Mwokozi wetu alijitambua kuwa na mahitaji na udhaifu wetu, na katika hilo alikuwa muhitaji, mwombaji, akitaka kutoka kwa Baba Yake nguvu mpya, ili aweze kuja kuimarishwa kwa ajili ya jukumu na jaribio. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, “akijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote; lakini kama mtu asiye na dhambi asili yake ilijiepusha na uovu; Alivumilia mapambano na mateso ya nafsi katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima, la muhimu. Alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Na ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa MUNGU, alihisi hitaji la maombi, ni kiasi gani watu dhaifu, wenye dhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa sala ya bidii na ya kudumu.—(Steps to Christ, 93, 94) [Pr 168.2; Maombi Aya ya 4]

Kristo alipambana mieleka kwa maombi ya dhati; Alitoa dua Zake kwa Baba Yake kwa kilio kikali/kizito na machozi kwa ajili ya wale ambao kwa ajili ya wokovu wao aliondoka mbinguni na kuja hapa duniani. Je, sasa ni sahihi kiasi gani basi, ndio, ni muhimu namna gani kwamba watu wanapaswa kuomba na sio kuzimia (kuzirai)!— (The Review and Herald, Aprili 1, 1890) [Pr 168.3; Maombi Aya ya 5]

Yesu Aliomba Nguvu za kustahimili Majaribu—Wachache watafuata mfano wa Mwokozi wetu kwa maombi ya bidii na ya mara kwa mara kwa MUNGU ili kupata nguvu

za kustahimili majaribu, na kuweza kutekeleza majukumu ya kila siku, ya maisha haya. Kristo Ndiye Kapteni wa wokovu wetu, na kwa mateso na dhabihu Yake Mwenyewe, Yeye ametoa mfano kwa wafuasi Wake wote, kwamba kukesha kwa maombi na bidii ya kudumu ni vitu muhimu kwa upande wao ikiwa watawakilisha kwa usahihi upendo uliokaa katika kifua Chake kwa ajili ya jamii ya ubinadamu iliyoanguka.—(The Review and Herald, Februari 23, 1886) [Pr 168.4; Maombi Aya ya 6]

Nguvu ya Yesu Ilitoka katika Maombi—Nguvu ya Kristo ilikuwa katika maombi. Alikuwa ameutwaa ubinadamu, na akachukua udhaifu wetu na akawa dhambi kwa ajili yetu. Kristo alitoka kwenda kwenye vijisitu/vichaka au milimani huku akijitenga na ulimwengu na mambo mengine yote (alijifungia kutoka kwenye mambo hayo yote ili apate nafasi ya kuomba). Alikuwa peke Yake na Baba Yake. Kwa dhati na bidii kubwa, Alimimina maombi yake, na kuelekeza nguvu zote za roho Yake katika kushikilia mkono wa Yeye Asiye na mwisho/kikomo. Majaribu mapya na makuu yalipokuwa mbele Yake, Yeye alijiondoa taratibu bila ya watu kujua na kuelekea mahali patulivu, kisha akawa peke Yake milimani, na kutumia usiku mzima kwa ajili ya maombi kwa Baba Yake wa Mbinguni. [Pr 169.1; Maombi Aya ya 7]

Kwa kuwa Kristo ni kielelezo chetu katika mambo yote, ikiwa tutaiga mfano Wake kwa kutochoka na kuwa na ari katika sala, tukiwasilisha maombi kwa MUNGU ili tuweze kuwa na nguvu katika Jina Lake Yeye Ambaye hakuangukia kwenye majaribu ya hila za adui mjanja Shetani, hata sisi hatutashindwa naye mwovu (tutashinda).— (The Youth's Instructor, April 1, 1873.) Katika maisha yaliyoweka wakfu kikamilifu kwa ajili ya kuwatendea wema wengine, Mwokozi aliona ni umuhimu wa kuchepuka kutoka katika njia alipokuwa safarini na kujiondoa kwenye umati uliomfuata Yeye siku baada ya siku. Ilikuwa ni lazima aachane na maisha ya pilikapilika zisizokoma kwa muda, aache kushugulika na mahitaji ya mwanadamu, na kisha atafute pumziko na pia ushirika usiovunjika na Baba Yake. Kama Mmoja pamoja nasi, mshiriki wa mahitaji na udhaifu wetu, alikuwa akimtegemea MUNGU kabisa, na katika pahali pa siri pa maombi alitafuta nguvu za Bwaba, ili aende akiwa amejipanga na kuimarishwa kwa ajili ya

wajibu na majaribu. Katika ulimwengu wa dhambi Yesu alivumilia mapambano na mateso ya nafsi. Kwa ushirika na MUNGU angeweza kutua mzigo wa huzuni zilizokuwa zikimpondaponda. Hapa Alipata faraja na furaha. [Pr 169.2; Maombi Aya ya 8]

Katika Kristo kilio cha wanadamu kilimfikia Baba wa huruma isiyo na kikomo. Kama mwanadamu alisihi kiti cha enzi cha MUNGU kwa dua, hadi ubinadamu Wake ulichajiwa (ulipewa nguvu) na umeme wa mbinguni ambao ulifanya mwunganiko wa ubinadamu na Uuungu. Kupitia ushirika wa daima alipokea uzima kutoka kwa MUNGU, ili aweze kuupa ulimwengu uzima. Uzoefu Wake unapaswa kuwa wetu pia. [Pr 169.3; Maombi Aya ya 9]

“Jitengeni ninyi wenyewe,” Bwana anaturalika. Ikiwa tutatii Neno Lake, tunapaswa kuwa na nguvu na wenye faida/manufaa zaidi (wenye kunufaisha zaidi). Wanafunzi wakamtafuta Yesu, wakamwambia yote; Naye Akawatia moyo na kuwafundisha. Ikiwa leo tutatenga muda kumwendea Yesu na kumwambia mahitaji yetu, nasi hatutakatishwa tamaa kamwe (au hatutadondoshwa).—(The Desire of Ages, 362, 363) [Pr 169.4; Maombi Aya ya 10]

Mtu wa Huzuni anamimina dua Zake kwa kilio kizito na machozi. Anaomba ili apate nguvu za kuvumilia jaribu hilo kwa niaba ya wanadamu. Ni lazima Yeye Mwenyewe apate kumshikilia vizuri Mweza wa yote, kwa kuwa ni kwa jinsi hiyo tu Anaweza kutafakari yajayo. Naye anamimina matamano ya moyo Wake kwa wanafunzi Wake, ili katika saa ya nguvu za giza, imani yao isianguke, isishindwe au kutindikiwa. Umande mzito ulioganda barafu juu, upo juu ya umbo Lake anaposujudu, lakini Yeye hafikirii kuhusu hili. Vivuli vya usiku vinakusanyika kumzunguka Yeye, lakini Yeye haangalii utusitisi wake (hali ya kizakiza au mawingumawingu).—(The Desire of Ages, 419, 420) [Pr 170.1; Maombi Aya ya 11]

Pale Yesu alipoingia nyikani alifungiwa ndani na utukufu wa Baba. Usikivu Wake wote ukiwa umefyonzwa katika ushirika na MUNGU, aliinuliwa juu ya udhaifu wa kibinadamu. Lakini utukufu uliondoka, na akaachwa apambane na majaribu. Majaribu yalikuwa yakimsonga, na kumbana kila dakika. Asili Yake ya kibinadamu ilisinyaa

(ilitaka kuepuka) kutoka katika pambano lililomngoja. Kwa siku arobaini alifunga na kuomba. Akiwa dhaifu na kukonda kutokana na njaa, akiwa amechoka, na kuchakaa na kudhoofika kwa maumivu ya akili, “uso Wake ulikuwa umeharibika kuliko wanadamu wote, na umbo Lake zaidi ya wanadamu” (Isaya 52:14). Sasa Shetani aliona amepata mwanya. Sasa Ibilisi akafikiri kwamba angeweza kumshinda Kristo.— (Selected Messages 1:227, 228) [Pr 170.2; Maombi Aya ya 12]

Kwa mtenda kazi aliyejiweka wakfu kuna faraja ya ajabu katika kujua kwamba hata Kristo wakati wa maisha Yake duniani alimtafuta Baba Yake kila siku kwa ajili ya ugavi mpya wa neema iliyohitajika; na kutokana na ushirika huu na MUNGU alienda kuwaimarisha na kuwabariki wengine. [Pr 170.3; Maombi Aya ya 13]

Mtazame Mwana wa MUNGU akiinama katika maombi kwa Baba Yake! (Kwa macho ya kiroho). Ingawa Yeye ni Mwana wa MUNGU, bado Yeye aliimarisha imani Yake kwa maombi, na kwa ushirika na Mbingu alijikusanyia nguvu za kupinga uovu na kuhudumia mahitaji ya wanadamu. Akiwa ni Kaka/Ndugu mkubwa wa jamii yetu ya ubinadamu, Yeye anajua mahitaji ya wale ambao wamezingirwa na udhaifu na wanaoishi katika ulimwengu wa dhambi na majaribu, ila bado wana matamania ya kumtumikia. Anajua ya kwamba Mitume ambao ndio wajumbe kwa sasa, wanafaa kutumwa kwenda duniani japo ni watu wadhaifu na wenye kutenda makosa na dhambi. Lakini kwa wote wanaojitoa kikamilifu kwa ajili ya utumishi Wake, Yeye anaahidi msaada wa Kiungu. Mfano Wake Mwenyewe ni uhakikisho kwamba dua ya dhati, yenye kudumu kwa MUNGU katika imani—imani inayoongoza kwenye kumtegemea MUNGU kabisa, na kujiweka wakfu bila kujibakiza kwa ajili ya kazi Yake—itafaa kuwaletea wanadamu msaada wa Roho Mtakatifu katika vita dhidi ya dhambi. [Pr 170.4; Maombi Aya ya 14]

Kila mfanyakazi anayefuata mfano wa Kristo, atakuwa tayari kupokea na kutumia nguvu ambazo MUNGU ameahidi kwa kanisa Lake kwa ajili ya kukomaa kwa mavuno ya dunia. Asubuhi baada ya asubuhi, watangazaji wa injili wanapopiga magoti mbele za Bwana na kufanya upya viapo

vyao vya kujiweka wakfu Kwake, Yeye atawapa uwepo wa Roho Wake, pamoja na nguvu Zake za kuhuisha, na za kutakasa. Wanapoendelea na kazi za siku hiyo, wana uhakika kwamba wakala asiyeonekana wa Roho Mtakatifu huwawezesha kuwa “wafanya kazi pamoja na MUNGU.” 1Wakorintho 3:9.]—(Gospel Workers, 510, 511) [Pr 171.1; Maombi Aya ya 15]

Maombi Yalimtia Nguvu Yesu kwa Ajili ya Kutahiniwa na Majaribu—Kristo Mwokozi wetu alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, lakini hakuwa na dhambi. Yeye Alichukua asili ya mwanadamu, tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, na mahitaji Yake yalikuwa mahitaji ya mwanadamu. Alikuwa ana mahitaji ya kimwili yaliyohitaji kutimizwa, uchovu wa mwili uliopaswa kuondolewa. Ilikuwa ni kwa maombi kwa Baba Yake ndipo alipoandaliwa na kuimarishwa kwa ajili ya wajibu na kwa majaribio. Siku baada ya siku Alifuata mzunguko Wake wa wajibu, akitafuta kuokoa roho.... Naye akakesha usiku kucha akiomba kwa ajili ya wale waliojaribiwa [Pr 171.2; Maombi Aya ya 16]

Majira ya usiku ya maombi ambayo Mwokozi alitumia mlimani au jangwani yalikuwa muhimu kumtayarisha Yeye kwa ajili ya mitihani ambayo ilikuwa lazima akutane nayo katika siku zijazo. Alihisi hitaji la kuburudishwa na kutiwa nguvu rohoni na mwilini, ili aweze kukabiliana na majaribu ya Shetani; na wale wanaojitahidi kuishi maisha Yake watahisi hitaji hilo hilo.— (Maranatha, 85) [Pr 171.3; Maombi Aya ya 17]

Wakati Yerusalemu ikiwa imenyamaza kimya/tuli, na wanafunzi wakiwa wamerudi nyumbani kwao ili kupata burudisho katika usingizi na kuweza kufanywa upya asubuhi, Yesu hakulala. Maombi Yake ya Kiungu/kimbingu yalikuwa yakipanda juu kwa Baba Yake kwa ajili ya wanafunzi Wake, ili waweze kuepukana na ushawishi mbaya ambao wangekutana nao kila siku katika dunia, na ili nafsi Yake Mwenyewe iweze kuimarishwa na kutayarishwa kwa ajili ya kazi na majaribu ya siku inayokuja.—(The Review and Herald, August 17, 1886) [Pr 171.4; Maombi Aya ya 18]

Maombi Yalimpa nguvu mpya Yesu na kumhuisha—Siku Zake zilipita kwenye huduma kwa umati uliomsonga, na

katika kufunua hila za marabi za usaliti, na kazi hii isiyokoma mara nyingi ilimwacha akiwa amechoka hoi (nyang'anyang'a) hata mama Yake, ndugu Zake, na pia wanafunzi Wake, waliogopa kwamba maisha Yake yangetolewa kafara. Lakini aliporudi kutoka katika saa za maombi zilizohitimisha siku Yake yenye taabu, mwonekano wa amani juu ya uso Wake uliweka alama usoni Mwake, hisia ya kuburudishwa, kufanywa upya, ambazo zilionekana kutawala uwepo Wake. Ilikuwa ni kutoka katika saa alizotumia na MUNGU asubuhi baada ya asubuhi, ndiyo Yeye alivyoweza kuleta nuru ya mbinguni kwa wanadamu. –(Thoughts from the Mount of Blessing, 102) [Pr 172.1; Maombi Aya ya 19]

Maombi Yalidumisha Maisha ya Kiroho ya Yesu— Haikuwa msalabani tu ndipo ambapo Kristo alijitoa mhanga Mwenyewe kwa ajili ya wanadamu. Alipokuwa “akizunguka huku na huko akitenda mema” (Matendo 10:38), uzoefu wa maisha Yake ya kila siku ulikuwa mmiminiko/kumiminwa kwa maisha Yake. Ni kwa njia moja tu maisha kama hayo yangeweza kudumishwa. Yesu aliishi kwa kumtegemea na kumtumaini MUNGU na kuwa na ushirika Naye. Mahali hapa pa siri, Pake Yeye Aliye juu, chini ya uvuli Wake Mwenyezi, watu huenda huko, hapa na pale (mara zingine-now and then) na kutulia huko kwa msimu, kwa muda, na matokeo yake yanadhihirika kwa matendo bora na mema miashani mwao, kisha imani yao inashindwa/inatindikiwa, ushirika unakatizwa, na kazi ya maisha kuharibiwa. Lakini maisha ya Yesu yalikuwa ni maisha ya imani endelevu daima, yaliyodumishwa kwa ushirika wa daima; na huduma Yake kwa mbingu na nchi/dunia ilifanyika bila kushindwa au kuyumba (haikufeli wala kutetereka). [Pr 172.2; Maombi Aya ya 20]

Kama mwanadamu alisihi kwa dua kiti cha enzi cha MUNGU hadi ubinadamu Wake ulipoongezewa nguvu (ulichajiwa) na mkondo wa umeme wa mbinguni ambao ulikuwa unauunganisha ubinadamu na Uungu. Na kwa kupokea uzima kutoka kwa MUNGU, Yeye Aliwapa wanadamu uzima/uhai.— (Education, 80, 81) [Pr 172.3; Maombi Aya ya 21]

Maisha ya Maombi ya Yesu Yanafichua Siri ya Nguvu za Kiroho—Maisha ya Mwokozi duniani yalikuwa maisha ya

ushirika na asilia (uumbaji) na MUNGU. Katika ushirika huu alitufunulia siri ya maisha ya nguvu za kiroho.- (Counsels on Health, 162) [Pr 173.1; Maombi Aya ya 22]

Yesu Aliomba Katika Kujitayarisha kwa ajili ya Kazi maalum— Yesu, alipokuwa akijitayarisha kwa ajili ya jaribu kubwa au kazi fulani muhimu, aliondoka na kujitenga katika milima yenye utulivu na kulala usiku kucha katika sala kwa Baba Yake. Usiku wa maombi ulitangulia kuwekwa mikono/wakfu kwa mitume na Mahubiri ya Mlimani, kugeuka sura kwa mng'ao, uchungu wa jumba la hukumu (praetorium au ikulu), msalaba, na utukufu wa ufufuo. [Pr 173.2; Maombi Aya ya 23]

Sisi pia lazima tutenge nyakati kwa ajili ya kutafakari na kusali na kupokea burudisho la kiroho. Sisi hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi jinsi tunavyopaswa.—(The Ministry of Healing, 509) [Pr 173.3; Maombi Aya ya 24]

Ubinadamu wa Yesu Ulifanya Sala Kuwa Lazima— kutokana na hali ya kuwa na ubinadamu, Yeye Alihisi hitaji Lake la nguvu kutoka kwa Baba Yake. Alikuwa na mahali pa pekee pa kuomba. Alipenda kufanya ushirika na Baba Yake kwenye upweke wa milima. Katika zoezi hili nafsi Yake takatifu, ya ubinadamu iliimarishwa kwa ajili ya kazi na majaribu ya siku hiyo. Mwokozi wetu anajitambulisha Mwenyewe na mahitaji na udhaifu wetu, katika hilo alifanyika mwombaji/mwombezi wa usiku, akitafuta kutoka kwa Baba Yake nguvu mpya, ili atoke akiwa ametiwa nguvu na kuburudishwa, akiwa amejiweka imara na thabiti kwa ajili ya wajibu na majaribio. Yeye ni Mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, lakini si katika kuwa na matamano mabaya ya mwili. Akiwa Yule asiye na dhambi, asili Yake ilijiepusha na uovu. Alivumilia mapambano na mateso ya nafsi katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu Wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima na muhimu. Alihitaji msaada/usaidizi wote wa Kiungu Wenye nguvu zaidi na faraja ambayo Baba Yake alikuwa tayari kumpa Yeye, Yeye ambaye kwa faida ya mwanadamu, aliacha furaha ya mbinguni na kuchagua makao Yake katika ulimwengu wenye ubaridi na usio na shukrani. Kristo alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Hapa aliweza kuutua mzigo wa moyo Wake wenye huzuni zilizokuwa

zikimsagasaga/zikimpondaponda. Alikuwa mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko. [Pr 173.4; Maombi Aya ya 25]

Alitumia siku Yake kufanya kazi kwa bidii na unyofu, kuwatendea wengine wema, kuwaokoa watu kutoka kwenye uharibifu. Aliponya wagonjwa, aliwafariji walioomboleza, na kuleta uchangamfu na tumaini kwa waliokata tamaa. Aliwafufua wafu. Baada ya kazi Yake kukamilika kwa siku hiyo, Aliondoka, jioni baada ya jioni, mbali na mkanganyiko wa jiji, na mwili Wake ukainamishwa kwa kusujudu katika dua kwa Baba Yake, katika kichaka kilichokuwa kwenye upweke. Wakati fulani miale angavu ya mwezi ilianguza juu ya mwili/umbo Lake lililokuwa katika ibada akisujudu. Na kisha tena mawingu na giza vilifunga nuru yote. Umande na barafu ya usiku vilikaa juu ya kichwa Chake na ndevu Zake wakati akiwa katika hali ya Mwombaji/Mwombezi. Mara kwa mara aliendelea na maombi Yake usiku kucha. Yeye ni mfano wetu. Ikiwa tungeweza kukumbuka hili, na kumwiga Yeye, tungekuwa na nguvu zaidi katika MUNGU. [Pr 174.1; Maombi Aya ya 26]

Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, pamoja na nguvu Zake za Kiungu, alihisi hitaji la maombi, ni zaidi kiasi gani basi kwa wanadamu wanyonge, wenye dhambi wanaokufa wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi—Sala ya bidii na ya daima! Wakati Kristo alipozingirwa na majaribu makali zaidi, Hakula chochote. Alijikabidhi kwa MUNGU na, kupitia maombi ya dhati na utii mkamilifu kwa mapenzi ya Baba Yake, aliibuka mshindi. Wale wanaoshuhudia ile Kweli katika siku hizi za mwisho, juu ya kila tabaka jingine la wale wanaodai kuwa Wakristo, wanapaswa kumwiga Yule ambaye ni Kielelezo Kikuu katika maombi. [Pr 174.2; Maombi Aya ya 27]

"Inatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake." Meza zetu hutapakaa/huchafuliwa mara kwa mara na anasa (luxury) zisizo za afya wala za lazima, kwa sababu tunapenda vitu hivi kuliko tunavyopenda kujinyima nafsi, kutokuwa na magonjwa, na utimamu wa akili. Yesu alitafuta kwa dhati na bidii nguvu kutoka kwa Baba Yake. Mwana Huyu wa MUNGU Mwenyewe, alionekana kuona hilo ni la thamani zaidi Kwake Mwenyewe, kuliko kuketi kwenye meza ya kifahari zaidi (luxury table). Yeye Ametupa ushahidi

kwamba maombi ni muhimu ili kupokea nguvu za kushindana na nguvu za giza, na kufanya sehemu ya kazi tuliyopewa kutimiza. Nguvu zetu wenyewe ni udhaifu tu, lakini kile ambacho MUNGU hutoa ni chenye nguvu na uhodari mkuu na kitamfanya kila mtu anayepokea kuwa zaidi ya mshindi.—(Testimonies for the Church 2:201-203) [Pr 174.3; Maombi Aya ya 28]

Yesu Alitenga Muda kwa ajili ya Maombi na Haikujalisha kwamba alikuwa na Shughuli Gani au uchovu kiasi gani—Kristo hakutoa huduma yoyote yenye ubahili au isiyo na ukarimu. Hakupima utendaji kazi Wake kwa masaa. Wakati Wake, moyo Wake, nafsi Yake na nguvu, vilitolewa kufanya kazi kwa manufaa ya wanadamu. Katika siku za uchovu alijitaabisha kwa shuguli nzito, na kwa usiku mrefu alsujudu/aliinama katika maombi kwa ajili ya neema na uvumilivu ili aweze kufanya kazi kubwa zaidi. Kwa kilio kikali na machozi, Yeye Alituma maombi Yake mbinguni, ili asili Yake ya ubinadamu ipate kuimarishwa, ili Aweze kuzingirwa na kulindwa, apate kukabiliana na adui mjanja katika kazi zake zote ya udanganyifu, na kuimarishwa kutimiza utume Wake wa kumnyanyua mwanadamu juu. Kwa watenda kazi Wake anasema, “Nimewapa kielelezo, ili nanyi mfanye kama Mimi nilivyofanya.” Yohana 13:15.—(Ministry of Healing, 500) [Pr 174.4; Maombi Aya ya 29]

Yesu Aliomba Mapema Asubuhi—Asubuhi na mapema mara nyingi ilimkuta katika sehemu fulani ya faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au katika sala. Kwa sauti ya uimbaji alikaribisha mwanga wa asubuhi. Kwa nyimbo za shukrani alizishangilia saa Zake na kuleta shangwe ya mbinguni kwa watu waliochoka na kazi zao za kila siku na wale waliovunjika moyo.—(Counsels on Health, 162) [Pr 175.1; Maombi Aya ya 30]

Yesu Alikuwa na Mahali Mahsus pa kufanyia Sala—Wewe uwe na mahali pa sala ya siri. Yesu alikuwa na maeneo teule ya ushirika na MUNGU, na sisi pia tunapaswa kuwa napo/nayo. Tunahitaji mara kwa mara kujitenga hadi mahali fulani, hata kama ni panyenyekevu kwa kiasi gani, mahali ambapo tunaweza kuwa peke yetu tu na MUNGU. — (Thoughts from the Mount of Blessing, 84) [Pr 175.2; Maombi Aya ya 31]

Yesu Aliomba kwa Ajili Yetu—Mara nyingi Yesu alikuwa amechoka kutokana na taabu isiyokoma na kujikana nafsi (kujinyima), kujitoa mhanga, ili kubariki wale wanaoteseka na wahitaji. Alitumia usiku mzima katika maombi juu ya milima pweke, si kwa sababu ya udhaifu Wake na mahitaji Yake, bali kwa sababu Aliona, Alihisi, udhaifu wa asili zetu katika kupinga majaribu ya adui katika vipengele vile vile ambavyo vinatushinda sasa. Alijua kwamba tusingejali kuhusu hatari zetu na tusingehisi hitaji letu la maombi. Ilikuwa ni kwa ajili yetu ndiyo sababu Alimimina maombi Yake kwa Baba Yake kwa vilio vizito na machozi.— (Testimonies for the Church 3:379) [Pr 175.3; Maombi Aya ya 32]

Wanafunzi wa Yesu Walivutiwa na Mazoea Yake ya Kuomba— “Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kuhudumu.” Si kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine, aliishi na kutafakari na kuomba. Kutoka katika saa alizotumia pamoja na MUNGU, alitoka asubuhi baada ya asubuhi kuleta nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za mapema za siku mpya, Bwana alimwamsha kutoka katika usingizi Wake, na nafsi Yake na midomo yake ilipakwa mafuta ya neema, ili aweze kuwagawia wengine. Alipokea Maneno Yake mapya kutoka katika makao mbinguni, Maneno ambayo angeweza kusema kwa majira yake kwa waliochoka na kuonewa. “Bwana MUNGU amenipa,” alisema, “ulimi wa hao waliofundishwa nipate kujua jinsi ya kumwambia Neno kwa wakati yeye aliyechoka: ananiamsha asubuhi kwa asubuhi, anaamsha sikio Langu kusikia kama waliofundishwa” [Pr 176.1; Maombi Aya ya 33]

Wanafunzi wa Kristo walivutiwa sana na maombi Yake na tabia Yake ya ushirika na MUNGU. Siku moja baada ya kutokuwepo kwa Mola wao kwa muda mfupi, walimkuta akiwa amezama katika maombi. Akionekana kutojua uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Mioyo ya wanafunzi iliguswa sana. Alipomaliza kuomba, wakasema, “Bwana, tufundishe kuomba.” The Review and Herald, Agosti 11, 1910) [Pr 176.2; Maombi Aya ya 34]

Sala ya Bwana inaonyesha Uzuri wa mambo kuwa rahisi/sahili— Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake kwamba ni sala ile tu inayotoka katika midomo isiyo na unafiki/feki, ikichochea na mahitaji halisi ya nafsi, ndiyo ya dhati, na

italeta baraka za mbinguni kwa mwombaji. Alitoa sala fupi na ya kina, yaani iliyojumuisha kila jambo kwa wanafunzi Wake. Sala hii, kwa usahili wake mzuri, haina ufanani. Ni sala kamilifu kwa ajili ya maisha ya hadhara na faragha; ni ya hadhi/heshima ya hali ya juu na iliyoinuliwa, ila ni rahisi sana kiasi kwamba mtoto aliye kwenye goti la mama yake anaweza kuelewa. Watoto wa MUNGU wamerudia sala hii kwa karne nyingi, na bado mng'ao wake haujafifia. Kama vito cha thamani kubwa, imeendelea kupendwa na kuthaminiwa. Maombi haya ni uzalishaji wa ajabu. Hakuna watakaomba bure ikiwa ndani ya maombi yao, hizi kanuni zimejumuishwa ndani yake. Maombi yetu ya hadharani yanapaswa kuwa mafupi, na yaeleze tu mahitaji halisi ya roho, tukiomba kwa usahili na imani rahisi ya kuamini kwa ajili ya vile vitu tunavyohitaji. Maombi kutoka kwenye moyo mnyenyekevu, uliopondeka ni pumzi muhimu ya roho yenye kiu ya haki. - (The Signs of the Times, Desemba 3, 1896) [Pr 176.3; Maombi Aya ya 35]

Yesu Alipiga Magoti Alipoomba—Katika ibada ya hadhara na faraghani, ni fursa yetu kupiga magoti mbele ya Bwana tunapotoa maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake imerekodiwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akaomba, akashukuru mbele za MUNGU wake." Messages to Young People, 251) [Pr 177.1; Maombi Aya ya 36]

Fikiria kwa Makini Masomo ya Yesu Kuhusu maombi—masomo ya Kristo kuhusu maombi yanapaswa kuangaliwa na kuzingatiwa kwa umakini. Kuna sayansi ya Kiungu/mbingu katika maombi, na kielelezo chake kinaleta kutazama kanuni ambazo kila mwanadamu anapaswa kuzielewa. Yeye Anaonyesha kile ambacho ni roho ya Kweli ya maombi, Anafundisha hitaji la kudumu katika kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU, na hutuhakikishia utayari Wake wa kusikia na kujibu maombi.—(Christ's Object Lessons, 142) [Pr 177.2; Maombi Aya ya 37]

SURA YA 16

MAOMBI YA FARAGHA

Ombi la Faragha Ni Muhimu—Haiwezekani kabisa kwa Nafsi kusitawi ilhali maombi sio mazoezi maalum ya akili. Maombi ya familia au ya halaiki peke yake hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika faragha nafsi inafunuliwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inachunguzwa na kupembuliwa kwa umakini. Maombi ya siri, yana thamani kubwa iliyoje! Nafsi inazungumza na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa tu na MUNGU anayesikia maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi hayo. Katika maombi ya siri roho haiathiriwi na ushawishi unaozunguka, ipo huru kutokana na hisia au mihemko yenye mikanganyiko. Kwa utulivu, lakini kwa bidii, yamfikia MUNGU. Maombi ya siri mara nyingi hupotoshwa, na miundo yake mizuri hupotea, kwa maombi ya sauti kubwa. Badala ya tumaini shwari, tulivu na imani katika MUNGU, nafsi ikiwa imetolewa katika sauti ya chini, na ya unyenyekevu, sauti inapandishwa na kuwa juu, na msisimko unatiwa moyo (unashawishiwa), na sala ya siri inapoteza ushawishi wake mtakatifu na laini. Kuna dhoruba ya hisia, dhoruba ya maneno, ambayo inapelekea kukosa uwezekano wa kutambua sauti ndogo, na tulivu inayozungumza na nafsi wakati inashiriki katika ibada yake ya siri, ya kweli, ya moyo wote. Ombi la siri, likitolewa ipasavyo, huleta manufaa makubwa, Lakini ombi linalowekwa hadharani kwa familia nzima na majirani sio ombi la siri, ingawa inadhaniwa kuwa hivyo, na nguvu za Bwana hazipokelewi kutoka katika ombi hilo. Ushawishi mzuri na wa kudumu utakuwa unatoka kwa Yeye anayeona kwa siri, ambaye sikio Lake liko wazi kusikia sala inayotokana na moyo. Kwa imani tulivu, iliyo sahili, nafsi hushikilia ushirika na MUNGU na kujikusanyia yenyewe miale ya Mungu ya nuru ili kuitia nguvu na kuitegemeza kustahimili mapambano ya Shetani. Mungu Ndiye nguzo/mnara wetu wa nguvu.—(Testimonies for the Church 2:189, 190) [Pr 178.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu.

Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake. (Testimonies for the Church 7:239) [Pr 179.1; Maombi Aya ya 2]

Wote tunahitaji Kukesha na Kuomba Daima—Mwanzo kabisa wa uovu ulikuwa ni kupuuza kukesha na maombi ya siri, kisha kukaja kupuuza majukumu mengine ya kidini/kiroho, na hivyo barabara ikafunguliwa kwa dhambi zote zilizofuata. Kila Mkristo anaweza kushambuliwa na vivutio vya ulimwengu, usumbufu wa asili ya tamaa za kimwili, na majaribu ya moja kwa moja ya Shetani. Hakuna aliye salama. Haijalishi uzoefu wetu umekuwaje, haijalishi kituo chetu kiko juu kiasi gani, tunahitaji kukesha na kuomba daima. Ni lazima tutawaliwe, na kudhibitiwa kila siku na Roho wa MUNGU la sivyo tutatawaliwa na Shetani.— (Testimonies for the Church 5:102) [Pr 179.2; Maombi Aya ya 3]

Sali Nyakati Zote—Jenga mazoea ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, wakati unapotembea, na unaposhughulika na kazi zako za kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili ya nuru, nguvu, na maarifa. Hebu kila pumzi unayovuta iwe sala.—(Temperance, 135) [Pr 179.3; Maombi Aya ya 4]

Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya kusali, lakini maombi yako ya kimya-kimya yanaweza kupaa kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama ambavyo huwa kwa kila mwanadamu, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono Yake ya milele itakuwa chini yako.— (Counsels on Health, 362) [Pr 179.4; Maombi Aya ya 5]

Maombi ya faragha Yanafaa Pahali Popote, Wakati Wowote—Sali chumbani mwako, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara. [Pr 180.1; Maombi Aya ya 6]

Ilikuwa kwa njia hiyo Henoka alitembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU. [Pr 180.2; Maombi Aya ya 7]

Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na unyofu. Katika umati wa watu waliosongamana mitaani, katikati shuguli za biashara, sisi tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje na kukaa kama mgeni wa mbinguni katika nafsi.—(Steps to Christ, 98, 99). [Pr 180.3; Maombi Aya ya 8]

Maombi hutuleta Katika Uwepo wa MUNGU Mwenyewe – Maombi, iwe yanatolewa katika mkusanyiko wa watu wote, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, humweka mwanadamu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata kanuni zilizo imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.—(My Life Today, 18) [Pr 180.4; Maombi Aya ya 9]

Maombi hutufanya tuunganishwe na Kristo – Tunapaswa kuwa katika maombi ya siri/faragha. Kristo Ndiye mzabibu, sisi ni matawi. Na kama tunataka kukua na kusitawi, lazima tuendeleo kuchota/kuteka utomvu (sap/xylem) na lishe kutoka kwenye Mzabibu Hai; maana kwa kutengwa na Mzabibu hatuna nguvu. [Pr 180.5; Maombi Aya ya 10]

Nilimwuliza malaika kwanini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, “wanaachilia mkono wa Bwana mapema sana. Peleka maombi yako kwenye kiti cha enzi kwa ari/usongo, na ungoje hapo kwa imani thabiti. Ahadi za Mungu ni za Kweli. Early Writings, 73) [Pr 180.6; Maombi Aya ya 11]

Maombi ya faragha Hutegemeza Roho - Kuishi kwa kutegemea Neno la MUNGU inamaanisha kuyasalimisha Kwake maisha yetu yote. Kutakuwa na hisia zinazoendelea za hitaji letu la kumtegemea Yeye daima, moyo utavutwa kumfuata MUNGU. Maombi ni jambo la lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndio unaodumisha maisha ya roho. [Pr 180.7; Maombi Aya ya 12]

Maombi ya Faragha yanahitajika Ili mtu mmoja mmoja, tumjue MUNGU wenyewe—Loo! Je, tunamjua MUNGU jinsi tunavyopaswa? Ni faraja iliyoje, furaha iliyoje, tunapaswa kuwa nayo ikiwa tungejifunza kila siku masomo ambayo Yeye anataka tujifunze! Lazima tumjue Yeye kwa uzoefu na ujuzi wa vitendo. Itakuwa faida kwetu kutumia muda mwingi katika maombi ya siri, katika kumjua binafsi Baba yetu wa mbinguni. - (Medical Ministry, 102) [Pr 181.1; Maombi Aya ya 13]

Watu wa MUNGU Hupuuzia Maombi ya faragha—Nimeona mara kwa mara kwamba watoto wa Bwana hupuuzia maombi, hasa maombi ya siri, kwa ujumla hupuuziwa kupita kiasi; kwamba wengi hawaizoeshi imani hiyo ambayo ni upendeleo/fursa na wajibu wao kuitumia, mara nyingi wakingojea ile hisia ambayo ni imani pekee inayoweza kuleta. Hisia sio imani; mambo haya mawili ni vitu tofauti.—(Early Writings, 72) [Pr 181.2; Maombi Aya ya 14]

Muumba wetu hudai kujitoa kwetu kwa hali ya juu, utii wetu wa kwanza. Chochote ambacho huelekea kutishia upendo wetu kwa MUNGU, au kuingilia kati huduma inayostahili Kwake, kinakuwa sanamu Imungul. Kwa baadhi ya watu ni ardhi zao, nyumba zao, mali zao, bidhaa zao, ndizo sanamu zao. Biashara na miradi vinatendeka kwa ari, jitihada na nguvu, wakati huduma ya MUNGU inafanywa kuwa ya pili kwa kipaumbele. Ibada ya familia imepuuzwa, maombi ya siri yamesahaulika.— (SDA Bible Commentary 2: 1011, 1012) [Pr 181.3; Maombi Aya ya 15]

Kupuuzia Maombi Ni Mchakato Endelevu—Jihadhari na jinsi unavyopuuzia maombi ya siri na kusoma Neno la MUNGU. Hizi ndizo silaha zako dhidi ya yule ambaye anaweka jitihada ili kuzuia maendeleo yako ya kuelekea mbinguni. Upuuziaji maombi na kusoma Biblia kwa mara ya kwanza, hufanya iwe rahisi kufanya hivyo mara ya pili tena. Upinzani wa kwanza dhidi ya kusihhi kwa Roho huandaa njia ya upinzani wa pili. Hivyo moyo unakuwa mgumu, na dhamiri inaunguzwa moto na kuacha chapa (inajeruhiwa).—(Messages to Young People, 96) Pr 181.4; Maombi Aya ya 16]

Sala Za Misimu Fulani Tu Unapopenda Zitakufanya Upoteze Utegemezi Wako Kwa MUNGU—Maombi ni pumzi

ya roho. Ndiyo siri ya nguvu ya kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na bado kukawa na afya ya roho na kisha mambo yakawa salama. Maombi huupatia moyo mguso wa haraka kwenye Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini/kiroho. Puuza zoezi la sala, au jihusishe na maombi kiholela, kwa kushtukiza hapa na pale kama utakavyo, na mara zingine usiombe kutokana na unavyoona inafaa kwako wewe binafsi, nawe utapoteza ushirika/utegemezi wako kwa MUNGU. Vitivo vya kiroho hupoteza nguvu, uzoefu wa kidini/kiroho huondokewa afya, nguvu na ushupavu. - (Messages to Young People, 249, 250) [Pr 182.1; Maombi Aya ya 17]

Maombi ya faragha yanapaswa kuwa ya faragha – Katika maombi ya faragha, wote wana nafasi ya kuomba maadamu wana matamaniao ya kufanya hivyo na kujieleza kinagaubaga kwa Mungu kama watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu na marafiki zao wote. Chumbani mwako, pale mahali pa faragha, ndipo mahali pa kusema shida zako zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu Mungu si mahali pa kufungua mambo yetu binafsi ya moyoni.— (Testimonies for the Church 2:578) [Pr 182.2; Maombi Aya ya 18]

Katika ibada ya faragha maombi yetu hayatakiwi kufikia masikio ya yeyote ila MUNGU asikiaye maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi hayo. [Pr 182.3;

Maombi. Uwe na mahali pa maombi ya siri. Yesu alikuwa na maeneo teule ya ushirika na MUNGU, na sisi pia tunapaswa kuwa nayo. Tunahitaji mara kwa mara kujitenga hadi mahali fulani, ijapokuwa ni panyenyekevu, na penye umasikini ila pawe ni pahali pale ambapo tunaweza kuwa peke yetu na MUNGU. [Pr 182.4; Maombi Aya ya 20]

"Omba kwa Baba yako aliye sirini." Kwa Jina la Yesu tunaweza njoo mbele za MUNGU na ujasiri wa mtoto. Hakuna mwanadamu anayehitajika kufanya kazi kama mpatanishi. Kupitia Yesu tunaweza kufungua mioyo yetu kwa MUNGU kama Yule anayetujua na anayetupenda. [Pr 182.5; Maombi Aya ya 21]

Katika mahali faraghani pa sala, ambapo hakuna jicho lolote linalokuona, isipokuwa lile la MUNGU linaloweza kuona yote, hakuna sikio lisikialo Ila Lake Yeye anayeweza kusikia, tunaweza kumimina matamano yetu yaliyojificha zaidi na shauku zetu kwa Baba wa huruma isiyo na kikomo, na katika utulivu na ukimya wa roho sauti hiyo ambayo kamwe haijawahi kushindwa kujibu kilio cha hitaji la mwanadamu itazungumza na mioyo yetu. [Pr 182.6; Maombi Aya ya 22]

“Bwana ni Mwenye huruma, na ni mwingi wa rehema.” Yakobo 5:11. Yeye Anasubiri kwa upendo usiochoka kusikia maungamo ya wale waliyoiacha njia na kukubali toba yao. Yeye Anatazamia tumrudishie shukrani, kama wakati ule mama anavyolitazamia tabasamu la utambuzi kutoka kwa mtoto wake mpendwa. Yeye Angetutaka tuelewe jinsi moyo Wake mwororo na ulio na matamano kwetu unavyotupenda kwa dhati. Yeye Anatalika tupeleke majaribu na mitihani yetu kwenye huruma Yake, huzuni zetu kwenye upendo Wake, majeraha yetu kwenye uponyaji Wake, udhaifu wetu kwenye nguvu Zake, utupu wetu kwenye utimilifu Wake. Kamwe hakuna hata mtu mmoja aliyekatishwa tamaa aliyemjia Yeye. “Walimtazama, wakaangazwa; na nyuso zao hazikuaibika.” Zaburi 34: 5. [Pr 183.1; Maombi Aya ya 23]

Wale wamtafuta MUNGU faraghani wakimwambia Bwana mahitaji yao na kuomba msaada, hawataomba bure. “Baba yako aonaye sirini, Yeye Mwenyewe atawapa thawabu.” Kadiri Tunavyomfanya Kristo kuwa Mwenzi wetu wa kila siku, tutahisi kuwa nguvu za ulimwengu usioonekana zikituzunguka; na kwa kumtazama Yesu tutafanana na sura Yake. Kwa kumtazama au kufanya ushirika Naye tunabadilishwa. Tabia hulainishwa, husafishwa, hutakaswa na kuboreshwa/kuheshimishwa kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Matokeo ya dhahiri ya tendo letu la ushirika na Bwana wetu yatakuwa ni ongezeko la ucha MUNGU, usafi wa moyo, na bidii. Kutakuwepo na ukuaji wa akili katika sala zetu. Tutapokea elimu ya Bwana/Kimbingu, na hili hudhirishwa katika maisha ya uadilifu na shauku. [Pr 183.2; Maombi Aya ya 24]

Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, sapoti, msaada, na uwezo, kwa maombi ya dhati ya kila

siku, itakuwa na matamano bora, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, magoli ya kina katika utendaji kazi, na njaa na kiu ya haki ya daima. Kwa kudumisha muunganiko na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine, kupitia ushirika wetu na wao, nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni mwetu. Nguvu inayopatikana katika maombi kwa MUNGU, imeunganishwa na bidii ya kudumu katika kufundisha akili kwa makini kwa kujali na kusaidia, nayo huandaa mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na huweka roho katika amani katika mazingira yote - (Thoughts from the Mount of Blessing,84, 85) [Pr 183.3; Maombi Aya ya 25]

Kuna wengine ambao nina hofu, hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, bali wanazirundika kwa ajili ya mkutano wa maombi, na huko wakifika hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na maombi. Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao marefu, yenye ubaridi ulioganda, hutupia wengine baridi ya kutetemesha mwili na giza pia, na kisha shuhuda zao ndefu za kurudi nyuma kwao huwatia watu kivuli tu. Watu wote hushusha pumzi kwa furaha wanapomaliza, na inakaribia kutowezekana kabisa kuondoa ubaridi unaotetemesha na giza ambalo maombi na mashauri yao huleta kwenye mkutano. Kutoka kwa nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii, yaani yenye uchangamfu na kirafiki (social), na sio mirefu sana. Kutoonyesha hisia zetu, au kujibakiza kwa kutokuwa kutozungumza, kutochangamka na kukosa moyo wa kirafiki (reserved), kiburi, ubatili, na hofu ya mwanadamu vinapaswa kuachwa huko-huko nyumbani. Tofauti ndogo na chuki tulizo nazo hatupaswi kwenda nazo kwenye mikutano hii. Kama ilivyo katika familia yenye umoja, unyenyekevu, upole, ujasiri, kujiamini, na upendo vinapaswa kuwepo mioyoni mwa akina kaka na dada ambao wanakutana ili kuhuishwa na kuongezewa nguvu kwa kuleta nuru zao pamoja. - (Testimonies for the Church 2: 578, 579) [Pr 184.1; Maombi Aya ya 26]

Maombi ya Faragha Hutoa Taswira au picha ya Wazi ya nafsi— Hakuna kitakachotoa maoni yaliyo wazi kama hayo kuhusu nafsi yako kama maombi ya siri. Yeye aonaye sirini na anayejua kila kitu, Naye atakuangazia ufahamu wako na

kuyajibu maombi yako. Majukumu ya wazi, na mepesi ambayo hayapaswi kupuuzwa yatafunguliwa mbele yako.— (Testimonies for the Church 5:163) [Pr 184.2; Maombi Aya ya 27]

Maombi ya Faragha Husitawisha Tabia tukufu—Katikati ya hatari za siku hizi za mwisho, usalama pekee wa vijana uko katika kukesha na maombi yanayoongezeka kila mara. Kijana anayepata furaha yake katika kusoma Neno la MUNGU, na katika saa ya maombi, atahuishwa mara kwa mara na rasimu kutoka kwenye chemchemi ya uzima (atafanywa upya mara kwa mara). Atafikia kilele cha ubora wa maadili na upana wa mawazo ambayo wengine hawawezi hata kuuwazia. Ushirika na MUNGU hutia moyo mawazo mazuri, matamanio bora, mitazamo iliyo wazi ya ile Kweli, na makusudio makuu ya utendaji. Wale wanaojiunganisha na MUNGU wanatambuliwa Naye kama wana na binti Zake. Daima wanaendelea kufikia juu na juu zaidi, wakipata mitazamo iliyo wazi zaidi juu ya MUNGU na ya umilele, hadi Bwana anawafanya kuwa mifereji ya nuru na hekima kwa ulimwengu. [Pr 184.3; Maombi Aya ya 28]

Lakini maombi hayaeleweki kama yanavyopaswa kueleweka. Maombi yetu hayapaswi kumpa taarifa ya habari MUNGU juu ya mambo ambayo Yeye hayajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU husoma wazo lililofichwa. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona sirini atasikia, na atatujazia thawabu waziwazi. [Pr 185.1; Maombi Aya ya 29]

Maombi ambayo hutolewa kwa MUNGU na kumweleza juu ya dhambi na unyonge wetu wote pamoja na sikitiko letu, wakati hatujisikii wanyonge hata kidogo, ni maombi ya unafiki. Ni maombi ya toba ambayo Bwana anayaangalia. “Kwa Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; Ninakaa mahali pa juu na Patakatifu, pamoja na yeye ambaye pia ni mwenye roho iliyopondeka na mnyenyekevu, ili kufufua roho ya wanyenyekevu, na kufufua moyo wa wale waliopondeka.” The Youth’s Instructor, August 18, 1898) [Pr 185.2; Maombi Aya ya 30]

Nguvu ya kiroho huja kupitia maombi ya Faragha—Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga

muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko wataunganishwa na mbingu na watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo mazuri, matamania bora, ufahamu dhahiri kuhusu Ukweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa na matamania ya usafi wa moyo, kuwa na nuru, kuwa na upendo, na kuwa na neema zote zinazozaliwa na mbingu. Maombi yao ya bidii kabisa yatapenya ndani ya **pazia (Waebrania 10:20)**. Kundi la watu hawa litakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na Mwisho/kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni ni kwaajili yao, na watasafishwa, watainuliwa, wataboreshwa na kuadilishwa na uhusiano huu wa karibu sana na MUNGU. Huo ndio upendeleo walio nao Wakristo wa kweli. [Pr 185.3; Maombi Aya ya 31]

Kutafakari kwa nadharia tu bila vitendo halisi hakutoshi; shughuli au utendaji mwingi hautoshi; vyote viwili ni muhimu kwa uundaji wa tabia ya Kikristo. Nguvu inayopatikana katika maombi ya dhati, na ya siri, hututayarisha kustahimili vishawishi vya jamii. Na bado hatupaswi kujitenga na ulimwengu, kwani uzoefu wetu wa Kikristo unapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. Jamii ya wasioamini haitatudhuru ikiwa tutachangamana nao kwa kusudi la kuwaunganisha na Mungu na kuwa na nguvu za kutosha kiroho kuhimili ushawishi wao hasi. - (Testimonies for the Church 5:112, 113) [Pr 185.4; Maombi Aya ya 32]

MUNGU Hukubali Maombi ya Kimyakimya—Bwana atakubali hata ombi la kimya la moyo uliolemewa. - (The SDA Bible Commentary 2: 1014) [Pr 186.1; Maombi Aya ya 33]

Kushuhudia Kunapaswa Kutanguliwa na Maombi—Jitihada binafsi kwa wengine zinapaswa kutanguliwa na maombi mengi ya siri; kwani inahitajika hekima kubwa kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na wanadamu, wasiliana na Kristo, kwenye kiti cha enzi cha neema ya mbinguni pata maandalizi ya kuhudumia watu. - (Christ Object Lessons, 149) [Pr 186.2; Maombi Aya ya 34]

Ni sharti tupokee nuru na baraka, ili tuwe na kitu cha kutoa. Ni fursa ya kila mtendakazi kuzungumza na MUNGU kwanza katika mahali pa siri pa maombi na kisha kuzungumza na watu kama kinywa cha MUNGU. Wanaume

na wanawake wanaowasiliana na MUNGU, walio na Kristo adumuye, huifanya angahewa kuwa takatifu, kwa sababu wanashirikiana na malaika watakatifu. Ushuhuda wa namna hiyo unahitajika kwa wakati huu. –(Testimonies for the Church 6:52) [Pr 186.3; Maombi Aya ya 35]

Kazi na maombi Sharti Vifungamanishwe- Lazima tuishi maisha ya pande mbili, maisha ya kufikiri na kutenda, maisha ya maombi ya kimya na kufanya kazi kwa dhati na bidii....Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, msaada (sapoti), na uwezo kwa maombi ya bidii ya kila siku, itakuwa na matamano bora, uelewa dhahiri wa Ukweli na wajibu, malengo ya hali ya juu katika utendaji wa kazi, na njaa na kiu ya haki ya kudumu.–(Testimonies for the Church 4:459, 460) [Pr 186.4; Maombi Aya ya 36]

Ikiwa tutaruhusu **kwenda kwa kasi au kuharakia kwenda** kwenye majukumu na kutuondoa kwenye kusudi letu la kumtafuta Bwana kila siku, tutatenda makosa makubwa zaidi; na kujipatia hasara, kwa kuwa Bwana hatakuwa pamoja nasi. Tumefunga mlango ili asipate nafasi kufikia roho zetu. Lakini ikiwa tunaomba, hata wakati mikono yetu inatenda kazi, sikio la Mwokozi liko wazi kusikia maombi yetu....MUNGU anakutunza mahali ambapo ni wajibu wako kuwepo hapo. Lakini hakikisha, mara nyingi, kwa kadiri iwezekanavyo kwenda mahali ambapo sala inazoeleka kufanywa (mahali pa maombi).– (Medical Ministry, 216) [Pr 186.5; Maombi Aya ya 37]

Tumia Lugha Rahisi katika Maombi-Lugha yenye misamiati migumu au mingi, yenye madoido mengi, yenye sauti ya juu ya kujifanya (bandia/feki) na yenye maelezo mengi haifai katika maombi, iwe ombi hilo linatolewa kwenye mimbari, kwenye mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana na ombi hilo. [Pr 187.1; Maombi Aya ya 38]

Ni sala inayotoka moyoni kwa imani, ndiyo ambayo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.–(Gospel Workers, 177) [Pr 187.2; Maombi Aya ya 39]

Ni Fursa yetu Kupiga Magoti Tusalipo- tunapokuwa kwenye umma na katika ibada binafsi ni fursa yetu kusujudu kwa kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa

maombi yetu Kwake. Yesu, Mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.— (Prophets and Kings, 48) [Pr 187.3; Maombi Aya ya 40]

Usijihusishe na matumbuizo/maburudisho yanayokufanya Usifae kufanya Maombi ya Faragha au yanayokutataza usifanye maombi yako binafsi—Starehe yoyote ambayo unaweza kujihusisha nayo na bado ukaomba baraka za MUNGU kupitia hiyo kwa imani, haitakuwa yenye hatari. Lakini starehe yoyote ile inayokufanya usiweze kufanya maombi ya siri, au usifanye ibada kwenye madhabahu ya maombi, au kushiriki katika mkutano wa maombi, hiyo hakika siyo salama, bali ni hatari.—(Messages to Young People, 386) [Pr 187.4; Maombi Aya ya 41]

MUNGU Hutuona Katika Mahali Petu pa Maombi ya Faragha— Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza Neno la MUNGU sisi wenyewe, na kuomba kwa ajili ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mtini atatuona mahali pa siri pa maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta mwongozo wa Bwana/mbingu.— (The Desire of Ages, 141) [Pr 187.5; Maombi Aya ya 42]

Maombi Yetu Hayawezi Kupotea—Ni jambo la ajabu kiasi gani kwamba sisi tunaweza kuomba kwa ufasaha na ufanisi; kwamba, sisi wanadamu tusiostahili, tunaokufa, na wakosefu, tunao uwezo wa kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kuitamani kuliko hii basi,- kuwa na ushirika na MUNGU asiye na kikomo? Mtu dhaifu, duni na mwenye dhambi ana nafasi na upendeleo wa kuzungumza na Muumba wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanakifikia kiti cha enzi cha Mfalme wa himaya ya malimwengu yote (sayari zote-Universe). Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume. [Tazama Zaburi 16: 8.] [Pr 187.6; Maombi Aya ya 43]

Twaweza kuzungumza/kuwasiliana na MUNGU mioyoni mwetu; tunaweza kutembea katika ushirika na Kristo. Tunapofanya kazi yetu ya kila siku, tunaweza kupumua matamano ya mioyo yetu, yasiyoweza kusikiwa na sikio la mwanadamu; lakini neno au ombi hilo haliwezi kufa kimya, wala haliwezi kupotea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Matamano ya moyo huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya kelele za mashine au viwandani. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na maombi yetu husikilizwa. [Pr 188.1; Maombi Aya ya 44]

Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, na ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile-vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini daima kwa faida yako- (kukunufaisha wewe). - (Gospel Workers, 258) [Pr 188.2; Maombi Aya ya 45]

We pour out our heart's desire in our closets, we breathe a prayer as we walk by the way, and our words reach the throne of the Monarch of the universe. They may be inaudible to any human ear, but they cannot die away into silence, nor can they be lost through the activities of business that are going on. Nothing can drown the soul's desire. It rises above the din of the street, above the confusion of the multitude, to the heavenly courts. It is God to

Hebu wote wanaoteswa au kutumiwa isivyo haki, wamlilie MUNGU. Jiepushe na wale ambao mioyo yao ni migumu kama chuma, na umjulishe Muumba wako maombi yako. Kila aliyemwendea Yeye kwa moyo uliopondeka, hakuna kati yao aliyewahi kupigwa teke, au aliyefukuzwa au kuchukiwa Naye. Hakuna ombi hata moja la dhati linalopotea. Katikati ya nyimbo zinazoinua moyo za kwaya

ya mbinguni, MUNGU husikia kilio cha mwanadamu dhaifu zaidi. Tunamwaga matamano ya moyo wetu katika vyumba vyetu, tunapumua maombi tunapotembea njiani, na maneno yetu yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Yanaweza yasikike kwenye sikio lolote la mwanadamu, lakini hayawezi kufa kimya, wala hayawezi kupotea kupitia mchakato wa shuguli zinazoendelea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Matamano huiuka juu ya makelele ya sauti za juu, yanayoendelea huko mitaani, juu ya machafuko ya umati, hadi nyua za mbinguni. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na sala yetu husikilizwa. - (Christ Object Lessons, 174) [Pr 188.3; Maombi Aya ya 46]

SURA YA 17

MAOMBI KATIKA MZUNGUKO WA NYUMBANI

Familia zapaswa kuomba Pamoja Kila Asubuhi na Jioni
–lbada ya Familia haipaswi kuongozwa na mazingira ya

namna fulani (mfano shida imeingia). Haupaswi kuomba kulingana na matukio fulani au wakati fulani, na kisha wakati una kazi kubwa ya kufanya siku hiyo, unaacha. Kwa kufanya hivi unawaongoza watoto wako kuona maombi kama hayana matokeo yoyote maalum. Maombi yana maana kubwa sana kwa watoto wa MUNGU, na utoaji wa shukrani unapaswa kuja mbele za MUNGU asubuhi na jioni. Mwandishi wa Zaburi anasema "Njoni, tumwimbie Bwana, tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele Zake kwa shukrani, na tumfanyie shangwe kwa Zaburi." [Pr 189.1; Maombi Aya ya 1]

Akina baba na akina mama, haijalishi shuguli zako ziwe za kushinikiza kwa kiasi gani, usishindwe/usifeli kukusanya familia yako karibu na madhabahu ya MUNGU. Omba ulinzi wa malaika watakatifu nyumbani kwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanakabiliwa na vishawishi. [Pr 189.2; Maombi Aya ya 2]

Katika jitihada zetu za kuwafariji, kuwahudumia na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mchoshwe kabisa kufurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Saa za mapema za jioni, wakati ambapo tunapoweza kuomba bila kuharakisha-harakisha na tukiwa katika ufahamu wetu (akili inafanya kazi vyema), tunapaswa kuwasilisha dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha, tukimsifu Mungu na kumpa shukrani zetu. [Pr 189.3; Maombi Aya ya 3]

Hebu wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na saa ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huwa na uboreshaji, usafishaji, utakasaji, ushawishi unaoiua juu ya wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho .—(Child Guidance, 520, 521) [Pr 190.1; Maombi Aya ya 4]

Bwana ana shauku na maslahi maalum katika familia za watoto Wake hapa chini. Malaika hutoa moshi wa ubani wenye harufu nzuri kwa watakatifu wanaoomba. Basi katika kila familia, hebu maombi yapande juu mbinguni asubuhi na wakati joto siyo kali, lituapo jua, kwa niaba

yetu tukiwasilisha mbele za MUNGU sifa na haki ya Mwokozi. Asubuhi na jioni ulimwengu wa mbinguni huandika katika kitabu cha kumbukumbu kila kaya inayoomba. - (My Life Today, 29) [Pr 190.2; Maombi Aya ya 5]

Asubuhi na jioni ulimwengu wa mbinguni unaitazama kila kaya inayoomba, na malaika aliye na ubani, akiwakilisha damu ya upatanisho, hutafuta njia ya kumfikia MUNGU. - (SDA Bible Commentary, vol. 7, 971) [Pr 190.3; Maombi Aya ya 6]

Asubuhi mawazo ya kwanza ya Mkristo yanapaswa kuwa juu ya MUNGU. Kazi ya kidunia na masilahi ya kibinafsi vinapaswa kuwa sehemu ya pili. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kuwa na kicho kwa saa ya maombi. Ni wajibu wa wazazi Wakristo, asubuhi na jioni, kwa sala ya dhati na imani yenye kudumu, na ustahimilivu, kuwajengea wigo/ua watoto wao. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto kwa subira— kwa fadhili na bila kuchoka jinsi ya kuishi ili kumpendeza MUNGU.— (Child Guidance, 519) [Pr 190.4; Maombi Aya ya 7]

Katika kila nyumba ya Kikristo Mungu anapaswa kuheshimiwa kwa dhabihu za asubuhi na jioni za maombi na sifa. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kuhusudu saa ya maombi. Ni wajibu wa wazazi Wakristo, asubuhi na kisha jioni, kwa maombi ya dhati na imani yenye kudumu, kuwajengea wigo watoto wao. [Pr 190.5; Maombi Aya ya 8]

Kanisani, na nyumbani watoto wanapaswa kujifunza kuomba na kumtegemea MUNGU. Wafundishe kurudia sheria ya MUNGU. Waisraeli waliagizwa hivi kuhusu amri: “Uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo;” Kumbukumbu la Torati 6:7. Njoo kwa unyenyekevu, na moyo mwororo, na kwa hisia za majaribu na hatari mbele yako na watoto wako; kwa imani uwafunge madhabahuni, na kuwaandaa kwa ajili ya huduma ya Bwana. Wafunze watoto kutoa maneno yao sahili/rahisi ya maombi. Waambie kwamba MUNGU anafurahi wamwite Yeye, Naye anawaalika kuzungumza na Yeye.— (Counsels

to Parents, Teachers, and Students, 110) [Pr 191.1; Maombi Aya ya 9]

Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja; na baba, au mama wakati baba hayupo, wanapaswa kumsihi MUNGU kwa bidii ili awahifadhi kwa siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu, na moyo mwororo, uliosheheni wema, upendo na upole, na kwa hisia moyoni za majaribu na hatari zilizo mbele yako na watoto wako; kwa imani uwafunge madhabahuni, na kuomba kwa bidii na moyo wote kwa ajili ya utunzaji wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamewekwa wakfu kwa MUNGU kwa namna hiyo.—(Child Guidance, 519) [Pr 191.2; Maombi Aya ya 10]

Familia Zinapaswa Kuwa na Nyakati za Maombi Maalum Zilizowekwa Asubuhi na Jioni—Katika kila familia kunapaswa kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Ni jambo la jema na la kufaa kwa kiasi gani kwa wazazi, kukusanya watoto wao pamoja nao kabla ya kifungua kinywa, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na mwongozo, pamoja uangalizi Wake wakati wa mchana! Ni jambo linalofaa na zuri kwa kiasi gani, wakati wa jioni unapofika pia, wazazi na watoto wakusanyike tena mbele Zake Bwana na kumshukuru kwa baraka za siku iliyopita!—(Child Guidance, 520) [Pr 191.3; Maombi Aya ya 11]

Maombi ya Familia ni ya muhimu - Maombi ya faragha, maombi ya familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara/umma kwa ajili ya ibada ya MUNGU— yote ni muhimu. Nasi pia tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika Kazi Yake (Tujiulize, Kazi ya Kristo ni ipi leo? Maombezi kwaajili yetu ni mojawapo, na zingine ziorodheshe pia!).—(Testimonies for the Church 7:239) [Pr 192.1; Maombi Aya ya 12]

Hakuna kitu Cha Kusikitisha Kama Nyumba isiyo na Maombi — Sijui chochote kinachonisababishia huzuni kubwa kama nyumba isiyo na maombi. Sijisikii salama katika nyumba kama hiyo hata kwa usiku mmoja; na isingekuwa kwa tumaini lenye tumaini la kuwasaidia wazazi kutambua hitaji lao na upuuziaji wao unaohuzunisha, wala nisingebakia ndani ya nyumba hiyo.

Watoto wanaonyesha matokeo ya upuuziaji huko, kwa maana hofu ya MUNGU haiko mbele yao.—(Child Guidance,518) [Pr 192.2; Maombi Aya ya 13]

Kila Nyumba iwe Nyumba ya Maombi—Kama kumewahi kuwa na wakati ambapo kila nyumba inapaswa kuwa nyumba ya maombi ni sasa. (Testimonies for the Church 7:42) [Pr 192.3; Maombi Aya ya 14]

Maombi ya Familia Hutuweka Katika Uwepo wa MUNGU wa Moja kwa Moja—Sala, iwe inatolewa katika kusanyiko la hadhara, yaani kwa watu wote, liwe kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, humweka mwanadamu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi yasiyokoma vijana wanaweza kupata kanuni zilizo imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.— (My Life Today, 18) [Pr 192.4; Maombi Aya ya 15]

Maombi ya Familia huleta Nguvu na Baraka — Tunapaswa kuomba kwa MUNGU zaidi kuliko tunavyofanya. Kuna nguvu kubwa na baraka katika kuomba pamoja katika familia zetu, kuomba pamoja na kwa ajili ya watoto wetu. Wakati watoto wangu wamefanya makosa, na nimezungumza nao kwa upole na kisha nikaomba nao, sijawahi kuona kuwa ni lazima baada ya hapo kuwaadhibu. Mioyo yao iliyeyuka kwa upole, na wema mbele ya Roho Mtakatifu aliyekuja kujibu maombi. - (Child Guidance, 525) [Pr 192.5; Maombi Aya ya 16]

Lugha Rahisi Ndiyo Inafaa Zaidi kwa Maombi— Lugha yenye misamiati migumu au mingi, yenye madoido mengi, yenye sauti ya juu ya kujifanya na maigizo tu, na yenye maelezo mengi haifai katika maombi (fake or high-flown); Haijalishi ombi hilo linatolewa kwenye mimbari, katika mzunguko wa familia, au kwa siri. Yule mhusika hasa, anayetoa ombi hilo la hadharani, anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waweze kuelewa yale yanayosemwa na kuungana na ombi hilo. [Pr 192.6; Maombi Aya ya 17]

Ombi la imani linalotoka moyoni ndilo ambalo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.—(Gospel Workers, 177) [Pr 193.1; Maombi Aya ya 18]

Wafundishe Watoto Wako kuheshimu Wakati wa Maombi — Watoto wako wanapaswa kuelimishwa kuwa wenye fadhili, wema wenye kufikiria wengine, wapole,

waungwana, rahisi kusihiwa (kuombwa kufanya kitu), na, zaidi ya yote, kuheshimu mambo ya kidini/kiroho na kuhisi umuhimu wa madai ya MUNGU. Wanapaswa kufundishwa kuheshimu saa ya maombi; wanatakiwa kuamka asubuhi ili waweze kuwa kwenye ibada ya familia. - (Child Guidance, 521) [Pr 193.2; Maombi Aya ya 19]

Maombi kwa Ajili ya Familia Yetu Ni vyema yanapofanywa/yanapoombewa Nyumbani – Hatupaswi kwenda kwenye nyumba ya MUNGU kuombea familia zetu isipokuwa hisia za ndani zitatuongoza, wakati Roho wa MUNGU anashawishi. Kwa ujumla, mahali sahihi pa kuombea familia zetu ni kwenye madhabahu ya familia. Wakati mada za maombi yetu ziko mbali (watu tunaowaombea nk wapo mbali na pale kanisani), mahali pa siri ni mahali pazuri pa kumsihi kwa bidii MUNGU kwa ajili ya mada hizo. Tunapokuwa katika nyumba ya MUNGU, tunapaswa kuomba baraka ya hapo tulipo na tunapaswa kutarajia MUNGU kusikia na kujibu maombi yetu. Mikutano kama hiyo itakuwa hai, yenye uchangamfu, kupendeza na ya kuvutia.–(Testimonies for the Church 1:145, 146) [Pr 193.3; Maombi Aya ya 20]

Bwana Hakubali Ibada ya Familia Ambayo Imekuwa ni mazoea au kaida fulani tu (ni mfano tu, mapokeo au desturi) –Katika nyumba nyingi ibada ya asubuhi na jioni ni desturi au mazoea tu, kwani ni duni (zinaboesha), inachosha kwa semi za kujirudiarudia, ambamo roho ya shukrani au hisia ya uhitaji wao wa Mungu hazidhiriki. Bwana hakubali huduma kama hiyo. Lakini maombi ya moyo mnyenyekevu na roho iliyopondeka Yeye hatayadharau/hatayapuuza. Kufungua mioyo yetu kwa Baba yetu wa mbinguni, kutambua na kukiri utegemezi wetu Kwake kuhusiana na kila kitu, kuelezea mahitaji yetu, ibada ya upendo wenye shukrani– ndiyo ombi la Kweli/dhati.– (Child Guidance, 518) [Pr 193.4; Maombi Aya ya 21]

Wazazi Wanahitaji Kuombea Hekima Ili kuwafunza/kuwalea Watoto Wao Kwa hekima–Kila familia inapaswa kuinua madhabahu yake ya maombi, ikitambua kwamba kumcha Bwana ndiyo chanzo cha hekima. Ikiwa kuna watu duniani wanahitaji nguvu na faraja ambayo dini hutoa, basi ni wale ambao wanawajibika kwa malezi na mafunzo ya watoto. Hawawezi kufanya kazi yao kwa njia

inayokubalika kwa MUNGU huku kielelezo chao cha kila siku kinawafundisha wale wanaotazamia kupata mwongozo kutoka kwao kwamba ‘wanaweza kuishi bila MUNGU’. Ikiwa wanawafundisha watoto wao kuishi kwa ajili ya maisha haya tu, hawatafanya maandalizi yoyote kwa ajili ya umilele. Watakufa kama walivyoishi bila MUNGU, na wazazi wao watawajibika kwa ajili ya kupoteza roho zao. Akina baba, akina mama, mnahitaji kumtafuta MUNGU asubuhi na jioni kwenye madhabahu ya familia, ili mpate kujifunza jinsi ya kuwafundisha watoto wenu kwa hekima, kwa upole, kwa wema na kwa upendo.— (Child Guidance, NW;517) [Pr 194.1; Maombi Aya ya 22]

Mmewaleta watoto katika ulimwengu ambao hawakuwa na sauti au maamuzi kuhusiana na uwepo wao. Mmejifanya wenyewe kuwajibika kwa kiwango kikubwa kuhusu furaha yao ya baadaye, na ustawi wao wa milele. Jukumu liko juu yenu, iwe mnalihisi hili au la, naam, wajibu wa kuwafundisha na kuwalea watoto hawa kwa MUNGU, kuwatunza kwa uangalifu wenye wivu mara tu adui mjanja anapotokezea na kuweka hatua yake ya kwanza, hebu ninyi muwe tayari kuinua kiwango dhidi yake. Jenga ngome ya maombi na imani juu ya watoto wako, na ufanye bidii kukesha humo. Wewe hauko salama hata nukta moja dhidi ya mashambulio ya Shetani. —(Testimonies for the Church 2:397, 398) [Pr 194.2; Maombi Aya ya 23]

Hebu wazazi wamtafute MUNGU kwa ajili ya mwongozo katika kazi zao. Wakiwa wamepiga magoti mbele Yake watapata ufahamu wa kweli wa wajibu wao mkuu na hapo wanaweza kuwakabidhi watoto wao kwa Yule ambaye hakosei kamwe katika ushauri na mafundisho.—(The Adventist Home, 321) [Pr 194.3; Maombi Aya ya 24]

Kwa maombi ya dhati na ya bidii wazazi wanapaswa kuwawekea ulinzi kwa watoto wao-kuwazunguka na ugo. Wanapaswa kuomba kwa imani kamili kwamba MUNGU atakaa pamoja nao, na kwamba malaika watakatifu watawalinda wao na watoto wao dhidi ya nguvu katili za Shetani.— (Testimonies for the Church 7:42, 43) [Pr 194.4; Maombi Aya ya 25]

Kwa subira, kwa upendo, kama mawakili waaminifu wa neema anuwai ya Kristo (neema za aina mbalimbali, tofauti-tofauti), wazazi wanapaswa kufanya kazi yao

waliyoagizwa. Wanatarajiwa kukutwa waaminifu. Kila kitu kifanyike kwa imani. Ni lazima waombe daima bila kuchoka ili MUNGU awapatie neema yake watoto wao. Kamwe hawapaswi kuchoka, kukosa subira, kufadhaika-fadhaika au kuudhika katika kazi zao. Lazima washikamane kwa karibu na watoto wao na MUNGU. Wazazi wakifanya kazi kwa subira na upendo, wakijitahidi kwa dhati na bidii kuwasaidia watoto wao kufikia kiwango cha juu zaidi cha usafi wa moyo, adabu, kujistahi na kiasi, nao watafaulu.— (The Adventist Home, 208) [Pr 195.1; Maombi Aya ya 26]

Bila juhudi za kibinadamu jitihada za Bwana/mbingu ni bure. MUNGU atafanya kazi kwa nguvu wakati wazazi wanamtegemea na kumtumainia Yeye, wakati ule ambapo wazazi watakapoamka kwa ajili ya jukumu lao takatifu lililo juu yao, na kutafuta kuwafunza, kuwazoeza na kuwalea watoto wao ipasavyo. Yeye Atashirikiana na wazazi ambao huwaelimisha watoto wao kwa uangalifu na kwa maombi, wakifanyia kazi wokovu wao na wa watoto wao. Yeye Atafanya kazi ndani yao, kunia na kutenda mapenzi Yake mema.—(The Adventist Home, 206, 207) [Pr 195.2; Maombi Aya ya 27]

Wazazi, Je! Wewe unafanya kazi kwa bidii isiyochoka na uvumilivu kwa niaba ya watoto wako? MUNGU wa mbinguni anaona kujali kwako, uzingatiaji wako wa makini, kazi yako ya dhati na bidii, kukesha katika ulinzi kwako kwa kila wakati. Yeye Anasikia maombi yako. Kwa uvumilivu na upole, wafunze watoto wako kwa ajili ya Bwana. Mbingu yote inapendezwa na kazi yako. Malaika wa nuru wataungana nawe unapojitahidi kuwaongoza watoto wako kwenda mbinguni. MUNGU ataungana nawe, akiwekea taji juhudi zako kwa mafanikio. Kristo anafurahi kuiheshimu familia ya Kikristo; kwa kuwa familia kama hiyo ni nembo/alama ya familia iliyo mbinguni. - (The Review and Herald, Januari 29, 1901) [Pr 195.3; Maombi Aya ya 28]

Umuhimu Mkuu wa Maombi ya Mama—Wale wanaoshika sheria ya MUNGU huwatazama watoto wao kwa hisia zisizoelezeka— za matumaini na hofu, wakijiuliza kama watawajibika kwa upande gani katika pambano kuu lililo mbele yao. Mama mwenye wasiwasi anauliza, "Je, nitachukua msimamo gani? Je! Ninaweza kufanya nini kuwaandaa kutenda vizuri sehemu yao, ili wawe wapokeaji wa utukufu wa milele? Wajibu mkubwa umelala juu yenu,

akina mama. Ingawa huwezi kusimama katika mabaraza ya kitaifa,wewe unaweza kufanya kazi kubwa kwa ajili ya MUNGU na nchi yako. Unaweza kuwaelimisha watoto wako. Unaweza kuwasaidia kukuza tabia ambazo hazitayumbishwa/hazitapindishwa au kushawishiwa kufanya uovu, lakini utashawishi na kushawishi wengine kutenda haki. Kwa maombi yako ya bidii na ya imani unaweza kuusogeza ule Mkono unaoongoza na kuusogeza ulimwengu.—(The Adventist Home, 264) [Pr 195.4; Maombi Aya ya 29]

Ushawishi wa mama anayeomba, na kumcha MUNGU utadumu milele. Mama huyu anaweza kufa, lakini kazi yake itadumu. —(Testimonies for the Church 4:500) [Pr 196.1; Maombi Aya ya 30]

Laiti wakina mama wangetambua umuhimu wa utume wao, wangeshinda kwenye maombi ya siri, wakiwaleta watoto wao kwa Yesu, wakiomba baraka Zake juu yao, na kuomba hekima ya kutekeleza ipasavyo majukumu yao matakatifu. Hebu mama aboreshe kila fursa ya kuunda na kutengeneza tabia, mazoea na haiba/hulka za watoto wake. Hebu na atazame kwa uangalifu ukuaji wa tabia, akizuia na kuikandamiza kabisa mienendo inayojitokeza kwa ukubwa (inatuna-tuna ila haipaswi kuwepo kwenye mwenendo), akiwatia moyo wale walio na upungufu. Hebu afanye maisha yake mwenyewe kuwa mfano safi na mzuri kwa uongozi wake wa thamani. [Pr 196.2; Maombi Aya ya 31]

Mama anapaswa kuanza kazi yake kwa ujasiri na nishati/nguvu, akitegemea mara kwa mara msaada wa Bwana katika juhudi zake zote. Hapaswi kamwe kupumzika kwa kuridhika hadi aone katika watoto wake mwinuko wa tabia ya kwenda juu unaoeleweka, hadi wawe na lengo la juu zaidi maishani kuliko kujitafutia starehe au raha zao wenyewe. [Pr 196.3; Maombi Aya ya 32]

Haiwezekani kabisa kukadiria nguvu ya ushawishi wa mama anayesali. Anamkiri MUNGU katika njia zake zote. Anawachukua watoto wake mbele ya kiti cha neema na kuwakabidhi kwa Yesu, akiomba baraka Zake juu yao. Ushawishi wa maombi hayo ni "chemchemi ya uzima" kwa watoto hao. Maombi haya, yanayotolewa kwa imani, ni msaada na nguvu ya mama Mkristo. Kupuuza wajibu wa

kuomba pamoja na watoto wetu ni kupoteza mojawapo ya baraka kuu zaidi zilizo karibu nasi, mojawapo ya silaha kuu katikati ya mashaka, masumbufu ya maisha, wasiwasi, na mizigo ya kazi yetu ya maisha. [Pr 196.4; Maombi Aya ya 33]

Nguvu ya maombi ya wakina mama haiwezi kukadiriwa kwa juu sana kama ilivyo. Yule anayepiga magoti kando ya mtoto wake wa kiume na wa kike kupitia mabadiliko na misukosuko ya utotoni, kupitia hatari za ujana, hatajua mpaka siku ya hukumu ifikapo, ushawishi wa maombi yake juu ya maisha ya watoto wake. Ikiwa ameunganishwa kwa imani na Mwana wa MUNGU, mkono mwororo wa mama waweza kumzuia mwanawe wa kiume na wa kike dhidi ya nguvu za majaribu, unaweza kumzuia binti yake asiendekeze dhambi. Wakati tamaa za mwili zinapigania ustadi na kutawala, nguvu za upendo, zenye kuzuia, zilizo dhati na zenye bidii za ushawishi wa mama ulioazimiwa, unaweza kuiegemeza roho upande wa haki-kuisawazisha upande wa haki (kuibalansi). - (The Adventist Home, 265, 266) [Pr 197.1; Maombi Aya ya 34]

Maombi ya akina mama Wakristo hayapuuzwi na Baba wa wote, Yeye aliyemtuma Mwanawe duniani ili akomboe watu kwa ajili Yake. Yeye Hatayakataa maombi yako na kukuacha wewe na ukiwa kwenye misukosuko ya makombora au vipigo vya Shetani katika siku ile kuu ya pambano la mwisho. Ni juu yako kufanya kazi kwa usahili na uaminifu, Naye MUNGU ataimarisha kazi ya mikono yako.—(Child Guidance, 526) [Pr 197.2; Maombi Aya ya 35]

Maombi ya Familia Ni Muhimu, Lakini Aina Nyingine za Maombi zinahitajika Vilevile—Maombi ya Familia au ya hadhara pekee hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika upweke nafsi inafunuliwa na kuanikwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inapekuliwa kwa karibu na kikamilifu. Maombi ya siri! Haya ni ya thamani kubwa sana! Nafsi inazungumza/inawasiliana na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na MUNGU tu anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi kama hayo.—Testimonies for the Church 2:189, 190. [Pr 197.3; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 18

MAOMBI NA IBADA

Maombi na Ibada ni Muhimu kwa ajili ya Ukuaji wa Kiroho— Tafuta kila fursa ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa (wana ratiba ya kufanya maombi). Wale ambao kweli wanatafuta ushirika na MUNGU wataonekana katika mkutano wa maombi, watakuwa waaminifu katika kufanya wajibu wao na kwa bidii na shauku kuvuna faida zote wanazoweza kuzipata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wataweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni. - (Steps to Christ, 98) [Pr 198.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, haya yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake.- (Testimonies for the Church 7:239) [Pr 198.2; Maombi Aya ya 2]

Katika mikutano yetu ya ibada au kujitoa wakfu kwa Mungu, sauti zetu zapaswa zidhihirishe kwa maombi na kumsifu Mungu kwa ibada yetu kwa Baba wa mbinguni, ili wote wajue kwamba tunamwabudu Mungu kwa urahisi/usahili na Kweli, na kwa uzuri wa utakatifu Wake Bwana.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 245) [Pr 198.3; Maombi Aya ya 3]

Makundi madogo na yajikusanye jioni, mchana au asubuhi na mapema ili kujifunza Biblia. Hebu wawe na msimu wa maombi, ili waweze kuimarishwa, kuangaziwa, na kutakaswa na Roho Mtakatifu. Kazi hii Kristo anataka kuifanya moyoni mwa kila mtendakazi. Ikiwa ninyi wenyewe mtafungua mlango wa kuipokea, baraka kubwa itakuja kwenu. Malaika wa MUNGU watakuwa katika kusanyiko lenu. Mtakula majani ya mti wa uzima. Ni ushuhuda gani unaoweza kubeba juu ya mguso wa upendo uliofanywa na watendakazi wenzako katika misimu hii ya thamani wakati wa kutafuta baraka ya MUNGU. Hebu kila mmoja aeleze uzoefu wake kwa maneno rahisi. Hii italeti faraja na furaha zaidi katika nafsi kuliko vyombo vyote vya

kupendeza vya ala za muziki vinavyoweza kuletwa makanisani. Kristo atakuja mioyoni mwenu. Ni kwa njia hii pekee ndipo unaweza kudumisha uadilifu wako.— (Testimonies for the Church 7:195) [Pr 198.4; Maombi Aya ya 4]

Jitayarishe kwa maisha ya mbinguni kwa ari na bidii ambayo bado hujawahi kuionyesha maishani mwako mwote. Ielimishe akili yako kupenda Biblia, kupenda mkutano wa maombi, kupenda saa ya kutafakari, na zaidi ya yote, saa ambayo nafsi inawasiliana na MUNGU. Kuwa na mawazo ya kimbingu endapo siku moja utaungana na kwaya ya mbinguni katika majumba ya juu. —(Testimonies for the Church 2:267) [Pr 199.1; Maombi Aya ya 5]

Pale Roho wa MUNGU atakapofanya kazi juu ya moyo, akilisafisha hekalu la nafsi na unajisi/uchafu wake wa mambo ya kidunia na kupenda anasa, wote wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na kwa dhati, ari, jitihada na matamanio ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Mfanyakazi mwaminifu kwa Bwana ataboresha kila upendeleo/fursa ya kujiweka moja kwa moja chini ya miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha MUNGU, na nuru hii itaakisiwa juu ya wengine.—(Testimonies for the Church 4:461) [Pr 199.2; Maombi Aya ya 6]

Uwepo wa MUNGU Hufanya Nyakati za Maombi na Ibada ya Hadhara Kuwa jambo takatifu—Uchaji Mungu wa kweli huchochewa na hisia ya ukuu Wake usio na kikomo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, moyo wa kila mtoto unapaswa kuvutiwa na kupendezwa kwa kina. Saa na mahali pa maombi na huduma za ibada ya hadhara, hizi mtoto anapaswa kufundishwa kuviona kuwa ni vitakatifu kwa sababu MUNGU Yuko pale. Na kadiri kicho kinavyoonyeshwa katika mtazamo na mwenendo, hisia inayochochea (ibada) itaongezeka kwa kina. —(Education, 242, 243) [Pr 199.3; Maombi Aya ya 7]

Maombi ya hadhara Hutuleta Katika Uwepo wa MUNGU Mwenyewe.- Haijalishi ikiwa Maombi yanatolewa katika mkutano wa hadhara, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, daima humweka mtu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata

kanuni zilizo thabiti/imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.— (My Life Today, 18) [Pr 200.1; Maombi Aya ya 8]

Maombi ya Hadhara Hayapaswi Kuwa Marefu na makavu—Kama watoto wa Mfalme wa mbinguni, mnapaswa kujielimisha wenyewe kutoa ushuhuda kwa sauti iliyo wazi, inayotambulika, maneno yakitamkwa vizuri na kueleweka, na kwa namna ambayo mtu yeyote asiweze kuwa na hisia kwamba mnasitasita au hamtaki, kuzungumza juu ya rehema za Bwana. Katika mkutano wa kijamii, sala inapaswa kutolewa ili wote waweze kujengwa, na wale wanaoshiriki katika zoezi hili wanapaswa kufuata mfano tuliopewa katika sala nzuri ya Bwana kwa ulimwengu. Sala ya Yesu ni rahisi/sahili, wazi, ya kina kwani inajumuisha kila kitu, lakini sio ndefu kiasi cha kukosa joto la kiroho (spiritless) kama yalivyo maombi makavukavu ambayo mara nyingi hutolewa hadharani. Maombi haya yasiyo na roho na ari ndani yake, bora yasitamkwe; kwani yanashindwa kubariki au kujenga, na ni mfumo tu bila nguvu muhimu, yaani hufuata kutimiza wajibu, na ratiba. - (Christian Education, 129) [Pr 200.2; Maombi Aya ya 9]

Maombi yanayotolewa hadharani yanapaswa kuwa mafupi na kwenda kwenye vipengele vinavyohusika. MUNGU hatuhitaji tufanye msimu wa ibada kuwa wa kuchosha kwa maombi marefu.....Dakika chache zinatoshwa kwa sala yoyote ya kawaida kwenye halaiki ya watu. - (Evangelism, 146) [Pr 200.3; Maombi Aya ya 10]

Maombi yetu na mikutano ya kijamii vinapaswa kuwa nyakati za msaada maalum na kutia moyo watu. Kila mmoja ana kazi ya kufanya ili mikusanyiko hii iwe ya kupendeza na yenye faida iwezekanavyo. Hii inaweza kufanywa vizuri kwa kuwa na uzoefu mpya kila siku katika mambo ya MUNGU, na kwa kutosita kusema juu ya upendo Wake katika makusanyiko ya watu Wake. Msiporuhusu giza au ukafiri kuingia mioyoni mwenu, havitadhihirika au kuonekana katika mikutano yenu. [Pr 200.4; Maombi Aya ya 11]

Mikutano yetu inapaswa ifanywe kuwa ya kuvutia sana. Inapaswa kuwa na angahewa la manukato ya mbinguni. Wala kusiwe na hotuba ndefu, kavukavu na maombi ya

mazoea, kwa sababu tu ya kujaza/kutimiza muda au kuendana na ratiba. - (Christian Service, 211) [Pr 201.1; Maombi Aya ya 12]

Katika ibada ya familia hebu waachie watoto washiriki sehemu. Acha wote walete Bibilia zao na kila mmoja asome mstari mmoja au miwili. Kisha wimbo au tenzi fulani inayojulikana iimbwe, ikifuatiwa na maombi. Kwa hili, Kristo ametoa mfano. Sala ya Bwana haikukusudiwa kurudiwa-rudiwa tu kama mfumo au desturi fulani, lakini ni kielelezo cha jinsi maombi yetu yanavyopaswa kuwasahili/rahisi, ya dhati, ya bidii, yenye usadikisho, na ya kina. Katika ombi rahisi mwambie Bwana mahitaji yako na onyesha shukrani kwa rehema Zake. Kwa kufanya hivyo, unamwalika Yesu kama mgeni aliyekaribishwa ndani ya nyumba na moyo wako. Katika familia maombi marefu kuhusu vitu vya mbali hayapaswi kuwepo (fafanua vitu vya mbali kwenye familia yako, ambavyo unaweza kupunguza na kufanya maombi kuwa ya kupendeza na kuongeza matamano ya watu kuomba). Vinafanya saa ya maombi kuwa ya kuchosha, wakati inapaswa kuzingatiwa kama fursa na baraka. Fanya msimu huu uwe wa kupendeza na wa kufurahisha. –(Child Guidance, 524) [Pr 201.2; Maombi Aya ya 13]

Mazungumzo ya muda mrefu na maombi marefu hayafai mahali popote, na haswa katika mkutano wa kijamii. Yanawachosha malaika, na vile vile watu wanaoyasikiliza. Maombi yetu yanapaswa kuwa mafupi, na ya moja kwa moja kwenye mada/pointi. Hebu Roho wa MUNGU ikae mioyoni mwa waabudio, Naye atafutilia mbali desturi za urasmi, na kaida zote na mambo duni (yasiyofaa, yasiyo ya kuboresha watu, yanayoboresha nk).—Review and Herald, October 10, 1882) [Pr 201.3; Maombi Aya ya 14]

Dakika moja au mbili ni ndefu za kutosha kwa maombi yoyote ya kawaida. (Testimonies for the Church 2:581) [Pr 201.4; Maombi Aya ya 15]

Maombi marefu hufanya ibada ichoshe – Katika kila familia, kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Inafaa na ni jambo zuri kama nini kwa wazazi kukusanya watoto wao pamoja nao kabla ya chakula cha asubuhi, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na

mwongozo na utunzaji Wake wakati jua limetokezea kwa siku nzima! Inafaa na ni jambo jema kiasi gani, pia, jioni inapofika, kwa wazazi na watoto kukusanyika tena mbele Zake Bwana na kumshukuru Yeye kwa baraka za siku iliyopita! [Pr 201.5; Maombi Aya ya 16]

Baba, au, akiwa hayupo, mama, anapaswa kuongoza ibada, akichagua sehemu ya Maandiko yenye kupendeza na kueleweka kwa urahisi. Huduma inapaswa kuwa fupi. Wakati sura ndefu inasomwa na maombi ya muda mrefu yakatolewa, huduma hufanywa kuwa ya kuchosha (kuboeshwa), na katika kumalizika kwake hisia ya unafuu/afueni husikika (watu wanashusha pumzi). MUNGU huaibishwa na kukosewa heshima wakati saa ya ibada inapofanywa kuwa kavukavu na ya kuwakasirisha (kuwasumbua moyoni) wana familia, inapokuwa kama shuguli nzito sana, ikapungukiwa na shauku, kiasi kwamba hata watoto wanaiogopa kwa kuifikiria kabla hata hawajaitwa kuja kushiriki. [Pr 202.1; Maombi Aya ya 17]

Akina baba na akina mama, fanyeni saa ya ibada/kuabudu iwe ya kupendeza sana. Hakuna sababu kwa nini saa hii isiwe ya kupendeza na kufurahisha zaidi ya siku hiyo. Kutafakari kwa kiasi kunakofanywa katika maandalizi yake kutakuwezesha kuifanya iwe kamilifu, ya kuvutia na ya kunufaisha familia. Mara kwa mara huduma iwe na utofauti (mambo anuwai). Maswali yanaweza kuulizwa kwenye sehemu ya Maandiko yaliyosomwa, na kisha hoja au mjadala na ufafanuzi mfupi, wa dhati ambao ni muafaka kutokana na wakati mliopo, unaweza kutolewa. Wimbo wa sifa unaweza kuimbwa. Ombi linalotolewa linapaswa kuwa fupi na la moja kwa moja (lisipindepinde au kumangamanga huku na kule). Katika maneno rahisi, na yaliyo dhati, basi yule anayeongoza katika maombi amsifu MUNGU kwa wema Wake na amwombe msaada. Kadiri hali inavyoruhusu, hebu watoto wajiunge katika usomaji na sala. [Pr 202.2; Maombi Aya ya 18]

Ulimwengu ujao wa milele peke yake, yaani mbinguni ndipo patakaofunua wema ambao majira hayo ya ibada yamejazwa na huo. —(Testimonies for the Church 7:43, 44) [Pr 202.3; Maombi Aya ya 19]

Maombi yetu hadharani yanapaswa kuwa mafupi, na yaeleze tu matakwa halisi ya roho, tukiomba kwa usahili na

kwa imani rahisi ya kuamini kwa ajili ya vitu tunavyohitaji. Maombi kutoka kwenye moyo mnyenyekevu, uliopondeka ni pumzi muhimu ya roho iliyo na kiu ya haki. - (The Signs of the Times, Desemba 3, 1896) [Pr 202.4; Maombi Aya ya 20]

Kutokana na nuru niliyonayo juu ya suala hili, nimefikia maamuzi kuwa MUNGU katika ibada Yake tunapokusanyika, hahitaji ziwe nyakati ndefu, zisizopendeza (zinazoboeshwa), za kuchosha watu na kisha wabakie wameinama kwa muda mrefu wakisikiliza maombi kadhaa marefu. Wale wenye afya dhaifu hawawezi kuvumilia usumbufu wa namna hii bila kuchoka sana na hata kuishiwa nguvu. Mwili huchoka kwa kuendelea kuinama kwa muda mrefu; na mbaya zaidi ni kwamba, akili huchoshwa na zoezi hilo la maombi endelevu yasiyotoa burudisho la kiroho na mkutano wa namna hiyo ni mbaya kuliko mtu aliyepata hasara (bora wasingeenda maana mkutano wa maombi umekuwa kama hasara sasa-worse than lost). Watu huchoka kiakili na kimwili na wanakuwa hawajapata nguvu zozote za kiroho. [Pr 202.5; Maombi Aya ya 21]

Mikutano ya makongamano na maombi isifanywe kuwa ya kuchosha. Kwa kadri inavyowezekana, hii mikutano yote inapaswa kuzingatia saa iliyowekwa; na ikiwa kuna watu wanaopenda kujichelewesha-chelewesha na kupoteza muda, basi wale ambao huchelewa kwa nusu saa au hata dakika kumi na tano nyuma ya wakati, hawapaswi kusubiriwa. Ikiwa wako hata watu wawili tu, hawa wanaweza kuanza mkutano kwa kudai ahadi (Wawili au watatu watakapokutanika Bwana Yupo katikati yao). [Pr 203.1; Maombi Aya ya 22]

Mkutano unapaswa kufunguliwa kwenye saa iliyopangwa kwa kadri inavyowezekana, iwe wamehudhuria wengi au wachache. Desturi au mapokeo ya urasmi na ubaridi uliokakamaa vinapaswa kuwekwa kando, na wote wanapaswa kuwajibika katika jukumu. Katika matukio ya kawaida kusiwe na maombi yanayondelea zaidi ya dakika kumi. Baada ya kubadilisha mkao (position), yaani kusimama, kukaa, zoezi la uimbaji, kusoma Neno la Mungu au kupiga magoti ili kuwapa watu

afueni kwa kutokaa mkao mmoja kwa muda mrefu au kufanya kitu kimoja kwa muda mrefu, hapa ndiyo mnaweza kurudi tena kusali, ikiwa kama kuna yeyote anayehisi mzigo wa kutoa sala, basi na aendelee kuomba ili watu wasikae katika nafasi na mkao ule ule (position moja huchosha) [Pr 203.2; Maombi Aya ya 23]

Wote wanapaswa kuhisi kuwa ni jukumu la Mkristo kuomba kwa kifupi. Mwambie Bwana kile unachotaka, bila kurandaranda/kumangamanga ulimwenguni kote. Katika maombi ya faragha wote wana nafasi ya kuomba kadiri ya matamaniao yao na kuwa wazi kama watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu zao na marafiki. Chumbani au mahali pa faragha, ndiyo mahali pa kusemea shida zao zote za binafsi, na mitihani/magumu, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo ya kibinafsi ya moyoni. [Pr 203.3; Maombi Aya ya 24]

Lengo la kukusanyika pamoja ni nini? Je! Ni kumjulisha MUNGU, kumfundisha kwa kumwambia yote tunayojua katika maombi? Tunakutana pamoja ili kujengana sisi kwa sisi kwa kubadilishana mawazo na hisia, kukusanya nguvu, na mwanga, na ujasiri kwa kufahamiana sisi kwa sisi kuhusu matumaini na matarajio ya kila mmoja wetu; na kwa sala zetu za dhati, za bidii, na za kutoka moyoni zinazotolewa kwa imani, tunapata burudisho na nguvu kutoka kwenye Chanzo cha nguvu zetu. Mikutano hii inapaswa kuwa misimu ya thamani zaidi na inapaswa kufanywa iwe ya kuvutia kwa wote ambao wana shauku yoyote ya mambo ya kidini. [Pr 203.4; Maombi Aya ya 25]

Kuna wengine, nina hofu kwamba hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, lakini wanayahifadhi na kuyalimbikiza kwa ajili ya mkutano wa maombi, na hapo hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na maombi (prayer and conference killers). Hawatoi nuru; wala hawamjengi mtu. Maombi yao ya baridi na marefu, yaliyoganda barafu na shuhuda zao ndefu, za kurudi nyuma kwao zinawekea watu kivuli. Wote wanafurahi

wanapomaliza, na ni vigumu kuutupilia mbali ubaridi na giza ambalo maombi, hotuba na mawasiliano yao huleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii (kirafiki na mahusiano-social), na sio mirefu sana. Kukosa roho ya urafiki, kutochangamka au kujibakiza kwa namna fulani, kunawaweka watu mbali nawe (reserved), kisha kiburi, ubatili, na hofu kwa mwanadamu vinapaswa kuachwa nyumbani. Tofauti ndogo na chuki haipaswi kwenda nasi kwenye mikutano hii. Kama ilivyo katika familia yenye umoja, usahili, unyenyekevu, upole, ujasiri, na upendo vinapaswa kuwepo mioyoni mwa akina kaka na dada ambao wanakutana ili kuburudishwa na kuongezewa nguvu kwa kuleta mianga yao pamoja. - (Testimonies for the Church 2: 578, 579) [Pr 203.5; Maombi Aya ya 26]

Maombi ya Hadhara yanapaswa kutamkwa kwa upekee na Kwa Uwazi— Hebu wale wanaoomba na wale wanaozungumza wayatamke maneno yao kwa udhahiri, ili kuyatofautisha na kusema kwa uwazi, kwa upekee, bila kuchanganya maneno, na kwa sauti yenye toni nzuri. Ombi, Likitolewa ipasavyo, ni nguvu ya mema. Ni njia mojawapo inayotumiwa na Bwana kuwasilisha kwa watu hazina muhimu za Ukweli. Lakini Ombi haliwi kama linavyopaswa kuwa, kwa sababu ya sauti zenye kasoro za wale wanaolitamka. Shetani hushangilia wakati maombi yanayotolewa kwa MUNGU yanatolewa kwa sauti ya chini, na hivyo maneno kutoeleweka au kutosikika ipasavyo. Hebu watu wa MUNGU wajifunze jinsi ya kuongea na kuomba kwa njia ambayo itawakilisha ipasavyo zile Kweli kuu walizonazo. Hebu shuhuda zilizobebwa na maombi yaliyotolewa viwe wazi na neno kwa neno litofautianishwe. Na kisha MUNGU atatukuzwa. —(Testimonies for the Church 6:382) [Pr 204.1; Maombi Aya ya 27]

Tumia Lugha Rahisi Unapoomba Hadharani—Lugha ya madoido mengi, misamiati mipya mingi, mashairi, sauti ya juu yenye kujieleza sana na ya kutia chumvi haifai katika sala, kujionyesha kama mtu ana akili mahiri (highflown), iwe ombi hilo linatolewa mimbarani, katika mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa kwa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana katika ombi hilo. [Pr 204.2; Maombi Aya ya 28]

Ni ombi la imani linalotoka moyoni ambalo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.—(Gospel Workers, 177) [Pr 204.3; Maombi Aya ya 29]

Maombi yetu yanapaswa kuwa na utaratibu - Nimeona kwamba machafuko hayampendezi Bwana, na kwamba kuwe na utaratibu katika kuomba na pia katika kuimba. Hatupaswi kwenda nyumbani kwa MUNGU kuziombea familia zetu isipokuwa hisia za ndani zitatuongoza wakati Roho wa MUNGU anawasadikisha wale wanaoombewa kule waliko. Kwa ujumla, mahali sahihi pa kuombea familia zetu ni kwenye madhabahu ya familia. Wakati mada za maombi yetu ziko mbali, mahali pa siri ni mahali pazuri pa kumuomba MUNGU kwa ajili ya mada hizo. Tunapokuwa katika nyumba ya MUNGU, tunapaswa kuomba baraka iliyopo na tunapaswa kutarajia MUNGU kusikia na kujibu maombi yetu. Mikutano kama hiyo itakuwa ya uchangamfu, yenye kupendeza na ya kuvutia watu.— (Testimonies for the Church 1:145, 146) [Pr 204.4; Maombi Aya ya 30]

Mungu Anapaswa kukaribiwa kwa kicho Katika Sala— Wengine hufikiri kuwa ni alama ya unyenyekevu kusali kwa MUNGU kwa njia ya mazoea au ya njia ya kawaida (common), kama vile wanavyozungumza na mwanadamu wenzao. Wanalichafua Jina Lake kwa kulichanganya pamoja bila ulazima na bila kicho sala zao kwa maneno, “MUNGU Mwenyezi,” Maneno matakatifu ya kutisha, ambayo hayapaswi kamwe kutoka midomoni mwao isipokuwa kwa sauti iliyotiishwa na kwa hisia ya kicho, inayohisi utukufu na utakatifu wa Mungu.— (Gospel Workers, 176) [Pr 205.1; Maombi Aya ya 31]

Ni Fursa Yetu Kupiga Magoti Tunapoomba Hadharani— Katika ibada ya hadhara na faraghani ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa MUNGU.—(Selected Messages 2:312) [Pr 205.2; Maombi Aya ya 32]

Kulingana na nuru ambayo imeletwa kwangu, ingempendeza MUNGU kwa wahudumu kupiga magoti mara tu wanapoingia kwenye mimbari, na kwa kicho waombe msaada kutoka kwa MUNGU. Je, hilo lingeleta hisia kubwa ya ibada moyoni kwa kiasi gani? Kungekuwa kicho na angahewa yenye utakatifu na mshangao juu ya watu.

Mhudumu wao anazungumza na MUNGU; anajitoa wakfu kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kipo juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Wahudumu wanapaswa kumtazama MUNGU kwanza wanapoenda kwenye kibweta, na hivyo kuwaambia wote: MUNGU Ndiye chanzo cha nguvu zangu. – (Testimonies for the Church 2:612) [Pr 205.3; Maombi Aya ya 33]

Pale mhudumu anaingia, yapaswa kuwe na heshima, na kicho katika mwenendo na mwonekano. Anapaswa kuinama katika sala ya kimya mara tu atakapoingia kwenye mimbari, na kuomba kwa dhati na bidii msaada wa MUNGU. Ni hisia ya kicho cha kiasi gani italetwa na jambo hili! Kutakuwa na taadhima na utukufu kwenye angahewa la watu. Mhudumu wao anazungumza na MUNGU; anajitoa wakfu kwa Mwenyezi Mungu kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinatawala juu ya watu, na malaika wa Mwenyezi MUNGU wanaletwa karibu sana. Kila mmoja katika kusanyiko, pia, anayemcha Mwenyezi MUNGU anapaswa kuungana Naye kwa kuinamisha kichwa chake katika sala ya kimya ili Mwenyezi MUNGU atoe neema Yake kwa kutano hilo kwa uwepo Wake na kuupa nguvu Ukweli Wake unaotangazwa/unaohubiriwa kutoka katika midomo ya wanadamu. Mkutano unapofunguliwa kwa maombi, kila goti linapaswa kupigwa mbele ya Yule Mtakatifu, na kila moyo unapaswa kupaa kwa Mwenyezi MUNGU katika ibada ya kimya. Maombi ya waumini waaminifu yatasikilizwa, na huduma ya Neno itathibitika kuwa yenye ufanisi. Mtazamo usio na uhai wa waumini katika nyumba ya MUNGU ni sababu moja kuu ya ya huduma kukosa matokeo mazuri zaidi. Sauti ya wimbo, unaomiminwa kutoka katika mioyo mingi katika semi zilizo wazi na za kipekee, ni mojawapo ya nyenzo za Mwenyezi MUNGU katika kazi ya kuokoa roho. Huduma zote zinapaswa kuendeshwa kwa kicho na utii, kana kwamba tu mbele ya Yule Mkuu wa makusanyiko. – (Testimonies for the Church 5:492, 493) [Pr 205.4; Maombi Aya ya 34]

Hadharani na katika ibada binafsi ni fursa yetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza,

"Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.—(Prophets and Kings, 48) [Pr 206.1; Maombi Aya ya 35]

Maombi ya halaiki ni muhimu lakini hayajitoshelezi yenyewe- sala ya familia au ya umma tu haitoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika upweke nafsi inafunuliwa wazi mbele ya jicho la Mwenyezi MUNGU lichunguzalo, na kila nia inapekuliwa na kuchunguzwa. Maombi ya siri! Yana thamani kubwa iliyoje! Nafsi inazungumza na Mwenyezi MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa tu na Mwenyezi MUNGU anayesikia maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi kama hayo (hakuna mmbeya anayepaswa kusikia maombi ya wengine ya faragha!).—Testimonies for the Church 2:189, 190. [Pr 206.2; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 19

MTAZAMO KATIKA MAOMBI

Mkao inayofaa kwa ajili ya Maombi ya hadhara— Nimepokea barua zinazoniuliza kuhusiana na mkao mzuri wa kuchukuliwa na mtu anayetoa ombi kwa Mfalme wa malimwengu yote- Sayari zote (universe). Ndugu zetu wamepata wapi wazo kwamba wanapaswa kusimama kwa

miguu yao wakati wa kuomba kwa Mwenyezi Mungu MUNGU? Mtu ambaye amesomea/ameshamesha kwa takribani miaka mitano huko Battle Creek, aliombwa aongoze kutoa ombi kabla Dada White hajazungumza na watu. Lakini nilipomwona amesimama wima kwa miguu yake wakati midomo yake ilikuwa karibu kufunguka katika kutoa maombi kwa Mwenyezi MUNGU, roho yangu ilisumbuliwa sana ndani kumpa karipio la wazi. Basi nikamwita kwa jina, na kumwambia, "Piga magoti." Huu ndio msimamo (mkao) sahihi wa mwili kila wakati [Pr 207.1; Maombi Aya ya 1]

Kupiga magoti wakati wa kuomba kwa MUNGU ndio mtazamo/tabia/zoea tunalofaa kuwa nalo. Tendo hili la ibada lilitakiwa kufanywa kwa wale mateka watatu wa Kiebrania kule Babeli Lakini tendo kama hilo la ibada, lilipaswa kutolewa kwa MUNGU peke yake— Mtawala Mkuu wa ulimwengu, Mtawala wa ulimwengu wote mzima (mbingu na sayari zote); na hawa Waebrania watatu walikataa kutoa heshima hiyo kwa sanamu yoyote ijapokuwa ilifanyizwa kwa dhahabu safi. Kwa kufanya hivyo, wangukuwa, kwa nia na makusudio yote, wamemsujudia yule mfalme wa Babeli. Kwa kukataa kufanya kama mfalme alivyoamuru, walipata adhabu, na wakatupwa ndani ya tanuru inayowaka moto. Lakini Kristo alikuja Mwenyewe (mbashara) na kutembea pamoja nao kwenye moto, nao hawakupata madhara yoyote. [Pr 207.2; Maombi Aya ya 2]

Hadharani na katika ibada binafsi, pote hapa ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa MUNGU [Pr 208.1; Maombi Aya ya 3]

"Ni wapi Ndugu H alipata elimu yake?" Huko Battle Creek. Je, inawezekana kwamba kwa nuru yote ambayo MUNGU amewapa watu Wake juu ya somo la uchaji-Mungu na kicho, kwamba wahudumu, wakuu, na walimu katika shule zetu, kwa kanuni na mifano, wafundishe vijana kusimama wima katika ibada kama walivyofanya Mafarisayo? Je! Tulitazame hili jambo muhimu kwamba linaashiria kujitosheleza kwao wenyewe na kujithamini wenyewe kwamba wao ndiyo bora? Je, tendo au sifa za namna hii zinapaswa kuonekana wazi na kukuzwa zaidi? [Pr 208.2; Maombi Aya ya 4]

Tunatumaini kwamba ndugu zetu hawataonyesha heshima na kicho kidogo wanapomkaribia MUNGU wa pekee wa Kweli na Aliye Hai kuliko wapagani wanavyoitendea na kujidhihirisha kwa miungu yao ya sanamu, la sivyo watu hawa watakuwa waamuzi wetu katika siku ya hukumu ile ya mwisho. Ningezungumza na wote wanaoshika nafasi ya walimu katika shule zetu. Wanaume na wanawake, msimdharau MUNGU kwa kutomheshimu kwenu kwa kujigamba, huku mkijionyesha ufahari na umuhimu wenu. Usisimame katika Ufarisayo wako na kutoa maombi yako kwa MUNGU. Usiamini nguvu zako mwenyewe. Usizitegemee nguvu zako; lakini mara kwa mara pigeni magoti mbele za MUNGU, na mmwabudu Yeye. [Pr 208.3; Maombi Aya ya 5]

Na mnapokusanyika kumwabudu Mwenyezi MUNGU, hakikisheni mnapiga magoti. Hebu tendo hili lishuhudie kwamba nafsi yote, mwili, na roho ziko chini ya Roho wa Kweli. Ni akina nani ambao wamechunguza Neno kwa ukaribu na kuona mifano na mwelekeo katika suala hili? Je! Ni akina nani tunaoweza kuwaamini kama waalimu katika shule zetu Marekani na nchi za nje? Baada ya miaka ya mafunzo, wanafunzi watarudi katika nchi yao wenyewe wakiwa na mawazo ya ukengeufu/potofu kuhusiana na adabu, kicho na staha anayopaswa kupewa Mwenyezi MUNGU, na kisha wasijisikie kuwa hawako chini ya wajibu wa kuheshimu wale watu wenye mvi (wazee), watu wenye uzoefu, watumishi waliochaguliwa na Mwenyezi MUNGU ambao wameunganishwa na kazi ya Mwenyezi MUNGU kwa takribani miaka yote ya maisha yao? Ninashauri wote wanaosoma shule za Marekani au mahali pengine popote duniani, wasiidake roho ya kukosa kicho. Hakikisha wewe mwenyewe unaelewa fika ni aina gani ya elimu unayohitaji, ili uweze kuelimisha wengine wapate kufaa kwa tabia ambayo itahimili mtihani ambao utawajia upesi wale wote wanaoishi duniani. Shirikiana na Wakristo wenye hekima na maadili mema kupita wote. Usiwachague wakufunzi au wanafunzi wenye kujifanya (feki), bali wale wanaoonyesha utauwa wa ndani kabisa, wale walio na roho ya akili mahiri yenye ufahamu katika mambo ya Mwenyezi MUNGU. [Pr 208.4; Maombi Aya ya 6]

Twaishi katika nyakati za hatari. Waadventista wa Sabato wanasemekana ni watu wa MUNGU wanaotunza

amri Zake; lakini wanapoteza roho yao ya ibada (roho ya kujitoa wakfu kwa dhati). Roho hiyo ya kuwa na kicho kwa MUNGU huwafundisha wanadamu jinsi ya kumkaribia Muumba wao—kwa utakatifu na kicho kupitia imani, si ndani yao wenyewe, bali kwa kupitia Mpatanishi. Kwa hivyo mwanadamu huwekwa imara, katika ulinzi makini, chini ya hali yoyote ambayo anakutana nayo. Mwanadamu lazima apige magoti, kama mnufaika wa neema, mwombaji aliye chini ya kiti cha rehema. Na anapoendelea kupokea rehema za kila siku kutoka katika mkono wa MUNGU, daima anapaswa kutunza na kuthamini shukrani moyoni mwake, na kuionyesha au kuidhihirisha kwa maneno ya shukrani na sifa kwa ajili ya neema hizi asizostahili. Malaika wamekuwa wakilinda njia yake katika maisha yake yote, na mitego mingi iliyojificha ambayo yeye ameepushwa dhidi yake hakuwahi kuiona kwa macho yake. Na kwa ajili ya uangalizi huu na ulinzi wa macho ambayo hayasinzii wala hayalali kamwe, mwanadamu anapaswa kutambua katika kila ombi utumishi wa MUNGU kwa ajili yake.—(Selected Messages 2:311-315) [Pr 209.1; Maombi Aya ya 7]

Kupiga Magoti Katika Maombi Hufunza Heshima na Kumcha MUNGU na kustaababia Utukufu Wake— Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba. Hebu walimu katika shule zetu na wahudumu katika makanisa yetu, wajifunze kila siku katika shule ya Kristo. Ndipo wataomba kwa dhati na bidii, na maombi yao yatasikilizwa na kujibiwa. Ndipo Neno litatangazwa kwa nguvu. [Pr 209.2; Maombi Aya ya 8]

Kote hadharani na katika ibada binafsi ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapoyaleta maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake." Imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na kushukuru mbele za MUNGU wake." [Pr 209.3; Maombi Aya ya 9]

Kumcha MUNGU katika kweli kunachochea na hisia ya ukuu Wake usio na kipimo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, kila moyo unapaswa kuvutiwa sana. Saa na mahali pa maombi ni vitakatifu, kwa

sababu MUNGU Yupo hapo; na kadiri heshima na kicho inavyodhihirika katika tabia, mkao, mwonekano wa uso na mwenendo, hisia inayovichochea itazidishwa." Jina Lake ni takatifu na la kuogopwa," mwandishi wa Zaburi anatangaza. Malaika, wanaponena Jina hilo, hufunika nyuso zao. Kwa heshima gani, basi, sisi ambao tumeanguka na ni wenye dhambi, tunapaswa kulichukua kwenye midomo yetu Jina hilo! [Pr 209.4; Maombi Aya ya 10]

Naam Ingekuwa vema kwa wazee na vijana kutafakari Maneno hayo ya Maandiko yanayoonyesha jinsi mahali palipotwiwa alama ya uwepo wa pekee kwa MUNGU panavyopaswa kuzingatiwa. "Vua viatu vyako miguuni mwako," Alimwamuru Musa kwenye kichaka kinachowaka moto, "kwa kuwa mahali hapo uliposimama ni ardhi takatifu." Yakobo, baada ya kuona maono ya malaika, akasema, "Bwana Yuko mahali hapa; nami sikuijua Hapa si mahali pengine bali nyumba ya MUNGU, na hili ndilo lango la mbinguni." Gospel Workers, 178, 179) [Pr 210.1; Maombi Aya ya 11]

Unyenyekevu wa Sulemani wakati alipoanza kubeba mizigo ya serikali, alipokiri mbele za MUNGU, "Mimi ni mtoto mdogo tu" (1 Wafalme 3:7), upendo wake wa ajabu kwa MUNGU, kicho na heshima yake kuu kwa mambo ya Bwana, kutojiamini kwake ndani ya nafsi yake, na kumwinua kwake Muumba wa yote asiye na kikomo—vipengele yote hii ya tabia, zinazostahili kuigwa sana, zilifichuliwa wakati huduma ya ibada zilizounganishwa na ukamilishaji wa ujenzi wa hekalu, wakati wa maombi yake ya kuweka wakfu hekalu alipiga magoti katika mkao/nafasi ya unyenyekevu ya mwombaji. Wafuasi wa Kristo leo wanapaswa kujilinda dhidi ya mwelekeo wa kupoteza roho ya staha, kicho na hofu ya Mwenyezi Mungu. Maandiko huwafundisha wanadamu jinsi wanavyopaswa kumwendea/kumsogelea Muumba wao—kwa unyenyekevu na kicho, kupitia imani katika Mpatanishi wa Kiungu.— — (Prophets and Kings, 47, 48) [Pr 210.2; Maombi Aya ya 12]

"Katikati mwa ua" la hekalu alikuwa ameweka "jukwaa la shaba," au jukwaa, "urefu wa mikono mitano, na upana wa mikono mitano, na urefu wa mikono mitatu." Juu yake Sulemani alisimama na kwa mikono iliyoinuliwa alibariki umati mkubwa mbele yake. "Na mkutano wote wa Israeli

wakasimama." 2 Mambo ya Nyakati 6:13, 3. [Pr 210.3; Maombi Aya ya 13]

"Asifiwe Bwana, Mungu wa Israeli," Sulemani akasema, "ambaye kwa mikono yake ametimiza kile alichosema kwa kinywa chake kwa baba yangu Daudi, akisema, Nimeichagua Yerusalemu, ili Jina Langu liwe hapo." Aya ya 4-6. [Pr 210.4; Maombi Aya ya 14]

Ndipo Sulemani akapiga magoti juu ya jukwaa la shaba, na katika usikivu wa watu wote alitoa ombi la kuweka wakfu hekalu. Akiinua mikono yake mbinguni, huku kutaniko likiwa limeinama kifudifudi (sura zao zikiwa kwenye ardhi), mfalme alisihi: "Bwana, MUNGU wa Israeli, hakuna MUNGU kama Wewe mbinguni, wala duniani; ushikaye maagano, na kuwarehemu watumishi Wako, waendao mbele Zako kwa mioyo yao yote.—(Prophets and Kings, 39, 40) [Pr 211.1; Maombi Aya ya 15]

Mfalme Sulemani alisimama juu ya jukwaa la shaba mbele ya madhabahu na kuwabariki watu. Kisha akapiga magoti na, akiwa ameinua mikono yake juu kuelekea mbinguni, akamimina sala ya dhati na kujitoa wakfu kwa MUNGU huku makutano wakiwa wameinamisha nyuso zao chini kwenye ardhi. Baada ya Sulemani kumaliza sala yake, moto wa miujiza ukatoka mbinguni na kuteketeza dhabihu hiyo.—(The Story of Redemption, 194) [Pr 211.2; Maombi Aya ya 16]

Mmepewa akili ili muweze kuelewa jinsi ya kufanya kazi. Mmepewa macho ili muweze kuwa makini katika kuzitambua fursa mlizopewa na MUNGU. Masikio yenu yasikilize maagizo ya MUNGU. Magoti yenu yanapaswa kupigwa mara tatu kwa siku katika maombi yanayotoka moyoni. Miguu yenu na ikimbie/itembee katika njia ya amri za MUNGU.—(Testimonies for the Church 6:297) [Pr 211.3; Maombi Aya ya 17]

Wahudumu wapige Magoti na kuomba kabla ya Kuhubiri- Kulingana na nuru ambayo nimepewa, ingempendeza MUNGU kwa wahudumu kupiga magoti mara tu wanapoingia kwenye mimbari, na kwa kicho na dhati waombe msaada kutoka kwa MUNGU. Je, hilo lingeleta hisia za ajabu namna gani? Kungekuwa kicho na hofu ya utukufu wa Mungu juu ya watu. Mhudumu wao anawasiliana na MUNGU; anajitoa wakfu kwa MUNGU kabla

hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinahisiwa juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Wahudumu wanapaswa kumtazama MUNGU, mara tu wanapoingia kwenye kibweta, na hivyo kuwaambia wote: MUNGU Ndiye chanzo cha nguvu zangu.— (Testimonies for the Church 2:612) [Pr 211.4; Maombi Aya ya 18]

Wakati mhudumu anaingia, yapaswa kuwe na kicho, taadhima na hadhi/heshima. Mhubiri anapaswa kuinama na kupiga magoti katika sala ya kimya, mara tu atakapoingia kwenye mimbari, na kuomba msaada kwa MUNGU kwa dhati na bidii (siyo kutimiza ratiba). Je, ni hisia ya namna gani italetwa kwa watu kwa kufanya jambo hili! Kutakuwa na kicho na hofu ya Mungu juu ya watu. Mhudumu wao anazungumza na Mwenyezi MUNGU; anajitoe kwa Mwenyezi MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kitahisiwa juu ya watu (kicho kinatua juu ya watu), na malaika wa Mwenyezi MUNGU wanaletwa karibu sana. Kila mmoja katika kusanyiko pia, anayemcha Mwenyezi MUNGU anapaswa kuungana naye kwa kuinamisha kichwa chake katika sala ya kimya ili Mwenyezi MUNGU ajaze neema kutano hilo kwa uwepo Wake na kuupa nguvu Ukweli Wake unaotangazwa kutoka katika midomo ya wanadamu. Mkutano unapofunguliwa kwa maombi, kila goti linapaswa kupigwa mbele ya Yule Aliye Mtakatifu, na kila moyo unapaswa kupanda juu kwa Mwenyezi MUNGU katika ibada ya kimya. Maombi ya waumini waaminifu yatasikilizwa, na huduma ya Neno itathibitika kuwa yenye ufanisi. Mtazamo usio na uhai wa waumini katika nyumba ya Mwenyezi MUNGU ni sababu moja kuu ya kwa nini huduma inakosa matunda mazuri zaidi. Sauti ya wimbo, unaomiminwa kutoka katika mioyo mingi katika usemi ulio wazi, unaoleweka maana mtu atamkapo maneno na wa kipekee, ni mojawapo ya vifaa vya Mwenyezi MUNGU katika kazi ya kuokoa roho. Huduma zote zifanyike kwa kicho na hofu ya Mungu, kama ni katika uwepo dhahiri wa Bwana wa makutano.—(Testimonies for the Church 5:492, 493) [Pr 211.5; Maombi Aya ya 19]

Kupiga Magoti si lazima mara zote Wakati wa kuomba
— Hatuwezi daima kuwa magotini katika sala, lakini njia ya kuelekea kiti cha rehema iko wazi siku zote. Tunapoendelea na kazi inayoshugulisha au kuhenyeshwa sana, tunaweza kuomba msaada; na tumeahidiwa na Yule

ambaye hatatudanganya, "Mtapokea." Mkristo anaweza na atapata muda wa kuomba. Danieli alikuwa Kiongozi wa taifa; majukumu mazito yalikuwa juu yake; lakini alimtafuta MUNGU mara tatu kwa siku, na Bwana akampa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo hata leo wanadamu wanaweza kukimbilia kwenye hema takatifu la Yeye Aliye Juu Zaidi na kuhisi uhakikisho wa ahadi Yake, "Watu Wangu watakaa katika mkao wa amani, na katika maskani zilizo salama, na mahali pa kupumzika penye utulivu." Isaya 32:18. Wote wanaotamani wanaweza kupata mahali pa ushirika na MUNGU, ambapo hakuna sikio linaloweza kusikia ila Lile lililo wazi kwa ajili ya vilio vya wasiojiweza, wenye huzuni na wahitaji—Yule anayeona hata kuanguka kwa shomoro (ndege wadogo wenye rangi nyeupe, nyeusi, kijivu na kahawia ambao rangi hayo haivutii sana-sparrow). Anasema, "Ninyi ni wa thamani kuliko shomoro wengi." Mathayo 10:31.—(Counsels on Health, 423, 424) [Pr 212.1; Maombi Aya ya 20]

Sababu kwa nini wengi wameachwa peke yao katika maeneo ya majaribu ni kwamba hawakumweka Bwana mbele yao daima. Tunaporuhusu ushirika wetu na MUNGU uvunjwe, ulinzi wetu unatoweka kwetu. Siyo madhumuni yako yote mazuri na nia njema ndiyo vitakuwezesha kuhimili uovu. Lazima muwe wanaume na wanawake wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu hapa na pale unapoamua, na ya kuzimia na kushtukiza kama kifafa, bali ya bidii, ya kudumu, na ya daima. Si lazima kila wakati kupiga magoti ili kuomba. Kuza tabia ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, unapotembea, na unapokuwa na shughuli nyingi zinazohusiana na kazi zako ya kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili ya nuru, nguvu, ufahamu na maarifa. Hebu kila pumzi iwe sala.—(The Ministry of Healing, 510, 511) [Pr 213.1; Maombi Aya ya 21]

Katika kazi ya kutunza mioyo ni lazima tuwe na utayari katika sala, bila kuchoka katika kukiomba kiti cha neema kwa ajili ya msaada. Wale ambao huchukua hubeba jina la "Mkristo" wanapaswa kumjia Mwenyezi MUNGU kwa unyofu na unyenyekevu, wakisihi msaada. Mwokozi ametuambia tuombe bila kukoma. Mkristo hawezi kuwa katika mkao wa kuomba kila wakati, lakini mawazo na matamano yake

yanaweza kupanda kuelekea juu kila wakati. Kujiamini nafsi zetu wenyewe kungetoweka, kama tungeongea kidogo tu na kusalizaidi.—(Sons and Daughters of God, 99) [Pr 213.2; Maombi Aya ya 22]

Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Wewe hutaweza kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri Pake Yeye Aliye Juu. Mikono Yake ya milele itakuwa chini yako. Acha maneno haya yakutie nguvu, “Lakini wako wachache huko Sardi ambao hawakuyachafua mavazi yao; nao watakwenda pamoja Nami wakiwa wamevaa mavazi meupe, kwa maana wamestahili.” Ufunuo 3:4.— (Counsels on Health, 362) [Pr 213.3; Maombi Aya ya 23]

Ikiwa watendakazi wetu wote wangekuwa katika hali ambayo wanaweza kutumia saa chache kila siku katika kazi za nje, na kujisikia huru kufanya hivi, ingekuwa baraka kwao; wangeweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu ya wito wao. Kama hawana muda wa kutosha kupumzika na kutuliza mawazo lrelaxl, wangeweza kuweka mikakati na kuomba waendeleo kufanya kazi kwa mikono yao, na hivyo wangeweza kurudi kwenye kazi yao wakiwa wameburudishwa katika mwili na roho—(Gospel Workers, 240) [Pr 213.4; Maombi Aya ya 24]

Ombi la dhati Halitegemei Wakati au Mahali au Hali/Mazingira— Omba chumbani mwako au mahali pa faragha, na unapoendelea na kibarua chako cha kila siku, acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara. [Pr 214.1; Maombi Aya ya 25]

Ilikuwa kwa namna hiyo Henoko alipotembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumtweza/kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU. [Pr 214.2; Maombi Aya ya 26]

Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutuma ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua moyo yetu katika roho ya maombi ya bidii. Katika msongamano wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kusih

mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu na faragha unaweza kupatikana popote tulipo. Mara zote tunapaswa kuacha mlango wa moyo ukiwa wazi na kutuma mwaliko wetu kwenda juu ili Yesu aje akae nasi kama mgeni kutoka mbinguni kwenye nafsi zetu -(Steps to Christ, 98, 99) [Pr 214.3; Maombi Aya ya 27]

Popote tuwapo, bila kujali ajira au shughuli zetu, mioyo yetu inapaswa kuinuliwa kwa Mwenyezi MUNGU katika maombi. Hii ni kuwa na utayari katika maombi wakati wowote. Hatuhitaji kusubiri hadi tuweze kupiga magoti kabla ya kuomba. Wakati fulani, Nehemia alipofika mbele ya mfalme, mfalme aliuliza ni kwanini alionekana kuwa mwenye huzuni, na ni ombi gani alikuwa anataka kutoa kwa mfalme. Lakini Nehemia hakuthubutu kujibu hapo hapo. Masilahi muhimu yalikuwa hatarini. Hatima ya taifa ilining'inia juu ya mtazamo ambao unapaswa kutengenezwa juu ya akili ya mfalme; naye Nehemia akatuma maombi kwa MUNGU wa Mbinguni, kabla hajathubutu kumjibu mfalme. Matokeo yakawa kwamba alipata yote aliyoomba au hata yale aliyoyatamani.—(The Signs of the Times, October 20, 1887) [Pr 214.4; Maombi Aya ya 28]

Madhumuni yako yote mema na dhamira njema havitakuwezesha kustahimili mitihani ya majaribu. Lazima muwe watu wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu yaani kushtukiza hapa na pale bila kanuni, na ya mihemko, bali ya bidii, ya dhati, ya kudumu, na ya mara kwa mara (au daima). Sio lazima uwe peke yako, au upige magoti kuomba; lakini katikati ya shughuli zenu, nafsi zenu zinaweza kuinuliwa mara kwa mara kwa MUNGU, zikishikilia nguvu Zake; ndipo mtakapokuwa watu wa kusudi la juu, bora, takatifu, na waadilifu ambao hawatageuzwa kwa namna yoyote kutoka katika ile Kweli, na njia sahihi, na haki.—(Testimonies for the Church 4:542, 543) [Pr 214.4; Maombi Aya ya 29]

Ni lazima tuombe daima, kwa akili ya unyenyekevu na roho ya upole na unyenyekevu. Hatuhitaji kusubiri nafasi ya kupiga magoti mbele ya MUNGU. Tunaweza kuomba na kuongea na Bwana popote tulipo.— (Selected Messages 3:266) [Pr 214.5; Maombi Aya ya 30]

Maombi ya Hadhara yanapaswa Kuwa mafupi nayo, yaambatane na Sauti ya asili—Baadhi ya Maombi marefu yanayotolewa na wachungaji na wahudumu yamekuwa yasiyo na mafanikio (yamefeli). Kuomba sala refu kama wengine wanavyofanya sio sawa, kwani sio mahali pake. Wanaumiza koo na viungo vya sauti, na kisha wanazungumza juu ya kuvunjika afya kwa kazi yao ngumu. Wanajiumiza wenyewe wakati haipaswi kuwa hivyo. Wengi huhisi kwamba kusali huumiza viungo vyao vya sauti zaidi kuliko kuzungumza. Hili ni tokeo/tunda la kuweka mwili kwa mkao usio wa kawaida, na jinsi ya kichwa kinavyowekwa. Wanaweza kusimama na kuzungumza, na wasijisikie kujeruhiwa. Mkao wa maombi (position) unapaswa kuwa wa asili kabisa. Kuomba kwa muda mrefu kunachosha, na sio kwa mujibu wa injili ya Kristo. Nusu au hata robo ya saa ni ndefu sana. Muda wa dakika chache unatosha kuleta haja zako mbele za Mwenyezi MUNGU na kumwambia kile unachotaka; na unaweza kuwachukua watu pamoja nawe na bado usiwachoshe na kupunguza hamu yao katika ibada na sala. Wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa, badala ya kuchoka. [Pr 215.2; Maombi Aya ya 31]

Kosa limefanywa na wengi katika mazoezi yao ya kidini katika kuomba kwa muda mrefu na kuhubiri kwa muda mrefu, kwa kupayuka au kutumia sauti ya juu sana, noti ya juu (high key), kwa sauti ya kulazimisha, kwa mkazo usio wa asili, mkao usio wa asili na sauti isiyo ya asili.—(Testimonies for the Church 2:617) [Pr 215.3; Maombi Aya ya 32]

Zungumza kwa Uwazi na toa sala kwa Uwazi—Kwa kielelezo chako mwenyewe wafundishe watoto wako kusali kwa sauti iliyo wazi na ukitofautisha maneno unapoyatamka. Wafundishe kuinua vichwa vyao kutoka kwenye kiti na kamwe wasifunike nyuso zao kwa mikono yao. Kwa kufanya hivyo wanaweza kutoa maombi yao sahili, wakirudia sala ya Bwana kwa pamoja.—(Child Guidance, 522, 523) [Pr 215.4; Maombi Aya ya 33]

Izoeze na kuinidhamisha akili kuwa makini Wakati wa kuomba—Maombi ya kila siku ni muhimu katika ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha muda cha hapa duniani, tunachokula kwa ustawi wa kimwili. Tunapaswa kujizoeshwa kuinua mawazo

kwa MUNGU katika sala. Akili ikimangamanga huko na kule, lazima tuirudishe; kwa jitihada za dhati na zenye uvumilivu, mazoea hatimaye yatafanya iwe rahisi.—(The Sanctified Life, 93) [Pr 216.1; Maombi Aya ya 34]

Ombi halihitaji Kuwa refu au kuwa la sauti kubwa— Kusali hakueleweki jinsi inavyopaswa. Maombi yetu hayapaswi kumjulisha MUNGU juu ya kitu ambacho Yeye hajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU anasoma mawazo yaliyofichika. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona katika siri atasikia, na atatupatia thawabu hadharani.—(Messages to Young People, 247) [Pr 216.2; Maombi Aya ya 35]

Hatupaswi Kujaribu Kumwamuru MUNGU Katika Maombi— Maombi yetu hayapaswi kuwa katika namna ya amri, kumwamrisha Mungu, bali yawe ni ya maombezi, Kwake Yeye, ili Ayafanye mambo tunayotamani kupata kutoka Kwake.—(Counsels on Health, 379) [Pr 216.3; Maombi Aya ya 36]

Omba kwa Imani—Omba kwa imani. Hakikisha unayapatanisha maisha yako na maombi yako, ili upate kupokea baraka ambazo unaziombea. Usiache Imani yako idhoofike, kwani baraka zinazopokelewa zinalingana na imani iliyopo, yaani inayozoezwa/inayoonyeshwa. "na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachomba katika sala, mtapata."Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu Yeye amejibu maombi yenu. Muendee Bwana kwa Neno Lake. "Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati linalopotea. Njia iko wazi; na mkondo unabubujika. Umebeba miliki ya uponyaji, ukimimina mawimbi ya kurudisha uzima, afya na wokovu. (Testimonies for the Church 7:274) [Pr 216.4; Maombi Aya ya 37]

Hebu uaminifu na imani viwe sifa ya maombi yako. Bwana Yu tayari kutufanyia sisi "mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo." Waefeso 3:20. Zungumza hilo; liombee hilo. Usiongee kuhusu kutokuamini. Hatuwezi kumuacha Shetani aone kwamba ana uwezo wa kuzitia nyuso zetu giza na kuhuzunisha

maisha yetu.—(Testimonies for the Church 7:273) [Pr 216.5; Maombi Aya ya 38]

SURA YA 20

KUOMBA KATIKA JINA LA YESU

Jina la Yesu Ndio Kiungo/Kiunganishi Katika Maombi Kati ya Ubinadamu wote na MUNGU—Katika Jina la Kristo maombi yetu yanapanda juu kwa Baba. Yeye hutuombea, na kututetea kwa niaba yetu, na Baba anazianika wazi hazina zote za neema Yake kwa ajili ya kutupatanisha/kutumengea sisi, ili sisi tufurahie na kuwagawia wengine. “Ombeni kwa Jina Langu,” Kristo asema. Sisemi kwamba nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda ninyi. Litumieni Jina Langu ili mpate kunufaika. Hii itayafanya maombi yenu yawe na ufanisi, na Baba atawapa utajiri wa neema Yake. Kwa hiyo ombeni, nanyi mtapata, ili furaha yenu iwe timilifu.” [Pr 217.1; Maombi Aya ya 1]

Kristo Ndiye kiungo kinachomwunganisha MUNGU na mwanadamu. Yeye Ameahidi maombezi Yake binafsi. Yeye Anaweka wema/fadhila yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo amamwombea mwanadamu, na mwanadamu, anayehitaji msaada wa Bwana, anasihi kwaajili yake mwenyewe mbele za MUNGU, akitumia nguvu ya ushawishi wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ulimwengu. Tunapokiri mbele za MUNGU ukubali wetu wa sifa na haki ya Kristo, uvumba wa manukato hutolewa kwa ajili ya maombezi yetu. Tunapomkaribia MUNGU kupitia fadhila ya haki na sifa za Mkombozi, Kristo hutuweka karibu na upande Wake, akituzunguka kwa mkono Wake wa kianadamu, wakati kwa mkono Wake wa Kiungu Yeye

anashika kiti cha enzi cha Yule Asiye na kikomo. Yeye huweka sifa na haki Yake, kama uvumba mtamu wa manukato, ndani ya chetezo mikononi mwetu, ili kutia moyo maombi yetu. Yeye Anaahidi kusikia na kujibu maombi yetu. [Pr 217.2; Maombi Aya ya 2]

Ndio, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na MUNGU (kiwambaza cha kati Ebrania 10:20). Pia amekuwa njia ya baraka kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Watu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya bidii, na jitihada za dhati zenye kudumu ili kuokoa wale ambao wako tayari kufa. - (Testimonies for the Church 8:178) [Pr 218.1; Maombi Aya ya 3]

Bado wanafunzi walikuwa hawajui rasilimali na nguvu za Mwokozi zisizo na kikomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Yeye Atakuwepo mbele za Baba kuwaombea. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu huwasilishwa Naye kama matamano Yake Mwenyewe kwa niaba ya roho hiyo. Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha/umbuji; lakini ikiwa linatoka moyoni (moyo umo ndani yake), litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na Yeye ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja lisilopendeza, lenye kuudhi, tata, gumu au lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe. –(The Desire of Ages, 667) [Pr 218.2; Maombi Aya ya 4]

Wanafunzi walipaswa kuendeleza kazi yao katika Jina la Kristo. Kila neno na tendo lao lilipaswa kukazia fikira juu ya Jina Lake, kama lililo na nguvu muhimu ambayo kwayo wenye dhambi wanaweza kuokolewa. Imani yao ilikuwa ni kujikita ndani Yake, Yeye ambaye ni Chanzo cha rehema na nguvu. Katika Jina Lake walipaswa kuwasilisha maombi yao kwa Baba, na wangepokea majibu. Walipaswa kubatiza kwa Jina la Baba, la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Jina la Kristo lilipaswa kuwa tamko la imani yao, kauli mbiu, kitambulisho cha utofauti wao, beji yao ya upekee, kifungo chao cha muungano, mamlaka ya mwenendo wao, na

chanzo cha mafanikio yao .— (The Acts of the Apostles, 28)
[Pr 218.3; Maombi Aya ya 5]

Patakatifu pa Patakatifu naliona sanduku; juu na pande zake ilikuwa dhahabu safi. Kila mwisho wa sanduku kulikuwa na kerubi mwenye kupendeza, na mabawa yake yametandazwa juu yake. Nyuso zao zilielekeana, na wakatazama chini. Kati ya malaika hao kulikuwa na chetezo cha dhahabu. Juu ya sanduku, pale waliposimama malaika, palikuwa na utukufu ung'ao sana, ukionekana kama kiti cha enzi alipokaa MUNGU (Shekina). Yesu alisimama kando ya sanduku, na sala za watakatifu zilipomjia, uvumba ndani ya chetezo ukatoka moshi, na Yeye alitoa sala zao pamoja na moshi wa uvumba kwa Baba Yake.—(Early Writings, 32) [Pr 218.4; Maombi Aya ya 6]

Ina maana gani kuomba Katika Jina la Yesu—Kuomba katika Jina la Kristo kunamaanisha mengi. Inamaanisha kwamba tunapaswa kukubali tabia Yake, kudhihirisha roho Yake, na kufanya kazi Zake. Ahadi ya Mwokozi inatolewa kwa masharti. “Mkinipenda,” Anasema, “mtazishika amri Zangu.” Yeye huwaokoa wanadamu, si katika dhambi, bali kutoka katika dhambi; na wale wanaompenda wataonyesha upendo wao kwa utii.—(The Desire of Ages, 668) [Pr 219.1; Maombi Aya ya 7]

Yesu alisema, "Ninyi mtaomba kwa Jina Langu; na siwaambii, kwamba nitaomba kwa Baba kwa ajili yenu: kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda. "Mimi Nimewachagua: ili chochote mtakachomwomba Baba kwa Jina Langu, awapatie." Yohana 16:26, 27; Yohana 15:16. Lakini kuomba katika Jina la Yesu ni jambo zaidi ya kutaja tu Jina hilo mwanzoni na mwisho wa ombi. Ni kuomba katika akili, nia na roho ya Yesu, huku tukiamini ahadi Zake, kutegemea neema Yake, na kufanya kazi Zake. —(Steps to Christ, 100, 101) [Pr 219.2; Maombi Aya ya 8]

MUNGU Anatalika Sisi Kuja Kwake katika Jina la Yesu —Wewe unaalikwa kuja, kuomba, kutafuta, kubisha; na umehakikishiwa kwamba hautatoka mtupu. Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.” Mathayo 7:7, 8. [Pr 219.3; Maombi Aya ya 9]

Kristo anaonyesha nia ya MUNGU kubariki kwa utayari wa baba kutimiza ombi la mtoto wake. Yeye Anasema, "Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe?" au akimwomba samaki atampa nyoka badala ya samaki? Na kama akimwomba yai, je, atampa ng'e? Ikiwa basi ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? Luka 11:11-13. [Pr 219.4; Maombi Aya ya 10]

Tunamwendea MUNGU katika Jina la Yesu kwa mwaliko maalum, Naye anatukaribisha kwenye chumba Chake cha faragha cha kusikiliza maombi. Yeye Anaikabidhi ile nafsi iliyonyenyekea, iliyotubu, ile imani katika Kristo ambayo kwayo anahesabiwa haki. Yesu anafuta uovu wake kama wingu zito, na moyo uliofarijiwa unapaza sauti kwa kushangilia, "Ee Bwana, nitakusifu; ingawa ulinikasirikia, hasira Yako imegeuka, nawe umenifariji. Isaya 12:1.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 242) [Pr 220.1; Maombi Aya ya 11]

Omba katika Jina la Yesu na kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu — Wakati mtu anatoa ombi la dhiti na bidii kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee tulilopewa chini ya mbingu litupasalo kuokolewa), katika ile nguvu na unyofu kuna ahadi kutoka kwa MUNGU kwamba Yeye Yupo karibu kujibu hilo ombi na zaidi, juu ya yote tunayoweza kumuomba au kufikiri (Efeso 3:20). Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Yesu, bali kwa uvuvio na uwepo wa moto/joto la Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa kuna maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa maumivu/kuugua kwingi kusikoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhiti. Kisha yatakifikia kiti cha rehema. Endelea kuomba bila kusita au kuchoka. MUNGU hasemi, Omba mara moja tu, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, kuwa mwepesi kuomba yaani uwe na utayari wa kutoa sala wakati wowote, ukiamini kwamba umekwishavipokea vile vitu ambavyo umeviomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu. - (Gospel Herald, Mei 28, 1902) [Pr 220.2; Maombi Aya ya 12]

Twaweza Kumkaribia MUNGU kwa Ujasiri Kupitia Jina la Yesu—Unyenyekevu na ucha Mungu vinapaswa kubainisha tabia ya wote wanaokuja katika uwepo wa MUNGU. Kwa Jina la Yesu sisi tunaweza kwenda mbele

Zake kwa ujasiri, lakini hatupaswi kumkaribia Yeye kwa ujasiri wenye udanganyifu, usiofuata mapenzi yake, au kiburi, au vile ambavyo Mungu hajatuelekeza (kwa dhana potofu), kana kwamba Yeye Yupo ngazi moja na sisi. Kuna wale ambao wanazungumza na MUNGU mkuu na Mwenye nguvu zote na mtakatifu, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kufikiwa, kama wanavyoweza kuongea na mtu wanayelingana naye, au hata mtu duni kuliko wao. Kuna wale wanaotenda katika nyumba Yake Mungu kwa namna ambayo hawawezi kufanya katika chumba cha kuonia na mtawala wa kidunia. Hawa wanapaswa kukumbuka kuwa wako machoni Pake Yeye Yule ambaye maserafi humwabudu, mahali ambapo malaika hufunika nyuso zao mbele Yake.- (Patriarchs and Prophets, 252) [Pr 220.3; Maombi Aya ya 13]

Kwa Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele za uwepo wa MUNGU na ujasiri wa mtoto. Hakuna mtu anayehitajika kufanya kazi kama mpatanishi. Kupitia Yesu, sisi tunaweza kufungua mioyo yetu kwa MUNGU kama kwa Yule anayetujua na kutupenda sisi.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 84) [Pr 221.1; Maombi Aya ya 14]

MUNGU Ataliheshimu Jina la Yesu Katika Maombi yetu
—Kila ahadi katika Neno la MUNGU hutupatia jambo la kuombea, ikiwasilisha Neno la Yehova aliloahidi kama uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayoihitaji, sisi tumependelewa kuidai kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa unyenyekevu na usahili wa mtoto kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi, tukamwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, nawe umealikwa kumuomba kuhusiana na hivi vyote. Ni kupitia Jina la Yesu tu, kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina Hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake (anatoa kwa uhuru mkubwa, watu wamehesabu ahadi 8100 kwenye Biblia, jaribu kuihesabu Ahadi 12 za Mungu katika Kutoka 20 leo!). —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 221.2; Maombi Aya ya 15]

Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa ina maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua na

maumivu makubwa yasiyoweza kutamkika." Warumi 8:26 MUNGU hufurahia kujibu maombi kama hayo. Tunapotoa ombi katika Jina la Kristo kwa dhati na nguvu, kuna ahadi yenye nguvu kutoka kwa MUNGU kwamba Yu karibu kujibu ombi letu "kwa wingi zaidi ya yote tunayoomba au kufikiri." Waefeso 3:20. [Pr 221.3; Maombi Aya ya 16]

Kristo amesema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Yohana 14:13. Naye Yohana mpendwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, anena kwa uwazi na uhakikisho ulio mkuu: "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba Yeye hutusikia, lolote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba." 1 Yohana 5:14, 15. Basi wasilisha maombi yako kwa ujasiri na msukumo kwa Baba katika Jina la Yesu. MUNGU ataliheshimu Jina hilo.—(Christ's Object Lessons, 147, 148) [Pr 221.4; Maombi Aya ya 17]

SURA YA 21

MWONGOZO WA BWANA KUPITIA MAOMBI

Tunaweza Kujifunza Mapenzi ya MUNGU Kwetu Kupitia Maombi—Bwana hafanyi kazi bila kanuni au kiholela bila mipango. Mtafuteni Bwana kwa dhati na bidii sana katika maombi. Yeye Ataivuvia akili, na atatoa ulimi na usemi. Watu wa MUNGU wanapaswa kuelimishwa kutotegemea mavumbuzi na ubunifu wa mwanadamu na mitihani isiyo na uhakika kama njia ya kujifunza mapenzi ya Mungu kuhusu wao. Shetani na mawakala wake daima wako tayari kuingia katika mpenyo wowote utakaopatikana ambao utawaongoza watu kutoka kwenye kanuni safi za Neno la MUNGU. Watu wanaoongozwa na kufundishwa na MUNGU hawatatoa nafasi kwa ubunifu na mawazo ambayo kwayo hakuna "Bwana asema hivi." (Selected Messages 2:326) [Pr 222.1; Maombi Aya ya 1]

Omba kwa ajili ya Mwongozo wa MUNGU—Ni lazima uelimishe maamuzi yako ili yasiwe dhaifu, duni, yasio na

ufanisi na yasiyofaa. Ni lazima uombe kwa ajili ya uongozi, na kukabidhi njia zako mbele za Bwana. Ni lazima uufunge moyo wako dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na kuufungua kwa kila mvuto wa mbinguni. Ni lazima utumie vyema wakati, na fursa zako zote, ili kukuza tabia linganifu.— (Fundamentals of Christian Education, 302) [Pr 222.2; Maombi Aya ya 2]

Katika kila familia inapaswa kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Ni jambo linalofaa kwa kiasi gani, kwamba wazazi wawakusanye watoto wao pamoja nao kabla ya kula kifungua kinywa kuanza, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake, mwongozo na utunzaji Wake wakati wa mchana! Ni jambo jema linanofaa kwa kiasi gani pia, jioni ifikapo, kwa wazazi na watoto kukusanyika kwa mara nyingine mbele Zake na kumshukuru kwa baraka za siku ambayo imepita!— (Testimonies for the Church 7:43) [Pr 223.1; Maombi Aya ya 3]

Jitoe wakfu kwa MUNGU asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako na liwe, “Nichukue, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako.” Hili ni suala la kila siku. Kila asubuhi jitoe wakfu kwa MUNGU kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au iharishwe au isifanyike kama ulivyopanga, kulingana na jinsi Majaliwa Yake yatakavyoongoza. Kwa namna hiyo unakuwa umeyatoa maisha yako mikononi mwa MUNGU siku kwa siku, na kwa njia hiyo maisha yako yatafanywa kuumbwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo. - (Steps to Christ, 70) [Pr 223.2; Maombi Aya ya 4]

Lazima ujifunze kuona kwa akili yako na pia macho yako. Lazima uyaelimishe maamuzi yako ili yasiwe dhaifu, duni na yasiyo na ufanisi au yasiyofaa. Ni lazima uombe kwa ajili ya uongozi, na kuweka njia yako kwa Bwana. Ni lazima uufunge moyo wako dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na kuufungua kwa kila mvuto/ushawishi wa mbinguni. Ni lazima utumie vizuri wakati na fursa zako, ili kusitawisha tabia yenye ulinganifu.—(Sons and Daughters of God, 283) [Pr 223.3; Maombi Aya ya 5]

Ombi kwa Ajili ya Mwongozo wa MUNGU linaweza Kutolewa Wakati Wowote, na mahali Popote—Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati na bidii. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya shuguli, pilikapilika au biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu kwa Masihi ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje na kukaa ndani yetu kama Mgeni wa mbinguni katika nafsi.—(Steps to Christ, 98, 99). [Pr 223.4; Maombi Aya ya 6]

Kuomba kama Nehemia alivyoomba katika saa yake ya uhitaji ni nyenzo ya kumuongoza Mkristo katika mazingira ambapo aina nyingine za maombi zinaweza kushindikana, watu wanaohenyeka katika vibarua vyenye shuguli nyingi maishani, waliojawa na msongo na karibu kuzidiwa au kutindikiwa na fedheha, wanaweza kutuma ombi kwa MUNGU kwa ajili ya kupata mwongozo Wake. Wasafiri baharini na nchi kavu, wanapotishiwa na hatari kubwa, wanaweza kujikabidhi katika ulinzi wa Mbingu. Wakati wa shida ya ghafla au hatari, moyo unaweza kutuma kilio chake cha kuomba msaada kwa Yule ambaye ameahidi Mwenyewe kuwasaidia waaminifu Wake wale waaminio kila wanapomwita. Katika kila jambo au mazingira, chini ya kila hali, nafsi iliyolemewa na huzuni na masumbufu ya maisha haya, au kushambuliwa vikali na jaribu, inaweza kupata uthibitisho, msaada, sapoti, na usaidizi katika ule upendo usiokoma na nguvu ya MUNGU Anayeshika agano.—(Prophets and Kings, 631, 632) [Pr 224.1; Maombi Aya ya 7]

Malaika Wako Karibu sana Kusaidia Tunapoomba Mwongozo wa MUNGU—Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza Neno la MUNGU kwaajili yetu wenyewe, na kusali kwa ajili ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mtini atatuona sisi mahali pa sirini pa maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta mwongozo wa Bwana.—(The Desire of Ages, 141) [Pr 224.2; Maombi Aya ya 8]

Ulimwengu unaoonekana na usioonekana upo katika mawasiliano ya karibu. Ikiwa pazia lingeondolewa, tungeliwaona malaika waovu wakisukuma giza lao kutuzunguka na kufanya kazi kwa uwezo wao wote kudanganya na kuharibu. Watu waovu wamezingirwa, wanashawishiwa, na kusaidiwa na roho waovu. Mtu wa imani na maombi ameitoa nafsi yake kwenye mwongozo wa Bwana, na malaika wa MUNGU huleta Kwake nuru na nguvu kutoka mbinguni.— (Testimonies for the Church 5:199) [Pr 224.3; Maombi Aya ya 9]

Ujuzi wa Ukweli haitegemei sana nguvu ya akili kama ilivyo juu ya usafi wa kusudi la moyo, na usahili wa imani ya dhati inayomtegemea Mungu. Kwa wale wanatafuta mwongozo wa MUNGU, kwa unyenyekevu wa moyo, malaika wa MUNGU huwakaribia (karibu). Roho Mtakatifu ametolewa ili kuwafungulia hazina nyingi za ile Kweli.— (Christ's Object Lessons, 59) [Pr 225.1; Maombi Aya ya 10]

Chochote Tunachohitaji, Twaweza Kudai Katika Ombi—Kila ahadi* katika Neno la MUNGU hutupatia mada kwa ajili ya ombi, ikiwasilisha Neno la Yehova lililoahidiwa kuwa uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayohitaji, sisi tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa usahili na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi yanayopita, tukimwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa wewe unahitaji vitu hivi vyote, nawe umealikwa kumwomba juu ya vyote. Ni kupitia Jina la Yesu kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake (*kila ahadi hutupa jambo la kuombea, zipo ahadi zaidi ya 8100 kwenye Biblia, hata zile amri kumi za Kutoka 20 zina angalau ahadi 12 za kudai!). —(Thoughts from the Mount of Blessing, 133) [Pr 225.2; Maombi Aya ya 11]

Wazazi waombe Mwongozo wa MUNGU—Wazazi, nyenyekezeni mioyo yenu mbele za MUNGU. Anza kazi kamilifu kwa watoto wako. Msihi Bwana akusamehe kwa kulipuuzia kwako Neno Lake, katika kutojali kuwazoeza watoto wako katika njia wanayopaswa kuiendea. Omba nuru na mwongozo, **dhamiri nyororo,** na maamuzi/utambuzi ulio wazi ili uone makosa na

kufeli/kushindwa kwako. MUNGU atasikia maombi kama hayo kutoka kwenye moyo mnyenyekevu na uliopondeka. - (Child Guidance, 557) [Pr 225.3; Maombi Aya ya 12]

Wale walio tayari Kuongozwa Wanaweza Kujua Mapenzi ya MUNGU— Bwana hufunua mapenzi Yake kwa wale walio na bidii ya dhati na wanaotamani kuongozwa Naye. Sababu ya kukosa kwako ufanisi ni kwamba umeacha wazo la kujua na kuyafanya mapenzi ya MUNGU, na hivyo haujui chochote katika mtazamo chanya. - (Ushuhuda kwa Kanisa 3: 466) [Pr 225.4; Maombi Aya ya 13]

Yachunguze Maandiko kwa Sala kwa ajili ya Uongozi wa Bwana — Wale ambao hawataki kukubali ule Ukweli ulio wazi, ule unaokatakata wa Biblia, na ulio thabiti, kisha daima wakaendelea kutafuta hekaya za kupendeza ambazo zitatuliza au kunyamazisha dhamiri zao, kadiri ya mafundisho yanavyokuwa na upungufu wa mionjo ya kiroho, kujikana nafsi, na kujidhili au kujinyenyekeza, ndivyo yanavyopokelewa kwa upendeleo mkubwa zaidi. Watu hawa wanapunguza nguvu za kiakili katika kutumikia tamaa zao za mwili. Hujiona wenye busara sana katika mawazo yao wenyewe yenye kiburi hata wasitafute Maandiko na kutubu kwa roho na maombi ya moyo uliopondeka na maombi dhati kwa ajili ya mwongozo wa Bwana, hawana ngao dhidi ya udanganyifu. Shetani yuko tayari kutimiza matamaniao ya mioyo yao, naye anaingiza udanganyifu wake alioushika mkoni mwake mahali pa ile Kweli na hivyo kuwatawala kirahisi sana.—(The Great Controversy, 523) [Pr 226.1; Maombi Aya ya 14]

Mtumaini MUNGU Naye Ataongoza Njia Yako — Wengi wanashindwa kupanga mipango bainifu/dhahiri ya siku zijazo. Maisha yao hayajatulia. Wanashindwa kutambua matokeo ya mambo, na hii mara nyingi huwajaza wasiwasi, fadhaa na machafuko (wanakosa utulivu). Hebu na tukumbuke kwamba maisha ya watoto wa MUNGU katika ulimwengu huu ni maisha ya safari ya hija (wasafiri na wapitaji). Sisi hatuna hekima ya kupanga maisha yetu wenyewe. Sio juu yetu kutengeneza au kuyaumba maisha yetu ya baadaye. “Kwa imani Abrahamu alimtii MUNGU alipoitwa aende katika nchi ambayo MUNGU angempa iwe urithi wake. Ingawa hakujua alikokuwa anakwenda, Abrahamu alienda. Waebrania 11: 8. [Pr 226.2; Maombi Aya ya 15]

Kristo katika maisha Yake humu duniani hakujifanyia/hakujipangia mikakati ya maisha Yake Yeye Mwenyewe. Alikubali mipango ya MUNGU Kwake, na siku hadi siku Baba aliifunua mipango Yake. Ndivyo nasi tunavyopaswa kumtegemea MUNGU, ili maisha yetu yaweze kuwa na utekelezaji rahisi yaani mtelemko unaoelekea kwenye mapenzi Yake. Tunapomkabidhi njia zetu, Yeye ataziongoza hatua zetu. [Pr 226.3; Maombi Aya ya 16]

Wengi sana, katika kupanga maisha mazuri ya baadaye, huishia kushindwa kabisa. Mwachie MUNGU akupangie. Kama mtoto mdogo, tumaini mwongozo Wake “Yeye ambaye atashikilia vyema miguu ya watakatifu Wake.” 1 Samweli 2: 9. Mungu kamwe hawaongozi watoto Wake tofauti na vile ambavyo wangechagua kuongozwa, ikiwa wangeweza kuona mwisho tangu mwanzo na kutambua utukufu wa kusudi ambalo wanalitimiza kama watenda kazi pamoja Naye.— (The Ministry of Healing, 478, 479) [Pr 226.4; Maombi Aya ya 17]

Ikiwa umejitoe kwa MUNGU kuifanya kazi Yake, hauna haja ya kuwa na wasiwasi juu ya kesho. Yeye ambaye wewe ni mtumishi Wake, anajua mwisho tangu mwanzo. Matukio ya kesho, ambayo yamefichwa machoni pako, yako wazi machoni Pake Yeye aliye na nguvu zote. [Pr 226.5; Maombi Aya ya 18]

Tunapojichukulia mikononi mwetu usimamizi wa vitu ambavyo tunapaswa kufanya, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa ajili ya mafanikio, tunajitwika mzigo ambao MUNGU hajatupatia, na tunajaribu kuibeba bila msaada Wake. Tunachukua jukumu ambalo ni la MUNGU, na kwa hivyo tunajiweka wenyewe katika nafasi Yake (GOD’s syndrome). Tunaweza kujiletea wasiwasi, fadhaa na kutarajia kukumbana na hatari na hasara, kwani mambo haya yatatupata kwa hakika. Lakini wakati tunaamini kabisa kwamba MUNGU anatupenda Naye ana kusudi la kututendea mema tutakoma kuwa na wasiwasi juu ya siku zijazo. Tutamtumaini MUNGU kama vile mtoto anavyomwamini mzazi wake mwenye upendo. Ndipo taabu

zetu na mateso yatatoweka, kwani mapenzi yetu yamemezwa katika mapenzi ya MUNGU. –(Thoughts from the Mount of Blessing, 100, 101) [Pr 227.1; Maombi Aya ya 19]

Eliezeri Aliomba kwa ajili ya—na Akapokea—Mwongozo wa MUNGU—Akikumbuka maneno ya Abrahamu, kwamba MUNGU atamtuma malaika Wake pamoja naye, alisali kwa dhati na bidii ili kupata mwongozo chanya. Katika familia ya bwana wake alikuwa amezoea tabia ya fadhili/wema, kukaribisha wageni na kuwakarimia/ukarimu, na sasa aliomba kwamba kitendo cha fadhila na ukarimu wa mwenyeji wake kiweze kuonyesha pia msichana ambaye MUNGU alimchagua. [Pr 227.2; Maombi Aya ya 20]

•

Punde baada ya kutolewa maombi, jibu likapatikana papo hapo. Miongoni mwa wanawake ambao walikuwa wamekusanyika kwenye kisima, fadhila/kujistahi/adabu ya mmoja wao ikawa imemvutia. Yule msichana alipokuwa anatoka kisimani, yule mgeni alikwenda kumlaki, akiomba maji kwenye mtungi ulio begani mwake. Ombi hilo lilipokelewa kwa jibu zuri, na ofa ya kuteka maji kwa ajili ya ngamia pia ikatamkwa na msichana huyu, huduma ambayo ilikuwa ni desturi kwa wageni hata kwa binti za wakuu kufanya kwa ajili ya mifugo na makundi ya baba zao. Kwa hivyo ishara iliyotarajiwa ilitolewa/ilionyeshwa na (Rebeka). - (Patriarchs and Prophets, 172) [Pr 227.3; Maombi Aya ya 21]

SURA YA 22

MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA

Maombi yanapaswa Kutolewa kwa ajili ya Wagonjwa kwa Imani tulivu—Nilionyeshwa kwamba katika suala la ugonjwa, pale ambapo njia iko wazi kwa ajili ya kutoa ombi kwa ajili ya wagonjwa, kesi ya mgonjwa inapaswa kukabidhiwa kwa Bwana kwa imani tulivu, sio kwa dhoruba ya msisimko. Yeye peke yake Ndiye anafahamu maisha ya zamani ya mtu huyo na Ndiye anayejua kesho yake itakuwaje. Yeye anayefahamu mioyo ya watu wote anajua ikiwa mtu huyo ataponywa na kisha atoke kitandani mwake, na kulitukuza Jina Lake au atamvunjia heshima Mungu kwa kurudi nyuma na kuasi. Yote tunayotakiwa kufanya ni kumwomba MUNGU awaponye wagonjwa ikiwa ni sawa na mapenzi Yake, tukiamini kuwa Yeye husikia sababu tunazowasilisha na maombi ya bidii yanayotolewa. Ikiwa Bwana ataona itamtukuza zaidi, Yeye atajibu maombi yetu. Lakini kuisitiza au kulazimisha mgonjwa apone bila kujisalimisha kwenye mapenzi Yake sio sawa. - (Testimonies for the Church 2:147, 148) [Pr 228.1; Maombi Aya ya 1]

Pamoja na matibabu yetu yote tunayowapa wagonjwa, maombi rahisi na ya bidii yanapaswa kutolewa kwa ajili ya baraka za uponyaji. Tunapaswa kuwaelekeza wagonjwa kwa Mwokozi Mwenye huruma, na nguvu Yake ya kusamehe na kuponya. —(Selected Messages 3:296). [Pr 228.2; Maombi Aya ya 2]

Wale ambao hufanya kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa za huduma katika namna nyingi (anuwai). Wanapaswa kuwaombea wagonjwa na wanapaswa kufanya yote katika uwezo wao kuwaondoa katika mateso. — (Testimonies for the Church 6:83, 84). [Pr 229.1; Maombi Aya ya 3]

Mwokozi angetutaka tuwatie matumaini wagonjwa wasio na tumaini, wale walio na shida ya maumivu au mateso,

kushikilia nguvu Zake. Kupitia imani na maombi, chumba cha wagonjwa kinaweza kubadilishwa kuwa Betheli (nyumba ya Mungu kama pale Yakobo alipita). - (The Ministry of Healing, 226) [Pr 229.2; Maombi Aya ya 4]

Ikiwa tuna udhaifu wa mwili, kwa kweli ni hakika kumtumainia Bwana, tukiomba dua kwa MUNGU wetu katika kesi yetu, na ikiwa tunajisikia kuwaomba wengine ambao kupitia wao tunao ujasiri wa kuungana nao kwa ajili ya maombi kwa Yesu ambaye ni Tabibu hodari, hakika msaada utakuja ikiwa tutaomba kwa imani. - (Medical Ministry, 16) [Pr 229.3; Maombi Aya ya 5]

Tulituma maombi yetu ya unyenyekevu kwa ajili ya yule aliye mgonjwa na aliyesumbuliwa, ambaye alikuwa njiani kupoteza maisha haya-akichungulia kaburi. Tulipowasilisha jambo hii mbele ya Bwana, tulihisi uhakikisho wa upendo wa MUNGU hata katika kuugua na mateso haya.—(The Review and Herald, October 11, 1887) [Pr 229.4; Maombi Aya ya 6]

Tulimuweka wakfu mtoto na kuomba juu yake, tukiamini kwamba Bwana atawapa mama na mtoto amani. Ikawa hivyo. Vilio vya mtoto vilikoma, na tukawaacha wakiendelea vizuri. —(Spiritual Gifts 2:110, 111) [Pr 229.5; Maombi Aya ya 7]

Wagonjwa wataongozwa kwa Kristo kwa umakini na utunzaji wa wauguzi ambao wanayawazia mahitaji yao kabla hata hawajauliza msaada wao, na ambao huinama katika ombi na kumwomba Mmishenari Mkuu wa Tiba kumtazama kwa huruma mgonjwa anayeteseka na kuruhusu ushawishi unaotuliza wa neema Yake usikike na urejeshwaji wa nguvu Zake udhihirike. - (Medical Ministry, 191, 192) [Pr 229.6; Maombi Aya ya 8]

Wauguzi wa kimishenari wanapowajali wagonjwa na kupunguza shida za maskini, watapata fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la MUNGU, na kuzungumza juu ya Mwokozi..... Wanaweza kuleta mwanga wa tumaini katika maisha ya watu walioshindwa na waliokata tamaa. (Medical Ministry, 246, 247) [Pr 229.7; Maombi Aya ya 9]

Ikiwa maombi zaidi yangetolewa katika vyumba vyetu vya Sanitarium vya wagonjwa wa muda mrefu kwa ajili ya

uponyaji wa wagonjwa, nguvu kuu ya Mponyaji ingeonekana. Wengine wengi pia wangeimarishwa na kubarikiwa, na magonjwa mengi ya dharura (acute) yangeponywa papo hapo. –(Selected Messages 3:295) [Pr 230.1; Maombi Aya ya 10]

Ningeenda mbele za Bwana na ombi hili: “Bwana, hatuwezi kusoma moyo wa mgonjwa huyu, lakini Wewe unajua huenda ni kwa faida ya roho yake na kwa utukufu wa Jina Lako kumuinua kiafya. Kwa wema Wako mkubwa, ulirehemu jambo hili (mhurumie mgonjwa), na ruhusu hatua za kiafya zifanyike katika mfumo wake. Kazi lazima iwe Yako Mwenyewe kabisa.” (Healthful Living, 239). [Pr 230.2; Maombi Aya ya 11]

Hebu sauti ya maombi isikike katika taasisi zetu kwa niaba ya wagonjwa ili waweze kujiweka mahali ambapo wanaweza kushirikiana na Yeye ambaye anaweza kuponya mwili na roho pia. [Pr 230.3; Maombi Aya ya 12]

Hapo awali tulibarikiwa na taasisi ambazo wagonjwa wangeweza kupata msaada dhidi ya mateso, kwa matibabu ya uadilifu na sala za dhati katika imani kwa MUNGU, tulibeba kesi ambazo zilionekana kukosa matumaini ya kufanikiwa. Leo Bwana anawaalika watu wanaoteseka kuwa na imani katika Yeye. Hitaji la mwanadamu ndiyo fursa ya MUNGU kutenda (Man’s necessity is God’s opportunity). – (Selected Messages 3:295, 296). [Pr 230.4; Maombi Aya ya 13]

Yote ambayo yanaweza kufanywa katika kuwaombea wagonjwa ni kumsihi tu MUNGU kwa dhati na bidii, na bila kuchoka kwa niaba yao, na kwa ujasiri kamili kabidhi suala hilo mikononi Mwake. Ikiwa tunazingatia uovu mioyoni mwetu Bwana hatatusikia. Yeye Anaweza kufanya apendavyo na watu Wake Mwenyewe.– (Testimonies for the Church 2:148) [Pr 230.5; Maombi Aya ya 14]

Mara nyingi imekuwa upendeleo wangu kuomba na wagonjwa. Tunapaswa kufanya hivi mara nyingi zaidi kuliko tunavyofanya katika maisha yetu. –(Selected Messages 3:295) [Pr 230.6; Maombi Aya ya 15]

Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka kwa Kristo mikononi mwa imani yetu Tunapaswa kushikilia ahadi Yake, na kuomba kwa ajili ya udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini cha injili ni urejesho/kurejeshwa, na

Mwokozi angetutaka sisi tuwaombe wagonjwa, wale wasio na tumaini, na wenye shida kwamba washizishikilie nguvu Zake. - (The Desire of Ages, 824, 825) [Pr 231.1; Maombi Aya ya 16]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa Ni Muhimu Sana hivyo yasishughulikiwe kwa Uzembe—Kuhusu kuombea wagonjwa, ni jambo la maana mno kiasi kwamba hatupaswi kushughulikia pasipo kujali. Ninaamini tunapaswa kupeleka kila kitu kwa Bwana, na kumjulisha MUNGU udhaifu wetu wote na kutaja shida zetu zote anuwai. - (Medical Ministry, 16) [Pr 231.2; Maombi Aya ya 17]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa yanafaa Leo kama katika Nyakati za Biblia—Mponyaji wa Kiungu/Mbinguni Yuko katika chumba cha wagonjwa; Yeye Anasikia kila neno la maombi yanayotolewa Kwake katika usahili wa imani ya kweli. Wanafunzi Wake leo wanapaswa kuwaombea wagonjwa, kama walivyofanya wanafunzi wa kale. Na kutakuwa na uponyaji; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa." (Gospel Workers, 215) [Pr 231.3; Maombi Aya ya 18]

Mungu Yuko tayari kurejesha afya ya wagonjwa sasa kama vile Roho Mtakatifu aliposema Maneno haya kupitia mwandishi wa- Zaburi. Na Kristo Ndiye Yule Yule, daktari/tabibu Mwenye huruma sasa kama alivyokuwa wakati wa huduma Yake hapa duniani. Ndani Yake kuna zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, nguvu ya uponyaji kwa kila udhaifu. Wanafunzi Wake kwa wakati huu wanapaswa kuwaombea wagonjwa kwa hakika kama vile wanafunzi wa zamani walivyoomba. Na uponyaji utafuata; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa." Tunayo nguvu ya Roho Mtakatifu, uhakika mtulivu wa imani, ambao tunaweza kudai ahadi za MUNGU. Ahadi ya Bwana, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya" (Marko 16:18), hili ni la kuaminika sasa kama katika siku zile za mitume. Ahadi hii inaonyesha fursa ya watoto wa MUNGU, na imani yetu inapaswa kushikilia yote ambayo tungeweza kuyashikilia. Watumishi wa Kristo ndio mfereji wa utendaji Wake, na kupitia kwao Bwana anatamani kutumia nguvu Zake za uponyaji. Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka Kwake Mungu, kwenye mikono ya imani yetu. Tunapaswa kuwafundisha kuamini katika Mponyaji Mkuu. - (The Ministry of Healing, 226) [Pr 231.4; Maombi Aya ya 19]

Maombi kwa ajili ya Wagonjwa Yapasa Kuzingatia Mapenzi ya MUNGU— Katika sala kwa ajili ya wagonjwa yapaswa ikumbukwe kwamba “hatujui tunalopaswa kuomba jinsi itupasavyo.” Warumi 8:26 Hatujui kama baraka tunayotaimani itakuwa bora au la. Kwa hivyo maombi yetu yanapaswa kujumuisha wazo hili: 'Bwana, unajua kila siri ya roho. Wewe unawafhamu watu hawa. Yesu, Wewe ni Wakili wao, Nawe ulitoa uhai Wako kwa ajili yao. Upendo Wako kwao ni mkubwa kuliko wetu unavyoweza kuwa. Ikiwa, ni kwa ajili ya utukufu Wako na mema ya wale wanaoteseka, tunaomba, kwa Jina lako Yesu, kwamba waweze kupona. Ikiwa sio mapenzi Yako kwamba waweze kurejeshewa afya zao, tunaomba kwamba neema Yako iwafaraji na uwepo Wako uwaimarisha na kuwasaidia katika mateso yao. [Pr 232.1; Maombi Aya ya 20]

“MUNGU anajua mwisho tangu mwanzo. Yeye Anajua mioyo ya watu wote. Yeye anasoma kila siri ya roho. Yeye Anajua kama wale ambao wanaombewa wangeweza au wasingeweza kustahimili majaribu ambayo yangewajia wanapoendelea kuishi. Yeye Anajua kama maisha yao yatakuwa mbaraka au laana kwao wenyewe na kwa ulimwengu. Hii ni sababu moja kwa nini, wakati tunawasilisha ombi letu kwa bidii, tunapaswa kusema, “Walakini sio mapenzi yangu, bali Yako yatimizwe.” Luka 22:42. (Ministry of Healing, 229, 230) [Pr 232.2; Maombi Aya ya 21]

Katika kuwaombea wagonjwa, tunapaswa kuomba kwamba ikiwa ni mapenzi ya MUNGU basi waponywe, na wawe na afya; lakini ikiwa ni vinginevyo basi Yeye awape neema Yake ya kuwafaraji, na uwepo Wake uwadumisha katika mateso yao. Wengi wanaopaswa kuweka nyumba zao sawa, yaani katika mpangilio, hupuza kufanya hivyo wakati wana tumaini kwamba watainuliwa kiafya katika kujibiwa maombi. Wakichochea na tumaini la uwongo, hawahisi hitaji la kutoa maneno ya mawaidha na ushauri kwa watoto wao, wazazi, au marafiki, na hii ni bahati mbaya sana. Wakikubali uhakikisho wa kwamba wangeponywa wakati wa kuombewa, hawathubutu kutaja jinsi mali zao zitakavyogawiwa, jinsi familia yao inavyopaswa kutunzwa, au kueleza matamano yoyote kuhusu mambo ambayo wangezungumza ikiwa walidhani wangeondolewa na kifo. Kwa njia hii janga huletwa

kwenye familia na marafiki; kwa maana mambo mengi ambayo yanapaswa kueleweka na watakaobakia mgonjwa akifa, yameachwa bila kutajwa au kuzungumziwa, kwa sababu wanaogopa kuwa kujieleza juu ya mambo haya itakuwa ni kuikana imani yao. Wakiamini watainuliwa kiafya kwasababu ya maombi, wanashindwa kutumia njia au kanuni za afya, au usafi ambazo ziko katika uwezo wao, wakihofia kuwa kutenda hilo ni kuikana imani yao. — (General Conference Daily Bulletin, February 26, 1897) [Pr 232.3; Maombi Aya ya 22]

“Tumeungana katika maombi ya dhati karibu na vitanda vya wagonjwa waume, na wake, na watoto, nasi tumehisi kuwa walirudishwa kwetu kutoka katika kifo kama jibu la maombi yetu ya dhati na bidii. Katika maombi haya tulifikiri lazima tuwe na mtazamo chanya, na ikiwa tuna imani, ni lazima tuombe kwaajili ya uhai tu. Hatukuthubutu kusema, “Ikiwa itamtukuza MUNGU,” tukiogopa kuwa ingekuwa sawa na kuwa na shaka. Tumewaangalia kwa wasiwasi wale ambao wamerudishwa kwetu kama wale waliotoka kifoni. Tumeona baadhi ya hawa, haswa vijana, wakirejeshewa afya, nao wakamsahau MUNGU, wakawa wenye tabia mbaya maishani, wakisababisha huzuni na uchungu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa aibu kwa wale ambao waliogopa kuomba mapenzi ya Mungu yatimizwe. Waliishi kwa kutomheshimu na kumtukuza MUNGU, bali kumlaani kwa maisha yao ya uovu. [Pr 233.1; Maombi Aya ya 23]

“Hatutengenezi njia tena wala kutafuta kumleta Bwana katika matamano yetu. Ikiwa maisha ya wagonjwa yanaweza kumtukuza Yeye, basi tunaomba kwamba waishi, hata hivyo, si kama sisi tutakavyo bali kama Yeye atakavyo. Imani yetu inaweza kuwa imara, na ya uhakika kwa kuyakabidhi matamano yetu kwa MUNGU Mwenye hekima yote, na, bila wasiwasi au homa, na kwa ujasiri mkamilifu, tukimwamini Yeye na kumkabidhi yote. Tunayo ahadi. Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake.— (Counsels on Health, 378, 379) [Pr 233.2; Maombi Aya ya 24]

Mungu Hujibu Maombi kwa ajili ya Wagonjwa — Hakuna nguvu ya kibinadamu inayoweza kuokoa wagonjwa, lakini, kupitia maombi ya imani, Mponyaji Mkuu ametimiza

ahadi Yake kwa wale ambao wameliitia Jina Lake.—
(Selected Messages 3:295). [Pr 233.3; Maombi Aya ya 25]

Hebu tufanye kama mitume wa Kristo walivyofanya; hebu tufanye maombi kwaajili ya wagonjwa, kwani wapo wengi ambao hawawezi kufaidika na vituo vyetu vya Sanitarium (tiba rahisi). Bwana ataondoa udhaifu katika kujibu maombi. - (Medical Ministry, 242) [Pr 233.4; Maombi Aya ya 26]

Kudumu katika Maombi ni Muhimu Wakati Tunaombea Wagonjwa — Katika kuwaombea wagonjwa, ni muhimu kuwa na imani; kwani kufanya hivyo ni kulingana na Neno la MUNGU. "Maombi ya bidii ya mwenye haki yanafaa sana." Yakobo 5:16. Kwa hivyo hatuwezi kutupilia mbali kuombea wagonjwa, na tunapaswa kusikitika sana ikiwa tungekosa fursa ya kumkaribia MUNGU, kwa kuweka mbele Zake udhaifu wetu wote na ugonjwa wetu, kumweleza Mwokozi Mwenye huruma juu ya mambo haya, tukiamini kwamba Yeye husikia maombi yetu. Wakati mwingine majibu ya maombi yetu huja mara moja; wakati mwingine tunalazimika kungojea kwa uvumilivu na kuendelea kuomba kwa bidii vitu tunavyohitaji, mahitaji yetu yakiwasiliswa na mahitaji ya mwombaji asiyechoka aliyeenda kuomba mkate usiku. "Ni yupi kati yenu ambaye atakuwa na rafiki, na atamwendea usiku wa manane," nk. Somo hili lina maana zaidi ya vile tunaweza kufikiria. Tunapaswa kuendelea kuomba, hata ikiwa hatujaona au kutambua majibu ya haraka ya maombi yetu. "Ninawaambia, ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa. Maana yeyote aombaye hupewa, atafutaye hupata na abishaye hufunguliwa. Luka 11: 9, 10. [Pr 234.1; Maombi Aya ya 27]

Tunahitaji neema, tunahitaji mwangaza kutoka kwa BWANA, ili kupitia Roho Mtakatifu tuweze kujua jinsi ya kuomba mambo hayo ambayo hakika tunayahitaji. Maombi yetu yakizingatiwa na Bwana yatajibiwa .— (Counsels on Health, 380) [Pr 234.2; Maombi Aya ya 28]

Dhambi Lazima Iwekwe Mbali ikiwa Maombi ya Uponyaji Yapasa Kujibiwa— Kwa wale wanaotamani maombi ya kurejeshewa afya, inapaswa kuwekwa wazi kuwa ukiukaji wa sheria za MUNGU, ziwe za asili au za kiroho, ni dhambi, na ili wao waweze kupokea baraka

Yake, lazima tuikiri dhambi yetu na kuitupilia mbali. [Pr 234.3; Maombi Aya ya 29]

"Maandiko yanatuambia," Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa." Yakobo 5:16. Kwa yule anayefanya maombi, hebu mawazo kama haya yawasilishwe: 'Sisi hatuwezi kusoma moyo wako, au kujua siri za maisha yako. Hizo zinajulikana kwako mwenyewe tu na kwa MUNGU. Ukizikiri dhambi zako, ni wajibu wako kuziungama. 'The Ministry of Healing, 228) [Pr 234.4; Maombi Aya ya 30]

Kujiamini Kupita Kiasi Huonekana Kama Imani katika Kuombea Wagonjwa— Nimeona mambo mengi sana, katika kuwaombea wagonjwa yanayochukuliwa kwa kupitiliza (ushabiki), hadi nikahisi kwamba sehemu hii ya uzoefu wetu inahitaji mawazo thabiti, yaliyotakaswa, tusije kufanya ushabiki fulani kwa kudhania kwamba ni imani, na hata tukaiita ni imani, kumbe si chochote zaidi ya dhana potofu, ambayo inaenda dhidi ya mapenzi ya Mungu, imani bandia au ni kiburi cha aina fulani (presumption). Watu waliochoka na shida ya ugonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili wasonge kwa busara na hivyo kutoharibu mambo au kujiabisha; na wakati wanajiweka mbele za MUNGU kuombewa ili waponywe, hawapaswi kuchukua msimamo kwamba njia za urejeshaji wa afya kulingana na sheria za asili zinapaswa kupuuzwa.

(tiba mbadala zinazofanya kazi, sisi tunapaswa kuwa na busara kuzitumia, ila kwenda hospitali na kuchunguzwa, kuchukua vipimo, maabara au xray ni muhimu kwenye dharura au hali tete, ila tunapaswa kujua jinsi ya kuzitumia tiba rahisi 8 Mungu alizotoa nazo ni zile wazungu wanaita **NEW START** Yaani Nutrition/Lishe, Exercise/Mazoezi, Water/Maji, Sunshine/Jua, Temperance/Kiasi, Air/Sunshine, Rest/Mapumziko, na Trust in Divine Power/Kumtegemea Mungu). [Pr 235.1; Maombi Aya ya 31]

Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuombea uponyaji lazima wasitumie tiba rahisi zilizotolewa na MUNGU ili kupunguza maumivu na kuisaidia asili katika kazi yake, hebu isije ikaonekana kwamba ni kuikana imani, wanachukua msimamo usio wa busara. Huku siko kuikana imani; Inaendana kabisa na mipango ya MUNGU. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa MUNGU alimletea ujumbe

kwamba lazima afe. Alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake na kufanya muujiza kwa niaba yake, akampelekea ujumbe kwamba miaka kumi na mitano ingeongezwa kwenye maisha yake. Sasa hapa Mungu angetumia Neno moja tu, na kisha angetibiwa kwa kuguswa mara moja tu kwa kidole cha Bwana, lakini maagizo maalum yalitolewa kuchukua tini na kuiweka kwenye sehemu iliyoathiriwa, na Hezekia akarejeshewa afya, yaani uzima wake ukarudishwa. Katika kila jambo tunahitaji kuenanda na mstari wa mipango na majaliwa ya MUNGU. [Pr 235.2; Maombi Aya ya 32]

Wakala wa kibinadamu unapaswa kuwa na imani na unapaswa kushirikiana na uwezo wa Bwana, mtu akitumia kila namna ya nyenzo, akichukua faida ya kila kitu ambacho kulingana na akili yake ni cha manufaa, akifanya kazi kwa kupatana na sheria za asili; basi kwa kufanya hivyo haikani wala hazuii imani.— (Counsels on Health, 381, 382) [Pr 235.3; Maombi Aya ya 33]

Katika Neno la MUNGU tuna maagizo yanayohusiana na maombi maalumu ya kupona kwa wagonjwa. Lakini utoaji wa ombi kama hilo ni tendo la wakfu kabisa na halipaswi kuchukuliwa bila kuzingatiwa kwa uangalifu. Katika visa vingi vya kuomba uponyaji wa wagonjwa, ile inayoitwa imani si kitu kingine tofauti na dhana potofu inayopingana na mapenzi ya Mungu au hata kiburi (presumption). [Pr 235.4; Maombi Aya ya 34]

Watu wengi hujiletea magonjwa kwa kujifurahisha au kujiendekeza kwao wenyewe. Hawajaishi kulingana na sheria ya asili au kanuni za usafi wa moyo thabiti. Wengine wamepuuza sheria za afya katika tabia zao za kula na kunywa, kuvaa, au kufanya kazi. Mara nyingi aina fulani ya uovu ndiyo sababu ya udhaifu wa akili au mwili. Ikiwa watu hawa wangepata baraka ya afya, wengi wao wangeendelea kufuata njia ile ile ya uasi wa kutozingatia sheria za asili na za kiroho za MUNGU, wakifikiri kwamba ikiwa MUNGU atawaponya katika kujibu maombi yao, basi wao wako huru kuendelea na mazoea yao ya afya yaliyo mabaya na yasiyofaa na kuendeleza kujifurahisha na tamaa za mwili potovu bila kujizua. Ikiwa MUNGU angefanya muujiza kuwarudishia watu hawa afya, angekuwa akiwatia moyo kuitenda dhambi. [Pr 235.5; Maombi Aya ya 35]

Ni kazi iliyopotea kuwafundisha watu kumtazama MUNGU kama mponyaji wa udhaifu wao, pasipo kuwafundisha pia kuacha mazoea yasiyofaa, yale ambayo yanapingana na afya. Ili kupokea baraka Yake katika kujibu maombi, lazima waache kufanya uovu na kujifunza kutenda vyema. Mazingira yao lazima yawe safi, mwenendo wao wa maisha uwe sahihi. Lazima waishi kwa kupatana na sheria ya MUNGU, asili na kiroho. - (The Ministry of Healing, 227, 228) [Pr 236.1; Maombi Aya ya 36]

Maombi ya Uponyaji wa Kimiujiza Yanaweza Kusababisha Ushupavu (au kupitiliza kiasi) - "Kwa nini," mmoja baada ya mwingine hujiuliza, "je, maombi hayatolewi kwa ajili ya uponyaji wa kimwujiza, badala yake hutolewa kwa ajili ya vituo vingi vya afya vya Sanitarium vilivyoanzishwa?" Hili likifanyika, ushupavu mkubwa utazuka katika vituo vyetu. Wale wanaojiamini kupita kiasi wangeanza kufanya mabadiliko.—(Evangelism, 594, 595) [Pr 236.2; Maombi Aya ya 37]

Kuzingatia Maelekezo ya Tabibu Sio Kuikana Imani Katika Maombi ya Uponyaji— Wengi wanaotafuta rehema ya uponyaji wa Bwana wanafikiri kwamba lazima wawe na jibu la moja kwa moja na la haraka kwa maombi yao, la sivyo imani yao ina hitilafu. Kwa sababu hii, wale ambao wamedhoofishwa na magonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili watende kwa hekima. Hawapaswi kupuuza wajibu wao kwa marafiki ambao wanaweza kuendelea kuishi wakati wao wameingia kaburini, au kupuuza kutumia wakala wa asili (au tiba mbadala) kwaajili ya urejeshaji wa afya. [Pr 236.3; Maombi Aya ya 38]

Mara nyingi kuna hatari ya kukosea hapa. Kwa kuamini kwamba wataponywa katika jibu la maombi, wengine wanaogopa kufanya chochote kile ambacho kinaweza kuonekana kwamba kinaashiria ukosefu wa imani kwa upande wao. Lakini hawapaswi kupuuza kuyaweka mambo yao sawa kama wanavyotamani kufanya ikiwa kuna tarajio la wao kuondolewa kwa kifo. Wala hawapaswi kuogopa kusema maneno ya kutia moyo au ushauri ambao wangetamani kuuotoa katika saa ya kuagana kwa wapendwa wao. - (The Ministry of Healing, 231) [Pr 237.1; Maombi Aya ya 39]

Lakini baada ya kuwaombea kwa dhati na bidii wagonjwa nini kifuate basi? Je, ninaacha kufanya yote niwezayo kwa ajili ya kupona kwao?—Hapana, ninafanya kazi kwa bidii zaidi, kwa maombi mengi kwamba Bwana apate kubariki njia ambayo mkono Wake Mwenyewe umetoa; ili aweze kutoa hekima iliyotakaswa kwa ajili ya kushirikiana Naye katika kuwaponya wagonjwa.— (Healthful Living, 240, [1897, 1898]). [Pr 237.1; Maombi Aya ya 40]

Matibabu ya Taasisi za Afya Yanapaswa Kutumiwa Pamoja na Maombi Kwa ajili ya Uponyaji (Maabara, Kumwona Daktari kwa uchunguzi na ushauri, kupasuliwa, kutumia vidonge katika hali ya dharura ukingoja suluhisho sahili linalosaidia afya kwa muda mrefu)—Wale wanaotafuta uponyaji kwa maombi hawapaswi kupuuza kutumia tiba rahisi (au tiba mbadala) ambayo ipo karibu nao, na wanaweza kuipata kwa urahisi, nayo ikawa na matokeo mazuri tu. Kutumia tiba zile ambazo MUNGU amezitoa katika kupunguza maumivu na kusaidia asili/mwili katika kazi yake ya urejeshaji afya sio kuikana imani. Kushirikiana na MUNGU, na kujiweka katika hali rafiki inayoleta uponyaji siyo kukana imani. MUNGU ameweka ndani ya uwezo/uwezekano wa kujipatia ujuzi wa sheria za uhai/uzima. Maarifa haya, Mungu yamewekwa ndani ya maeneo yetu ya karibu luwezo wetul, ili tuweze kuyafikia, kwaajili ya matumizi/kuyatumia. Tunapaswa kutumia kila njia au miundombinu kwaajili ya urejeshaji wa afya, tukitumia kila fursa inayowezekana, kwa kufanya kazi kwa kulingana na sheria za asili. Wakati tumesali ili wagonjwa wapone, tunaweza kufanya kazi kwa nguvu nyingi zaidi, tukimshukuru MUNGU kwamba tunao upendeleo wa kushirikiana Naye, na kuomba baraka Zake juu ya njia ambazo Yeye Mwenyewe ametuandalia/ametujalia.—(The Ministry of Healing, 231, 232) [Pr 237.2; Maombi Aya ya 41]

Mtumaini MUNGU bila kujali Matokeo Ya Maombi Yatakuwaje- Tunapomba kwa ajili ya kupona kwa wagonjwa, haijalishi matokeo ya jambo hilo, hebu tusipoteze imani kwa MUNGU. Ikiwa tutaitwa kukutana na msiba, hebu tukubali kikombe chenye uchungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba ndiyo unakishikilia kikombe hicho kwenye midomo yetu. Lakini ikiwa afya

itarejeshwa, haipaswi kusahaulika kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba. - (The Ministry of Healing, 233) [Pr 237.3; Maombi Aya ya 42]

SURA YA 23

MAOMBI KWA AJILI YA MSAMAHA

Ombi la Msamaha Daima Hujibiwa haraka yaani papo hapo— Tunapoomba baraka za kidunia, jibu la ombi letu linaweza kucheleweshwa, au MUNGU anaweza kutupa kitu kingine tofauti na tunachoomba, lakini si hivyo tunapoomba ukombozi kutoka katika dhambi. Ni mapenzi Yake Yeye, kutusafisha dhambi, kutufanya sisi watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Masihi “alijitoa nafsi Yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atukomboe na ulimwengu huu mbovu wa sasa, kama yalivyo mapenzi ya MUNGU Baba yetu.” Wagalatia 1:4. “Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye anatusikia; na kama tukijua ya kuwa anatusikia, tuombalo lolote, twajua ya kuwa tunazo haja tulizoziomba Kwake.” 1 Yohana 5:14, 15. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. 1 Yohana 1:9 .— (The Desire of Ages, 266) [Pr 238.1; Maombi Aya ya 1]

Mara tu mtoto wa MUNGU anapokaribia Kiti cha Rehema, ndipo anakuwa mteja wa Wakili mkuu. Katika tamko lake la kwanza la toba na ombi la msamaha Kristo hutetea kesi yake na kuifanya iwe Yake Mwenyewe, akiwasilisha ombi hilo mbele ya Baba Yake kama ombi Lake Mwenyewe.—(Testimonies for the Church 6:364) [Pr 238.2; Maombi Aya ya 2]

Mwambie Yesu mahitaji yako kwa unyofu wa nafsi yako. Hautakiwi kushikilia mdahalo au hoja/mabishano marefu, au kumtolea mahubiri Mungu, bali kwa moyo wa huzuni kwa ajili ya dhambi zako, sema, “Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia.” Kuna tumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu anakapokuwa ameuondoa mzungu wa dhambi unayoiponda nafsi, utapata baraka za amani ya Kristo.—(Our High Calling, p. 131) [Pr 239.1; Maombi Aya ya 3]

Tunapona ubaya wa dhambi, tunaanguka bila msaada mbele ya msalaba, tukiomba msamaha na nguvu, maombi yetu yanasikika na kujibiwa. Wale wanaowasilisha maombi yao kwa MUNGU katika Jina la Kristo hawataachwa kamwe. Bwana asema, “Yeye ajaye Kwangu sitamtupa kamwe.” “Atayatazama maombi ya mtu aliye mkiwa.” Msaada wa Maombi yetu ya Msamaha unatoka kwa Yeye ambaye anashikilia vitu vyote mikononi Mwake. Amani anayotuma ni uhakikisho wa upendo Wake kwetu. [Pr 239.2; Maombi Aya ya 4]

Hakuna kitu kinachoweza kuwa/kupata msaada na kisichoweza kushindwa kabisa kuliko roho inayohisi kutokuwa na kitu (utupu wake), na hivyo kuzitegemea kabisa sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka (kujidondosha kabisa kwa Mwokozi). MUNGU atatuma kila malaika mbinguni kumsaidia yule anayeweka tegemeo lake lote kwa Kristo, badala ya kumruhusu kushindwa.—(The Signs of the Times, Oktoba 29, 1902) [Pr 239.3; Maombi Aya ya 5]

Wale Wanaotafuta Msamaha Lazima Wenyewe Wawe na Tabia ya Kusamehe—Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha katika mioyo yetu wenyewe. Tunawezaje kuomba basi, “Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu,” na bado tuendekeze na

roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatazamia sala zetu kusikiwa na Mwenyezi Mungu, basi ni lazima tuwasamehe wengine kwa namna ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotamani kusamehewa.—(Steps to Christ, 97) [Pr 239.4; Maombi Aya ya 6]

Baada ya kumaliza Sala ya Bwana, Yesu aliongeza hivi: “Mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Mathayo 6:14, 15. Yeye asiyesamehe anafunga kila mfereji ambao kwa huo peke yake anaweza kupokea rehema kutoka kwa MUNGU. Hatupaswi kufikiri kwamba wale waliotuumiza wasipokiri kosa lao, basi sisi tuna haki ya kuwanyima msamaha wetu. Ni sehemu ya wajibu wao, bila shaka, kunyenyekeza mioyo yao kwa toba na maungamo; lakini tunapaswa kuwa na roho ya huruma kwa wale ambao wametukosea, haijalishi kama wameungama makosa yao kwetu au la.—(The Faith I Live By, p. 131) [Pr 239.5; Maombi Aya ya 7]

Katika sala ambayo Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake kulikuwa na ombi: Utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe wale wanaotukosea. Hatuwezi kurudia sala hii kutoka moyoni na kuthubutu kuwa watu tusiosamehe, kwani tunamwomba Bwana atusamehe makosa yetu dhidi Yake kama vile sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Lakini ni wachache wanaotambua umuhimu wa kweli wa sala hii. Ikiwa wale wasiosamehe wangeelewa kina cha maana yake wasingethubutu kuirudia sala hii, na kumwomba MUNGU awashughulikie kama wanavyoshughulika na wanadamu wenzao wafao.—(Testimonies for the Church 3:95). [Pr 240.1; Maombi Aya ya 8]

Tunahitaji kuchunguza mioyo yetu kama matayarisho ya kwenda mbele za MUNGU katika maombi, ili tujue sisi wenyewe tumeshiklia roho ya namna gani. Ikiwa hatutawasamehe wale waliotukosea, maombi yetu ya msamaha hayatasikilizwa. "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu." Sisi kama wadhambi tunapokaribia Kiti cha Rehema, hatuwezi kueleza hisia ya ombi hili bila kuwa na msamaha moyoni mwetu kwa wale wote ambao wametuumiza. Juu ya ombi hili Yesu anatoa maelezo: “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na

Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.” (The Signs of the Times, August 21, 1884) [Pr 240.2; Maombi Aya ya 9]

Kuongama Lazima Kuwe Mahususi (taja jambo lile kwa jina lake, bainisha dhambi gani unayoizungumzia)—maungamo ya kweli daima ni ya tabia maalum, na hukiri dhambi fulani. Yanaweza kuwa ya namna ya kuletwa mbele za MUNGU tu na sio kwa binadamu wengi, yanaweza kuwa makosa ambayo yanapaswa kuongama mbele ya watu ambao wameumizwa majereraha kupitia kwazo, au yanaweza kuwa ya aina ya jumla ambayo yanapaswa kujulikana katika kusanyiko la watu. Lakini maungamo yote yanapaswa kuwa mahususi na mtu anapasa kwenda kwenye pointi/kipengele, yakikiri dhambi zote ambazo una hatia nazo.—(Testimonies for the Church 5:639) [Pr 240.3; Maombi Aya ya 10]

Yesu Anasikia Ombi Rahisi la Msamaha—Sio lazima kwamba wote wataweza kubainisha kwa uhakika wakati dhambi zao ziliposamehewa. Somo la kufundishwa kwa watoto ni kwamba dhambi na makosa yao yanapaswa kuletwa kwa Yesu katika maisha yao ya utotoni. Wafundishe watoto kuomba msamaha Wake kila siku kwa kosa lolote walilofanya, na kwamba Yesu anasikia sala rahisi ya moyo uliotubu na wenye huzuni, Naye atasamehe, na kuyapokea, kama vile alivyowapokea watoto walioletwa Kwake alipokuwa duniani.—(Child Guidance, 494, 495) [Pr 241.1; Maombi Aya ya 11]

Kisha, watoto, njooni kwa Yesu. Mpe MUNGU sadaka ya thamani kuliko zote uwezavyo kutoa; mpe moyo wako. Yeye Anazungumza nawe akisema, “Mwanangu, binti yangu, Nipe moyo wako. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, nitazifanya nyeupe kama theluji; kwa maana nitawatakasa kwa damu Yangu Mwenyewe. Nitawafanya ninyi wanachama wa familia Yangu— watoto wa Mfalme wa mbinguni. Pokeeni msamaha Wangu, Amani Yangu ninayowapa ninyi bure. Nitawavika ninyi kwa haki Yangu, vazi la harusi, na kuwafanya mstahili karamu ya harusi ya Mwana- Kondoo. Mnapovikwa haki Yangu, kwa maombi, kwa kukesha, kupitia kujifunza Neno Langu kwa bidii, mtaweza kufikia kiwango cha juu. Mtaelewa Ukweli, na tabia yenu itaundwa/itafinyangwa na ushawishi wa

Bwana; “Ombeni kwa ajili ya Msamaha kwani haya ni mapenzi ya MUNGU, hata kutakaswa kwenu.” (The SDA Bible Commentary 3:1162) [Pr 241.2; Maombi Aya ya 12]

Ni muhimu sana kwamba tunapaswa kuomba ili tupate nguvu kutoka juu ya kuyaona na kuyapinga majaribu ya adui; lakini Shetani hutafuta siku zote kuwazuia watu wasiombe, kwa kuujaza muda wao kwa biashara, pilikapilika au starehe, au kwa kuwaongoza katika uovu wa namna hiyo hata wasiwe na hamu ya kuomba. Bwana Yesu amefanya mbingu ifikike kwa wote wanaoenda Kwake, Naye anawaalika watoto na vijana waje Kwake. Yeye anasema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa MUNGU ni wao.” Yesu angetaka watoto na vijana waje Kwake wakiwa na ujasiri ule ule wanaoenda nao kwa wazazi wao (wema). Kama vile mtoto anavyomuomba mama yake au baba yake chakula akiwa na njaa, ndivyo Bwana anavyotaka ninyi muombe kile mnachohitaji. Ikiwa dhambi zako ni nzito juu ya moyo wako, unapaswa kwenda kwa MUNGU na kusema, “Kwa ajili ya Masihi, nisamehe dhambi zangu.” Kila sala ya unyofu itasikiwa mbinguni, na kila ombi la dhati na bidii la neema na nguvu litajibiwa.—(The Youth’s Instructor, July 7, 1892) [Pr 241.3; Maombi Aya ya 13]

Ombi la Msamaha Lazima Lionyeshwe Kuwa la Unyofu (litoke moyoni)— “Usinitenge na uso Wako, wala usimwondoe Roho Wako Mtakatifu.” Toba pamoja na msamaha ni zawadi ya MUNGU kupitia Masihi. Ni kupitia ushawishi wa Roho Mtakatifu ndipo tunasadikishwa kuhusu dhambi, na kuhisi hitaji letu la msamaha. Hakuna wanaosamehewa isipokuwa wale walio na moyo uliopondeka; lakini ni neema ya Bwana ifanyayo moyo kutubu. Yeye Anafahamu udhaifu na mapungufu yetu wote, Naye atatusaidia. Yeye Atasikia maombi ya imani; lakini unyofu wa sala unaweza kuthibitishwa tu kwa jitihada zetu za kujileta kwenye mapatano na kile kiwango kikuu cha maadili ambacho kitapima tabia ya kila mtu (Amri Zake Kumi). Tunahitaji kufungua mioyo yetu kwa ajili ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, na kupata uzoefu wa nguvu Zake zinazobadilisha.—(The Review and Herald, June 24, 1884) [Pr 242.1; Maombi Aya ya 14]

“Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa,” Kwa nini hatumwendei

MUNGU kwa Neno Lake? kuomba na kupokea vimeunganishwa pamoja kwa ukaribu. Ikiwa utaomba kwa imani mambo ambayo MUNGU ameahidi, wewe utapokea. Mwangalie Yesu kwa ajili ya mambo unayohitaji. Mwombe msamaha wa dhambi, na unapoomba kwa imani moyo wako utalainishwa(mwororo), na utawasamehe wale waliokuumiza, na maombi yako yatakwenda kwa MUNGU yakiwa na harufu nzuri ya upendo. Pamoja na kuomba huja kukesha katika maombi, na kila wazo na neno na tendo vitaambatana kwa mapatano na ombi lako la dhati kwa ajili ya matengenezo katika maisha. Maombi ya imani huleta matunda yanayoendana na imani yetu stahiki. Lakini kutamka aina ya maneno tu kwa desturi, bila unyofu na matamano ya dhati kwa msaada, bila kutarajia utapokea, haitakufaa kitu, itakuwa ni kazi bure tu. Mwombaji wa namna hii asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Wale wanaokuja kwa MUNGU lazima waamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba Yeye ni mtoa thawabu kwa wale wanaomtafuta kwa bidii.—(The Review and Herald, March 28, 1912) [Pr 242.2; Maombi Aya ya 15]

SURA YA 24

MAOMBI YA KUOMBEA WENGINE- MAOMBEZI (intercessory prayer)

Waombeeni Wengine—Hebu na tujitahidi kutembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. Bwana aligeuza kifungo/kongwa Ayubu alipoomba, si kwa ajili yake tu, bali kwa ajili ya wale waliokuwa wakimpinga. Wakati Alipohisi kutamani sana kwamba roho zilizomkosea zipate kusaidiwa, yeye mwenyewe alipata msaada. Hebu na tuombe, sio kwa ajili yetu tu, bali kwa wale ambao wametuumiza, na wanaoendelea kutuumiza. Omba, omba, hasa akilini mwako (moyoni). Usimpe Bwana pumziko; kwa maana masikio Yake Yako wazi ili kusikia maombi yenye unyofu, yasichoka na yenye kusihi, wakati nafsi inaponyenyekwa/inapojidhili mbele Zake.— (The SDA Bible Commentary 3:1141) [Pr 244.1; Maombi Aya ya 1]

Unapaswa kuwa wakala ambaye kupitia Kwake MUNGU atazungumza na Roho. Mambo ya thamani yataletwa kwenye kumbukumbu yako, wewe utakumbushwa, na kwa moyo unaofurika kwa upendo wa Yesu, utazungumza Maneno ya kupendeza, yenye maslahi muhimu. Usahili wako na unyofu wako utakuwa umbuji/ufasaha wa hali ya juu zaidi, na maneno yako yataandikwa katika vitabu vya mbinguni kuwa maneno yanayofaa, ambayo ni kama matunda/tufaha za dhahabu katika picha za fedha. MUNGU atayafanya kuwa mafuriko ya uponyaji ya mvuto wa mbinguni, yakiamsha kusadikishwa na shauku, na Yesu ataongeza maombezi Yake kwenye maombi yako, na kudai kwa ajili ya mwenye dhambi zawadi ya Roho Mtakatifu, na kuimwaga juu ya nafsi yake. Na kutakuwa na shangwe mbele ya malaika wa MUNGU kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja anayetubu.— (Sons and Daughters of God, 274) [Pr 244.2; Maombi Aya ya 2]

Kuna wale wanaokuzunguka ambao wana huzuni, ambao wanahitaji maneno ya huruma, upendo, na nyororo/laini, na maombi yetu ya unyenyekevu, yenye kuonyesha sikitiko. — (Testimonies for the Church 3:530) [Pr 245.1; Maombi Aya ya 3]

Katika kumwita MUNGU Baba yetu, tunatambua watoto Wake wote kama ndugu zetu. Sisi sote ni sehemu ya mtandao mkuu wa ubinadamu, sote ni washiriki wa familia moja. Katika maombi yetu tunapaswa kujumuisha majirani zetu na sisi wenyewe. Hakuna anayeomba kwa njia ifaayo ambaye anajitafutia baraka yake peke yake tu-kwaajili yake binafsi tu.— (Sons and Daughters of God, 267) [Pr 245.2; Maombi Aya ya 4]

Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho katika maombi yetu, mioyo yetu itapatwa na ushawishi wa kuhuisha wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu yatang'aa zaidi kwa jitihada za Bwana; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa ya kweli na halisi zaidi, yenye bidii zaidi, na ya kusali zaidi. - (Christ Object Lessons, 354). [Pr 245.3; Maombi Aya ya 5]

Kuna nafsi ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, uwaombee. Kuna wale wanaohitaji Mkate wa Uzima. Wasomee kutoka katika Neno la MUNGU. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri inayoweza kuugusa, hakuna dawa

inayoweza kuponya. Waombe hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote, Kristo atakuwepo kufanya mguso wenye ushawishi katika mioyo ya wanadamu.— (Welfare Ministry, 71) [Pr 245.4; Maombi Aya ya 6]

Hebu wale walio wa kiroho wazungumze na nafsi hizi. Omba nao na kwa ajili yao. Hebu muda mwingi utumike katika maombi na kulichunguza Neno kwa karibu. Hebu wote wapate mambo ya halisi na ya kweli ya imani katika nafsi zao wenyewe kwa njia ya imani kwamba Roho Mtakatifu atakamwagwa kwao kwa sababu wana njaa na kiu ya Kweli ya haki.— (Testimonies for the Church 6:65). [Pr 245.5; Maombi Aya ya 7]

Wakati Ubinafsi unapokufa, kutakuwa na uamsho wa hamu kubwa kuhusiana na wokovu wa wengine, - matamania ambayo yatasababisha juhudi za kudumu na zenye uvumilivu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na dua ya dhati, zizsiochoka, maombi ya kudumu, yataingia mbinguni kwa ajili ya nafsi zinazoangamia.—(Gospel Workers, 470). [Pr 246.1; Maombi Aya ya 8]

Oh jamani! kama sala ya dhati na a imani zingetokezea kila mahali, “Nipe roho zilizoziwa sasa kwenye uchafu wa makosa, la sivyo nife! Nawe zilete nafsi hizi kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu.—(This Day With God, 171). [Pr 246.2; Maombi Aya ya 9]

Anzeni kuombea roho; njooni karibu na Kristo, karibu na ubavu Wake unavuwa damu. Hebu roho ya upole na utulivu iwapambe maisha yenu, Hebu maombi yenu ya dhati na bidii, yaliyopondeka, ya unyenyekevu yapande Kwake kwa ajili ya hekima ili mpate kufanikiwa katika kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na nafsi za wengine.— Testimonies for the Church 1 :513) [Pr 246.3; Maombi Aya ya 10]

Kuna wengi ambao matumaini yamewatoka. Warudishie mwanga wa jua hawa. Wengi wamepoteza ujasiri wao. Zungumza nao maneno ya furaha na ya kuwachangamsha. Omba kwa ajili yao.—(Prophets and Kings, 719) [Pr 246.4; Maombi Aya ya 11]

Nafsi zinapaswa kutafutwa, kuombewa, kufanyiwa kazi. Rufaa za kusihi kwa dhati zinapaswa kufanywa. Maombi ya dhati yanapaswa kutolewa. Maombi yetu dhaifu, yasiyo na roho yanapaswa kubadilishwa kuwa maombi ya dhati,

matamano, imani na bidii sana.—(Testimonies for the Church 7:12). [Pr 246.5; Maombi Aya ya 12]

Kazi hii inakuhitaji uzilinde roho kama yule ambaye lazima utazitolea hesabu siku ya hukumu. Upole wa Kristo lazima ujaze moyo wa Mtendakazi kwa Sala ya Maombezi. Ikiwa una upendo kwa roho utaonyesha kujali kwa dhati kwa ajili yao. Utatoa maombi ya unyenyekevu, ya dhati, ya kutoka moyoni kwa wale unaowatembelea. Harufu ya upendo wa Kristo itadhihirishwa katika kazi yako. Yeye ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu atashirikiana na mtenda kazi asiye na uchoyo au ubinafsi kuweka msukumo juu ya mioyo ya wanadamu.— (Testimonies for the Church 6:75, 76) [Pr 246.6; Maombi Aya ya 13]

Hebu na tuufanyie kazi mpango huu, na tuombeane, tukipelekana moja kwa moja katika uwepo wa MUNGU kwa imani iliyo hai.—(The Review and Herald, August 28, 1888) [Pr 247.1; Maombi Aya ya 14]

Omba Upate Baraka Ili Kuwabariki Wengine—Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi ya uchoyo au ubinafsi, kwa faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. “Kwa ajili yao,” Bwana alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, “Najiweka wakfu, ili nao watakaswe.” Yohana 17:19. Kujitoka huko huko, kujitolea nafsi kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao uliodhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake.

Utume au misheni yetu kwa ulimwengu sio kujitumikia wenyewe, au kujifurahisha au kujipendeza wenyewe; tunapaswa kumtukuzwa MUNGU kwa kushirikiana Naye katikakuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasilisha kwa wengine. Uwezo wa kupokea huhifadhiwa kwa kutoa tu (tunapokea tu tukitoka). Hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasilisha na kuwasiliana na wale wanaotuzunguka.— (Christ's Object Lessons, 142, 143) [Pr 247.2; Maombi Aya ya 15]

Tunapomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” tunaomba kwa ajili ya wengine na pia sisi wenyewe. Na tunakubali kwamba kile ambacho MUNGU anatupa si kwa

ajili yetu wenyewe tu. Hakika MUNGU hutukabidhi sisi kama amana, ili tuwalishe wenye njaa.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 111, 112) [Pr 247.3; Maombi Aya ya 16]

Waombee Wengine Katika Ombi la faragha—Katika ombi la faragha wote wana fursa ya kuomba kwa kadiri wapendavyo na kuwa wazi wapendavyo. Wanaweza kuomba kwa ajili ya jamaa na marafiki zao wote. Chumbani, yaani mahali popote pa faragha ulipo wewe mwenyewe (closet), ndipo mahali pa kueleza shida zao zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo binafsi au siri za moyoni.— (Testimonies for the Church 2:578) [Pr 247.4; Maombi Aya ya 17]

Ombea Wale Wanaohubiri na Kuhudumu—Miongoni mwa watu wa MUNGU kunapaswa kuwa na misimu ya mara kwa mara ya maombi ya dhati na ya bidii. Akili inapaswa kuwa katika mkao/mtazamo wa maombi kwa kiasi kikubwa. Nyumbani na kanisani hebu kuwe na maombi ya dhati na bidii na yatolewe kwa niaba ya wale ambao wamejitoa katika kuhubiri Neno.—(In Heavenly Places, 87) [Pr 247.3; Maombi Aya ya 18]

Wakati vijana wanapoenda kuhubiri Ukweli, mnapaswa kuwa na majira ya maombi kwa ajili yao. Omba kwamba MUNGU awaunganishe na Yeye Mwenyewe na awape hekima, neema, na maarifa. Ombeni ili waweze kulindwa na mitego ya Shetani iliyojificha na kuwekwa safi katika mawazo na utakatifu wa moyo. Ninawasihi ninyi mnaomcha Bwana, msipoteze wakati katika mazungumzo yasiyofaa, yasinufaisha au katika kazi isiyo na maana, ili kujipatia kiburi, au kuridhisha tamaa ya chakula kwa ulafi au ya mwili. Hebu wakati unaopatikana utumike katika kupambana mieleka na MUNGU kwa ajili ya wachungaji/wahudumu wenu. Inueni mikono yao kama Haruni na Huri walivyoifanya mikono ya Musa.— (Testimonies for the Church 5:162) [Pr 248.1; Maombi Aya ya 19]

Omba kwa ajili ya Vijana wa Kanisa — Hebu wale walio wazee katika uzoefu waangalie vijana; na wanapowaona wakijaribiwa, wawachukue kando, na waombe nao na kwa

ajili yao. —(Messages to Young People, 18). [Pr 248.2; Maombi Aya ya 20]

Walimu wa Shule ya Sabato Ombeeni Washiriki wa Darasa Lenu—Kama wafanyakazi wa MUNGU tunahitaji zaidi kuwa kama Yesu na kupunguza ubinafsi-Ndani yetu awe Yesu zaidi na ubinafsi utokomee. Tunapaswa kuwa na mzigo zaidi kwa ajili ya nafsi, na tunapaswa kuomba kila siku kwamba nguvu na hekima ziweze kutolewa kwa ajili ya Sabato. Waalimu, kutaneni na madarasa yenu. Ombeni pamoja nayo, na uwafundishe wanafunzi jinsi ya kuomba. Hebu moyo ulainishwe, na maombi yawe mafupi na sahili, lakini ya dhati, usadikisho na bidii.—(Counsels on Sabbath School Work, 125) [Pr 248.3; Maombi Aya ya 21]

Wanafunzi waombe kwaajili ya Walimu-Wanafunzi wanapaswa kuwa na nyakati zao za maombi, ambapo wanaweza kutoa maombi ya kudumu, marahisi ili MUNGU ambariki Kiongozi wa shule kwa nguvu za mwili, akili timamu, nguvu ya maadili, na utambuzi wa kiroho, na kwamba kila mwalimu awe na stahiki/sifa kwa neema ya MUNGU za kufanya kazi yake. — (Fundamentals of Christian Education, 293) [Pr 248.4; Maombi Aya ya 22]

Omba kwa ajili ya Wakristo Wenzako—Mara nyingi sana tunasahau kwamba watenda kazi wenzetu wanahitaji nguvu, kushangiliwa na kutiwa moyo, furaha na uchangamfu. Katika nyakati za wasiwasi fulani na mzigo, kuweni makini kuwahakikishia wenzenu kujali kwenu na huruma. Wakati mnapojaribu kuwasaidia kwa maombi yenu, wajulishe kwamba mnafanya hivyo. Muambatanishe ujumbe wa MUNGU kwa watendakazi Wake: “Iweni hodari na moyo wa ushujaa.” Yoshua 1:6.—(Testimonies for the Church 7:185) [Pr 249.1; Maombi Aya ya 23]

Wazazi wawaombe Watoto Wao—MUNGU ameahidi kuwapa hekima wale wanaoomba kwa imani, Naye Atafanya kama vile Yeye alivyosema. Yeye Anapendezwa na imani inayomuendea kupitia Neno Lake. Mama Augustine aliomba kwa ajili ya uongofu wa mwanaye. Hakuona ushahidi wowote kwamba Roho wa MUNGU alikuwa akiushawishi moyo wake, lakini hakuvunjika moyo. Aliweka kidole chake kwenye maandiko, akiwasilisha mbele za MUNGU Maneno Yake Mwenyewe, na kusihi kama mama awezavyo kusihi. Kujidhili kwake kwa dhati, kusihi kwake

kwa bidii bila ya kuchoka, imani yake isiyoyumbayumba, ilishinda, na Bwana akampa haja ya moyo wake. Yeye Yuko tayari kusikiliza maombi ya watu Wake, hata hivi leo. “Mkono Wake si mfupi hata usiweze kuokoa wala sikio Lake si zito hata lisiweze kusikia”; na wazazi Wakristo wakimtafuta kwa bidii, Yeye atajaza vinywa vyao hoja, na, kwa ajili ya Jina Lake, atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili yao katika wongofu wa/kwa watoto wao.— (Testimonies for the Church 5:322, 323. [Pr 249.2; Maombi Aya ya 24]

Tunapaswa kuomba kwa MUNGU zaidi ya tunavyoomba. Kuna nguvu nyingi na baraka katika kuomba pamoja katika familia zetu, kuomba pamoja na watoto wetu na pia kuwaombea tukiwa wenyewe.—(Child Guidance, 525). [Pr 249.3; Maombi Aya ya 25]

Hebu Kristo akupatie mkono Wake wa msaada ili kutekeleza makusudi Yake. Kwa maombi unaweza kupata uzoefu ambao utafanya huduma yako kwa watoto wako iwe na mafanikio kamili.— (Child Guidance, 69) [Pr 249.4; Maombi Aya ya 26]

Haukuona kuwa ni kazi ngumu au mzigo ikiwa njia ingefunguka ili uweze kuwatunza watoto wako na kuwakinga kutokana na uovu ulioenea katika zama hizi za ulimwengu. Ulikuwa mzigo wa moyo wako kuwaona wao wakimgeukia Bwana. Uliomba mbele za MUNGU kwa ajili ya watoto wako kwa vilio vikali na machozi. Ulitamani sana uongofu wao. Wakati fulani moyo wako ulikata tamaa na kuzimia, na ukaogopa kwamba maombi yako yasingejibiwa; lakini ukawaweka tena wakfu watoto wako kwa MUNGU upya, na moyo wako wenye matamano makali, ukawaweka juu ya madhabahu tena. [Pr 249.4; Maombi Aya ya 27]

Walipoingia jeshini, maombi yako yaliwafuata. Walihifadhiwa kwa ajabu dhidi ya madhara. Wao waliita kuwa ni ‘bahati yao nzuri’; lakini maombi ya mama kutoka kwenye nafsi yenye wasiwasi, fadhaa, yenye kulemewa na mzigo, alipohisi hatari ya watoto wake na hatari ya kukatiliwa mbali katika ujana wao bila tumaini kwa MUNGU yalikuwa na mengi ya kufanya juu ya kuhifadhiwa kwao. Ni maombi mangapi yaliingia mbinguni ili wana hawa wahifadhiwe ili wamtii MUNGU, na kisha wayatoe maisha yao kwa utukufu Wake! Katika mahangaiko yako kwa ajili ya watoto wako ulimsihi MUNGU awarudishe kwako tena,

na ulitafuta kwa bidii zaidi kuwaongoza katika njia ya utakatifu.—(Testimonies for the Church 2:274, 275) [Pr 250.1; Maombi Aya ya 28]

Yeye [MUNGU] hatakataa kusikia maombi ya dhati na bidii ya wazazi, ambayo yanaungwa mkono na bidii ya kudumu, ili watoto wao wapate baraka kutoka Kwake, na kuwa watendakazi waaminifu katika kazi Yake. Wazazi wanapofanya wajibu wao kwa njia iliyowekwa na MUNGU, wanaweza kuwa na uhakika kwamba maombi yao ya msaada Wake katika kazi yao ya nyumbani yatakubaliwa.— (The Signs of the Times, May 4, 1888) [Pr 250.2; Maombi Aya ya 29]

Kesha kila wakati ili kukata mkondo na kurudisha nyuma uzito wa uovu ambao Shetani anausukuma juu ya watoto wako. Watoto hawawezi kufanya hili wenyewe. Wazazi wanaweza kufanya mengi. Kwa ombi la dhati na bidii na imani iliyo hai, ushindi mkubwa utapatikana.—(Spiritual Gifts 4b, 139) [Pr 250.3; Maombi Aya ya 30]

Ili mzazi afanye kazi yake inavyopaswa kufanywa, kunahitajika talanta na ustadi na uvumilivu wenye umakini mkubwa. Inahitaji kutojiamini nafsi na kuomba kwa bidii. Hebu kila mama na ajitahidi kwa bidii katika kutimiza wajibu wake. Hebu awalete watoto wake wadogo kwa Yesu kwa mikono ya imani, akimwambia Yeye hitaji lake kubwa, na kuomba hekima na neema.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 128) [Pr 250.4; Maombi Aya ya 31]

Juhudi zenye bidii na zenye maumivu, maombi na imani, vikiunganishwa na mfano sahihi, havitakosa matunda. Walete watoto wako kwa MUNGU kwa imani, na utafute kushawishi akili zao kupata hisia ya wajibu wao kwa Baba yao wa mbinguni.— (Temperance, 157, 158) [Pr 251.1; Maombi Aya ya 32]

Usitarajie badiliko lifanyike kwa watoto wako pasipo subira, kazi ya dhati, iliyochanganyika na maombi ya bidii. Kusoma na kuelewa tabia zao mbalimbali/anuwai, na siku baada ya siku kuwafinyanga kulingana na Kielelezo cha Bwana, ni kazi inayohitaji bidii kubwa na ustahimilivu, na maombi mengi, pamoja na imani yenye kudumu katika ahadi za MUNGU.— (The Signs of the Times, May. 4, 1888) [Pr 251.2; Maombi Aya ya 33]

Hata mtoto mchanga mikononi mwa mama yake anaweza kukaa chini ya uvuli wa Mwenyezi kwa imani ya mama anayeomba. - (The Desire of Ages, 512) [Pr 251.3; Maombi Aya ya 34]

Akina baba na akina mama, je, hamtashikilia kazi yenu kwa nguvu, uvumilivu, na upendo? Panda mbegu ya thamani kila siku, kwa maombi ya dhati ili MUNGU aimwagilie kwa umande wa neema, na kukupa mavuno mengi sana. Mwana wa MUNGU alikufa ili kukomboa jamii ya ubinadamu yenye dhambi na iliyoasi. Je, basi, sisi tujiepushe na taabu, kujitoa mhanga au dhabihu yoyote ili kuokoa watoto wetu wapendwa?—(The Signs of the Times, November 24, 1881) [Pr 251.4; Maombi Aya ya 35]

Baada ya kufanya wajibu wako kwa uaminifu kwa watoto wako, basi wabebe na uwapeleke kwa MUNGU na umwombe akusaidie. Mwambie kwamba umetimiza sehemu yako ya Sala ya Maombezi, kisha kwa imani umwombe MUNGU afanye sehemu Yake, ambayo wewe hauwezi kuifanya.—(Child Guidance, 256) [Pr 251.5; Maombi Aya ya 36]

SURA YA 25

MALAIKA NA MAOMBI

Malaika Huweka katika kumbukumbu Kila Ombi la Dhati— Tunapaswa kumfahamu MUNGU sasa kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika huweka katika rekodi, kila ombi ambalo ni la dhati, usadikisho na lenye bidii. Afadhali tutupilie mbali kuuridhisha ubinafsi kuliko kupuuza ushirika na MUNGU. Umaskini mkubwa zaidi, kujikana zaidi pamoja na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, wadhifa, urahisi wa maisha, na urafiki bila kibali Chake Bwana. Ni lazima tuwe na muda wa kuomba (tutenge muda kuomba). (The Great Controversy, 622) [Pr 252.1; Maombi Aya ya 1]

Hebu malaika wanaotunza kumbukumbu waandike historia ya mapambano matakatifu na migogoro ya watu wa MUNGU, hebu na waandike maombi yao na machozi; lakini hebu MUNGU asidharauliwe kwa madai kutoka katika midomo ya wanadamu, inayotangaza, “Mimi sina dhambi. Mimi ni mtakatifu.” Midomo iliyotakaswa haitatamka kamwe maneno hayo yenye imani bandia, kiburi na dhana potofu isiyo na kibali cha Mungu (presumptuous prayer).— (The Signs of the Times, May 23, 1895) [Pr 252.2; Maombi Aya ya 2]

Malaika Wanaweza Kusikia Maombi yetu— kama wanadamu wangeweza kuona kwa maono ya mbinguni, basi wangeona makundi ya malaika walio na nguvu nyingi zaidi wakiwa na wale ambao wameshika Neno la subira ya Kristo. Kwa huruma nyororo, malaika wameshuhudia dhiki yao na wamesikia maombi yao. Pr 252.3; Maombi Aya ya 3]

Malaika Hupeleka Maombi yetu Mbinguni—Familia iliyo na nidhamu nzuri, inayompenda na kumtii MUNGU, itakuwa na furaha na uchangamfu. Baba anaporudi kutoka katika kazi yake ya kila siku, hataleta mashaka, fadhaa, mkanganyiko au misongo yake nyumbani kwake. Atahisi

kuwa nyumba, na mzunguko wa familia, ni vitakatifu sana kiasi kwamba haviwezi kuharibiwa na fadhaa zisizoleta furaha au zinazoleta huzuni. Baba huyu alipoondoka nyumbani kwake, hakumuacha nyuma Mwokozi wake na dini yake. Vyote viwili vilikuwa katika ushirika naye. Ushawishi mzuri wa nyumba yake, baraka ya mke wake, na upendo wa watoto wake, vinafanya mizigo yake kuwa miepesi; na anarudi akiwa na amani moyoni mwake, na maneno ya uchangamfu, yenye kutia moyo kwa mke wake na watoto, ambao wanangoja kwa shangwe kukaribisha ujio wake. Anapoinama pamoja na familia yake kwenye madhabahu ya sala ili kutoa shukrani zake kwa MUNGU kwa ajili ya utunzaji Wake kwake pamoja na wapendwa wake siku nzima, malaika wa MUNGU wanakuwa kwenye chumba hicho wakizunguka-zunguka, na kubeba maombi ya shauku na bidii ya wazazi wanaomcha MUNGU mbinguni, kama uvumba mzuri, ambao hujibiwa kwa baraka zinazorudi.—(Selected Messages 2:439, 440) [Pr 253.1; Maombi Aya ya 4]

Malaika husikia sifa zinazotolewa na ombi la imani, na hupeleka maombi kwa Yeye ambaye huhudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na kuombea wema na haki Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli humshikilia Mweza wa yote, na huwapa wanadamu ushindi. kwa kupiga magoti yake, Mkristo hupata nguvu za kukinzana na kupingana na vishawishi.—(The Review and Herald, February 1, 1912) [Pr 253.2; Maombi Aya ya 5]

MUNGU hawaachi watoto Wake wapotovu walio dhaifu katika imani, na wanaofanya makosa mengi. Bwana husikiliza na kusikia maombi yao na ushuhuda wao. Wale wanaomtazama Yesu siku kwa siku na saa kwa saa, wanaokesha kwa maombi, wanavutwa na kumkaribia Yesu. Malaika walio na mbawa zilizochanuliwa hungoja kupeleka sala zao za toba kwa MUNGU, na kuzisajili katika vitabu vya mbinguni.—(The SDA Bible Commentary 4:1184) [Pr 253.3; Maombi Aya ya 6]

Malaika Hungoja Kujibu Maombi Yetu—Mara nyingi katika kujali watu wanaoteseka/wagonjwa, uangalifu mwingi unatolewa juu ya mambo madogomadogo, huku hitaji la wagonjwa la zile Kweli zote kuu za wokovu wa injili, ambazo zitahudumu kwenye roho na mwili, zimesahaulika. Unapopuuza kuwaombea wagonjwa, wewe unawanyima baraka kubwa; kwa maana malaika wa MUNGU

wanangoja kuhudumu kwenye nafsi hizi katika kuitikia maombi yako.—(Medical Ministry, 195) [Pr 253.4; Maombi Aya ya 7]

Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja; na baba, au mama wakati baba hayupo, anapaswa kumwomba MUNGU kwa ari na bidii ili awahifadhi kwa siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu (kwa Bwana), kwa moyo mwororo, na kwa hisia ya majaribu na hatari mbele zinazowazunguka ninyi na watoto wenu; kwa imani uwafunge juu ya madhabahu, na kuwaombea utunzaji wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamewekwa wakfu kwa namna hiyo na MUNGU.—(Child Guidance, 519) [Pr 254.1; Maombi Aya ya 8]

Malaika Mahsusni Huteuliwa Kujibu Maombi—Viumbe wa Mbinguni wameteuliwa kujibu maombi ya wale wanaofanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya maslahi ya kazi ya MUNGU. Malaika wa juu kabisa katika nyua za mbinguni wameteuliwa kufanyia kazi maombi ambayo hupanda kwa MUNGU kwa ajili ya kuendeleza kazi ya MUNGU. Kila malaika ana kituo cha kazi na wadhifa wake maalum wa kazi, ambapo haruhusiwi kuondoka kwenda mahali pengine popote. Kama angeondoka, nguvu za giza zingepata mpenyo na faida... [Pr 254.2; Maombi Aya ya 9]

Siku baada ya siku, mzozo/vita kati ya wema na uovu unaendelea. Kwa nini wale ambao wamepata fursa nyingi na manufaa hawatambui uzito mkubwa wa kazi hii? Wanapaswa kutumia akili katika suala hili. MUNGU Ndiye Mtawala. Kwa uweza Wake mkuu Yeye huwadhiti na kuwaongoza watawala wa kidunia. Kupitia mawakala Wake, Yeye Anafanya kazi ambayo iliamriwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. [Pr 254.3; Maombi Aya ya 10]

Kama binadamu hatuelewi jinsi tunavyopaswa kuelewa lile pambano kuu linaloendelea kati ya mashirika yasiyoonekana, pambano kati ya malaika waaminifu na wasio waaminifu. Malaika waovu wanafanya kazi kila mara, wakipanga safu yao ya mashambulizi, wakitawala kama makamanda, wafalme, na viongozi, wa majeshi ya wanadamu wasio waaminifu.....Ninatoa wito kwa wahudumu wa Kristo kushinikiza nyumbani juu ya uelewa wa wote wanaoweza kufikiwa na sauti zao, Ukweli wa

huduma ya malaika. Msijiingize katika dhana za kufikirika zinazopendezesha moyo. Neno lililoandikwa ndio usalama wetu pekee. Ni lazima tuombe kama Danieli, ili tulindwe na akili za mbinguni (wakazi wa mbinguni). Kama roho watumikao, malaika hutumwa kuwahudumia wale watakaorithi wokovu. Ombeni, ndugu zangu, ombeni kuliko mlivyowahi kuomba kabla. Sisi hatuko tayari kwa ajili ya ujio wa Bwana. Tunahitaji kufanya kazi kamilifu, ya kinagaubaga, kwa ajili ya umilele.—(The SDA Bible Commentary 4:1173) [Pr 254.4; Maombi Aya ya 11]

MUNGU ameweka malaika wanaofanya mapenzi yake, kujibu maombi ya wanyenyekevu wa dunia, na kuwaongoza watumishi Wake kwa ushauri na maamuzi. Mawakala wa mbinguni wanatafuta kila mara kutoa neema na nguvu na ushauri kwa watoto waaminifu wa MUNGU, ili waweze kutenda sehemu yao katika kazi ya kuwasilisha nuru kwa ulimwengu.—(Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 484) [Pr 255.1; Maombi Aya ya 12]

Malaika wanaohudumu wanangojea karibu na kiti cha enzi kutii mara moja agizo la Yesu Kristo la kujibu kila ombi linalotolewa kwa imani hai ya dhati na iliyo ya bidii.—(Selected Messages 2:377) [Pr 255.2; Maombi Aya ya 13]

Oh! Laiti sote tungeweza kutambua ukaribu wa mbingu na dunia! Watoto waliozaliwa duniani hawalijui hili, kwamba wana malaika wa nuru kama wenzi na walinzi wao; kwa maana wajumbe wa mbinguni wanatumwa kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Shahidi wa siri, aliye kimya hulinda kila nafsi inayoishi, akitafuta kushinda na kuivuta kwa Kristo. Malaika hawamwachi kamwe yule anayejaribiwa kuwa mawindo kwa adui ambaye ataangamiza roho za watu ikiwa ataruhusiwa kufanya hivyo. Maadamu kuna tumaini, mpaka watakapompinga Roho Mtakatifu kwa uharibifu wao wa milele, wanadamu wanalindwa na walinzi wa mbinguni. [Pr 255.3; Maombi Aya ya 14]

Oh jamani! Kama wote wangeweza kumwona Mwokozi wetu wa thamani kama alivyo, Mkombozi wetu. Hebu mkono Wake uweke kando pazia ambalo huficha utukufu Wake dhidi ya macho yetu. Ndipo Yeye atakapoonekana katika mahali Pake pa juu na Patakatifu. Je! Sisi tunaona nini? Mwokozi wetu, si katika hali ya ukimya na kutotenda.

Akiwa amezungukwa na viumbe wa mbinguni wenye utashi (malaika), makerubi, na maserafi, elfu kumi mara elfu kumi ya malaika. Viumbe hawa wote wa mbinguni wana kitu kimoja juu ya vingine vyote, ambacho wanapendezwa nacho sana –kanisa Lake katika ulimwengu wa uharibifu. Wanafanya kazi kwa ajili ya Kristo chini ya agizo Lake, ili kuwaokoa kabisa wale wote wamtazamao na kuamini ndani Yake. [Pr 255.4 15]

Malaika wa mbinguni huagizwa kuwatazama kondoo wa malisho ya Kristo. Wakati Shetani akiwa na mitego yake yenye udanganyifu ambayo angewapotosha ikiwezekana hata wale wateule, malaika hawa walianzisha mkakati/operesheni ambayo itaokoa roho zilizojaribiwa ikiwa watalitii Neno la Bwana, watambue hatari yao, na kusema, “La, sitaingia katika mpango huo wa Shetani. Nina Ndugu yangu mkubwa kwenye kiti cha enzi mbinguni, ambaye ameonyesha kwamba ana nia ya upole na wema kwangu, na sitauhuzunisha moyo Wake wa upendo.” [Pr 256.1; Maombi Aya ya 16]

Tukiwa tunaishi katikati ya nguvu hizi zinazopingana (uovu na wema), kupitia kuizoesha imani yetu na maombi, tunaweza kuita msafara wa malaika wa mbinguni kuja upande wetu na kutusindikiza, na hao watatulinda dhidi ya kila ushawishi wenye uovu.— (Our High Calling, 23.) [Pr 256.2; Maombi Aya ya 17]

Malaika Huzingatia na Kuyatia Alama maombi yetu, Kisha Hutoa Msaada—Unapoamka asubuhi, Je! unahisi kutokuwa na uwezo kwako, na uhitaji wako wa nguvu kutoka kwa MUNGU? Na je, wewe humjulisha Baba yako wa mbinguni mambo unayotaka kwa unyenyekevu na wasema haya kutoka moyoni? Ikiwa ni hivyo, Malaika huzingatia maombi yako, na kuyawekea alama, na ikiwa maombi haya hayakutoka katika midomo ya kujifanya/feki, unapokuwa katika hatari ya kufanya makosa bila kujua, na kusukuma ushawishi ambao utawaongoza wengine kufanya maovu, malaika wako mlezi/mlinzi atakuwa upande wako, kukuelekeza kwenye njia bora zaidi, kukuchagulia maneno yako, na kuathiri/kushawishi matendo yako. [Pr 256.3; Maombi Aya ya 18]

Ikiwa hauhisi hatari yoyote, na ikiwa haufanyi maombi ya msaa na nguvu ya kupinga vishawishi, hakika

utapotea; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile mbaya ya hukumu. - (Testimonies for the Church 3: 363, 364) [Pr 256.4; Maombi Aya ya 19]

MUNGU Hutuma majeshi ya Malaika wa Kuthibiti na Kutusaidia Katika Kujibu maombi—Ikiwa Shetani anaona kwamba yuko katika hatari ya kupoteza nafsi moja, atajitahidi kadiri ya uwezo wake wote kuishikilia/kuihifadhi hiyo nafsi moja. Na mtu huyo anapoamshwa kwenye hatari yake, na, kwa dhiki na bidii, akamtazama Yesu ili kupata nguvu, Shetani anaogopa kwamba atampoteza mfungwa, naye anaita majeshi ya malaika zake kudhibiti mambo na kuifunga roho hiyo maskini, na kuunda ukuta wa giza kumzunguka, ili nuru ya mbinguni isimfikie. Lakini ikiwa yule aliye hatarini anavumilia, na katika hali ya kutokuwa na uwezo wake akijidondosha na kujisalimisha juu ya wema wa damu ya Kristo, Mwokozi wetu husikiliza ombi la dhati la imani, na kutuma jeshi la ziada la wale malaika wenye uwezo mkubwa ili kumkomboa. Shetani hawezi kuvumilia kuona mpinzani wake Mwenye nguvu anategemewa na kusihiwa wakati wa hii dharura. Majeshi ya malaika waovu kwani anaogopa na kutetemeka mbele ya nguvu na ukuu Wake. Kwa sauti ya ombi la bidii, jeshi zima la Shetani hutetemeka. Anaendelea kuita majeshi ya malaika waovu ili kutimiza lengo lake. Na wakati malaika, wenye uwezo uliosheheni wa nguvu tele, waliovikwa silaha nzito za mbinguni, wanapokuja kusaidia nafsi iliyozimia, inayofuatiliwa kama mawindo, Shetani na jeshi lake wanarudi nyuma, wakijua vema kwamba wameshindwa katika vita yao. Raia walio chini ya Shetani kwa mapenzi yao (mapepo), ni watenda kazi hodari, na wameunganishwa katika kitu kimoja. Na ingawa wanachukiana na kupigana wao kwa wao, bado wanaboresha kila fursa ili kuendeleza misheni yao inayowafanya wawe pamoja. Lakini Kamanda Mkuu wa mbinguni na duniani amewekea mipaka nguvu za Shetani.- (Testimonies for the Church 1:345, 346) [Pr 256.5; Maombi Aya ya 20]

Ulinzi wa jeshi la mbinguni umetolewa kwa wanadamu wote ambao watafanya kazi katika njia za MUNGU na kufuata mipango Yake. Tunaweza katika ombi la dhati, la

toba na moyo uliopondeka, kuwaita wasaidizi wa mbinguni upande wetu. Majeshi yasiyoonekana ya nuru na yenye nguvu yatafanya kazi pamoja na watu wanyenyekevu, wapole, wale wa hali ya chini na wanaojishusha.— (Selected Messages 1:97) [Pr 257.1; Maombi Aya ya 21]

Niliona baadhi, wakiwa na imani yenye nguvu na vilio vya uchungu, wakimsihi MUNGU. Nyuso zao zilikuwa zimedhoofu na zilikuwa na wasiwasi mwingi, zikionyesha mapambano yaliyo ndani yao. Uthabiti na bidii kubwa ilionyeshwa katika nyuso zao; matone makubwa ya jasho yakaanguka kutoka kwenye vipaji vya nyuso zao. Nyuso zao ziling'aa hapa na pale kwa alama za kibali cha MUNGU, na tena ule mwonekano wa umakini mzito wa dhati, na wa wasiwasi ukaja tena juu yao. [Pr 257.2; Maombi Aya ya 22]

Malaika waovu waliwasonga na kuwazunguka, wakitandaza giza juu yao, na kulishinikiza kwa watu, ili kumzinga Yesu asionekane kwa wanadamu, ili macho yao yavutwe kwenye giza lililowazunguka, na hivyo kuongozwa kutomwamini MUNGU na kumnung'unikia. Usalama wao pekee ulikuwa katika kuelekeza macho yao juu. Malaika wa MUNGU walikuwa na mamlaka juu ya watu Wake, na anga lililojawa sumu ya malaika waovu liliposogezwa karibu na hawa wenye wasiwasi, malaika wa mbinguni walikuwa wakipepea mbawa zao juu yao ili kulitawanya giza nene. [Pr 257.3; Maombi Aya ya 23]

Waombaji walipokuwa wakiendelea na kilio chao cha dhati, nyakati fulani mwali wa nuru ya Yesu uliwajia, ili kutia moyo mioyo yao na kuangaza nyuso zao. Baadhi, niliwaona, hawakushiriki katika kazi hii ya kulia kwa uchungu na kusihi. Walionekana kutozingatia na kutojali. Hawakuwa wakipinga giza lililowazunguka, nalo liliwafunga kama wingu zito. Malaika wa MUNGU waliwaacha hawa na kwenda kusaidia wale walio na bidii ya dhati, wanaosali. Niliona malaika wa MUNGU wakiharakisha kuwasaidia wale wote waliokuwa wakihangaika kwa uwezo wao wote, kuwapinga malaika waovu na kujaribu kujisaidia wenyewe kwa kumwita MUNGU kwa ustahimilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakufanya jitihada yoyote ya kujisaidia, nao wakapotea katika upeo wa macho yangu.—(Early Writings, 269, 270) [Pr 258.1; Maombi Aya ya 24]

Maombi Marefu Huwachosha Malaika—Mazungumzo marefu yenye kujirudia-rudia kama mashairi, yanayochosha watu (yanayoboa), yasiyo na umuhimu na sala ndefu havifai mahali popote, na hasa kwenye mikutano ya halaiki. Huwachosha malaika pamoja na watu wanaowasikiliza. Maombi yetu yanapaswa kuwa mafupi, na yanayogusa dhima moja kwa moja -yanalenga pointi au hoja moja kwa moja, na siyo kuzunguka.—(The Review and Herald, October 10, 1882) [Pr 258.2; Maombi Aya ya 25]

Malaika Watatufundisha Jinsi ya Kuomba—Washiriki wa Kanisa, vijana kwa wazee, wanapaswa kuelimishwa ili kwenda kutangaza ujumbe huu wa mwisho kwa ulimwengu. Wakienda kwa unyenyekevu, malaika wa MUNGU watakwenda pamoja nao, wakiwafundisha jinsi ya kuinua sauti katika sala, jinsi ya kuinua sauti katika nyimbo, na jinsi ya kutangaza ujumbe wa injili kwa ajili ya wakati huu. — (Messages to Young People , 217) [Pr 258.3; Maombi Aya ya 26]

Malaika Hushangaa Kwamba Wanadamu Huomba Kidogo Sana—Je, Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini juu ya wanadamu dhaifu wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo una matamano nao, tayari kuwapa zaidi ya wawezavyo kuomba au kufikiria, na bado wanaomba kidogo sana, na wana imani ndogo sana? (Efeso 3:20). Malaika hupenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona ushirika na MUNGU kuwa furaha yao kuu; na bado watoto wa dunia, ambao wanahitaji sana msaada ambao MUNGU pekee Ndiye anayeweza kutoa, wanaonekana kutosheka kutembea bila nuru ya Roho Wake na ushirika wa uwepo Wake.—(Steps to Christ, 94) [Pr 258.4; Maombi Aya ya 27]

SURA YA 26

MAOMBI BANDIA

Usimkaribie MUNGU kwa Mazoea, Bila Kuweka Umakini, katika Maombi (lightly)—Unyenyekevu na uchaji Mungu, vinapaswa kuujenga mwenendo wa wote wanaoenda mbele za MUNGU. Katika Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele Zake kwa ujasiri, lakini hatupaswi kumkaribia kwa ujasiri bandia, kinyume cha mapenzi Yake Yeye, au kwa dhana zetu potofu na kiburi (presumptuous), kana kwamba Yeye Yuko sawa na sisi. Kuna wale wanaozungumza na MUNGU Mkuu na Mwenye uwezo wote, na mtakatifu, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kufikiwa, kama ambavyo wangezungumza na mtu aliye sawa nao, au hata kama wanavyozungumza na yule wanayefikiria ni duni kwao. Kuna wale wanaoenenda au kutenda katika nyumba Yake jinsi wasivyoweza kufanya katika chumba cha kumwona mtawala wa kidunia. Hawa wanapaswa kukumbuka kwamba wako mbele za macho Yake ambapo maserafi wanaabudu, ambapo mbele Yake malaika hufunika nyuso zao.—(Patriarchs and Prophets, 252) [Pr 259.1; Maombi Aya ya 1]

Maombi ya Unafiki—Maombi yanayotolewa kwa MUNGU ili kumwambia unyonge, uchafu na upotofu wetu wote, wakati hatujisikii kutofaa au unyonge wetu hata kidogo, ni maombi ya unafiki. Ni maombi ya moyo uliopondeka pekee ndiyo ambayo Bwana anajali. “Kwa maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele, ambaye Jina Lake ni Mtakatifu, asema hivi; Mimi nakaa mahali palipoinuka, palipo patakatifu, tena pamoja naye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.” [Pr 259.2; Maombi Aya ya 2]

Maombi hayakusudii kufanya mabadiliko yoyote kwa MUNGU; ila yanatuleta sisi katika mapatano na MUNGU. Maombi hayachukui mahali pa wajibu.—(Messages to Young People, 247, 248) [Pr 260.1; Maombi Aya ya 3]

Maombi Yanayoleta Kivuli Mwanana— Kuna baadhi, nina wasiwasi, ambao hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, bali wanazirundika kwa ajili ya mkutano wa maombi, na kisha huko huyafyatua maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji

wa mikutano na wauaji wa maombi. Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao baridi, yaliyoganda na shuhuda ndefu, za kurudi nyuma kwao zinatia watu kivuli. Wote hufurahi wanapomaliza, na ni vigumu kukung'uta ubaridi unaotetemesha na giza ambalo maombi na kuamrisha kwao katika dua kunaleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimepokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii, na sio mirefu sana. Kujiweka mbali na watu (kutokuwa na moyo wa kirafiki), kiburi, ubatili, na hofu kwa mwanadamu vinapaswa kuachwa nyumbani. Tofauti ndogo na chuki havipaswi kubebwa nasi kwenye mikutano hii. Tunapaswa kuwa kama familia iliyoungana, usahili, utulivu, upole, ujasiri, na upendo vinapaswa kuwepo katika mioyo ya akina kaka na akina dada wanaokutana ili kufanywa upya na kutiwa nguvu kwa kuleta taa/mwangaza wao pamoja.— Testimonies for the Church 2:578, 579) [Pr 260.2; Maombi Aya ya 4]

Kutarajia Kwamba Maombi Yetu Yatajibiwa Daima Kwa Njia ile Tunayotaka Ni Kujiamini Kupita Kiasi, dhana ambayo Mungu haiungi mkono (Presumption)— Maombi ya Imani hayapotei kamwe; lakini kudai kuwa yatajibiwa kila wakati kwa njia ile ile na kwa jambo fulani maalum ambalo tumetarajia, ni dhana ambayo haina kibali cha Mungu, yaani imani bandia, ni kudhania kwamba Mungu atakuunga mkono katika lile unalotaka tu (wengine wameifafanua kama kiburi au imani bandia).(Testimonies for the Church 1:231) [Pr 260.3; Maombi Aya ya 5]

Maombi yetu yanapoonekana kutojibiwa, tunapaswa kung'angania ahadi; kwani wakati wa kujiliwa hakika utakuja, na tutapokea baraka tunazohitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa njia ile ile na kwa jambo fulani maalumu tunalolitamani, ni dhana ambayo haina kibali cha Mungu, (au kiburi na imani bandia). MUNGU ni Mwenye hekima sana hata asiweze kukosea, na ni mwema sana hata asiweze kuwanyima kitu chochote kizuri wale waendao kwa unyofu. Basi msiogope kumwamini, ijapokuwa hamuoni jawabu la haraka la maombi yenu. Tegemea ahadi Yake ya hakika, “Ombeni, nanyi mtapewa.” (Steps to Christ, 96) [Pr 260.4; Maombi Aya ya 6]

Maombi ndani Yake pekee, Hayana thawabu ya kuosha Dhambi—Wapagani waliona maombi yao kama

ndani yake yenyewe yana kustahili na kuwa yana sifa na haki ya upatanisho wa dhambi ndani yao. Kwa hiyo kadiri maombi yanavyozidi kuwa marefu ndivyo ubora na haki yao inavyokuwa kubwa zaidi. Ikiwa wangepoteza kuwa watakatifu kwa juhudi zao wenyewe wangepoteza na kitu ndani yao cha kufurahia, naam, sababu fulani ya kujigamba. Wazo hili kwamba sala ni utimilifu wa kanuni ya utakaso lipo kwenye msingi wa mifumo yote ya dini za uwongo. Mafarisayo walikuwa wameiga wazo hili la kipagani la sala, na halijapotea hata kidogo katika siku zetu, hata miongoni mwa wale wanaodai kuwa Wakristo. Kurudiwa kwa seti za misemo iliyozeleka kama destruri au mapokeo, wakati moyo hauhisi hitaji/haja ya MUNGU, ni tabia sawa na ile ya "kupayuka maneno mengi bure na kuyarudia rudia" kama wapagani (Mathayo 6:7). [Pr 261.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi si utakaso wa dhambi; hayana haki wala sifa ndani yake yenyewe. Maneno yote ya madoido tunayoweza kuyatoa yaliyo ndani ya amri yetu hayapatani na haja takatifu. Maombi yenye ufasaha zaidi ikiwa hayaonyeshi hisia za kweli za moyo ni kazi bure tu. Lakini maombi yatokayo katika moyo wa dhati na bidii, pale mahitaji ya nafsi yanapowasilishwa, kama vile ambavyo tungemwomba rafiki wa kidunia atupe msaada wake, tukitarajia kuupokea—haya ndiyo maombi ya imani. MUNGU hataki kumsifia kwetu kwa sherehe au kaida za maonyesho, ila Yeye anataka kilio kisichotamkwa cha moyo uliovunjika na kutiishwa na hisia ya dhambi ya huo na udhaifu mkubwa hupata njia Yake kwa Baba wa rehema zote.—(Thoughts from the Mount of Blessing, 86, 87) [Pr 261.2; Maombi Aya ya 8]

Maombi Sio Ushahidi wa Kuongoka Ikiwa Maisha Hayajabadilishwa—Shetani huwaongoza watu kufikiri kwamba kwa sababu wamehisi unyakuo wa hisia, basi wao wameongoka. Lakini uzoefu wao haujabadilika. Matendo yao ni sawa na hapo awali. Maisha yao hayaonyeshi matunda mazuri. Wanaomba mara kwa mara na kwa muda mrefu, na daima wanarejelea hisia walizokuwa nazo nyakati fulani-fulani. Lakini hawaishi maisha mapya. Hawa wamedanganyika. Uzoefu wao hauzami ndani zaidi kuliko hisia zao. Wanajenga juu ya mchanga, na upepo mkali unapokuja, nyumba yao inafagiliwa mbali. [Pr 261.3; Maombi Aya ya 9]

Nafsi dhaifu za walio wengi zinapapasa gizani, zikitafuta hisia ambazo wengine wanasema wamekuwa nazo katika uzoefu wao. Wanapuuza Ukweli kwamba mwumini katika Kristo lazima aifanyie kazi wokovu wake mwenyewe kwa hofu na kutetemeka. Mwenye dhambi aliyesadikishwa ana jambo la kufanya. Ni lazima atubu na aonyeshe imani ya kweli. [Pr 262.1; Maombi Aya ya 10]

Wakati Yesu anapozungumza juu ya moyo mpya, anamaanisha akili, utu wote, nafsi yote na mtindo wa maisha (mind set and deeds). Kuwa na badiliko la moyo ni kuondoa mapenzi kutoka katika ulimwengu, na kuyafunga kwa Kristo. Kuwa na moyo mpya ni kuwa na akili mpya, makusudio mapya, nia mpya. Ni nini ishara ya moyo mpya? —Maisha yaliyobadilika. Kila siku, kila saa kuna kufa kwa ubinafsi, uchoyo na kiburi.—(Messages to Young People, 71,72) [Pr 262.2; Maombi Aya ya 11]

Maombi Hayachukui Nafasi ya Utiifu—Wanaume na wanawake, katika kukabili amri chanya zaidi za MUNGU, hufuata mwelekeo wao wenyewe, na kisha kuthubutu kuliombea jambo hilo, ili kumshawishi MUNGU ili akubali kuwaruhusu kwenda kinyume na mapenzi Yake Mwenyewe aliyoyasema. MUNGU hapendezwi na maombi hayo. Shetani anakuja upande wao, kama alivyofanya kwa Hawa katika Edeni, na kuwavutia, nao wanapata mguso fulani akilini, na hilo wanasimulia kuwa tukio la ajabu sana ambalo Bwana amewapa.— (The Review and Herald, July. 27, 1886) [Pr 262.3; Maombi Aya ya 12]

Ushirika na MUNGU huipa nafsi ujuzi wa ndani wa mapenzi Yake. Lakini wengi wanaokiri imani hawajui uongofu wa Kweli ni nini. Hawana uzoefu katika ushirika na Baba kwa njia ya Yesu Kristo, na hawajawahi kuhisi nguvu ya neema ya Bwana ya kutakasa moyo. Huomba na kutenda dhambi, hutenda dhambi na kuomba, maisha yao yamejaa uovu, ubaya, udanganyifu, hila, husuda, wivu, kijicho na kujipenda wenyewe. Maombi ya tabaka hili ni chukizo kwa MUNGU. Maombi ya kweli hushirikisha nguvu za roho na huathiri maisha. Yeye anayemimina mahitaji yake mbele za MUNGU anahisi utupu wa kila kitu kilicho chini ya mbingu.—(Testimonies for the Church 4:534, 535) [Pr 262.4; Maombi Aya ya 13]

Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi kamwe hayawezi kuchukua nafasi ya wajibu. “Mkinipenda,” Kristo asema, “mtazishika amri zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” Yohana 14:15, 21. Wale wanaoleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai Ahadi Yake huku hawatimizi masharti, wanamtukana Yehova. Wanaoleta Jina la Masihi kama mamlaka yao kwa ajili ya utimilifu wa ahadi, ila hawafanyi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake.— (Christ's Object Lessons, 143) [Pr 263.1; Maombi Aya ya 14]

Kuomba ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Jicho la imani litamtambua MUNGU Kwa Ukaribu sana, na mwombaji anaweza kupata uthibitisho wenye thamani wa upendo na utunzaji wa Bwana kwake. Lakini kwa nini basi maombi mengi sana hayajibiwi? Anasema Daudi: “Nilimlilia kwa kinywa changu, Naye alitukuzwa na ulimi wangu. Nikiuangalia uovu moyoni mwangu, Bwana hatanisikia.” kupitia nabii mwingine Bwana anatupa ahadi: “Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.” Tena, anazungumza kuhusu wengine ambao “hawajanililia kwa mioyo yao.” Maombi kama hayo ni maombi ya mazoea ni mfano tu, ibada ya midomo tu, ambayo Bwana hakubali.— (Testimonies for the Church 4:533) [Pr 263.2; Maombi Aya ya 15]

Maombi ya Haraka, Ya Nyakati Fulani tu Si Ushirika Halisi na MUNGU—Mbingu haijafungwa dhidi ya maombi ya bidii ya wenye haki. Eliya alikuwa mwanadamu mwenye hisia kama sisi, lakini Bwana alisikia na akajibu maombi yake kwa njia ya kushangaza zaidi. Sababu pekee ya kukosa kwetu nguvu na MUNGU inapatikana ndani yetu wenyewe. Ikiwa maisha ya ndani ya wengi wanaokiri Ukweli yangewasilishwa mbele yao, basi wasingedai kuwa wao ni Wakristo. Hawakui katika neema. Ombi la haraka linatolewa hapa na pale, lakini hakuna ushirika wa kweli na MUNGU. [Pr 263.3; Maombi Aya ya 16]

Ni lazima tudumu sana katika maombi ikiwa tunakusudia kufanya maendeleo katika maisha ya Kiungu/mbingu. Ujumbe wa kweli ulipotangazwa kwa mara ya kwanza, tuliomba sana. Ni mara ngapi sauti ya maombezi ilisikika

chumbani, ghalani, kwenye miti ya bustani, na kwenye vijisitu au shambani. Mara kwa mara tulitumia saa nyingi katika maombi ya dharti na bidii, wawili au watatu pamoja tukidai ahadi; mara nyingi sauti ya kilio ilisikika na kisha sauti ya shukrani na wimbo wa sifa.—(Testimonies for the Church 5:161, 162) [Pr 263.4; Maombi Aya ya 17]

MUNGU Huchukia Maombi ya Wenye Ubinafsi—Niliona kwamba kulikuwa na watu kama Yuda Iskariote miongoni mwa wale wanaodai kuwa wanamngoja Bwana wao. Shetani anawadhibiti, lakini wao hawajui. MUNGU hawezi kuridhia hata kiwango kidogo cha tamaa au ubinafsi, na Yeye Anachukia maombi na dua za kuamrisha za wale wanaoendekeza katika tabia hizi ovu. Shetani anavyoona kwamba wakati wake ni mfupi, huwaongoza wanadamu kuwa wachoyo, wabinafsi na wenye tamaa zaidi na zaidi, na kisha hujiinua kwa kujitutukuza, anapowaona watu wakiwa wamejifungia ndani yao wenyewe (wanajifikiria wenyewe), ni bahili wa kutupwa, masikini wa roho, wasio na faida, wachoyo, na wenye ubinafsi. Ikiwa macho ya hao yangefumbuliwa, wangemwona Shetani akiwa anashangilia ushindi wa kuzimu, akishangilia juu yao na kuucheka upumbavu wa wale wanaokubali madokezo yake na kuingia katika mitego yake.— (Early Writings, 268) [Pr 264.1; Maombi Aya ya 18]

Maombi Makavu, Malegevu Hayamsaidii Mtu yeyote—Kanisa linahitaji uzoefu mpya (freshi), na hai wa washiriki ambao wamekuwa na mazoea ya ushirika na MUNGU. Ushuhuda mkavu, uliochakaa, uliousu/kuchacha (stale) na maombi bila udhihirisho wa Kristo ndani yake, havina msaada kwa watu. Ikiwa kila mtu anayedai kuwa mtoto wa MUNGU angejazwa na imani na nuru na uzima, ni ushahidi wa ajabu jinsi gani ungetolewa kwa wale wanaokuja ili kusikia ile Kweli! Je, ni roho ngapi zingeweza kuokolewa kwa Kristo!—(Testimonies for the Church 6:64) [Pr 264.2; Maombi Aya ya 19]

Hazina zote za mbinguni zilikabidhiwa kwa Yesu Kristo, ili aweze kutoa karama hizi za thamani kwa mtafutaji mwenye bidii, mwadilifu na aliye mvumilivu. Yeye “Amemfanya Yeye kuwa hekima yetu, haki yetu na utakaso na ukombozi.” 1 Wakorintho 1:30. Lakini hata maombi ya wengi ni yale ya urasmi, yasiyo na moyo au jotojoto, ya

mazoea, makavu na ya kwenda na ratiba tu (rasmi), kiasi kwamba hayana ushawishi wowote kwa ajili ya wema. Haya sio manukato au harufu iletayo uzima (2Wakorintho 2:16). [Pr 264.3; Maombi Aya ya 20]

Ikiwa walimu wangenyenyekeza mioyo yao mbele za MUNGU na kutambua jukumu ambalo wamekubali katika kuwasimamia vijana wakiwa kwa lengo la kuwaelimisha kwa ajili ya maisha yajayo ya umilele, badiliko kubwa lingeonkana upesi katika mtazamo wao. Maombi yao yasingekuwa makavu na yasiyo na uhai, bali wangeomba kwa dhati, usadikisho na bidii kwaajili ya nafsi zinazohisi hatari zao.— (Counsels to Parents, Teachers, and Students, 371, 372) [Pr 265.1; Maombi Aya ya 21]

Onyo Juu ya Maombi Ambayo Yana ubinafsi kama Kiini Chake—Maombi yetu kwa MUNGU hayapaswi kutoka katika mioyo iliyojaa matamano binafsi. MUNGU anatusihi tuchague karama ambazo zitaongezeka kwaa utukufu Wake. Yeye Angetaka tuchague ya mbinguni badala ya yale ya duniani. Yeye Anatufungulia na kutudhihirishia mbele zetu uwezekano na manufaa ya uchumi wa mbinguni, kununua vile vya mbinguni. Yeye Anatia moyo malengo yetu ya juu zaidi, usalama katika hazina yetu iliyo bora zaidi. Wakati mali ya kidunia itafagiliwa mbali, muumini atafurahi katika hazina yake ya mbinguni, utajiri ambao hauwezi kupotea katika maafa yoyote ya kidunia. — (Sons and Daughters of God, 188) [Pr 265.2; Maombi Aya ya 22]

Maombi ya Kweli na ya Bandia Yalinganishwa—Yule mtoza ushuru maskini aliyeomba, “MUNGU unirehemu mimi mwenye dhambi” (Luka 18:13), alijiona kuwa mtu mwovu sana, na wengine walimtazama katika nuru hiyo hiyo; lakini mtu huyu alihisi hitaji lake, na kwa mzigo wake wa hatia na aibu alienda mbele ya MUNGU, akiomba rehema Yake. Moyo wake ulikuwa wazi kwa ajili ya Roho wa MUNGU kufanya kazi Yake ya ukarimu na neema na hivyo kumweka huru dhidi ya nguvu za dhambi. Ombi la farisayo la kujigamba, la kujihesabia haki lilionyesha kwamba moyo wake ulikuwa umefungwa na kufuli dhidi ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Kwa sababu ya umbali wake kutoka kwa MUNGU, hakuwa na hisia ya unajisi wake mwenyewe, alikuwa tofauti na ukamilifu wa utakatifu wa Bwana. Yeye hakuona hitaji/uhitaji, naye hakupokea

chochote.—(Steps to Christ, 30, 31) [Pr 265.3; Maombi Aya ya 23]

Kuna aina mbili za maombi - maombi ya mazoea, kwaajili kutimiza wajibu tu au mfano tu na maombi ya imani. Kurudiwa kwa seti za sentensi zilizozoeleka, wakati moyo hauhisi haja ya MUNGU, ni maombi ya urasmi, yale ya kutimiza wajibu au kuendana na ratiba tu, maombi yasiyo na moyo au joto ndani, kukariri maneno fulani rasmi....Tunapaswa kuzingatia sana katika maombi yetu yote kunena matakwa ya moyo na kusema kile tunachomaanisha tu. Maneno yote ya madoido mengi ambayo yamo kwenye uwezo wetu kutoa, hayalingani na shauku moja takatifu. Maombi yenye ufasaha zaidi huwa ni maneno ya kupayuka-payuka kwa kurudia-rudia tu yale ambayo yamekaririwa, nayo hayaonyeshi hisia za kweli za moyo bali ni makavu, yenye kutimiza wajibu, na kuendana na ratiba ya urasmi (formal prayers). Lakini maombi yatokayo katika moyo mnyofu, pale matakwa rahisi ya nafsi yanapoonyeshwa kama ambavyo tungeomba upendeleo kwa rafiki wa duniani, tukitazamia kwamba tutapewa—hili ndilo ombi la imani. Mtoza ushuru aliyepanda kwenda hekaluni kuomba ni kielelezo kizuri cha mwumini mnyoofu, aliyejitoa kikamilifu. Alihisi kwamba alikuwa mtenda-dhambi, na uhitaji wake mkubwa ulipelekea mlipuko wa tamanio lenye shauku, “MUNGU unirehemu mimi mwenye dhambi.”— (My Life Today, 19) [Pr 265.4; Maombi Aya ya 24]

Imesemwa juu ya Kristo: "Na akiwa katika dhiki, Aliomba kwa bidii zaidi." ni tofauti ya jinsi gani kuhusu maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni na unapolinganisha na maombi duni, yasiyo na moyo ambayo hutolewa na wanadamu kwa MUNGU. Wengi wameridhika na maudhui ya midomo (huduma za mdomo tu, maneno matupu bila matendo au moyo ndani yake), na ni wachache walio na hamu ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU. [Pr 266.1; Maombi Aya ya 25]

Ushirika na MUNGU huipa nafsi ujuzi wa ndani wa mapenzi Yake. Lakini wengi wanaokiri imani hawajui uongofu wa kweli ni nini. Hawana uzoefu katika ushirika na Baba kwa njia ya Yesu Kristo, na hawajawahi kuhisi nguvu ya neema ya Mungu inayotakasa moyo. Huomba na kutenda dhambi, hutenda dhambi na kuomba, maisha yao yamejaa

udanganyifu, hila, husuda, chuki, wivu, na kujipenda wenyewe. Maombi ya tabaka hili ni chukizo kwa MUNGU. Maombi ya Kweli hushirikisha nguvu za roho na huathiri maisha. Yeye anayemimina mahitaji yake mbele za MUNGU anahisi ubatili na utupu wa kila kitu chini ya mbingu. “Shauku yangu yote i mbele Zako,” akasema Daudi, “na kuugua kwangu hakufichiki Kwako.” “Nafsi yangu ina kiu ya MUNGU, MUNGU Aliye hai, ni lini nitakuja nionekane mbele za MUNGU?” “Ninapokumbuka mambo haya, naimimina nafsi yangu iliyo ndani yangu.”—(Testimonies for the Church 4:534, 535) [Pr 266.2; Maombi Aya ya 26]

SURA YA 27

SHETANI NA MAOMBI

Shetani Anajaribu Kuziba njia ili Maombi yetu Yasimfikie MUNGU—Giza la yule mwovu linawafunika wale wanaopuuzia kuomba. Majaribu yanayonong’onwa na adui yanawavuta watu hao kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatunii upendeleo ambao MUNGU amewapa katika miadi mitakatifu Naye, kupitia Maombi. Kwa nini basi wana na binti za MUNGU wawe wenye kusitasita au kutotaka kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za hazina za mbinguni, ambako kunatunzwa rasilimali zenye thamani isiyo na kikomo, za Yule ambaye ni Mweza wa yote? Bila maombi na kukesha daima kwa uadilifu tuko katika hatari ya kuongeza kutojali na kukengeuka kutoka katika njia iliyo sawa/sahihi. Adui anatafuta daima kuifunga njia ya kuelekea kwenye Kiti cha Rehema, ili tukileta maombi ya dhati na imani tusipate neema na uwezo wa kuyapinga majaribu.— (Steps to Christ, 94, 95) [Pr 267.1; Maombi Aya ya 1]

Kuna nguvu kuu katika maombi. Adui wetu mkuu anatafuta daima anaendelea kuiweka nafsi inayopitia dhoruba, mbali na MUNGU. Ombi la kwenda mbinguni la yule mtakatifu, aliye mnyenyekevu zaidi ndilo linaloogopwa zaidi na Shetani kuliko sheria za bunge na mamlaka ya wafalme.— (The SDA Bible Commentary 2:1008) [Pr 267.2; Maombi Aya ya 2]

Adui huwazuia wengi wenu msiombe, kwa kuwaambia kwamba hamhisi roho ya maombezi ndani yenu, na kwamba ingefaa mngoje mpaka roho ya maombezi iwajie ili maombi yenu yasije yakawa ni dhihaka. Lakini unapaswa kumwambia Shetani, "Imeandikwa" kwamba "wanadamu wanapaswa kuomba siku zote, na wala wasizimie." Tunapaswa kuomba mpaka tuwe na mzigo wa mahitaji yetu juu ya nafsi zetu; na tukivumilia tutapata. Bwana atatuajaza Roho Wake Mtakatifu. Bwana anajua, na Ibilisi anajua, kwamba sisi wanadamu hatuwezi kupinga majaribu ya Shetani bila nguvu kutoka juu. Kwa sababu hii yule mwovu anatafuta kutuzuia tusimshike Yeye aliye na uwezo Mkuu wa kuokoa. Bwana wetu alifanya hili kuwa ni wajibu wetu, pamoja na upendeleo wetu, kuunganisha udhaifu wetu sisi wanadamu tunaokufa, ujinga wetu, hitaji letu, pamoja na hekima Yake, Haki Yake na nguvu Zake. Yeye anaunganisha uwezo Wake usio na kikomo na juhudi za viumbe wenye ukomo, ili wawe zaidi ya washindi katika vita na adui wa nafsi zao. [Pr 268.1; Maombi Aya ya 3]

Hebu mwanadamu yeyote asivunjike moyo, maana Yesu Yu hai ili atumbee. Kuna mbingu ya kujipatia/kuingia, na jehanamu ya kutoroka, na Kristo anapendezwa na ustawi wetu (maslahi yetu). Yeye Atawasaidia wale wote wamwitao. Ni lazima tuchanganye imani na maombi yetu yote. Hatuwezi kumshusha Kristo chini, lakini, kupitia njia ya imani, sisi tunaweza kujiinua wenyewe hadi tukawa na umoja na mapatanao, na mshikamano kwa kiwango kamili cha haki. Tuna adui mdanganyifu wa kukutana naye na kumshinda, lakini twaweza kufanya hivyo katika Jina la Yule Mmoja Mwenye Nguvu zote.—(The Review and Herald, October 30, 1888) [Pr 268.2; Maombi Aya ya 4]

Usiruhusu Mapendekezo ya Shetani yakuzuie Kuomba
— Hatupaswi kutindikiwa/kulemewa sana na mawazo ya dhambi na makosa yetu kiasi cha kuacha kuomba. Wengine hutambua udhaifu wao mkuu na dhambi, na kukata tamaa. Shetani anaweka kivuli chake cheusi kati yao na Bwana Yesu, ambaye Ndiye dhabihu yao ya upatanisho. Wanasema, Haina faida kwangu kuomba. Maombi yangu yamechanganyika na mawazo maovu kiasi kwamba Bwana hatayasikia. [Pr 268.3; Maombi Aya ya 5]

Mapendekezo haya yanatoka kwa Shetani. Katika ubinadamu Wake Kristo alikutana na kupinga jaribu hili, na

Yeye Anajua jinsi ya kuwasaidia wale wanaojaribiwa hivyo. Kwa niaba yetu, “ Yeye alitoa maombi na dua pamoja na kilio kikuu na machozi” (Waebrania 5:7). [Pr 268.4; Maombi Aya ya 6]

Wengi, bila kuelewa kwamba mashaka yao yanatoka kwa Shetani, wanakata tamaa na kuzimia na kisha kushindwa katika pambano hilo. Usiache kuomba kwa sababu mawazo yako ni maovu. Kama tungeweza kwa hekima na nguvu zetu kuomba ipasavyo, tungeweza pia kuishi sawa, na hivyo tusingehitaji dhabihu ya upatanisho. Lakini kutokamilika kupo juu ya ubinadamu wote. Ielimishe, izoeze na kufundisha akili yako, ili uweze kumwambia Bwana kwa usahili/urahisi kile unachohitaji. Unapotoa maombi yako kwa MUNGU, ukitaifuta msamaha wa dhambi, angahewa ya usafi wa moyo na takatifu zaidi itaizunguka nafsi yako.—(In Heavenly Places, 78) [Pr 269.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi yanafadhaisha na kupumbaza Juhudi Zenye Nguvu Zaidi za Shetani—Mwanadamu ni mateka wa Shetani na kwa asili ana mwelekeo wa kufuata mapendekezo yake na kutenda maagizo/matakwa yake yule mwovu. Yeye mwenyewe ndani yake hana uwezo wa kumpinga mwovu na kumsukumilia mbali yule uovu. Ni pale tu Kristo atakapokaa ndani yake kwa imani hai, akishawishi matamano yake na kumtia nguvu kwa zile nguvu zitokazo juu, ndipo mwanadamu ataweza kujitosa kumkabili adui huyu wa kutisha sana. Njia nyingine zozote za ulinzi ni bure kabisa. Ni kwa njia ya Kristo pekee ndiyo nguvu za Shetani zinadhibitiwa (zinawekewa mipaka). Huu ni Ukweli mzito (mlima wa ukweli) ambao wote wanapaswa kuelewa kwani unahusu hatima yao. Shetani yupo kazini akishugulika kwa bidii sana (busy) kila dakika, akienda huku na huko, akitembea juu na chini katika nchi, akitaifuta mtu ammeze. Lakini maombi ya dhati na bidii ya imani yatazuia juhudi zake zenye nguvu. Kisha chukueni “ngao ya imani,” ndugu zangu , “ambayo kwayo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.”(Testimonies for the Church 5:294) [Pr 269.2; Maombi Aya ya 8]

Maombi Huzuia Mashambulizi ya Shetani—Maombi hutuunganisha sisi kwa sisi pia pamoja na MUNGU. Maombi humleta Yesu kando yetu, na kuipa roho iliyozimia, iliyofadhaika nguvu mpya ya kuushinda ulimwengu, mwili,

na Ibilisi. Maombi huzuia mashambulizi ya Shetani.—
(Christ's Object Lessons, 250) [Pr 269.3; Maombi Aya ya 9]

Ni lazima tuvae silaha zote za MUNGU na kuwa tayari wakati wowote kwa ajili ya mapambano na nguvu za giza. Majaribu na mitihani vinapotujia, sisi tumwendee MUNGU na tumlilie kwa uchungu katika maombi. Yeye Hatatuambia turudi tukiwa watupu, bila chochote, bali atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui.—(Early Writings, 46) [Pr 269.4; Maombi Aya ya 10]

Shetani Hutetemeka akisikia Sauti ya Maombi—Wakati Shetani anapona kwamba yuko katika hatari ya kupoteza nafsi moja, atajitahidi kadiri ya uwezo wake wote kuihifadhi. Na mtu huyo anapoamshwa kwenye hatari yake, na, kwa dhiki na bidii na usongo, akamtazama Yesu ili kupata nguvu, Shetani anaogopa kwamba atampoteza mateka wake, naye anaita majeshi ya malaika wake ili kuizunguka roho hiyo dhaifu, na kuunda ukuta wa giza kumzunguka, ili nuru ya mbinguni isimfikie. Lakini ikiwa yule aliye hatarini anastahimili bila kuchoka, na katika hali yake ya kutokuwa na uwezo akajisalimisha juu ya wema na sifa za damu ya Kristo, Mwokozi wetu husikiliza ombi la dhati la imani, na kutuma jeshi la wale malaika wenye uwezo mkubwa ili kumkomboa. Shetani hawezi kuvumilia kuona mpinzani wake mwenye nguvu anaitwa/anasihiwa, kwa kuwa anaogopa na kutetemeka mbele ya nguvu za ajabu na ukuu Wake Mwenyezi Mungu. Kwa sauti ya ombi la dhati, jeshi zima la Shetani hutetemeka kama majani, bila kujizuia. Ibilisi huendelea kuita majeshi ya malaika waovu ili kutimiza lengo lake. Na wakati malaika, waliosheheni uwezo*, waliovikwa la silaha za mbinguni, wanapokuja kusaidia nafsi iliyozimia, inayofuatiliwa kama mawindo, Shetani na jeshi lake wanarudi nyuma na kuanguka chini, wakijua vema kwamba wameshindwa katika vita yao. Raia au wafuasi waliojitolea kwa Shetani, (tunaowajua kwa jina kama mapepo) ni waaminifu, watenda kazi wenye bidii, na wameunganishwa katika kusudi lao moja. Na ingawa wanachukiana na kupigana wao kwa wao, huwa wanaboresha kila fursa ili kuendeleza maslahi yao ambayo wote wanaafikiana nayo (kumsikitisha Mungu kwa kumtendea mwanadamu ubaya na ukatili, ni mojawapo ya yale wanavyoafikiana). Lakini Kamanda mkuu mbinguni na duniani amewekea mipaka nguvu za Shetani (*Angels that

excel in strength).- (Testimonies for the Church 1:345, 346) Pr 270.1; Maombi Aya ya 11]

Shetani Anaogopa Maombi ya Mtakatifu Mnyenyekevu Zaidi— Kuna nguvu kuu katika maombi. Adui wetu mkuu anatafuta mara kwa mara kuiweka nafsi yenye shida mbali na MUNGU. Ombi la kwenda mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi huogopwa zaidi na Shetani kuliko maagizo ya mabaraza au maagizo ya wafalme.— (The SDA Bible Commentary 2:1008) Pr 270.2; Maombi Aya ya 12]

Maombi ni Silaha Dhidi ya Shetani—Jihadhari jinsi unavyopuuzwa maombi ya siri na kujifunza Neno la MUNGU. Hizi ni silaha zako dhidi ya yeye ambaye anajitahidi kuzuia safari yako ya kwenda mbinguni. Kupuuza kwa mara ya kwanza maombi na kusoma Biblia hurahisisha upuuziaji wa mara ya pili tena. Kumpinga Roho wa Mungu anapokusihi mara ya kwanza, hutayarisha njia ya upinzani wa pili. Hivyo moyo unafanywa kuwa mgumu, na dhamira inachomwa ili isiwe nyeti.— (Messages to Young People, 96) Pr 270.3; Maombi Aya ya 13]

Maombi Huvunja Mtego uliojificha wa Shetani—Pale tunapohisi kwamba hatujisikii sana kuzungumza na Yesu, basi na tuombe zaidi. Kwa kufanya hivyo tutavunja mtego wa Shetani uliojificha, mawingu ya giza yatatoweka, nasi tutatambua uwepo mzuri wa Yesu.— (Lift Him Up, 372) [Pr 271.1; Maombi Aya ya 14]

Maombi Yanashinda Dhidi ya Shetani—Ombi la imani ndiyo nguvu kuu ya Mkristo, na hakika litashinda dhidi ya Shetani. Ndiyo maana adui anadokeza ushauri kwamba hatuna haja ya maombi. Jina la Yesu, Mwombezi wetu, yeye analichukia sana; na tunapomwendea kwa dhati ili kupata msaada, jeshi la Shetani hufadhaika na kupata mshtuko. Kusudi lake linatimia vyema ikiwa tutapuuzia zoezi la kuomba, kwa maana basi maajabu yake ya uwongo yatapokelewa kwa urahisi zaidi.— (Testimonies for the Church 1:296) [Pr 271.2; Maombi Aya ya 15]

Maombi Ni Muhimu Hasa Katika hali tete na za dharura katika Mapambano Yetu dhidi ya Shetani—Katika pambano na mashirika ya kishetani kuna nyakati za maamuzi ambazo zitaamua ushindi ama kwa upande wa MUNGU au upande wa mtawala wa ulimwengu huu. Ikiwa wale wanaohusika katika vita hii hawako makini na macho

kabisa, wakiweka bidii na umakini/uangalifu, wakiomba kwa dhati hekima, wakikesha katika maombi, ... Shetani ataibuka kama mshindi, wakati angeweza kushindwa na majeshi ya Bwana.....Walinzi waaminifu wa MUNGU hawapaswi kuzipa nguvu za uovu manufaa au mwanya wowote—(The SDA Bible Commentary 6:1094) [Pr 271.3; Maombi Aya ya 16]

Shetani Anakasirishwa na Maombi yenye bidii kubwa— Shetani huwaongoza watu wengi kuamini kwamba maombi kwa MUNGU ni bure na ni desturi tu. Anajua vizuri jinsi kutafakari na kuomba kunavyohitajika ili kuwafanya wafuasi wa Kristo waendeleo kuamshwa usingizini ili kuupinga ujanja na udanganyifu wake. Kwa hila zake hugeza akili kutoka kwenye mazoezi haya muhimu, ili nafsi isiegeme msaada wa Yule Mwenye Nguvu zote, na kupata nguvu kutoka Kwake za kupinga mashambulizi yake. Nilielekezwa kwenye maombi ya bidii na yenye matokeo/matunda ya watu wa MUNGU wa kale. “Eliya alikuwa mtu mwenye tabia kama sisi, naye aliomba kwa bidii.” Danieli alimwomba MUNGU wake mara tatu kwa siku. Shetani anakasirishwa na sauti ya ombi lenye shauku kubwa kwa kuwa anajua kwamba atajipatia hasara kubwa. —(Testimonies for the Church 1:295) [Pr 271.4; Maombi Aya ya 17]

Shetani Hufurahi Maombi yanapohenwa bila kutamkwa kwa Uwazi —Hebu wale wanaoomba na wale wanaotamka wayatamke maneno yao ipasavyo na kusema kwa uwazi, dhahiri, wakibainisha maneno, kwa toni isiyo ya juu au chini sana, au inayobadilika-badilika, yaani sauti iliyo thabiti. Ombi likitolewa ipasavyo, ni nguvu ya wema. Ni mojawapo ya njia mojawapo zinazotumiwa na Bwana kuwajulisha watu hazina za Kweli za thamani. Lakini ombi haliwi linavyopaswa kuwa, kwa sababu ya sauti zenye kasoro za wale wanaolitamka. Shetani anafurahi wakati maombi yanayotolewa kwa MUNGU yanakaribia kutosikika masikioni mwa watu (sauti inakuwa na hitilafu, aidha chini au mtu anakuwa kama anakula jojo au ameinamisha uso chini nk). Hebu watu wa MUNGU wajifunze jinsi ya kusema na kuomba kwa njia ambayo itawakilisha ipasavyo zile Kweli kuu walizonazo. Hebu shuhuda zinazotolewa na sala zinazonenwa viwe wazi na kusikika vyema neno kwa neno.

Na Hivyo MUNGU atatukuzwa.—(Testimonies for the Church 6:382) [Pr 272.1; Maombi Aya ya 18]

Shetani Hujaribu Kutusadikisha Kwamba Kuomba Si Lazima (sala siyo jambo la lazima)— Wazo la kwamba maombi si jambo la lazima, ni mojawapo ya mbinu za Shetani zenye ufanisi zaidi za kuharibu nafsi. Maombi ni ushirika pamoja na MUNGU, Chemchemi ya hekima, Chanzo cha nguvu, na amani, na furaha (Maombi ni kuzungumza na Mungu, na Biblia ni Mungu anazungumza na sisi, vyote Shetani hataki mwanadamu avifikie).—(Child Guidance, 518) [Pr 272.2; Maombi Aya ya 19]

Shetani anaona watumishi wa Bwana wamelemewa mzigo, kwasababu ya giza la kiroho linalowafunika watu. Naye huyasikia maombi yao ya dhati kwa ajili ya neema ya Bwana na uwezo wa kuvunja uchawi wa kukosa shauku na kutojali, uvivu na kutokuwa makini. Akiwa na usongo mpya, anaikobeka sanaa yake. Yeye huwajaribu watu kuendekeza uchu wa tamaa ya chakula au namna nyingine ya tamaa ya mwili ya kujiridhisha, na hivyo kuzifisha hisia zao hata washindwe kusikia mambo yale ambayo wanahitajika sana kujifunza. [Pr 272.3; Maombi Aya ya 20]

Shetani anajua vyema kwamba wote wale ambao yeye anaweza kuwaongoza kwenye kupuuzia maombi na kuyachunguza Maandiko, watatekewa na hivyo kuzidiwa na mashambulizi yake. Kwa hivyo yeye huvumbua kila nyenzo inayowezekana ili kuishugulisha na kuiteka akili. Daima kumewahi kuwa na tabaka la watu wanaokiri kumcha MUNGU, ambao, badala ya kuifuatilia na kuijua ile Kweli, wanaifanya dini yao kuwa ni kutafuta kasoro fulani ya tabia au makosa fulani ya kiimani kwa wale ambao hawakubaliani nao. Hao ndio wasaidizi wa mkono wa kulia wa Shetani. Washitaki wa ndugu si wachache, na daima wapo kibaruanii wakati MUNGU anapofanya kazi na watumishi Wake, wanaomtolea ibada ya Kweli. Wataweka rangi za uwongo juu ya maneno na matendo ya wale wanaoipenda na kuitii ile Kweli. Watawashutumu watumishi wa Kristo walio wanyofu/waaminifu zaidi, wenye bidii na wanaojikana nafsi zao kama waliodanganyika au wadanganyifu. Ni kazi yao kupotosha nia ya kila tendo la Kweli na bora/adhimu, kusambaza maneno ya hiana, na kuibua mashaka katika akili za wale wasio na uzoefu. Kwa kila njia inayowezekana watatafuta

kufanya kile kilicho safi na cha haki au uadilifu, kionekane kuwa najisi, kichafu na cha udanganyifu.—(The Great Controversy, 519) [Pr 273.1; Maombi Aya ya 21]

SURA YA 28

MAOMBI KATIKA SIKU ZA MWISHO

Wale Wanaoishi hasa Katika Siku za Mwisho Wanahitaji Kuomba haswa—Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, na nguvu Zake za Kiungu, alihisi hitaji la maombi/kuomba,

Je, ni kiasi gani watu wanyonge, wenye dhambi wanapaswa kuhisi umuhimu wa maombi—maombi ya bidii na ya kudumu! Wakati Kristo alipopatwa na majaribu makali zaidi, Yeye Hakula chochote. Alijikabidhi kwa MUNGU, na kupitia maombi ya dhati, na kujitiisha kikamilifu kwenye mapenzi ya Baba Yake, Naye aliibuka kama mshindi. Wale wanaoukiri na kuushuhudia Ukweli kwa ajili ya siku hizi za mwisho, zaidi ya jamii nyingine yoyote ya wanaodai kuwa Wakristo, wanapaswa kumwiga Yeye Yule aliye Kielelezo Kikuu katika maombi.— (Counsels on Diet and Foods, 52, 53) [Pr 274.1; Maombi Aya ya 1]

Watu wa MUNGU Wana Wajibu wa Kuomba kwa ajili ya Miaka Michache Zaidi ya Neema Kabla Mwisho haujafika— Lazima kuwe na hali ya kiroho zaidi, kujitolea wakfu kwa kina zaidi kwa MUNGU, na usongo/ari katika kazi Yake ambayo haijapata kufikiwa bado. Lazima muda mwingi lutumike katika maombi, ili mavazi yetu ya tabia yasafishwe na kufanywa meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. [Pr 274.2; Maombi Aya ya 2]

Tunapaswa kuwa na imani isiyoyumba haswa, tunapaswa kumtafuta MUNGU ili neema na nguvu zitolewe kwa watu Wake sasa. Hatuamini kwamba wakati umetimia wa kuwekwa vikwazo juu ya uhuru wetu. Nabii aliona “malaika wanne wamesimama katika pembe nne za dunia, wakizulia pepo nne za dunia, ili upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wowote. Malaika mwingine, akipanda kutoka mashariki, akawalilia, akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumishi wa MUNGU wetu katika vipaji vya nyuso zao.” Hii inasonda kazi tunayopaswa kufanya sasa. Wajibu mkubwa umekabidhiwa kwa wanaume na wanawake wa maombi katika nchi nzima kuomba ili MUNGU afagilie mbali wingu la uovu na kutoa miaka michache zaidi ya neema ya kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Hebu tumlilie MUNGU ili malaika wazizuie pepo nne hadi wamishenari watakapotumwa katika sehemu zote za ulimwengu na kutangaza onyo dhidi ya kutotii sheria ya Yehova.— (Testimonies for the Church 5:717, 718. [Pr 274.3; Maombi Aya ya 3]

Maombi Katika Nyakati za Amani yatawatayarisha Watu wa MUNGU kwa ajili ya Nyakati za Taabu Mwishoni —Watumishi wa Kristo hawakupaswa kutayarisha maelezo

au hotuba yoyote ya kutoa watakapofikishwa mahakamani. Maandalizi yao yalipaswa kufanywa siku baada ya siku katika kuzitunza zile Kweli za thamani za Neno la MUNGU, na kwa njia ya maombi kuimarisha imani yao. Walikapofikishwa mahakamani, Roho Mtakatifu atawakumbusha zile Kweli ambazo zitahitajika haswa. [Pr 275.1; Maombi Aya ya 4]

Juhudi za kila siku za dhati za kumjua MUNGU, na Yesu Kristo ambaye Yeye amemtuma, zitaleta nguvu na ufanisi kwenye nafsi. Ujuzi unaopatikana kwa kuchunguza Maandiko kwa bidii uliangaziwa katika kumbukumbu kwa wakati ufaao. Lakini kama kuna yeyote ambaye alikuwa amepuuza kujizoeza na kujifahamisha na Maneno ya Kristo, endapo hawakupata kamwe kujaribu na kujihakikishia wenyewe uwezo wa neema Yake katika majaribu, basi wasingeweza kutarajia kwamba Roho Mtakatifu angeleta Maneno Yake kwenye kumbukumbu zao. Walipaswa kumtumikia MUNGU kila siku kwa upendo usiogawanyika, na kisha kumtumaini Yeye.—(The Desire of Ages, 355) [Pr 275.2; Maombi Aya ya 5]

Tunaishi katika kipindi nyeti, cha kutafakari kwa umakini zaidi katika historia ya ulimwengu huu. Hatima ya umati wa watu duniani inakaribia kuamuliwa. Ustawi wetu wenyewe wa wakati ujao, na pia wokovu wa roho nyingine, unategemea njia tunayofuata sasa. Tunahitaji kuongozwa na Roho wa Kweli. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kuomba na kuuliza dhati na kwa bidii, “Bwana, wataka mimi nifanye nini?” Tunahitaji kujinyenyekeza mbele za Bwana, kwa kufunga na kuomba, na kutafakari sana Neno Lake, hasa kuhusiana na matukio ya hukumu. Inatupasa sasa kutafuta uzoefu wa kina na ulio hai katika mambo ya MUNGU. Hatuna hata nukta ya kupoteza. Matukio ya muhimu sana yanaendelea kufanyika karibu nasi; tuko kwenye ardhi ya Shetani iliyorogwa.—(The Great Controversy, p. 601) [Pr 275.3; Maombi Aya ya 6]

Majira ya dhiki na uchungu mbele yetu yatahitaji imani inayoweza kustahimili uchovu, uchelewesho/kukawia, na njaa— imani ambayo haitazimia ingawa imejaribiwa vikali. Muda wa mlango wa rehema kuwa wazi umetolewa kwa wote kujiandaa kwa ajili ya wakati huo. Yakobo alishinda kwa sababu alivumilia, aliazimia na kujizatiti. Ushindi wake Yakobo, ni ushahidi wa nguvu ya maombi yasiyochoka

na yenye bidii. Wote watakaoshikilia ahadi za MUNGU, kama yeye na kuwa dhati na wavumilivu kama alivyokuwa, watafanikiwa kama Yakobo alivyofaulu. Wale ambao hawako tayari kujikana nafsi, kuteseka mbele ya MUNGU, kuomba kwa muda mrefu na kwa bidii kwa ajili ya baraka Zake, hakika hawataipata. Kushindana mweleka na MUNGU (mfano wa Yakobo na Malaika)—ni wachache kiasi gani wanaojua ina maana gani! Ni wachache kiasi gani ambao wamewahi kuvutiwa roho zao kumfuata Mwenyezi MUNGU kwa matamania makubwa kiasi cha kunyumbulisha kila nguvu. Wakati mawimbi ya kukata tamaa ambayo hakuna lugha inayoweza kueleza yanapomkumba mwombaji, ni wachache kiasi gani wanaoshikamana na imani isiyobadilika kwenye ahadi za MUNGU.— (The Great Controversy, 621) [Pr 276.1; Maombi Aya ya 7]

Maombi yawe ulinzi hata Mwisho—Hadi pambano hilo litakapokoma, kutaendelea kuwa na wale ambao watamwacha MUNGU. Shetani atatengeneza mazingira kiasi kwamba tusipotunzwa na uwezo wa Bwana, yatakaribia kuharibu ngome za nafsi bila kujua. Tunahitaji kuomba katika kila hatua, “Je, hii ndiyo njia ya Bwana?” kadiri maisha haya yanavyoendelea kuwapo na bado tunaendelea kupumua, kutakuwa na haja ya kulinda mapenzi na shauku kwa kusudi thabiti. Hakuna hata nukta moja tunayoweza kuwa salama isipokuwa tunamtegemea MUNGU, maisha yaliyofichwa pamoja na Kristo. Kukesha na maombi ni ulinzi wa usafi wa moyo. [Pr 276.2; Maombi Aya ya 8]

Wote wanaoingia katika Jiji la MUNGU wataingia kupitia mlango mwembamba tu— kwa bidii yenye uchungu mkubwa; kwa maana “hakitaingia humo chochote kilicho najisi. Ufunuo 21:27. Lakini hakuna yeyote aliyeanguka anayehitaji kukata tamaa. Wazee, ambao hapo awali waliheshimiwa na MUNGU, wanaweza kuwa walitia unajisi roho zao, wakitoa mhanga wema katika madhabahu ya tamaa za mwili; lakini wakitubu, na kuacha dhambi, na kumgeukia MUNGU, bado kulikuwa na matumaini kwao. Yeye atangazaye, “Uwe mwaminifu hata kufa, Nami nitakupa taji ya uzima,” pia anatoa mwaliko, “Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake, amrudie Mwenyezi-MUNGU apate kumhurumia, amwendee MUNGU wetu maana atamsamehe kabisa.” Ufunuo 2:10;

Isaya 55:7. MUNGU anachukia dhambi, lakini anampenda mwenye dhambi. “Nitaponya uasi wao,” asema; “Nitawapenda kwa ukunjufu wa moyo.” Hosea 14:4.— (Manabii na Wafalme, 83, 84.) [Pr 276.3; Maombi Aya ya 9]

Kundi dogo Litakuwa Likiombea Kanisa Katika Wakati wa Hatari Yake Kubwa Zaidi—Chachu ya utauwa haijapoteza nguvu zake kabisa. Wakati ambapo hatari na mfadhaiko wa kanisa ni mkubwa zaidi, kundi dogo ambalo limesimama kwenye nuru litakuwa likiugua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa katika nchi. Lakini zaidi sana maombi yao yatainuliwa kwa niaba ya kanisa kwa sababu washiriki wake wanafanya kulingana na namna ya ulimwengu. [Pr 277.1; Maombi Aya ya 10]

Maombi ya bidii ya waaminifu hawa wachache hayataenda bure. Wakati Bwana atakapokuja kama muhukumu, atakuja pia kama mlinzi wa wale wote ambao wameilinda imani katika usafi wake na kujilinda wenyewe bila mawaa dhidi ya ulimwengu. Ni wakati huu ndio ambao MUNGU ameahidi kulipiza kisasi kwa niaba ya wateule Wake ambao humlilia mchana na usiku, ingawa Yeye huchukuliana nao na kuwavumilia kwa muda mrefu — (Testimonies for the Church 5:209, 210) [Pr 277.2; Maombi Aya ya 11]

Omba kwa ajili ya Roho Wakati wa Mvua ya Masika—Hatuwezi kutegemea mazoea au taasisi za nje. Tunachohitaji ni ushawishi wa kuhuisha wa Roho Mtakatifu wa MUNGU. “Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa Majeshi.” Ombeni bila kukoma, na kesheni kwa kufanya kazi sawasawa na maombi yenu. Unapoendelea kuomba, amini, mtumaini MUNGU. Ni wakati wa mvua ya masika, ambapo Bwana atatoa Roho Wake kwa wingi. Uwe na bidii na ari/usongo katika maombi, na ukeshe katika Roho.—(The Review and Herald, March 2, 1897) [Pr 277.3; Maombi Aya ya 12]

Maombi ndio Usalama wa Mkristo katika siku za Mwisho— Niliona baadhi, wakiwa na imani yenye nguvu na vilio vya uchungu, wakimsihi MUNGU. Nyuso zao zilikuwa zimedhoofu na zilikuwa zina alama ya fadhaa na wasiwasi mwingi, zikionyesha mapambano yao ya ndani. Uthabiti na bidii kubwa vilionyeshwa katika nyuso zao; matone makubwa ya jasho yakaanguka kutoka kwenye vipaji vya

nyuso zao. Mara kwa mara nyuso zao ziling'aa kwa alama za ukubali/kibali cha MUNGU, na tena ule mwonekano ulio mzito (makini, usio na tabasamu), wa dhati, na wa wasiwasi ukakaa juu yao. [Pr 278.1; Maombi Aya ya 13]

Malaika waovu walikusanyika kuwazunguka, wakisukuma giza juu yao ili kumfungia Yesu asionekane kwao (wasimwone), ili macho yao yavutwe kwenye giza lililowazunguka, na hivyo kuongozwa kutomwamini MUNGU na kumnung'unikia. Usalama wao pekee ulikuwa katika kuelekeza macho yao juu. Malaika wa MUNGU walikuwa na mamlaka juu ya watu Wake, na anga hewa lenye sumu ya malaika waovu liliposogezwa karibu na hawa watu wenye kufadhaika na wasiwasi, malaika wa mbinguni walikuwa wakipepea mbawa zao juu yao ili kulitawanya giza nene. [Pr 278.2; Maombi Aya ya 14]

Waombaji walipokuwa wakiendelea na kilio chao cha dhati, nyakati fulani nuru ya Yesu iliwajia, ili kuwatia moyo yao na kuangaza nyuso zao. Baadhi, niliwaona, hawakushiriki katika kazi hii ya kulia kwa uchungu na kusihi. Walionekana kutozingatia na kutojali. Hawakuwa wakipinga giza lililowazunguka, na liliwafunga kama wingu zito. Malaika wa MUNGU waliwaacha hawa na kwenda kusaidia wale walio na bidii, wanaosali. Niliona malaika wa MUNGU wakiharakisha kuwasaidia wale wote waliokuwa wakihangaika kupambana kwa uwezo wao wote kuwapinga malaika wabaya na kujaribu kujisaidia wenyewe kwa kumwita MUNGU kwa ustahimilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakufanya jitihada yoyote ya kujisaidia, nao wkapotea katika upeo wa macho yangu.— (Early Writings, 269) [Pr 278.3; Maombi Aya ya 15]

Watu wa MUNGU Wataomba na Kushinda Mwishoni Kama Alivyofanya Yakobo—Yakobo na Esau wanawakilisha matabaka mawili; Yakobo mwenye haki, na Esau mwovu. Kufadhaika kwa Yakobo alipojua kwamba Esau alikuwa anakuja dhidi yake, pamoja na gwaride la watu mia nne, kunawakilisha taabu ya wenye haki wakati amri inapotoka ya kuwaua, kabla tu ya kuja kwa Bwana (Yeremia 30:7). Waovu wanapokusanyika kuwazunguka, watajawa na mateso ya akili na mwili, kwani hawawezi kuona njia ya kuyaponya maisha yao kama Yakobo. Malaika akajiweka mbele ya Yakobo, naye akamshika malaika huyo, na kumng'ang'ania, na akashindana Naye mieleka usiku

kucha. Vivyo hivyo na wenye haki, wakati wa taabu na dhiki zao, watahindana mweleka na MUNGU katika maombi, kama vile Yakobo alivyoshindana mweleka na malaika. Yakobo katika dhiki yake aliomba usiku kucha kwa ajili ya ukombozi kutoka kwenye mkono wa Esau (Mwanzo 32). Wenye haki katika uchungu wao unaohisiwa kiakili, watamlilia MUNGU mchana na usiku ili awakomboe kutoka katika mkono wa waovu wanaowazunguka. [Pr 278.4; Maombi Aya ya 16]

Yakobo alikiri kutostahili kwake. "Sistahili hata kidogo rehema Zako zote, na Kweli yote uliyonionyesha mtumishi Wako." Wenye haki, katika dhiki yao, watakuwa na hisia ya kina ya kutostahili kwao, na kwa machozi mengi watakiri kutostahili kwao kabisa, na kama vile Yakobo wataomba ahadi za MUNGU kupitia njia ya Kristo, zilizofanywa kwa ajili ya wadhambi kama hao na wategemezi, wasiojiweza, na wenye dhambi wanaotubu. [Pr 279.1; Maombi Aya ya 17]

Yakobo akamng'ang'ania huyo Malaika katika shida yake, wala hakumruhusu aende Zake. Alipokuwa akiomba dua kwa machozi, Malaika huyo alimkumbusha makosa yake ya zamani, na akajaribu kumtoroka Yakobo, ili kumjaribu na kumthibitisha. Ndivyo hivyo wenye haki, katika siku ya dhiki yao, watapimwa, na kuthibitishwa, na kujaribiwa, ili kudhihirisha nguvu zao za imani, ustahimilivu wao na ujasiri usiotikisika katika uwezo wa MUNGU wa kuwakomboa (Malaika Herufi kubwa ni Kristo). [Pr 279.2; Maombi Aya ya 18]

Yakobo hakuweza kugeuzwa. Alijua kwamba MUNGU ni Mwenye rehema, na aliomba rehema Yake. Aliangalia nyuma kwenye huzuni yake ya zamani na toba ya makosa yake, na akashinikiza ombi lake la ukombozi dhidi ya mkono wa Esau. Hivyo ombi lake lisilochoka na lenye msukumo likaendelea usiku kucha. Alipopitia upya makosa yake ya zamani, ilimfanya kukaribia kukata tamaa. Lakini alijua kwamba lazima apate msaada kutoka kwa MUNGU au aangamie. Ndipo akamshika Yule malaika, na kushinikiza ombi lake kwa kilio cha uchungu, cha bidii, hata akashinda. Ndivyo itakavyokuwa kwa watu wema. Wanapopitia matukio ya maisha yao ya zamani, matumaini yao yatakaribia kuzama. Lakini wanapotambua kwamba ni jambo la uzima au kifo, watamlilia MUNGU kwa bidii, na

kumsihi kuhusiana na huzuni yao ya zamani na toba ya unyenyekevu ya dhambi zao nyingi, na kisha watarejelea kwenye ahadi Yake, “Hebu ashike nguvu Zangu, na afanye amani Nami, naye atafanya amani Nami.” Hivyo maombi yao ya bidii yatatolewa kwa MUNGU mchana na usiku.— (Spiritual Gifts 3:131- 133) [Pr 279.3; Maombi Aya ya 19]

SURA YA 29

FURSA YA MAOMBI -UPENDELEO WA MAOMBI

Kupitia asili na mafunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, MUNGU huzungumza nasi. Lakini basi, haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake Yeye. Ili tuwe na uzima na nguvu za kiroho, ni lazima tufanye ushirika halisi na Baba yetu wa mbinguni. Akili zetu zinaweza kuvutwa kumwelekea Yeye; tunaweza kutafakari juu ya kazi Zake, rehema Zake, baraka Zake; lakini hii sio maana kamili ya kuwa na ushirika Naye. Ili kuwa na ushirika na MUNGU, ni lazima tuwe na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi. [Pr 280.1; Maombi Aya ya 1]

Kuomba ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Si kwamba ni lazima tumjulishe MUNGU jinsi tulivyo, bali ili kutuwezesha sisi kumpokea Yeye. Maombi hayamshushi MUNGU kwetu, bali hutuina juu Kwake. [Pr 280.2; Maombi Aya ya 2]

Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kumtwika Yeye mahangaiko yao yote. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikika, ni uhakikisho wetu pia. [Pr 280.3; Maombi Aya ya 3]

Yesu Mwenyewe, alipokuwa akiishi miongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi. Mwokozi wetu alijitambulisha Mwenyewe na mahitaji na udhaifu wetu, na katika hilo alifanyika muhitaji, mwombaji, akitafuta kutoka kwa Baba Yake nyongeza ya nguvu, ili apate kwenda akiwa imara kwa ajili ya kazi, wajibu na

majaribu. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni ndugu katika udhaifu wetu, “Yeye alijaribiwa katika mambo yote kama sisi; bali kama mtu asiye na dhambi. asili yake ilijiepusha na uovu; Alivumilia mapambano na mateso ya nafsi katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu Wake ulifanya maombi kuwa hitaji la lazima na kipaumbele. Alipata faraja na furaha katika ushirika na Baba Yake. Na kama Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa MUNGU, alihisi hitaji la maombi, ni kiasi gani wanadamu wanyonge, wenye dhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi ya bidii, yenye ari, endelevu - ya kudumu. [Pr 280.4; Maombi Aya ya 4]

Baba yetu wa mbinguni anangoja kutupa utimilifu wa baraka Zake. Ni fursa yetu kunywa kwa kiasi kikubwa kwenye chemchemi ya upendo usio na mipaka. Inashangaza sana kwamba tunaomba kidogo sana! MUNGU ameridhia na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya aliye mnyenyekevu zaidi kati ya watoto Wake, na bado kuna kusitasita kwa wazi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU mahitaji yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini juu ya wanadamu dhaifu wasiojiweza, ambao wanakandamizwa chini ya majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo unawahitaji, tayari kuwapa zaidi ya wanavyoweza kuomba au kufikiria, na bado wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo? Malaika hupenda kusujudu mbele za MUNGU; wanapenda kuwa karibu Naye. Wanaona ushirika na MUNGU kuwa ndiyo furaha yao kuu; na bado wana wa dunia, ambao ni wahitaji sana wa msaada ambao MUNGU pekee anaweza kutoa, wanaonekana kutosheka kutembea bila nuru ya Roho Wake, kuandamana na uwepo Wake. [Pr 281.1; Maombi Aya ya 5]

Giza la yule mwovu linawafunika wale wanaopuuzwa kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui yanawavuta kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii fursa ambayo MUNGU amewapa katika miadi mitakatifu Naye Katika maombi. Kwa nini wana na binti za MUNGU wanakuwa wenye kusitasita kuomba, wakati maombi ni ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala la mbinguni, ambako kunatunzwa rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote? Bila maombi na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuongeza roho ya kutojali, uzembe na kukengeuka kutoka katika njia iliyo sahihi. Adui anatafuta

daima kufunga njia ya kuelekea Kiti cha Rehema, ili kwamba kwa maombi ya dhati na imani tusipate neema na uwezo wa kupinga majaribu. [Pr 281.2; Maombi Aya ya 6]

Kuna masharti fulani ambayo tunaweza kutarajia kwamba MUNGU atasikia na kuyajibu maombi yetu. Mojawapo ya hayo ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Yeye Ameahidi, “Nitamimina maji juu yake yeye aliye na kiu, na mito juu ya nchi kavu.” Isaya 44:3. Wale walio na njaa na kiu ya haki, wenye matamanio na MUNGU, wanaweza kuwa na hakika kwamba watashibishwa. Moyo lazima uwe wazi kwa ushawishi wa Roho, vinginevyo baraka za MUNGU haziwezi kupokelewa. [Pr 282.1; Maombi Aya ya 7]

Haja yetu kubwa yenyewe ni hoja tosha, nayo inasihi kwa umbuji/ufasaha zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa kutafutwa afanye mambo haya kwa ajili yetu. Yeye Anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa. Na “Yeye ambaye hakumhurumia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye?” Mathayo 7:7; Warumi 8:32. [Pr 282.2; Maombi Aya ya 8]

Tukiendekeza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote inayojulikana, Bwana hatatusikia; lakini ombi la mtu aliyetubu na aliyekiri hukubaliwa daima. Makosa yote yanayojulikana yanaporekebishwa, tunaweza kuamini kwamba MUNGU atajibu maombi yetu. Haki yetu sisi wenyewe au mazuri yetu sisi wenyewe hayatatufanya tupate kibali cha MUNGU; ni kustahili Kwake Yesu tu, ndiko kutatuokoa, damu Yake itatusafisha; lakini bado tuna kazi ya kufanya kwa kuzingatia masharti ya kukubalika. [Pr 282.3; Maombi Aya ya 9]

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. “Mtu amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.” Waebrania 11:6. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. Je, tunamuendea Yeye kwa Neno Lake? [Pr 282.4; Maombi Aya ya 10]

Uhakikisho ni mpana na hauna kikomo, na Yeye Aliye mwaminifu ambaye ameahidi, Naye Atatenda. Wakati hatupokei vile vile tulivyoomba, wakati tunaomba, bado

tunapaswa kuamini kwamba Bwana anasikia na kwamba atajibu maombi yetu. Sisi ni wakosefu sana na hivyo hatuoni mbali kiasi kwamba wakati fulani tunaomba mambo ambayo hayatakuwa ya baraka kwetu, na Baba yetu wa mbinguni kwa upendo anajibu maombi yetu kwa kutupa yale ambayo yatakuwa kwa manufaa yetu ya juu—yale ambayo sisi wenyewe tungetamani ikiwa kwa nuru ya maono ya Bwana tungeweza kuona mambo yote jinsi yalivyo Kweli. Maombi yetu yanapoonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia ahadi; kwani wakati wa kujibu hakika utakuja, na tutapokea baraka tunazohitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa njia ile ile na kwa jambo lile lile bayana/mahsusuni tunalotamani, ni dhana potofu ambayo haiendani na mapenzi ya Mungu, ni imani na ujasiri bandia, na pengine hata ni kiburi (presumption). MUNGU ni Mwenye hekima sana kiasi kwamba hawezi kamwe kukosea, na ni Mwema sana hata asiweze kuwanyima kitu chochote kizuri wale waendao kwa unyofu. Basi usiogope kumtumaini/kumwamini, ingawa hauoni majibu ya haraka ya maombi yako. Tegemea ahadi Yake ya hakika, “Ombeni, nanyi mtapewa.” [Pr 282.5; Maombi Aya ya 11]

Ikiwa tunashauriana na mashaka na hofu zetu na tunajaribu kutatua kila tatizo wakati ambapo hatuna upeo wa kuona mambo kwa uwazi, basi mashaka na hofu badala ya kuwa na imani yataongezeka na kuwa ya kina. Lakini tukimwendea MUNGU, tukijihisi kuwa hatuna msaada na wategemezi, kama tulivyo kihalisia, na kwa imani ya unyenyekevu, yenye kumtumaini, tukiweka wazi matakwa yetu Kwake Yeye ambaye ujuzi Wake hauna kikomo, ambaye huona kila kitu katika uumbaji, na anayetawala kila kitu kwa mapenzi Yake na Neno Lake, basi Yeye Anaweza na atasikiliza kilio chetu, na ataacha nuru iangaze ndani ya mioyo yetu. Kupitia maombi ya dhati tunaletwa katika mshikamano na mawazo ya Yeye Asiye na mwisho. Huenda tusiwe na ushahidi wa ajabu wakati huo kwamba uso wa Mkombozi wetu unainama juu yetu kwa huruma na upendo, lakini ndivyo ilivyo haswa. Huenda tusihisi mguso Wake unaonekana, lakini mkono Wake uko juu yetu kwa upendo na huruma nyingi. [Pr 283.1; Maombi Aya ya 12]

Tunapoenda kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Je, tunawezaje kuomba, “Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu,” na bado tuwe na roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatarajia maombi yetu sisi binafsi yasikilizwe, ni lazima tuwasamehe wengine kwa namna sawa na kwa kiwango sawa na tunachotarajia kusamehewa. [Pr 283.2; Maombi Aya ya 13]

Kudumu katika maombi kwa uvumilivu bila kuchoka kumefanywa kuwa sharti la kupokea. Ni lazima tuombe kila mara ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu. Tunapaswa kuwa “wenye utayari katika kuomba mara zote,” na “kudumu katika maombi, na kukesha katika hayo kwa kutoa shukrani.” Warumi 12:12; Wakolosai 4:2. Petro anawasihi waumini wawe na kiasi, na msawaziko wa akili, na kukesha katika maombi. 1 Petro 4:7. Paulo anaagiza, “Katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na MUNGU.” Wafilipi 4:6. “Lakini ninyi, wapenzi,” asema Yuda, “mkiomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa MUNGU.” Yuda 20, 21. Ombi lisilokoma ni muungano usiovunjika wa nafsi na MUNGU, ili uzima kutoka kwa MUNGU utiririke ndani ya maisha yetu; na kutoka nje ya maisha yetu, usafi na utakatifu utatiririke kurudi kwa MUNGU. [Pr 283.3; Maombi Aya ya 14]

Kuna ulazima wa uadilifu na bidii katika maombi; usiruhusu chochote kikuzuie. Fanya kila juhudi kuweka wazi ushirika kati ya Yesu na roho yako mwenyewe. Tafuta kila nafasi ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa. Wale ambao kwa kweli wanatafuta ushirika na MUNGU wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na kwa bidii na shauku ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wanaweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni. [Pr 284.1; Maombi Aya ya 15]

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ni uzima wa nafsi. Haiwezekani kabisa nafsi kusitawi wakati maombi ya faragha yamepuuzwa. Sala ya familia au hadhara pekee yake haitoshi. Katika upweke roho iwekwe wazi (ianikwe) mbele ya jicho la

upekuzi/ukaguzi la MUNGU. Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na MUNGU pekee anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi hayo. Katika maombi ya siri nafsi inakuwa huru dhidi ya vishawishi vinavyoizunguka, huru dhidi ya msisimko. Kwa utulivu, lakini kwa bidii, itamfikia MUNGU. Mvuto unaotoka kwake Yeye aonaye kwa siri utakuwa mtamu/mzuri na wa kudumu, Yule ambaye sikio Lake liko wazi kusikia maombi yanayotoka moyoni. Kwa imani tulivu, iliyo sahili, roho hushikilia ushirika na MUNGU na kujikusanyia miale ya nuru ya Bwana ili kuiimarisha na kuitegemeza katika pambano na Shetani. MUNGU Ndiye mnara wetu wa nguvu zetu. [Pr 284.2; Maombi Aya ya 16]

Omba chumbani mwako au mahali pa faragha, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara. Ilikuwa kwa namna hiyo ambapo Henoko alitembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU. [Pr 284.3; Maombi Aya ya 16b]

Katika maombi ya siri nafsi haivutiwi na vile inavyoizunguka, iko huru kutokana na misisimko. Kwa utulivu, lakini kwa ari na shauku, hakika itamfikia Mungu. Utamu na ulio wa kudumu utakuwa mvuto unaotoka kwa Yeye aonaye kwa siri, ambaye sikio Lake liko wazi kusikia sala inayotoka moyoni. Kwa imani tulivu, iliyo sahili, roho hushikilia ushirika na Mungu na kujikusanyia miale ya nuru ya Bwana ili kuiimarisha na kuitegemeza katika pambano na Shetani. Mungu Ndiye mnara wa nguvu zetu. [Pr 284.2; Maombi Aya ya 18]

Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi yaliyo dhati na ya bidii. Katika umati wa watu barabarani na mitaani, katikati ya pilikapilika za shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kusihhi mwongozo wa Bwana, kama alivyofanya Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Chumba cha ushirika wa faragha kinaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu uwe unaendelea

kupanda ili Yesu aje na kukaa ndani ya moyo kama mgeni wa mbinguni katika nafsi. [Pr 284.4; Maombi Aya ya 19]

Ingawa kunaweza kuwa na mazingira machafu, yaliyoharibika karibu nasi na yenye giza, sisi hatuhitaji kupumua hewa yake chafu na yenye kunuka vibaya, lakini tunaweza kuishi katika hewa safi ya mbinguni. Tunaweza kufunga kila mlango wa fikra chafu na mawazo machafu yasiyo matakatifu kwa kuinua roho katika uwepo wa MUNGU kupitia maombi ya moyo wa dhati. Wale ambao mioyo yao iko wazi kupokea msaada na baraka za MUNGU watatembea katika angahewa takatifu zaidi kuliko ile ya dunia na watakuwa na ushirika wa kudumu/endelevu na mbingu. [Pr 285.1; Maombi Aya ya 20]

Tunahitaji kuwa na maoni dhahiri zaidi ya Yesu na ufahamu kamili zaidi wa thamani ya uhalisia wa milele. Uzuri wa utakatifu unapaswa kujaza mioyo ya watoto wa MUNGU; na ili hili liweze kutimizwa, tunapaswa kutafuta mafunuo ya Bwana yahusuyo mambo ya mbinguni. [Pr 285.2; Maombi Aya ya 21]

Hebu roho ivutwe nje na kwenda juu, ili MUNGU atujalie pumzi ya angahewa la mbinguni. Tunaweza kuwa karibu sana na MUNGU ili kwamba katika kila changamoto au jaribu lisilotazamiwa, mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili, yaani kama kawaida kama vile ua linavyogeukia jua (naturally au automatik). [Pr 285.3; Maombi Aya ya 22]

Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za MUNGU. Wewe auwezi kumlelea Yeye; wewe hauwezi kumchosha Bwana. Yeye Anayehesabu nywele za kichwa chako hayuko tofauti juu ya mahitaji ya watoto Wake (hujali mahitaji ya watoto Wake). “Bwana ni mwingi wa huruma, ni mwingi wa rehema.” Yakobo 5:11. Moyo Wake wa upendo unaguswa na sikitiko letu na hata sisi tunavyozitamka huzuni hizi. Mpelekee Yeye kila kitu kinachotatanisha akili. Hakuna lililo kubwa Kwake kustahimili, kwani Yeye Ndiye anayeshikilia malimwengu (sayari zote), Yeye Anatawala mambo yote ya kila mahali (mbingu na nchi Universe au galaksi zote). Hakuna jambo lolote ambalo kwa njia yoyote ile linahusu amani yetu ni dogo sana Kwake hata asilitambue. Hakuna sura katika uzoefu wetu ambayo ina giza sana Kwake hata asiweze kuisoma; hakuna wasiwasi

ulio mgumu sana Kwake hata asiwe kuutatua. Hakuna janga liwezalo kumpata hata yule aliye mdogo kabisa kati ya watoto Wake, hakuna uonevu au masumbufu yoyote yanayosumbua nafsi, hakuna furaha ya shangwe, hakuna sala ya unyoofu inayotoka midomoni, ambayo Baba yetu wa mbinguni haioni, au ambayo Yeye haizingatii mara moja kwa kuonyesha shauku Yake. "Yeye huwaponya waliovunjika moyo, na kufunga majeraha yao." Zaburi 147:3. Mahusiano kati ya MUNGU na kila nafsi ni dhahiri na yamesheheni (ni makamilifu) kana kwamba hakuna nafsi nyingine duniani inayoshiriki ulinzi Wake, au nafsi nyingine ambayo kwayo Yeye alimtoa Mwanawe Mpendwa kwa ajili Yake. [Pr 285.4; Maombi Aya ya 23]

Yesu alisema, "Mtaomba kwa Jina Langu; si Mimi niliyewaambia, kwamba nitamuomba Baba kwa ajili yenu: kwani Baba anawapenda ninyi" "Nimewachagua ili chochote muombacho kwa Jina Langu, Awapatie." Yohana 16:26, 27; Yohana 15:16. Lakini kuomba kwa Jina la Yesu ni zaidi ya kutaja tu Jina hilo mwanzoni na mwisho wa maombi. Ni kuomba katika akili na roho ya Yesu, huku tunaamini ahadi Zake, na kutegemea neema Yake, na kutenda kazi Zake. [Pr 286.1; Maombi Aya ya 24]

MUNGU hamaanishi kwamba yeyote kati yetu ajiepushe na watu au awe mtawa na kujitenga na ulimwengu ili kujishughulisha na ibada- kwa kwenda kuishi wasipo watu kabisa au kuishi katika jumba moja na waumini fulani tu (hermit na monk). Maisha lazima yawe kama maisha ya Kristo—kati ya mlima na umati wa watu. Yule ambaye hafanyi chochote isipokuwa kuomba ataacha hivi karibuni kuomba, au maombi yake yatakuwa ya mazoea ya kila siku. Watu wanapojiondoa katika maisha ya kijamii, mbali na nyanja ya wajibu wa Kikristo na pia kubeba msalaba; wanapoacha kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Bwana wao, ambaye alifanya kazi kwa bidii kwa ajili yao, wanapoteza kusudi la msingi la maombi na wanapoteza kichocheo cha kujitoa kwa ibada au kujitoa wakfu. Maombi yao yanakuwa ya kibinafsi na ya ubinafsi/uchoyo. Hawawezi kuomba kuhusiana na mahitaji ya wanadamu au ya kujengwa kwa ufalme wa Kristo, wakiomba nguvu za kuifanya kazi Yake. [Pr 286.2; Maombi Aya ya 25]

Tunapata hasara kubwa tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo katika utumishi

wa MUNGU. Kweli za Neno Lake hupoteza udhahiri/uangavu na umuhimu Wake katika bongo zetu. Mioyo yetu inaacha kuangazwa na kuamshwa na mvuto Wake wa kutakasa, na tunapungua katika hali ya kiroho. Katika ushirika wetu kama Wakristo tunapoteza mengi kwa kukosa kuhurumiana sisi kwa sisi. Yule anayejifungia nafsi yake ili akae mwenyewe, haikalii nafasi ambayo MUNGU alipanga aijaze. Ukuzaji ufaao wa vipengele vya kijamii katika asili yetu hutuleta katika huruma na wengine na ni njia ya maendeleo ya utu wetu na nguvu kwetu katika utumishi wa MUNGU. [Pr 286.3; Maombi Aya ya 26]

Ikiwa Wakristo wangeshirikiana pamoja, wakisemezana juu ya upendo wa MUNGU na zile Kweli zenye thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingefanywa upya na kuwafanya upya wenzao. Tunaweza kuwa tunajifunza zaidi juu ya Baba yetu wa mbinguni kila siku, tukipata uzoefu mpya wa neema Yake; ndipo tutatamani kuzungumzia juu ya upendo Wake; na tunapofanya hivi, mioyo yetu itatiwa jotojoto na kutiwa moyo. tungewaza na kuzungumza zaidi juu ya Yesu, badala yetu sisi wenyewe, basi tungekuwa na uwepo Wake mwingi zaidi. [Pr 287.1; Maombi Aya ya 27]

Ikiwa tungemfikiria MUNGU pekee mara nyingi tunapokuwa na ushahidi wa ulinzi na utunzaji Wake kwetu, tungetakiwa kumweka daima katika mawazo yetu na tunapaswa kufurahi kuzungumza juu Yake na kumsifu. Tunazungumza juu ya mambo ya kupita, yale yasiyodumu, kwa sababu tunapendezwa nayo. Tunazungumza juu ya marafiki zetu kwa sababu tunawapenda; furaha zetu na huzuni zetu zimefungamana nao. Hata hivyo tuna sababu kubwa isiyo na kikomo ya kumpenda MUNGU kuliko kuwapenda marafiki zetu wa duniani; inapaswa kuwa jambo la kawaida zaidi ulimwenguni kumfanya Yeye kuwa wa kwanza katika mawazo yetu yote, kuzungumza juu ya wema Wake na kueleza juu ya uwezo Wake. Zawadi nono alizotupa hazikukusudiwa kuchukua mawazo na upendo wetu hata tusiwe na kitu cha kumpa MUNGU; hizi zinapaswa kutukumbusha daima juu Yake na kutufunga katika vifungo vya upendo na shukrani kwa Mfadhili wetu wa mbinguni. Tunageukia sana nyanda za chini za dunia (yakatishayo tamaa au yaliyo hasi). Hebu na tuyainue macho yetu kwenye mlango uliofunguliwa wa Patakatifu pa juu, ambapo nuru ya utukufu wa MUNGU inang'aa katika

uso wa Kristo, ambaye “aweza kuwaokoa kabisa wao wanaomwendea MUNGU kwa njia Yake Yesu.” Waebrania 7:25. [Pr 287.2; Maombi Aya ya 28]

Tunahitaji kumsifu MUNGU zaidi “kwa ajili ya wema Wake, na kwa ajili ya matendo Yake ya ajabu kwa wanadamu.” Zaburi 107:8. Mazoezi yetu ya ibada hayapaswi kuhusisha kuomba na kupokea peke yake. Hebu tusiwe tunafikiria kila mara matakwa yetu na sio faida tunazopata. Mara nyingi hatuombi kiasi cha kutosha (hatuombi kupindukia), ila tuna tabia ya kutoa shukrani zetu kwa ubahili sana. Sisi ni wapokeaji wa rehema za MUNGU mara kwa mara, na bado ni shukrani ndogo kiasi gani tunaonyesha, ni mara chache kiasi gani tunamsifu kwa yale ambayo Yeye ametufanyia. [Pr 287.3; Maombi Aya ya 29]

Hapo zamani za kale Bwana aliwaambia Israeli, walipokutana pamoja kwa ajili ya utumishi Wake, “Mtakula mbele za Bwana, MUNGU wenu, nanyi mtafurahi katika yote mtakayotia mkono wenu, ninyi na nyumba zenu, ambazo Bwana, MUNGU wenu, amewabarikia ninyi.” Kumbukumbu la Torati 12:7. Kile kinachofanyika kwa utukufu wa MUNGU kinapaswa kufanywa kwa furaha, kwa nyimbo za sifa na shukrani, sio kwa huzuni na masikitiko. [Pr 288.1; Maombi Aya ya 30]

MUNGU wetu ni Baba mpole, Mwenye moyo mwororo, huruma na rehema. Utumishi Wake haupaswi kuangaliwa kama zoezi gumu la kuhuzunisha moyo, na kuleta msongo. Inapaswa kuwa furaha kumwabudu Bwana na kushiriki katika kazi Yake. MUNGU asingetaka watoto Wake, ambao wokovu mkuu umetolewa kwao, watende kana kwamba Yeye ni msimamizi mgumu na mkali (mnyapara), mwenye kutubebesha majukumu mazito. Yeye ni rafiki yao/yetu mkubwa; na tunapomwabudu, Yeye anatazamia kuwa pamoja nasi, na kutubariki na kutufariji, akijaza mioyo yetu shangwe na upendo. Bwana anatamani sisi watoto Wake tupate faraja katika huduma Yake na kupata raha zaidi kuliko shida katika kazi Yake. Yeye Anatamani kwamba wale tunaokuja kumwabudu Yeye tuchukue pamoja nasi mawazo ya thamani ya ulinzi, utunzaji Wake na upendo Wake, ili tuweze kuchangamshwa katika shughuli zote za maisha ya kila siku, ili tupate neema ya

kutenda kwa ukweli/kikweli na uaminifu katika mambo yote. [Pr 288.2; Maombi Aya ya 31]

Ni lazima tukusanyike kwenye msalaba. Kristo na kusulubiwa Kwake inapaswa kuwa mada yetu kutafakari, ya mazungumzo, na ya hisia zetu za furaha na shangwe zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayopokea kutoka kwa MUNGU, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kukabidhi kila kitu kwenye mkono ule uliopigiliwa msumari msalabani kwa ajili yetu. [Pr 288.3; Maombi Aya ya 32]

Nafsi inaweza kupaa juu karibu na mbingu kwa mbawa za sifa. Mungu anaabudiwa kwa nyimbo na muziki katika makao yaliyo juu, na tunapoonyesha shukrani zetu, basi tunakaribia ibada ya majeshi ya mbinguni. Yeye “Atoaye sadaka ya sifa humtukuzi MUNGU. Zaburi 50:23. Hebu na tuje mbele ya Muumba wetu kwa shangwe ya uchaji, kwa “shukrani, na sauti ya shangwe.” Isaya 51:3. [Pr 288.4; Maombi Aya ya 33]

Sura hii inaonekana katika Steps to Christ, 93-104

SURA YA 30

SALA YA BWANA

“Basi ninyi salini hivi.” Mathayo 6:9.

Sala ya Bwana ilitolewa mara mbili na Mwokozi wetu, kwanza mbele ya umati katika Mahubiri ya Mlimani, na kisha, miezi kadhaa baadaye kwa wanafunzi peke yao. Wanafunzi walikuwa wamekaa mbali kwa muda mfupi na Bwana wao, nao waliporudi walimkuta amezama/ametekewa katika ushirika/mawasiliano na MUNGU. Akiwa ameonekana kwao kwamba hajui uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Uso wa Mwokozi ulin’gaa, ukimulikwa na mwangaza wa mbinguni. Waliona kama Yupo mbele Zake Yeye Yule Asiyeonekana kabisa (Mungu BABA), na kulikuwa na nguvu hai katika Maneno Yake kama ya mtu anayezungumza na MUNGU. [Pr 289.1; Maombi Aya ya 1]

Mioyo ya wanafunzi waliokuwa wakisikiliza ilitekewa kwa kuguswa sana. Walikuwa wamehesabu ni mara ngapi Alikuwa ameenda kwa muda mrefu katika upweke kwenye ushirika na Baba Yake. Siku zake zilipita katika huduma kwa makutano waliomsonga, na katika kufunua hila za udanganyifu wa viongozi wa kidini, na kazi hii isiyokoma mara nyingi ilimfanya awe hoi kwa kuchoka sana hata mama Yake na ndugu Zake na pia wanafunzi Wake waliogopa kwamba ingemgarimu maisha (afya Yake ingetolewa mhanga). Lakini aliporudi kutoka katika saa za maombi zilizofunga siku ile yenye taabu, walishuhudia mwonekano wa amani juu ya uso Wake, hisia ya kuburudishwa ambayo ilionekana kutawala uwepo Wake. Upya na hali hii kwa ujumla vilitokana na saa alizotumia na MUNGU na ndipo alienda, asubuhi baada ya asubuhi, kuleta

nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Wanafunzi Wake wakafikia hatima ya kuzihusisha saa Zake za maombi na nguvu za Maneno Yake na kazi Zake. Sasa, walipokuwa wakisikiliza ombi Lake, mioyo yao ilipata hofu takatifu (awe), kwa ule utukufu, na kisha wakanyenyekea. Alipomaliza kuomba tu, ilikuwa ni kwa usadikisho wa hitaji lao la ndani na kina, ndipo walipopaza sauti na kusihi, “Bwana, tufundishe sisi kusali.” Luka 11:1. [Pr 289.2; Maombi Aya ya 2]

Yesu hawapi watu aina mpya ya ombi. Yale Aliyowafundisha hapo awali Anayarudia, kana kwamba Angesema kwetu leo, Mnahitaji kuelewa kile nilichokwisha kutoa. Kuna maana ya kina ambayo bado hamjajielewa. [Pr 290.1; Maombi Aya ya 3]

Mwokozi, hata hivyo, hatuzui kutumia maneno haya kama yalivyo. Akiwa mmoja na ubinadamu, Yeye Anawasilisha wazo Lake la maombi yaliyo bora, maneno sahili./mepesi sana kiasi kwamba yanaweza kukaririwa na mtoto mdogo, lakini yanafunika kila kitu na yanaeleweka sana kiasi kwamba umuhimu wake hauwezi kamwe kueleweka kikamilifu, hata na akili za watu werevu zaidi (**genius**). Tunafundishwa kumwendea MUNGU na zawadi yetu ya shukrani, kumweleza mahitaji yetu, kuungama dhambi zetu, na kudai rehema Zake kwa mujibu wa ahadi Zake. [Pr 290.2; Maombi Aya ya 4]

“Mnaposali, semeni Baba Yetu.” Luka 11:2.

Yesu anatufundisha kumwita Baba Yake, Baba yetu. Yeye haoni haya kutuita ndugu Zake. Waebrania 2:11. Moyo wa Mwokozi kwa matamano makubwa uko tayari kutukaribisha kama wanachama wa familia ya MUNGU, ndio sababu katika Maneno Yake ya utambulisho Wake wa kwanza kabisa, tumeambiwa tupasavyo kuyatumia katika kumwendea/kumsogelea MUNGU, Yeye ameweka humo uhakikisho wa uhusiano wetu wa Kiungu Naye (na Mungu), “Baba yetu.” [Pr 290.3; Maombi Aya ya 5]

Hili ni tangazo la Ukweli huo wa ajabu, Ukweli unaotia moyo na faraja mno, kwamba MUNGU anatupenda jinsi anavyompenda Mwanawe. Hivi ndivyo Yesu alisema katika sala Yake ya mwisho kwa ajili ya wanafunzi Wake, “Umewapenda wao kama ulivyonipenda Mimi.” Yohana 17:23. [Pr 290.4; Maombi Aya ya 6]

Ulimwengu ambao Shetani amedai kuuchukua na kuwa wake na kisha kuutawala kwa jeuri yenye ukatili, Mwana wa MUNGU, kwa ushindi mmoja mkubwa, ameuzingira katika upendo Wake na kuunganisha tena pamoja na kiti cha ufalme cha Yehova. Makerubi na maserafi, na majeshi yasiyohesabika ya ulimwengu (universe) wote usioanguka, waliimba nyimbo za sifa kwa MUNGU na Mwana-Kondoo wakati ushindi huu ulipohakikishwa. Walifurahi kwamba njia ya wokovu ilikuwa imefunguliwa kwa jamii iliyoanguka na kwamba dunia ingekombolewa kutoka katika laana ya dhambi. Je! ni shangwe ya ajabu kiasi gani basi, inayopaswa kuwabubujikia wale ambao ndio walengwa wa upendo huo wa ajabu! [Pr 290.5; Maombi Aya ya 7]

Je, tunawezaje basi kuwa katika mashaka na kutokuwa na uhakika, na kuhisi kwamba sisi ni yatima? Ilikuwa ni kwa niaba ya wale ambao walikuwa wameivunja sheria ndipo Yesu akachukua juu Yake asili ya ubinadamu; Yeye Akawa kama sisi, ili tuwe na amani ya milele na uhakikisho. Tunae Wakili mbinguni, na yeyote anayemkubali kama Mwokozi wake binafsi haachiwi kamwe kama yatima kubeba mzigo wa dhambi zake mwenyewe. [Pr 291.1; Maombi Aya ya 8]

"Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU." "Na ikiwa ni watoto, basi tu warithi; warithi wa MUNGU, warithio pamoja na Kristo; ikiwa tukiteswa pamoja Naye, ili tupate kutukuzwa pamoja Naye." "Bado haijadhihirika tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa tutafanana Naye; kwa maana tutamwona jinsi alivyo." 1 Yohana 3:2; Warumi 8:17. [Pr 291.2; Maombi Aya ya 9]

Hatua ya kwanza kabisa ya kumkaribia MUNGU ni kujua na kuamini upendo alionao kwetu (1 Yohana 4:16); kwa maana ni kupitia kuvutiwa na upendo Wake ndipo tunapoongozwa kwenda Kwake. [Pr 291.3; Maombi Aya ya 10]

Kuusikia, kuhuhisi na kuuishi upendo wa MUNGU hufanya kazi katika kuukana ubinafsi. Katika kumwita MUNGU Baba yetu, tunawatambua watoto Wake wote kama ndugu zetu. Sisi sote ni sehemu ya mtandao mkuu wa ubinadamu, sote ni washiriki wa familia moja. Katika maombi yetu tunapaswa kujumuisha majirani zetu na sisi wenyewe. Hakuna anayeomba kwa usahihi ambaye anatafuta baraka

kwa ajili yake peke yake (anayejiombea shida au mahitaji yake binafsi tu). [Pr 291.4; Maombi Aya ya 11]

MUNGU wa milele yaani Yeye Yule Asiye na kikomo, alisema Yesu ameifanya iwe fursa kwetu sisi, kumwita Yeye kwa Jina la Baba. Elewa yote ambayo hii inamaanisha. Hakuna mzazi wa duniani aliyewahi kusihi kwa ajili ya mtoto Wake mwenye makosa kwa bidii kama Yeye Alituumba anavyotukaribisha na anavyosihi kwa ajili ya sisi wapotovu. Hakuna maslahi ya upendo wa kibinadamu yaliyowahi kuwafuata wasiotubu kwa mialiko hiyo ya huruma. MUNGU anakaa katika kila makazi; Yeye husikia kila neno linalonenwa, husikiliza kila ombi linalotolewa, huonja huzuni na kukatishwa tamaa kwa kila nafsi, huangalia jinsi anavyotendewa baba, mama, dada, rafiki na jirani. Yeye Anajali mahitaji yetu, na upendo Wake na rehema na neema vinaendelea kumiminika daima ili kutosheleza hitaji letu. [Pr 291.5; Maombi Aya ya 12]

Lakini mkimwita MUNGU Baba yenu mwaafikiana kuwa ninyi ni watoto Wake, na mu tayari kuongozwa na hekima Yake na kuwa watiifu katika mambo yote, mkijua kwamba upendo Wake haubadiliki. Mtakubaliana na mpango Wake kwa ajili ya maisha yenu. Kama watoto wa MUNGU, mtaishikilia hadhi Yake, heshima Yake, tabia Yake, familia Yake, kazi Yake, kama malengo ya shauku yenu ya juu zaidi. Itakuwa furaha yenu kutambua na kuheshimu uhusiano wenu na Baba yenu na kwa kila mwanafamilia Yake. Mtafurahi kufanya tendo lolote, hata liwe la unyenyekevu kwa kiasi gani, litakalopelekea kuleta utukufu Wake Mungu au ustawi wa ndugu zetu au udugu wetu (binadamu sote). [Pr 292.1; Maombi Aya ya 13]

"Uliyeko juu mbinguni." Yeye ambaye Kristo anatubidisha tumtazame kama "Baba yetu" "Yuko mbinguni: Yeye amefanya yale yote yanayompendeza." Katika utunzaji na ulinzi Wake tunaweza kupumzika kwa usalama, tukisema, "Wakati ninaoogopa, nitakutumaini Wewe." Zaburi 115:3; Zaburi 56:3. [Pr 292.2; Maombi Aya ya 14]

"Jina lako litukuzwe." Mathayo 6:9.

Kulitukuza Jina la Bwana kunahitaji kwamba maneno ambayo tunazungumza juu ya Yeye Aliye Mkuu Zaidi

yatamkwe kwa heshima. “Jina Lake ni takatifu na lenye kuheshimiwa ‘*kwa kicho*’.” Zaburi 111:9. Kamwe hatupo katika nafasi ya kuchukulia kwa wepesi vyeo au majina ya Uungu. Katika maombi tunaingia kwenye chumba cha kuonana na Yeye Aliye Juu; nasi tunapaswa kwenda mbele Zake kwa kicho kitakatifu. Malaika hufunika nyuso zao mbele Yake. Makerubi na maserafi angavu na watakatifu wanakaribia kiti Chake cha enzi kwa heshima kuu (kicho). Je! ni zaidi kiasi gani kwetu basi, sisi viumbe wenye ukomo, wenye dhambi, tunapaswa kwenda kwa njia ya uchaji/kicho mbele za Bwana, Muumba wetu! [Pr 292.3; Maombi Aya ya 15]

Lakini kulitukuza Jina la Bwana kunamaanisha mengi zaidi ya haya. Tunaweza, kama Wayahudi wa siku za Kristo, tukadhihirisha heshima kubwa zaidi ya nje kwa MUNGU, na bado tunachafua Jina Lake sikuzote. “Jina la Bwana” ni “Mwenye huruma na neema, mvumilivu, na mwingi wa fadhili na Kweli, ... Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi.” Kutoka 34:5-7. Imeandikwa hivi kuhusu kanisa la Kristo: “Na mji huo utaitwa ‘Mwenyezi-MUNGU ni Ukombozi Wetu, Mwenyezi Mungu ni haki yetu’.” Yeremia 33:16. Jina hili limewekwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Ni urithi wa mtoto wa MUNGU. Familia inaitwa kwa jina la Baba. Nabii Yeremia, katika wakati wa taabu na dhiki kuu za Israeli, aliomba, “Tumeitwa kwa Jina Lako; usituache.” Yeremia 14:9. [Pr 292.3; Maombi Aya ya 16]

Jina hili linatukuzwa na kusujudiwa na malaika wa mbinguni, na wakazi wa malimwengu yasiyoanguka (universe-galaxies zote). Unapoomba, “Jina lako litukuzwe,” wewe unaomba kwamba litukuzwe katika ulimwengu huu, na pia litukuzwe ndani yako wewe mwenyewe. Mwenyezi MUNGU amekukiri wewe mbele za watu na Malaika kwamba u mtoto Wake; ombea ili usilikufuru na kulivunja heshima “Jina lile jema tuliloitiwa.” Yakobo 2:7. MUNGU anakutuma ulimwenguni kama mwakilishi Wake. Katika kila tendo la maisha unatakiwa kudhihirisha Jina la MUNGU. Ombi hili linakutaka tumiliki tabia Yake. Wewe huwezi ukalitukuza Jina Lake, huwezi kumwakilisha kwenye ulimwengu, isipokuwa katika maisha na tabia tunawakilisha maisha na tabia ile ile ya MUNGU (tabia Yake Mwenyewe). Hili

unaweza kufanya tu kwa kukubali neema na haki ya Kristo.
[Pr 293.1; Maombi Aya ya 17]

“Ufalme wako uje.” Mathayo 6:10.

MUNGU ni Baba yetu, anayetupenda na kutujali sisi kama watoto Wake; Yeye pia Ndiye Mfalme mkuu wa malimwengu yote (sayari zote). Maslahi na shauku ya ufalme Wake ni masilahi yetu, na tunapaswa kufanya kazi kwa ajili ya kuujenga huo ufalme. [Pr 293.2; Maombi Aya ya 18]

Wanafunzi wa Kristo walikuwa wanatazamia ujio wa haraka wa ufalme Wake wa utukufu, lakini katika kuwapa ombi hili Yesu alifundisha kwamba ufalme usingesimikwa wakati huo. Walipaswa kuombea ujio Wa Ufalme huo kama tukio la wakati ujao. Lakini ombi hili pia lilikuwa uhakikisho kwao. Japo wasingeweza kuuona ujio wa ufalme huo katika siku zao, uhakika wa kwamba Yesu aliwaambia wauombe ni uthibitisho kwamba katika wakati aliouweka MUNGU Mwenyewe, hakika utakuja. [Pr 293.2; Maombi Aya ya 19]

Ufalme wa neema ya MUNGU sasa unasimikwa, siku baada ya siku mioyo ambayo imejaa dhambi na uasi inajitoa na kujisalimisha kwenye ukuu wa upendo Wake. Lakini kusimamishwa kikamilifu kwa ufalme wa utukufu Wake hakutafanyika mpaka ujio wa pili wa Kristo katika ulimwengu huu. “Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii” watapewa “watu watakatifu wa MUNGU Mkuu.” Danieli 7:27. Wataurithi ufalme uliotayarishwa kwa ajili yao “tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Mathayo 25:34. Naye Kristo atajitwalia uweza Wake mkuu na kutawala. [Pr 293.3; Maombi Aya ya 20]

Malango ya mbinguni yatainuliwa tena, na pamoja na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya watakatifu, Mwokozi wetu atakuja kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Yehova Imanueli

“atakuwa Ndiye mfalme pekee wa dunia yote; Naye atakuwa Ndiye Mwenyezi-MUNGU pekee, Mmoja tu, na Jina Lake litakuwa ndilo Jina pekee.” “Maskani ya MUNGU” Itakuwa pamoja na wanadamu, “Naye atakaa pamoja nao, nao watakuwa watu Wake, na MUNGU Mwenyewe atakuwa pamoja nao, na atakuwa MUNGU wao.” Zekaria 14:9; Ufunuo 21:3 [Pr 294.1; Maombi Aya ya 21]

Lakini kabla ya kuja huko, Yesu alisema, “Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote.” Mathayo 24:14. Ufalme Wake hautakuja mpaka habari njema ya neema Yake ifikishwe duniani kote. Kwa hiyo, tunapojitua kwa MUNGU, na kuleta nafsi nyingine Kwake, sisi tunaharakisha ujio wa ufalme Wake. Ni wale tu wanaojitua kwa ajili ya utumishi Wake, wakisema, “Mimi hapa; nitume” (Isaya 6:8), kufungua macho ya vipofu, kuwaongoa watu “kutoka gizani hadi kwenye nuru na kutoka katika nguvu za Shetani na kumwelekea MUNGU, ili wapate ondoleo la dhambi na urithi miongoni mwao waliotakaswa” (Matendo 26:18)—wao pekee wanaomba kwa uaminifu, “Ufalme wako uje.” [Pr 294.2; Maombi Aya ya 22]

“Mapenzi Yako yafanyike duniani kama huko mbinguni.” Mathayo 6:10.

Mapenzi ya MUNGU yanaonyeshwa katika kanuni za sheria Yake takatifu, na kanuni za sheria hii ni kanuni za mbinguni. Malaika wa mbinguni hawapati ujuzi wa juu zaidi kuliko ule wa kuyajua mapenzi ya MUNGU, na kuyafanya mapenzi Yake ndiyo huduma ya juu zaidi kabisa ambayo wao wanaweza kuzihusisha nguvu zao. (Mapenzi ya Mungu ndiyo sheria Yake na sheria Yake ndiyo Mapenzi Yake, malaika wao hawataki kujua chochote isipokuwa yale yaliyokuwa kwenye duara la mapenzi ya Mungu tu-hawataki uovu kwa ufupi!) [Pr 294.3; Maombi Aya ya 23]

Lakini mbinguni, huduma haitolewi katika roho ya kisheria. Shetani alipoasi sheria ya Yehova, wazo la kwamba kulikuwa na sheria lilikuja kwa malaika kama ufahamu wa wazo ambalo wao hawakuwa wamelifikiria. Katika huduma yao malaika si kama watumishi, bali kama wana. Kuna umoja kamili kati yao na Muumba wao. Utii

kwao sio jukumu zito au kongwa. Upendo wao kwa MUNGU hufanya utumishi wao uwe wenye shangwe yaani wa kushangilia. Kwa hiyo katika kila nafsi ambayo iko ndani ya Kristo, tumaini la utukufu, hutamalaki, Maneno Yake hurudiwa kama mwangwi tena na tena, “Kuyafanya mapenzi Yako, Ee MUNGU wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria Yako imo moyoni mwangu..” Zaburi 40:8. [Pr 294.4; Maombi Aya ya 24]

Ombi, “Mapenzi yako yatimizwe duniani kama huko mbinguni,” ni sala ya kusihhi kwamba utawala wa uovu humu duniani uweze kukomeshwa, ili dhambi iteketezwe milele, na ufalme wa haki usimamishwe. Kisha duniani kama vile ilivyo mbinguni, patasheheni “raha yote ya wema Wake.” 2 Wathesalonike 1:11. [Pr 295.1; Maombi Aya ya 25]

"Utupe leo mkate wetu wa kila siku." Mathayo 6:11.

Nusu ya kwanza ya ombi ambalo Yesu ametufundisha inahusu jina na ufalme na mapenzi ya MUNGU—ili Jina Lake liheshimiwe, ufalme Wake usimikwe, na mapenzi Yake yatimizwe. Unapofanya utumishi wa MUNGU kuwa jambo la kipaumbele cha Kwanza kwako, unaweza kuomba kwa uhakika na ujasiri kwamba mahitaji yako mwenyewe yaweze kutimizwa. Ikiwa umejinyima na kuikana na nafsi yako na kujitoa kwa Kristo, wewe ni mwanachama wa familia ya MUNGU, na kila kitu ndani ya nyumba ya Baba ni kwa ajili yako. Hazina zote za MUNGU zimefunguliwa kwako, yaani za ulimwengu uliopo sasa na ule ujao. Huduma ya malaika, karama ya Roho Wake, kazi ya watumishi Wake—zote zipo hapo kwaajili yako. Dunia, yenye kila kitu ndani yake, ni yako kwa kadiri inavyoweza kukutendea wema/fadhila. Hata uadui wa waovu utathibitika kuwa baraka kwa kukunidhamisha kwa ajili ya mbingu. Ikiwa “ninyi ni wa Kristo,” “vitu vyote ni vyenu.” 1 Wakorintho 3:23, 21. [Pr 295.2; Maombi Aya ya 26]

Lakini wewe ni kama mtoto ambaye bado hajawekwa kuutawala/kuudhibiti urithi wake. MUNGU hakukabidhi mali yako ya thamani, ili Shetani asije akakudanganya kwa ujanja wake, kama alivyowafanyia ile jozi ya watu wa kwanza kule Edeni. Kristo anashikilia urithi kwa ajili yako kwa usalama ili usifikiwe na mharibifu. Kama mtoto,

utapokea siku baada ya siku kile kinachokidhi mahitaji lyako ya kila siku. Kila siku unatakiwa kuomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku.” Usifadhaike ikiwa hauna vya kutosha kwa ajili ya kesho. Wewe una uhakika wa ahadi Yake, “Basi mtakaa katika ardhi, na hakika mtalishwa.” Daudi anasema, “Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee; lakini sijamwona mwenye haki ameachwa, wala watoto wake wakiombaomba chakula. Zaburi 37:3, 25. Yule MUNGU aliyetuma kunguru kumlisha Eliya karibu na kijito Kerithi hatampita mmoja wa watoto Wake mwaminifu na wenye kujitoa. Imeandikwa hivi kuhusu yeye aendaye kwa haki: “Mkate atapewa; maji yake yatadumu.” “Hawataaibishwa wakati wa uovu; na siku za njaa watashiba. “Yeye hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye?” Isaya 33:16; Zaburi 37:19; Warumi 8:32. Yeye ambaye alipunguza mizigo na mahangaiko ya mama Yake mjane na kumsaidia kwa kuleta riziki nyumbani kule Nazareti, anamhurumia kila mama katika jitihada zake za kuwaandalia watoto wake chakula. Yeye ambaye alikuwa na huruma kwa umati kwa sababu “walichoka na kutawanyika” (Mathayo 9:36), bado ana huruma kwa maskini wanaoteseka. Mkono Wake umenyooshwa kuelekea kwao katika kubariki; na katika ombi lile lile alilowapa wanafunzi Wake, Yeye anatufundisha kuwakumbuka maskini. [Pr 295.3; Maombi Aya ya 27]

Tunapomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” tunaomba kwa ajili ya wengine na sisi wenyewe pia. Na tunakubali kwamba kile ambacho MUNGU anatupa si kwa ajili yetu wenyewe. MUNGU hutukabidhi sisi kama amana, ili tuwalishe wenye njaa. Kwa wema Wake, Yeye amewaandalia maskini. Zaburi 68:10. Naye anasema, “Ufanyapo chakula cha usiku au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako matajiri.....Bali ufanyapo karamu, waite maskini, na vilema, viwete, vipofu, nawe utabarikiwa; kwa maana wao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo

wa wenye haki." Luka 14:12-14. [Pr 296.1; Maombi Aya ya 28]

“MUNGU aweza kuwajaza kila neema kwa wingi; ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema.” “Yule Apandaye haba atavuna haba; na apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.” 2 Wakorintho 9:8, 6. [Pr 296.2; Maombi Aya ya 29]

Ombi la mkate wa kila siku halijumuishi tu chakula cha kutegemeza mwili, bali mkate wa kiroho ambao utailisha roho hata uzima wa milele. Yesu anatuagiza, “Msikifanyie kazi chakula chenye kuharibika, bali kile kidumucho hata uzima wa milele.” Yohana 6:27. Anasema, “ Mimi ni Mkate wa Uzima uliotoka mbinguni. Mtu yeyote akiula mkate huu ataishi milele. Kifungu cha 51. [Pr 297.1; Maombi Aya ya 30]

Mwokozi wetu Ndiye mkate wa uzima, na ni kwa kuutazama upendo Wake tu, kwa kuupokea ndani ya roho, ndipo tunakuwa tukila mkate ulioshuka kutoka mbinguni. [Pr 297.2; Maombi Aya ya 31]

Tunampokea Kristo kupitia kwenye Neno Lake, na Roho Mtakatifu anatolewa ili kufungua Neno la MUNGU katika ufahamu wetu, na kuleta kwetu ile Kweli Yake kwenye mioyo yetu. Tunapaswa kuomba siku baada ya siku kwamba tunaposoma Neno Lake, MUNGU atume Roho Wake ili kutufunulia Ukweli ambao utaimarisha roho zetu kwa mahitaji ya siku hiyo. [Pr 297.3; Maombi Aya ya 32]

Katika kutufundisha kuomba kila siku kile tunachohitaji – baraka za kimwili za muda mfupi na zile za kiroho—MUNGU ana kusudi la kutimiza kile ambacho ni kwa manufaa yetu wenyewe. Yeye Anatutaka tutambue kutegemea kwetu daima ulinzi Wake, kwa kuwa anatafuta kutuvuta katika ushirika Naye Mwenyewe. Katika ushirika huu na Kristo, kwa njia ya maombi na kujifunza zile Kweli kuu na za thamani za Neno Lake, kama roho zenye njaa tutalishwa; kama wale walio na kiu, kisha tutaburudishwa kwenye chemchemi ya uzima. [Pr 297.4; Maombi Aya ya 33]

“Utusamehe dhambi zetu kwa kuwa na sisi tunawasamehe wote wanaotukosea.” Luka 11:4.

Yesu anafundisha kwamba tunaweza kupokea msamaha kutoka kwa MUNGU pale tu tunapowasamehe wengine. Upendo wa MUNGU ndio unaotuvuta Kwake, na upendo huo hauwezi kugusa mioyo yetu bila kuumba upendo kwa ndugu zetu. [Pr 297.5; Maombi Aya ya 34]

Baada ya kumaliza Sala ya Bwana, Yesu aliongeza hivi: “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Yeye asiyesamehe hukata njia ambayo kwayo pekee anaweza kupokea rehema kutoka kwa MUNGU. Hatuna haki kufikiri kwamba wale ambao wametuumiza wasipokiri kosa lao kwetu basi sisi tuna haki ya kuwanyima msamaha wetu. Hakika na bila shaka, ni sehemu yao kunyenyekeza mioyo yao kwa toba na maungamo; lakini sisi tunapaswa kuwa na roho ya huruma kwa wale ambao wametukosea, endapo wanakiri makosa yao au la. Haijalishi wametujeruhi vibaya kiasi gani, hatupaswi kuthamini kutotendewa haki kwetu na kujihurumia wenyewe kuhusiana na majeraha yetu; lakini kama tunavyotarajia kusamehewa makosa yetu dhidi ya MUNGU tunapaswa kuwasamehe wote wale waliotutendea sisi uovu. [Pr 297.6; Maombi Aya ya 35]

Lakini msamaha una maana pana kuliko wengi wanavyodhani. MUNGU anapotoa ahadi kwamba “atasamehe kabisa,” anaongeza, kana kwamba maana ya ahadi hiyo inapita yote tunayoweza kuelewa kwa utashi wetu: “Mawazo Yangu si kama mawazo yenu, wala njia zenu si kama njia Zangu, asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu kuliko mawazo yenu.” Isaya 55:7-9. Msamaha wa MUNGU si tu tendo la haki ambalo kwalo Yeye hutuweka huru dhidi ya hukumu. Sio tu msamaha wa dhambi, bali ni ukombozi kutoka katika dhambi. Ni ububujikaji wa upendo unaokomboa, unaogeuzi moyo. Daudi alikuwa na dhana ya Kweli ya msamaha alipoomba, “Uniumbie moyo safi, ee MUNGU, uweke ndani yangu roho mpya na thabiti..” Zaburi 51:10. Na tena anasema, “Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.” Zaburi 103:12. [Pr 298.1; Maombi Aya ya 36]

MUNGU katika Kristo alijitoa kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye Aliteseka kwa kifo cha kikatili cha msalabani, alitubebea mzigo wa hatia, “wenye haki kwa wasio haki,” ili aweze kutufunulia upendo Wake na kutuvuta Kwake. Naye anasema, “Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na MUNGU katika Kristo alivyowasamehe ninyi. Waefeso 4:32, Hebu Kristo, Aliye maisha matakatifu, akae ndani yako na kupitia kwako adhihirishe upendo uliozaliwa mbinguni ambao utahuisha tumaini kwa wasio na tumaini na kuleta amani ya mbinguni kwenye moyo uliosumbuliwa na kupipigwa-pigwa na dhambi. Tunapomwendea MUNGU, hili ndilo sharti tinalokutana nalo kwenye kizingiti, kwamba, tukipokea rehema kutoka Kwake, basi nasi tunajitoa ili kudhihirisha neema Yake kwa wengine. [Pr 298.2; Maombi Aya ya 37]

Jambo moja la muhimu kwetu ili tuweze kupokea na kutoa kwa wengine upendo huu wa Mungu wa kusamehe, ni kuujua na kuuamini upendo Yeye alionao kwetu. 1 Yohana 4:16. Shetani anafanya kazi kwa kila udanganyifu anaoweza kuuamuru, ili tusiweze kuutambua upendo huo. Adui atatuongoza kufikiri kwamba makosa na maovu yetu yamekuwa ya kutisha na kuhuzunisha sana kiasi kwamba Bwana hataheshimu maombi yetu na hatatubariki na kutuokoa. Ndani yetu wenyewe hatuwezi kuona chochote ila udhaifu, hakuna kitu cha kutupatia haki mbele za MUNGU (hatuna CV ya kufaa), na Shetani anatuambia haisaidii kitu, kwani hatuwezi kurekebisha kasoro zetu za tabia. Tunapojaribu kumwendea MUNGU, adui atanong'ona kwetu, Haifai kitu kwako kuomba; Je, haukufanya ubaya huo kweli? Je! haujamtenda MUNGU dhambi na kukiuka dhamiri yako mwenyewe? Lakini tunaweza kumwambia adui kwamba “damu ya Yesu Kristo Mwanawe inatutakasa dhambi zote.” 1 Yohana 1:7. Tunapohisi kwamba tumetenda dhambi na hivyo hatuwezi kuomba, basi huo ni wakati wa kuomba haswa. Tunaweza kuona aibu usoni na kuona tumenyenyekeswa sana, lakini lazima tuombe na kuamini. “Neno hili ni la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi; ambao mimi ni mkuu wao.” 1 Timotheo 1:15. Msamaha, upatanisho na MUNGU, huja kwetu, si kama haki au thawabu kwaaajili ya matendo yetu, hautolewi kwa sababu ya wema wa sifa yetu au haki yetu sisi wenye dhambi, bali ni zawadi kwetu,

iliyokita kwenye msingi wa utoaji kutoka katika ile Haki isiyo na mawaa ya Kristo. [Pr 298.3; Maombi Aya ya 38]

Hatupaswi kujaribu kupunguza hatia yetu kwa kutolea udhuru dhambi. Ni lazima tukubali makadirio ya MUNGU ya dhambi (jinsi anavyoipima), nayo ni mazito kweli kweli. Kalvari pekee yake, ndiyo inaweza kudhihirisha ukubwa na uzito wa kuogofya wa dhambi. Kama ingebidi tuibebe hatia yetu wenyewe, basi ingetusagasaga kabisa. Lakini Yule asiye na dhambi amechukua mahali petu; Japokuwa hastahili, amebeba maovu yetu. “Tukiziungama dhambi zetu,” MUNGU ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1 Yohana 1:9. Kweli tukufu!— Mwenye haki na Mwaminifu juu ya sheria Yake Mwenyewe, na bado ni Mwenye kuwahesabia haki wote wanaomwamini Yesu. “Ee MUNGU, ni nani aliye kama Wewe? Mwenye kusamehe uovu, na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia, wala huyaangalii makosa yao. Hasira Yako haidumu milele, ila wapendelea zaidi kutuonesha fadhili Zako.” Mika 7:18. [Pr 299.1; Maombi Aya ya 39]

**"Usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu."
Mathayo 6:13, R.V.**

Majaribu ni ushawishi wa kutenda dhambi, na huu hautoki kwa MUNGU, bali kwa Shetani na kutoka kwenye uovu wa mioyo yetu wenyewe. “MUNGU hawezi kujaribiwa na maovu, wala Yeye Mwenyewe hamjaribu mtu.” Yakobo 1:13 R.V. [Pr 300.1; Maombi Aya ya 40]

Shetani anatafuta kutuingiza katika majaribu, ili ubaya wa tabia zetu udhihirishwe mbele ya wanadamu na malaika, ili apate kudai na kutuchukua kama wake. Katika unabii wa ishara wa Zekaria, Shetani anaonekana amesimama mkono wa kuume wa Malaika wa Bwana, akimshtaki Yoshua, kuhani mkuu, ambaye amevaa mavazi machafu, na akipinga kazi ambayo Malaika anatamani kumfanyia. Hii inawakilisha mtazamo wa Shetani kwa kila nafsi ambayo Kristo anatafuta kuivuta Kwake. Adui hutuongoza katika dhambi, na kisha anatushtaki mbele ya anga la mbinguni kuwa hatustahili upendo wa MUNGU (hatustahili kupendwa na Mungu). Lakini “Mwenyezi-MUNGU na akulaani, ewe Shetani! Naam, Mwenyezi-MUNGU aliyeuteua mji wa Yerusalemu na akulaani! Je! hiki

si kama kinga kilichonyakuliwa kutoka motoni?" Naye akamwambia Yoshua, Tazama, nimekuondolea uovu wako, Nami nitakuvika mavazi ya thamani; Zekaria 3:1-4. [Pr 300.2; Maombi Aya ya 41]

MUNGU katika upendo Wake mkuu anatafuta kukuza ndani yetu neema za thamani za Roho Wake. Yeye Anaturuhusu tukabiliane na vikwazo, mateso, na magumu, si kama laana, bali kama baraka kuu zaidi maishani mwetu. Kila jaribu linalopingwa, kila mtihani unaobebwa kwa ujasiri, hutupatia uzoefu mpya na hutukuza katika kazi ya kujenga tabia. Nafsi ambayo kwa uwezo wa Bwana inapinga majaribu inaudhirishia ulimwengu na anga la mbinguni ufanisi wa neema ya Kristo. [Pr 300.3; Maombi Aya ya 42]

Lakini huku tukiwa hatupaswi kufadhaishwa na majaribu, hata yawe na uchungu wa kiasi gani, sisi tunapaswa kuomba ili MUNGU asituruhusu tupelekwe mahali ambapo tutavutwa mbali na tamaa za mioyo yetu wenyewe yenye uovu. Katika kutoa ombi ambalo Kristo ametupatia, tunajisalimisha katika uongozi wa MUNGU, tukimwomba atuongoze katika njia salama. Hatuwezi kutoa ombi hili kwa dhati, na bado tukaamua kutembea katika njia yoyote tunayoichagua sisi wenyewe. Tutasubiri mkono Wake utuongoze; tutaikiliza sauti Yake, ikisema, "Njia ni hii, ifuateni." Isaya 30:21. [Pr 300.4; Maombi Aya ya 43]

Si salama kwetu kujikawiza kwa kutafakari manufaa tunayoweza kujichumia kwa kukubali madokezo ya Shetani. Dhambi maana yake ni fedheha na balaa kwa kila nafsi inayojiendekeza nayo; lakini inapofusha na inadanganya katika asili yake, na itatuvutia kwa maonyesho ya kubembeleza na udanganyifu. Ikiwa tutajitosa kwenye ardhi ya Shetani, basi sisi hatuna uhakika wa kulindwa dhidi ya uwezo wake. Kwa kadiri ilivyo ndani yetu, tunapaswa kufunga kila njia ambayo kwayo mjaribu yanaweza kupata mpenyo wa kutufikia. [Pr 300.5; Maombi Aya ya 44]

Ombi kwamba, "Usitutie majaribuni," lenyewe ni ahadi. Tukijikabidhi kwa MUNGU tuna uhakika, Yeye "hataruhusu tujaribiwe kupita nguvu zenu, ila pamoja na majaribu, Yeye atawapeni pia nguvu ya kustahimili na njia ya kutoka humo salama." 1 Wakorintho 10:13. [Pr 301.1; Maombi Aya ya 45]

Kinga pekee dhidi ya uovu ni kutamalaki kwa Kristo ndani ya moyo kupitia imani katika haki Yake. Ni kwa sababu ubinafsi upo ndani ya mioyo yetu ndiyo maana majaribu yana nguvu juu yetu. Lakini tunapouona upendo mkuu wa MUNGU, ubinafsi unaonekana kwetu katika tabia yake kutisha na ya kuchukiza, na tunatamani ufukuziliwe mbali kutoka katika nafsi. Roho Mtakatifu anapomtukuza Kristo, mioyo yetu inalainika na kutiishwa, majaribu yanapoteza nguvu zake, na neema ya Kristo inabadilisha tabia. [Pr 301.2; Maombi Aya ya 46]

Kristo hataiacha kamwe nafsi ambayo Yeye ameifia. Nafsi inaweza kumwacha Yeye na kulemewa na majaribu, lakini Kristo hawezi kamwe kugeuka na kumwacha yule mtu ambaye amemlipia gharama ya maisha Yake Mwenyewe. Ikiwa maono yetu ya kiroho yangeweza kuhuishwa, tungeweza kuziona nafsi zilizoinama chini ya ukandamizaji na kulemewa na mizigo ya huzuni, zikisukumwa kama mkokoteni chini ya miganda na tayari kufa kwa kuvunjika moyo. Tunapaswa kuona malaika wakiruka kwa upesi ili kuwasaidia watu hawa waliojaribiwa, ambao wamesimama kama ukingoni mwa kilele cha mwamba. Malaika kutoka mbinguni huyarudisha nyuma majeshi ya mwovu ambayo yanazingira roho hizi, na kuziongoza kusimika miguu yao juu ya msingi thabiti na wenye hakika. Vita vinavyopiganwa kati ya majeshi hayo mawili ni halisi sawa na vile vinavyopiganwa na majeshi ya ulimwengu huu, na kuhusu suala la mzozo huu wa kiroho, hatima za milele zimejiegemeza huko. [Pr 301.3; Maombi Aya ya 47]

Kwetu sisi, kama kwa Petro, Neno hili linazungumzwa, “Shetani ameomba ili awapepete kama ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isipotee. Luka 22:31, 32. Namshukuru MUNGU, hatujaachwa peke yetu. Yeye ambaye “aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16), hatatuacha katika vita vya adui wa MUNGU na wanadamu. Naye Anasema, “Tazama, nimewapa uwezo wa kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Luka 10:19. [Pr 301.4; Maombi Aya ya 48]

Ishi kwa kuwasiliana pamoja na Kristo aliye hai, Naye atakushikilia kwa nguvu kwa mkono ambao hautaweza kukuacha kamwe. Tambueni na kuamini upendo Mungu alio nao kwetu, nanyi mmekuwa salama; kwamba upendo ni ngome isiyoweza kushindwa au kupenyeka na udanganyifu na mashambulizi yote ya Shetani. "Jina la Bwana ni ngome imara; Mwenye haki hulikimbilia, akawa salama." Mithali 18:10. [Pr 302.1; Maombi Aya ya 49]

"Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu." Mathayo 6:13.

Sentensi ya mwisho kama sentensi ya kwanza ya Sala ya Bwana, inaelekeza kwa Baba yetu kama Yule aliye juu ya nguvu zote na mamlaka na kila jina linalotajwa. Mwokozi aliona miaka iliyokuwa inakuja mbele ya wanafunzi Wake, kwamba haikuwa kama walivyoiotea, wakiwa wamelala kwenye mwanga wa jua wa mafanikio na heshima ya ulimwengu, bali katika giza na tufani za chuki ya kibinadamu na ghadhabu ya shetani. Katikati ya vita na uharibifu wa kitaifa, hatua za wanafunzi zilisongwa na hatari, na mara nyingi mioyo yao ilikandamizwa na woga. Wangeiona Yerusalemu ikiwa ukiwa, hekalu likifagiliwa mbali, ibada yake ikikoma milele, na Israeli ikitawanywa katika nchi zote, kama mabaki kwenye ufuo wa jangwa. Yesu alisema, "Mtasikia habari za vita na tetesi za vita. "Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na tauni, na matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali. Yote hayo ndiyo mwanzo wa uchungu." Mathayo 24:6-8. Hata hivyo, wafuasi wa Kristo hawakupaswa kuogopa kwamba tumaini lao limepotea au kwamba MUNGU alikuwa ametelekeza dunia. Nguvu na utukufu ni Vyake Yeye ambaye makusudi Yake makuu yangeendelea bila kuzuiliwa kuelekea utimilifu wake. Katika sala inayotoa pumzi ya matakwa yao ya kila siku, wanafunzi wa Kristo walielekezwa kupeleka nguvu zote juu ya mambo yote ya utawala wa uovu, kwa Bwana MUNGU wao, ambaye ufalme Wake unatawala juu ya yote na ambaye ni Baba yao na Rafiki wa milele. [Pr 302.2; Maombi Aya ya 50]

Kuangamia kwa Yerusalemu ilikuwa ishara ya uharibifu wa mwisho ambao ungeufadhaisha ulimwengu. Unabii uliotimizwa kiasi fulani katika kupinduliwa kwa Yerusalemu

unahusiana moja kwa moja na mambo ya siku za mwisho. Sasa tumesimama kwenye mlango wa matukio makubwa na mazito. Mgogoro tete ulio mbele yetu ambao ulimwengu haujawahi kushuhudia, uko mbele yetu. Habari njema kwetu, kama kwa wanafunzi wa kwanza, unakuja uhakikisho kwamba ufalme wa MUNGU unatawala juu ya yote. Mpango wa matukio yanayokuja uko mikononi mwa Muumba wetu. Mkuu wa mbinguni Ana hatima ya mataifa, pamoja na maslahi ya kanisa Lake, chini ya usimamizi na uwezo Wake Mwenyewe. Mwalimu wa Kiungu anamwambia kila wakala katika utimilifu wa mipango Yake, kama vile alivyomwambia Koreshi, “Nilikutia nguvu, ingawa wewe haukunijua.” Isaya 45:5. [Pr 303.1; Maombi Aya ya 51]

Katika maono ya nabii Ezeieli kulikuwa na kuonekana kwa mkono chini ya mabawa ya makerubi. Hii ni kuwafundisha waja Wake kwamba ni uweza wa Mungu ndio unaowapa mafanikio. Wale ambao MUNGU huwaajiri kama wajumbe Wake, wasihisi kwamba kazi Yake inawategemea wao. Viumbe wenye ukomo hawakuachwa kubeba mzigo huu wa wajibu. Yeye asiyesinzia kamwe, ambaye daima anafanya kazi kwa ajili ya kutimiza makusudi Yake, ataendeleza kazi Yake Mwenyewe. Bali makusudi ya watu waovu huyasukumilia mbali, na kuyavuruga/kuyakanganyisha mashauri ya wale wanaopanga mabaya juu ya watu Wake. Yeye aliye Mfalme, Bwana wa majeshi, aketiye juu ya makerubi, na katikati ya migogoro na ghasia za mataifa, bado huwalinda watoto Wake. Yeye Anayetawala mbinguni ni Mwokozi wetu. Yeye hupima kila jaribu, hulinda moto wa tanuru ambao lazima ujaribu kila nafsi. Ngome za wafalme zitakapopinduliwa, mishale ya hasira itakapoingia mioyoni mwa adui Zake, watu Wake watakuwa salama mikononi Mwake. [Pr 303.2; Maombi Aya ya 52]

“Ee Bwana, ukuu ni Wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni Vyako... uwezo na nguvu vimo mkononi Mwako; na mkononi Mwako wawakuza uwapendao, na huwaimarisha wote.” 1 Mambo ya Nyakati 29:11, 12. [Pr 303.3; Maombi Aya ya 53]

Sura hii inaonekana katika (Thoughts from the Mount of Blessing, 102-122)

SURA YA 31

KUOMBA ILI KUTOA KWA WENGINE

Kristo alikuwa akipokea daima kutoka kwa Baba ili aweze kuwasiliana nasi. “Neno hilo mnalolisikia,” alisema, “si Langu, bali ni la Baba aliyenituma.” Yohana 14:24. “Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika.” Mathayo 20:28. Aliishi na kufikiria na kuomba, sio kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine. Kutoka katika saa alizotumia pamoja na MUNGU alitoka asubuhi baada ya asubuhi kupeleka nuru ya mbinguni kwa wanadamu. Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za mapema (alfajiri) za siku mpya Bwana alimwamsha kutoka katika usingizi Wake, na nafsi Yake na midomo Yake ilipakwa neema, ili aweze kuwagawia wengine. Alipatiwa Maneno mapya kutoka kwenye nyua za mbinguni, Maneno ambayo angeweza kuzungumza katika msimu unaofaa kwa waliochoka na kuonewa. “Bwana MUNGU amenipa,” alisema, “ulimi wa hao wafundishwao, nipate kumtegemeza kwa Neno yeye aliyechoka, huniamsha asubuhi baada ya asubuhi; huniamsha, sikio langu lipate kusikia kama watu wafundishwao.” Isaya 50:4. [Pr 304.1; Maombi Aya ya 1]

Wanafunzi wa Kristo walivutiwa sana na maombi Yake na mazoea Yake ya ushirika na MUNGU. Siku moja baada ya kutokuwepo kwa Mola wao kwa muda mfupi, walimkuta ametekewa/amezama katika dua. Akionekana kutojua uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Mioyo ya wanafunzi iliguswa sana. Alipoacha kuomba, wakapaza sauti kwa shauku kubwa, “Bwana, tufundishe kuomba.” [Pr 304.2; Maombi Aya ya 2]

Katika kujibu, Kristo alirudia sala ya Bwana, kama alivyokuwa ameitoa katika mahubiri ya mlimani. Kisha katika kisa alitoa mfano wa somo alilotaka kuwafundisha. [Pr 305.1; Maombi Aya ya 3]

“Ni nani kwenu,” akasema, “aliye na rafiki, naye atamwendea usiku wa manane, na kumwambia, Rafiki, nikopeshe mikate mitatu; kwa maana rafiki yangu amekuja kwangu katika safari yake, nami sina kitu cha kumpatia? Naye aliye ndani ajibu, na kusema, Usinisumbue; mlango sasa umefungwa, na watoto wangu wako pamoja nami kitandani; siwezi kuinuka na kukupa. Nawaambia, ijapokuwa hataamka kumpa kwa kuwa ni rafiki yake, lakini kwa sababu ya kusisitiza kwake ataamka na kumpa kadiri ya haja yake.” [Pr 305.2; Maombi Aya ya 4]

Hapa Kristo anamwakilisha mwombaji anayesihhi/anayebembeleza kama yule anayeomba kwa makusudi ya kutoa tena. Ni lazima apate mkate, la sivyo hawezi kumpatia msafiri aliyechoka, aliyechelewa. Ijapokuwa jirani yake hayuko tayari kusumbuliwa, hataacha kushinikiza ombi lake; rafiki yake lazima asaidiwe; na hatimaye ombi lake linajibiwa, mahitaji yake yanatimizwa. [Pr 305.3; Maombi Aya ya 5]

Katika namna ifananayo na hiyo, wanafunzi walipaswa kutafuta baraka kutoka kwa MUNGU. Katika kulisha makutano na katika mahubiri yahasuyo mkate kutoka mbinguni, Kristo alikuwa amewafungulia kazi yao kama wawakilishi Wake. Walipaswa kuwapa watu mkate wa uzima. Yeye aliyewapa kazi yao, aliona ni mara ngapi imani yao itajaribiwa. Mara nyingi walitupwa katika mazingira yasiyotarajiwa, na walitambua upungufu wao wa kibinadamu. Nafsi zilizokuwa na njaa ya mkate wa uzima ziliwajia, na walijiona kuwa maskini na wasio na msaada. Ni lazima wapokee chakula cha kiroho, la sivyo wasingekuwa na chochote cha kuwapa wengine. Lakini hawakupaswa kuiacha nafsi hata moja kurudi kwao bila kulishwa. Kristo anawaelekeza kwenye chanzo cha ugavi na usambazaji. Mtu ambaye rafiki yake alienda kwake kwa ajili ya kuburudishwa/burudani, hata saa isiyofaa ya usiku wa manane, yeye hakumfukuza. Hakuwa na kitu cha kumwekea kwenye meza yake ili ale, lakini alimwendea mmoja aliyekuwa na chakula na kusisitiza ombi lake mpaka jirani akamtimizia haja yake. Na je, MUNGU, ambaye alikuwa ametuma watumishi Wake kulisha wenye njaa, Je, asingeweza kuyatosheleza mahitaji yao ya kazi Yake Mwenyewe? [Pr 305.4; Maombi Aya ya 6]

Lakini jirani mwenye ubinafsi katika mfano huo haiwakilishi tabia ya MUNGU (mifano huwa haiwakilishi vipengele vyote vyema!). Somo limetolewa/limechotwa, si kwa kulinganisha, bali kwa kutofautisha. Mtu mwenye ubinafsi ataitikia na kulitenda ombi lililotolewa kwa haraka, ili kujiepusha na mtu anayesumbua pumziko lake. Lakini MUNGU anafurahia kutoa. Yeye ni mwingi wa huruma, na anatamani sana kutimiza maombi ya wale wanaomjia kwa imani. Anatupa sisi ili tuweze kuwahudumia wengine na hivyo kuwa kama Yeye. [Pr 306.1; Maombi Aya ya 7]

Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.” [Pr 306.2; Maombi Aya ya 8]

Mwokozi anaendelea: “Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe? Au je, akimwomba samaki, atampa nyoka? Kama basi nyinyi, ingawa ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, Je! Baba yenu wa mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” [Pr 306.3; Maombi Aya ya 9]

Ili kuimarisha tumaini na ujasiri wetu kwa MUNGU, Kristo anatufundisha kumwita kwa Jina Jipya, Jina lililoambatanishwa na ushirika wa dhati zaidi wa moyo wa mwanadamu. Yeye Anatupa fursa ya kumwita MUNGU ambaye hana kikomo Baba yetu. Jina hili, Linapotamkwa Kwake na kuhusu Yeye, ni ishara ya upendo na uaminifu wetu Kwake, na ahadi ya kujali katika mahusiano Yake Nasi/kwetu. Linapotamkwa Kwake wakati wa kuomba upendeleo (feva) au baraka Zake, ni kama muziki masikioni Mwake. Ili tusifikirie kuwa ni kujiamini kwa kupitiliza kinyume cha mapenzi ya Mungu kumwita kwa Jina hili (au kuwa na kiburi) Bwana amerudia tena na tena. Yeye Anatamani tulitambue na kujizoeza na Jina hilo. [Pr 306.4; Maombi Aya ya 10]

MUNGU anatuona sisi ni watoto Wake. Ametukomboa kutoka katika ulimwengu usiojali na ametuchagua tuwe washiriki wa familia ya kifalme, wana na binti za Mfalme wa mbinguni. Yeye Anaturalika tumtumaini Yeye tukiwa na matumaini na imani yenye kina na yenye nguvu zaidi kuliko

ile ya mtoto kwa baba yake wa duniani. Wazazi wanawapenda watoto wao, lakini upendo wa MUNGU ni mkubwa, mpana, na wa kina zaidi kuliko upendo wa kibinadamu unavyoweza kuwa. Upendo Wake hauna kipimo. Basi ikiwa wazazi wa kidunia wanajua kuwapa watoto wao zawadi nzuri, je! Baba yetu aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu wale wamwombao? [Pr 306.5; Maombi Aya ya 11]

Masomo ya Kristo kuhusu maombi yanapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. Kuna sayansi ya Bwana katika maombi, na mfano Wake unaleta mtazamo wa kanuni ambazo wote tunapaswa kuelewa. Yeye Anaonyesha kile ambacho ni roho ya Kweli ya maombi, Anafundisha umuhimu wa kudumu katika kuwasilisha maombi yetu kwa MUNGU, na anatumakikishia nia Yake ya kusikia na kujibu maombi. [Pr 307.1; Maombi Aya ya 12]

Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi yenye ubinafsi, ya kujipatia vitu kwa faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. “Kwa ajili yao,” Yeye alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, “Najiweka wakfu, ili nao watakaswe.” Yohana 17:19. Kujitoa vile vile, kujitoa mhanga kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao ulidhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake. Utume wetu kwa ulimwengu sio kujitumikia au kujifurahisha wenyewe; tunapaswa kumtukiza MUNGU kwa kushirikiana Naye kuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasiliana na wengine. Uwezo wa kupokea kutoka Kwake au kupewa Naye, huhifadhiwa au unakuwepo tu kwa kutoa. Sisi hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasiliana na wale wanaotuzunguka (kutoa kwa ukarimu).— (Christ's Object Lessons, 142, 143) [Pr 307.2; Maombi Aya ya 13]

Katika kisa cha mfano cha aliyeomba/mwombaji, ni kwamba alikataliwa tena na tena, lakini hakuliacha kusudi lake. Kwa hiyo maombi yetu mara zingine hayaonekani kupata jibu la haraka; lakini Kristo anafundisha kwamba hatupaswi kuacha kuomba. Dhumuni la maombi sio kumbadilisha MUNGU au kuleta mabadiliko Kwake; bali ni kutuleta katika upatanifu na MUNGU. Tunapomwomba Yeye, anaweza kuona kwamba ni muhimu kwetu

kuipeleleza mioyo yetu na kutubu dhambi. Kwa hiyo anatingiza katika majaribu na mitihani, hutupitisha kwenye njia ya kujidhili na unyenyekevu, ili tupate kuona kile kinachozuia utendaji wa Roho Wake Mtakatifu kupitia kwetu. [Pr 307.3; Maombi Aya ya 14]

Kuna masharti ya kutimizwa kwa ahadi za MUNGU, na maombi hayawezi kamwe hayawezi kuchukua nafasi ya wajibu. “Mkinipenda,” Kristo asema, “mtazishika amri Zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, Yeye Ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” Yohana 14:15, 21. Wale wanaoleta maombi yao kwa MUNGU, wakidai ahadi Yake huku wao hawaendani na masharti, wanamtukana Yehova. Wanaleta Jina la Kristo kama mamlaka yao ya utimizo wa ahadi, lakini hawatendi mambo yale ambayo yangeonyesha imani katika Kristo na upendo Kwake. [Pr 307.4; Maombi Aya ya 15]

Wengi wanapoteza haki ya kukubalika na Baba. Tunahitaji kuchunguza kwa makini tendo la kumtumaini Mungu, tunapokuwa tunamkaribia Yeye. Tusipotii, sisi tunamletea Bwana hundi ya kulipwa wakati hatujatimiza masharti ambayo yangetufanya tulipwe. Tunawasilisha kwa MUNGU ahadi Zake, na kumwomba au kumwuliza azitimize, wakati kwa kufanya hivyo angelivunjia heshima Jina Lake Mwenyewe. [Pr 308.1; Maombi Aya ya 16]

Ahadi ni “Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7. Naye Yohana anatangaza hivi: “Katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika amri Zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake. Bali yeye alishikaye Neno Lake, ndani yake huyo pendo la MUNGU limekamilika hakika.” 1 Yohana 2:3-5. [Pr 308.2; Maombi Aya ya 17]

Mojawapo ya amri za mwisho za Kristo kwa wanafunzi Wake ilikuwa “Mpendane kama nilivyowapenda ninyi.” Yohana 13:34. Je, tunatii amri hii, au tunafurahia na kuendekeza sana tabia zisizo za Kikristo? Ikiwa kwa namna yoyote tumehuzunisha au kuwajeruhi wengine, ni jukumu letu kuungama kosa letu na kutafuta upatanisho. Haya ni maandalizi muhimu ili tuweze kwenda mbele za MUNGU

kwa imani, katika kuomba baraka Zake. [Pr 308.3; Maombi Aya ya 18]

Kuna jambo lingine ambalo mara nyingi hupuuzwa na wale wanaomtafuta Bwana katika maombi. Je, umekuwa mwaminifu na mkweli kwa MUNGU? Kupitia nabii Malaki Bwana anatangaza, “Tangu siku za baba zenu mmeziacha amri Zangu, wala hamkuzishika. Nirudieni Mimi, Nami nitawarudia ninyi, asema Bwana wa majeshi. Lakini ninyi mwasema, Turudi kwa namna gani? Je, mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmeniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa jinsi gani? Mmeniibia zaka na dhabihu.” Malaki 3:7, 8. [Pr 308.4; Maombi Aya ya 19]

Kama Mpaji wa kila baraka, MUNGU anadai sehemu fulani ya vyote tulivyo navyo. Hili ni fungu lililo katika mpango Wake ili kuendeleza mahubiri ya injili. Na kwa kumrudishia MUNGU, tunakuwa tumeonyesha kuthamini kwetu zawadi Zake. Lakini tukimzuilia kile ambacho ni Chake Mwenyewe, tunawezaje kudai baraka Zake? Ikiwa sisi ni mawakili wasio waaminifu wa mambo ya duniani, tunawezaje kumtarajia Yeye kutuamini kwa kutukabidhi vitu vya mbinguni? Huenda hapa ndio kuna siri ya maombi yasiyojibiwa. [Pr 309.1; Maombi Aya ya 20]

Lakini Bwana katika rehema Zake kuu Yu tayari kusamehe, Naye asema, “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha kuipokea. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu matunda ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika shamba. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi. Malaki 3:10-12. [Pr 309.2; Maombi Aya ya 21]

Ndivyo ilivyo kwa kila takwa au sharti jingine la MUNGU. Zawadi Zake zote zimeahidiwa kwa sharti la utii. MUNGU ana mbingu iliyojaa baraka kwa wale watakaoshirikiana Naye. Wote wanaomtii wanaweza kudai kwa ujasiri kutimizwa kwa ahadi Zake [Pr 309.3; Maombi Aya ya 22]

Lakini ni lazima tuonyeshe tumaini thabiti na lisilokengeuka kwa MUNGU. Mara nyingi Yeye hucheleweshwa kutujibu ili kujaribu imani yetu au kujaribu

unyofu/ukweli wa shauku yetu. Baada ya kuomba kulingana na Neno Lake, tunapaswa kuamini ahadi Yake na kusisitiza maombi yetu kwa mtazamo wenye kuazimia kwamba hayatakataliwa. [Pr 309.4; Maombi Aya ya 23]

MUNGU hasemi, Ombeni mara moja, nanyi mtapata. Yeye Anatubidisha tuombe. Dumu katika maombi bila kuchoka. Kuomba kwa bidii humleta mwombaji katika mtazamo wa dhati zaidi, na kumpa shauku kubwa ya kupokea mambo ambayo anaombea. Kristo alimwambia Martha kwenye kaburi la Lazaro, “Kama ukiamini, utaona utukufu wa MUNGU.” Yohana 11:40. [Pr 309.5; Maombi Aya ya 24]

Lakini wengi hawana imani iliyo hai. Na hii ndiyo sababu hawazoni nguvu ya MUNGU zaidi. Udhaifu wao ni matokeo ya kutokuamini kwao. Wana imani zaidi katika kazi na juhudi zao wenyewe kuliko katika utendaji wa MUNGU kwao. Wamejiweka katika kujitunza na kujishugulikia wenyewe. Wanapanga na kufikiri, lakini wanaomba kidogo, na wana imani ndogo ya Kweli kwa MUNGU. Wanafikiri wana imani, lakini ni msukumo tu wa wakati huo (mhemko). Kwa kushindwa kutambua hitaji lao wenyewe, au nia ya MUNGU kuwapa, hawadumu katika kuweka maombi yao mbele za Bwana. [Pr 310.1; Maombi Aya ya 25]

Maombi yetu yanapaswa kuwa ya dhati na yasiyochoka kama yalivyokuwa maombi ya yule rafiki mhitaji aliyeomba mikate usiku wa manane. Kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na Kristo utakavyokuwa karibu zaidi. Tutapokea baraka nyingi kwa sababu tumeongeza imani. [Pr 310.2; Maombi Aya ya 26]

Sehemu yetu ni kuomba na kuamini. Kesheni katika maombi. Kesha, na ushirikiane na MUNGU asikiaye maombi. Kumbuka kwamba “sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU.” 1 Wakorintho 3:9. Zungumza na kutenda kulingana na maombi yako. Itafanya tofauti ya kudumu kwako hata jaribu litaipima imani yako kuwa ya kweli, au itaonyesha kuwa maombi yako ni ya desturi/mazoea au mfano tu. [Pr 310.3; Maombi Aya ya 27]

Wakati mashaka yanapotokea, na matatizo yanakukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Tumainia yote kwa MUNGU. Mazoea ya kuwaambia wengine magumu yetu hutufanya tu kuwa dhaifu, na hayaleti nguvu kwao.

Inaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawawezi kuutatua au kutuletea afueni. Tunatafuta nguvu za mwanadamu mwenye dhambi, anayekosea, na mwenye kikomo, wakati tunaweza kuwa na nguvu za MUNGU asiyekosea, na asiye na mwisho. [Pr 310.4; Maombi Aya ya 28]

Hauhitaji kwenda kwenye miisho ya dunia kwa ajili ya hekima, kwa maana MUNGU Yuko karibu. Sio uwezo ulionao sasa au utakaowahi kuwa nao wakati wowote ule, ndio utakaokupa mafanikio. Ni yale ambayo Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na imani ndogo sana katika kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya na kuwa na ujasiri zaidi katika kile ambacho MUNGU anaweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini. Yeye Anatamani kukufanya wewe umfikie Yeye kwa imani. Yeyey Anatamani sana wewe utarajie mambo makubwa kutoka Kwake. Yeye Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kimwili, yaani yale ya muda mfupi na yale kiroho. Yeyey Anaweza akazinoa akili. Yeyey Anaweza kutoa busara na ujuzi. Weka talanta/vipawa vyako kazini, na kisha mwombe MUNGU hekima, nawe utapewa. [Pr 310.5; Maombi Aya ya 29]

Lichukue Neno la Kristo kama uhakikisho wako. Kwani Yeye hajakualika wewe uje Kwake? Usijiruhusu kamwe kuzungumza kwa njia isiyo na matumaini, iliyovunjika moyo. Ukifanya hivyo utapoteza sana. Kwa kutazama mwonekano na kulalamika shida na shinikizo vinapokujia, unatoa uthibitisho wa imani yenye ugonjwa na iliyodhoofika. Ongea na tenda kana kwamba imani yako haiwezi kushindwa. Bwana ni tajiri wa mali; Yeye Anamiliki dunia. Tazama mbinguni kwa imani. Mwangalie Yeye aliye na nuru na uwezo na ufanisi. [Pr 311.1; Maombi Aya ya 30]

Katika imani ya kweli kuna uchangamfu, uthabiti wa kanuni, na uimara wa kusudi ambao hakuna wakati wala taabu inayoweza kudhoofisha. “Hata vijana watafifia na kulegea; naam, wataanguka kwa uchovu. Lakini wote wanaomtumainia Mwenyezi MUNGU, watapata nguvu mpya. Watapanda juu kwa mabawa kama tai; watakimbia bila kuchoka; watatembea bila kulegea.” Isaya 40:30, 31, [Pr 311.2; Maombi Aya ya 31]

Kuna wengi wanaotamani kuwasaidia wengine, lakini wanahisi kwamba hawana nguvu za kiroho au nuru ya kuwapa wengine. Hebu wawasilishe maombi yao kwenye kiti cha neema. Omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. MUNGU anasimama nyuma ya kila ahadi Yake aliyoitoa (uhakika). Ukiwa na Biblia yako mikononi mwako sema, nimefanya kama ulivyosema. Ninawasilisha ahadi Yako, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa.” [Pr 311.3; Maombi Aya ya 32]

Hatupaswi kuomba kwa Jina la Kristo tu, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii inafafanua kile kinachomaanishwa inaposemwa kwamba Roho “hufanya maombezi kwa ajili yetu kwa uchungu mzito usioweza kutamkika.” (kuugua kusikotamkika) Warumi 8:26. Ombi kama hilo MUNGU hufurahia kulijibu. Tunapotoa ombi katika jina la Kristo kwa dhati, bidii na mkazo wa kina, kuna ahadi kubwa kutoka kwa ule mkazo kwamba MUNGU atajibu ombi letu “kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo.” Waefeso 3:20. [Pr 311.4; Maombi Aya ya 33]

Kristo amesema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. “Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.” Yohana 14:13. Naye Yohana mpendwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, anasema kwa uwazi na uhakikisho mkubwa: “Tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, Yeye anatusikia; na kama tukijua ya kuwa atusikia, tumwombalo lo ote, twajua ya kuwa tunazo haja tulizomwomba.” 1 Yohana 5:14, 15. Basisi wewe wasilisha ombi lako kwa Baba katika Jina la Yesu. MUNGU ataliheshimu Jina hilo. [Pr 311.5; Maombi Aya ya 34]

Upinde wa mvua unaokizunguka kiti cha enzi ni uthibitisho kwamba MUNGU ni Kweli/Mkweli, kwamba ndani Yake hakuna kubadilikabadilika, wala kugeuka kama kivuli. Tumemtendea dhambi na hatustahili rehema Zake. lakini Yeye Mwenyewe ameweka katika midomo yetu maombi yale ya ajabu sana, “Usitutupe, kwa heshima ya Jina Lako; usikidharau kiti Chako cha enzi kitukufu. Ukumbuke agano ulilofanya nasi, wala usilivunje.” Yeremia 14:21. Tunapoenda kKwake tukiungama kutostahili na dhambi zetu, Yeye amejitolea kukisikiliza kilio chetu. Heshima ya kiti Chake cha enzi imo hatarini kwa ajili ya

utimilifu wa Neno Lake kwetu (heshima Yake ipo hatarini Neno Lake lisipotimia). [Pr 312.1; Maombi Aya ya 35]

Kama Haruni, aliyefananishwa na Kristo, Mwokozi wetu anabeba majina ya watu Wake wote moyoni Mwake katika Patakatifu. Kuhani wetu Mkuu anakumbuka Maneno yote ambayo kwayo ametutia moyo kuyatumaini. Daima Yeye hukumbuka na kujali Agano Lake. [Pr 312.2; Maombi Aya ya 36]

Wote watafutao kutoka Kwake watapata. Wote wanaobisha watafunguliwa mlango. Udhuru hautatolewa, kwamba Usinisumbue; mlango umefungwa; Sitaki kufungua. Kamwe hataambiwa mtu, 'siwezi kukusaidia'. Wale wanaoomba mkate usiku wa manane ili kulisha roho zenye njaa watafanikiwa. [Pr 312.3; Maombi Aya ya 37]

Katika kisa cha Mfano, cha yule anayeomba mkate kwa ajili ya mgeni, hupokea "kwa wingi kadiri ya haja yake." Na ni kwa kipimo gani basi MUNGU atatugawia ili tuwagawie wengine? "Kwa kadiri ya kipimo cha kipawa cha Kristo." Waefeso 4:7. Malaika wanatazama kwa hamu kubwa kuona jinsi mwanadamu anavyoshughulika na wanadamu wenzake (anavyohusiana na wenzake). Wanapona mtu akidhihirisha huruma kama ya Kristo kwa wakosaji, wanajongea kwa karibu sana naye na kuleta kwenye kumbukumbu yake maneno ya kusema ambayo yatakuwa kama Mkate wa Uzima kwenye nafsi hiyo "MUNGU atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Wafilipi 4:19. Ushuhuda wako katika Ukweli na uhalisia wake, Yeye ataufanya kuwa na nguvu katika uwezo ya maisha yajayo. Neno la Bwana litakuwa kinywani mwako kama Kweli na haki. [Pr 312.4; Maombi Aya ya 38]

Juhudi binafsi kwa wengine zinapaswa kutanguliwa maombi mengi ya siri; kwa maana inahitaji hekima kubwa kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na wanadamu, fanya ushirika na Kristo. Katika kiti cha enzi cha neema ya mbinguni, wewe pata maandalizi ya kuwahudumia watu. [Pr 313.1; Maombi Aya ya 39]

